YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA 9
1.0 UTANGULIZI 9
1.1 MAJINA YA WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI 9
1.1.1 Wajumbe wa Kamati 9
1.1.2 Sekretarieti ya Kamati 10
1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI 10
1.4 MUUNDO WA RIPOTI 11
SEHEMU YA PILI 12
MAUDHUI YA RIPOTI 12
3.1: SHIRIKA LA MAGAZETI 12
3.2: SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) 15
3.2.1 Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato 18
3.3: CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI 20
3.4: MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA) 22
3.4.1 Kutokamilika kwa baadhi ya visima vya mradi wa Ras El Kheimah Unguja na Pemba, Tsh. 1,835,645,325.68 24
3.5: MAMLAKA YA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA) 26
3.5.1 Wadaiwa wa Mamlaka Tsh. 1,867,389,598 32
Hoja Na. 3.5.2 Ucheleweshwaji wa ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ya Vitega Uchumi, Pemba 38
3.6: CHUO CHA UTAWALA WA UMMA – IPA 39
3.7: CHUO CHA UANDISHI WA HABARI 42
3.8: CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA) 45
3.9 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA 49
3.10 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR 56
3.8 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF) 59
3.8.1 Kutokufanyia kazi mapendekezo ya ripoti ya tathmini ya makisio ya takwimu zinazohusiana na uhai wa wachangiaji (Actuarial valuation report) kama ilivyoelekezwa na Bodi 61
3.8.2 Mapungufu katika udhibiti wa bajeti iliyoidhinishwa 65
3.8.3 Udhaifu katika usimamizi na udhibiti wa mapato ya kodi za pango. 67

3.8.4 Kasoro zilizobainika katika mikopo ya wafanyakazi 69
3.8.5 Kukosekana kwa uthibitisho kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa malipo ya gharama za awali za mradi wa mji mpya Kwahani, TZS Billioni 1.19. 71
3.10 SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) 74
3.10.1 Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani 77
3.10.11 Mapungufu katika matumizi ya mafuta ya Shilingi 151,517,080 78
3.11: SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) 81
3.11.1 Kukosekana kwa mapato ya jengo la Kitega Uchumi, Tsh. 172,900,816.99 85
3.11.2 Matumizi yaliyofanyika kabla ya utayarishwaji wa hati za malipo Tsh. 23,794,520,13386
3.12: MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR 89
3.13: MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA) 91
3.14: MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI MAFUTA NA GESI ASILI ZANZIBAR (ZPRA) 96
3.15: SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR 99
3.16: MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA) 102
5.7.2: TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS) 106
5.8.3: MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR 110
5.8.4: BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR 113
5.8.5: TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA 115
5.2.13: BARAZA LA MANISPAA MJINI 120
5.2.13.1 Kukosekana kwa takwimu za wafanyabiashara wanaolipa leseni za biashara 125
5.2.14: BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “A” 125
5.2.14.1 Kukosekana takwimu za wafanyabiashara wanaolipa leseni za biashara 128
5.2.15: BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “B” 129
5.2.15.1 Kukosekana takwimu za wafanyabiashara wanaolipa leseni 131
5.2.16: BARAZA LA MJI KASKAZINI “A” 132
5.2.18: BARAZA LA MJI KATI 139
5.2.19: HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI 141
5.2.20: BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE 142
5.2.21: BARAZA LA MJI MKOANI 143
5.2.22: BARAZA LA MJI WETE 147
5.2.23: HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI 148

3.1: SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO) 152
3.1.1 Mapungufu katika daftari la kuhifadhia Mali za kudumu 156
3.1.2 Madeni ya muda mrefu shilingi 40,872,991,281 163
3.1.4 Hali ya upotevu wa Nishati ya Umeme 171
3.1.5 Kushindwa kufanya tathmini ya thamani ya mali za kudumu 172
3.1.6 Dosari katika mfumo wa urejeshwaji wa mikopo kwa wateja 173
3.1.7 Kushindwa kutumika kwa Mfumo wa Uhasibu wa kielektroniki wa USD 65,000 174
3.2: BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ) 175
3.2.1 Kutokutekeleza muongozo wa Benki kuu (BOT) 177
3.2.2 Mapato ya ujira ambayo hayakupokelewa shilingi 395,889,294 181
3.3: BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB) 189
3.3.1: Kushindwa kutenganisha Ardhi na Majengo katika hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 7,530,308,731 191
3.3.2: Taarifa za fedha ambazo hazikufanyiwa usuluhishi wa kibenki kwa muda mrefu 192
3.3.3: Taarifa ya Madeni ya Kodi 195
3.4.2 Kushindwa kufanya ufuatiliaji wa malipo kwa wakati kutoka kwa Mawakala na Madalali. 208
3.4.3 Malipo ya madai yaliyolipwa kinyume na Sera ya Madai ya Shirika la Bima Tzs: 87,613,000 209
3.4.4 Madai yatokanayo na wabia wengine wa Bima (Due to other reinsurance and treaty) Tzs. 1,784,659,276 211
3.4.5 Madai ya Kodi (VAT) yaliyokosa uthibitisho Tzs. 772,343,656 212
3.4.6 Malipo yasiyokuwa na tija kwa Shirika la Bima Tzs. 141,369,500. 214
3.4.7 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio ya Tzs. 83,884,000 218
3.4.8 Uwepo wa tuhuma za madai ya bima kwa muda mrefu Tzs. 104,300,000 220
3.4.9 Kuchelewa kupelekwa kwa fedha benki Tzs. 186,637,556 222
3.4.10 Uwepo wa mikopo ya muda mrefu na mapato ya ada ya bima (premium) yaliyokuwa hayajakusanywa kutoka kwa Mawakala na Madalali Tzs. 648,891,615 223
3.4.11 Uwepo wa wadaiwa na malipo ya Bima Tawi la Arusha Tzs. 55,721,830 224
3.4.13 Dosari katika ukataji wa bima kwa vyombo vikubwa 227
3,4,14 Bakaa ya Fedha katika hesabu ya FBME Tzs. 90,830,291 229
3.5: SHIRIKA LA BANDARI 233

3.5.1 Madeni yasiyolipwa kwa muda wa mrefu TSH. 467,856,819.73 240

3.5.2 Kukosekana kwa uhalisia wa bajeti 241

3.5.3 Kutofuatwa kwa viwango vya kimataifa vya uandaaji na utayarishaji wa Taarifa za Hesabu kwa kipengele cha sera ya Uhasibu (IAS 8) 242

3.5.4 Kutofautwa kwa viwango vya kimataifa vya uandaaji na utayarishaji wa Taarifa za hesabu kuhusu mahusiano ya pande mbili za mkataba (IAS 24). 243

3.5.5 Mapungufu katika kuzingatia utaratibu wa ununuzi wa umma katika ujenzi wa ghala la Saateni TSH. 674,949,910. 244

3.5.6 Thamani ya mali za kudumu ambazo hazikuoneshwa katika hesabu za mwisho wa mwaka za Shirika la Bandari. 245

3.5.7 Malipo Kinyume na Taratibu za Utumishi Tsh. 55,944,292.3 246

3.5.8 Malipo Yaliokosa Kukatwa Kodi ya Zuio Shilingi 17,040,000 248

3.5.9 Malipo kwa Wafanyabiashara ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi Shilingi 55,356,201 249

3.5.10 Masurufu Yasiokuwa na Marejesho (Returns) Shilingi 25,220,260 249

3.6: SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) 251

3.6.1 Taarifa za Wadaiwa na Wadai wa Shirika 254

3.6.2 Ucheleweshwaji wa fedha za mapato kupelekwa benki shilingi 140,565,900 na dola 20,783 257

3.6.3 Fedha zilizokopwa na Shirika kutoka kwa watu binafsi shilingi 6,771,848,000 258

3.6.4 Ulipaji wa Mishahara kwa wafanyakazi wa muda bila kupewa Mikataba 259

3.6.5 Tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo 260

3.6.6 Kutokuingizwa kwa taarifa za madeni katika hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 7,794,086,747.56 264

3.6.7 Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya shilingi 246,631,737 265

3.6.8 Madeni ya muda mrefu shilingi 543,605,532.33 265

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA - PEMBA 266

3.6.9 Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda wasiokuwa na mikataba ya kazi shilingi 83,446,225. 266

3.6.10 Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda na vibarua kinyume na utaratibu shilingi 4,632,500 267

3.6.11 Deni la kiwanda kwa watoa huduma shilingi 8,114,990 267

3.6.12 Hasara iliyosababishwa na uvujaji wa mafuta wakati wa uzalishaji shilingi 101,144,000 268

3.6.13 Mafuta ambayo hayakuingizwa katika daftari la ghalani shilingi 2,674,800 269

UKAGUZI MAALUM WA KAMATI KATIKA TAWI LA SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) DAR - ES - SALAAM 270

3.7: SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA (ZMA) 274

MATOKEO YA UKAGUZI 280

3.7.1 Kutowasilisha makato ya Kisheria shilingi 203,895,169 280

3.7.2 Kukosekana kwa Ufanisi katika Meli ya Ukombozi II 282

3.7.3 Kukosekana kwa mfumo wa usimamizi wa viashiria vya hatari kwa Taasisi. 284

3.7.4 Kukosekana kwa ripoti ya kiufundi katika usimamizi wa matengenezo ya meli ya MV. Maendeleo uliyogharimu jumla ya shilingi 3,322,810,664.23 286

UKAGUZI MAALUM WA KAMATI YA LAAC KWA SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA DAR - ES - SALAAM 288

3.9: MFUKO WA BARABARA (ZRF) 291

MATOKEO YA UKAGUZI 295

3.9.1 Ucheleweshaji wa utekelezaji wa kazi za ukarabati wa barabara 295

3.9.2 Kukosekana kwa ushahidi wa mapokezi ya vifaa shilingi 134,321,000 298

3.9.2 Mikataba iliyosainiwa na Wakandarasi walio na leseni zilizomaliza muda na wasio na leseni 300

3.9.3 Utekelezaji wa kiwango cha chini wa kazi zilizopangwa za matengenezo ya barabara 301

3.9.4 Kukosekana kwa ushahidi wa ukaguzi uliofanywa kwa bidhaa zilizonunuliwa shilingi 86,890,900 302

3.10: SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) 303

3.10.1 Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani 306

3.10.11 Mapungufu katika matumizi ya mafuta ya Shilingi 151,517,080 307

3:11: SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC) - UNGUJA 310

MATOKEO YA UKAGUZI 313

3.11.1 Kuripotiwa kwa mapato pungufu ya shilingi 586,000,000 313

3.11.2 Ufanisi katika uendeshaji wa Shirika la Nyumba. 314

3.11.3 Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 2,243,400 316

3.11.4 Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslim shilingi 1,430,000 316

3.14 SHIRIKA LA MAGAZETI 319

3.14.1 Kutokufanya Kazi kwa Kamati ya Ukaguzi 323

3.14.2 Manunuzi ambayo yamekiuka utaratibu Tsh, 102,364,625 324

3.15: MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA) 326

3.15.1 Manunuzi ya Mashine na Pampu za maji yaliyokiuka utaratibu wa manunuzi shilingi 126,766,686.00. 330

3.15.2 Ongezeko la gharama za matumizi ya mafuta 331

3.15.4 Ufanisi katika uendeshaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar 333

3.15.5 Hati za malipo zilizokosa vielelezo shilingi 6,899,290 334

3.15.6 Malipo kwa wafanyabiashara waliokuwa hawajasajiliwa Shilingi 34,237,762.60 336

3.15.7 Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 276,118,668 340

3.15.8 Malipo kwa wafanyabiashara waliokuwa hawajasajiliwa Shilingi 37,163,447.44 345

3.15.9 Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji mapato Shilingi 6,866,873,986.55 345

3.15.10 Madeni ya huduma ya maji ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu shilingi 16,007,884,152.98 347

3.16: MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA) 348

3.16.1 Vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la ghalani Shilingi 615,000 358

3.16.2 Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslimu Shilingi 1,205,000 359

3.17: MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR 360

MATOKEO YA UKAGUZI 366

3.17.1 Kukosekana kwa mikataba ya ukusanyaji wa mapato 366

3.17.2 Kutowasilishwa mikato ya kodi na michango ya ZSSF ya wafanyakazi kwa wakati shilingi 639,932,727 368

3.17.4 Dosari katika uwasilishaji wa taarifa za Mamlaka shilingi 46,620,728,123 370

3.17.5 Kukosekana kwa mikataba ya ujenzi na utoaji huduma yenye thamani ya shilingi 382,649,624 371

3.17.6 Kushindwa kufikia malengo ya kukusanya mapato shilingi 618,378,900 372

3.17.7 kukosekana kwa uthibitisho wa uletwaji wa vitabu vya kukusanyia mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020 373

3.17.8 Mamlaka kushindwa kukusanya mapato ya shilingi 65,609,020 374

3.17.9 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu bila ya kulipwa shilingi 130,542,607 375

3.17.10 Hati za malipo zilizokosa vielelezo shilingi 95,636,945 376

3.17.11 vifaa ambavyo havikurikodiwa ghalani shilingi 16,524,383 377

3.17.12 malipo ya fedha kwa wafanyakazi ambao hawakusajiliwa shilingi 74,525,422 378

UKAGUZI WA MRADI WA MAENDELEO WA UJENZI WA UWANJA WA NDEGE WA NUNGWI. 379

3.14: SHIRIKA LA MAGAZETI 381
3.14.1 Kutokufanya Kazi kwa Kamati ya Ukaguzi 385
3.14.2 Manunuzi ambayo yamekiuka utaratibu Tsh, 102,364,625 386
3.19: MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA (ZPPDA) 388
MATOKEO YA UKAGUZI 390
3.19.1 Kutofanyakazi kwa kamati ya ukaguzi 390
3.21: MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA) 392
MATOKEO YA UCHUNGUZI 396
3.21.1 Vitabu vya mapato ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi 396
3.21.2 Kukosekana kwa Mapato yatokanayo na usajili wa vyombo vya uvuvi 398
3.22: MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR (VTA) 399
3.22.1 Tofauti iliyojitokeza baina ya makusanyo halisi na kilichoripotiwa katika taarifa ya fedha shilingi 283,171,319.44 401
3.22.2 Kukosekana kwa uhalisia wa makisio ya makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi. 402
3.22.3 Vifaa vilivyohifadhiwa muda mrefu bila matumizi vyenye thamani ya shilingi 118,901,079 403
3.22.4 Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika Dakhalia kulinganisha na uwezo wa Dakhalia (Hostel) 404
3.22.5 Dosari iliyobainika katika malipo ya mikataba ya zabuni yenye jumla ya shilingi 332,376,974 405
3.22.6 Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya kukusanya mapato ya shilingi 51,620,000 406
3.22.7 Kukosekana kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani 407
3.22.8 Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa Mamlaka. 407
ZIARA MAALUM YA UKAGUZI WA KAMATI KATIKA DAKHALIA YA CHUO CHA MAFUNZO YA AMALI MKOKOTONI 417
3.22: MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR (VTA) 418
MATOKEO YA UKAGUZI 421
3.22.1 Tofauti iliyojitokeza baina ya makusanyo halisi na kilichoripotiwa katika taarifa ya fedha shilingi 283,171,319.44 421
3.22.2 Kukosekana kwa uhalisia wa makisio ya makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi. 422
3.22.3 Vifaa vilivyohifadhiwa muda mrefu bila matumizi vyenye thamani ya shilingi 118,901,079 423
3.22.4 Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika Dakhalia kulinganisha na uwezo wa Dakhalia (Hostel) 424

3.22.5 Dosari iliyobainika katika malipo ya mikataba ya zabuni yenye jumla ya shilingi 332,376,974 425

3.22.6 Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya kukusanya mapato ya shilingi 51,620,000 425

3.22.7 Kukosekana kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani 426

3.22.8 Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa Mamlaka. 427

3.22.9 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 13,296,979 428

3.22.10 Kukosekana kwa zabuni ya Mkandarasi wa Ujenzi wa Jengo la Maabara katika Chuo cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba. 430

3.22.11 Kukosekana kwa zabuni ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi shilingi 236,296,842.1 431

3.22.12 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 21,225,000 432

3.22.14 Kukosekana kwa muongozo wa ulipwaji wa posho na gawio la faida shilingi 23,962,398 434

3.22.15 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 29,196,971 435

ZIARA MAALUM YA UKAGUZI WA KAMATI KATIKA DAKHALIA YA CHUO CHA MAFUNZO YA AMALI MKOKOTONI 437

3.24: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR 438

3.29 TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA 442

SEHEMU YA TATU 445

HITIMISHO 445

RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI YA MITAA NA MASHIRIKA (LAAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 NA 2019/2020

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) imeundwa baada ya kuonekana kwamba Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Serikali na Mashirika (PAC) kuwa na Taasisi nyingi za kufuatilia.

Hivyo, Kamati hii imeundwa pamoja na mambo mengine kutoa muda wa kutosha kwa Kamati mbili hizi kufuatilia hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC imeanza rasmi shughuli zake katika Baraza la Kumi la Wawakilishi la Zanzibar, ingawa ilikuwa inatambulika kikanuni tokea mwaka 2016.

Hivyo, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa kipindi hiki imefanikiwa kufanya ukaguzi wa Ripoti mbili zilizowasilishwa katika vipindi tofauti katika Baraza, Ripoti zenyewe ni:

i. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na

ii. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka wa fedha 2019/2020.

1.1 MAJINA YA WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali ya Mitaa na Mashirika, kwa mwaka huu wa uwasilishaji ripoti (2020/2021), inaundwa na Wajumbe 7 na Sekretarieti kama ifuatavyo:

1.1.1 Wajumbe wa Kamati

1. Mhe. Habib Ali Mohamed - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
4. Mhe. Shaib Hassan Kaduara - Mjumbe
5. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe

6. Mhe. Haji Shaaban Wazir - Mjumbe
7. Mhe. Bakar Hamad Bakar - Mjumbe

1.1.2 Sekretarieti ya Kamati

Sekretarieti ya Kamati hii iliongozwa na Makatibu wa Kamati kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi na Maafisa wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sekritarieti yenyewe ni:

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
2. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu
3. Ndg. Hamad Akida Hamad - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti
4. Ndg. Mwajuma Hassan Iddi - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti
5. Ndg. Juma Mohammed Juma - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti

1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Kamati imefanya kazi kwa mujibu wa masharti yaliyoelezwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020. Vile vile, Kamati hii ilizingatia matakwa ya Kanuni ya Kudumu inayoitaka Kamati kujipangia kazi zake baada ya kushauriana na Spika pamoja na kujipangia utaratibu mzuri wa kutekeleza majukumu yake.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Kamati ilijipangia kukutana na Watendaji wa Serikali za Mitaa na Mashirika yanayojitegemea yaliyopo Unguja, Pemba na Dar - es - Salaam na kufanya nao vikao, mahojiano na majadiliano. Aidha, Kamati ya LAAC ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kufanya ukaguzi ili kushuhudia uhalisia na usahihi wa maelezo yaliyowasilishwa na watendaji hao. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mizunguko mitatu tofauti kama ifuatavyo:

Mzunguko wa Kwanza: Tarehe 11 Januari, 2021 hadi tarehe 16 Februari, 2021.

Mzunguko wa Pili: Tarehe 23 Machi, 2021 hadi tarehe 24 Aprili, 2021.

Mzunguko wa Tatu: Tarehe 09 Agosti, 2021 hadi tarehe 26 Agosti, 2021.

Mzunguko wa Nne: Tarehe 08 Novemba, 2021 hadi tarehe 26 Novemba, 2021.

Mzunguko wa Tano: Tarehe 17 Januari, 2022 hadi tarehe 04 Februari, 2022.

1.4 MUUNDO WA RIPOTI

Ripoti hii imegawika katika sehemu kuu tatu; Utangulizi, Maudhui na Hitimisho kama

inavyoainishwa na Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

1. **Utangulizi umejumuisha;** Utangulizi, Wajumbe wa Kamati na Sekretarieti, Utaratibu wa Kazi za Kamati na Muundo wa Ripoti.

2. **Maudhui ya Ripoti yamejumuisha**; Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Mashirika yanayojitegemea ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

   Kila ripoti imegusia mambo manne; ambayo ni Hoja ya Mdhibiti na Mkuu wa Hesabu kama ilivyoripotiwa katika ripoti husika, Majibu ya Wizara au Taasisi na mwisho ni Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati hii.

3. **Hitimisho;** limegusia maelezo ya Ripoti kwa ujumla pamoja na shukurani.

SEHEMU YA PILI

MAUDHUI YA RIPOTI

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MASHIRIKA NA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

3.1: SHIRIKA LA MAGAZETI

Taarifa ya Mapato

Shirika la Magazeti lilikadiriwa kukusanya Tsh. 1,268,700,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali. Kati ya hizo, Tsh 618,700,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 650,000,000 ikiwa ni makusanyo ya vyanzo vya ndani vya Shirika.

Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 1,429,540,404 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali, sawa na 113% ya makadirio. Kati ya hizo, jumla ya Tsh. 598,364,684 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini, Tsh, 713,838,220 ikiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani vya Shirika na Tsh. 117,337,500 ikiwa ni misaada.

Majibu ya Shirika

Ongezeko hili la Tsh. 63,838,220 ambalo ni sawa na 13% za makadirio lilitokana na kuongezeka kwa matangazo mbali mbali pamoja na matoleo kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 kwa taasisi mbali mbali hasa taasisi za Serikali. Aidha, mapato ya Shirika la Magazeti yamepungua kutoka Tsh. 1,138,894,225 kwa mwaka 2016/2017 hadi kufikia Tsh. 713,838,220 kwa mwaka 2017/2018 kukiwa na upungufu wa Tsh. 425,056,005 sawa na 37% ya upungufu.

Mapungufu haya yanatokana na kuwepo kwa wapewa huduma na Shirika (matangazo) hasa taasisi za Serikali na kutolipia huduma zao ipasavyo, kitu ambacho kinapelekea kuliathiri Shirika kwa kupungua kwa mapato.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia mapato ya Shirika, Kamati ilihitaji ipatiwe taarifa ya Ukaguzi wa Ndani, ambayo ilikwishaihitaji kabla ya siku ya kukutana na Shirika hili na kuliandikia barua kama ilivyofanya kwa taasisi zote ilizokutana nazo, hata hivyo, Shirika halikuiandaa taarifa hiyo, kitendo ambacho kiliashiria dharau kwa Kamati.

Aidha, kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Baraza, Kamati ilipoliandikia Shirika kutaka kufanya kazi nalo, ililiarifu kupitia njia ya barua na maelekezo ya kikao cha kuthibitisha ratiba kuwa, majibu ya hoja zote zinazofanyiwa kazi na Shirika ikiwa ni pamoja na

taarifa za Mapato na Matumizi kama zilivyoainishwa na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, zilitakiwa zijibiwe kwa njia ya maandishi na zikabidhiwe kwa Kamati siku mbili kabla ya kazi za Kamati na Shirika hili. Hata hivyo, majibu hayo nayo hayakujibiwa kwa njia ya maandishi na kukabidhiwa Kamati kwa mnasaba wa maelekezo ya Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

Aidha, ili kufahamu zaidi namna ya utekelezaji wa bajeti ya Shirika na taarifa ya mapato yake, Kamati ilihitaji pia Mpango Kazi wa Shirika na utekelezaji wake, lakini ilikwishauhitaji kabla ya kazi za Kamati kupitia barua ya Kamati iliyopokelewa tarehe 31/12/2020 yenye kumbu kumbu namba BLW/K.10/32/3. Hata hivyo, Kamati ilipatiwa Mpango Kazi tu, bila ya kupewa utekelezaji wake, hali iliyokwamisha juhudi za Kamati katika kufanya kazi na Shirika la Magazeti.

Vile vile Kamati ilihitaji kupatiwa Kanuni za Shirika lakini haikupatiwa kwa kuelezwa kuwa Shirika halina Kanuni yoyote inayosimamia utekelezaji wa shughuli zake na baada ya kuulizwa sababu za kukosekana kwa Kanuni hizo wakati Sheria iliyoeleza kutungwa kwake ni ya mwaka 2008, uongozi wa Shirika ulisema kuwa, walitaarisha Kanuni hizo na kuzipeleka kwa Mheshimiwa Waziri tokea mwaka 2010, lakini hadi Waziri huyo anastaafu kupisha Uchaguzi Mkuu wa 2010, hakuwahi kuzisaini Kanuni hizo.

Kamati imeelezwa kuwa Shirika lilitegemea vyanzo viwili vya mapato; Kuuza magazeti ya Serikali na Kuuza matangazo katika magazeti hayo. Aidha, Kamati ilipohitaji kupatiwa mnyambuliko wa vipi makusanyo ya Tsh. 650,000,000 ulivyokadiriwa, haikupatiwa taarifa hiyo kwa sababu Shirika halikujiandaa kuwasilisha. Kimsingi, Kamati haikupata taarifa za kina juu ya mapato ya Shirika na kwa namna ilivyohoji, haikuwezeshwa kupatiwa taarifa hizo. Na kilichofanyika baadae ni kupatiwa taarifa mbali mbali bila ya Shirika kuandaa kikao cha kujadiliana na Kamati, na ni sawa na kusema, Shirika hili limekwepa majukumu yake na kuitaka Kamati izingatie taarifa ilizoziwasilisha Afisi ya Baraza la Wawakilishi bila ya majadiliano yoyote na Uongozi wa Shirika hilo, kazi ambayo Kamati haikuona busara kuifanya.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati haikuridhishwa na utendaji kazi wa Uongozi wa Shirika hili la Magazeti na imezuiliwa kufahamu kwa kina vyanzo halisi vya mapato ya Shirika na namna vilivyokusanywa kama ilivyoelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukulia hatua zinazostahiki ili kuepusha kutokezea tena vitendo vya dharau na kuzinyima Kamati za Baraza kufanya kazi zao.

Taarifa ya Matumizi

Shirika la Magazeti lilikadiriwa kutumia Tsh. 1,268,700,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 1,427,052,287 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na 112% ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Matumizi ya Shirika la Magazeti yanaonekana kuongezeka kutoka Tsh. 1,268,700,000 ya makadirio, hadi kufikia Tsh. 1,427,052,287 kukiwa na ongezeko la Tsh. 158,352,287 sawa na 12.5%. Ongezeko hili linatokana na utanuzi wa ofisi, kwa kuengeza maeneo ya wafanyakazi pamoja na vitendea kazi, kwani hapo awali, kulikuwa na uhaba mkubwa wa ofisi na kupelekea Shirika kukosa ufanisi wa utendaji wake. Vile vile Shirika lilipunguza madeni yaliyokuwa yamekaa muda mrefu kwa kutokuwa na uwezo wa kuyalipa, wakati Shirika lilipoona linakidhi haja ya kufanya hivyo, Shirika liliweza kuyalipa.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imehoji ongezeko la matumizi ya Tsh. 158,352,287 katika matumizi ya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Shirika na Uongozi wa Shirika kueleza kuwa, wao hawana majibu ya kutosha ya fedha hizo kwa sababu zimetoka moja kwa moja Serikali Kuu kwenda kwa Wakala wa Majengo. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa, fedha hizo zimeongozeka kutokana na agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mstaafu, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kuombwa kufuatia ziara yake aliyoifanya kwenye Shirika hilo.

Vile vile Kamati ilihitaji kupatiwa mnyambuliko wa fedha zilizotumika kwa matumizi ya 'Purchase of non corrent assets' lakini haikuweza kupatiwa kwa siku hiyo na badala yake Shirika liliahidi kuiwasilisha baadae kwa Kamati. Aidha, Kamati haikupatiwa ufafanuzi wa kina juu ya 'Net Increase / Net Decrease' kwa kisingizio cha kuelezwa kuwa Shirika halina Mhasibu kwani wakati ilipofika na kufanya kazi, alikuwa amekwenda kujifungua.

Kwa ujumla wake, Kamati haikuridhishwa na matayarisho ya Uongozi wa Shirika, wakati Kamati ilitoa taarifa za mahitaji yake mapema kwa njia ya barua, lakini Shirika hili halikujitayarisha na kutoa mashirikiano kikamilifu kwa Kamati.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati haikuridhishwa na matayarisho ya Shirika na imeshindwa kupata usahihi wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2017/2018.

3.2: SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)

Taarifa ya Mapato

Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) lilikadiriwa kukusanya Tsh. 3,169,900,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali. Kati ya hizo, Tsh. 2,569,900,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 600,000,000 ikiwa ni makusanyo ya vyanzo vya ndani vya Shirika.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 3,582,622,247 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali ikiwa ni sawa na 113% ya makadirio. Kati ya hizo, Tsh. 2,572,757,355 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 1,009,864,892 ikiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani vya Shirika.

Majibu ya Shirika

Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni sahihi na kama zinavyoainishwa hapa chini:-

Nam	Chanzo cha Mapato	Makadirio	Mapato Halisi	Asilimia
1.	Ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali	2,569,900,000	2,572,757,355	100%
2.	Makusanyo ya ndani	600,000,000	1,009,864,892	168.3%
Jumla		**3,169,900,000**	**3,582,622,247**	**113%**

Shirika lilieleza sababu za kuongezeka kwa mapato hayo kwa kiwango cha 113% ni kama zifuatazo:

- Kuongezeka kwa waajiriwa wapya katika eneo la ufundi, watayarishaji wa vipindi, wapiga picha na Afisa Manunuzi kulipelekea kuongezeka kwa ruzuku ya mishahara kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.
- Kubadilishwa kwa ngazi za mishahara kwa wafanyakazi waliorudi masomoni katika kada za utumishi, manunuzi, secretary, waandishi pamoja na mafundi, kulipelekea kuongezeka kwa ruzuku ya mishahara kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.
- Kulipwa kwa posho la mazingira magumu kwenye mishahara ya wafanyakazi wa kada za ufundi, utangazaji, wapiga picha, waandishi na watayarishaji vipindi.
- Kuongezeka kwa vipindi vya kulipiwa na kuanza kulipiwa kwa LIVE PROGRAM kwa taasisi za Serikali na binafsi, kulipelekea kuongezeka kwa makusanyo ya

vyanzo vya ndani.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imeelezwa makusanyo ya ndani ya Shirika pamoja na mambo mengine, ikiwa ni pamoja na matangazo ya kulipia na kodi ya minara. Matangazo hayo ni ya vifo, matangazo maalum na matangazo ya biashara. Kamati iligundua Shirika limetumia pesa za makusanyo kwa matumizi ya ruzuku kinyume na bajeti ya Shirika na kinyume na ridhaa ya Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika.

Mapendekezo ya Kamati

Ni vyema Uongozi wa Shirika ukasimamia ipasavyo vyanzo vyake vya mapato, ili kudhibiti kuvuja kwa mapato hayo. Aidha, elimu inahitajika kwa viongozi wa Shirika kuhakikisha wanakusanya mapato yao kama ilivyoidhinishwa na Bodi yao ya Wakurugenzi ambayo ndio yenye dhamana ya kuidhinisha bajeti ya makusanyo ya Shirika hilo.

Taarifa ya Matumizi

Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 3,169,900,000 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kati ya hizo, Tsh. 3,118,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 51,900,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 3,557,328,958 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na 112% ya makadirio. Kati ya hizo, Tsh. 3,530,283,370 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 27,045,588 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Majibu ya Shirika

Shirika lilifanya matumizi yake kwa kuzingatia mchanganuo ufuatao:-

Nam		**Makadirio**	**Matumizi Halisi**	**Asilimia**
1.	Matumizi ya Kawaida	3,118,000,000	3,530,283,370	113.2%
2.	Kazi za Maendeleo	51,900,000	27,045,588	52.1%
Jumla		**3,169,900,000**	**3,557,328,958**	**112%**

Aidha, sababu za kuongezeka kwa matumizi kwa asilimia 12 ni kama ifuatavyo:

- Kuongezeka kwa mishahara ya waajiriwa wapya katika eneo la ufundi,

watayarishaji vipindi, wapiga picha na Afisa Manunuzi, kulipelekea ongezeko la matumizi.

- Kubadilishwa kwa ngazi za mishahara kwa wafanyakazi waliorudi masomoni katika kada za utumishi, manunuzi, secretary, waandishi pamoja na mafundi kulipelekea ongezeko la mishahara kwa Shirika.
- Kulipwa kwa posho la mazingira magumu kwenye mishahara ya wafanyakazi wa kada za ufundi, utangazaji, wapiga picha, waandishi na watayarishaji vipindi.
- Ongezeko la matumizi ya mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wafanyakazi wa Shirika la Utangazaji, nje na ndani ya nchi.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imejiridhisha kuwa, Shirika lilifanya matumizi ya fedha zake kwa mwaka 2017/2018 bila ya kuwa na Bodi ya Zabuni wala Kitengo cha Manunuzi, na hivyo lilitegemea zaidi Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Manunuzi cha Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ya wakati huo. Aidha, Shirika kwa mwaka 2017/2018 halikuwa na Mpango wa Manunuzi, na hivyo ilifanya matumizi ya fedha zilizoidhinishwa bila ya kufuata mpango huo.

Aidha, Kamati imeshtushwa na kiwango kikubwa cha malipo ya posho walilokuwa wanalipana Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Utangazaji Zanzibar, takriban kulikuwa na matumizi mabaya ya fedha za Shirika. Kwa mfano, Ndg. Nasra Moh'd Hilali ambae alikuwa Mwenyekiti mwaka 2017/2018, alikuwa alilipwa takriban Tsh. 668,000 kwa kikao cha tarehe 6 Oktoba 2017. Aidha, Ndg. Imane O. Duwe alilipwa Tsh. 518,000 na Ndg. Nassor Rajab Dachi alilipwa Tsh. 988,000 huku Ndg. Kombo Shaame Kai alilipwa Tsh. 1,258,000 kwa kikao cha siku hiyo.

Vile vile, Kamati imejiridhisha kuwa, Shirika kwa mwaka 2017/2018 halikuwa na Daftari Moja la Kumbu kumbu (Fixed Asset Register), ingawaje wakati wa ukaguzi wa Kamati, Daftari hilo lilikwishapatikana tokea mwaka 2019. Vile vile, Kamati imepitia baadhi ya taarifa za Mafuta ya 'Diesel' ya Shirika na kukukta mapungu kadhaa ikiwa ni pamoja na kutooneshwa mapokezi ya jumla ya mafuta hayo, kukosekana kwa 'Sign' ya mpokeaji, hakuna taarifa za muda wa kupokelewa kwake na kutoandikwa kwa aina ya gari iliyoingizwa mafuta hayo.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati haikuridhishwa na matumizi ya Shirika na imejiridhisha kuwa, kwa mwana 2017/2018, Viongozi wa Bodi ya Shirika na Uongozi wa Shirika, umetumia vibaya fedha za Shirika. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua za kuwawajibisha

viongozi wanaohusika na matumizi mabaya ya fedha za Umma.

3.2.1 Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato

Ukaguzi umebaini kwamba, Shirika la Utangazaji Zanzibar halina usimamizi mzuri katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na huduma ya uendeshaji wa vituo mbali mbali vya kurushia matangazo. Vituo vingi vya utangazaji vinafanya kazi zake za urushaji wa matangazo kwa kutumia minara ya Shirika bila ya kulipia huduma hiyo kwa muda mrefu.

Aidha, ukaguzi umebaini baadhi ya vituo vya urushaji wa matangazo vinatumia huduma hiyo bila ya kuwa na mkataba wa utoaji wa huduma hiyo ambao utaeleza thamani halisi inayotakiwa kulipwa kwa mujibu wa huduma hiyo. Kutokuwepo kwa mikataba hiyo kunapelekea kutokujua thamani halisi ya fedha inayotakiwa kulipwa na fedha inayodaiwa kwa taasisi husika. Hali halisi ni kama inavyoonekana hapo chini:-

Nam	Kituo cha Urushaji wa Matangazo	Tarehe ya mwisho ya Matumizi ya Mkataba	Kinachodaiwa
1.	Chuchu Media Ltd	1/7/2017 – 30/6/2018	4,000,000
2.	Zan Link	Hakuna mkataba	Haijulikani kima cha fedha kinachodaiwa
3.	China Radio International (CRI)	Hakuna mkataba	Haijulikani kima cha fedha kinachodaiwa
4.	British Broadcasting Corporation (BBC)	Hakuna mkataba	Haijulikani kima cha fedha kinachodaiwa
5.	Helios Tower Tanzania Limited (HTT)	Hakuna mkataba	Haijulikani kima cha fedha kinachodaiwa

Majibu ya Shirika

Vituo vyote viavyotumia huduma za Shirika vina mikataba maalum. Vituo

vilivyoainishwa katika ukaguzi kwa mwaka 2017/2018 kuwa havina mikataba, mikataba yao ipo na inaendelea kutumika. Mikataba hiyo ina viwango maalum vinavyolipiwa kwa kila kipindi husika. Jadweli liliopo hapa chini linaonesha kituo husika, tarehe ya mkataba na kiasi wanachotakiwa kulipa:

Nam	Kituo cha Urushaji wa Matangazo	Tarehe ya Mkataba	Kiasi Kinachotakiwa kulipwa
1.	Chuchu Media Ltd	1/7/2017 – 30/6/2018	4,000,000 = kimelipwa
2.	Zan Link	31 July 2017	USD 3,000 Annually
3.	China Radio International (CRI)	26th February, 2018	USD 33,340.00 Annually
4.	British Broadcasting Corporation (BBC)		USD 15,000 Annually
5.	Helios Tower Tanzania Limited (HTT)	13th March, 2013	USD 1,000 per Month

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imeshuhudia Mikataba iliyowasilishwa kwake wakati wa ukaguzi, Hata hivyo, Kamati imeikagua Mikataba hiyo na kukuta kasoro kadhaa ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Zan Link ambao ulitakiwa usainiwe na 'Accounting Officer' ambae ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika, lakini kinyume chake umesainiwa na Fundi Mussa kama ni Msimamizi Mkuu.

Aidha, Mkataba wa Biritish Broadcasting Corporation (BBC) ni wa muda mrefu na ulitakiwa ufanyiwe marejeo (reviewed) kwa kila miaka mitano, lakini Mkataba huo haujafanyiwa mapitio yoyote, na hivyo wakati wa ukaguzi umekosa uhalali kwa sababu ya kupitwa na muda. Mkataba wa 'Helios Tower Tanzania Limited (HTT)' umehusisha ardhi na sio mnara. Kwani Kampuni hiyo imekodi eneo la ZBC na kuweka mnara wake.

Vile vile Kamati ilifanya ukaguzi katika mnara wa Shirika uliopo Masingini na kugundua mambo mbali mbali ikiwa ni pamoja na ukubwa wa gharama za umeme zinazotumika kuendeshea mnara huo.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaishauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kazi kwa umakini zaidi na ijiridhishe juu ya kuwepo au kukosekana kwa taarifa inazozihitaji, hasa mikataba katika taasisi husika.

3.3: CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI

Taarifa ya Mapato

Chuo cha Kilimo Kizimbani kilikadiriwa kukusanya Tsh. 1,331,762,480 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali, kati ya hizo Tsh. 886,045,480 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 445,717,000 ikiwa ni makusanyo ya vyanzo vya ndani.

Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 1,194,890,795 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali ikiwa ni sawa na 89.7 ya makadirio. Kati ya hizo, jumla ya Tsh. 881,393,895 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 313,496,900 ikiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani.

Majibu ya Chuo

Mapato kwa kilichokuwa Chuo cha Kilimo Kizimbani yameongezeka kutoka Tsh. 915,625,219 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, Chuo cha Kilimo Kizimbani kilikusanya Tsh. 1,194,890,795 kutoka katika vyanzo vyake vine vya mapto, sawa na 30, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 279,265,576 la makadirio.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Chuo kina bajeti ya asili (Origanal) na ya mwisho (Final) kwa kuwa katika mwaka huo wa fedha Chuo kiliifanyia mapitio bajeti yao.
2. Wizara ya Kilimo ilimteua Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Dahalia za Chuo cha Kilimo Kizimbani, ambapo Mkandarasi huyo anadai kuwa anaidai Wizara jumla ya Tsh. 65,000,000. Kwa kuwa shughuli yote ilisimamiwa na Wizara, Chuo hakina kumbukumbu ya malipo yaliyofanyika. Hata hivyo, Chuo kimemkabidhi Mkandarasi huyo Wizarani kwa ajili ya kulisema suala hilo pamoja na kulipwa fedha zake, isipokuwa kwamba, katika mwaka wa fedha 2018/2019 malipo hayo hayajaoneshwa.

Mapendekezo ya Kamati

Taasisi za Serikali zihakikishe kuwa zinahifadhi vizuri kumbukumbu mbali mbali ili ziweza kuwa na uhakika ya kile kinachodaiwa.

Taarifa ya Matumizi

Chuo cha Kilimo Kizimbani kilikadiriwa kutumia Tsh. 1,327,031,275 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 1,217,425,820 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida ambazo ni sawa na 91.7%. ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Matumizi kwa kilichokuwa Chuo cha Kilimo Kizimbani yameongezeka kutoka Tsh. 905,029,670 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, matumizi yalikuwa ya jumla ya Tsh. 1,217,425,820 ikiwa kama ongezeko la Tsh. 312,396,150 sawa na 34.5% ya ongezeko la matumizi kwa kazi za kawaida, mishahara, tafiti na ushauri.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kuwa Chuo hakina utaratibu wa kufanya tathmini katika miradi inayotekeleza, hivyo, miradi hiyo haiwezi kujulikana mradi husika ulileta tija ya kiasi gani.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imekishauri Chuo kufanya tathmini juu ya miradi yote inayoitekeleza ili kujua mafanikio yaliyopatikana katika miradi hiyo, ingawa miradi hiyo haijaanzishwa moja kwa moja na Chuo.

Vile vile, Kamati ya LAAC imebaini kuwa sehemu ya eneo la Chuo limepewa Kitengo cha Utafiti jambo linalopelekea Chuo kicho kuwa na eneo finyu la kufanyia shughuli zake.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuwatafutia Kitengo cha Utafiti eneo jengine ili Chuo kipate kulitumia eneo lake hilo ipasavyo.

3.4: MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilikadiriwa kukusanya Tsh. 17,727,947,387 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali. Kati ya hizo, Tsh. 11,820,000,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 5,907,947,387 ikiwa ni makusanyo ya vyanzo vya ndani. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 18,375,430,857 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali ikiwa ni sawa na 104% ya makadirio. Kati ya hizo, Tsh. 15,242,115,985 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 3,133,314,875 ikiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka imepata 104% ya makadirio kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ongezeko hilo limetokana na sababu kuu ya kupata fedha zenye jumla ya Tsh. 9.1 bilioni kwa ajili ya marejesho ya bima kutoka kwa kampuni ya Jubilee Insurance. Marejesho hayo yakiwa ni “advance payment” pamoja na “performance bond” zinazotokana na kufilisika kwa mkandarasi ‘SPENCON COOPERATION’ kupitia mradi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Magharibi (ZUWSP).

Uchunguzi wa Kamati

Kumekuwa na ugumu wa kupatikana taarifa sahihi na fasaha zinazohusiana na miradi ya ZAWA, kwani hata Kamati ilipohoji taratibu za upatikanaji wa Kampuni ya SPENCON COOPERATION ilielezwa kuwa, ZAWA hawakuhusika na kupatikana kwake, bali ni mkataba baina ya Serikali na African Development Bank (ADB), ambapo ADB ndio hatimae waliopendekeza kupatikana kwa Kampuni ya SPENCON. Aidha, Kamati imejiridhisha kuwa, Mamlaka ya Maji Zanzibar ilipokea Tsh. 500,000,000 kutoka ZURA baada ya kuomba Tsh. 100,000,000 lakini uchambuzi wa fedha hizo na usahihi wake umefichwa.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inapendekeza Serikali kusimamia kwa karibu makusanyo ya mapato yanayosimamiwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar, kwani kuna dalili kubwa za upotevu wa mapato hayo na Uongozi haufatilii ipasavyo wala haidhibiti ipasavyo mapato yake yanayotokana na vyanzo vyake vya mapato.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilikadiriwa kutumia Tsh. 17,727,947,387 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 13,241,618,931 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida ambazo ni sawa na 75% ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka imetumia 75% ya makadirio, upungufu wa matumizi hayo kwa 25% umetokana na sababu kuu zifuatazo:

- Kupungua kwa matumizi ya kawaida ya Mamlaka “Other Charges” kumetokana na kupungua kwa makusanyo ya ndani ambayo yamefikia 53% ya makadirio.

- Sababu kuu iliyopelekea makusanyo ya ndani kutofikia malengo, kumetokana na mwitiko mdogo wa wananchi kuchangia huduma ya maji ambapo watumiaji wengi wanachangia kiwango cha Tsh. 4,000 kwa mwezi kutokana na upungufu wa mita kwa watumiaji wengi wa Taasisi.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imegundua kuwa, Mamlaka ya Maji Pemba walirejesha Unguja fedha za matumizi kukamilisha taratibu za manunuzi, hali inayodhihirisha kuwa, Mamlaka kwa upande wa Pemba haikuwa na uwezo wa kufanya matumizi kwa thamani ya fedha inayohitaji kuitishwa zabuni. Hivyo, Afisi ya Mamlaka ya Maji Unguja ndiyo inayofanya manunuzi yote na kupeleka Pemba kwa matumizi pekee.

Mapendekezo ya Kamati

Serikali iiwezeshe Afisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar, kwa upande wa Pemba ili itekeleze majukumu yake kwa uhuru na mamlaka kamili kama Afisi inayojitegemea na sio kila kuendelea kutegemea hata manunuzi yake lazima yafanyike Afisi Kuu, Unguja.

Ni vyema Serikali ikasimamia kwa karibu sana matumizi ya ZAWA, kwani Kamati imegundua kasoro nyingi imekuwa na mashaka na uadilifu wa matumizi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar.

3.4.1 Kutokamilika kwa baadhi ya visima vya mradi wa Ras El Kheimah Unguja na Pemba, Tsh. 1,835,645,325.68

Katika kipindi cha mwaka 2017/2018, jumla ya Tsh. 1,835,645,325.68 zilitumika kwa ukamilishaji wa visima vya mradi wa Ras el Kheimah vilivyochimbwa Unguja na Pemba. Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kuharakisha upatikanaji wa vifaa mbali mbali ili kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Ukaguzi umebaini kwamba, kuna baadhi ya visima bado havijakamilika kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa jamii. Baadhi ya visima hivyo ni kama ifuatavyo:

Nam	Visima vya Unguja na Pemba
1.	Jambiani Kikadini
2.	Mbuzini Meli Nane
3.	Bumbwini Misufini
4.	Mzungu Punda – Dole

5.	Fuoni Chunga – U26
6.	Moga Kibeberu Gamba
7.	Kilindini Micheweni
8.	Shumba Viamboni
9.	Gombani Mchuwa

Majibu ya Mamlaka

Ras el Kheimah ni mradi uliotokana na mazungumzo yaliyofanywa baina ya Ras el Kheimah na Mamlaka ya Maji Zanzibar. Hata hivyo, makubaliano ya Kimkataba yalifanywa na Serikali na Ras el Kheiman, huku Mamlaka ya Maji Zanzibar haikuhusika na Mkataba huo.

Uongozi wa ZAWA ulipoelezwa kuhusiana na visima hivyo, haukuridhika na kuona kuwa havifai kwa matumizi. Maoni yao yalizingatiwa kidogo lakini sio kwa kiwango walichokikusidia. Aidha, ZAWA hawakuhusika hata kidogo na ununuzi wa pumps za visima hivyo. Serikali ndio iliyobeba jukumu la kuviendeleza visima hivyo 150 kwa kuvichimba, kutia pumps, kutia umeme na mambo mengine, huku ZAWA ikihusishwa pekee katika kuviendeleza visima hivyo.

Aidha, kuhusiana na hoja hii, ZAWA wanakiri kuwa wakati wa ukaguzi, Mradi huo ulikuwa haujakamilika lakini hivi sasa mradi wa visima hivyo, umeshakamilika na visima hivyo vilivyoainishwa na Mkaguzi, vinafanya kazi. Aidha, kwa upande wa Pemba kwenye visima vya Kilindi Micheweni, Shumba Viamboni na Gombani Mchuwa tayari vimeshakamilika na vinatoa huduma.

Aidha, ZAWA wamejenga vibanda wenyewe kwa gharama zao katika visima hivyo na hivyo kila kisima kina kibanda kimoja. Miongoni mwa visima hivyo vilimalizika mwaka 2019 na vyengine 2020. Aidha, visima hivyo havikuweza kukamilika mwaka 2017/2018, kwa sababu fedha zilizopatikana mwaka huo hazikutosheleza kumaliza kujengwa kwa visima hivyo.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na maelezo yaliyoelezwa na Mamlaka, Kamati imeshangazwa na majibu yao kuwa wao ndio waliochimba visima hivyo na Ras el Kheimah walihusika na kuviendeleza tu, kinyume na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, Kamati imejiridhisha kuwa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni sahihi kuwa, fedha zimetoka kwa wakati na Mdhibiti alizikagua kama alivyoeleza katika

ripoti yake na alipofika katika eneo la utekelezaji, bado visima hivyo vilikuwa havijakamilika.

Katika kuvifuatilia visima hivyo, Kamati imefanya ukaguzi kwa baadhi ya visima hivyo na kugundua kuwekewa ulinzi kwa walinzi walioajiriwa na ZAWA na wengine wananchi wa jirani wameajiriwa kwa mkataba wa mwaka mmoja na kulipwa Tsh.100,000 kama sabuni. Hata hivyo, Kamati haikupata kuikagua mikataba hiyo. Aidha, kuna baadhi ya visima maeneo yao yamevamiwa na wananchi kwa shughuli za ujenzi. Kisima cha Mbuzini Meli Nane kimefukiwa na mvua za masika, ZAWA wamekisafisha kisima hicho na kutaraji kukiendeleza hapo baadae.

Aidha, kuhusiana na visima vilivyopo Pemba ambavyo ni Kilindini Micheweni, Shumba Viamboni na Gombani Mchuwa, Kamati ilielezwa kuwa vimetumia Tsh. 58,625,200. Hata hivyo, Kamati imejuilishwa kuwa, jumla ya Tsh. 4,040,000 fedha za Mwakilishi zilitolewa kwa kisima cha Kilindini Micheweni.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaitaka Serikali izingatie umuhimu wa kuzishirikisha kikamilifu Taasisi husika katika usimamizi wa miradi inayokusudiwa kuwaletea wananchi maendeleo kupitia kwa Taasisi hizo. Kitendo cha Wizara inayohusika na fedha kusimamia manunuzi yote ya mradi wa Ras el Kheimah hakileti tija kwa maendeleo ya wananchi.

3.5: MAMLAKA YA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Vitega Uchumi (ZIPA) ilikadiriwa kukusanya Tsh. 3,614,120,300 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali, kati ya hizo Tsh. 843,400,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini, Tsh. 1,557,349,300 ikiwa ni makusanyo ya vyanzo vya ndani, Tsh. 763,371,000 ikiwa ni misaada na Tsh. 450,000,000 ikiwa ni mkopo kutoka Serikalini.

Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 2,225,588,021 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali ikiwa ni sawa na 62% ya makadirio. Kati ya hizo, jumla ya Tsh. 843,400,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini, Tsh. 1,275,385,733 ikiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani na Tsh. 106,802,288 ikiwa ni misaada kutoka Serikalini.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) haikufikia lengo la makusanyo kwa mwaka 2017/2018 kama inavyoelezwa katika Jadweli la hapa chini:

Na	Maelezo	Makisio kwa	Mapato	Tofauti na	Asili	Maelezo

		Mwaka	Halisi kwa mwaka	Makisio na Mapato Halisi	mia ya Mapato kwa mwaka	
1.	Kodi ya mabanda	773,289,300	496,329,817.39	276,959,482.61	64.18	Kupungua huko kunatokana na madeni ya baadhi ya wawekezaji: mfano Zanzibar (Quality, Zantel, SHAMON, Safari Co. Savannah Rag, n.k)
2.	Leseni	466,935,000	375,293,640	91,641,360	80.37	
3.	Ada ya huduma	300,625,000	378,485,655.88	(77,860,655.88)	125.90	Mamlaka imevuka lengo. Hii inatokana na kupata 5% ya makusanyo ya msamaha wa ushuru kwa miradi mikubwa kama vile ZSSF, Lootah, CPS, Azam diary, ZANTEL, uhaulishaji wa hisa za kwa mradi wa LaRosa Dei Venti, Kiwengwa Ltd, Palolo Co.Ltd.

4.	Fomu za maombi	7,000,000	10,557,200	(3,557,200)	150.82	Lengo limefikiwa kwa sababu ya muamko wa wawekezaji kuekeza Zanzibar kutokana na vivutio vingi vya uwekezaji
5.	Mapato mengineyo	9,500,000	14,719,420	(5,219,420)	154.94	Lengo limefikiwa kutokana na mwamko kwa wawekezaji kujitangaza kupitia katika kalenda au "Guideline"
6.	Ruzuku	843,400,000	843,400,000	0	100	
7.	Washirika wa Maendeleo (ADB, UNDP)	763,371,000	106,802,287.50	656,568,712.50	13.99	Hii inatokana na ucheleweshaji wa kupata fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo na taratibu za upatikanaji wa fedha zinachukua muda mrefu
8.	Mfuko Mkuu wa Serikali	450,000,000	0	450,000,000	0	Fedha zilizopangwa hazikupatikana
Jumla		**3,614,120,300**	**2,225,588,020.77**	**1,388,532,279.23**	**61.58**	

Uchunguzi wa Kamati

Mamlaka imejikusanyia mapato ya 62% kwa sababu tofauti ikiwa ni pamoja na kukosa fedha Serikalini, kuchelewa kuingia kwa fedha za washirika wa maendeleo na kupungua kutokana na Mamlaka kulipa madeni. Aidha, Kamati imejiridhisha kuwa, Mamlaka imeshindwa kufikia lengo la makusanyo yake kutokana na kutoona umuhimu wa kuyafuatilia madeni yake inayowadai wadaiwa wake kwa nguvu za Kisheria, pamoja na ukweli kuwa wawekezaji waliowengi wa Mamlaka, wanakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na kushuka kwa biashara ulimwenguni kwa sababu moja au nyengine.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaishauri Mamlaka kusimamia Sheria katika kufuatilia madeni yake kwa wawekezaji mbali mbali wanaokodi maeneo mbali mbali ya Mamlaka. Kuendelea kuwaridhia wawekezaji na kutofuatilia kwa karibu madeni yao, kutaendelea kuikosesha Mamlaka mapato yake ya kiwal mwaka.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Vitega Uchumi (ZIPA) ilikadiriwa kutumia Tsh. 3,614,120,300 kwa mwaka 2017/2018. Kati ya hizo, Tsh. 3,418,057,400 ikiwa ni matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 196,062,900 ikiwa ni matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 1,888,084,828 ziliingizwa, kati ya hizo, jumla ya Tsh. 1,862,410,428 zilitumika kwa kazi za kawaida, sawa na 54% ya makadirio na Tsh. 25,674,400 zilitumika kwa kazi za maendeleo, sawa na 13% ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Matumizi ya Mamlaka yameonekana kutofikia lengo kwa mwaka huu wa fedha. Hali hii ilitokana na kutotekelezwa kwa shughuli mbali mbali zilizopangwa kutokana na upungufu wa fedha hasa zile zilizotegemewa kutoka kwa mfadhili na Mfuko Mkuu wa Serikali. Taarifa ya matumizi ya Mamlaka ni kama inavyoonekana katika Jadweli hii ifuatayo:-

Na	Shughuli zilizopangwa	Makisio ya Matumizi kwa 2017/2018	Matumizi Halisi kwa mwaka 2017/2018	Tofauti	Asilimia ya Matumizi	Maelezo

					kwa mwaka	
1.	Kushajiisha wawekezaji wa ndani na nje kuekeza nchini, kurahisisha huduma kwa wawekezaji na kuendeleza huduma TEHAMA na maktaba, kushiriki katika ziara za uenezi, kutoa matangazo, kuchapisha nyaraka za uenezi, kuendeleza uanachama	882,710,000	369,333,344.50	513,376,655.50	41.84	Kuchelewa kwa fedha kutoka kwa wafadhili kulichelewesha kazi katika kupatikana vitendea kazi zaidi kwa wafanyakazi wa One Stop Centre. Vile vile safari za uenezi zilipunguzwa
2.	Kuendeleza utafiti mitaji binafsi na juu ya fursa mpya za uwekezaji	102,260,000	13,558,900	88,701,100	13.26	Kuchelewa kwa fedha kutoka kwa wafadhili kulipelekea baadhi ya kazi kutotekelezwa kwa wakati hasa zile za utafiti
3.	Kuimarisha mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji katika maeneo	532,840,000	71,169,530	461,670,470	13.36	Uhaba wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo kuingiza fedha kwa wakati wa

	huru ya uchumi					'Master Plan' ya eneo la Micheweni
4.	Masuala ya kiutawala na mahitaji mengine katika kufanikisha kazi za Mamlaka	2,096,310,300	1,434,023,053.06	662,287,246.94	68.41	Baadhi ya kazi hazikutekelezwa kwa wakati kama vile ukarabati wa jengo la ofisi ya ZIPA Maruhubi, ujenzi wa Ofisi ya ZIPA Pemba
Jumla		**3,614,120,300**	**1,888,084,827.56**	**1,726,035,472.44**	**52.24**	

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imebaini na kukubaliana na Mamlaka kuwa, kukosekana kwa fedha kutoka Serikalini, kumekwamisha juhudi za Mamlaka kutekeleza malengo yake iliyojiwekea. Aidha, kwa fedha wafadhili wa ADB pamoja na UNDP, Mamlaka hupeleka 'Terms of Reference' tu, lakini matumizi yote yanafanywa na Serikali kuu.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaitaka Serikali Kuu hasa Wizara inayohusiana na fedha kuhakikisha kuwa, Taasisi husika inashirikishwa ipasavyo katika kuandaa, kutekeleza na kuisimamia miradi inayohusu Taasisi hizo. Sio busara kwa Wizara kusimamia miradi hiyo, wakati watekelezaji na wasimamizi wakawa hawahusiki na usimamizi wa miradi hiyo, hasa katika eneo la matumizi ya fedha za miradi hiyo.

3.5.1 Wadaiwa wa Mamlaka Tsh. 1,867,389,598

Ukaguzi umebaini kwamba, jumla ya Tsh. 1,867,389,598 ni deni wanalodai Mamlaka ya ViteganUchumi kwa Makampuni mbali mbali yaliyoweka vitega uchumi katika maeneo ya Zanzibar. Waidaiwa hao ni kama wanavyoonekana hapa chini:-

Na.	Mhusika / Mdaiwa	Idadi ya fedha (Shilingi)
1.	Almahra Processing	83,581,212
2.	ASAALAM	68,520,000

3.	AUTOZONE (LTD)	19,199,875
4.	Blue Horizon	303,733,712
5.	Best Import	5,025,000
6.	Breik Motor	16,396,835
7.	CITY Motor	1,598,000
8.	FLEMINGO INTERNATIONAL LTD	14,862,675
9.	Fumba Beach Lodge	192,166,000
10.	Hakuna Matata Used Car	8,858,340
11.	HLS Management	44,428,800
12.	ISSZAI Motor	20,566,430
13.	Malik Food	112,823,524
14.	Marco Polo	4,382,817
15.	MD Motor	5,338,418
16.	Mtoni Motor	27,038,075
17.	OZTI	66,568,560
18.	Relaxo Footwear (HAWAII)	21,840,000
19.	ROYAL MOTORS	24,208,520
20.	SAFARI CO. LTD	93,862,504
21.	Savannah Rags Int. Ltd	55,340,220
22.	SHAMON	111,842,173
23.	SM Motor	4,989,004
24.	SUCCESS Motors	22,606,701
25.	Super shine	8,939,000
26.	SWABI Motor	13,216,000

27.	TANTEX	32,349,700
28.	VISIWANI MOTORS	29,372,598
29.	ZAN BOTTLING	88,476,981
30.	ZANTEL	37,189,521
31.	ZANOP	10,560,000
32.	Zanzibar Fashion	44,323,517
33.	SISSAN Enterprises	3,000,000
34.	Zanzibar Quality	162,916,833
35.	Zanzibar Spare parts	34,352,036
36.	ZAREC	48,214,517
37.	Zenj Motor	24,701,500
JUMLA		**1,867,389,598**

Majibu ya Mamlaka

Yapo yale madeni ambayo miradi yao iliidhinishwa na wawekezaji hao walikodishwa mabanda kwa mkataba na makubaliano ya kodi lakini walishindwa kuanza utekelezaji kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo kukosa nafasi/ardhi stahiki kwa shughuli za msingi za uwekezaji wake. Kwa kuwa deni hili linatokana na pango la mabanda ambalo hukuwa kadri ya muda unavyosonga na kuwa na muda mrefu ulipita, licha ya kuwa kwa sasa mabanda hayo yamepatiwa mwekezaji mwengine, deni hili bado lipo katika rikodi za Mamlaka. Uwezekano wa muwekezaji kuendelea na mradi haupo kwa sasa hali inayopelekea kusababisha ugumu wa kulipa deni hili. Miradi ya magari vile vile imeshindwa kufanya kazi lakini Mamlaka imejikuta katika njia panda baina ya kudai na kuomba kufutwa kwa deni hili kwa kupitia utaratibu unaokubalika.

Kuna miradi ambayo inafanya kazi lakini imekuwa na madeni. Mamlaka inategemea kuwa yatalipika ja juhudi za kuyakusanya madeni hayo zimeimarishwa. Baada ya kuweka mikakati kama vile ya kuwaandikia barua za ukumbusho, kuwafuatilia mmoja mmoja na kwa kuwanyima baadhi ya huduma mpaka walipe, kumeonesha dalili ya kulipwa madeni hayo. Pia yapo madeni ya miradi ambayo inaendelea na shughuli zake lakini kutokana na mwenendo wa biashara, malipo yanafanywa kulingana na mapato

yao, hivyo deni hulimbikizika kwa kuwa malipo yanategemea uwezo wa ulipaji wao.

Vile vile kuna banda ambalo linatumika na kampuni ya ushoni ya vikosi vya Idara Maalum za Serikali. Tokea kuanzishwa kwake na kupewa banda, licha ya juhudi mbali mbali za kudai na kukumbusha deni hili, halijawahi kulipia pango hilo. Kwa kuwa mdhamini mkuu wa kampuni hii ni Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Mamlaka inaona kuwa ni wakati muafaka kulipatia ufumbuzi suala hili. Yale ambayo Mamlaka inategemea kuwa yatalipika na juhudi za kuyakusanya madeni hayo zimeimarishwa. Hivyo, uhalisia wa ulipwaji wa madeni hayo ni kama ifuatavyo:-

Hali Halisi ya Ukusanyaji wa madeni kwa wawekezaji kwa mwaka 2017/2018

Na.	Mhusika / Mdaiwa	Idadi ya fedha (Shilingi) zinazodaiwa	Deni linalodaiwa hadi kumaliza mwaka 2017/2018 (Tsh)	Malezo
1.	Fumba Beach Lodge	192,166,000	173,159,000	Wamepunguza Tsh. 19,007,000
2.	Malik Food	112,823,524	112,823,524	Alikumbushwa kulipa deni. Hatua zinazoendelea ni kuufuta mradi Kisheria na kuangalia jinsi gani deni litalipwa
3.	OZTI	66,568,560	36,798,560	Wamelipa Tsh. 29,770,000
4.	SHAMON	111,842,173	70,932,173	Wamelipa Tsh. 40,910,000
5.	ZAN BOTTLING	88,476,981	88,476,981	
6.	SAFARI CO. LTD	93,862,504	0	Wamelipa

7.	Savannah Rags Int. Ltd	55,340,220	0	Wamelipa
8.	Best Import	5,025,000	0	Wamelipa
9.	Mtoni Motor	27,038,075	27,038,075	
10.	Relaxo Footwear (HAWAII)	21,840,000	21,840,000	
11.	ROYAL MOTORS	24,208,520	24,208,520	
12.	TANTEX	32,349,700	16,697,155	Wamelipa Tsh. 15,652,542
13.	ZANOP	10,560,000	5,221,200	
14.	SISSAN Enterprises	3,000,000	0	Wamelipa
15.	Zanzibar Fashion	44,323,517	44,323,517	
	Zanzibar Spare parts	34,352,036	9,313,486	Wamelipa Tsh. 25,038,550
16.	ZANTEL	37,189,521	0	Wamelipa
17.	Zenj Motor	24,701,500	24,701,500	
JUMLA		**1,143,245,864**	**814,591,419**	

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipofanya mahojiano na Mamlaka, kufanya ziara kwa baadhi ya wadaiwa wake na kukaa pamoja baina ya Mamlaka na Wadaiwa hao ilibaini kuwa, Mamlaka imekodisha na kufuatilia madeni yake kwa njia zaidi ya maelewano kuliko njia ya nguvu za kisheria. Hali hii inaifanya Mamlaka kufuatilia wadaiwa wake kwa kuwaridhia na kuangalia hali halisi ya kiuchumi na athari zake. Aidha, Mamlaka inadai wadaiwa wake kirafiki zaidi na inaangalia sana athari za kumfungia biashara zao iwapo wadaiwa hao wataifikisha Mamlaka Mahakamani, bado itabaki ni jukumu la Serikali kumlipa thamani halisi ya vitenga uchumi vyao.

Aidha, wadaiwa wa Mamlaka wanaofanya biashara hasa za utalii, wameathirika sana na janga la maradhi ya Korona (COVID 19), ikiwa ni pamoja na Mdaiwa Fumba Beach Lodge, ambae aliieleza Kamati juu ya athari hizo, wakati Kamati ilipofika eneo alilokodishwa huko Fumba. Muwekezaji huyu amejitahidi kupunguza deni lake lakini

amekwamishwa kwa kuanguka biashara ya utalii kutokana na maradhi ya Covid 19.

Aidha, Kamati ilipokutana na uongozi wa Kampuni ya ASAALAM inayodaiwa Tsh. 68,520,000 ulieleza kuwa Kampuni yao imefikia kiwango hicho cha deni kwa sababu hapo awali kabla ya kuanguka kibiashara, Kampuni hiyo ilikuwa inalipa kodi yake ipasavyo, lakini kuanzia mwaka 2012, ilianguka kibiashara na kuijuulisha Mamlaka juu ya hali hiyo, huku wakitaraji kuinuka kibiashara ili walipe kodi wanayodaiwa. ZIPA imeongea na Kampuni hii na kimsingi imeieleza Kamati mbele yao kuwa hawana tatizo la kulipwa deni lao na hivyo, Mamlaka imeitaka Kampuni kuiandikia rasmi Mamlaka ili kulikabidhi eneo hilo walilokodi na baadae aitwe Mtathmini wa Serikali ili atie thamani, kwa lengo la kufaidika kila upande. Na ikitokea tathmini iliyolipwa ni ndogo kuliko deni linalodaiwa, Kampuni ya ASAALAM itakuwa tayari kulipa deni lililobakia.

Pamoja na Kamati kupokea taarifa ya Kampuni ya ASAALAM kuwa ilipoona hali yake ya kifedha na kibiashara imeyumba, waliiandikia Mamlaka ya Vitega Uchumi barua ya kueleza hali hiyo na utayari wao wa kurejesha eneo walilolikodi, Kamati imebaini kuwa Mamlaka haikujibu chochote kwa barua hiyo, katika barua hiyo.

Kamati ilipoendelea na ziara kwa wawekezaji mbali mbali ikiwa ni pamoja na Malik Food, Zan Bottling, OZTI na hata SHAMON imegundua kiufupi kuanguka kwa biashara zao kwa sababu mbali mbali kumewapunguzia wawekezaji hao uwezo wao wa kulipa kodi kwa Mamlaka na wamekuwa wakisikitika juu ya anguko lao kibiashara, tatizo kubwa Mamlaka haitumii nguvu za kisheria ilizonazo katika kufuatilia madeni ya wadaiwa hao. Hata hivyo, baada ya Kamati kufuatilia madeni hayo, baadhi ya wadaiwa hao waliahidi kulipa madeni yao ikiwa ni pamoja na OZTI waliahidi kulipa USD 4000 kwa mwezi.

Aidha, Pamoja na udhaifu wa Mamlaka kujiwekea utaratibu wa kutotumia nguvu katika kufuatilia madeni ya wadaiwa wake, Kamati imejiridhisha kuwa, Mamlaka ya ZIPA haikuwa ikitoa ushirikiano kamilifu kwa wawekezaji hao wanaoeleza matatizo yao au hali za kiuchumi zinazowakabili kwa njia ya barua, ambapo katika ziara ilizozifanya na kukutana na wawekezaji hao walieleza kuwahi kuandika barua mara kadhaa kwa Mamlaka, lakini hakuna majibu yoyote waliyokuwa wakipokea kutoka kwenye Mamlaka.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaishauri Mamlaka isimamie kwa karibu na kufuatili wadaiwa wake ili wahakikishe wanalipa madeni yao kwa wakati.

Hoja Na. 3.5.2 Ucheleweshwaji wa ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ya Vitega Uchumi, Pemba

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Vitega Uchumi hutumia fedha nyingi kwa kumlipa mmiliki wa nyumba Ndg. Said Ahmed Nassor, kwa ajili ya ukodishwaji wa

sehemu ya ghorofa ya kwanza, nyumba namba 27338, iliyopo Tibirinzi Chake Chake Pemba kwa ajili ya shughuli za Ofisi. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka imetumia Tsh. 33,450,000 kwa ajili ya kulipia gharama za kodi ya Ofisi. Ukaguzi unaishauri Mamlaka kuchukuwa jitihada za makusudi kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ili kuepuka gharama za ulipaji wa kodi kwa kila mwaka.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli Mamlaka ilikodi nyumba hiyo kwa bei ya Tsh. 2,787,500 kwa mwezi kutokana na Mamlaka kukosa Ofisi yake kwa mwaka 2017/2018, na kiwango hicho cha kodi kwa mwezi, ni cha kawaida kwani kuna Ofisi nyingi za Serikali zilizokodi majengo kwa gharama kubwa zaidi kuliko Mamlaka ya Vitega Uchumi. Mamlaka imekodi eneo la Chake Chake kwani ni sehemu muhimu kibiashara na ni rahisi kufikiwa na wawekezaji, kuliko kuitumia ofisi yake iliyopo Micheweni Pemba, ambayo iko mbali na eneo la mji. Hata hivyo, kwa kipindi hiki, Mamlaka imeshahama katika jengo hilo walilolikodi na hivi sasa wamehamia katika majengo ya Serikali yaliyopo Gombani na pia inaendelea na juhudi zake za kujenga ofisi yake mwenyewe.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na Mamlaka kusema kuwa kiwango hicho cha kodi si kikubwa kulinganisha na gharama zinazoingia Taasisi nyengine za Serikali katika kukodi majengo ya Ofisi zao, Kamati imejiridhisha kuwa kiwango cha kodi kwa mwaka cha Tsh. 33,450,000 ni kikubwa na inatosha kwa Mamlaka kujenga Ofisi yake kwa muda ambao imeutumia kukodi jengo hilo.

Aidha, kiwango cha fedha za kodi kilicholipwa kwa mwaka, ingestahiki kwa Mamlaka kuitisha zabuni ili kumpata mtoa huduma kwa taratibu za Kisheria, lakini Kamati haikupata taarifa zozote za Mamlaka kufanya mlinganisho wa gharama za kodi, isipokuwa moja kwa moja imemtumia Ndg. Said Ahmed Nassor, kuwakodisha jengo lake hilo, huku Mkodishaji huyu akiwa ni mtoa huduma pekee ya Ofisi kwa Mamlaka. Aidha, Kamati haikuridhishwa na matumizi ya fedha nyingi za kodi kwa lengo tu la kuwavutia wawekezaji badala ya kuzingatia uwezo halisi wa Mamlaka.

Mapendekezo ya Kamati

Serikali iendelee kujenga majengo mbali mbali ili kuzisaidia Taasisi zake kuepukana na kutumia fedha nyingi za kodi ya majengo kwa matumizi ya Ofisi.

3.6: CHUO CHA UTAWALA WA UMMA – IPA

Taarifa ya Mapato

Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) kilikadiriwa kukusanya Tsh. 3,314,440,000 kwa

mwaka 2017/2018, fedha ambazo zingelikusanywa kutoka vyanzo mbali mbali vya Chuo. Kati ya fedha hizo, jumla ya Tsh. 604,500,000 zikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 2,709,940,000 zikiwa ni makusanyo ya vyanzo vya ndani vya Chuo cha Utawala wa Umma.

Aidha, ilipofikia tarehe 30 Juni 2018, Tsh. 2,623,161,450 zilipatikana kutoka vyanzo mbali mbali ikiwa ni sawa na 79% ya makadirio. Kati ya fedha hizo, Tsh. 625,943,755 zikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 1,997,217,695 zikiwa ni makusanyo halisi kutoka vyanzo vya ndani vya Chuo hiki.

Majibu ya Chuo

Mapato ya Chuo cha Utawala wa Umma yanaonesha kuongezeka kutoka Tsh. 1,765,049,390 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia Tsh. 2,623,161,450 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kukiwa na ongezeko la Tsh. 858,112,060 ambapo ni sawa na 48%. Ni kweli kwamba mapato ya Chuo yameongezeka kutoka Tsh. 1,765,049,390 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia Tsh. 2,623,161,450 kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Ongezeko hili linatokana na kuanzishwa kwa Shahada ya Kwanza pamoja na Taasisi za Umma kupata mwamko wa kutekeleza matakwa ya Sheria ya Utumishi ya Umma, Namba 2 ya mwaka 2011 kwa kuwapatia mafunzo ya Awali kwa Waajiriwa wapya. Hii inaonekana wazi katika taarifa za hesabu za Mwisho wa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ukilinganisha na Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Jaduweli la Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Maelezo	**Makadirio ya Mapato 2017/2018**	**Mapato Halisi 2017/2018**	**Asilimia**
Maombi ya Fomu	9,000,000	13,370,000	148.55
Mafunzo Mafupi	76,500,000	176,845,000	231.16
Ada ya Wanafunzi	2,624,440,000	1,789,605,695	68.19
Mapato Mengineyo	-	17,397,000	100
Ruzuku	604,500,000	625,943,755	103.54
Jumla	**3,314,440,000**	**2,623,161,450**	**79.14**

Aidha, kwa mnasaba wa Jadueli hilo, Chuo cha Utawala wa Umma kimekusanya makusanyo yake kupitia vyanzo vyake vya ndani ambavyo ni maombi ya fomu, ada ya mafunzo mafupi, ada ya wanafunzi na mapato mengineyo, ambayo ni 'penalty', malipo ya majoho na ukodishwaji wa ukumbi.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipohoji kuhusiana na mapato ya ada ya mafunzo mafupi, ilielezwa kuwa, Chuo kinatoa 'Induction Course' ya siku tatu kwa malipo ya Tsh. 50,000 kwa kila mwanafunzi. Mapato ya mafunzo haya yameongezeka kwa mwaka 2017/2018 ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa juhudi za Serikali za kuzitaka Taasisi zake ziwapeleke Chuoni hapo wafanyakazi wake wapya na ambao bado hawajapata mafunzo ya awali ya utumishi wao.

Aidha, Chuo pia kinatoa mafunzo ya kustaafu kwa salama kwa siku tatu kwa ada ya Tsh. 50,000. Vile vile, Chuo kinatoa mafunzo ya kujenga uwezo, lakini kiwango halisi cha tozo ya mafunzo haya hakikupatikana kwa Kamati na badala yake imeelezwa kuwa malipo hayo yanategemea makubaliano ya Uongozi wa Chuo na mleta maombi ya mafunzo hayo, hata hivyo, hakuna muongozo halisi wa ada ya kutozwa uliotolewa na Chuo wala Serikali.

Kamati pia ilipohoji juu ya chanzo cha ukodishwaji wa ukumbi wa Chuo, imebaini kuwa hakukuwa na kiwango kamili cha utozwaji wa malipo ya ukodishwaji wa ukumbu huo, pamoja na kuelezwa kuwa, kwa siku Chuo kinatoza Tsh. 50,000 na mara nyingi ukumbi huo hukodishwa kwa Taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara inayokisimamia Chuo hiki. Kamati pia imebaini kuwa, ukumbi huo hauko katika hadhi nzuri, kiasi ya kuendelea kutokipatia Chuo mapato halisi.

Mapendekezo ya Kamati

Katika kuongeza mapato ya Chuo kupitia ada ya mafunzo mafupi, Kamati inashauri kutolewa kwa muongozo halisi utakaoainisha kima halisi cha malipo ya waombaji wa mafunzo hayo, kwani kufanya kinyume chake ni kupoteza mapato ya Chuo kwa kushindwa kuainishwa kima halisi cha mapato kilichokusanywa. Aidha, kiwango cha Tsh. 50,000 kwa mafunzo ya 'Induction Course' na mafunzo ya kustaafu kwa salama, ni kidogo. Kamati inapendekeza kiwango hicho kirekebishwe kuendana na wakati na thamani ya mafunzo yanayotolewa.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Chuo cha Utawala wa Umma kwa mwaka 2017/2018 yalikadiriwa kuwa Tsh. 2,804,500,000, ambapo kati ya fedha hizo, Tsh. 2,528,000,000 zilikadiriwa kutumika kwa matumizi ya kawaida na Tsh. 72,500,000 zilikadiriwa kwa matumizi ya kazi za

maendeleo.

Aidha, ilipofika tarehe 30 Juni 2018, Tsh. 2,495,716,393 ziliingizwa na kutumika. Kati ya fedha hizo, jumla ya Tsh. 2,295,507,657 zilitumika kwa kazi za kawaida, sawa na 91% ya makadirio na Tsh. 2,140,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo, sawa na 3% ya makadirio.

Majibu ya Chuo

Matumizi ya Chuo cha Utawala wa Umma yameonekana kuongezeka kutoka Tsh. 2,096,616,016 kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi kufikia Tsh. 2,495,716,393 kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kukiwa na ongezeko la Tsh. 426,100,377 ambapo ni sawa na 20%. Ni kweli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 matumizi yameongezeka kutokana na sababu zifuatazo:

- Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji.
- Gharama za malipo ya vipindi cha ziada.

Athari ya gharama hizo ni kuongezeka kwa malipo ya vipindi vya ziada kwa walimu wa ndani na nje kulikosababishwa na kuanzishwa kwa program za Shahada ya Kwanza kwa Kada tatu katika fani za Utunzaji wa Kumbu Kumbu na Nyaraka, Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia pamoja na Usimamizi wa Rasilimali Watu.

Jaduweli la Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Maelezo	**Makadirio ya Matumizi 2017/2018**	**Matumizi Halisi 2017/2018**	**Asilimia**
Ruzuku	604,500,000	625,943,755	103.54
Matumizi yanayotokana na Mapato ya Chuo	2,200,000,000	1,869,772,638	84.98
Jumla	**2,804,500,000**	**2,495,756,393**	**88.99**

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imeridhishwa na juhudi ilizozichukua Chuo katika kudhibiti matumizi ya fedha walizotengewa, ingawaje imebaini kuwa, kwa mwaka 2017/2018 Chuo hakikuwa na Kitengo cha Manunuzi wala Bodi ya Zabuni. Hali hii pamoja na athari nyengine ilipelekea kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi na hatimae matumizi ya Chuo yalitegemea sana

Wizara husika.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati imeridhika na juhudi za Chuo katika kutatua kasoro zilizobainika na Kamati na Kamati inaendelea kukitaka Chuo, kiongeze juhudi kubwa katika kukusanya mapato na kutumia fedha za wananchi kwa kufuata kikamilifu muongozo wa Sheria za fedha.

3.7: CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Taarifa ya Mapato

Chuo cha Uandishi wa Habari kilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 781,692,800 katika kipindi cha mwaka 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali, kati ya hizo Tsh. 542,992,800 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 238,700,000 ikiwa ni makusanyo ya vyanzo vya ndani.

Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 770,048,355 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali ikiwa ni asilimia ya makadirio. Kati ya hizo, jumla ya Tsh. 625,605,355 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 144,443,000 ikiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani.

Majibu ya Chuo

Hali halisi ya upatikanaji wa fedha kwa Chuo cha Uandishi wa Habari kwa kipindi cha miaka miwili, yaani 2016/2017 na 2017/2018 ni kama ifuatavyo:

Mwaka	**Makadirio**	**Uhalisia**
Makusanyo ya 2016/2017	207,025,000	165,362,500
Ruzuku 2016/2017	831,847,000	482,480,054
Jumla	**1,038,872,000**	**647,842,554**
Makusanyo 2017/2018	220,700,000	144,443,000
Ruzuku 2017/2018	542,992,800	625,605,355
Jumla	**763,692,800**	**770,048,355**
Ongezeko 2017/2018	**275,179,200**	**122,205,801**
Asilimia		**19%**

Ni kweli Chuo cha Uandishi wa Habari kimepata ongezeko la Tsh. 122,205,801 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 sawa na 19% ukilinganisha na mwaka 2016/2017, ongezeko hili halitokani na makusanyo ya ndani wala matumizi mengineyo (OC), bali ongezeko hili limetokanana na mishahara ya wafanyakazi kumi (10) waliohamishiwa Chuo cha Uandishi wa Habari kutoka Taasisi mbali mbali kuja kuendelea na kazi, pamoja na marekebisho ya mshahara na malimbikizo kwa wafanyakazi waliorudi masomoni.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati iliridhika na majibu ya Chuo.

Taarifa ya Matumizi

Chuo cha Uandishi wa Habari kilikadiriwa kutumia Tsh. 781,692,800 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kati ya hizo, Tsh. 703,692,800 kwa matumizi ya kawaida na Tsh. 78,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 772,769,709 ziliingizwa sawa na 99% ya makadirio. Kati ya hizo, Tsh. 704,331,614 zimetumika kwa matumizi ya kawaida na Tsh. 68,438,095 zimetumika kwa kazi za maendeleo.

Majibu ya Shirika

Chuo cha Uandishi wa Habari kwa mwaka 2017/2018 kiliidhinishiwa jumla ya Tsh. 781,692,800 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, kiasi cha Tsh. 772,769,709 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida na maendeleo, sawa na 99% ya makadirio.

Mwaka	**Makadirio**	**Uhalisia**
2016/2017	1,038,872,000	668,723,674.60
2017/2018	1,563,385,600	772,769,709
Asilimia		**99%**

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kuwa utaratibu wa ujenzi haukufuatwa Bodi iliidhinisha Tsh. 24,000,000, isipokuwa kwamba, matumizi halisi yaliyofanyika ni Tsh. 68,438.095 na mkataba unaonesha wamekopa Tsh. 29,025,000.

Vile vile, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Chuo kilijenga ofisi za dharura ambazo hazimo kwenye Mpango wa Ununuzi na wala hawakuufanyia mapitio Mpango wao kama Sheria ya Ununuzi unavyoelekeza.

Fedha za ujenzi huo wa ofisi zilitolewa na Wizara ya Habari baada ya Mheshimiwa Waziri kufanya ziara Chuoni hapo.

Sambamba na hayo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ilitakiwa kulipa jumla ya Tsh. 92,000,000 ikiwa ni madai mbali mbali ya Watendaji na Wafanyabiashara, isipokuwa kwamba, Ofisi hiyo imelipa Tsh. 20,000,000 tu ambazo ni za Wafanyabiashara na Watendaji bado hawajalipwa.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro hizo zilizobainika, Kamati ya LAAC ilikitaka Chuo kuwa makini katika kutekeleza majukumu yake ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika miaka ijayo.

Vile vile, Kamati ya LAAC inaitaka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kulipa fedha zilizosalia ambazo ni za Watendaji ili kuwatia moyo ya kiutendaji Wafanyakazi hao.

Mengineyo

Katika kufuatilia hoja hizi Kamati ya LAAC ilibaini changamoto zifuatazo zinazozikabili Chuo hiki baada ya kuunganishwa na Chuo Kikuu cha taifa cha Zanzibar (SUZA):

i. SUZA kuchelewa kujibu barua za Chuo hicho jambo linalopelekea kuzorota utendaji wa Chuo. Kutokana na changamoto hiyo Chuo hulazimika kufuatilia barua hizo “physically” Tunguu jambo ambalo inawakwaza kiutendaji.
ii. Chuo hakipati fedha kwa wakati kutoka SUZA.
iii. Chuo hakiruhusiwi kufanya matumizi ya fedha hadi kipate ridhaa kutoka SUZA, ingawa, Skuli ya Biashara ya Chwaka ina mamlaka ya kufanya matumizi kwa kiwango fulani cha fedha bila ya kupitia SUZA.

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo;

i. SUZA iachane na tabia ya kutojibu barua mbali mbali zinazowasilishwa hapo ili kuondosha usumbufu kwa wadau wao.
ii. SUZA ijitahidi kukipatia fedha Chuo hiki kwa wakati ili kiweze kutekeleza majukumu yake bila ya usumbufu wowote.

iii. SUZA izichukulie Skuli zake kuwa zina hadhi sawa ili kuondosha malalamiko yasiyokuwa na msingi.

3.8: CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)

Taarifa ya Mapato

Chuo cha Taifa Zanzibar (SUZA) kilikusanya Tsh. 19,354,024,738 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali, kati ya hizo, Tsh. 11,230,990,665 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini, jumla ya Tsh. 7,197,543,676 ikiwa ni makusanyo ya vyanzo vya ndani na Tsh. 925,490,397 ikiwa ni misaada.

Majibu ya Chuo

Ni kweli kama ukaguzi ulivyobaini kwamba, kuna upungufu wa mapato kwa asilimia 0.72% kutoka mwaka 2016/2017 kwenda mwaka 2017/2018 kwa makusanyo ya jumla, wakati kwenye makusanyo ya ndani ya mapato kupunguwa kumekuwa kukubwa sana ambapo ni 26% ukilinganisha na mapato ya mwaka 2016/2017 kama Jaduweli Namba moja linavyoonesha:-

Maelezo	2016/2017	2017/2018	% ya Ongezeko au Upungufu
Mapato kutoka vyanzo vya ndani			
Mapato halisi	5,388,560,151	6,907,212,988	-27%
Mapato kutoka kutathmini Mali	4,440,000,000	0	
Ruzuku kutoka Serikalini	8,399,637,175	11,230,990,665	
Misaada	1,265,638,880	925,490,397	
Jumla ya Mapato	**19,493,836,206**	**19,354,024,738**	**-0.72%**

Kiuhalisia katika mwaka wa fedha 2016/2017 kulifanyika utathmini wa mali (Revaluation of Assets) ambao ulionesha mali za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) zilipanda thamani kwa Tsh. 4,440,000,000 ambayo ilipelekea mapato yaliyokusanywa kutoka kwenye vianzio vya ndani kufikia Tsh. 9,828,560,151 lakini

mapato hayo hayakuwa mapato halisi badala yake ilikuwa ni kupanda thamani ya rasilimali za Chuo. Hivyo basi, makusanyo halisi ya fedha kwa mwaka unaoishia June 2017 yalikuwa Tsh. 5,388,560,151.

Kiukweli Uongozi wa Chuo unafahamu umuhimu wa kutafuta fedha kwa washiriki wa kimaendeleo kwa ajili ya kukiendeleza Chuo jhasa kwenye masuala ya miundombinu na taaluma ili kuweza kuongeza ubora (quality) wa program zake na aina ya ufundishaji wake. Kwa hivyo, Chuo kinaendelea kufanya mikakati mbali mbali ikiwemo ya kuwashajihisha wanataaluma na wafanyakazi wengine kuandaa maandiko ya miradi au kuitikia miito ya maandiko (call for Proposal) kwa ajili ya miradi au tafiti.

Aidha, Chuo kinashirikiana na Taasisi nyengine za ndani na nje kwa ajili ya kuweza kupata miradi ambayo itaweza kukiendeleza Chuo, kitaaluma na kiutendaji. Hii ndio maana makusanyo halisi huongezeka kutoka mwaka hadi mwaka.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imejiridhisha kuwa miongoni mwa vyanzo vya mapato vya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar ni ukumbi wa Dr. Ali Mohamed Shein (Dr. Ali Mohamed Shein Hall) ambao ni mkubwa na hautumiki ipasavyo kukusanya mapato ya Chuo. Pamoja na ukweli kuwa ukumbi huo unatumika zaidi kwa shughuli za Serikali, iwapo utaimarishwa ipasavyo, Kamati inaona ni chanzo kizuri cha kuongeza mapato ya Chuo. Aidha, Kamati imejiridhisha kuwa, mapato kadhaa ya makusanyo ya Maholi ya Chuo hayakuwa katika utaratibu wa kufikishwa benki mara tu baada ya makusanyo kwa mwaka 2017/2018, hali iliyoidhihirishia Kamati kuwa, kwa mwaka huo, Chuo hakikuwa na nidhamu nzuri ya makusanyo ya mapato yake.

Aidha, Kamati ilipohoji chanzo cha mapato cha Majaribio ya Lugha za Kigeni (Proficiency Test) iliyokuwa inatolewa na Taasisi ya Lugha za Kigeni, na sasa hivi SUZA, Kamati imejiridhisha kuwa, mapato yaliyokuwa yanakusanywa kupitia ‘test’ hizo yaliingia mikononi mwa baadhi ya wafanyakazi waliosimamia ‘test’ hiyo na sio kupitia ‘Account’ ya SUZA. Hivyo, imeendelea kuusisitiza uongozi wa SUZA kulifanyia kwa haraka suala hili, ili makusanyo yake yaingie moja kwa moja Chuoni hapo, hasa baada ya Kamati kuelezwa kuwa, tayari Chuo kimetafuta Mshauri Elekezi wa kushauri namna bora ya kukusanya mapato ya chanzo hiki.

Aidha, Kamati imehoji chanzo cha mapato ya Mabweni kilichokuwa kinasimamiwa na kilichokuwa Chuo cha Uongozi wa Fedha Zanzibar, lakini taarifa hizo hazikupatikana kwa Kamati, pamoja na Kamati kuahidiwa kuwa zitawasilishwa kwake kutoka kwa wahusika wa Chuo hicho.

Mapendekezo ya Kamati

Chuo kinawajibika kufuatilia kwa karibu vyanzo vyake vya mapato kwani Kamati inaamini bado haijavifanyia kazi ipasavyo, hali inayokipelekea Chuo kushindwa kukusanya mapato yake kwa ufanisi na kwa kiwango kilichokusidiwa.

Taarifa ya Matumizi

Katika mwaka 2017/2018, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kilitumia Tsh. 21,890,073,457 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kilitumia jumla ya Tsh. 16,209,250,509 kukiwa na ongezeko la Tsh. 5,680,822,948, sawa na 35.05 ya ongezeko.

Majibu ya Chuo

	2017/2018	**2016/2017**
Matumizi ya Chuo	21,890,073,457	16,209,250,509

Kuongezeka kwa matumizi katika mwaka 2017/2018 ni kutokana na kuunganishwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Vyuo vyengine, ambavyo ni Chuo cha Uongozi wa Fedha sasa ni School of Business, Chuo cha Utalii ambacho kwa sasa ni 'Insitute of Tourism' na kilichokuwa Chuo cha Afya, Mbweni, ambacho kwa sasa ni 'School of Health and Medical Science'. Kwa ujumla kuunganishwa kwa vyuo hivi na SUZA kulipelekea kuongezeka kwa Ruzuku ya Mshahara kutoka Tsh. 8,399,637,175 na kufikia Tsh. 11,230,990,665.

Sambamba na hilo kuna ongezeko la matumizi ya huduma ya Ushauri kutoka 'ZISPE Consultancy'. Na vile vile mali za Chuo zilifanyiwa tathmini upya na thamani ilionekana kuongezeka, hivyo basi uchakavu (depreciation) uliongezeka ambao ulipelekea gharama za matumizi kupanda (hata hivyo, gharama hizo si gharama halisia).

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja kuelezwa kuwa Chuo kimefanikiwa sana kuongeza mapato yake kwa kuunganishwa na Vyuo vyengine, Kamati inaamini Serikali inapaswa kuangalia upya juu ya athari za kimapato na matumizi juu ya kuunganishwa kwa vyuo hivyo.

Aidha, pamoja Uongozi wa Chuo kutoa ufafanuzi wa fedha za ZISPE Consultancy ambayo ilielezwa kutumiwa kwa Tsh. 909,487,440 ikiwa ni mradi wa kubadilishana walimu wa masomo ya sanaa kuweza kusomesha masomo sayansi, Kamati haikujitosheleza juu ya maelezo ya Chuo na hasa ikizingatiwa kuwa, ufuatiliaji wa suala hili unahitaji muda wa kutosha na utulivu.

Vile vile, Kamati ilielezwa kuwa Chuo kilifanya matumizi ya Tsh. 35,248,409 kwa matumizi ya utafiti wa maji ya ardhini katika eneo la Unguja kwa lengo la kuangalia 'ingredients' katika maji baridi, fedha zilipatikana kutoka WUHAN –China na kusimamiwa na Dr. Abdul Juma wa Skuli ya Sayansi Asilia na Jamii, SUZA.

Aidha, Kamati imegundua kuwa, pamoja na taarifa zilizowasilishwa kwake na ufafanuzi wa masuala mbali mbali kuhusiana na matumizi haya, kuna marejesho ambayo Dr. Abdul anakabidhi Chuoni ili aweze kupatiwa fedha nyengine, lakini marejesho hayo hayakuwahi kukabidhiwa kwa Kamati ili kujiridhisha uhalali wa mapokezi na matumizi ya fedha hizi.

Kamati imefanya uhakiki wa matumizi ya Tsh. 130,964,699 zilizotumika kwa matumizi madogo madogo ya majengo ya Chuo kwenye Kampasi mbali mbali, ambapo Kamati ilielezwa kuwa fedha hizo zilitumika kwa matengenezo ya Skuli ya Afya ambapo Kamati imejiridhisha kuwa, matumizi yake yalitakiwa kufuata taratibu za manunuzi ikiwa ni pamoja na kuitishwa kwa Zabuni na kumtafuta Mjenzi wa majengo ya Chuo hiki, lakini ilithibitishiwa kuwa, hakukuwa na zabuni yoyote iliyoitishwa na badala yake fedha hizo ziligawiwa katika makundi madogo ya matumizi (splitting) ili kukwepa taaratibu za manunuzi.

Aidha, Kamati ilielezwa kati ya Tsh. 130,964,699, baada ya kufanywa 'Splitting' Tsh. 4,930,095 zililipwa Tunguu na Tsh. 126,034,604 zilitumika kwa Skuli ya Afya. Vile vile, Tsh. 50,920,453.78 zilitumika Tunguu, hata hivyo, Kamati imekuwa na mashaka makubwa na usahihi wa matumizi haya na imejiridhisha juu ya matumizi mabaya ya Chuo kwa mwaka 2017/2018.

Mapendekezo ya Kamati

Serikali ifuatilie na kuusimamia kwa karibu Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kwani kuna dalili nyingi za kutumika vibaya kwa matumizi ya Chuo hiki. Aidha, Uongozi wa Chuo usimamie kwa uadilifu miradi inayoombwa na kusimamiwa na Chuo ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za miradi hiyo.

3.9 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA

Taarifa ya Mapato

Shirika la Meli na Uwakala lilikusanya Tsh. 10,156,959,371 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali.

Majibu ya Shirika

Mapato ya Shirika yanatokana na vyanzo vikuu vitatu:

1. Mapato yanayotokana na usafirishaji wa abiria na mizigo. Shirika lina meli mbili zinazotumika kusafirisha abiria na mizigo. Meli hizi ni MV. Maendeleo na MV. Mapinduzi II.

2. Ukodishaji wa meli za mafuta. Kwa kipindi hichi Shirika lilikua na meli moja ya Mafuta ambayo ni MT. Ukombozi.

3. Mapato ya Uwakala wa meli za kigeni. Shirika linapata ujira wa Uwakala (Agency Commission) pamoja na mapato ya utoaji mizigo (Release).

Aidha, katika hesabu za Shirika, kuna mapato mengineyo ambayo yanatokana na mambo yafuatayo:

1. Mapato ya kodi ya vyumba katika jengo la Ofisi la Shirika la Meli liliopo Mkoani Pemba, Shirika linakodisha baadhi ya vyumba kwa Mamlaka ya Usafiri baharini (ZMA) kwa matumizi ya kiofisi.

2. Mapato ya mkahawa uliomo katika meli ya MV. Mapinduzi II.

3. Mapato ya kodi ya sehemu ya ofisi katika jengo la Ofisi Kuu Unguja.

4. Malipo kwa ajili ya mafunzo ya wanafunzi wanaosomea ubaharia (seatime).

5. Uuzaji wa nyaraka za Zabuni (Tender Documents).

Mchanganuo wa mapato yaliyokusanywa pamoja na makisio yake kwa mwaka 2017/2018 ni kama ifuatavyo:

Makisio (budget) ya mapato na mapato halisi (actual) ya Shirika 2017/2018

Chanzo cha mapato	Makisio	Makusanyo halisi	Tofauti	%
MV. Maendeleo	0.0	0.0	0.0	0.0
MV. Mapinduzi II (Abiria na Mizigo)	8,696,472,000	2,635,320,378.81	6,061,151,621.19	30.30
MT. Ukombozi (Mafuta)	2,678,005,000	2,577,738,854.35	100,266,145.65	96.26

Uwakala wa Meli za Kigeni	4,150,720,000	4,904,373,706.44	-753,653,706.44	118.16
Mengineyo	21,360,000	39,526,431.41	-18,166,431.41	185.05
Jumla	**15,546,557,000**	**10,156,959,371.01**	**5,389,597,628.99**	**65**

Mapato ya halisi (actual) ya Shirika 2017/2018

Chanzo cha mapato	**2017/2018**	**2016/2017**	**Tofauti**	**%**
MV. Maendeleo	0.0	318,310,866.00	(318,310,866.00)	0.0
MV. Mapinduzi II	2,635,320,378.81	4,015,716,017.70	(1,380,395.638.89)	(34.37)
MT. Ukombozi	2,577,738,854.35	2,560,712,216.25	17,026,638.10	0.66
Uwakala wa Meli za Kigeni	4,904,373,706.44	5,422,198,962.35	(517,825,255.91)	(9.55)
Mengineyo	39,526,431.41	28,156,442.00	11,369,989.41	40.38
Jumla	**10,156,959,371.01**	**12,345,094,504.30**	**(2,188,135,133.29)**	**(18)**

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipohoji chanzo cha Shirika cha Mkahawa uliomo katika meli ya MV. Mapinduzi II, Kamati imegundua kuwa Mkahawa huo unaendeshwa na wafanyakazi wenyewe wa Shirika wakisimamiwa na Captain wa meli, lakini wafanyakazi hao hawana uwezo wa kitaaluma wa kusimamia fedha zinazopatikana katika biashara hiyo na wala hawakuwa wakitunza kumbu kumbu za mapato wanayoyakusanya kwa usahihi. Kwa maana hiyo, Kamati imekosa kumbukumbu za mapato yaliyotokana na Mkahawa na imejiridhisha kupata maelezo ya Mkaguzi wa Ndani wa Shirika aliyeithibitishia Kamati kuwa, hata ukaguzi wake wa ndani wa mapato haya ulikuwa mgumu kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu za mapato ya Mkahawa huo. Hata hivyo, pamoja na upungufu wake na kukosekana kwa taarifa sahihi za makusanyo ya fedha hizo, kiwango kilichokuwa kinapatikana baada ya kufikishwa kwa Shirika, zilikuwa zinapelekwa Benki.

Aidha, Kamati imehoji juu ya chanzo cha ukodishwaji wa nyumba za Shirika ziliopo Dar es Salaam, ambapo Kamati haikupewa taarifa zake kabla na kama sio juhudi za Kamati, chanzo hiki kisingelitolewa maelezo yake na Shirika. Pamoja na kufichwa huko, Kamati ilielezwa kuwa, nyumba hizo sasa zinatumika kwa malazi ya wafanyakazi wa Shirika wanaokwenda masomoni Dar es Salaam, kutokana na kukosekana kwa fedha za kuzijenga ghorofa na kukodishwa kama nyumba za kulaza wageni.

Hata hivyo, Kamati imejiridhisha baada ya kuangalia taarifa za Shirika kuwa nyumba hizo zinaonekana kuingiza Tsh. 40,000 kwa mwaka 2017/2018 huku nyumba hizo zikihudumiwa na Mlinzi na Msafishaji ambao wote wanalipwa mshahara na Shirika. Kwa maana hii, Kamati imejiridhisha kuwa, nyumba hizo zinaipa hasara Shirika kwa sababu bado hazijajengwa na kushughulikiwa kwa kiwango cha biashara yenye tija.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati haikuridhishwa na makusanyo ya mapato ya Shirika la Meli na Uwakala na imejiridhisha kuwepo kwa uvujaji wa mapato katika vyanzo vyake mbali mbali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa karibu mianya ya uvujaji wa mapato ya Shirika hili.

Taarifa ya Matumizi

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Shirika la Meli na Uwakala lilitumia Tsh. 2,519,201,825 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo Shirika la Meli na Uwakala lilitumia jumla ya Tsh. 2,471,219,672 kukiwa na ongezeko la Tsh. 47,982,153 sawa na 2% ya ongezeko.

Majibu ya Shirika

Kwa mujibu wa hesabu zilizopelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kama zilivyoambatanishwa kwenye kitabu cha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2017/2018), matumizi ya Tsh. 2,519,201,525 na Tsh. 2,471,982,153 kwa mwaka 2017/2018 na mwaka 2016/2017 ni matumizi ya shughuli za kiutawala za Shirika pekee na sio matumizi yote ya Shirika, Matumizi yote ya Shirika yakijumuisha matumizi ya meli (Direct Shipping Expenses) ni Tsh. 9,202,642,050 kwa mwaka 2017/2018 baada ya kutoa gharama za uchakavu (Depreciation Charges) wakati matumizi yote kwa mwaka 2016/2017 yalikuwa ni Tsh. 10,959,807,128.

Kwa ujumla matumizi yamepungua kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kupungua kwa matumizi ya MV. Maendeleo, meli hii ilikua nangani ikisubiria kuuzwa.

ii. Kupungua kwa matumizi ya kawaida ya MV. Mapinduzi II. Meli hii ilipata maharibiko makubwa na kukaa nangani ikiendelea na matengenezo.

Jaduweli Namba 3 na Namba 4 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa matumizi halisi pamoja na makisio yake kwa kazi za kawaida. Aidha, Jaduweli Nambari 5 linaonesha matumizi ya kazi za Maendeleo (Capital Expenditure).

Makisio ya matumizi na matumizi halisi ya Shirika 2017/2018 (kazi za kawaida)

Aina ya Matumizi	**Makisio (Approved Budget)**	**Makisio (Revised Budget)**	**Halisi**	**Tofauti**	**(%)**
MV. Maendeleo	0.0	329,102,285	279,710,465.30	49,391,819.7	84.99
MV. Mapinduzi II	9,793,050,845	7,463,041,321	5,587,877,276.21	1,875,164,044.75	74.87
MT. Ukombozi	1,050,549,370	1,194,859,984	945,737,973.49	249,122,010.51	79.15
Uwakala na Uendeshaji	4,038,512,091	3,557,089,175	2,389,316,335.66	1,167,772,839.34	67.17
Jumla ya Matumizi ya Kawaida	**14,882,112,306**	**12,544,092,766**	**9,202,642,050**	**3,341,450,716**	**73**

Gharama hizi hazijumuishi gharama za uchakavu (Depreciation charges)

Jaduweli Nambari 4 hapa chini linaonesha mlinganisho wa matumizi ya kawaida kwa mwaka 2017/2018 na mwaka wa nyuma yake 2016/2017. Kama inavyoonekana kwenye Jaduweli hili, matumizi ya Kawaida yalipungua kutoka Tsh. 10,959,807,128 (10.96 bilioni) kwa mwaka 2016/2017 na kufikia Tsh. 9,202,642,050 (9.2 bilioni) kwa mwaka

2017/2018 ikiwa ni tofauti ya Tsh. 1,757,165,078 (1.76 bilioni) sawa na 16.03% ya upungufu.

Matumizi halisi ya Shirika 2016/2017

Aina ya Matumizi	**2017/2018**	**2016/2017**	**Tofauti**	**(%)**
MV. Maendeleo	279,710,465.30	1,353,383,504.82	(1,073,673,039)	(79.33)
MV. Mapinduzi II	5,587,877,276.21	6,314,713,095.33	(726,835,816)	(11.51)
MT. Ukombozi	945,737,973.49	967,553,444.94	(21,815,471)	(2.25)
Uwakala na Uendeshaji	2,389,316,335.66	2,323,207,083.07	66,109,253	2.8
Jumla	**9,202,642,050**	**10,958,857,128**	**(1,756,215,077)**	**(16.03)**

Gharama hizi hazijumuishi gharama za uchakavu (Depreciation charges)

Makisio ya matumizi na matumizi halisi ya Shirika 2017/2018 (capital expenditure)

Aina ya Matumizi	**Makisio (Original Budget)**	**(Revised Budget)**	**Halisi**	**Tofauti**	**(%)**
Ununuzi wa Magari	150,000,000	62,731,000	62,731,000	0.0	100
Ununuzi wa Samani	83,980,000	83,980,000	52,769,651	31,210,349	62.83
Ujenzi wa Nyumba za	360,000,000	360,000,000	0.0	360,000,000	0.0

Ofisi					
Matengenezo ya Meli	0.0	2,809,748,776	2,925,291,605	(115,542,829)	104
Jumla	**593,980,000**	**3,316,459,776**	**3,040,793,256**	**275,667,520**	**61.69**

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imejiridisha kuwa, Wizara iliyokuwa inahusika na Shirika la Meli na Uwakala kwa mwaka 2017/2018, haikuwa ikilipa Shirika uhuru wa kuendesha mambo yake na badala yake lilikuwa linatoa maelekezo tofauti kwa utendaji wa Shirika bila ya kufuata ushauri wa Kitaalamu wa wataalamu mbali mbali wa Shirika. Katika kuhakikisha Shirika linabanwa na kunyimwa uhuru wake, Mikataba ya Shirika ikiwa ni pamoja na Mkataba CAPCO ulisainiwa na Katibu Mkuu wa Wizara, badala ya kusainiwa na Afisa Masuuli wa Shirika.

Aidha, Kamati imejiridhisha kuwa, Wataalamu wa Shirika, ikiwa ni pamoja na Mabaharia wa Meli hiyo, walikabidhiwa Meli ya Mv. Mapinduzi II bila ya kupewa mafunzo ya kutosha juu ya matumizi sahihi ya meli hiyo.

Vile vile, Kamati imejiridhisha kuwa, katika kuzisimamia na kuziendesha meli zake, Shirika lilikuwa linatumia fedha nyingi kuliko uwezo wake. Kwa maana nyengine, matumizi yanayotumiwa kusimamia meli za Shirika ikiwa ni pamoja na gharama za matengenezo ya meli hizo ni kubwa sana kuliko mapato yanayokusanywa katika kuzisimamia meli hizo.

Aidha, Kamati imeshtushwa na kiwango kikubwa cha maposho waliyokuwa walikipwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika. Kwa mfano, Kamati ilielezwa kuwa, kila mjumbe wa Bodi alikuwa analipwa Tsh. 500,000 kwa kila kikao cha Bodi huku Mwenyekiti wake alikuwa analipwa Tsh. 600,000.

Vile vile Kamati imeshangazwa sana na Shirika kutenga fedha na kuzitumia kwa kununulia simu, posho za sikukuu na posho kwa ajili ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, huku Shirika hilo likipata hasara zaidi ya bilioni 2 kwa mwaka 2017/2018.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaitaka Serikali kutekeleza ahadi yake ya kuziuza meli za Shirika ambapo kimsingi Kamati imejiridhisha kuwa hazina tija na zinaitia zaidi Serikali hasara.

3.10 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR

Taarifa ya Mapato

Shirika la Bandari Zanzibar lilikadiriwa kukusanya Tsh. 29,498,787,457 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vianzio vyake mbali mbali. Aidha, hadi ilipofikia Juni 2018, Shirika lilikusanya Tsh. 34,361,996,258 sawa na 116.5%.

Majibu ya Shirika

Shirika limefanya juhudi katika kuvisimamia vyema vyanzo vyake vya mapato, hali iliyopelekea kuongezeka kwa makusanyo. Vyanzo hivyo ni Corporation Income, Marine Income na Mengineyo, yanayojumuisha House Rent,

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imefanya uchambuzi wa vyanzo mbali mbali vya Shirika ikiwa ni pamoja na Kodi za Nyumba (House Rent) na kujiridhisha kuwa Shirika linamiliki nyumba tatu, mbili ziliopo Maisara ambazo zimekabidhiwa Serikalini na sasa zinatumiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) na Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) na moja iliyopo Shangani ilikodishwa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mstaafu, Mhe. Aman Abeid Aman Karume, kwa kukodi miaka 33 na Mkodishwaji amesita kulipa kwa muda sasa, huku Kamati ikielezwa kuwa, Shirika limo katika mchakato wa kuchukua hatua za Kisheria. Kwa mfano, katika kipindi cha kodi hiyo kutoka mwaka 2018 hadi 2021, Mkodishwaji alikuwa anadaiwa USD 57,600 ambapo amelipa USD 7,200 pekee na kufanya deni lake analodaiwa na hajalipa ni USD 50,400.

Aidha, Mkataba wa ukodishwaji wa nyumba ya Shangani haujapitiwa (Not reviewed) ili kurekebishwa kwa gharama za kodi kwa muda mrefu sasa, huku Bodi ya Shirika ikiwahi kutoa maelekezo hayo. House Rent kwa upande wa Pemba, Shirika lina nyumba ya Wageni (Bomani Guest House) ambayo haipo na muonekano huo na Kigomasha Light House inayoendeshwa kwa hasara.

Vile vile, Kamati imejishuhudia vyanzo mbali mbali vya Shirika havikutajwa wala kuainishwa wakati wa kazi za Kamati, hali inayoishangaza Kamati kufahamu iwapo Shirika halivitambui vyanzo vyake vyote au baadhi yao vinafichwa taarifa zake. Kwa mfano, Kamati haikupewa taarifa yoyote ya Hoteli ya Shirika iliyopo Bopwe Pemba, ambayo awali ilikuwa inakodishwa, lakini Shirika lilijitetea kwa kueleza kuwa, hivi sasa inatumiwa kama ni sehemu ya kukaa wafanyakazi wao.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inalitasha Shirika lifuatilie kwa karibu madeni yake inayozidai Taasisi au watu binafsi wanaoingia mikataba nao na kufaidika na rasilimali za Shirika. Aidha, hatua za Kisheria zichukuliwe kwa wadaiwa wanaokataa kulipa madeni yao au kushindwa kutekeleza masharti ya mikataba wanaoingia nao.

Shirika lifuatilie vyanzo vyake vya mapato kwa uhakika na litoe taarifa zake pale inapohitajika kufanya hivyo kwa maslahi ya nchi. Aidha, Serikali iusimamie kwa karibu uongozi wa Shirika, ili kuhakikisha kuwa unawajibika katika ukusanyaji wa mapato ya Shirika hili.

Taarifa ya Matumizi

Shirika la Bandari lilikadiriwa kutumia Tsh. 22,157,186,398 kwa mwaka 2017/2018 na ilipofikia Juni 2018, jumla ya Tsh. 18,547,171,652 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na 84% ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Shirika limetumia fedha hizo kwa matumizi ya kawaida kama ilivyo katika bajeti yao ya mwaka 2017/2018 na wamejitahidi kufikia malengo, pamoja na kutopatikana kwa fedha hizo kwa kiwango cha asilimia 100.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imepitia matumizi mbali mbali ya Shirika na kwa umuhimu wa kipekee ilifanya uchunguzi kuhusiana na matumizi ya Meli ya LCT Jitihada na kujiridhisha kuwa kwa mwaka 2017/2018, mapato ya LCT Jitihada yaliyokusanywa yalikuwa ni Tsh. 264,100,739.60 wakati matumizi ya kuigharamia meli hiyo yakiwa ni Tsh. 377,512,489.86. Hii ina maana kuwa, tokea Mei 2011 hadi Oktoba 2020, Meli hiyo inaendeshwa kwa hasara kwa kutumia fedha nyingi zaidi katika kuendeshwa kwake kuliko fedha zinazopatikana kutokana na meli hiyo.

Vile vile, imebainika kuwa, meli hiyo inatumia ziada ya 33% dhidi ya mapato. Aidha, matumizi makubwa ya uendeshaji wa meli hiyo pia yanachangiwa na ununuaji wa vitu vilivyo chini ya kiwango kwa bei kubwa. Kwa lugha nyengine, Kamati imejiridhisha kuwa, kuna ubadhirifu mkubwa na matumizi mabaya katika uendeshaji mzima wa meli ya LCT Jitihada.

Aidha, Kamati imeshuhudia matumizi makubwa katika uendeshaji wa vikao vya Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, ambapo kwa mwaka 2017/2018 zaidi ya Tsh. 345,647,960 zimetumika kwa matumizi ya vikao vya Bodi, Safari na matumizi mengine, ambayo kimsingi Kamati imejiridhisha kuwa hayakuwa na tija kubwa kwa Shirika.

Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na kuelezwa kuwa Shirika limefanya marekebisho ya uendeshaji wa meli ya LCT Jitihada, Kamati inashauri suala hili liendelee kufuatiliwa kwa karibu na lichukuliwe hatua muafaka, kabla ya kuendelea kulilisha hasara Shirika na Taifa kwa ujumla.

3.8 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

Taarifa ya Mapato

Mapato ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar yameongezeka kutoka TZS 110,270,566,408 kwa mwaka 2018/2019 kufikia TZS114,372,053,812 kwa mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la TZS 4,101,487,404 sawa na asilimia 3.7.

Majibu ya Mfuko

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mfuko ulipata mapato ya TZS 114,372,053,812 dhidi ya lengo la kupata mapato ya TZS 138,561,286,637.7 ikiwa ni sawa na asilimia 80 ya lengo.

Mfuko ulishindwa kufikia lengo ililojipangia kutokana na kupungua kwa michango ya wanachama wake kulikosabishwa na mripuko wa ugojwa wa uviko wa 19 na kupelekea sekta nyingi za utalii kufunga biashara.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Michango ya wanachama kwa Taasisi za Pemba hulipwa moja kwa moja Makao Mkuu ya Taasisi (Unguja) hizo, isipokuwa kwamba, wakati wa kustaafu malipo ya mafao ya mtumishi husika hulipwa moja kwa moja katika Taasisi yake.
2. Serikali za Mitaa hazitoi mashirikiano kwa Mfuko huu katika kuainisha Taasisi ambazo zimeanzishwa katika maeneo yao. Hata hivyo, baada ya Mfuko kuzibaini Taasisi hizo huzichulia hatua na kuzitaka kuwalipia michango watendaji wake tokea kuanzishwa kwa Taasisi hizo.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kuimarisha utendaji wa Mfuko huu Kamati ya LAAC ilipendekeza mambo yafuatayo:

1. Kila Taasisi (Tawi) ilipe michango ya watumishi wake ili kupima utendaji wa Mfuko huu kwa Taasisi husika.
2. Serikali za Mitaa kutoa mashirikiano kwa Mfuko huu ili uweze kutekeleza

majukumu yake bila ya usumbufu wowote.

3. Mfuko uendelee na jitihada ya kufungua Matawi yake katika kila Mkoa ili kuwaondoshea usumbufu wateja wake pamoja na kusimamia vyema majukumu yake na kwa ile Mikoa ambayo tayari Matawi ishafunguliwa basi watendaji wa Mfuko wajitahidi kufanya ziara katika mikoa yao na wasibakie ofisini ili kufikia dhamira ya kuanzishwa kwa Matawi hayo.

4. Mfuko kuanzisha utaratibu wa kuwapatia mafao yao wateja wao wote ambao kwa namna moja au nyengine wamelazimika kuacha kazi kabla ya muda uliopangwa. Kwa mnasaba huo, Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ifanyiwe marekebisho ili iweze kutekelezeka katika kila mazingira yatakayojitokeza.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar yamepungua kutoka TZS 48,658332,212 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia TZS 42,320,530,058 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na upungufu matumizi ya TZS 6,337,802,154 sawa na asilimia 13.

Majibu ya Mfuko

Kupungua kwa matumizi kunatokana na uamuzi wa Menejiment ya Mfuko ya kupunguza matumizi hayo kutokana na kupungua kwa mapato. Kitendo hiki kimepelekea baadhi ya miradi mipya kutotekelezwa, kwa mfano; ujenzi wa jengo la maegesho la Michezani, ujenzi nyumba za Mombasa na utanuzi wa jengo la biashara Mwanakwerekwe.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yamebainika:

1. Licha ya Mfuko huu kuamua kupunguza matumizi yake, hata hivyo, shughuli za uendeshaji wa afisi na miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa imetekelezwa kama ilivyopangwa.
2. Baadhi ya vifungu “Note” matumizi yake yamefanywa nje ya vifungu husika jambo ambalo limeipa mashaka Kamati hii, kwa mfano; kifungu cha “ICT Expenses” Tsh. 1,380,000 zimelipwa kwa ajili ya mafunzo wakati Mfuko una kifungu maalum kinachohusiana na Mafunzo. Vile vile, kwenye kifungu cha “Transport on Leave” yamefanyika malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ambapo jumla ya Tsh. 279,125 zilitumika.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kuimarisha utendeji wa Mfuko huu, Kamati ya LAAC iliushauri Mfuko kufanya matumizi yake kwa mujibu wa bajeti ilivyopangwa ili kuwa na nidhamu ya matumizi pamoja na kuondosha dhana zisizo za msingi.

3.8.1 Kutokufanyia kazi mapendekezo ya ripoti ya tathmini ya makisio ya takwimu zinazohusiana na uhai wa wachangiaji (Actuarial valuation report) kama ilivyoelekezwa na Bodi

Katika kikao chake cha tarehe 29 Septemba, 2019, Bodi ilipokea ripoti ya tathmini ya makisio ya takwimu zinazohusiana na uhai wa wachangiaji *(Actuarial valuation report)* iliyotayarishwa na Kampuni ya *African Risk and Insurance Services* kwa mwaka 2018. Ripoti hiyo ilibainisha kasoro ambazo zinahitaji mikakati imara ichukuliwe na Uongozi wa ZSSF ili kuongeza uendelevu na ukwasi wa Mfuko.

Ripoti hiyo ilibainisha hatari kubwa zikiwemo uwekezaji katika mali zisizolipa na zisizopangiliwa vizuri faida ndogo kutokana na uwekezaji wa wigo mdogo wa michango ya wanachama. Ripoti ilitahadharisha kuwa iwapo kama hatua za kurekebisha hali ya ukwasi ya Mfuko hazitochukuliwa, fedha zitakazokuwa zinaingia katika Mfuko wa ZSSF zitazidiwa na fedha zitakazokuwa zinatoka katika Mfuko katika kipindi cha baina ya mwaka 2039 hadi 2050. Hata hivyo, ripoti haikueleza ni lini hasa Mfuko utafilisika.

Baada ya kupokea ripoti hiyo, Bodi iliagiza Uongozi wa Mfuko kufanyia kazi mapendekezo ya ripoti hiyo ya tathmini ya makisio ya takwimu zinazohusiana na uhai wa wachangiaji ikiwemo kupitia upya muundo wa mkusanyiko wa uwekezaji, kuwekeza katika uwekezaji wenye tija ya kutosha, uwekezaji katika miradi inayolipa haraka pamoja na kuwa na uanishaji mzuri wa mitaji.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 ZSSF ilikuwa na vitu vifuatavyo:-

1. ZSSF imewekeza kwa kiasi kikubwa katika majengo ikiwemo ujenzi unaoendelea shilingi bilioni 29. Aidha, tumebaini faida ndogo inapatikana katika majengo ikiwemo nyumba za Mbweni ambazo mauzo yake yamepata hasara ya asilimia 2.
2. Uwepo wa uwekezaji usio na tija ikiwemo shilingi bilioni 3.15 zilizowekezwa ZAFICO.
3. Uwekezaji wa baadae umepangwa uwe katika majengo, Mradi wa kukamilisha majengo matatu yaliyopo Mbweni pamoja utafutaji fedha kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya Mradi wa Mji Mpya Kwahani.
4. Wigo wa Michango hauridhishi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ZSSF imewafikia asilimia 17 tu ya watu walioajiriwa. Aidha hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2020, Mfuko ulikuwa unadai michango ya shilingi bilioni 1.256.

Kutokufanyia kazi ushauri wa kitaalam wa mtathmini wa vihatarishi unaweza kupelekea Mtiririko wa fedha na uwekezaji unaweza kushindwa kulipia madeni ya Mfuko.

Uongozi wa ZSSF kupitia muundo wake wa uwekezaji na ipeleke fedha nyingi katika miradi yenye tija na inayolipa haraka.

Majadiliano ya Hoja hizi yalikuwa kama ifuatavyo:

i. **ZSSF imewekeza kwa kiasi kikubwa katika majengo ikiwemo ujenzi unaoendelea shilingi bilioni 29. Aidha, ukaguzi umebaini kuwa faida ndogo inapatikana katika majengo ikiwemo nyumba za Mbweni ambazo mauzo yake yamepata hasara ya asilimia 2.**

Majibu ya Mfuko

ZSSF imejipanga kupunguza uwekezaji wa majengo kwa mwaka 2021/2022 na kuelekeza uwekezaji wake katika miradi yenye gharama ndogo na faida kubwa.

Aidha, ZSSF imefanya mapitio ya bei ya uuzaji wa nyumba za Mbweni kuanzia mwezi Februari 2021 kama ifuatavyo;

1. Kutoka TZS 168 milioni hadi TZS 175 milioni kwa nyumba za vyumba viwili;
2. Kutoka TZS 190 milioni hadi TZS 197 milioni kwa nyumba za vyumba vitatu; na
3. Kutoka TZS 249 milioni hadi TZS 255 milioni kwa nyumba za vyumba vinne.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu iliyopelekea Mfuko huu kushindwa kufuata maelekezo ya Bodi na ilielezwa kuwa Mfuko ulishindwa kufuata maelekezo hayo kwa kuwa ilivyofanywa tathmini ilikuwa tayari miradi hiyo imeshaanza kutekelezwa.

Vile vile, kwa upande wa kupatikana kwa faida ndogo katika nyumba za Mbweni, Kamati ilibaini kuwa:

1. Hapo awali nyumba hizo zilipigwa thamani kwa kutumia fedha za Kimarekani (USD) ambapo kati ya nyumba zote 210 ni nyumba 200 ambazo zimeuzwa na nyumba 10 tayari watu wameshaonesha nia ya kuzinunua.

2. Idadi kubwa ya nyumba hizo ziliuzwa kwa mkopo na nyumba sita tu ndio zimeuzwa kwa fedha taslimu.

Wanunuzi hao bado hawajapatiwa Hati miliki kwa kuwa kwa wakati ule Bodi ya Kondominiamu ilikuwa haijateuliwa, isipokuwa kwamba, kwa hivi sasa kuna matumaini makubwa ya kupatikana kwa Hati hizo.

Kwa kuwa baadhi ya wanunuzi wa nyumba hizo hawajakamilisha malipo yao, Kamati ya LAAC iliushauri Mfuko kutokuwapatia Hati miliki wanunuzi hao hadi watakapomaliza malipo yao, hivyo, waendelee kutumia Cheti (Certificate).

Aidha, Kamati iliutaka Mfuko uhakikishe kuwa wanunuzi ambao hawajakamilisha malipo yao wanakamilisha malipo hayo katika muda uliokusudiwa.

i. **Uwepo wa uwekezaji usio na tija ikiwemo shilingi bilioni 3.15 zilizowekezwa ZAFICO.**

Majibu ya Mfuko

Ni kweli hadi sasa ZSSF haijaanza kupokea gawio kutoka kwa Kampuni ya ZAFICO. ZSSF inatarajia kuwa Kampuni hiyo itakapoanza biashara itapata faida na kuanza kugawa gawio kwa wanahisa wa Kampuni hiyo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC imeishauri Serikali kutokuyalazimisha Mashirika na Taasisi zake Zinazojitegemea kuingia kwenye miradi au kutekeleza mambo inayohisi inafaa. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya miradi au mambo wanayowaamulia kuyafanya huwa hayana tija kwa upande wao, jambo linalopelekea kuyatia hasara Mashirika au Taasisi hizo.

ii. **Uwekezaji wa baadae umepangwa uwe katika majengo. Mradi wa kukamilisha majengo matatu yaliyopo Mbweni pamoja na utafutaji fedha kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya Mji Mpya wa Kwahani.**

Majibu ya Mfuko

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanya mapitio ya mipango yake ya uwekezaji na kuondoa miradi yote ya majengo ambayo ilitarajiwa kutumia gharama kubwa na kuleta faida ndogo kwa Mfuko. Nguvu kubwa ya uwekezaji kwa sasa imeelekezwa katika uwekezaji wenye gharama ndogo ambayo itazalisha faida kubwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC imeunga mkono maamuzi hayo ya Mfuko na hasa ikizingatiwa kuwa miradi mingi mikubwa iliyofanywa na Mfuko huu inaonesha kuwa haikuleta tija iliyotarajiwa.

iii. **Wigo wa michango hauridhishi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ZSSF imewafikia asilimia 17 tu ya watu walioajiriwa. Aidha, hadi kufika mwisho wa mwaka wa fedha 2020, Mfuko ulikuwa unadai michango ya shilingi bilioni 1.256**

Majibu ya Mfuko

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umejipanga kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kufanya utafiti wenye lengo la kuongeza wigo wa wanachama. Aidha, Mfuko umejipanga kuongeza wastani wa wanachama kutoka asilimia 17 iliyopo hadi kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2025.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na juhudi hizo zilizokusudiwa kuchuliwa na Mfuko huu, Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuhakikisha kuwa michango ya Tsh. Bilioni 1.256 ambayo haijalipwa hadi mwaka wa fedha 2020 inalipwa pamoja na adhabu yake kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 9 cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya mwaka 1998.

iv. **Uongozi wa ZSSF upitie muundo wake wa uwekezaji na ipeleke fedha nyingi katika miradi yenye tija na inayolipa haraka.**

Majibu ya Mfuko

Uongozi wa ZSSF unakamilisha zoezi la kupitia muundo wake wa uwekezaji kwa kutekeleza miradi yenye tija kubwa na inayolipa haraka. Mfuko unategemea kufanya uwekezaji zaidi katika soko la fedha badala ya kufanya uwekezaji katika miradi ya majengo ambayo yana faida ndogo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC iliusisitiza Mfuko kumaliza haraka iwezekanavyo zoezi hilo ili shughuli ya uwekezaji iendelee kwa kuwa ni miongoni mwa chanzo cha mapato cha Mfuko huo.

3.8.2 Mapungufu katika udhibiti wa bajeti iliyoidhinishwa

a. **Matumizi yaliyozidi kiwango cha bajeti pasi na kupata idhini, TZS 2,001,314,302.**

Kanuni nambari 6.2.2 ya Kanuni ya Fedha ya ZSSF inamruhusu Mkurugenzi Mkuu kufanya matumizi kama yalivyoidhinishwa na Bodi ya Wadhamini. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka wa fedha huu, matumizi yalizidi bajeti kwa shilingi 2,001,324,302, na bodi ya wadhamini hawakuidhinisha matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Kanuni nambari 15.5 ya Kanuni ya Fedha ya ZSSF ambayo inasema

“hakuna matumizi yatakayoruhusiwa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa”. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Nambari 4.

Majibu ya Mfuko

Bajeti ya mwaka 2019/2020 ambayo imepitishwa na Bodi ya Wadhamini ya ZSSF iliidhinisha TZS 8,585,960,759.84 kwa matumizi ya kawaida ya uendeshaji, na matumizi halisi ya uendeshaji kwa kipindi husika yalikuwa ni TZS 8,126,242,438 ambapo hakukua na matumizi ya ziada.

Matumizi ya TZS 2,001,314,302 hayakuzidi kiwango kilichoidhinishwa na Bodi bali yalitokana na kuchelewa kwa uhaulishaji wa baadhi ya vifungu vidogo vidogo vya matumizi. Bodi iliidhinisha uhaulishaji wa vifungu hivyo katika Kikao cha Kamati ya Bodi kilichofanyika 18/07/2020 kwa Waraka Na. 1/K.12/KFU/7BD/2020 ambapo Kamati iliridhia uhaulishaji huo na kupeleka mapendekezo yake kwa Bodi ambao pia nao waliridhia.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na maelezo yaliyotolewa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya matumizi yaliyofanywa yalikuwa sio ya haraka. Hivyo, Kamati ya LAAC iliutaka Mfuko huu kuhakikisha kuwa unafuata taratibu zote zilizowekwa ili kuepusha kasoro kama hizo zisijitokeze siku zijazo.

b. Hakuna udhibiti wa moja kwa moja kuhakikisha kuwa matumizi yanadhibitiwa dhidi ya bajeti

Nyaraka za matumizi ikiwemo fomu za maombi ya malipo na hati za malipo hazina maelezo ya udhibiti wa bajeti ili kuangalia kama kifungu husika cha bajeti kimeshatumia fedha zote, hitaji la kufanya uhaulishaji au kifungu kimeshazidi kiwango cha bajeti. Aidha, mfumo wa uhasibu hauna udhibiti wa kuzuia matumizi zaidi ya bajeti.

Majibu ya Mfuko

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii tayari umeimarishwa mfumo wake wa fedha wa Micrsoft NAVISION ili kuweza kutoa tahadhari ya matumizi yaliyozidi bajeti husika.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilitaka kujua mfumo huo ulioanzishwa umeanza lini hata ikawa hauwezi kudhibiti bajeti hiyo sambamba na kujua sababu zilizopelekea mfumo huo kushindwa kudhibiti bajeti ya Mfuko.

Watendaji wa Mfuko waliielezea Kamati hii kuwa mfumo huo umeanza mwaka 2017,

isipokuwa kwamba, mfumo huo ulikuwa unaimarishwa kwa awamu.

Kwa kuwa miaka mingi imepita tangu kuanzishwa kwa mfumo huo, na kwa kuwa baadhi ya mambo yanakuwa ni muhimu kutekelezwa ingawa mfumo umekusudiwa kuimarishwa kwa awamu. Hivyo basi, Kamati ya LAAC iliushauri Mfuko huu kuyachukulia hatua haraka iwezekanavyo mambo yote ambayo yanapaswa kutekelezwa chini ya mfumo huo ili kuepusha hoja zisizo za lazima pamoja na kuondosha dhana mbaya kwa wasimamizi au wafuatiliaji wa Mfuko huo.

c. Ripoti za utekelezaji za kila mwezi haziandaliwi ili kupima utekelezaji

Kanuni ya 7.6.7 ya kanuni inataka kutayarishwa ripoti ya utekelezaji ya mwezi ili kulinganisha na bajeti. Uchambuzi na sababu za tofauti zinahitaji kufuatiliwa kwa makini pamoja na kuchukua hatua muafaka mapema iwezekanavyo. Hata hivyo, ukaguzi haukupata ripoti za utekelezaji ili kupima utekelezaji.

Majibu ya Mfuko

Mfuko ulikuwa ukiandaa ripoti ya miezi mitatu mitatu kupima utekelezaji wa bajeti na kuiwasilisha kwa kamati ya bodi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Mfuko na hasa ikizingatiwa kuwa kuandaa Ripoti kila baada ya miezi mitatu ni kwenda kinyume na matakwa ya Kanuni. Hivyo, Kamati hii iliutaka Mfuko huo kuhakikisha kuwa inaandaa Ripoti ya mwezi ili uweze kujipima kiutendaji katika mwezi husika na kuanza kuzichukuliwa hatua kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza na baadae iandae Ripoti ya miezi mitatu ambayo itawasilishwa katika Kamati ya Fedha ya Bodi hiyo.

3.8.3 Udhaifu katika usimamizi na udhibiti wa mapato ya kodi za pango.

Ukaguzi umebaini kasoro zifuatazo katika usimamizi wa mapato ya kodi ya pango:

a) Uwepo wa deni la muda mrefu la wadaiwa shilingi milioni 826

Uzoefu wa upangishaji unataka kodi kulipwa kwa kutangulizwa fedha kabla ya nyumba kukaliwa na mpangaji. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa ZSSF inaruhusu wapangaji kutumia ofisi na nyumba pasi na kulipa kodi. Ukaguzi ulitembelea majengo ya Mbweni, Mwanakwerekwe, Hoteli ya Mapinduzi na hoteli ya Archipelago na umebaini uwepo wa kodi inayodaiwa ya shilingi milioni 826.

Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Madeni yatokanayo na ukodishwaji wa maje ngo ya ZSSF

Namba	Jengo lililokodishwa	Fedha za kodi zinazodaiwa (Shs.)
1	NIDA	54,500,000
2	Archipelago Hotel	180,220,236
3	Mnarani - PBZ	14,016,884
4	Zanzibar Cable Television	56,000,000
5	Mwanakwerekwe	89,419,611
6	Jumba la Treni	38,000,000
7	Mbweni Old	169,212,078
Jumla		**592,368,809**

i) Ufuatiliaji mdogo wa kodi inayodaiwa. Hakukuwepo na ripoti za uongozi zilizotayarisha kuhusiana na kodi zinazodaiwa na maamuzi ya uongozi.

ii) Mfumo hauwezi kutoa Ripoti ya umri au muda wa madeni yanayodaiwa.

iii) Hakuna mikataba na wapangaji.

Majadiliano ya Kamati juu ya hoja hizo ni kama ifuatavyo:

Majibu ya Mfuko
Mfuko ulifanya jitihada ya kupunguza kodi inayodaiwa ya TZS 826 milioni

i. **Ufuatiliaji mdogo wa kodi zinazodaiwa. Hakukuwepo na ripoti za uongozi zilizotayarishwa kuhusiana na kodi zinazodaiwa na maamuzi ya uongozi.**

Majibu ya Mfuko
Ripoti zinawasilishwa kwa uongozi wa Mfuko zinazoonesha kodi zinazodaiwa, hali za nyumba, hali za mikataba na changamoto zinazotokea na hatua zinazochukuliwa kuondoa changamoto zilizojitokeza.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Kamati ya LAAC imeitaka ZSSF kufuatilia kwa ukaribu madeni hayo ili kuhakikisha kuwa mapato ya Mfuko yanaongezeka.

ii. Mfumo hauwezi kutoa ripoti ya umri au muda wa madeni yanayodaiwa

Majibu ya Mfuko
Mfuko utafanya jitihada za kuweza kupata ripoti za umri wa madeni kwenye mfumo kwani katika mahitaji ya mwanzo kaikuwemo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Kutokana na majibu hayo ya Mfuko, Kamati hii imeibakisha hoja hii kama ilivyo.

iii. Hakuna mikataba ya wapangaji

Majibu ya Mfuko
Mikataba ya wapangaji imetayarishwa na kusainiwa na wapangaji na wanunuzi wa nyumba za Mbweni. Bado kuna baadhi ya wapangaji ambao hawajarejesha mikataba kutokana na kuwa wapo nje ya nchi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Kwa kuwa Mfuko umekiri kuwa baadhi ya Wapangaji hawajarejesha mikataba yao, hivyo, Kamati hii imeibakisha hoja hii kama ilivyo na imewataka watendaji wa Mfuko kuhakikisha kuwa wapangaji wote wanajazishwa mikataba na kuirejesha kama taratibu zinavyoelekeza.

3.8.4 Kasoro zilizobainika katika mikopo ya wafanyakazi

Ukaguzi umebaini kasoro zifuatazo katika usimamizi wa mikopo ya wafanyakazi:

a. Mikopo ya wafanyakazi iliyotolewa TZS bilioni 1.154 haikuthibitishwa na Bodi ya Wadhamini

Ukaguzi umebaini kuwa bajeti ya mikopo ya wafanyakazi kwa mwaka unaoshia 30 June, 2020 ilikuwa ni TZS milioni 500, hata hivyo mikopo iliyotolewa kwa mwaka ni billioni 1.154. Kanuni za fedha za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii zinamtaka Mkurugenzi Mkuu kutumia fedha kama zilivyotajwa na kuidhinishwa katika bajeti, kwa tofauti hiyo kubwa kulikuwa na haja ya kupata idhini ya Bodi, hata hivyo ukaguzi haukupatiwa idhini ya Bodi kwa tofauti hiyo.

Majibu ya Mfuko

Ongezeko hilo la fedha kwa mkopo wa wafanyakazi iliidhinishwa na Bodi ya Wadhamini kupitia Kikao cha Kamati cha 18/07/2020 Waraka Na. 1/K.12/KFU/7BD/2020 na kuridhiwa pia na Kikao cha Bodi baada ya kupata mapendekezo ya Kamati.

Ucunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Kikao cha Bodi ya Wadhamini kilifayika katika mwaka wa fedha 2020/2021 na sio katika mwaka unaohusika (2019/2020), hivyo, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

Sambamba na hayo, Kamati hii ilibaini kuwa matumizi hayo yalifanyika kwanza na baadae ndio yakawasilishwa mbele ya Bodi ya Wadhamini kwa ajili ya kupata idhini jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC iliutaka Mfuko huu kutekeleza majukumu yake kama Sheria zinavyoelekeza na sio kufanya kazi kwa mujibu wa utashi wao.

Vile vile, Kamati ya LAAC iliishauri Bodi kuhakikisha kuwa Watendaji wa Taaisi hii wanatekeleza majukumu yao kama Sheria zinavyoelekeza kwani endapo Bodi zitaridhia mambo ambayo yametekelezwa kinyume na Sheria itaashiria kuwa ama Bodi hiyo haina wataalamu kuhusiana na majukumu yake au Watendaji wa Mfuko wanawarubuni Wajumbe wa Bodi kwa kuwapatia fedha kidogo kwa lengo la kuridhia kila kinachowasilishwa mbele yao.

Sambamba na maelezo hayo, Kamati ya LAAC inazidi kusisitiza kuwa, kiujumla endapo Taasisi itashindwa kutekeleza shughuli zake ipasavyo basi na Bodi ya Taasisi hiyo inahesabika pia kuwa nayo imeshindwa.

b. Mikopo iliyotolewa haikuwa na kodi

Sheria ya kodi yamwaka 2004 inaainisha vigezo vya mikopo kutokukatwa kodi ni lazima isiwe mara tatu ya mshahara na iwe imerejeshwa si zaidi ya miezi 12. Hata hivyo, tumebaini kuwa mikopo inazidi mara tatu ya mishahara haina riba na inarejeshwa zaidi ya miezi 12.

Majibu ya Mfuko

Mfuko ulipata ridhaa ya Bodi ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi bila ya riba ikiwa kama motisha kwa wafanyakazi na kwa sasa Mfuko unaandaa utaratibu wa kutekeleza Sheria

ya Kodi ya mwaka 2004.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilihoji kwa nini Sheria husika haikutekelezwa ipasavyo na Mfuko huo na kupelekea kuikosesha mapato Serikali?. Watendaji wa Mfuko waliieleza Kamati hii kuwa Mwanasheria aliyekuwepo wakati ule alikuwa hajui kama kuna kifungu cha Sheria kinachohitaji kulipwa kodi hiyo.

Kwa kuwa misingi ya Sheria inaeleza kuwa kutokujua Sheria sio utetezi Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Mfuko na imewataka Watendaji wa Mfuko kutekeleza majukumu yao kama Sheria za nchi zinavyoelekeza.

Vile vile, Kamati ya LAAC imebaini kuwa ni kweli mikopo hiyo haikuwa na ukomo kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hivyo, hoja hiyo imebaki kama ilivyo.

Sambamba na hayo, Kamati ya LAAC iliikagua orodha ya mkopo ya watumishi na kujiridhisha kuwa watumishi hao wana uwezo wa kulipa mikopo yao hiyo kinyume na ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti. Hivyo, utolewaji wa mikopo hiyo imezingatia kanuni ya 84 ya Kanuni za Utumishi za Umma 2014.

3.8.5 Kukosekana kwa uthibitisho kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa malipo ya gharama za awali za mradi wa mji mpya Kwahani, TZS Billioni 1.19.

Tarehe 4 Oktoba, 2019 ZSSF iliingia mkataba na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya ufadhili wa Mradi wa Mji Mpya Kwahani. Katika utangulizi, mkataba huo unasema kwamba Mkopaji (Wizara) amekubali kulipa gharama za awali zilizolipwa na Mkopeshaji (ZSSF) pasi na kutaja gharama halisi zilizolipwa hadi mkataba huo unakwenda saini. Gharama za awali zilikuwa ni shilingi 1.19 wakati wa kusaini Mkataba. Bakaa ni kubwa na thamani yake ilipaswa kutajwa katika Mkataba.

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa barua ya tarehe 6 Oktoba, 2019 kutoka ZSSF kwenda kwa Katibu Mkuu (OR) Fedha na Mipango inayoomba uthibitisho kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Hata hivyo, ukaguzi hakupata barua kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango iliyokubali bakaa iliyodaiwa. Hali hii inaleta maswali iwapo gharama za awali za Mradi zitarejeshwa kwa ZSSF ama hazitarejeshwa.

Kukosekana kwa barua kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inayokubali bakaa inayodaiwa na ZSSF inawezekana kuwa imepata hasara ambayo haitalipika baadae.

Ukaguzi unashauri ZSSF waombe barua ya kukubali deni *(commitment letter*) kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa gharama za awali zilizotumika.

Majibu ya Mfuko

Kwa sasa Mfuko ushawasiliana na Ofisi ya Rais. Fedha na Mipango juu ya deni hilo kwa barua Namba ZSSF/A.B199/246/69/01 ya tarehe 24 Mei, 2021 na deni hilo litakuwa ni sehemu ya mkopo wa TZS billioni 20 ambapo, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango umekopa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa mji mpya wa Kwahani.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilielezwa mambo yafiatayo:

1. Jumla ya gharama za awali zilizotumika katika mradi huo ni Tsh. 1.11 bilioni na sio Tsh. bilioni 1.19 kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
2. Mfuko umeipatia Ofisi ya Rais ya Fedha jumla ya Tsh. 19,170,265,483.35 kwa ajili ya ujenzi wa mji mpya wa Kwahani ambapo mkataba uliofungwa tarehe 04 Oktoba, 2019 unaonesha kuwa mkopo huo ni wa Tsh. 20,000,000,000.
3. Mkopo huo ulitakiwa kulipwa kuanzia mwezi wa Disemba, 2020. Hata hivyo, hadi Kamati hii inafanya ziara katika Mfuko huo tarehe 08 Novemba, 2021 fedha hizo hazijaanza kulipwa jambo ambalo ni kinyume na mkataba uliofungwa.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC iliandaa kikao cha pamoja na Mfuko huu na Watendaji wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango tarehe 18 Januari, 2022 ili kupata ufafanuzi zaidi wa suala hilo na yafuatayo yamebainika:

1. Mawasiliano mbali mbali kuhusiana na utekelezwaji wa mradi na ulipwaji wa mkopo huu yalifanywa kwa njia ya mazungumzo baina ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Mfuko Ndg. Sabra Machano na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Ndg. Iddi Haji Makame. Kitendo hiki ni kwenda kinyume taratibu za kiofisi kwa mujibu wa kanuni ya 48(2) ya Kanuni za Utumishi ya mwaka 2014.

   Katika mazungumzo yao hayo, walikubaliana kuwa matumizi ya fedha za awali yaliyofanywa na Mfuko ambayo ni jumla ya Tsh. 1.111 bilioni yasiingizwe kwenye mkataba na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango itazilipa fedha hizo kwa kutumia fedha zake za Matumizi Mengineyo (OC).

   Vile vile, walikubaliana kuwa fedha za mkopo zilipwe baada ya Mkandarasi kuwasilisha Cheti “Certificate” na sio kulipwa kwa mkupuo mmoja.

2. Gharama zote za ujenzi wa mji mpya wa Kwahani ukitoa gharama za awali ni jumla ya Tsh. 18 bilioni. Hivyo, Mfuko umeikopesha Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango jumla ya Tsh. 19,170,265,483.35, isipokuwa kwamba, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango itawajibika kulipa Tsh. 27,862,500,000 pamoja na riba.
3. Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango umekubali kulipa matumizi ya awali yaliyofanywa na Mfuko kuhusiana na ujenzi huo.
4. Viongozi wa sasa wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar walikaa pamoja na kukubaliana kuwa uandaliwe mkataba wa nyongeza "Addendum" na ueleze mambo yote ambayo hayakuwemo katika mkataba wa awali ili kuwa na kumbukumbu sahihi na kile kinachotekelezwa.
5. Kwa kuwa kulitolewa muda wa msamaha "grace period" mkopo huo sasa utalipwa kuanzia tarehe 01 Mei, 2022.

Kutokana na maelezo hayo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imuandikie barua Mkurugenzi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na nakala ya barua hiyo itumwe kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na kuridhia kwa Ofisi hiyo kulipa matumizi ya awali yaliyofanywa na Mfuko huo juu ya ujenzi husika na barua hiyo iandikwe ndani ya siku tatu kuanzia siku ya kikao hicho.
2. Ofisi hizi zihakikishe kuwa mkataba wa nyongeza "Addendum" utakaoandaliwa ujumuishe mambo yote ambayo hayakuwemo katika mkataba wa awali ili kuwa na kumbukumbu sahihi na kile kinachotekelezwa pamoja na kuwa na uwelewa wa pamoja juu ya suala husika kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa masharti yaliyofikiwa.
3. Watendaji wa Serikali wahakikishe kuwa wanafanya mawasiliano ya kikazi kwa maandishi kama Kanuni za Utumishi zinavyoelekeza ili kuwa na kumbukumbu sahihi ya kile kilichokubaliwa na kinachotekelezwa. Hatua hii pia, hutoa fursa kwa mtu yeyote anayehitaji kutoa au kupata taarifa juu ya jambo husika kupata nafasi hiyo baada ya kuisoma taarifa hiyo.

   Kamati ya LAAC imelisisitiza hili kwani ni kawaida kwa watendaji wa umma kuhama sehemu moja kwenda sehemu nyengine, hivyo, hata ikitokea mtendaji kuondoka katika sehemu hiyo basi isiwe kikwazo kwa watendaji wengine kujua taarifa za kina juu ya jambo fulani.

3.10 SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)

Taarifa ya Mapato

Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020 limepangiwa kukusanya jumla ya Tsh. 1,500,000,000.00 kutoka katika vyanzo vyaka vya ndani na kutarajiwa kupata Tsh. 4,120,900,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka katika mfuko mkuu wa Serikali.

Hadi kufikia tarehe 30 June, 2020 jumla ya Tsh. 793,735,630.94 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ambayo ni sawa na asilimia hamsini na mbili nukta tisa (52.9) ya makadirio na kupata Tsh. 3,441,852,125 ambayo ni Ruzuku kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ambayo ni sawa na 83.5 ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Ni kweli kwamba katika mwaka huo wa fedha Shirika hili lilikusanya kiwango hicho cha fedha kupitia vyanzo vyake kama ifuatavyo:

Nam.	Chanzo cha Mapato	Makadirio	Mapato halisi	Asilimia ya Mapato
1.	Ruzuku kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali	4,120,900,000	3,441,852,125	83.5%
2.	Makusanyo ya vyanzo vya ndani	1,500,000,000	793,735,630.94	52.9%
Jumla		**5,620,900,000**	**4,235,587,755.94**	**75.4%**

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalijitokeza:

1. Kamati ya ilitaka kujua sababu zilizopelekea Shirika hili kushindwa kufikia malengo iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2019/2020, ambapo, ilielezwa kama ifuatavyo:
    a. Shirika lilipendekeza kukusanya jumla ya Tsh. 800,000,000, hata hivyo, Wizara inayohusiana na masuala ya Fedha ililitaka kukusanya Tsh. 1,500,000,000 kiwango ambacho hakiendani na uhalisia wa vianzio vyake vya mapato.
    b. Shirika halikurusha vipindi vingi kwa njia ya mubashara “live” kutokana na maradhi ya uviko 19. Hii ni kutokana na kuwa watu wengi walishindwa kutoa mashirikiano kutokana na masharti yaliyowekwa juu ya maradhi hayo. Vipindi vinavyorushwa kwa njia hii ndio vyenye tija zaidi.
    c. Shirika lilishindwa kuwafikia Washirika wao wa maendeleo kwa ajili ya kufanya “lobbing” kutokana na maradhi ya uviko 19.

2. Taarifa za Hesabu za Mapato na Matumizi zilizoelezwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani wa Shirika zimetofautiana na taarifa zilizoelezwa kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) ya Shirika.
3. Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani wa Shirika ilikuwa haiwasilishwi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama kifungu cha 117(6) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kinavyoelekeza.
4. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikuwa haifanyii kazi taarifa ya Mkaguzi wa Ndani wa Shirika kwa kuwa taarifa yake ilikuwa haijadiliwi kwenye Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya Shirika.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro zilizobainika Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Kitengo cha Mapato ihakikishe kuwa inavifanyia uhakiki vianzio vya ndani vya mapato vya kila Taasisi kabla ya kuzipangia kiwango cha kukusanya ili kuepusha malalamiko yasiyo ya lazima sambamba na kutozitia dosari Taasisi hizo kwa kuonekana kuwa hazikufikia malengo.
2. Wakaguzi wa Ndani wa Taasisi mbali mbali wahakikishe kuwa wanaziwasilisha taarifa za ukaguzi za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama Sheria ya Fedha inavyoelekeza.
3. Wakaguzi wa Ndani wa Taasisi mbali mbali wahakikishe kuwa taarifa za fedha wanazozieleza kwenye taarifa zao zimetolewa na mtendaji au chanzo sahihi ili kuwa na taarifa zinazofanana katika Taasisi moja.
4. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali azichukulie hatua Taasisi zote ambazo haziwasilishi taarifa za ukaguzi wa ndani kama Sheria inavyoelekeza.

Taarifa ya Matumizi

Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha Tsh. 5,620,900,000 kwa kazi za kawada pamoja na mishahara. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020, Shirika limeingiziwa Tsh. 4,181,912,094.49 ambayo ni sawa na 74.4% ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Ni kweli kwamba katika mwaka wa fedha husika Shirika hili lilitumia jumla ya kiasi hicho cha fedha ikiwa ni upungufu wa Tsh. 1,438,987,906.51 ambayo ni sawa na 25.6% ya makadirio.

Upungufu huo umeleta usumbufu kwa baadhi ya kazi kutokamilika kwa wakati. Kazi

zenyewe ikiwemo:

(i) Ukarabati wa minara;
(ii) Ukarabati wa baadhi ya majengo na ofisi za Shirika;
(iii) Ukarabati wa uzio wa Masingini;
(iv) Upatikanaji wa hatimiliki kwa baadhi ya maeneo ya Shirika.

Pamoja na upungufu huo, Shirika liliweza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mpango kazi wake ili kukwepa kuachwa nyuma katika ushindani wa soko la habari ambalo kwa sasa limevamiwa na vyombo vingi vya habari.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalibainika:

1. Umoja wa Maaskari Wastaafu (UMAWA) walifunga mkataba na Shirika hili kwa kazi ya ulinzi kwa thamani ya Tsh. 35,280,000. Hata hivyo, Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka inaonesha kuwa matumizi yaliyofanywa kwa mwaka huo ni Tsh. 46,576,517. Hii ni kutokana na kuwa Shirika hili lilikuwa linadaiwa na Umoja huo katika mwaka uliopita. Hivyo, kwa kuwa Shirika linafunga hesabu zake kwa kutumia mfumo wa “Cash” imebidi malipo hayo yajumuishwe pia kwenye taarifa hiyo.
2. Watendaji wa Shirika hawaelewi sababu iliyopelekea Umoja huo ukawa unalidai Shirika hili hasa ikizingatiwa kuwa fedha za ulinzi zilipaswa kulipwa kwa mujibu wa masharti yaliyoelezwa kwenye mkataba huo.
3. Baadhi ya matumizi hufanyika kila mwaka isipokuwa kwamba, Shirika halitengi bajeti kwa ajili ya shughuli hizo. Kwa mfano; Tukio la kusherehekea mwaka.

Kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC ililishauri Shirika kutenga bajeti kwa kila shughuli ambayo inatekelezwa ndani ya Shirika hilo ili kuepuka kuwa na dhana mbaya juu ya matumizi inayoyafanya.

3.10.1 Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani

Kwa mujibu wa kifungu cha118(1) cha Sheria ya fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, inataka kila Taasisis inayohusika na bajeti ya Serikali kuwa na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani itakayoteuliwa na Afisa Mhasibu kwa kushauriana na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Utangazaji Zanzibar halina Kamati ya Ukaguzi wa Ndani.

Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kunapelekea kutokuwepo kwa chombo kitakachosimamia na kuleta mawasiliano ya vihatarishi na kutoa taarifa kwenye maeneo husika kwa Shirika pamoja na kutoa ushauri kwa Afisa Mhasibu juu ya hatua za

kuchukuliwa kutokana na mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti ya ukaguzi wa ndani au kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali.

Majibu ya Shirika

Shirika la Utangazaji Zanzibar tokea kuanzishwa kwake lilikuwa likitumia Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo. Kamati hiyo ilitumika kutokana na kukosekana kwa Kamati ya Shirika. Hali hii ilitokana na kuchelewa kukamilika kwa muundo wa Shirika ambao hadi kufikia Juni, 2020 baadhi ya Wakurugenzi wa ndani walikuwa bado hawajateuliwa na baadhi ya walioteuliwa kuchelewa kuthibitishwa na Ofisi ya GSO. Kwa sasa Shirika linayo Kamati yake ya ukaguzi wa ndani ambayo inaendelea na majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha ili kuimarisha usimamizi wa ndani.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Shirika hasa ikizingatiwa kuwa Shirika hili liliundwa tangu mwaka 2013 hivyo, Kamati hiyo ilipaswa kuundwa tangu mwaka huo ili kuheshimu matakwa ya Sheria husika. Vile vile, kutokukamilika kwa muundo wa Shirika hakuzuwii Shirika hili kushindwa kuunda Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kwa kuwa Wakurugenzi waliokuwa hawajateuliwa hawahusiki moja kwa moja na Kamati hiyo. Kwa mnasaba huo, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

3.10.11 Mapungufu katika matumizi ya mafuta ya Shilingi 151,517,080

Ukaguzi ulipitia taarifa za usimamizi wa mafuta na kufanya ulinganisho wa rekodi zilizo kwenye madaftari la kuhifadhia kumbukumbu za mafuta.

Jumla ya shilingi 151,517,080 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta, malipo ambayo yalilipwa kwa wasambazaji wa kampuni ya United Group Limited shilingi 133,517,080 na shilingi 18,000,000 kutoka Zanzibar Petroleum kwa ajili ya matumizi ya Shirika. Aidha, ukaguzi umebaini kujitokeza kwa mapungufu mbali mbali ya kiutendaji katika uwekaji wa kumbukumbu za mafuta hayo, kasoro zenyewe ni kama hizi zifuatazo: -

i. Kutokuwepo kwa daftari la kuonyesha mapokezi na matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa na Shirika.

ii. Kutokuwepo na taarifa za ulinganishaji wa kumbukumbu za matumizi ya mafuta katika daftari la kurikodiwa mafuta ya Shirika na Kampuni ya Mafuta ili kuweza

kuangalia taarifa za usuluhishi wa mafuta.

iii. Kukosekana kwa mkataba wa manunuzi baina ya Shirika na Kampuni ya Mafuta.

Matumizi ya mafuta kwa Shirika yanagharimu fedha nyingi sana, hivyo basi, kutakuwa na uwekaji na utunzaji mzuri wa kumbukumbu za mafuta huweza kupelekea mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, kutokuwepo kwa taarifa za usuluhishi wa mafuta yaliyonunuliwa na kutumika kulipelekea kushindwa kutambua matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa matumizi yasiyofaa ya mafuta.

Katika kufuatilia hoja hizi yafuatayo yalijitokeza:

a. **Kutokuwepo kwa daftari la kuonyesha mapokezi na matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa na Shirika**

Majibu ya Shirika

Shirika la Utangazaji Zanzibar lilitumia fedha hizo kwa ununuzi wa mafuta kwa kazi za Shirika. Kazi hizo zikiwemo kazi za utafutaji na ufuatiliaji wa habari na kurusha matangazo ya moja kwa moja kwa kazi za Serikali kutoka katika maeneo tofauti Unguja na Pemba. Katika kutunza kumbukumbu za uingizaji na utoaji wa mafuta Shirika lilitumia daftari maalum kwa ajili ya udhibiti wa mafuta. Daftari hilo lilikuwa na mapungufu katika rekodi zake.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea Shirika hili kutokuwa na daftari hilo katika mwaka huo wa fedha, ambapo Watendaji wa Shirika waliieleza Kamati hii kuwa daftari lilikuwepo isipokuwa kwamba, katika daftari hilo kulikuwa na mapungufu mbali mbali kutokana na kutokuwepo kwa Mtunza Ghala kwa wakati ule.

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu hayo, kwa kuwa wakati Kamati hii inafuatilia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2017/2018 tarehe 13 -14 Januari, 2021 ilihoji kuhusiana na daftari la kutunzia mali ambapo, Shirika hili liliieleza Kamati kuwa mapungufu yaliyobainika kwenye daftari hilo yalijitokeza kwa kuwa Shirika halina Mtunza Ghala, hata hivyo, tayari Shirika limeshaomba mtendaji huyo kunakohusika.

Sambamba na maelezo hayo, Kamati ya LAAC ilitaka kujiridhisha na maelezo ya Shirika kwa kulikagua daftari hilo ambapo, Shirika liliipatia Kamati ya LAAC daftari hilo na kulikagua. Cha kushangaza wakati Mdhibiti anafanya ukaguzi wake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 daftari hilo hakupatiwa na kuandika hoja hiyo kama inavyojieleza.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea Watendaji wa Shirika wasimpatie daftari hilo Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alivyofanya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2019/2020 wakati daftari hilo lilikuwepo. Vile vile, Kamati ilitaka kujua Mtunza Ghala huyo alianza lini kazi katika Shirika hilo?.

Watendaji wa Shirika hawakuwa na majibu juu ya maswali yote hayo ya Kamati, hali hii ilipelekea Kamati hii kuwa na mswali mbali mbali juu ya Watendaji wa Shirika na hata ilidiriki kuwaambia kuwa inawezekana waliipatia Kamati daftari hilo lilipofika ofisini hapo tarehe 13 -14 Januari, 2021 wakifikiria kuwa Kamati hiyo haina uweledi juu ya suala hilo na Afisa wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yeye hakupewa kwa kuwa ni mtaalamu na anaweza kutoa dosari mbali mbali ndani ya daftari hilo.

Vile vile, Kamati ya LAAC baada ya kulipitia daftari hilo ilibaini yafuatayo:

b. Baadhi ya gari huingiziwa mafuta kila siku tena kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano; gari yenye namba ya usajili SMZ 475B iliingiziwa mafuta katika mtiririko ufuatao:

Namba	Tarehe	Idadi ya Litre
1.	10/03/2020	30
2.	11/03/2020	40
3.	12/03/2020	30
4.	13/03/2020	30

i. Hakuna “log book” lililothibitisha matumizi ya gari hiyo, hali hii ilizidi kuitia mashaka Kamati juu ya matumizi ya mafuta ya gari hii.

ii. Shirika huingiza mafuta kwenye gari za Watendaji wake jambo ambalo ni kinyume na utaratibu. Hata hivyo, Shirika liliieleza Kamati kuwa hali hiyo imefikiwa kutokana na tatizo la uhaba wa gari lililokuwa linalikabili Shirika hili.

iii. Kamati haikuona taarifa za utokaji wa mafuta kutoka tarehe 14 Machi, 2020 hadi tarehe 06 Mei, 2020.

Kiujumla Kamati ya LAAC haikupendezewa na hali hiyo na iliwataka Watendaji wa

Shirika kutekeleza majukumu yao vyema pamoja na kumheshimu mtu yeyote anayefika ofisini hapo.

c. **Kutokuwepo na taarifa za ulinganishaji wa kumbukumbu za matumizi ya mafuta katika daftari la kurikodiwa mafuta ya Shirika na Kampuni ya Mafuta ili kuweza kuangalia taarifa za usuluhishi wa mafuta**

Majibu ya Shirika

Kampuni ya United Group LTD haina utaratibu wa kutoa '*Statement*' ya mafuta jambo ambalo lilipelekea Shirika hili kushindwa kufanya upatanisho (reconciliation) wa matumizi mafuta. Kutokana na hali hiyo, Shirika liliamua kuchukua mafuta katika Kampuni ya United Group LTD.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC ililishauri Shirika hili kabla ya kuingia mkataba na mtu mwengine kufanya utafiti wa kina juu ya utendaji wa mtu huyo ili kuepuka usumbufu usio wa lazima pamoja na kuweza kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za nchi.

Kamati ya LAAC haikuwa na maelezo zaidi na kutokana na majibu ya Shirika hoja hii imebaki kama ilivyo.

d. **Kukosekana kwa mkataba wa manunuzi baina ya Shirika na Kampuni ya Mafuta**

Majibu ya Shirika

Kwa upande wa mikataba na watoa huduma, Shirika lilikuwa likichukua mafuta yake kutoka katika Kampuni ya United Group LTD ambapo baada ya kuona Kampuni hiyo haitoi '*Statement*' ya mafuta kwa ajili ya kufanya upatanisho (reconciliation) wa matumizi mafuta. Uongozi wa Shirika uliamua kuhama kwenye Shirika hilo na kuanza makubaliano mapya na Kampuni ya Zanzibar Petroleum.

Kampuni hiyo ina utaratibu wa kutoa mikataba kwa wateja, lakini hadi kufikia Juni, 2020 Kampuni ya Zanzibar Petroleum walikuwa hawajatoa mkataba wa kazi hiyo kwa Shirika. Kwa sasa, Shirika linaendelea na mkataba wa mafuta na Kampuni ya Zanzibar Petroleum katika Kituo kilichopo Kijangwani.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikuwa na maelezo zaidi juu ya majibu ya Shirika na kutokana na majibu ya Shirika, hata hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

3.11: SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

Taarifa ya Mapato

Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) lilikusanya Tsh. 27,234,629,383 kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Majibu ya Shirika

Ni kweli Shirika lilikusanya kima cha 27,234,629,383 kikiwa ni mapato yaliyotokana na vyanzo vyao mbali mbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa karafuu, mapato yatokanayo na mafuta na mapato yatokanayo na majengo. Mapato hayo ni makubwa ukilinganisha na mwaka 2016/2017 kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya karafuu yakiwa ni tani 5450 wakati mwaka 2016/2017 tani za karafuu zilikuwa 2206. Kwa maana hiyo, mapato ya Shirika hasa katika eneo la uuzaji wa karafuu, hupanda na kushuka baina ya mwaka mmoja na mwengine.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipofanya mahojiano na Shirika kuhusiana na vyanzo vyao mbali mbali vya mapato imejiridhisha kuwa, katika vyanzo vyao vya majengo, kwa mfano maghala, imebaini kuwa yapo yaliyochakaa na mabovu, kiasi ambacho hukwamisha juhudi za makusanyo ya mapato yatokanayo na chanzo hiki.

Kamati imefanya ukaguzi katika majengo mbali mbali ya Shirika, ikiwa ni pamoja na maghala na kujiridhisha kuwa, kuna baadhi ya maghala hayo hayakukodishwa kwa mwaka 2017/2018, kwa mfano ghala la Malindi, wakati liliekewa bajeti ya kukusanya Tsh. 7,000,000 kwa mwaka huo wa fedha. Aidha, Kamati ilipofanya ziara maghala ya Shirika yaliyopo Saateni, imepata taarifa ya maghala yaliyokodishwa kwa Kampuni ya 'Ever Green' lakini ilipofanya ukaguzi wa Mkataba husika, imegundua kasoro ya kukosa saini ya 'Accounting Officer'. Vile vile Kamati ilibaini kuwepo kiwanda cha Kuchonga lakini hakikutajwa wala kuainishwa kwa Kamati kuwa ni chanzo cha mapato cha Shirika, hali inayothibitisha wazi kuvuja kwa mapato ya Shirika la ZSTC.

Aidha, Kamati imekubaliana na Shirika kuhusiana na Tawi lao lilioko Dubai kuwa kwa sasa kutokana na mabadiliko mbali mbali, tawi hilo limekuwa mzigo kwa Shirika badala ya kuleta faida iliyokusudiwa. Kamati imebaini kuwa, wakati tawi hili linafanya vizuri lilikuwa halitozwi kodi, ila kwa sasa Shirika linalazimika kulipa kodi.

Aidha, tawi hilo hivi sasa halifanyi vizuri kimapato kutokana na kuongeza kwa

maendeleo ya sayansi na teknolojia ambapo biashara hufanywa kwa teknolojia zaidi kuliko ulazima wa kuwekwa duka sehemu fulani. Vile vile tawi hilo limekuwa ni mzigo kwa Shirika, na katika hali ya kupunguza gharama, Shirika limeamua kurejesha 'Go down' na wamebakia na mlango tu.

Kuhusiana na vyanzo vya mapato vya Shirika vilioko Makonyo Pemba, ambavyo ni Kiwanda cha Makonyo kinachozalisha mafuta mbali mbali, Shamba linalotumika zaidi kuzalisha mali ghafi za kiwanda na kupandwa mazao mengine na Nyumba ya Wageni iliopo hapo hapo Makonyo, Kamati imekuwa na wasi wasi mkubwa wa kuvuja kwa mapato ya Nyumba hiyo ya wageni hasa baada ya Shirika kushindwa kuiridhisha Kamati katika udhibiti mzima wa idadi halisi ya wageni wanaolala na kupata huduma mbali mbali katika nyumba hizo na mapato yanayokusanywa. Kwa mfano, makisio yaliyokisiwa kukusanywa kwa mwaka 2017/2018 kwa Nyumba za Wageni na Ukumbi wa Mikutano (ambao kwa masikitiko, Kamati haikuelezwa hasa mapato ya Ukumbi huo) ilikisiwa Tsh. 95,000,000/- lakini taarifa zilizofika kwa Kamati ni kukusanywa kwa Tsh. 6,000,000 pekee.

Vile vile, kuhusiana na Chanzo cha Mapato cha Shamba huko Pemba, Kamati imebaini kuwa kuna miti mbali mbali ya mikaratusi na miti mengine iliyomo katika Shamba hilo inakatwa na kuuzwa kwa ajili ya matumizi ya miti ya kujengea na wengine kufanya kuni za kupikia, lakini taarifa za mapato yake hazikuianishwa kwa Kamati. Na jambo la kushangaza ni pale Kamati ilipoelezwa kuwa mapato hayo hayaainishwi katika taarifa za mapato za Shirika, wakati kwa mauzo yanayofanyika, kuna kiwango Fulani cha fedha kinachopatikana.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika lizidishe jitihada ya kuyakarabati maghala yake mbali mbali yaliyochakaa, ili yaweze kuliingizia Shirika mapato kwa uhakika. Kuhusiana na Kituo cha ZSTC Dubai, Kamati inalishauri kufanyiwa utafiti suala hili hasa ikizingatiwa kuna mabadiliko makubwa ya kibiashara na teknolojia kwa wakati tulionao sasa, hivyo ni vyema baada ya utafiti huo, Shirika likapeleka Waraka Serikalini ili kupata maamuzi sahihi juu ya ya tawi hilo kwa vile sasa linaendeshwa kwa hasara.

Bodi ya Shirika lisimamie kwa karibu mapato yanayokusanywa kupitia nyumba za wageni iliopo Makonyo kwani kuna mianya mingi ya kupenya kwa mapati hayo, hasa katika eneo la kutunza kiikamilifu taarifa za wageni wanaofika na kupata huduma ya nyumba hiyo. Kamati inaendelea kuitaka Serikali isimamie kwa karibu vyanzo vya mapato vinavyosimamiwa na Shirika huko Pemba, ili viweze kuwa na tija kwa Shirika.

Taarifa ya Matumizi

Kwa mwana wa fedha 2017/2018, Shirika la Biashara la Taifa lilitumia Tsh. 19,782,036,133. Na kwa kulinganishwa na mwaka 2016/2017, Shirika lilitumia Tsh. 12,183,774,726 huku kukiwa na ongezeko la Tsh. 7,598,261,407 sawa na 62.4% ya ongezeko.

Majibu ya Shirika

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Shirika lilitumia Tsh. 19,782,036,133 ukilinganisha na mwaka 2016/2017 ambapo Shirika lilitumia Tsh. 12,183,774,726, kukiwa na ongezeko la Tsh. 7,598,261,407 sawa na 62.4% ya ongezeko.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imeelezwa kuongezeka kwa matumizi hayo kunatokana na kuongezeka kwa msimu wa karafuu, hali iliyopelekea Shirika kutumia zaidi kuliko mwaka 2016/2017. Lakini fedha zote hizo, Tsh. 19,782,036,133 ni gharama za uendeshaji pekee (operating expenses) na haziusiani na fedha za ununuzi wa karafuu, huku Kamati ikibaini kuongezeka kwa kiwango kikubwa hicho, wakati bajeti iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika, ilikuwa ni matumizi ya Tsh. 12.5 Bilioni.

Hata hivyo, baada ya mahojiano ya muda mrefu, Kamati ilielezwa kuwa, matumizi hayo yalipata ridhaa ya Bodi. Lakini ilipohitaji uthibitisho wa kumbu kumbu za Kikao cha Bodi kilichoidhinisha na Bajeti ya ziada (supplementary budget), Shirika liliwasilisha kumbukumbu ambayo Kamati imeiridhia kuwa ni uthibitisho uliotakiwa, lakini imebaini zaidi kuwa, Shirika lilifanya matumizi ya nyongeza ya bajeti kinyume na utaratibu kwa kufanya matumizi hayo kabla ya kuidhinishwa kwa Bajeti hiyo ya ziada. Kwa maana hiyo, Shirika lilifanya maumizi ya fedha hizo, kabla hazijaidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika hilo.

Mapendekezo ya Kamati

Kuna haja kufanyika uchunguzi maaluma na wa kina juu ya matumizi ya fedha za karafuu hasa ikizingatiwa kuwa, kwa muda mrefu sasa, matumizi ya fedha hizo hayajawa wazi kwa wananchi.

3.11.1 Kukosekana kwa mapato ya jengo la Kitega Uchumi, Tsh. 172,900,816.99

Ukaguzi umebaini jumla ya mita za mraba 912.73 katika jengo la Uwekezaji la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar hazina wapangaji kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kutokodishwa kwa eneo hilo kumepelekea Shirika kukosa Tsh. 172,900,816.99 ambazo zingeweza kupatikana kutokana na ukodishwaji huo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Shirika

Kwa lengo la kupunguza utegemezi wa mapato yanayotokana na karafuu, Shirika limewekeza katika jengo la Kitega Uchumi liliopo Gulioni Mjini Zanzibar. Shirika limeingia Mkataba na Kampuni ya Night Frank Tanzania Ltd, ambayo ni Wakala wa Shirika katika kulisimamia na kulishughulikia jengo katika shughuli zake zote zinazohusiana na usafi, matengenezo madogo madogo, kulitangaza, kutafuta wapangaji wapya, kukodisha, kudai malipo, kukusanya malipo ya huduma na kadhalika.

Hadi kufikia Juni 2018, Jengo la Shirika lina jumla ya mita za mraba sqm 3387.6 zinazoweza kukodishwa, kati ya hizo kwa mwaka 2017/2018 jumla ya sqm 2910.88 zilizodishwa kwa wapangaji, hii ni sawa na 14% ya eneo linalokodishwa. Eneo ambalo kama lingelikodishwa lingeweza kuliingizia Shirika jumla ya Tsh. 92,102,304.00. Aidha, kutokana na uzoefu wa ukodishaji wa majengo pamoja na mahitaji ya wateja hupelekea majengo yaliyo mengi kuwa na nafasi iliyo tupu badala ya kukodiwa jengo zima. Aidha, kwa mujibu wa viwango, ukodishaji wa majengo ya aina hiyo, jengo ambalo limepangishwa kwa zaidi ya 80%(occupancy rate) linahesabiwa kwamba limekidhi mahitaji ya ukodishwaji.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipohoji kwa nini jengo hilo lisikodishwe kwa 100%, lilielezwa kuwa, kwa asili ya 'real estate', ni ngumu kufikia kiwango hicho mara moja. Hivyo, Shirika kufikia 95% ya ukodishwaji wa jengo hilo, imefanya juhudi kubwa na huku likiendelea kutafuta wapangaji wengine.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika liendelee na juhudi za kutafuta taasisi ama wafanyabiashara wa kuekeza katika eneo hilo, ili mapato zaidi yaweze kupatikana.

3.11.2 Matumizi yaliyofanyika kabla ya utayarishwaji wa hati za malipo Tsh. 23,794,520,133

Ukaguzi umebaini kwamba, jumla ya Tsh. 23,794,520,133 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Shirika. Dosari iliyobainika na Ukaguzi ni kufanyika kwa malipo hayo bila ya utayarishwaji wa hati za malipo. Kufanya hivo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nambari 12 ya mwaka 2016. Malipo hayo ni kama

ifuatavyo:

Nam	Tarehe ya utayarishaji wa hati za malipo	Hati namba	Tarehe iliyofanyika matumizi	Thamani iliyotumika	Maelezo
1.	29.12.2017	PV0717180098/12	27.12.2017	5,140,500,000	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
2.	29.12.2017	PV0717180096/12	4.12.2017	14,485,121	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
3.	13.12.2017	PV0717180090/12	11.12.2017	6,691,900	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
4.	28.02.2018	PV0717180122/2	20.02.2018	178,800,000	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
5.	20.02.2018	PV0717180121/2	15.02.2018	3,468,900,000	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika

6.	12.02.2018	PV0717180119/2	07.02.2018	8,802,684	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
7.	26.01.2018	PV0717180122/1	24.01.2018	6,688,630	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
8.	24.01.2018	PV0717180108/1	15.01.2018	446,600,000	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
9.	24.01.2018	PV0717180107/1	08.01.2018	2,453,000,000	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
10.	08.01.2018	PV0717180104/1	04.01.2018	3,345,000,000	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika
11.	03.01.2018	PV0717180102/1	04.10.2017	450,001,708	Kuwa ni malipo ya Uhamisho wa matumizi ya Shirika

Jumla	**23,794,520,133**

Majibu ya Shirika

Shirika kwa mwaka 2017/2018 lilifanya Uhaulishaji wa fedha, Jumla ya Tsh. 23,794,520,133.00, Uhaulishaji huo kwa kiwango kikubwa umehusisha fedha kutoka katika Akaunti ya fedha za kigeni (USD) ya Shirika iliyopo PBZ LTD Unguja ambayo kikawaida huhifadhi fedha zote zinazoingia kutoka kwa wateja wa karafuu na kuziingiza katika Akaunti ya Shirika ya fedha za Kitanzania iliyopo PBZ LTD ambayo hutumika kwa ajili ya matumizi ya Shirika ikiwemo unununzi wa Karafuu katika vituo vya Unguja na Pemba.

Aidha, katika uhaulishaji huo wa fedha kumejitokeza ucheleweshaji wa ufanyaji wa hati za malipo uliosababishwa na mfumo wa kutengeneza hati hizo uitwao "Smart Voucher System" ambao Shirika limekuwa likiutumia kwa wakati huo kwa baadhi ya wakati kukosa huduma ya "internet" wakati wa kutayarisha hati za malipo, hali inayopelekea Watendaji kushindwa kutayarisha hati za malipo kwa wakati. Aidha, kutokana na umuhimu na uharaka wa utumaji wa fedha za karafuu kwa ajili ya kuondosha kadhia kwa Wakulima wanaofika Vituoni mapema kwa kuuza karafuu hizo.

Uhaulishaji hufanyika kwa kuidhinishwa na wahusika wa kuidhinisha malipo ya Shirika kwa mujibu wa utaratibu wa Shirika. Vile vile, Shirika hutengeneza hati za malipo kwa uharaka pindi tu huduma ya mfumo wa uhasibu unaporejea. Kwa sasa Shirika limehabadilisha mafumo wa uhasibu ili kuondokana na kadhia hiyo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imebaini kuhusiana na hoja hii kuwa, hakukuwa na wizi ama upotevu wowote wa fedha za Shirika, lakini zimehaulishwa kutoka Akaunti moja kwenda nyengine, ambapo kuna ulazima wa Shirika kuaiandikia barua Benki ya Tanzania (B.O.T) na ni lazima kuwepo huduma ya intanenti ya kutosha, na Kamati imekubaliana na hoja ya kukosekana kwa huduma ya uhakika ya 'internet' na imeridhishwa kuelezwa kuwa, hivi sasa Shirika limehama katika mfumo huo wenye usumbufu.

Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na Shirika kuhamia katika mfumo mpya, ni vyema likahakikisha kuwa, hakuna dosari zitakazotokea na kuleta athari katika mfumo huo.

3.12: MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) ilikusanya Tsh. 11,039,978,608 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ilikusanya kiwango hicho cha fedha kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya ndani ikiwa ni pamoja na Garama za Utuaji Ndege (Landing Fees) wanazotoza kwa ndege zinazotua katika viwanja vyake vyote viwili, Unguja na Pemba. Aidha, Mamlaka imekusanya fedha hizo kupitia ada ya Usalama ambayo wanatoza kwa kila abiria anaeondoka kupita viwanja vya Mamlaka, Ada ya Biashara, ada ya 'Cupps' inayotozwa kwa kila abiria wa kigeni anaeondoka nchini, Ada ya Vitambulisho, Ada ya Maegesho ya Magari na vyanzo vyengine vya mapato.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipofanya mahojiano na Mamlaka kwa upande wa Ada ya Biashara, ilijiridhisha kuwa Mamlaka haikukusanya mapato kupitia chanzo hiki kwa upande wa Pemba. Aidha, kwa upande wa Ada za Maegesho ya Magari Kamati imesikitika kuona Mamlaka imepunguza makusanyo kwa mwaka 2017/2018 ukilinganisha na mwaka 2016/2017 na baada ya kuhoji kwa kina kuhusiana na sababu zilizopelekea kushuka kwa makusanyo hayo, ilijiridhisha kuwa, Mamlaka imewapa jukumu la kukusanya mapato hayo (out source) kwa Kampuni ya Nje, wakati wao Mamlaka wanapokea mgao wa 20% wa makusanyo hayo.

Kamati haikuridhika na makusanyo hayo ambayo ni madogo na hayaendani na maslahi ya Mamlaka, pamoja na kuelezwa kuwa, Mamlaka walifanya maamuzi hayo, kutokana na kujiona na majukumu ya ziada ya kulipa mishahara, umeme na gharama nyengine, walipokuwa wanakusanya wenyewe mapato hayo ya maegesho ya magari. Aidha, Kamati imepitia Mkataba huu na kujiridhisha kuwa, Kampuni walichukua faida ya 80% huku Mamlaka ikichukua 20% ambapo Kamati imejiridhisha kuwa ni Mkataba usio na tija kwa Mamlaka. Aidha, Kamati ilipopitia Mikataba mbali mbali ilibaini kuwa Mikataba hiyo haikuwa na saini ya Afisa Masuuli (Accounting Officer) ambae kimsingi ndie alietakiwa kuitia saini Mikataba hiyo.

Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na juhudi za Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuipitia Mikataba ya Mamlaka, Kamati inaishauri Mamlaka kusimamia vyema vyanzo vyake vya mapato na kuingia mikataba yenye tija.

Taarifa ya Matumizi

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) ilitumia jumla ya Tsh. 7,985,753,958 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo ilitumia Tsh. 7,545,474,145 kukiwa na ongezeko la Tsh. 440,279,814 sawa na 6% ya ongezeko.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli Mamlaka imetumia kiwango hicho cha Tsh. 7,985,753,958 kwa ongezeko la 6% ikilinganishwa na mwaka 2016/2017 kwa sababu, Mamlaka ilifanya makisio na matumizi yyenye upungufu kwa takriban miaka mitatu nyuma, hivyo, kwa mwaka 2017/2018 iliendelea kufanya makisio madogo ya matumizi lakini ikajikuta imepata ziada na hivyo, kuongeza kiwango hicho cha 6% cha matumizi yake kwa mlinganisho na mwaka 2016/2017.

Katika matumizi ya kujiletea maendeleo, Mamlaka ilikopa fedha Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na kuzitumia fedha hizo kwa mabasi ya wafanyakazi wake na baadae kukopa mashine za uchunguzi (X-Ray Machines) Islamic Banking, lakini tayari Mamlaka imesharejesha mikopo iliyokopa. Aidha, Mamlaka ilikuwa imetumia fedha zake kwa mwaka huo kwa kuanza kulipa ya madeni ya wafanyakazi wake ambapo ilipofunga hesabu zake mnamo June 2018, kulikuwa na madeni ambayo walikuja kuyamaliza kulipa mwaka uliofuata.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imeshangazwa kwa kukosekana kwa taratibu za kimanunuzi kwa Mamlaka na Kikosi cha KVZ kutokana na Mamlaka kuhitaji na kupatiwa huduma ya ulinzi kutoka KVZ bila ya kuitisha zabuni na kupata ushindani na Kampuni nyengine za ulinzi. Hata hivyo, Mamlaka imekuwa na deni la Tsh. 34,000,000 na katika wakati wa ukaguzi, deni hilo lilibakia Tsh. 12,000,000.

Kamati imegundua kuwa Mamlaka inatoa huduma zake kwa kuingia Mikataba na Taasisi mbali mbali za Serikali na Kampuni za watu binafsi, lakini kumekuwa na kasoro nyingi katika utayarishaji na utekelezaji wa mikataba hiyo. Hali hii iliilazimu Kamati kuitaka Mamlaka kuwasilisha kwake Mikataba mbali mbali ikiwa ni pamoja na ya huduma na biashara na Mamlaka ikaikabidhi mikataba hiyo, lakini kutokana na Mamlaka kushindwa kupata muda wa ziada wa kukutana tena na Kamati, Kamati imeshindwa kuihakiki kwa kina na kupata majibu sahihi juu ya maeneo dhaifu ya mikataba hiyo.

Mapendekezo ya Kamati

Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ihakikishe kuwa, Uongozi wa Mamlaka unasimamia Sheria katika kufanya matumizi ya fedha. Aidha, kuhusiana na suala la mikataba, Serikali ifuatilie kwa karibu suala la Mamlaka kuingia mikataba na taasisi mbali mbali, ili kuhakikisha kasoro zilizopo zinarekebishwa.

3.13: MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA) ilikadiriwa kukusanya Tsh. 5,112,728,012 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 3,718,893,422 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali sawa na 73% ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Katika mwaka wa 2017/2018 Mamlaka ya ZMA haikufanikiwa kukusanya mapato zaidi kufuatia agizo lililotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kutangaza rasmi kusitishwa usajili wa meli za Kimataifa. Aidha, kabla ya tangazo hilo, ZMA ilikuwa tayari ishaanza kuiendesha na kusimamia wenyewe usajili wa meli za Kimataifa, suala ambalo lilipelekea Makampuni na wamiliki wa meli kuwa na imani na kuvutiwa na kusajili meli zao katika taasisi ya ZMA.

Kwa mwaka 2017/2018 mpango wa Mamlaka kutoka vianzio mbali mbali vya mapato ilikuwa kama ifuatavyo pamoja na utekelezaji wake:-

Na.	Vyanzo vya Mapato	Makisio	Halisi	Asilimia
1.	Mapato yatokanayo na vyanzo vya Usajili wa Meli za Ndani	279,802,439	243,712,000	87
2.	Mapato yatokanayo na vyanzo vya Usajili wa Meli Kimataifa	2,371,320,000	2,274,932,373	96
3.	Mapato yatokanayo na huduma Bandarini	2,178,105,573	937,749,049	43

4.	Mapato kutoka kwa Wahisani kuimarisha sekta ya usafiri Baharini	283,500,000	262,500,000	92
Jumla Kuu		**5,112,728,012**	**3,718,893,422**	**73**

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Mamlaka katika kudhibiti mapato yake yanayotokana na usajili wa meli za ndani, Kamati imejiridhisha kuwa, kuna vyombo vingi havijasajiliwa na bado vinafanya kazi. Hali hii inapelekea kupotea kwa mapato ya Mamlaka.

Aidha, Kamati imekubaliana na Mamlaka kuwa imepungukiwa na mapato kutokana na kusitishwa kwa usajili wa meli za Kimataifa mnamo mwezi wa Januari 2018, kwani kabla ya kusitishwa huko Mamlaka ilikusanya vizuri mapato yake. Kusitishwa huko kunatokana na taarifa ya meli iliyotuhumiwa kubeba madawa ya kulevya ilipeperusha bendera ya Tanzania, lakini usajili wake ulifanyika Zanzibar. Kufuatia hali hiyo, Mhe. Rais John Pombe Magufuli aliunda Kamati ya kufuatilia suala hilo, wakati huo huo kuzuia usajili wa meli hizo ambapo hadi tunaandika taarifa hii, bado ruhusa hiyo haijatoka. ZMA imeathiriwa na kusitishwa huko, kwani usajili wa meli za nje unafanyika Zanzibar na sio Tanzania bara.

Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na kuruhusiwa kwa Mamlaka kusajili meli za Kimataifa, suala hili linahitaji kusimamiwa kwa karibu ili kuihakikishia Serikali inapata mapato yake kwa ufanisi. Aidha, Mamlaka ipiganie kuondosha kasoro zilizojitokeza awali, ili kusitokezee kufutwa kwa usajili wa meli za kigenzi, ambapo hasara zake ni kubwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya ZMA ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 4,698,217,200 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kati ya hizo Tsh. 3,665,241,200 ikiwa ni matumizi ya kazi za kawaida na 683,976,000 ni za matumizi ya maendeleo. Aidha, ilipofika tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 3,925,006,905 ziliingizwa na kutumika, sawa na 81% ya makadirio. Kati ya hizo, Tsh.

3,194,650,685 zimetumika kwa kazi za kawaida na Tsh. 578,871,867 zimetumika kwa kazi za maendeleo.

Majibu ya Mamlaka

Kwa mwaka 2017/2018 Mamlaka ya Usafiri Baharini ilipanga shughuli zifuatazo:-

Nam.	Shughuli	Makisio	Halisi	Asilimia
1.	Kuwapa motisha na uwezo wa wafanyakazi	1,178,884,240	1,158,826,636	98
2.	Kuwajengea uwezo wafanyakazi	289,330,000	208,956,962	72
3.	Kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi vya Ofisini	1,166,032,960	999,094,037	86
4.	Kuhudumia Bodi ya Wakurugenzi	200,055,000	190,630,000	95
5.	Kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kutunza kumbu kumbu	102,660,000	98,342,168	96
6.	Kuratibu na kushiriki mikutano ya Kitaifa na Kimataifa	501,388,000	632,276,200	126
7.	Kuandaa Mpango Kazi na Bajeti ya Mamlaka	850,000	0	0
8.	Kuandaa Sheria, Kanuni pamoja na miongozo ya kazi	160,840,000	87,013,813	54
9.	Kuimarisha na kutoa huduma bora za usajili wa meli	20,154,000	29,487,000	145

10.	Kuhakikisha vifaa vinavyotumika katika ukaguzi, vinapatikana	45,047,000	10,265,700	23
11.	Kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya ZMA Pemba pamoja na uanzishaji wa Chuo cha Mabaharia, vinapatikana	171,576,000	0	0
12.	Kuimarisha mfumo wa kumbu kumbu za meli pamoja na usalama wa usafiri baharini, vinapatikana	512,400,000	449,064,388	89
Jumla Kuu		**4,698,217,200**	**3,863,956,904**	**82**

Katika matumizi ya kazi za maendeleo, Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) imetumia fedha zilizopatikana kwa kufanikisha miradi mbali mbali ambayo imeleta mafanikio mbali mbali kwa Mamlaka ambayo ni kupata taarifa kamili za meli na wamiliki, kupata taarifa za ukaguzi wa meli, kupata takwimu za muda wa mwisho wa matumizi ya vyeti, kupunguza ufujaji wa vyeti vya meli, kutoa vitabu vya ubaharia vyenye viwango kama ilivyoainishwa na toleo la IMO la mwaka 2010 kuhusu vitabu vya ubaharia, kudhibiti mapato yatokanayo na meli na mabaharia, kupata taarifa mbali mbali zinazohusu mabaharia na meli na Mamlaka kuwa ni taasisi ya kwanza Afrika Mashariki kutumia mfumo wa kielectroniki katika usajili meli na mabaharia.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imethibitishiwa kuwa, kabla ya kufungiwa kusajili meli za kigeni, Mamlaka iliandikiwa barua Serikalini ya kutakiwa kuchangia 25% ya mapato yake (sawa na Tsh. 55,000,000/-) kwa kila mwezi, ikiwa ni gawio la faida, lakini imeshindwa kutekeleza maagizo hayo baada ya kuchangia kwa mwezi mmoja tu.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka iendelee na juhudi za kuongeza makusanyo yake na isimamie ipasavyo

matumizi yake kwa namna Sheria za Usimamia fedha za Umma zinavyoelekeza.

3.14: MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI MAFUTA NA GESI ASILI ZANZIBAR (ZPRA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (ZPRA) ilikusanya Tsh. 956,480,797 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kati ya hizo, Tsh. 730,000,000 zikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini, Tsh. 23,708,800 zikiwa ni kutoka katika vyanzo mbali mbali na Tsh. 202,771,997 zikiwa ni msaada.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ilikadiriwa kupokea Tsh. 840,000,000 ikiwa ni ruzuku ya Serikali katika kipindi cha mwaka 2017/2018. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, Mamlaka ilipokea Tsh. 730,000,000, sawa na 87% ya makadirio. Aidha, Mamlaka imepata fedha za misaada ambazo ni Tsh. 202,771,997 na fedha za mapato ya vyanzo vya ndani ni Tsh. 23,708,800.

Aidha, fedha hizo za misaada zilihusisha gari yenye thamani ya Tsh. 90,000,000, furniture za Ofisi zenye thamani ya Tsh. 81,000,000 na vifaa vya kutendea kazi vya Tsh. 31,000,000. Misaada hiyo imetoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), kwa maana Mamlaka imepokea fedha hizo kutoka Serikalini kupitia ZURA.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imehoji kama Mamlaka ilipokea fedha za msaada kutoka ZURA kwa barua yoyote na kujiridhisha kuwa hakukuwa na maandishi yoyote ya mapokezi ya msaada huo. Msaada ambao haukuwa fedha kamili (Cash) bali ulikuwa ni gari, furnitures na vifaa vilipokelewa na Mamlaka ya ZPRA kutoka Mamlaka ya ZURA kwa kutekeleza maelekezo ya Baraza la Mapinduzi.

Kuhusiana na mapato ya Mamlaka, Kamati imegundua kuwa Mamlaka imepata mapato ya Tsh. 23,708,800 yanayotokana na vyanzo vya ‘permits’ za Kampuni zinazofanya utafiti wa mafuta, Tsh. 22,758,400, madai ya bima Tsh. 650,400 na kuuza ‘Documents’ za ndani kupitia Zabuni Tsh. 300,000. Hata hivyo, pamoja na kuwa vyanzo hivyo vya mapato vipo Kisheria, Uongozi wa Mamlaka umefanya makisio katika kiwango kidogo cha makusanyo kwa kutumia mazoea (Best Practice) kwa mwaka 2017/2018.

Vile vile, Kamati imebaini kuwa, Bajeti ya kwanza ya Mamlaka waliyopendekeza Serikalini ilikuwa Bilioni 2 ikiwa ni pamoja na mishahara, lakini walielekezwa na Serikali kushusha kiwango hicho. Aidha, walipanga tena hadi Bilioni 1, na baadae walipata 'Celinig' ya kupokea makadirio ya ruzuku ya Tsh. 840,000,000 kwa mwaka 2017/2018.

Mapendekezo ya Kamati

Ni vyema Taasisi moja ya Serikali inapokabidhi msaada wowote kwa Taasisi nyengine kukawa na makabidhiano ya maandishi ili kuthibitisha usahihi zaidi wa kupokelewa kwa msaada huo. Aidha, Serikali iisimamie Mamlaka kufanya makisio sahihi ya makusanyo ya mapato kwa kuzingatia vyanzo halisi vya Mamlaka.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya ZPRA ilikadiriwa kutumia Tsh. 840,000,000 kwa mwaka 2017/2018, kati ya hizo, Tsh. 510,552,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 329,448,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 763,105,037 ziliingizwa na kutumika, sawa na 91% ya makadirio. Kati ya hizo, Tsh. 494,624,367 zikiwa ni matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 268,480,670 zikiwa ni matumizi ya kazi za maendeleo.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakiri kupokea Tsh.763,105,037 za matumizi zilizoingizwa na kutumika, ikiwa ni sawa na 91% ya makadirio. Mamlaka imezitumia fedha hizo kwa kazi za kawaida na kuzitumia kwa kazi za maendeleo, kama ilivyoelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imebaini na kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia imefanya matumizi ya fedha ilizotengewa kwa mwaka 2017/2018 bila ya kuwa na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Hata hivyo, Kamati imepokea taarifa kuwa hivi sasa tayari Mamlaka imeshaanzisha Kitengo hicho.

Aidha, Kamati hairidhishwi na tabia ya Wizara za Serikali kuzitumia Mamlaka zilizo chini yake kwa kuziamuru kutoa fedha kwa matumizi mbali mbali ya Wizara hizo, wakati Wizara zenyewe zimetengewa bajeti ya matumizi hayo. Kwa mfano, Mamlaka ya ZPRA wametakiwa na Wizara inayosimamia Ardhi kwa mwaka 2017/2018 kuchangia ujenzi wa matengenezo ya jengo la Wizara hiyo na pia kutakiwa kuchangia matumizi mbali mbali, ikiwa ni pamoja na 'stationaries'.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka kuzitumia fedha za Umma zinazokasimiwa kwake na Serikali, kwa kufuata taratibu za Kisheria.

Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2017/2018 kwa ajili ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2016, inazitaka Taasisi zote za Serikali zitayarishe na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka, zinazojumuisha mapato na matumizi ya Taasisi husika.

Aidha, kifungu cha 119(2) cha Sheria hiyo, kinawataka wasimamizi wa fedha katika Taasisi za Serikali kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu zao za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kukamilika kwa kipindi cha mwaka. Aidha, Mamlaya ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (ZPRA), iliwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa kuchelewa mnamo 30/10/2018.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakiri kutokea kwa ucheleweshaji wa kuwasilisha Taarifa hizo za mwaka wa fedha 2017/2018 na ni kinyume na Sheria ya Fedha za Umma (The Public Finance Management Act, No. 12 ya mwaka 2016) kifungu cha 119(1) kinachosisitiza uwasilishaji wa Taarifa za Fedha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali si zaidi ya miezi mitatu toka kumalizika kwa Mwaka wa Fedha. Aidha, Mamlaka inaomba radhi kwa ucheleweshaji huu ambapo mwisho ilikuwa tarehe 30/09/2018 na Hesabu ziliwasilishwa tarehe 30/10/2018.

Sababu kubwa ya ucheleweshaji huu ni upya wa Mamlaka ambayo imeundwa rasmi tarehe 18/03/2017 baada ya kuteuliwa Mkurugenzi Mwendeshaji na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hivyo, mwaka wa fedha 2017/2018 ni mwaka wa kwanza kwa Mamlaka kufunga hesabu zake.

Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka haikuwa na Bodi ya Wakurugenzi, hivyo ililazimu kuwasiliana na Waziri ili kuweza kuidhinishwa kwa Hesabu na kuwasilishwa rasmi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mamlaka ilizidi kujiimarisha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kufanikiwa kuziwasilisha hesabu kwa wakati na kusaidia ukaguzi kufanyika kwa wakati uliopangwa.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imejiridhisha kuwa Mamlaka ilichelewa kuwasilisha hesabu zake kwa wakati na kukubaliana na sababu zilizoelezwa na Mamlaka, kwa ahadi kuwa kasoro hizo zitarekebishwa kwa miaka inayofuata.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaitaka Mamlaka kuhakikisha kuwa kasoro hiyo ya kuchelewa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka hairejei tena.

3.15: SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

Taarifa ya Mapato

Shirika la Nyumba la Zanzibar kwa mwaka 2017/2018 lilikusanya jumla ya Tsh. 2,007,144,882 kutoka katika vyanzo mbali mbali.

Majibu ya Shirika

Ni kweli Shirika la Nyumba la Zanzibar lilikusanya Tsh. 2,007,144,882 wakati mapato yaliyokadiriwa kukusanywa yalikuwa ni Tsh. 2,578,000,000, kwa kupitia vyanzo vyake mbali mbali kama ifuatavyo:

Vyanzo vya Mapato 2017/2018	**Makisio kwa mwaka 2017/2018**	**Fedha halisi zilizopatikana 2017/2018**
Kodi ya Majengo	2,050,000,000	1,910,097,130
Mikataba na Dhamana	278,000,000	82,570,252
Tozo na Adhabu	150,000,000	14,477,500
Mauzo ya Nyumba	100,000,000	-
Jumla	**2,578,000,000**	**2,007,144,882**

Shirika limejitahidi sana kukusanya mapato, ingawaje haikufikia kiwango kilichokadiriwa kwa asilimia 100, lakini juhudi ilizozichukua ni kubwa na zinastahiki pongezi. Juhudi hizo ni baada ya kupokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Shirika lilichukua jitihada za kuhakikisha ongezeko la ukusanyaji wa mapato ikiwemo

kufuata taratibu za kumtumia Dalali wa Mahakama ambapo Shirika liliandaa Mkataba na kuuwasilisha kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri wake.

Shirika pia lilichukua juhudi za kuwakumbusha wapangaji kulipa madeni yao ikiwemo kuwaandikia barua za ukumbusho mara kwa mara na kutowa matangazo kwenye vyombo vya habari, utaratibu uliofanikiwa kiasi Fulani kuongeza mapato ya Shirika.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na juhudi za Shirika za kutaka kumtumia Dalali wa Mahakama, Kamati imegundua kuwa juhudi hizi zilikwamishwa na Serikali kwa kukosesha utashi wa kisiasa, hali iliyodhihirisha kuwa Serikali haikuwa tayari kwa Shirika hili kutumia nguvu zake za Kisheria katika kudai kodi za majengo yake inayoyakodisha kwa wananchi na badala yake ililielekeza kutumia njia za kisiasa na kuwaridhia wakodishwaji. Kamati inasema hivi baada ya kujiridhisha juu ya usahihi wa juhudi za Shirika kuandaa Waraka na kuupeleka Baraza la Mapinduzi, wamefanya juhudi za kuwasiliana na Wizara inayolisimamia Shirika hili juu ya haja ya kurekebishwa kiwango cha kodi za majengo yake, lakini hakukuwa na majibu waliyoyataka.

Kamati imejiridhisha kuwa Shirika linawafahamu wananchi walionunua nyumba zao kwa njia ya vilemba na kuwakodisha ama kuwauzia wananchi wengine kwa bei ya juu zaidi, lakini juhudi zo za kutaka kuwachukulia hatua watu hao zimekwamishwa kwa kutokubaliwa Waraka wao waliouwasilisha Serikalini.

Kamati imeshangaa kwa Shirika hili kukodisha nyumba zake hasa ziliopo Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kiwango kidogo sana cha kodi na kwa kiwango hiki Shirika linashindwa kukusanya mapato kwa kiwango kinachotakiwa.

Mapendekezo ya Kamati

Serikali iliache Shirika lisimamie Sheria yake na Sheria nyengine zinazohusika, katika kusimamia majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufuatilia madeni yake ya nyumba inazozikodishwa kwa wananchi. Aidha, kiwango cha kodi za nyumba zinazokodishwa na Shirika zimeshapitwa na wakati, kuna haja ya kuzifanyia marekebisho ili ziendane na thamani halisi ya fedha na wakati tulionao sasa.

Taarifa ya Matumizi

Kwa mwaka 2017/2018 Shirika la Nyumba la Zanzibar lilitumia Tsh. 1,632,457,161 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo lilitumia Tsh. 1,140,546,112 kukiwa na ongezeko la Tsh. 491,911,049 sawa na 43% ya ongezeko.

Majibu ya Shirika

Shirika lilipanga kutumia Tsh 2,577,600,000 kwa mwaka 2017/2018, lakini matumizi halisi hadi kufikia Juni 2018 yalikuwa ni Tsh. 1,632,457,161. Ongezeko la matumizi la Tsh. 491,911,049 kwa mwaka 2017/2018 ukilinganisha na mwaka 2016/2017 sawa na 43% ya ongezeko yalitokana na Mpango Kazi wa Shirika uliojipangia kwa mwaka 2017/2018 kwa kazi za matengenezo ya majengo mbali mbali. Matumizi halisi ya Shirika kwa mwaka 2017/2018 yalikuwa katika mambo yafuatayo:

- Matengenezo makubwa ya nyumba 8 za Maendeleo, Madungu Chake Chake Pemba.
- Matengenezo ya jengo linalotumiwa na Wakala wa Serikali wa Uchapaji, Chake Chake Pemba.
- Ujenzi wa shimo kubwa la maji machafu, Block Na. 4 Michenzani Unguja, na
- Kuezeka nyumba za Kikwajuni, Block L na Block E.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilihitaji kupatiwa kiwango cha fedha zilizotumika katika kutengeneza nyumba 8 za Maendeleo, Madungu Chake Chake Pemba na kuelezwa kuwa zilitumika Tsh. 104,000,000 ambazo zinasemwa kutumika kwa matengenezo ya makaro, mfumo wa maji na mengineyo. Kamati ilielezwa kuwa Shirika lilitumia Qoutation tatu, wakati fedha zilizotumika zilitosha kuitishwa kwa zabuni na kusimamiwa matumizi yake ipasavyo.

Aidha, Kamati ilipohoji matumizi ya ujenzi wa shimo kubwa la maji machafu, Block Na. 4 hapo Michenzani, iligundua ‘quotation’ tatu zinazofanana sana katika maandishi yake tofauti pekee ni kiwango cha gharama zilizoainishwa katika ‘quotation’ hizo. Hii ina maana mjenzi mmoja ametoa ‘quotations’ tatu kuhalalisha matumizi ya fedha hizo.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati haikuridhishwa na matumizi ya Shirika kwa mwaka 2017/2018 na inaishauri Uongozi wa Shirika, kusimamia kwa karibu na kufuatilia matumizi ya Shirika ili dosari zilizojitokeza mwaka 2017/2018 zisijirejee.

3.16: MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ilikadiriwa kukusanya Tsh. 17,282,500,000 katika kipindi cha mwaka 2017/2018 kutoka vyanzo mbali mbali. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni, jumla ya Tsh. 16,362,952,000

zimekusanywa kutoka vyanzo mbali mbali, sawa na 95% ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ilikusanya mapato yake kupitia vyanzo vyake mbali mbali kama ifuatavyo:-

Na.	Kasma	Aina ya Mapato	Kiwango kilichopangwa	Kiwango kilichokusanywa
1.	1151004	Tozo la Udhibiti	13,200,000,000	14,981,574,000
2.	1145005	Malipo ya Leseni	200,000,000	169,547,000
3.	1145004	Mapato Mengineyo	50,000,000	36,009,000
4.	2401003	Faida ya Benki	1,822,500,000	1,167,376,000
5.	1430000	Adhabu	10,000,000	7,695,000
6.	2631000	Ruzuku	2,000,000,000	0
7.		Exchange Gain/ Loss		750,000
Jumla			**17,282,500,000**	**16,362,951,000**

Kiwango kikubwa cha mapato kinatokana na malipo ya tozo ya mafuta kwa vile Mamlaka ndio iliyoanza nayo na hakukuwa na mchango wowote uliopokelewa kutoka Sekta ya Maji na Umeme. Kiwango cha mafuta kilichokadiriwa kupokelewa kilipungua katika mchakato wa ununuzi wa mafuta kwa njia ya pamoja (Bulk Procurement System

– BPS) ambapo baadhi ya kampuni za uagizaji wa mafuta zilitoa kiwango kidogo kwa muagizaji wa pamoja, utaratibu ambao ulikuwa wa kipindi cha miezi miwili mitatu, Septemba 2017. Hali hiyo ilipunguza makusanyo ya mapato.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imebaini kuwa, Mamlaka ingelikuwa na makusanyo makubwa zaidi kama ingelikuwa na Kanuni za Tozo la Udhibiti wa huduma ya maji na umeme angalau tokea mwaka 2017/2018, kwani makusanyo hayo yaliongozeka baada ya Kanuni hizo kutungwa na kuanza kazi mwaka 2020.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka iendelee kuimarisha makusanyo yake kwa kudhibiti vyanzo vyake vikuu vya mapato ili kufikia lengo la makusanyo linalopangwa mwaka hadi mwaka.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar ilikadiriwa kutumia Tsh. 25,597,200,000 kwa mwaka 2017/2018. Kati ya hizo, Tsh. 14,952,200,000 ikiwa ni matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 10,645,000,000 kwa kazi za maendeleo. Aidha, ilipofika tarehe 30 Juni 2018 Tsh. 12,634,289,000 ziliingizwa na kutumika, sawa na 50% ya makadirio. Kati ya fedha hizo, Tsh. 8,962,657,000 zimetumika kwa kazi za kawaida na Tsh. 3,671,632,000 zimetumika kwa kazi za maendeleo.

Majibu ya Mamlaka

Katika mwaka 2017/2018 Mamlaka ilikuwa katika mchakato wa kuanzisha ujenzi wa jengo la ofisi yake ambayo ilichelewa kuanza na ilikuwa imeshatenga fedha kwa tahadhari ya kujiandaa na malipo ya ujenzi endapo kazi ingeanza mapema. Vile vile kwa kuwa ofisi ya Mamlaka ilikuwa bado ni mpya, ilihitaji vitendea kazi kwa wafanyakazi wake ambao idadi yao ilikuwa inaongezeka taratibu.

Katika mwaka 2017/2018 Mamlaka ilipanga kuajiri wafanyakazi 14 katika nafasi za Afisa Mipango, Afisa Takwimu, Wakaguzi wa Mafuta, Madereva, Wakutubi na Wahudumu wa Masjala. Ruhusa ya kibali cha ajira kilichotolewa baadae kiliridhia ajira za watumishi saba kutoka kada ya Afisa Utumishi (1), Usalama wa Mazingira (1), Afisa Manunuzi na Ugavi (1), Afisa Mkaguzi Mafuta (2), Afisa Utatuzi wa Migogoro (1) na Afisa Mchambuzi Fedha (1). Hivyo, baadhi ya malipo ya kawaida kwenye bajeti ya ZURA yalitakiwa yafanyike kwa kulipia mishahara na mafao ya wafanyakazi hao 14.

Aidha, kutokana na ujenzi wa jengo la Ofisi ya ZURA, gharama za matumizi hazikuwa

kubwa kwani malipo makuu yalifanyika katika utangulizi (Advance) kwa mjenzi. Hata hivyo, Mamlaka ilipokea agizo kutoka Serikalini la kusaidia uanzishwaji wa Taasisi mpya ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na hivyo kuchangia gharama za ukarabati wa jengo la Ofisi hapo Forodhani, Ununuzi wa vitendea kazi na Ununuzi wa gari.

Aidha, kwa upande wa matumizi ya fedha za maendeleo, Mamlaka ilitumia fedha ilizoingiziwa kwa matumizi mbali mbali ikiwa ni pamoja na matumizi ya Tsh. 3,142,222,581 kwa matayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi na kwa matumizi mengineyo zimetumika Tsh. 529,409,419. Vile vile, Mamlaka ilitumia Tsh. 374,922,000.56 kwa matengenezo ya jengo la ofisi, ununuzi wa gari, ununuzi wa samani na ulipaji kodi.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na matumizi yaliyotumiwa na Mamlaka, Kamati imehoji pamoja na mambo mengine, matumizi ya fedha Tsh. 500,000,000 zilizotoka ZURA kupewa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na hadi tunaandika taarifa hii, Kamati haikupata majibu ya kuridhisha kuhusiana na fedha hizo. Kamati ilielezwa kuwa, ZAWA waliomba kupewa fedha na ZURA Tsh. Bilioni Moja na ZURA walitoa kwanza Tsh. 500,000,000 kwa sharti la kupewa marejesho kabla ya kutoa fedha zilizobakia, lakini kwa kushindwa kwao kufanya marejesho hayo, hatimae fedha hizo hazikutoka.

Kamati imejiridhisha kuwa, Mamlaka imefanya matumizi mbali mbali kwa ujenzi wa Ofisi yake mpya pamoja na kuisaidia Mamlaka ya ZPRA na matumizi mengine kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa na Bodi ya Mamlaka.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka iendelee kuimarisha juhudi za kukusanya mapato na kufanya matumizi kwa kuzingatia Sheria, ili matunda ya matumizi hayo yaweze kupatikana.

Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2017/2018 kwa ajili ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2016, inazitaka Taasisi zote za Serikali zitayarishe na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka, zinazojumuisha mapato na matumizi ya Taasisi husika. Aidha, kifungu cha 119(2) cha Sheria hiyo, kinawataka wasimamizi wa fedha katika Taasisi za Serikali kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu zao za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kukamilika kwa kipindi cha mwaka. Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), iliwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka tarehe 28/06/2019, zaidi ya miezi tisa baadae.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), iliwasilisha ripoti za hesabu zake za mwaka 2017/2018 tarehe 28/06/2019 ikiwa ni mwaka wa fedha wa 2018/2019 badala ya mwaka 2017/2018. Kuchelewa huko kulitokana na kuwa, mtendaji wa Mamlaka aliyetakiwa kufunga hesabu hizo kwa wakati, hakuwa na uwezo wa kukamilisha vipengele vyote vinavyotakiwa katika kukamilisha ripoti ya ufungaji wa mahesabu.

Hali hii ilipelekea kutafuta msaada wa kiutaalamu kutoka kwa taasisi nyengine, jambo ambalo lilichukuwa muda na hivyo kushindikana kuwasilisha mahesabu hayo kwa ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kabla ya tarehe 30 Septemba 2018. Hata hivyo, kwa vile jukumu la kisheria kwa kila taasisi ni kuwasilisha ripoti hizo ili zikaguliwe na kupatiwa maoni ya Serikali juu ya utendaji na ufanisi wa taasisi husika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) iliwasilisha ripoti ya mwaka 2017/2018 katika tarehe ya 28/6/2019 na inakiri kuwa tayari ilichelewa.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imepokea maelezo ya Mamlaka ya kasoro zilizojitokeza kwa mwaka 2017/2018 na kujiridhisha kuwa hivi sasa kasoro hizo zimerekebishwa.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka ihakikishe inawasilisha hesabu zake za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati, kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

5.7.2: TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)

Taarifa ya Mapato

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ilikadiriwa kukusanya Tsh. 3,110,384,198 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, ZBS ilikusanya Tsh. 2,181,402,699.30 sawa na 70% ya makadirio.

Majibu ya Taasisi

Ni kweli Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) haikuweza kufikia malengo ya makusanyo yake kwa mwaka 2017/2018 kutokana na sababu zifuatazo:-

- Muitiko mdogo wa wananchi katika ununuaji wa viwango vilivyoandaliwa na ZBS.
- Wazalishaji na Wajasiriamali wengi walishindwa kumudu gharama za kuthibitisha ubora wa bidhaa, hali iliyopelekea maombi ya kupatiwa alama ya ubora

kutokamilika.

- Udhibiti wa mapato kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi, ulitegemea zaidi na mashirikiano na Taasisi nyengine za Serikali ambazo huhusika moja kwa moja katika utoaji wa mizigo bandarini kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Bndari Zanzibar (ZPC), Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), hii ilitokana na changamoto zifuatazo:-

    i. Kutokuwepo na muongozo wa pamoja wa utoaji wa mizigo bandarini (Cargo Clearance Guidelines).

    ii. Kutokuwepo na mfumo wa uhakiki wa malipo kimtandao katika kipindi hicho (Online banking) ambapo kwa kiasi kikubwa unasaidia kuhakiki "s=Slip" za malipo yaliyofanyika benki na kiwango cha fedha kilichoingia.

    iii. ZBS kutotumia mfumo wa TANCIS ambao unatumika na TRA katika utoaji wa mizigo hali ambayo ingesaidia sana udhibiti wa malipo na ukaguzi ubora wa bidhaa.

- Idadi ya bidhaa inayopaswa kukaguliwa kwa mizigo na gari zilizoingia katika kipindi hicho kuwa ndogo kutokana na uwezo husika wa Bandari ya Zanzibar.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imejiridhisha kuwa, Taasisi hii haikufikia lengo la makusanyo kutokana na sababu zilizoelezwa hapo awali, lakini pia kwa upya wa kuanzishwa kwake na kukosa usimamizi mzuri wa kusimamia vyanzo vyake vya mapato hayo, kwa mwaka 2017/2018.

Mapendekezo ya Kamati

Taarifa ya Matumizi

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa mwaka 2017/2018 ilikadiriwa kutumia Tsh. 5,695,251,648 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, ZBS ilifanikiwa kupokea na kutumia Tsh. 2,395,811,374.96 sawa na 42.07% ya makadirio.

Majibu ya Taasisi

Taasisi ya Viwango (ZBS) walitumia fedha hizo Tsh. 2,395,811,374.96 sawa na 42% ya makadirio kwa matumizi mbali mbali, ikiwa ni pamoja na kutumia Tsh. 96,800,000 kwa matumizi ya 'Minor Civil Works' kwa matengenezo madogo madogo ya majengo mbali mbali yaliopo Mkoani, Wete na Chake Chake Pemba na Unguja kujenga Kibanda cha Mlinzi na Choo katika Ofisi zao ziliopo Amani Viwanda Vidogo Vidogo.

Vile vile, Mamlaka ilitumia fedha ilizokadiriwa kwa mwaka 2017/2018 ujenzi wa Ofisi za

Taasisi ambapo walitarajia kujenda Block A na B, lakini hatimae ujenzi ulianza na Block B. aidha, matumizi hayo ni pamoja na ununuzi wa Vyombo vya Moto vya Maringi mawili na Magari.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imeshtushwa na kitendo cha Taasisi ya Viwango (ZBS) kutoa Tsh. 100,000,000 kuipa iliyokuwa Wizara ya Biashara kwa wakati huo kwa kuchangia Maonesho ya Biashara, wakati bajeti ya matumizi hayo ilitengwa Wizarani. Fedha hizo zimetolewa kufuatia maombi ya barua ya Wizara kwa Taasisi hiyo ambayo haikuonesha kima halisi walichoomba. Barua hiyo ya tarehe 12/12/2017 yenye kumbu kumbu namba WBVM/B/TSHA/9 VOL.2/5 ilikaguliwa na Kamati na Kamati kushangazwa kuwa hakuna kima kilichotajwa lakini ZBS walitoa Dokezo la malipo ya Tsh. 100,000,000 lenye namba 22/2018 la tarehe 10/1/2018 huku Hati ya Malipo (Payment Voucher) ikiidhinisha malipo hayo, hali inayoithibitishia Kamati kuwepo kwa matumizi mabaya katika Tasisi hii.

Aidha, Kamati baada ya kuangalia uhalisia wa matumizi ya Taasisi hii kupitia 'Finantial Statement' yake ilijiridhisha kuwa Taasisi hii haina nidhamu ya matumizi, kwanza kwa kukisia (Budget) kiwango cha fedha ambacho sicho walichokitumia, kwani wametumia fedha nyingi zaidi kuliko walivyojipangia, na matumizi mengine ya fedha yalifanyika bila ya kilichotumiwa kufanyiwa bajeti yake kabla, kwa maana imetumia bila ya kuwa na bajeti ya matumizi.

Kamati imegundua kuwa, Taasisi hii kwa mwaka 2017/2018 haikuwa na Bodi ya Zabuni, hali iliyowalazimu kuitumia Bodi iliyo chini ya Wizara husika. Hata hivyo, hali hii ilipelekea Taasisi kutumia fedha nyingi kununua mahitaji mbali mbali, kinyume na kiwango na vigezo vilivyohitajika na Taasisi. Kamati ilithibitishiwa na ZBS kuwa, mwaka 2017/2018 waliletewa gari zilizonunuliwa na Wizara husika ambazo sio zenye viwango na vigezo walivyovihitaji, hali iliyowalazimu kuzirejesha. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa hali hii ilirekebishwa mwaka 2019/2020.

Mapendekezo ya Kamati

Serikali isimamie kwa karibu Taasisi ya Viwango Zanzibar ili iweze kuchukua hatua zinazostahiki kwa wakati muafaka. Mapendekezo haya yanatokana na ukweli kuwa, Kamati haikuridhika utendaji mzima wa Taasisi hii.

Kwa mujibu wa kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2016, inazitaka Taasisi zote za Serikali zitayarishe na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka, ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 imebainika kwamba uwasilishaji wa taarifa za hesabu za Serikali umeimarika ambapo hesabu hizo zimewasilishwa kwa wakati. Hata hivyo, Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imechelewa kwa kuwasilisha tarehe 12/11/2018.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli Taasisi imechelewa kuwasilisha taarifa hizo kwa wakati kutokana na kukwepa gharama za kuitisha kikao cha Bodi kwa agenda moja tu ya upitishaji wa hesabu hizo kwa kipindi hicho. Kikao cha Bodi cha kawaida cha 'Quarter' kilikuwa bado na hivyo kuitishwa kwake kwa agenda moja tu ni tatizo. Aidha, Taasisi ilichelewa kufunga na kuwasilisha hesabu hizo kwa wakati kutokana na kuchelewa kupokea taarifa ya miradi na kuchelewa kupokea taarifa kutoka Wizarani. Pia Taasisi ilichelewa kutokana na kutumia mfumo mpya wa 'quick book' ambao ni mpya na ulichelewa kupokea taarifa.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imepokea maelezo ya Taasisi ya ZBS juu ya kasoro zilizojitokeza zilizowapelekea kukiuka Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa kuchelewa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka wa 2017/2018 kwa wakati na kujiridhisha kuwa hivi sasa kasoro hizo zimerekebishwa.

Hata hivyo, wakati Kamati inafanya ukaguzi wake na kuipitia 'Finantial Statement' ya mwaka 2017/2018 ya Taasisi hii, Kamati iligundua kuwa imesainiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya ZBS mnamo tarehe 27/09/2018 wakati tarehe iliyosainiwa na Mkurugenzi wa ZBS ni 1/10/2021 na tarehe ya kupokelewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikuwa 12/11/2018. Aidha, tarehe hizi tatu tofauti zinathibitisha wazi kuwa, ZBS ilikiuka Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2016, na imefanya hivyo kwa dharau na kutoheshimu kufuata Sheria.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaitaka Taasisi ya ZBS kuheshimu Sheria na kuacha kutafuta visingizio ambavyo havileti tija. Aidha, Kamati inaitaka Taasisi hii isirejee tena kuchelewesha kuwasilisha Hesabu zake za mwisho wa mwaka na iziwasilishe kwa wakati kwa Ofisi ya

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

5.8.3: MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya Tsh. 26,400,000 katika kipindi cha mwaka 2017/2018 na ilipofika tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 22,322,340 zilikusanywa sawa na 84% ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Kwa mwaka 2017/2018 Mamlaka ilikusanya mapato yake kupitia vyanzo vyake mbali mbali ikiwa ni hivi vifuatavyo:

Nam.	Kianzio	Kiwango
1.	SMZ	5,497,300,000
2.	VTA	160,000,000
3.	Mradi wa EQWIP HUBs	26,400,000
JUMLA		**5,683,700,000**

Aidha, kwa mwaka 2017/2018 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar ilisimamia vituo vitatu ambavyo ni:-

(i) Chuo cha Amali Mkokotoni

(ii) Chuo cha Amali Vitongoji

(iii) Chuo cha Amali Mwanakwerekwe

Kianzio kikuu cha mapato kwa Mamlaka kwa mwaka 2017/2018 ilikuwa ni malipo ya ada ya masomo zinazolipwa na wanafunzi. Vituo hivyo vilipangiwa kuchangia bajeti ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ambayo ni Tsh. 160,000,000. Kati ya hizo, Tsh. 60,000,000 ni ada ya wanafunzi na Tsh. 100,000,000 ni fedha zilizotengwa kwa kuwakopesha Wahitimu wa Mafunzo ya Amali, waliounda vikundi vya ushirika wa kujiajiri na kusajiliwa katika Idara ya vyama vya Ushirika.

Pia, Mamlaka kwa mwaka 2017/2018 ilikadiria kukusanya jumla ya Tsh. 26,400,000 kupitia kwa wahisani na hadi kufika tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 22,322,340 zilizokusanywa sawa na 84 ya makadirio, huku mradi ulikuwa bado unaendelea.

Hii ni kutokana na uingizwaji wa fedha kutoka Wahisani ambapo Mamlaka inapenda kuweka wazi kuwa:

(a) Wahisani wanaingiza fedha kwa mujibu wa shughuli husika, na

(b) Miezi miezi ya kuanza kwa mwaka wa bajeti wa Wahisani unatofautiana na mwaka wa fedha wa Serikali.

Aidha, Mamlaka ilikadiria kutumia jumla ya Tsh. 5,497,300,000 kwa matumizi ya kawaida na ilipofika Juni 2018, fedha iliyopatikana kwa Mamlaka ilikuwa Tsh. 5,137,777,612 sawa na 93% ya makadirio. Hii ni kutokana na uhaba wa fedha kutoka Serikali kuu.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na taarifa za vyanzo vya mapato ya Mamlaka vilivyowasilishwa, Kamati imegundua kuwepo kwa tofauti kwa taarifa za makusanyo baina ya ripoti ya Mamlaka ya Mkaguzi wa Ndani alieleza kukusanywa kwa Tsh. 5,140,305,025 kuwa ni mapato halisi yaliyokusanywa kwa mwaka 2017/2018, fedha ambazo zinatofautiana na 'Finantial Statement' ya Mamlaka, inayoeleza kukusanywa kwa Tsh. 5,137,777,612 na ni tofauti na yaliyowasilishwa moja kwa moja kwa Kamati kama yalivyoelezwa hapo juu kuwa Tsh. 5,683,700,000.

Pamoja na hayo, Kamati ilipoendelea kuhoji taarifa za fedha za Mamlaka, iliendelea kukuta tofauti takriban kwa kila taarifa ya fedha iliyowasilishwa kwa Kamati, baina ya taarifa zilizoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani ya Mamlaka ya mwaka 2017/2018, Bajeti yao ya mwaka 2017/2018, 'Finantial Statement' ya Malmaka ya mwaka 2017/2018 na majibu yaliyowasilishwa kwa Kamati.

Aidha, Kamati ilishangazwa na Wahasibu wa Mamlaka baada ya kuhojiwa kuhusiana na mapato ya ada za wanafunzi yaliyokadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2017/2018 na kueleza kuwa walikadiria kukusanya Tsh. 60,000,000, lakini ada halisi iliyokusanywa kwa mwaka huo hawaijui. Hivyo, Kamati haikuridhishwa na kitendo cha Mamlaka kushindwa kujua kima halisi cha mapato ya ada ya wanafunzi kwa mwaka 2017/2018 na pia hakikuwemo katika taarifa walizoziwasilisha kwa Kamati, hali inayothibitisha wazi kuwa, Mamlaka imeshindwa kudhibiti ipasavyo mapato halisi ya ada za wanafunzi kwa mwaka 2017/2018.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka iwe makini na taarifa zake za fedha inazoziandaa na ihakikishe inadhibiti vyema vyanzo vyake vya mapato, ili kuleta tija ya makusanyo kwa maslahi ya nchi yetu.

Taarifa ya Matumizi

Kwa mwaka 2017/2018, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar ilikadiriwa kutumia Tsh. 5,497,300,000 kwa matumizi ya kawaida na ilipofika tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 5,137,777,612 zilitumika ikiwa ni sawa 93% ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Katika kipindi cha mwaka 2017/2018 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imepanga kutumia Tsh. 5,896,553,653 na hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka ilitumia Tsh. 4,346,815,974 kwa ajili ya kuendesha program ndogo yake ambayo ni tofauti na Tsh. 1,549,737,679 sawa na 74% ya kamadirio ya matumizi kama inavyoonekana hapa chini:-

MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018				
Mwezi	**Makadirio**	**Halisi**	**Tofauti**	**Asilimia**
July - Sept 2017	811,504,874,	609,000,600	202,504,274	75%
Oct - Dec 2017	1,906,841,504	869,609,364	1,037,232,140	46%
Jan - March 2018	1,734,824,375	862,559,590	872,264,785	50%
April - June 2018	1,443,382,900	2,005,646,420	(562,263,520)	139%
Jumla	**5,896,553,653**	**4,346,815,974**	**1,549,737,679**	**74%**

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imejiridhisha tena tofauti ya taarifa za Mamlaka kuhusiana na matumizi ya fedha za mwaka 2017/2018, kuwa ni tofauti na zilizoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hali iliyodhihirishia Kamati juu ya tofauti ya hesabu za Mamlaka kati ya taarifa zake mbali mbali za kifedha.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka iwe makini katika usimamizi na utumiaji wa fedha za Umma lakini pia itunze taarifa zake za fedha katika usahihi na uhakika, ili kuepusha kupatikana kwa dhana ya

matumizi mabaya ya fedha za Umma.

5.8.4: BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR

Taarifa ya Mapato

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar ilipata ruzuku ya Tsh. 505,601,855, kati ya fedha hizo, Tsh. Mishahara ni Tsh. 368,138,525, sawa na 115% ya bajeti iliyopangwa, na kwa matumizi ya uendeshaji wa wa Ofisi, Tsh. 137,463,855 zilipatikana, sawa na 91.6% ya kilichopangwa.

Majibu ya Bodi

Pamoja na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na mapato ya Bodi ya Huduma za Maktaba, katika kipindi cha mwaka 2017/2018 ilikusanya Tsh. 5,533,100 zilizotokana na ada za kujiunga na uanachama, chumba cha kompyuta na ukodishaji ukumbi. Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilionesha kuwa Bodi hii ina kasoro ya kutokuwepo kwa Afisa Manunuzi na kuchelewa kupelekwa benki kwa makusanyo yanayopatikana ndani na kushuka kwa makusanyo hayo.

Kasoro ya kutokuwepo Afisa Manunuzi ilianza kufanyiwa kazi kwa kuteua Afisa Maalum wa kusimamia masuala yote ya ununuzi wa vifaa na huduma. Aidha, Bodi ilichukuwa jitihada ya kuomba kibali cha ajira ya Afisa Manunuzi kutoka Utumishi, lakini kwa masikitiko makubwa bado haijafanikisha. Kuhusiana na kupelekwa benki kwa wakati, makusanyo ya ndani, Bodi imezingatia ushauri huo wa Mkaguzi. Makusanyo yote yanayopatikana yanapelekwa benki katika muda sahihi.

Aidha, kuhusu kushuka kwa makusanyo, Bodi inakusanya fedha kutokana na ada ya uanachama, chumba cha kompyuta na kodi ya ukumbi. Idadi ya wanachama wanaojiunga na Maktaba hairidhishi kutokana na jamii kutokuwa na utamaduni wa kusoma vitabu. Shughuli mbali mbali za kuhamasisha matumizi ya maktaba yanafanyika ili wananchi watumie maktaba lakini bado namba ni ndogo, ukilinganisha na idadi ya wananchi. Kuna changamoto ya umbali na uhaba wa maktaba za Umma nchini. Changamoto hii pia inachangia kwa kiasi kikubwa wananchi kushindwa kutumia maktaba hususan watoto.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imejiridhisha kuwa, Bodi hii ya Huduma za Maktaba inafanya vizuri katika kusimamia mapato yake, pamoja na ukweli wa uchache wa vyanzo hivyo. Aidha, Kamati imeridhishwa sana na uadilifu wa watendaji wa Bodi na kuwataka kuendelea na

uzalendo wao.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaishauri Bodi ya Huduma za Maktaba kuendelea na juhudi zake za kukusanya mapato kupitia vyanzo vyake mbali mbali na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza makusanyo hayo.

Taarifa ya Matumizi

Shirika la Huduma za Maktaba lilikadiriwa kutumia Tsh. 469,400,000 kwa kazi za kawaida. Hata hivyo, ilipofika tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 505,601,855 ziliingizwa na kutumika, sawa na 107% ya makadirio.

Majibu ya Bodi

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar ilipangiwa bajeti ya matumizi ya Tsh. 469,400,000, kati ya hizo, mshahara ni Tsh. 319,400,000 na matumizi ya kawaida ni Tsh. 150,000,000.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na uchanga wake, Kamati imeshuhudia Uongozi wa Bodi ya Huduma za Maktaba kujiandaa vyema na kuiridhisha Kamati kwa kila taarifa iliyoihitaji. Aidha, Kamati imejiridhisha kuwa, Bodi hii inasimamia vyema mapato na matumizi ya fedha za Serikali zinazokasimiwa hapo kwa matumizi ya maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inapendekeza Uongozi wa Bodi ya Huduma za Maktaba kuongeza wigo wa kukusanya mapato yake na iendelee kufanya juhudi za kutumia vyema fedha za Serikali kwa kuhakikisha malengo inayojiwekea kwa kila mwaka, yanafikiwa.

5.8.5: TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Taarifa ya Mapato

Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ilikadiriwa kukusanya Tsh. 395,000,000 katika kipindi cha mwaka 2017/2018. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ilikusanya Tsh. 258,344,006 sawa na 65% ya makadirio.

Majibu ya Taasisi

Ili kutekeleza matakwa ya Mpango Mkakati wa 2015 – 2020, mwaka wa fedha 2017/2018 zilihitajika Tsh. 3,685,851,961 kati ya fedha hizo, Tsh. 531,252,000 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la madarasa na samani za jengo hilo. Fedha hizi zimo katika kasma ya mradi wa ALSD II na ambazo hazikujumuishwa katika bajeti hii. Ukitoa kiwango hicho cha fedha, Taasisi ilikadiria kukusanya Tsh. 1,724,770,000.

Mwaka wa fedha 2017/2018 Taasisi imepangiwa ruzuku kutoka Serikalini, Tsh. 1,348,600,000 na Taasisi ya Karume imekadiria kukusanya Tsh. 395,000,000 kiwango ambacho kilijipangia kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hivyo kufanya makadirio kwa mwaka huu wa fedha kuwa ni Tsh. 1,743,600,000. Ruzuku kutoka Serikalini inachukua 77% na mapato ya ndani ya Taasisi ya Karume yanachukua 23% ya mapato yote.

Ongezeko la 34.2% ya ruzuku imelenga katika kuboresha huduma za Idara sambamba na mishahara ya waajiriwa 10 wapya ya mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, ongezeko hilo ukilinganisha na mwaka 2016/2017 yanatokana na utaratibu mpya wa ukusanyaji wa mapato ya Taasisi pamoja na ongezeko la mchango wa wanafunzi ambao umechukua 97% ya mapato yote ya Taasisi. Katika mapato mengineyo ambayo yanachukua 3%, hakukuwa na ongezeko kubwa sana mbali na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka vitengo na kazi zinazofanywa na Idara za Taasisi. Jadueli zifuatazo zinaonesha zaidi taarifa hizo za mapato ya Taasisi:-

Makadirio ya Mapato ya Taasisi ya Karume kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Chanzo cha Mapato	**Makadirio ya Mapato**		
Ruzuku ya Serikali	**2016/2017**	**2017/2018**	**Ongezeko**
Ruzuku ya Serikali	1,004,730,000	1,348,600,000	343,870,000
Maendeleo	Hapana	Hapana	-
Taasisi ya Karume	300,000,000	395,000,000	95,000,000
Jumla	**1,304,730,000**	**1,743,600,000**	**438,870,000**

Jadueli No.2 Mchanganuo wa Makadirio ya mapato ya Taasisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Makadirio ya Mapato kutoka Taasisi ya Karume

(i)	*Mapato ya Taaluma*				
Kifungu	**Mchango**	**Kipimo**	**Idadi**	**Gharama**	**Makadirio**
(a)	Wanafunzi wa NTA (Ufundi na Biashara)	Mwanafunzi	530	232,500	123,225,000
(b)	Mwanafunzi NTA (VTT)	Mwanafunzi	60	322,000	19,320,000
(c)	Mwanafunzi NTA (Walimu)	Mwanafunzi	100	172,490	17,249,000
(d)	Mwanafunzi (VET)	Mwanafunzi	800	76,000	60,800,000
(e)	**Usajili wa wanafunzi KIST**	Mwanafunzi	693	10,000	6,930,000
(f)	Usajili wa wanfunzi NACTE	Mwanafunzi	693	20,000	13,860,000
(g)	**Dakhalia**	Mwanafunzi	144	75,000	10,800,000
(h)	Computer Maintanance	Mwanafunzi	693	15,000	10,395,000
(i)	Serikali ya Wanafunzi na Michezo	Mwanafunzi	693	6,000	4,158,000
(j)	Kitambulisho	Mwanafunzi	1,493	3,000	4,479,000
(k)	Mchango wa Usafiri	Mwanafunzi	593	100,000	59,300,000
	Mchango wa Usafiri (TT)	Mwanafunzi	100	50,000	5,000,000
	Mafunzo Viwandani	Mwanafunzi	693	50,000	34,650,000
	Mahafali	Mwanafunzi	693	20,000	13,860,000
	Jumla ndogo				**384,026,000**
(ii)	*Mapato Mengineyo*				
Kifungu	**Maelezo**	**Kipimo**	**Idadi**	**Gharama**	**Makadirio**
(p)	Mafunzo ya Magari (Kodi)	Mwezi	12	250,000	3,000,000
(q)	Mafunzo kazini (*Zantel Intership Commission)*	Mwezi	12	100,000	1,200,000

(r)	Mchango wa karakana ya magari	Mwezi	12	190,000	2,280,000
(s)	Idara (*Services & Consultancy)*	Mwezi	12	150,000	1,800,000
(t)	Mapato mengineyo	Mwezi	12	224,500	2,694,000
	Jumla ndogo				**10,974,000**
	Jumla ndogo (i + ii)				**395,000,000**

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imegundua kuwa Taasisi inapungukiwa na mapato yake kutokana na unyonge wa wanafunzi wanaojiunga na Taasisi hiyo, kuwa wengi wao ni wanyonge kiuchumi, hali inayopunguza makusanyo kupitia chanzo cha ada ya wanafunzi, kikiwa ni sehemu ya vyanzo vya mapato vya Taasisi ya Karume. Aidha, Taasisi pia inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa vifaa vyake, ambavyo vingi ni vya zamani.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha kivifaa vya kisasa Taasisi ya Chuo cha Karume, ili kuinua uwezo wake wa kujiendesha.

Taarifa ya Matumizi

Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia iliidhinishiwa kutumia Tsh. 1,348,600,000 kwa kazi za kawaida na ilipofikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tsh. 1,470,039,440 ziliingizwa na kutumika, ikiwa ni sawa na 109 ya makadirio.

Majibu ya Taasisi

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Taasisi ya Karume imekadiria kutumia Tsh. 1,743,600,000 kwa matumizi ya kawaida, makadirio ambayo yamezingatia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa 2015 – 2020 ingawa si program ndogo zote zilizoweza kupangiwa fedha za matumizi ambazo hazikulinganisha mahitaji halisi ya Mpango Mkakati wa 2015 - 2020 na kiwango cha fedha kilichopangiwa kutoka ruzuku ya Serikali.

Kwa mazingatio ya utaratibu wa *PBB (Program Based Budget)*, Taasisi kwa mwaka 2017/2018 ilikuwa na program kuu tatu na program ndogo kumi na moja, huduma zinazotolewa pamoja na shughuli zilizopangwa kutimiza malengo makuu.

Aidha, hali halisi ya matumizi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, Taasisi imefanya matumizi ya Tsh. 1,683,122,759 sawa na 96.5% ya makadirio ya matumizi yote ya mwaka 2017/2018, ikiwa ni matumizi ya mishahara, kazi za kawaida (OC) pamoja na mchango wa muajiri wa 13% za ZSSF. Mchanganuo mdogo wa matumizi hayo ni kama ufuatao:

Maelezo	Makadirio ya matumizi kwa 2017/2018	Matumizi halisi ya mwaka 2017/2018	Asilimia
Jumla	1,743,600,000	1,683,122,759	96.5%

Baada ya kufanya matumizi ya Tsh. 1,683,122,759 kutoka katika Tsh. 1,763,023,535 zilizokusanywa, Taasisi imebakia na Tsh. 79,900,776 ambazo ziliingia katika mwaka wa fedha 2018-2019, kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, Taasisi ilikuwa na Tsh. 55,974,691 ambazo ziliendelea katika kufanikisha program zilizofuata.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imepitia taarifa za matumizi ya Taasisi ya Karume na kugundua kasoro ndogo za kibinaadamu katika hesabu zao, kasoro ambazo Kamati imezivumilia baada ya kupata ufafanuzi wa kina kutoka kwa viongozi wa Taasisi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaitaka Taasisi ya Karume kuongeza juhudi katika kutunza taarifa za matumizi yake na kuepusha kasoro mbali mbali zilizojitokeza wakati wa ukaguzi wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MAWIZARA YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

5.2.13: BARAZA LA MANISPAA MJINI

Kamati ya LAAC ilifanya ziara katika Baraza la Manispaa Mjini tarehe 08 Aprili, 2021, hata hivyo, kikao hicho kiliakhirishwa bila ya mafanikio baada ya Watendaji wa Baraza la Manispaa hiyo kuonekana kutojiandaa vyema. Kitendo hicho kiliwapelekea Watendaji hao kushindwa kujibu kwa usahihi asilimia kubwa ya maswali ya Kamati hii kwa madai kwamba Watendaji wengi waliokuwepo katika Manispaa hiyo kwa wakati ule ni wapya ingawa, Kamati hii katika barua yake iliwataka Watendaji hao kuwashirikisha watu wote

waliohusika katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Kutokana na hali hiyo, Watendaji wa Baraza la Manispaa waliandaa kikao chengine tarehe 28 Julai, 2021 na yafuatayo yalijitokeza:

Taarifa ya Mapato

Baraza la Manispaa Mjini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 6,469,160,843, kati ya hizo jumla ya Tsh. 3,535,518,000 ni kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya Tsh. 2,933,642,843 ikiwa ni Ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini.

Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 6,959,873,636.19 zilikusanywa sawa na asilimia 107 ya makadirio, kati ya hizo jumla ya Tsh. 3,537,595,623.19 ni kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya shilingi 3,422,278,013 ni ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini sawa na asilimia 117 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Baraza la Manispaa Mjini lilikuwa na vyanzo vya mapato vya aina mbili kama ifuatavyo:

i. Mapato kutoka katika vyanzo vyake vya ndani; na
ii. Ruzuku kutoka Serikali Kuu

Isipokuwa kwamba, chanzo cha Ruzuku pia kiligawika sehemu mbili kama ifuatavyo: Ruzuku ya mshahara na matumizi mengineyo kwa sekta zilizogatuliwa ikiwemo Afya ya Msingi, Elimu ya Maandalizi na Msingi na Kilimo cha Ugani. Hii ni kutokana na kuwa katika mwaka huo wa fedha ndio ilianza kutekelezwa dhana ya ugatuzi ambapo Serikali Kuu ilikasimu baadhi ya majukumu kwa Serikali za Mitaa chini ya usimamizi wa Mikoa. Jadweli lifuatalo linaonesha mgawanyo wa Mapato kiasilimia

Nam.	Chanzo	Makadirio	Asilimia
1.	Mapato ya vyazo vya ndani	3,535,518,000	54.65
2.	(a) Ruzuku ya Mshahara	2,500,000,000	38.65
	(b) Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (Ugatuzi)	433,642,843	6.70
	Jumla	**6,649,160,843**	**100.00**

Bajeti ya Makusanyo ya vyanzo vya ndani 2017/2018

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Baraza la Manispaa lilikuwa na vyanzo vya mapato 15. Vyanzo hivyo vilihusisha mapato yanatokana na mapato katika masoko, maegesho, leseni za biashara, matangazo, umiliki wa majengo, ada za usafi, ukaguzi wa afya na bustani. Mchanganuo wa mapato hayo unaonekana katika Jadweli linalofuata.

Nam	Vianzio Vya Mapato	Mpango wa Bajeti ya Mwaka	Makusanyo halisi
1.	Mapato ya masoko	1,030,431,000	948,059,300.00
2.	Mapato ya maegesho	712,800,000	777,782,500.00
3.	Mapato ya leseni za biashara	730,500,000	704,336,000.00
4.	Mapato ya matangazo	215,000,000	226,926,308.19
5.	Kodi ya umiliki wa jengo	79,350,950	420,541,765.00
6.	Kodi ya ukodishaji	48,650,000	97,928,250.00
7.	Ada za usafi makao makuu	12,500,000	47,712,500.00
8.	Ada za usafi kitengo cha michirizi	440,000,000	81,538,000.00
9.	Ada za kukodisha milango ya maduka	110,400,000	50,165,000.00
10.	Ada za viwanja vya sikukuu	27,200,000	16,097,000.00
11.	Mauzo ya fomu za maombi ya leseni	37,700,000	37,124,000.00
12.	Tozo za Mahkama	10,800,000	15,304,000.00
13.	Ada za ukaguzi wa afya	12,480,000	4,335,000.00
14.	Ada za huduma za bustani	4,680,000	2,169,000.00
15.	Mapato mengineyo	63,026,050	107,577,000.00
	Jumla ya Vyanzo vya ndani	**3,535,518,000**	**3,537,595,623.19**
16.	Ruzuku ya Mshahara	2,500,000,000	3,076,349,625.00

17.	Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (Ugatuzi)	433,642,843	345,928,388.00
	Jumla ya Ruzuku	**2,933,642,843**	**3,422,278,013.00**
	Jumla ya Mapato	**6,469,160,843**	**6,959,873,636,19**

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalibainika:

1. Chanzo cha mapato cha vibali vya ujenzi mapato yake hayakukadiriwa kwa kuwa Kitengo cha Udhibiti na Usimamizi wa Ujenzi (DCU) ilikuwa ndio kwanza inaanzishwa. Hata hivyo, kianzio hicho kilikusanya Tsh. 50,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Kijangwani na fedha hizo ziliingizwa katika kianzio cha mapato mengineyo.

2. Viwango vya ufungwaji wa hesabu ya mwaka havikufutwa, hii ni kutokana na kuwa mapato yote yameingizwa kwenye kifungu cha cha mapato mengineyo "Other Receipt".

3. Mapato ya Baraza yameongezeka kwa upande wa Ruzuku kutokana na ongezeko la mshahara.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC imelishauri Baraza la Manispaa Mjini kuhakikisha kuwa linafunga hesabu zake za mwaka kwa kuzingatia vigezo na misingi iliyowekwa ili kuepuka hoja zisizo za lazima.

2. Aidha, Kamati hii ilipendekeza kianzio cha mapato cha adhabu ya papo kwa papo kisomeke kama jina lake lilivyo.

3. Vile vile, Kamati ya LAAC imeishauri Wizara ya Nchi, Fedha na Mipango kuwateuwa Wahasibu Wakuu wa Taasisi wenye sifa ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa taratibu.

Taarifa ya Matumizi

Baraza la Manispaa katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 6,469,160,843 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia 30 Juni, 2018 jumla ya Tsh. 6,659,873,636 zilitumika ikiwa sawa na asilimia 103 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini

Katika mwaka 2017/2018 Baraza la Manispaa Mjini lilikadiria kutumia jumla ya Tsh 6,469,160,843 kati ya hizo makadirio ya Mshahara yalikuwa 2,500,000,000 na Tsh 3,969,160,843 makadirio ya Matumizi ya kazi za Kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 Baraza la Manispaa Mjini limetumia jumla ya Tsh. 6,659,873,636 kati ya matumizi hayo Tsh. 3,076,349,625.00 sawa na asilimia 123 ya lengo la Tsh. 2,500,000,000 ya mishahara. Jadweli lifuatalo linaonesha mchanganuo wa Matumizi hayo.

Maelezo	**Makadirio**	**Matumizi halisi**	**Pungufu/ziada**
	A	**B**	**C = A - B**
	TZS	**TZS**	**TZS**
Huduma za jamii na Mazingira	641,845,000.00	479,361,755.00	162,483,245.00
Mipango miji kazi na ujenzi	466,221,000.00	470,927,046.54	(4,706,046.54)
Sheria na Utawala	4,148,462,500.00	4,939,182,694.10	(790,720,194.10)
Fedha, Mipango na Uchumi	200,989,500.00	78,846,302.20	122,143,197.80
Huduma za Usafi (Sewerage and Sanitation Division)	578,000,000.00	660,640,216.00	(82,640,216.00)
Afya	344,337,562.00	143,991,204.00	200,346,358.00
Elimu	81,614,000.00	54,609,720.00	27,004,280.00
Kilimo	7,691,281.00	7,003,297.00	687,984.00
	6,469,160,843.00	**6,834,562,234.84**	**(365,401,391.84)**

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa taarifa za matumizi zipo tofauti baina ya taarifa yao waliyoiwasilisha kwenye Kamati na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC ilishindwa kupata maelezo ya kutosha kutoka kwa Watendaji wa Manispaa kwa kisingizio kuwa siku zimekuwa nyingi hivyo hawakumbuki kila kitu.

Kwa kuwa maswali mengi hayakupata majibu ya kujitosheleza kutokana na sababu iliyoelezwa na Watendaji wa Manispaa, hivyo, Kamati ya LAAC haikuwa na maelezo zaidi juu ya matumizi hayo.

MATOKEO YA UKAGUZI

5.2.13.1 Kukosekana kwa takwimu za wafanyabiashara wanaolipa leseni za biashara

Ukaguzi ulifanya tathmini ya vyanzo vya mapato ya Baraza la Manispaa Mjini ili kubaini idadi halisi ya wanaopaswa kulipa leseni za biashara na idadi halisi ya kilicholipwa. Ukaguzi umebaini kuwa katika kitengo cha ukusanyaji wa mapato ya leseni ya biashara na kitengo cha mabango hakukuwa na takwimu sahihi juu ya idadi ya wanaopaswa kulipa, hivyo ukaguzi umeshindwa kujua idadi halisi ya wafanyabiashara wanaopaswa kulipia leseni za biashara na huduma ya matangazo kupitia mabango.

Kutokuwa na takwimu halisi ya idadi ya wafanyabiashara wanaopaswa kulipia leseni za biasharana huduma ya mabango ya matangazo kunaweza kupelekea Baraza kutowatambua wafanyabiashara wanaopaswa kulipia leseni hivyo kulikosesha baraza mapato.

Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini

Ni kweli kwa kipindi kirefu Baraza la Manispaa Mjini lilikosa takwimu sahihi juu ya idadi ya wanaopaswa kulipia leseni za biashara na huduma za matangazo kupitia mabango. Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021, Baraza limeunda Kamati maalumu kwa ajili ya kutathmini mali za Baraza sambamba na kufanya utafiti kwa ajili ya kuwatambua wafanyabiashara na taasisi zote zinazopaswa kulipa leseni, Kamati hiyo tayari inaendelea kazi hiyo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kwa kuwa Baraza la Manispaa Mjini lilikiri kosa hilo Kamati ya LAAC imeibakisha hoja hiyo kama ilivyo na imelitaka Baraza hili kuzidisha juhudi katika kutekeleza suala hilo.

5.2.14: BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “A”

Taarifa ya Mapato

Baraza la Manispaa Magharibi “A” lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,566,374,523,

kati ya hizo jumla ya shilingi 699,980,000 ikiwa ni kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya shilingi 866,394,523 ikiwa ni Ruzuku ya mishahara na ya kazi za kawaida kutoka Serikalini.

Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 1,640,147,656 zilikusanywa sawa na asilimia 105 ya makadirio, kati ya hizo jumla ya shilingi 818,147,381 kutoka vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya shilingi 802,000,275 ikiwa ni ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini na jumla ya shilingi 20,000,000 ikiwa ni ruzuku kutoka katika Kitengo cha Udhibiti na Usimamizi wa Ujenzi (DCU).

Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini

Baraza la Manispaa Magharibi "A" katika mwaka huo wa fedha lilifanikiwa kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato yake. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarisha huduma za leseni, mazingira na makusanyo kutoka katika vyanzo vya ndani vya Baraza.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hiyo Kamati ya LAAC ilibaini kuwa miongoni mwa chanzo cha mapato katika mwaka husika wa fedha ni kodi ya mabanda ya mbao yaliopo Chumbuni ambapo jumla ya mabanda hayo ni thelani (30) na kila banda lilikodishwa kwa Tsh. 80,000, hata hivyo, baadhi ya mabanda bado hayajakodiwa.

Vile vile, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa wakoshishwaji wa mabanda hayo walikuwa wanalipa kwa miezi mitatu.

Kwa kuwa gharama za ukodishaji wa vitu huongezeka kutokana na hali ya maisha, na kwa kuwa imezoweleka kuwa mali nyingi za Serikali hukodishwa katika thamani ndogo kinyume na uhalisia wake na jambo hilo huipelekea Serikali kupata hasara. Hivyo basi, Kamati ya LAAC ililishauri Baraza hilo kutosita kuongeza thamani ya kodi hiyo ili Baraza hilo liweze kukusanya mapato yake zaidi kwa maslahi ya Baraza na wananchi wake kwa ujumla.

Sambamba na hayo, Kamati ya LAAC ililishauri Baraza la Manispaa Magharibi "A" kubadilisha jina la chanzo cha mapato kinachosomeka kuwa ni "mazingira" na chanzo hicho kisomeke kuwa ni "ada ya usafi" ili kiweze kujulikana kwa urahisi.

Taarifa ya Matumizi

Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa

kutumia jumla ya shilingi 1,397,054,523. Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 1,458,364,481 zilitumika ikiwa sawa na asilimia 104 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Manispaa Magharibi "A"

Baraza la Manispaa Magharibi "A" lilitumia kiasi hicho cha fedha kukiwa na ongezeko la asilimia 104 ya makadirio kutokana na sababu zifuatazo:

i. Ukarabati wa jengo la ofisi;

ii. Ununuzi wa vifaa vya usafi;

iii. Malipo ya vikundi vya usafi; na

iv. Utekelezaji wa shughuli za kawaida kama vile ununuzi wa mafuta na vifaa vya kuandikia

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalibainika:

i. Baraza la Manispaa Magharibi "A" lilikadiria kutumia fedha kidogo katika mwaka husika kwa kuwa Baraza hilo lilikuwa ndio kwanza limeasisiwa, hivyo, lilikuwa linahofu ya kujakushindwa kutekeleza malengo yao ipasavyo.

ii. Hakukuwa na Bodi ya Zabuni, hivyo, vikundi vya usafi vilipatikana baada ya kuwashajihisha vijana wa Shehia mbali mbali ndani ya Baraza hilo kuanzisha vikundi hivyo. Hivyo, fedha husika zililipwa moja kwa moja kwa vikundi vyenyewe.

iii. Ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka haukuzingatia vigezo vinavyotakiwa Kitaifa na Kimataifa. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya matumizi yalifanywa kinyume na vifungu husika. Kwa mfano; fedha za matengenezo zimeingizwa kwenye kifungu cha ununuzi wa vifaa.

iv. Tsh. 20,000,000 kutoka Kitengo cha Udhibiti na Usimamizi wa Ujenzi (DCU) hazikuwahi kutumika katika mwaka wa fedha husika kwa kuwa fedha hizo zimeingizwa mwishoni mwa mwaka wa fedha.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC ilipendekeza mambo yafuatayo:

i. Baraza la Manispaa Magharibi “A” lihakikishe kuwa linafunga hesabu zake za mwaka kwa kuzingatia vigezo na misingi iliyowekwa ili kuepuka hoja zisizo za lazima.

ii. Wizara ya Nchi, Fedha na Mipango kuwateuwa Wahasibu Wakuu wa Taasisi wenye sifa ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

iii. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi husika yapangwe kwa mujibu wa hali halisi iliyopo. Hivyo, Kitengo cha Mapato kilichopo Wizara Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kihakikishe kuwa kinapanga bajeti za Taasisi kwa mujibu wa hali halisi ya vyanzo vyao vya mapato.

MATOKEO YA UKAGUZI

5.2.14.1 Kukosekana takwimu za wafanyabiashara wanaolipa leseni za biashara

Ukaguzi ulifanya tathmini ya vyanzo vya mapato ya Baraza la Manispaa ya Magharibia “A” ili kubaini idadi ya wafanyabiashara wanaopaswa kulipa kodi na idadi halisi ya kilicholipwa.

Ukaguzi umebaini kuwa hakukuwa na takwimu sahihi juu ya idadi ya wanaopaswa kulipa, hivyo, ukaguzi umeshindwa kujua idadi halisi ya wafanyabiashara wanaopaswa kulipia leseni za biashara na huhuma ya matangazo kupitia mabango.

Kutokuwa na takwimu halisi ya idadi ya wafanyabiashara wanaopaswa kulipia leseni za biashara na mabango ya matangazo kunaweza kupelekea Baraza kutowatambua wafanyabiashara wanaopaswa kulipa leseni hivyo kulikosesha Baraza hilo mapato.

Majibu ya Baraza la Manispaa Magharibi “A”

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Baraza hili lilikuwa na jumla ya wafanyabiashara 3,510 kati ya hao wafanyabiashara 3,336 waliopata huduma ya leseni na mabango 34 yalifanikiwa kulipiwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Baraza hilo na ilitaka kujua sababu zilizopelekea Baraza hilo kushindwa kumpatia Mkaguzi Mkuu takwimu za wafanyabiashara wake wakati wa ukaguzi ambapo, Baraza la Manispaa Magharibi “A” liliieleza Kamati hii kuwa lilishindwa kumpatia Mkaguzi Mkuu takwimu hiyo kutokana na kuwa Baraza hilo lilikuwa ndio kwanza linaanzishwa hivyo, mipaka yake ilikuwa

haijajulikana.

Kutokana na majibu hayo, Kamati ya LAAC iliishauri Serikali kujitahidi kufanya maandalizi ya kina kwa kila jambo au kitu inachokianzisha ili kuepusha usumbufu kwa Watendaji wa jambo au kitu husika.

5.2.15: BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "B"

Taarifa ya Mapato

Baraza la Manispaa Magharibi "B" kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 2,509,958,605. Kati ya hizo jumla ya Tsh. 1,480,000,000 ni kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya Tsh. 984,958,605 ikiwa ni Ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini.

Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 2,298,534,312 zilikusanywa sawa na asilimia 92 ya makadirio. Kati ya hizo jumla ya Tsh. 1,390,476,302 sawa na asilimia 94 ni kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya shilingi 908, 058,010 ni Ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini sawa na asilimia 92 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Manispaa Magharibi "B"

Baraza la Manispaa Magharibi "B" halikuwasilisha moja kwa moja taarifa ya mapato kwa Kamati hii kama ilivyozoweleka, isipokuwa kwamba, taarifa hizo zilipatikana kwa mujibu wa majadiliano yaliyofanywa na Kamati.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalibainika:

1. Katika mwezi wa Januari hadi Machi, 2018 baadhi ya vianzio vilishindwa kukusanya fedha kutokana na sababu zifuatazo:

    a. Kianzio cha Huduma ya Bidhaa na Mazao hakikukusanya fedha kwa kuwa kipindi hicho kilikuwa kipindi cha mpito.

    b. Mradi wa taka haukukusanya fedha kwa kuwa mradi huo walipewa wananchi, isipokuwa kwamba, kutokana na kasoro mbali mbali zilizojitokeza wananchi hao walionekana kushindwa kuusimamia mradi huo.

2. Mapato ya Fumba walitakiwa wasiyaunganishe kwenye Mapato ya Mengineyo ambapo jumla ya Tsh. 51,336,100 zilikusanywa. Kamati ilitaka kujua sababu ya kufanya hivyo, ambapo Baraza halikuwa na majibu ya ziada juu ya swali hilo.

3. Baada ya Serikali kuanzisha mfumo wa ugatuzi jumla ya Tsh. 984,958,605 zilizotengwa kwa ajili ya Ruzuku zilitumika kwa kuwalipa watendaji mishahara yao pamoja na kutumika kwa kazi za maendeleo.

4. Kianzio cha mapato cha Mradi wa matofali hakikuwepo kuanzia mwezi wa Aprili, 2018 kutokana na uhaba wa mchanga ndio maana kianzio hicho kimekusanya kiwango kidogo chenye thamani ya Tsh. 3000.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na mapungufu hayo, Kamati ya LAAC ililitaka Baraza la Manispaa Magharibi "B" kuhakikisha kuwa linafanya utafiti wa kina linapotaka kumkasimia madaraka yake mtu mwengine ili kuepusha karoso zisizo na msingi pamoja na kukosa mapato.

Vile vile, Baraza la Manispaa Magharibi "B" lihakikishe kuwa linayajumuisha mapato yote linayoyakusanya kwenye Taarifa ya Hesabu ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) kwa yake mapato ambayo hayakutarajiwa kwani kwenye Taarifa hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kifungu cha Mapato Mengineyo kinaonekana kama hakikukusanya fedha wakati zipo jumla ya Tsh. 51,336,100.

Taarifa ya Matumizi

Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,509,958,605. Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 2,427,477,723 zilitumika ikiwa sawa na asilimia 104 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Manispaa Magharibi "B"

Baraza la Manispaa Magharibi "B" halikuwasilisha moja kwa moja taarifa ya matumizi kwa Kamati hii kama ilivyozoweleka, isipokuwa kwamba, taarifa hizo zilipatikana kwa mujibu wa majadiliano yaliyofanywa na Kamati kwa kuzingatia Taarifa ya Utekelezaji.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilitaka kujua kwa nini Baraza la Manispaa Magharibi "B" katika mwaka huo wa fedha lilitumia fedha nyingi ingawa walikusanya kidogo?. Kutokana na swali hilo, Baraza hili liliieleza Kamati kuwa lilitumia fedha nyingi kinyume na makusanyo yake kwa kuwa walikuwa na bakaa ya fedha katika mwaka uliopita.

Kiujumla Kamati hii iliridhika na matumizi yaliyofanywa na Baraza la Manispaa Magharibi "B".

MATOKEO YA UKAGUZI

5.2.15.1 Kukosekana takwimu za wafanyabiashara wanaolipa leseni

Ukaguzi ulifanya tathmini ya vyanzo vya mapato ya Baraza la Manispaa ya Magharibia "B" ili kubaini idadi ya wafanyabiashara wanaopaswa kulipa kodi na idadi halisi ya kilicholipwa.

Ukaguzi umebaini kuwa hakukuwa na takwimu sahihi juu ya idadi ya wanaopaswa kulipa, hivyo, ukaguzi umeshindwa kujua idadi halisi ya wafanyabiashara wanaopaswa kulipia leseni za biashara na huhuma ya matangazo kupitia mabango.

Kutokuwa na takwimu halisi ya idadi ya wafanyabiashara wanaopaswa kulipia leseni za biashara na mabango ya matangazo kunaweza kupelekea Baraza kutowatambua wafanyabiashara wanaopaswa kulipa leseni hivyo kulikosesha Baraza hilo mapato.

Majibu ya Baraza la Manispaa Magharibi "B"

Ni kweli kwamba Baraza la Manispaa Magharibi "B" katika mwaka wa fedha 2017/2018 halikuwa na takwimu sahihi za wafanyabiashara wanaolipa leseni kutokana na:

i. Mgawanyo wa wafanyabiashara ambao walikuwa wanalipa leseni za Biashara katika iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi.
ii. Kutokana na Mfumo wa kieletroniki (Database) wa kuhifadhia Takwimu.
iii. Kutokuwa na Afis Takwimu ambae ndio Muhusika wa uandaaji na uhifadhi wa Takwimu.

Hivyo kwa wakati huo taarifa zote zilikuwa zikihifadhiwa katika mfumo wa "Manual" ambao ulikuwa si rahisi kupata taarifa za wafanyabiashara hususan wadogowadogo ambao mara nyingi huwa wanahama kutoka sehemu moja kwenda nyengine au kubadilisha aina ya biashara.

Kutokana na mabadiliko makubwa yanayoendelea kufanyika juu ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato hasa makusanyo yatokanayo na Leseni za Biashara, Ofisi ya Baraza la Manispaa Magharibi "B" imefanya mabadiliko makubwa ya mfumo wake wa leseni ili kuboresha utoaji wa huduma pamoja udhibiti wa upotevu wa mapato, hivyo, kwa sasa Baraza lina mfumo (Database) ambao umehifadhi kumbukumbu zote za wafanyabiashara wote wanaokatisha leseni, mpaka kufikia mwaka 2019/2020 kuna jumla ya Wafanyabiashara 5981 wa leseni, wafanyabiashara wadogo 1,798 na (viosk, Migahawa na Mama/Baba lishe) ni 1005.

Ofisi inaendelea kuimarisha takwimu ya Mfumo wa Leseni kwa mujibu wa Mahitaji pamoja na takwimu za wafanyabiashara wadogo ambao wataingizwa katika mfumo wa pamoja wa vitambulisho.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC iliridhika na majibu ya Baraza la Manispaa Magharibi "B", hivyo, haikuwa na maelezo ya ziada.

Mengineyo

Baada ya majadiliano hayo yafutayo yalijitokeza:

1. Mfumo wa IFM's unachelewesha malipo ya fedha jambo linalopelekea matumizi kuzorota. Kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC iliiomba Wizara ya Nchi, Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa fedha za Serikali za Mitaa zinapatikana kwa wakati ili kuondosha usumbufu kwa watendaji.

2. Madiwani kuongezwa posho ili waweze kwenda sambamba na kasi ya ongezeko ya maisha.

5.2.16: BARAZA LA MJI KASKAZINI "A"

Maelezo ya Baraza la Mji Kaskazini "A" kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanasomeka kuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja.

Kamati ya LAAC ilifanya ziara katika Baraza la Mji Kaskazini "A" tarehe 20 Aprili, 2021, hata hivyo, kikao hicho kiliakhirishwa bila ya mafanikio baada ya Watendaji wa Baraza hilo kuonekana kutojiandaa vyema. Hii ni kutokana na kuwa Baraza hilo lilishindwa kuwasilisha mbele ya Kamati taarifa nyingi zilizotakiwa, kwa madai kwamba Watendaji wengi waliokuwepo katika Baraza hilo kwa wakati ule ni wapya ingawa, Kamati hii katika barua yake iliwataka Watendaji hao kuwashirikisha watu wote waliohusika katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Kutokana na hali hiyo, Watendaji wa Baraza la Mji Kaskazini "A" waliandaa kikao chengine tarehe 01 Julai, 2021 na yafuatayo yalijitokeza:

Taarifa ya Mapato

Baraza la Mji Kaskazini "A" kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 505,500,000 kutoka katika vyanzo vya mapato mbali mbali.

Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 699,307,178 zilikusanywa sawa na asilimia 138 ya makadirio.

Majibu ya Baraza

Ni kweli kwamba katika mwaka huo wa fedha Baraza hili lilikusanya mapato hayo kwa upungufu kutokana na sababu zifuatazo:

1. Kuandaa mpango mpya wa ukusanyaji wa mapato katika maeneo yaliyomo ndani

ya Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja.

2. Kufanya takwimu ya kuvitambua vianzio vyote vya mapato na kuvifikia.
3. Kuongezeka kwa wafanyakazi wa mkataba kwa lengo la kudhibiti mapato kutoka katika vianzio vyake
4. Kuandaa “operation” za mara kwa mara ili kubaini wanaokwepa kulipa ada na kuwachukulia hatua za kisheria.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Baraza la Mji Kaskazini “A” lilikusanya fedha kidogo kwa baadhi ya vianzio vyake kutokana na sababu zifuatazo:

    a. Kianzio cha mapato cha Uhifadhi wa Mazingira – Baraza liliingia mkataba na vikundi vya kijamii na hatimae lilipata hasara.
    b. Kianzio cha mapato cha Mchanga – Serikali haikutoa kipaumbele kuchimbwa mchanga katika Wilaya ya Kaskazini “A”.
2. Baadhi ya vianzio vya mapato havikutengewa bajeti ya kukusanya fedha wakati vianzio hivyo vilikusanya fedha nyingi. Vianzio vyenyewe ni:

    a. Kianzio cha Vibali vya ujenzi ambacho kilikusanya jumla ya Tsh. 137,123,000 kiwango ambacho ni kikubwa mno na hata kikaitia mashaka Kamati hii.
    b. Kianzio cha Matangazo ambacho kilikusanya jumla ya Tsh. 43,941,500, kianzio hiki hakikutengewa fedha kwa kuwa katika miaka ya nyuma kianzio hiki kilikuwa kimeingizwa kwenye kianzio cha Leseni.
3. Idadi ndogo ya Watendaji wanaohusika na shughuli ya ukusanyaji mapato.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na mapungufu hayo yaliyojitokeza Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Baraza la Mji Kaskazini “A” lifanye utafiti wa kina kabla ya kukasimu shughuli zake kwa mtu mwengine ili kuepuka kupata hasara.
2. Ili Baraza hili liweze kukusanya vyema mapato yake na kufika katika kila kianzio chake cha mapato kwa kuwa eneo la Wilaya hii ni kubwa ni busara kwa Serikali kuliongezea Baraza hili watendaji wenye taaluma ya ukusanyaji mapato.
3. Baraza la Mji Kaskazini “A” lihakikishe kuwa linakuwa makini wakati wa kuandaa bajeti ya Baraza ili kila kifungu kilichopo kitengewe bajeti yake.

Taarifa ya Matumizi

Baraza la Mji Kaskazini "A" kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 545,500,750 kwa kazi za kawaida.

Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 528,372,031 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 97 ya makadirio.

Majibu ya Baraza

Baraza la Mji Kaskazini 'A' Unguja limepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa kazi zake za kila siku za kuweza kutoa huduma bora kwa jamii miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

1. Kuwataka wafanyabiashara wakuu kulipia benki.
2. Kuongezeka kwa ubora wa utoaji wa huduma mbali mbali kwa jamii kwa kupitia sekta ya Afya, Elimu na Kilimo.
3. Kuishirikisha jamii katika shughuli mbali mbali za maendeleo na za kijamii ikiwemo kuibua vipaumbele vya Shehia na Wadi kwa lengo la kufanyiwa kazi na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja.

Pamoja na mafanikio mbali mbali yaliyopatikana, lakini pia, Baraza la Mji Kaskazini "A" Unguja linakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo:-

1. Baadhi ya vianzio vya mapato kuhamishwa kukusanywa kutoka Baraza la Mji na kupelekwa katika maeneo mengine. Mfano ukusanyaji wa leseni za vileo.
2. Kwa upande wa sekta za Ugatuzi:-
    - Sekta ya Elimu inakabiliwa na changamoto za Upungufu wa madarasa ya kusomea, vyoo kwa skuli za maandalizi na msingi pamoja na uchache wa walimu wa maandalizi.
    - Upungufu wa Watumishi na uchakavu wa miundombinu katika sekta ya Afya ikiwemo maji, umeme na majengo.
    - Upungufu wa pembejeo, matrekta na zana nyengine za kilimo kwa upande wa sekta ya Kilimo.
4. Uhaba wa ruzuku kutoka Serikali kuu katika kusaidia shughuli mbali mbali za kijamii na maendeleo.
5. Uelewa mdogo wa wananchi katika mfumo wa ugatuzi na ukusanyaji wa mapato.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Taarifa za hesabu ya matumizi zilizoainishwa kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) zinatofautiana na taarifa iliyoandikwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
2. Taarifa za hesabu ya Matumizi ya "Note" 5 zinatofautiana ndani ya Taarifa moja ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka jambo ambalo ni kinyume na taratibu za ufungaji wa hesabu. Kwa mfano; kwenye Taarifa ya Mlinganisho (Statement of Comparison) imeelezwa kuwa "Note" 5 imetumia jumla ya Tsh. 403,273,407.16 wakati kwenye Taarifa ya Mtiririko wa Fedha "Cash Flow" "Note" 5 imeelezwa kuwa imetumia jumla ya Tsh. 339,965,011.

Kutokana na kasoro hizo zilizobainika Kamati ya LAAC haikuendeleza majadiliano zaidi na imewataka Wahasibu wa Baraza hilo kuwa makini wakati wanaandaa taarifa mbali mbali za fedha.

Vile vile, Kamati ya LAAC imeishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwapatia mara kwa mara mafunzo Wahasibu wake ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao.

5.2.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI "B"

Maelezo ya Baraza la Mji Kaskazini "B" kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanasomeka kuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja.

Taarifa ya Mapato

Baraza la Mji Kaskazini "B" kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 1,136,113,071 kati ya hizo jumla ya Tsh. 746,509,000 ni kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya Tsh. 389,523,071 ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 1,463,600,076 zilikusanywa sawa na asilimia 129 ya makadirio, kati ya hizo jumla ya Tsh. 1,023,154,676 ni kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza na jumla ya shilingi 440,445,400 ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

Majibu ya Baraza la Mji Kaskazini "B"

Baraza la Mji Kaskazini "B" katika kipindi cha Julai - Juni 2017/2018 lilikadiria kukusanya Tsh. 1,136,113,071/=, kati ya hizo Tsh. 746,590,000/= kutoka katika vianzio vyake vya ndani na Tsh. 389,523,071/= ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini, na kufanikiwa kukusanya Tsh. 1,639,929,149/= sawa na asilimia 144 ya ongezeko la makadirio. Kati ya hizo Tsh. 1,210,689,749/= ni makusanyo ya ndani na Tsh. 429,239,400/= ni Ruzuku

kutoka Serikalini.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Baraza la Mji Kaskazini "B" lilipokea Ruzuku kutoka Tsh. 389,523,071/= hadi kufikia Tsh. 429,239,400/=, ongezeko la mapato lilitokana na maandalizi ya ugatuzi katika Baraza hilo.

Kwa upande wa mapato ya Baraza, yaliongezeka hadi kufikia asilimia 163 ya makadirio, kutokana na sababu zifuatazo:

1. Kuandaa mpango mpya wa ukusanyaji wa mapato katika Wadi.
2. Kugawanywa kwa watendaji wa nje katika Wadi ambao walikuwa wanalipwa kwa asilimia baada ya makusanyo ili kuziba mianya ya makusanyo na kuboresha vianzio vya ndani vya mapato,
3. Kuvifanyia uhakiki vianzio vyote vya ndani vya mapato.
4. Kuandaa 'operation' za mara kwa mara ili kuwabaini wanaokwepa kulipa ada na kuwachukulia hatua za kisheria.
5. Kutoa elimu juu ya ukusanyaji wa mapato kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar - ZBC.
6. Kuwafuata wafanyabiashara katika maeneo yao na kuwapatia elimu juu ya umuhimu wa kulipa ada kwa hiyari.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa kuna mapungufu ya kiuandishi kati ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka husika na Taarifa ya Hesabu za Mwaka (Financial Statement).

Kutokana na mapungufu hayo yaliyobainika, Kamati hii ilitaka kujua ni ipi taarifa sahihi kati taarifa mbili hizo, ambapo Watendaji wa Baraza hili waliieleza Kamati kuwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameandika taarifa ambazo zilikosewa ingawa alitakiwa kuandika taarifa zilizofanyiwa marekebisho na Taasisi yake.

Baada ya maelezo hayo ya Watendaji, Kamati ya LAAC ilitaka kuona barua inayothibitisha kauli hiyo, hata hivyo, Watendaji hao waliieleza Kamati hii kuwa mawasiliano hayo yalifanyika kwa njia ya mdomo na sio kwa maandishi. Kamati ya LAAC ilishindwa kukubaliana na maelezo ya Watendaji hao kwa kuwa hakukuwa na kielelezo chochote kinachothibitisha maelezo yao hayo.

Hivyo, kutokana na mapungufu hayo Kamati ya LAAC ililishauri Baraza hilo kujitahidi kutekeleza majukumu yake kwa maandishi kwani kikiwepo kielelezo kinarahisisha na kuthibitisha kile ambacho kinaelezwa, Hivyo basi, Watendaji wa Baraza hili watekeleze shughuli zao kwa mujibu wa taratibu zilivyowekwa na Serikali ili kuepusha dhana mbaya

zisizo na msingi.

Kwa ujumla, Kamati ya LAAC ilishindwa kufanya majadiliano zaidi juu ya kipengele hiki (Taarifa ya Mapato) kutokana na mapungufu hayo.

Taarifa ya Matumizi

Baraza la Mji Kaskazini 'B' kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiria kutumia jumla ya Tsh. 341,932,180 kwa kazi za kawaida na jumla ya Tsh. 256,592,820 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 322,293,085 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 94 ya makadirio na Tsh. 321,074,632 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 125 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Mji Kaskazini "B"

Baraza la Mji Kaskazini 'B' kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiria kutumia jumla ya Tsh.1,305,863,258/= kati ya hizo Tsh. 680,266,124/= kwa kazi za kawaida na jumla ya Tsh. 236,074,062.88/= kwa kazi za maendeleo na ugatuzi Tsh. 389,523,071.12/=.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya Tsh.529,924,923.27/= zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 78% ya makadirio na Tsh. 183,957,492.13/= zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 78% ya makadirio na Tsh. 429,239,400/= zilitumika kwa ugatuzi sawa na asilimia 110% ya makadirio.

Hivyo, Taarifa ya Matumizi iliyoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2017/2018, ukurasa Nam. 47 inaonesha taarifa ya fedha ya mwaka 2016/2017 na sio taarifa ya fedha ya mwaka 2017/2018.

Kwa upande wa mafanikio; Baraza la Mji Kaskazini 'B' limepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa kazi zake za kila siku za kuweza kutoa huduma bora kwa jamii miongoni mwa mafanikio yaliopatikana ni kama ifutavyo:-

1. Kuendelea kukusanya mapato kwa mfumo wa electronic pamoja nakuanzisha mfumo mpya wa utoaji lesseni kwa lengo la kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.
2. Kuongezeka kwa ubora wa utoaji wa huduma kwa jamii kwa kupitia sekta ya Afya, Elimu na Kilimo.
3. Kuimarika kwa ushirikishwaji wa wananchi katika kuibua Miradi inayoendana na utatuzi wa changamoto zinazowakabili.

Pamoja na mafanikio iliyoyapata Baraza la Mji pia limekabiliwa na changamoto zifuatavyo:-

1. Kushuka kwa mapato yanayotokana na mchanga kadri siku zinavyosonga.
2. Baadhi ya vianzio vya mapato kushuka kufuatia mabadiliko yaKanuni ya Huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2020, pamoja na baadhi ya vianzio vya mapato vimehamishwa katika ngazi ya Baraza.
3. Kwa upande wa sekta za Ugatuzi:-
    a. Sekta ya Elimu inakabiliwa na changamoto za Upungufu wa madarasa ya kusomea, vyoo kwa skuli za maandalizi na msingi pamoja na uchache wa walimu wa maandalizi.

    b. Upungufu wa watumishi na uchakavu wa miundombinu katika sekta ya Afya ikiwemo maji, umeme na majengo.

    c. Upungufu wa pembejeo, matrekta na zana nyengine za kilimo kwa upande wa sekta ya Kilimo.

4. Uelewa na mwamko mdogo wa wananchi katika mfumo mpya wa ukusanyaji na udhibiti wa mapato.
5. Mgongano wa Sheria za ukusanyaji wa mapato ambao kwa kiasi fulani unazorotesha ukusanyaji wa mapato katika Baraza.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kwa kuwa taarifa za fedha zilitofautiana kama ilivyoelezwa kwenye majibu ya Baraza la Mji Kaskazini "B" na kwa kuwa Kamati ya Baraza hutekeleza shughuli zake endapo kutakuwa na taarifa sahihi ya jambo linalolifanyia kazi, hivyo basi, Kamati ya LAAC haikuwa na maelezo zaidi juu ya kipengele hiki.

5.2.18: BARAZA LA MJI KATI

Maelezo ya Baraza la Mji Kati kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanasomeka kuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Kati.

Taarifa ya Mapato

Baraza la Mji Kati kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 500,000,000 kutoka katika vianzo vyake vya mapato ya ndani na ilikadiriwa kuingiziwa jumla ya Tsh. 611,263,925 ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 667,184,457 zilikusanywa kutoka katika vianzio vyake sawa na asilimia 133 ya makadirio na liliingiziwa jumla ya Tsh. 420,476,782 sawa na asilimia 68 pamoja na Tsh. 10,000,000 kutoka katika Kamati ya Udhibiti na Usimamizi wa Ujenzi (DCU).

Majibu ya Baraza la Mji Kati

Baraza la Mji Kati halikuwasilisha maelezo ya maandishi kwa Kamati hii ilipofanya ziara Barazani hapo kuhusiana na mapato iliyokusanya kama ilivyotarajiwa, isipokuwa kwamba, liliweza kujibu maswali ya Kamati na kuwasilisha vielelezo vilivyohitajika. Hivyo, maelezo ya kilichobainika katika ziara hiyo ni kama yalivyoelezwa kwenye kipengele cha Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati hii.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC iliridhika na majibu ya Halmashauri hii, hata hivyo, pamoja na kuridhika kwake huko ilibaini yafuatayo:

1. Kianzio cha mapato cha vibali vya ujenzi mapato yake yamepungua kutoka Tsh. 135,575,000 hadi Tsh. 74,316,400 kwa kuwa kianzio hicho kinasimamiwa na Kitengo cha Udhibiti na Usimamizi wa Ujenzi.
2. Baraza la Mji Kati limevuka malengo ya kukusanya mapato yake kutokana na sababu zifuatazo:
    a. Kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kulipa kodi
    b. Kufuatilia kwa karibu maeneo yote ya vianzio vya mapato.

Pamoja na juhudi hizo zilizochukuliwa na Baraza hilo, Kamati ya LAAC ililitaka Baraza kuongeza jitihada ya kukusanya mapato kwani bado kuna vianzio vya mapato ambavyo havijafikiwa, sambamba na kuwataka watendaji wa Baraza hili kuwa wabunifu ili kuliongezea mapato Baraza.

Taarifa ya Matumizi

Baraza la Mji Kati kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 1,111,263,925 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 1,059,921,182 zilitumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 95 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Mji Kati

Baraza la Mji Kati halikuwasilisha maelezo ya maandishi kwa Kamati hii ilipofanya ziara Barazani hapo kuhusiana na matumizi iliyofanya kama ilivyotarajiwa, isipokuwa kwamba, liliweza kujibu maswali ya Kamati na kuwasilisha vielelezo vilivyohitajika. Hivyo, maelezo ya kilichobainika kwa upande wa matumizi ni kama yalivyoelezwa kwenye kipengele cha Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati hii.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yamebainika:

1. Taarifa ya Hesabu ya Mwaka (Financial Statement) inaonesha kuwa jumla ya Tsh. 42,672,134 zimetengwa kwa ajili ya kazi za maendeleo, hata hivyo, fedha hizo zimetumika kwenye miradi midogo ya maendeleo ambayo kiuhalisia haikupaswa kutekelezwa kama ni miradi ya maendeleo.
2. Taarifa ya utekelezaji inaeleza kuwa Baraza hili lilitenga Tsh. 25,000,000 na kutumia Tsh. 27,240,500, hata hivyo, Taarifa ya Hesabu ya Mwaka haioneshi kama fedha hizo zilitengwa.

Kutokana na mapungufu hayo, Kamati ya LAAC ililishauri Baraza hili kuwa makini wakati wa kutekeleza majukumu yao ili kuepusha kasoro zisizo za msingi.

5.2.19: HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI

Taarifa ya Mapato

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 369,198,550 kutoka katika vyanzo vya mapato mbali mbali. Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 488,313,205 zilikusanywa sawa na asilimia 132 ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kusini

Mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Kusini yaliongezeka katika mwaka huo wa fedha baada ya Halmashauri hii kuanza kuifanyia kazi Kanuni ya Huduma za Serikali za Mitaa ambayo ilipelekea kuongezeka kwa baadhi ya tozo. Tozo zenyewe ni kama zifuatazo:

Nam.	Chanzo	Kiwango cha awali (Tsh.)	Kiwango kilichoongezeka (Tsh.)
1.	Leseni ya Hoteli ya nyota 4 na 5	4,000,000	5,000,000
2.	Leseni ya Hoteli ya nyota 2 na 3	3,000,000	4,000,000
3.	Leseni ya Hoteli ya nyota 1	2,000,000	3,000,000
4.	Leseni ya Hoteli ya nyota AAA	1,000,000	2,000,000
5.	Fomu za Vileo	100,000	150,000
6.	Leseni za maduka	600	620
7.	Usafirishaji maliasili ya kuni	50	300

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Halmashauri hii ilikuwa haipati fedha yoyote kutoka kwa kianzio cha rasilimali ya misitu. Hii ni kutokana na kuwa makusanyo yote ya kianzio hiki yalikuwa yanapelekwa Idara ya Misitu, hata hivyo, hivi sasa makusanyo ya kianzio hicho kinagawiwa na kupelekea Halmashauri hii kunufaika.

Kwa ujumla, Kamati ya LAAC iliridhika na majibu ya maswali mbali mbali iliyouliza na kujibiwa na Watendaji wa Halmashauri hii.

Taarifa ya Matumizi

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 816,327,100 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia 30 Juni 2018 jumla ya Tsh. 664,891,183 zilitumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 81 ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kusini

Halmashauri hii haikuwasilisha maelezo ya maandishi kwa Kamati hii kuhusiana na matumizi iliyoyafanya kama ilivyotarajiwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

1. Watendaji wa Baraza hili walishindwa kuipatia maelezo ya kina Kamati ya LAAC juu ya matumizi ya Tsh. 295,692,623, ingawa Taarifa ya Hesabu ya Mwaka inaonesha kuwa matumizi hayo yamefanyika, isipokuwa kwamba, matumizi hayo yalielezwa kiujumla jumla.
2. Vile vile, kutokana na ufinyu wa muda Kamati ya LAAC ilishindwa kufuatilia kwa kina matumizi ya kazi za maendeleo ambayo ni jumla ya Tsh. 150,305,000.
3. Kiujumla, Kamati ya LAAC haikuridhika na matumizi yaliyofanywa na Baraza la Mji Kusini.

5.2.20: BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

Taarifa za Mapato

Baraza la Mji Chake Chake katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiria kukusanya Tsh. 390,000,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya Tsh. 440,228,787 zilikusanywa sawa na asilimia 112.88 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake

Baraza la Mji Chake Chake halikuwasilisha taarifa za mapato moja kwa moja kwa Kamati, isipokuwa kwamba, taarifa za mapato zilipatikana kufuatia mahojiano na Kamati hii.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalijitokeza:

4. Mfumo wa uwekaji wa majalada haukuwa mzuri jambo lililopelekea kutopatikana kwa nyaraka mbali mbali zilizohitajika na Kamati hii.
5. Asilimia kubwa ya nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati zilikuwa haziendani na mahitaji au jambo halisi lililokusudiwa.
6. Waraka wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 uliowasilishwa na kuridhiwa na Kikao cha Madiwani wa Baraza la Mji Chake Chake haukuonesha mnyambuliko halisi wa mapato na matumizi wa Baraza hilo.
7. Taarifa za nyaraka mbali mbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati zilikuwa zinatofautiana kwenye kipengele cha mapato na matumizi ya mwaka husika.
8. Baadhi ya nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati zilikuwa na viashiria kuwa nyaraka hizo ziling'ushiwa jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha 24 cha Sheria ya Kinga, Fursa na Uwezo wa Wajumbe ya mwaka 2007.

Kutokana na kasoro hizo zilizojitokeza Kamati ya LAAC ilishindwa kuendelea kufanyakazi na iliakhirisha kikao hicho bila ya mafanikio yaliyokusudiwa, kwa msingi huo, Taarifa za Matumizi nazo hazikuweza kujadiliwa. Hivyo, Kamati hii haikuweza kuyafatilia mapato na matumizi ya Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

5.2.21: BARAZA LA MJI MKOANI

Taarifa za Mapato

Baraza la Mji Mkoani katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiria kukusanya Tsh. 230,000,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya Tsh. 295,034,898.26 zilikusanywa sawa na asilimia 128.28 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Mji Mkoani

Baraza la Mji Mkoani halikuwasilisha taarifa za mapato moja kwa moja kwa Kamati, isipokuwa kwamba, taarifa za mapato zilipatikana kufuatia mahojiano na Kamati hii.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yamebainika:

1. Baraza la Mji Mkoani limevuka malengo ya kukusanya mapato kutokana na sababu zifuatazo:
    a. Lilifanya zoezi la kuwatambua wafanyabiashara wote wa Wilaya ya Mkoani ambao wanapaswa kulipa ada mbali mbali; na
    b. Lilibadilisha kanuni za ada za ukusanyaji wa mapato.

2. Vianzio vya mapato ya ndani vya Baraza hili haviko imara (unstable) jambo linalopelekea Baraza hili kupanga makadirio ya makusanyo kwa kubahatisha tu.
3. Kianzio cha mapato cha Soko la Samaki la Mbuyuni limevuka malengo ya ukusanyaji kwa kuwa katika soko hilo kuna diko.
4. Kianzio cha mapato cha Milango ya Maduka hakikukusanya vyema kwa kuwa baadhi ya milango haikupata wateja, pia na baadhi ya wateja hawakulipa kodi kwa wakati.
5. Ruzuku iliyoingizwa kutoka Serikalini ni jumla ya Tsh. 1,030,408,082, hata hivyo, fedha hizo hazikuoneshwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wala kwenye Bajeti ya Baraza la Mji Mkoani, isipokuwa kwamba, ilioneshwa kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka pekee, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa kihesabu.
6. Bajeti ya Ruzuku huwa hawaiwasilishi kwa Baraza la Madiwani kitendo ambacho ni kinyume na utaratibu wa uwasilishaji wa bajeti.
7. Mapato yanayotokana na Taasisi zilizogatuliwa yanaendelea kukusanywa katika Wizara husika, kitu ambacho ni kinyume na utaratibu.
8. Mkataba wa ukodishwaji wa Kware iliopo Mwambe haukuwekwa saini na upande mmoja wa mkataba huo.
9. Baadhi ya mikataba sehemu ya jina limewekwa kwa “slag” badala ya kuandikwa kwa mkono au kuchapwa.

Kwa ujumla, Kamati ya LAAC ililishauri Baraza la Mji Mkoani kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo ili liweze kutekeleza shughuli zake kitaalamu pamoja na kuepuka karoso zisizo na msingi.

Taarifa za Matumizi

Baraza la Mji Mkoani katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 1,178,216,117,73 kwa kazi za kawaida na jumla ya Tsh. 175,300,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia 30 Juni, 2018 jumla ya Tsh. 1,120,009,160.98 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ikiwa ni sawa na asilimia 95.1 ya makadirio na Tsh. 205,519,200 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 117.2 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Mji Mkoani

Baraza la Mji Mkoani liliieleza Kamati kuwa katika mwaka huo wa fedha lilitekeleza miradi ifuatayo:

Nam.	Jina la Mradi	Makisio (Tsh.)	Matumizi Halisi (Tsh.)	Maelezo
1.	Kusaidia miradi ya jamii katika Wadi tano	35,000,000	35,000,000	Miradi iliyotekelezwa ni: (i) Ujenzi wa banda la vyumba viwili vya Skuli ya Msingi Mizingani; (ii) Ujenzi wa matungu sita ya vyoo vya Skuli ya Msingi Ngwachani; (iii) Ukarabati wa barabara ya Bububu – Shaangini; (iv) Ujenzi wa vyoo vya Skuli ya Makombeni; na (v) Ujenzi wa msingi wa maji taka Mtambile.
2.	Kufanya ukarabati wa Soko la Samaki na Matunda Kangani na Ukarabati wa barabara ya Mbuyuni - Chokaani	51,000,000	56,707,500	Ukarabati wa Soko la Samaki na Matunda Kangani umefanyika na Barabara ya Mbuyuni – Chokaani imetiwa fusi.
	JUMLA	**86,000,000**	**91,707,500**	

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC katika kufuatilia hoja hii ilibaini kuwa kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) ya Baraza la Mji Mkoani kifungu cha matumizi ya kazi za maendeleo yamechanganyishwa na matumizi ya kifungu cha ununuzi wa

vifaa vya ofisi jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

Pamoja na kasoro hiyo iliyobainika na Kamati, Kamati hii ilishindwa kuendelea kufanya shughuli zake baada ya Watendaji wa Baraza hili kushindwa kujibu maswali ya Kamati kwa kisingizio kuwa asilimia kubwa ya Watendaji waliokuwepo kikaoni hapo ni wapya.

Kamati ya LAAC haikukubaliana na kauli hiyo hasa ikizingatiwa kuwa katika barua yake ililitaka Baraza hili kuwashirikisha Watendaji wote waliohusika kiutendaji katika mwaka wa fedha 2017/2018 ili kurahisisha shughuli hiyo pamoja na kupata taarifa sahihi kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinavyolekeza.

Baada ya Kamati kuhoji juu ya kutokutekelezwa kwa maelekezo iliyotoa, Watendaji wa Baraza walieleza kuwa waliwasiliana na aliyekuwa Mkurugenzi wa Baraza hilo Ndg. Rashid Abdalla Rashid ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Jimbo la Kiwani. Hata hivyo, Mheshimiwa huyo hakuhudhuria kikao hicho kama alivyoombwa na alishindwa hata kutoa dharura ya kutokuhudhuria kwake kwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Kutokana na hali hiyo Kamati ya LAAC iliakhirisha kikao chake bila ya mafanikio yaliyotarajiwa.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inawashauri wale wote walioshiriki katika kutekeleza shughuli za kitaifa kwa namna moja au nyengine kutoa mashirikiano yao ya dhati pale wanapohitajika juu ya jambo ambalo walilisimamia au walilitekeleza kwa maslahi ya nchi na taifa kwa ujumla.

5.2.22: BARAZA LA MJI WETE

Taarifa za Mapato

Baraza la Mji Wete katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiria kukusanya Tsh. 250,000,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya Tsh. 257,108,143 zilikusanywa sawa na asilimia 103 ya makadirio.

Majibu ya Baraza la Mji Wete

Baraza la Mji Wete lilikiri kukadiriwa kiasi hicho cha fedha katika mwaka wa fedha husika, isipokuwa kwamba, liliweza kukusanya jumla ya Tsh. 257,528,048.

Vile vile, baada ya mfumo wa ugatuzi kuanza rasmi katika mwezi wa Julai, 2017 Baraza hili lilikadiriwa kupata Ruzuku ya Tsh. 934,406,000 kutoka Serika Kuu.

Baraza la Mji Wete lilifanikiwa kuvuka malengo ya kukusanya mapato yake kutokana na mashirikiano mazuri kati ya Watendaji na Waheshimiwa Madiwani hasa katika kufuatilia ada ya ujenzi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yamebainika:

1. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka ya Baraza la Mji Wete kiwango sahihi kilichokusanywa ni Tsh. 257,108,143 kama ilivyoeleza kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na sio kama ilivyoelezwa na Baraza hili kwenye taarifa yao waliyoiwasilisha mbele ya Kamati.

   Aidha, kiwango hicho cha fedha (Tsh. 257,108,143) kilitajwa kwenye Kiambatanisho No. 1 kilichowasilishwa na Baraza hili mbele ya Kamati hii.

2. Kianzio cha mapato cha Soko hakikuweza kuvuka malengo ya ukusanyaji kwa kuwa Soko hilo lilikabidhiwa kwa Baraza hili katika ya mwaka wa fedha husika.

Pamoja na Kamati kuandika uchunguzi na mapendekezo hayo, kwa masikitiko makubwa Kamati ilishindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na kushuhudia mkanganyiko mkubwa wa taarifa za Baraza hili, kwani taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka (Financial Statement), Taarifa ya Utekelezaji ya Mwisho wa Mwaka na Taarifa ya Majibu ya Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, waliyoiwasilisha mbele ya Kamati.

Hali hiyo iliikwaza Kamati kiutendaji na hivyo kulazimika kuakhirisha kikao bila ya mafanikio.

5.2.23: HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

Taarifa za Mapato

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiria kukusanya Tsh. 170,000,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya Tsh. 185,348,155.19 zilikusanywa sawa na asilimia 109.03 ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni lilikiri kukadiriwa na kukusanya kiasi hicho cha fedha katika mwaka wa fedha husika.

Vile vile, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni liliieleza Kamati hii kuwa lilikusanya zaidi katika mwaka huo wa fedha kutokana na sababu zifuatazo:

1. Mwamko wa wafanyabiashara kulipia ada na tozo mbali mbali kwa wakati. Mwamko huu ulitokana na jitihada maalum zilizochukuliwa kwa pamoja baina ya

Ofisi ya Halmashauri na Waheshimiwa Madiwani.
2. Utoaji wa elimu kwa wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kulipa ada zao kwa wakati.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Kianzio cha mapato cha Mauzo ya Mazao kilivuka malengo ya ukusanyaji kwa kuwa mwaka huo ulikuwa msimu mkubwa wa zao la karafuu.
2. Kianzio cha mapato ya Ada ya Mnada makusanyo yake yamepungua kwa kuwa katika mwaka huo wa fedha Halmashauri hii ilikuwa na diko moja tu la Shumba Mjini, hivyo, samaki waliuzwa zaidi katika diko hilo.
3. Pamoja na juhudi mbali mbali zilizochukuliwa na Halmashauri, Kamati ya LAAC imebainikuwa bado vipo vianzio vya mapato ambayo vimetelekezwa na Halmashauri hii kwa mfano, Kituo cha gari na Soko la Matunda na Mbogamboga vilivyopo karibu na Afisi ya Mkuu wa Wilaya.

Hivyo, Kamati ya LAAC iliitaka Halmashauri hii kuhakikisha kuwa inavifikia vianzio vyake vyote vya mapato ili Halmashauri hii iweze kutekeleza vyema shughuli zake.

Taarifa ya Matumizi

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni katika mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 660,048,000 kwa kazi za kawaida na jumla ya Tsh. 249,200,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia 30 Juni, 2018 jumla ya Tsh. 606,581,039 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ikiwa ni sawa na asilimia 91.8 ya makadirio na Tsh. 228,566,380.80 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 71.7 ya makadirio.

Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni katika mwaka huo wa fedha lilitekeleza yafuatayo:

Nam.	Shughuli Mahsusi	Maelezo
1.	Kuendeleza huduma za jamii	Uendelezaji wa ujenzi wa Skuli ya Chimba na Mjini Wingwi, Ukarabati wa kituo cha Afya Mkia wa Ngombe na nyumba ya Daktari Maziwa Ngombe, Uekaji wa matangi 4 ya kuhifadhia maji Micheweni na Skuli ya Mtamani, ujenzi wa choo cha kituo cha Afya Msuka, ukamilishaji wa

		Soko la Samaki Njuguni, ukarabari wa barabara ya Kiuyu kwa manda – Makangale na uanzishwaji wa maeneo ya maegesho Micheweni.
2.	Kuendeleza ujenzi wa ukumbi wa mikutano wa Micheweni	Kazi ya uwekaji wa milango na madirisha imefanyika.
3.	Kuipatia afisi huduma za uendeshaji na vitendea kazi	Huduma na uendeshaji na vitendea kazi vimepatikana kwa wakati.
4.	Kutoa huduma lishe kwa wanafunzi wa elimu ya maandalizi	Wanafunzi 1,578 wa maandalizi wamepatiwa huduma ya lishe, Wanafunzi wapya 1001 wa maandalizi, sawa na asilimia 100 na wanafunzi 4081 wa msingi sawa na asilimia 97 wameandikishwa.
5.	Kuwalipa Wafanyakazi stahiki zao	Walimu 225 wamelipwa nauli (bus fare), wasaidizi 182 wa vituo vya TUTU wamepatiwa maslahi yao pamoja na wafanyakazi 139 wamepatiwa huduma ya likizo.
6.	Kutoa huduma ya ugani na chanjo kwa mifugo	Mifugo 33,294 wakiwemo mbwa 458 na kuku 32,836 wamepatiwa chanjo ya kichaa cha mbwa na magwa pamoja na kutoa ushauri kwa wafugaji 5,882 juu ya mbinu bora ya ufugaji.
7.	Kuotesha miche ya matunda na misitu pamoja na uhifadhi wa misitu	Mikarafuu 6,900, miembe 165, mistafeli 320, midalasini 680, mikungu 675, mivinje 2,070, matunda mchanganyiko 2,649. Aidha jumla ya miche 3,600 ya mikarafuu imegaiwa kwa wananchi na miche 500 ya misitu imepandwa

		katika maeneo ya barabara kuu ya Wingwi – Konde.
8.	Kutoa elimu kwa Wakulima	Jumla ya ekari 1031 zimechimbuliwa ikiwa ekari 986 zimelimwa kwa jembe la mkono na ekari 45 zimelimwa kwa kutumia trekta.
9.	Kuendeleza vikundi vya ukulima wa mwani na ufugaji wa samaki	Vikundi vya ufugaji wa samaki vya shehia ya Micheweni na Sizini vimepatiwa mipira na pampu za kutolea maji.
10.	Kuvipatia Vituo vya Afya vifaa tiba	Glucose plus mshine, frusted slide, blood grouping, mipira ya kuzalishia. UPT, Delivery set, vacutener tube, HB strips, aoutoclave, Cord, VDRL na Oxytocin.
11.	Kuendeleza huduma za chanjo na huduma za mkoba (outreach)	Mama wajawazito 4,954 na watoto 5,368 wamepatiwa chanjo ikiwemo BCG 6,188, Penta 1 ni 5,368, Penta 3 ni 5,046 na Surua 5,627.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa taarifa ya makadirio ya bajeti ya matumizi ya kazi za maendeleo imetofautiana baina ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Taarifa ya Mwelekeo wa Bajeti iliyowasilishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni mbele ya Kikao cha Madiwani. Hii ni kutokana na kuwa Taarifa ya Mwelekeo wa Bajeti inaeleza kuwa matumizi ya kazi za maendeleo ni Tsh. 80,000,000 wakati Ripoti ya Mdhibiti inaeleza kuwa ni Tsh. 249,200,000.

Kamati ya LAAC baada ya kuhoji juu ya utofauti huo ilielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni lilipokea fedha za ziada kwa ajili ya ugatuzi fedha ambazo hazikuwemo kwenye bajeti ya awali ya Halmashauri hii.

Kwa ujumla Kamati ya LAAC iliridhika na utendaji wa Baraza la Mji Micheweni.

Mengineyo

Kamati ya LAAC baada ya kumaliza shughuli ya kufuatilia hoja ilifanya mazungumzo na Madiwani na yafuatayo yalijitokeza:

1. Posho la Madiwani ni dogo sana, hivyo, Kamati inapendekeza posho hilo litoke Serikalini kama zinavyotoka posho za Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge.

2. Fedha kutoka Serikalini zinachelewa kupatikana jambo ambalo linapelekea kuzorota kwa shughuli za Baraza. Hivyo, Kamati ya LAAC iliishauri Serikali kuhakikisha kuwa inalipatia Baraza hili fedha zinazoomba kwa wakati ili liweze kutekeleza shughuli zake bila ya usumbufu wowote.

3. Kuna viashiria kwa Baraza la Madiwani la Baraza hili kuamua mambo kwa pamoja na baadae maamuzi hayo yakakataliwa na Mwenyekiti wa Baraza na Mkurugenzi pekee.

3.1: SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umefanya uchambuzi wa ukusanyaji wa mapato ya Shirika la Umeme Zanzibar na kubaini mapato hayo yameongezeka hadi kufikia Tsh. 120,870,387,033 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na Tsh. 114,591,339,203 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la Tsh. ,279,047,830 sawa na asilimia 5.5 ya ongezeko.

Majibu ya Shirika

Mapato halisi ya mauzo ya Umeme na Mapato mengineo kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2019/2020 ni jumla ya TZS 120.870 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 102.849 bilioni zimetokana na mauzo ya umeme na TZS 18.021 bilioni zimetokana na mapato mengineo.

Ongezeko hilo la mapato linatokana na juhudi za Shirika la Umeme katika kutekeleza mikakati yake iliyojiwekea katika kipindi hicho kama ifuatavyo:-

1. **Ubadilishwaji wa Mita za zamani (Post Paid) na kuwekwa mita mpya za TUKUZA (Prepaid)**.

   Shirika la Umeme hadi kufikia Juni 2020, lilikamilisha zoezi la kuzibadilisha mita zilizokuwa zikitumia mfumo wa zamani (post-paid) zote Unguja na Pemba kwa wateja wake wote wadogo na wakati kwa kuwafungia mita za TUKUZA (Pre-paid) hali iliyoimarisha upatikanaji wa mapato.

2. **Ubadilishwaji wa Mita Mbovu**

   Shirika la Umeme katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, liliendeleza mkakati wake wa ubadilishwaji wa mita mbovu mitaani ambapo jumla ya mita 26,574 zilibadilishwa.

3. **Uimarishwaji wa Miundo Mbinu ya Umeme**

   Shirika la Umeme limeendelea za zoezi la kuifanyia matengenezo na ujengaji wa miundo mbinu yake ya umeme mikubwa na midogo ambapo jumla ya 75.43km ziliimarishwa, urekebishwaji wa transfoma zilizozidiwa katika maeneo tofauti ambapo jumla ya transfoma 93 zilirekebishwa na ubadilishwaji wa nguzo mbovu ambapo jumla ya nguzo 1553 zilibadilishwa.

4. **Ukaguzi wa Wateja wa mara kwa mara**

   Shirika kupitia slogan yake ya Umeme day limefanya ukaguzi wa wateja wake ili kuthibiti wizi wa umeme unaofanywa na wateja wasio waaminifu. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 jumla ya wateja waliokaguliwa ni 113,000 na walikutikana na makosa ni 105 ambapo hatua za kuwalipisha makisio ya upotevu yalifanyika.

5. **Ongezeko la wateja wapya**

   Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 idadi ya wateja wapya waliosajiliwa iliongezeka na kufikia 199,004 ukilinganisha na mwaka 2018/2019 186,794. Hivyo, jumla ya wateja wapya 13,992 waliungiwa umeme ukilinganishwa na wateja 12,388 kwa mwaka 2018/2019.

6. **Kupungua kwa kiwango cha upotevu wa Umeme**

   Kupungua kwa kiwango cha upotevu kutoka asilimia 18 hadi kufikia asilimia 17 katika robo ya mwisho ya mwaka 2019/2020 hali hii ilipelekea kuongezeka kwa makusanyo yaliyotoka na udhibiti wa upotevu.

Licha ya juhudi hizo zilizochukuliwa na Shirika hili, hata hivyo, Shirika halikuweza kufikia malengo yake ya ukusanyaji wa mapato kutokana na changamoto zilizojitokeza zikiwemo:-

7. **Maradhi ya Uviko 19**

   Karibu asilimia 30 ya mapato ya Shirika la Umeme yanatokana na hoteli za kitalii zilizopo Zanzibar na kwa kipindi cha miezi mitatu ya mwisho wa mwaka hoteli hizo zilifungwa hali iliyopelekea kushuka kwa mapato ya Shirika.

8. **Baadhi ya Taasisi za Serikali kutolipa matumizi yao ya Umeme**

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Shirika limekosa jumla ya TZS 7.2 bilioni kutokana na baadhi ya Taasisi za SMZ na SMT kutokulipia huduma ya matumizi ya umeme.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC ilikubaliana na maelezo yaliyotolewa na Shirika hili, hata hivyo, pamoja na kukubaliana kwake huko ilisisitiza mambo yafuatayo:

1. Shirika liendelee na juhudi ya kuwaungia umeme wananchi kwa kuwa bado huduma hii inahitajika lakini pia italiongezea mapato Shuirika hili.

2. Kwa kuwa baadhi ya Taasisi za Umma hazilipi huduma ya matumizi ya umeme ipasavyo, ingawa fedha hizo hutengwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na Bodi za Taasisi zinazojitegemea, hivyo basi, Shirika hili lizifungie Taasisi ambazo sio nyeti mita za pre paid ili kuziepusha Taasisi hizo kuwa na madeni yasiyokuwa na msingi.

3. Shirika lizidishe juhudi ya kufanya uchunguzi mara kwa mara ili kuwabaini wezi wa umeme pamoja na kugundua upotevu wa umeme.

4. Kwa kuwa waya uliopo unahimili matumizi ya kawaida ya Mega watt 100 na kwa sasa tunatumia Mega watt 70 hadi 88 kwa siku za sikukuu na kwa kuwa muelekeo wa Serikali ni kuwa na Zanzibar ya viwanda na kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wameshajihishika kutumia huduma ya umeme. Hivyo basi, Shirika liendelee na juhudi zake ilizozianzisha za kutumika kwa umeme wa jua pamoja na kubadilisha waya uliopo na kuweka waya mpya wenye Mega watt kubwa zaidi ili kuepusha kuutumia waya huo kinyume na uwezo wake na kupelekea waya huo kupata hitilafu na hatimae kutolewa huduma ya umeme kwa njia ya mgao.

5. Kwa kuwa malipo ya huduma ya matumizi ya umeme “service charge” inajulikana kwa kuwa huduma hii hulipiwa kila mteja anavyonunua umeme, hivyo, mapato ya kifungu hiki yasiunganishwe kwenye kifungu cha “Sales of Energy” na badala yake kiwekwe kuwa ni kifungu kinachojitegemea.

Taarifa ya Matumizi

Ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia Tsh. 101,007,122,054 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na Tsh. 95,776,615,528 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni ongezeko la Tsh. 5,230,506,526 sawa na asilimia 5.5.

Majibu ya Shirika

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Shirika la Umeme Zanzibar limetumia jumla ya TZS 101.007 bilioni kwa ajili ya uendeshaji wa Shirika hilo ikiwa ni ongezeko la TZS 6.279 ukilinganisha na TZS 95.776 kwa mwaka wafedha 2018/2019 zilizotumika.

Ongezeko la matumizi hayo ukilinganisha mwaka 2019/2020 na mwaka 2018/2019 linatokana na sababu kubwa zifutazo:-

1. **Ununuzi wa umeme kutoka TANESCO**

Kiwango cha uniti kilichonunuliwa kutoka TANESCO kiliongezeka na kufikia Uniti 454,054,000 kwa mwaka 2019/2020 ambapo jumla ya TZS 66 bilioni zilitumika ukilinganisha na uniti 371,136,505 ambapo jumla ya TZS 61 bilioni zilitumika kununuwa umeme kutoka TANESCO.

2. **Gharama za Uchakavu wa Rasilimali za kudumu (Depreciation)**

Uchakavu unaotokana na kupungua thamani kwa Rasilimali (Assets) ambazo zinatumika kuzalisha mapato zimeongezeka na kufikia TZS 13.775 bilioni ukilinganisha na TZS 13.456 bilioni mwaka 2018/2019. Hii inatokana na ongezeko la Rasilimali mpya zilizoingia kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

3. **Gharama za matengenezo ya miundo mbinu na Magari ya Shirika la Umeme**

Gharama za utengenezaji wa magari ya Shirika zimeongezeka na kufikia TZS 1.410 bilioni ukilinganishwa na TZS 1.333 bilioni kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hii ni kawaida kwa mafuta na vifaa vya magari kubadilika bei kwani hununuliwa kwa bei iliopo sokoni (market price).

4. **Gharama za Ununuzi wa gari, vifaa vya Umeme, na Mitambo**

Shirika la Umeme Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020 limefanya ununuzi wa gari, vifaa vya umeme na mitambo vyenye thamani ya TZS 5.93. Hii inatokana ongezeko la vifaa vilivyohesabiwa ghalani ambapo vimefikia thamani ya TZS 17.182 bilioni hadi Juni 2020 ukilinganisha na TZS 11.252 bilioni kwa hesabu zinazoishia June 2019.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC imeridhika na majibu ya Shirika hivyo haikuwa na maelezo zaidi.

3.1.1 Mapungufu katika daftari la kuhifadhia Mali za kudumu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Umeme Zanzibar limenunua mali za kudumu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020. Hata hivyo, daftari la mali za kudumu halijafanyiwa maboresho ya kuziingiza mali mpya na kuzitoa zilizochakaa au

kuharibika, jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa ugumu wa kutambua mali zilizokosekana, mali zilizoharibika, mali zilizopo na hali ya uchakavu au uzima wa mali zenyewe pamoja na kutokufahamika nambari za utambulisho wa mali hizo, kutokana na dosari hizo kumepelekea kujitokeza kwa udhaifu katika udhibiti wa mali za Shirika.

Katika kuimarisha udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa mali za kudumu, ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe katika kufanyia maboresho daftari la kuhifadhia mali za kudumu kwa kuingiza taarifa zilizo sahihi kwa mujibu wa usahihi wa mali zilizopo.

Majibu ya Shirika

Shirika la Umeme Zanzibar limekwisha kamilisha taratibu za uimarishaji wa daftari la Mali za kudumu kwa kutoa vifaa vilivyochakaa au kuharibika na kuingiza vifaa vipya katika daftari hilo, ambapo marekebisho hayo yamefanyika ndani ya mfumo wa kielektroniki SAP unaotumika kutunza mali za Shirika.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini mambo yafuatayo:

1. Shirika la Umeme lilikuwa linamiliki gari chakavu ambapo baadhi ya vifaa vya gari hizo vilikuwa vinatumika ndani ya Shirika hilo kama ni vipuri “spare”.
2. Shirika la Umeme lilikuwa lipo katika hatua ya kuomba kuuzwa au kutoa (despose) gari hizo, hata hivyo, Shirika hili lilipokea taarifa kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusiana na kusimamishwa kwa zoezi la kutoa gari. Hata hivyo, hatua iliyofuata ni kuchukuliwa kwa gari hizo chakavu na kupelekwa katika viwanja vya Ofisi ya Mamlaka ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar – ZAECA kwa agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar lililosimamiwa na Mkuu wa Magari wa Ofisi ya Rais – Ikulu.

   Jumla ya gari chakavu 11 za Shirika hili zilichukuliwa ambapo Meneja Mkuu wa Shirika hilo aliwaarifu watendaji wake juu ya kadhia hiyo. Gari zenyewe ni hizi zifuatazo:

   a. SLS 103A ESCUDO
   b. SLS 122A ESCODO
   c. SLS 158B TATA CARRY
   d. SLS 130B NISSAN HARDBODY
   e. SLS 142B HILUX
   f. SLS 137A PRADO

g. SLS 139B HILUX
h. SLS 123A RAV 4
i. SLS 160B HILUX VIGO
j. SLS 170A TERRANO
k. DFP 5493 NISSAN HARDBODY

3. Kati ya gari hizo 11 zilizochukuliwa ni gari 5 tu ambazo Shirika hili lilitakiwa kukabidhi Kadi na Funguo za gari hizo kwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia barua ya tarehe 23 Septemba, 2021 yenye kumbukumbu Namba BA.26/454/01/21/12 iliyoandikwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kutumwa kwa Meneja Mkuu wa Shirika hilo. Gari zenyewe ni :
   a. SLS 103A ESCUDO
   b. SLS 122A ESCODO
   c. SLS 158B TATA CARRY
   d. SLS 130B NISSAN HARDBODY
   e. SLS 160B HILUX VIGO

4. Shirika la Umeme halina taarifa kuhusiana na hatma ya gari zake 6 zilizopelekwa katika kiwanja cha ZAECA. Gari zenyewe ni:
   a. SLS 142B HILUX
   b. SLS 137A PRADO
   c. SLS 139B HILUX
   d. SLS 123A RAV 4
   e. SLS 170A TERRANO
   f. DFP 5493 NISSAN HARDBODY

5. Barua ya tarehe 23 Septemba, 2021 yenye kumbukumbu Namba BA.26/454/01/21/12 iliyoandikwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kutumwa kwa Meneja Mkuu wa Shirika hili ziliorodhesha gari 3 ambazo hazipo chini ya himaya ya Shirika hili na wala Shirika halijui gari hizo zipo chini ya Taasisi gani. Gari zenyewe ni:
   a. SLS 132 B NISSAN BODY
   b. SLS 157B SUPER ACE (TATA)
   c. SLS 229B NISSAN DOUBLE CABIN

Kutokana na uvumbuzi huo, na kwa kuwa Shirika la Umeme halikuwa na majibu ya kina kwa baadhi ya maswali ya Kamati. Kamati hii ilihisi ni vyema ikaandaa kikao cha pamoja kitakachowajumuisha Watendaji wa Shirika hili, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Ikulu na Mkuu wa Usafiri wa Ofisi ya Rais – Ikulu ili kujiridhisha na kile kilichofanyika ambapo, tarehe 02 Februari, 2022, Kamati iliandaa kikao hicho na yafuatayo yalibainika:

1. Tarehe 10 Februari, 2021, Serikali ilitoa agizo la kuchukuliwa gari za Serikali zilizokuwa zikitumiwa na Naibu Mawaziri, Naibu Makatibu Wakuu na gari zote zilizotelekezwa kwenye maegesho na magereji.
2. Baadhi ya gari zilizochukuliwa zikiwemo gari za ZECO na ZAWA zilikuwa zinatumiwa na Taasisi hizo kama kawaida, nyengine zilikuwa zinasubiria vifaa kwa ajili ya matengenezo na nyengine ilikuwa ishauzwa.

Ufuatao ni uhalisia wa hali (condition) za gari za ZAWA zilizochukuliwa:

Gari zilizochukuliwa ambazo ni nzima

Nam	Namba ya gari	Kabila ya gari	Sehemu iliyokuwa inatumika
1.	S L S 159 A	PRADO	MKURUGENZI FEDHA NA MIPANGO
2.	S L S 176 A	SUZUKI SCUDO	AFISI YA MHASIBU- ZAWA

Gari zilizokuwa kwenye matengenezo

Nam	Namba ya gari	Kabila ya gari	Sehemu iliyokuwa inatumika
1.	S L S 198 B	TOYOTA TOWN ACE	WILAYA YA KASKAZINI "A" -ILIBEBWA IKIWA NA FUNDI KWENYE MATENGENEZO NA VIFAA VYAKE
2.	S M Z 5362	TOYOTA LAND CRUISER	IDARA YA UFUNDI, KWA KAZI ZA UFUNDI - MTANDAO WA MAJI

Gari zilizokuwa hazijatengenezwa (zinasubiri vifaa)

Nam	Namba ya gari	Kabila ya gari	Sehemu iliyokuwa inatumika
1.	S L S 190 B	TOYOTA TOWN ACE	WILAYA YA KASKAZINI "B" - OPERESHENI ZA WILAYA
2.	S L S 202 B	TOYOTA TOWN ACE	WILAYA YA KUSINI - OPERESHENI ZA WILAYA
3.	S L S 225 B	TOYOTA HILUX	WILAYA KASKAZINI "B" - OPERESHENI ZA WILAYA
4.	S L S 151 B	NISSAN HARD BODY	AFISI KUU - IDARA YA RASILIMALI MAJI

5.	SLS 158 A	SUZUKI VITARA	

Gari zilizokuwa mashine zake mbovu

Nam	Namba ya gari	Kabila ya gari	Sehemu iliyokuwa inatumika
1.	S L S 160 A	NISSAN MINI BUS	IDARA YA BIASHARA - KUSOMA MITA, KUSAMBAZA BILI NA UKUSANYAJI MAPATO
2.	S L S 166 B	NISSAN HARD BOD	AFISI KUU - KAZI ZA OPERESHENI ZA UFUNDI/ BOMBA KUU
3.	DFP	NISSAN HARD BODY	AFISI KUU
4.	S L S169 B	NISSAN HARD BODY	AFISI KUU - MRATIBU AFISI ZA MAJI WILAYA

Gari iliyokuwa matengenezo yake makubwa

Nam	Namba ya gari	Kabila ya gari
1.	SLS 175 A	HOND CRV

Kwa upande wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) gari zilizochukuliwa zilikuwa na hali zifuatazo:

Gari zilizokuwa kwenye matengenezo

Nam.	Nambari ya gari	Sehemu iliyokuwa inatumika	Kabila la Gari
1.	SLS 160B	Uendeshaji `	Hilux Vigo
2.	SLS 139B	Uendeshaji	Hilux
3.	DFP 5493	Uendeshaji	Nissan Hard Body
4.	SLS 143B	Uendeshaji (Mains}	
5.	SLS 170A	Uendeshaji (Upimaji)	Terrano

Gari zilizokuwa Chakavu

Nam.	Nambari ya Gari	Sehemu iliyokuwa inatumika	Kabila la Gari

1.	SLS 130B	Uendeshaji Service Line	Nissan Hard Body
2.	SLS 123		Rav 4

Gari zilizokuwa Mbovu

Nam.	Nambari ya Gari	Sehemu iliyokuwa inatumika	Kabila la Gari
1.	SLS 122A	Upimaji	Escudo
2.	SLS 103A	Generation Mtoni	Escudo
3.	SLS 158B	Uendeshaji Kaskazini	Tata Carry
4.	SLS 142B	Upimaji	Hilux
5.	SLS 137A	Uendeshaji(Upimaji	Prado

Gari ilikuwa tayari ishauzwa

Nam.	Nambari ya Gari
1.	SLS 157B

Kuchukuliwa kwa gari hizo kumerudisha nyuma utendaji wa Taasisi hizi na kumepelekea baadhi ya Watendaji ambao wana haki ya kuwa na usafiri kukosa haki yao hiyo ya msingi.

Kwa mantiki hiyo, kitendo cha kuchukua gari zilizokuwa zinatumika hakikuwa halali kwa mujibu wa agizo hilo.

1. Shirika hili halikupata taarifa rasmi kuhusiana na agizo hilo kwa madai kuwa agizo hilo lilitekelezwa kwa njia ya kushtukiza ili Taasisi husika zisipate muda wa kuzificha gari hizo.
2. Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango halikulishirikisha Shirika hili wala ZAWA katika zoezi la uuzaji wa gari hizo, isipokuwa kwamba, walilielekeza tu kuwasilisha kadi na funguo za gari walizozihitaji kupitia barua ya tarehe 23 Septemba, 2021 yenye kumbukumbu Namba BA.26/454/01/21/12 iliyotumwa kwa Meneja Mkuu –

Shirika la Umeme.

3. Watendaji wa Ikulu waliieleza Kamati kuwa Taasisi zote zilizochukuliwa gari zao baada ya zoezi hilo kukamilika zilitakiwa kuzichukua gari zao hizo na kuzifanyia matengenezo kwa lengo la kutumika na zile gari ambazo hawawezi kuzitengeneza basi ichukuliwe hatua ya kuuzwa na Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

   Hata hivyo, Watendaji wa ZECO na ZAWA kwa pamoja hawakukubaliana na kauli hiyo iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Watendaji wa Ikulu na walizidi kusisitiza kuwa hawakupokea taarifa yoyote kuhusiana na maelekezo hayo. Kwa kuwa taarifa zinazotolewa mbele ya Kamati zinatakiwa kuwa ni taarifa sahihi. Hivyo basi, endapo Mtoa taarifa kwa makusudi atatoa maelezo ya uongo mbele ya Kamati kwa nia ya kupotosha, basi Mtoa taarifa huyo atakuwa ni mkosa kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria ya Kinga, Fursa na Uwezo wa Wajumbe ya mwaka 2014 na atapaswa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Jinai. Kwa mnasaba huo,

   Kamati hii iliomba kupatiwa barua iliyotoa maelekezo au muongozo huo ili kujiridhisha na kile kilichoelezwa. Hata hivyo, Watendaji wa Ikulu waliieleza Kamati kuwa barua hiyo haipo. Kutokana na kauli hiyo, Kamati ya LAAC ilizidi kupata mashaka juu ya usahihi wa taarifa zilizokuwa zinatolewa na Watendaji wa Ikulu hasa ikizingatiwa kuwa kwa mujibu wa kanuni ya 48(2) ya Kanuni ya Utumishi ya mwaka 2014 kuwa mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali yatakuwa kwa njia ya maandishi na kwa eneo hilo utaratibu huo haukufanyika.
4. Gari zote za ZAWA zilizochukuliwa na kupelekwa katika kiwanja cha ZAECA hazipo tena katika kiwanja hicho na wala hakuna mawasiliano yoyote juu ya kadhia hiyo na Taasisi husika.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kufutilia hoja hii Kamati ya LAAC ilipendekeza mambo yafuatayo:

1. Pamoja na maelezo ya Shirika la Umeme kuhusiana na kukamilisha taratibu za uimarishaji wa daftari la mali za kudumu, Hoja hii imebaki kama ilivyo kwa kuwa shughuli hiyo imefanywa baada ya kupita Mkaguzi Mkuu wa Serikali.
2. Kwa kuwa Watendaji wa Ikulu walitekeleza agizo la Mheshimiwa Rais kinyume na alivyoelekeza, na kwa kuwa miongoni mwa mambo yaliyokiukwa ni kuvunjwa kwa kanuni ya 48(2) ya Kanuni za Utumishi ya mwaka 2014.

Hivyo basi, Kamati ya LAAC haina budi kutamka kuwa haikuridhika na utaratibu

uliotumika juu ya utekelezwaji wa agizo hilo halali la Serikali. Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inapendekeza yafuatayo:

1. Gari zilizochukuliwa na kufanyiwa matengenezo zirejeshwe kwa Taasisi husika kutokana na tatizo la uhaba wa gari katika Taasisi hizo na endapo Serikali itazihitaji gari hizo basi utaratibu wa kisheria ufuatwe.
2. Endapo kuna gharama zozote zilitumika kwa kuzifanyia matengenezo gari hizo basi Taasisi husika ipatiwe stakabadhi za malipo yaliyofanywa ili iweze kufanya marejesho kwa Taasisi iliyotengeneza.
3. Watendaji wa Serikali, wahakikishe kuwa wanatekeleza shughuli zao kama Sheria, Kanuni na taratibu za nchi zinavyoelekeza badala ya kufuata utashi wao ili kulinda nidhamu ya utendaji na uwajibikaji.
4. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afuatilie kwa kina namna zoezi hilo lilivyotekelezwa pamoja na kujua gari hizo 32 zimeishia katika mikono ya nani, ili kujiridhisha kuwa baadhi ya gari hizo hazikuishia mikononi mwa watu visivyo halali.

3.1.2 Madeni ya muda mrefu shilingi 40,872,991,281

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo hakuna jitihada zozote zilizofanywa katika ufuatiliaji wa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa Shirika kujiendesha kiufanisi. Kutokuwepo kwa ufuatiliaji mzuri wa madeni kunapelekea uwepo wa madeni sugu ambayo hayataweza kulipika na kusababisha hasara kubwa kwa shirika na kuibebesha mzigo mkubwa Serikali. Kuongezeka kwa wadaiwa kunachangiwa na kutokuwepo kwa jitihada za ukusanyaji wa madeni pamoja na kukosekana kwa sera nzuri ya ukusanyaji wa madeni hayo.

Aidha, ukaguzi umebaini baina ya kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018 hadi 30 Juni, 2020 madeni hayo yameongezeka kutoka asilimia 10 hadi kufikia asilimia 24. Mwenendo wa ukusanyaji wa madeni hayo unaonesha kuwa kati ya shilingi 78,456,504,879 zinazodaiwa hadi tarehe 30 Juni 2020 ni shilingi 37,583,513,598 zilizolipwa sawa na asilimia 47.9 na kusalia kwa deni la jumla ya shilingi 38,807,510,305 sawa na asilimia 52.1 ambazo hazijalipwa hadi ukaguzi unakamilika. Mchanganuo wa maelezo hayo ni kama inavyooneka kwenye jadweli lifuatalo:-

	Mwaka wa fedha		
Maelezo	**30.06.2020**	**30.06.2019**	**30.06.2018**
	(Shs.)	**(Shs.)**	**(Shs.)**

Mwenendo wa Madeni	38,807,510,305	36,188,845,046	33,105,814,933

Aidha, ukaguzi umebaini Shirika la Umeme limeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa madeni ambapo sehemu kubwa ya wanaodaiwa madeni hayo ni wadau wa Serikali kupitia Wakala ambao wanachangia uwepo wa deni la shilingi 38,807,510,305 ya jumla ya mapato yanayotokana na biashara sawa na asilimia 95.0 jambo ambalo linadhoofisha uwezo wa Shirika kufikia malengo yake.

Mchanganuo wa maelezo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Wadaiwa	**Unguja (Shs.)**	**Pemba (Shs.)**	**Jumla (Shs.)**	**Asilimia**
Mamlaka ya Maji Zanzibar	19,266,965,539	15,520,864,159	34,787,829,698	85
JWTZ	1,240,277,216	430,516,034	1,670,793,250	4
Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	883,091,173	-	883,091,173	2
Sauti ya Tanzania Zanzibar (ZBC)	438,976,830	-	438,976,830	1
Jeshi la Polisi	400,403,738	-	400,403,738	1
Wizara ya Afya	40,511,118	332,971,752	373,482,870	1
Kikosi cha KMKM	252,932,746	-	252,932,746	1
Jumla	**22,523,158,360**	**16,284,351,945**	**38,807,510,305**	**95**

Kutokana na machanganuo wa maelezo ya jadweli lilokuwepo hapo juu jitihada za makusudi zichukuliwe katika kuimarisha ukusanyaji wa madeni kutoka kwa taasisi na wakala wa Serikali ili Shirika kuweza kujiendesha kwa ufanisi na tija. Ukaguzi unashauri Shirika la Umeme Zanzibar, kundaa mikakati na mbinu madhubuti zitakazowezesha kukusanya madeni hayo kwa wakati pamoja na kuandaa sera ya ufuatiliaji madeni.

Majibu ya Shirika

Shirika la Umeme Zanzibar linaendelea na hatua za kufuatilia ulipaji wa madeni ya Taasisi za Serikali kwa kufanya mazungumzo na kuingia makubaliano ya kulipa madeni yao kwa awamu pamoja na kulipa matumizi yao ya kila mwezi.

Mchanganuo wa maelezo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli

JINA LA TAASISI	DENI HADI SEPT, 2021	HATUA ILIYOCHUKULIWA	MALIPO YALIYOFANYWA	DENI LILOBAKIA HADI SEPT, 2021
ZAWA	43,389,533,568	ZECO huwasilisha barua za maombi ya malipo ya matumizi ya umeme ya ZAWA kila mwezi, hata hivyo, bado malipo hayo hayajapatikana	0.00	43,389,533.568
MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE (ZAA)	1,283,513,720	Shirika limefanya makubaliano ya kulipa deni la umeme na Uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ambapo Mamlaka hiyo itakuwa inalipia kwa ukamilifu matumizi ya umeme ya kila mwezi sambamba na kulipa deni la nyuma kwa kiwango cha TZS 20,000,000 kwa	124,000,000	1,159,513,720

		kila mwezi. Makubaliano yamefanyika mwezi Septemba, 2021 na utekelezaji wake umeanza		
ZBC REDIO	580,943,504	Shirika limefanya makubaliano ya kulipa deni la umeme na Uongozi wa ZBC Redio ambapo ZBC itakuwa inalipia kwa ukamilifu matumizi ya umeme ya kila mwezi sambamba na kulipa deni la nyuma kwa kiwango cha TZS 5,000,000 kwa kila mwezi. Aidha, makubaliano haya yameanza kutekelezwa.	18,000,000	562,943,504
JESHI LA POLISI	472,346,686.01	Jeshi la Polisi limeshafanya uhakiki wa deni hilo ambapo limeahidi kufanya malipo katika mwaka wa fedha 2021/2022.	0.00	472,346,686.01
JWTZ	2,092,307,686	Kufuatia juhudi	333,000,000	1,759,307,686

		kubwa iliyofanywa na Viongozi wa Shirika, JWTZ imefanya sehemu ya malipo katika mwezi Januari 2021 na hivi sasa Idara ya Hazina ya SMT inaendelea kufanya uhakiki wa deni lilobakia		
WIZARA YA AFYA	688,525,433.6	Uongozi wa Shirika umekutana na Uongozi wa Wizara ya Afya na kujadili hatua za ulipaji wa deni hilo ambapo Wizara hiyo inaendelea kulipa matumizi ya vitengo vyake kila mwezi na kutoa ahadi ya kupanga mkakati wa kulipa deni la nyuma	86,000,000	533,079,902
KMKM	345,000,000	Shirika na Kikosi cha KMKM limeingia mkataba wa kufidiana malipo ya umeme na malipo ya	210,000,000	135,000,000

		huduma ya ulinzi ambapo katika mwezi Novemba, 2021 fidia hiyo ilikuwa TZS 210,000,000		
JUMLA	**48,852,170,598**		**771,000,000**	**48,011,725,066**

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia Hoja hii yafuatayo yamebainika na Kamati ilitoa mapendekezo yake kama ifuatavyo:

Shirika hili halina Sera ya ukusanywaji wa mapato jambo ambalo limepelekea Shirika kushindwa kuwachulia hatua wateja wao wanaowadai hususan Taasisi za Umma.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati hii imeishauri Shirika kuandaa Sera hiyo ili liweze kuwabana na kuwachulia hatua wale wote ambao hawaiipii huduma hii.

Sambamba na hilo, kwa kuwa hivi sasa Sera hiyo haipo, na kwa kuwa Shirika hili linazidai fedha nyingi Taasisi za Umma na kwa kuwa Taasisi ikiwa na Wateja wengi inaowadai kuna uwezekano mkubwa wa Taasisi hiyo kushindwa kutekeleza vyema majukumu yake kutokana na uhaba wa mapato. Hivyo basi, Kamati hii inaishauri Serikali kuzikata fedha za Matumizi Mengineyo Taasisi zenye deni moja kwa moja.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya LAAC ilikutana na baadhi ya Wadaiwa wakiwemo Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na kueleza kuwa sababu kuu inayopelekea Taasisi hizo zisilipie huduma hiyo kwa wakati ni uhaba wa fedha unaoukabili Taasisi hizo.

Hata hivyo, Taasisi hizo ziliieleza Kamati hii kuwa tayari Serikali imeshatoa agizo la kuitaka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kulipa deni hilo hadi mwaka wa fedha 2019/2020 na kuanzia hapo Taasisi husika zilipe zenyewe deni hilo.

Katika kujiridhisha na majibu ya Taasisi hizo mbili pamoja na kujua ni lini deni hilo litalipwa na Wizara hiyo, Kamati ya LAAC ilifanya mazungumzo na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango tarehe 02 Februari, 2022. Katika kikao hicho, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ilikiri kupokea agizo hilo la Serikali na inatarajia kulilipa deni hilo ndani ya mwaka wa fedha 2021/2022 baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa

Hesabu za Serikali na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kumaliza uhakiki wa deni hilo.

Kutokana na maelezo hayo, Kamati ya LAAC imewataka Wahakiki hao kumaliza haraka shughuli hiyo ili Serikali iweze kulipa deni hilo na kuiwezesha ZECO kufanya kazi zake bila ya usumbufu wowote.

3.1.3 Kutokuthibitishwa kwa deni la shilingi 14,993,787,676

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zilizoripotiwa na Shirika la Umeme Zanzibar, imebainika uwepo wa deni la shilingi 14,993,787,676 zinazodaiwa na Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) linalotokana na huduma ya kuuziwa umeme ambayo ni tofauti ya thamani ya kila kipimo cha umeme (unit price) na thamani halisi ya fedha.

Ukaguzi ulipitia taarifa za Kikao cha Bodi ya Wakurugenzi, Kikao nambari 7/2019 kilichofanyika tarehe 28 Disemba, 2019 pamoja na mambo mengineyo yaliyojadiliwa maazimio ya kikao hicho yalieleza wazi wazi kwamba kiasi cha fedha kinachotakiwa kulipwa kwa TANESCO bado kipo kwenye mzozo, ambapo pande zote mbili (TANESCO na ZECO) zimeshindwa kufikia makubaliano juu ya bei kuuza kwa kila kiwango *(unit)* ambacho kinapaswa kulipishwa kwa ZECO.

Aidha, ukaguzi ulitumia juhudi mbali mbali ikiwemo ya kuwaandikia barua Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) yenye kumbukumbu ZEC/CONF.2TNS./VOL.II/60 ya tarehe 28 Januari, 2021 inayowataka kuthibitisha uwepo wa deni hilo na kujua bakaa ya deni lililolipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020.

Kutokana hadi hiyo ukaguzi umeshindwa kupata ufafanuzi na majibu ya barua hiyo na kupelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa deni hilo. Ukaguzi unapendekeza busara na jitihada za makusudi zichukuliwe baina ya pande mbili hizo ili kutatua mgogoro kuhusu uuzwaji wa umeme kwa kila kipimo cha umeme *(unit price)* na thamani halisi ya fedha ili kuepusha kujitokeza kwa deni kubwa ambalo halitoweza kulipika.

Majibu ya Shirika

Shirika la Umeme Zanzibar bado linaendelea na jitihada za mazungumzo na Shirika la Umeme (TANESCO) kwa ajili ya kutatua tofauti ya bei ya mauziano ya umeme baina ya pande mbili ili kuweza kuondosha tofauti ya bei iliyopo na kufikia muafaka katika bei ya mauziano ya umeme.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kwa kuwa suala hili lipo katika majadiliano kwenye ngazi ya Muungano hivyo, Kamati ya LAAC halikulijadili.

3.1.4 Hali ya upotevu wa Nishati ya Umeme

Ukaguzi umefanya tathmini ya hali ya upotevu wa nishati ya umeme kwa mujibu wa taarifa za uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme iliyotolewa na Idara ya Biashara ya Shirika la Umeme Zanzibar inaonesha kwamba kwa wastani kiwango cha *(unit)* 6,910,041 zinapotea kila mwezi ambayo ni sawa na asilimia 18.2. Upotevu huo unatokana na hali za kiufundi na hali zisizokuwa za kiufundi.

Ukaguzi umebaini kiwango cha upotevu wa nishati ya umeme ni kikubwa jambo ambalo litapelekea Shirika la Umeme kukosa ufanisi katika utendaji wake.

Majibu ya Shirika

Shirika la Umeme Zanzibar linaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kupunguza upotevu wa umeme zikiwemo ubadilishaji wa mita mbovu, transforma zilizozidiwa, waya chakavu, kufanya ukaguzi wa wateja mara kwa mara na uboreshaji wa miundo mbinu ya usambazaji wa umeme. Aidha, Shirika linaendelea na utaratibu wa kuwachukulia hatua wanaojihusisha na vitendo vya uhujumu wa kujiungia umeme bila ya kufuata utaratibu.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia Hoja hii Kamati ilihoji nafasi ya watendaji wa Shirika hili ambao wamestaafu kwa kuwa watendaji hawa wanauelewa mpana juu ya masuala ya umeme, hivyo, wanaweza wakajiingiza katika mambo yasiyostahiki na kulipatia hasara Shirika.

Kutokana na swali hilo na katika kuzuia kitu hicho kisitokee Kamati ilielezwa kuwa Shirika hili lina mpango wa kuanzisha Chuo (College) ambayo itawatumia Wastaafu hao kuwafundishia watendaji wapya na wale wanaoendelea na kazi ili watendaji hao waweze kutekeleza shughuli zao kwa weledi mkubwa.

Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na juhudi mbali mbali zilizoelezwa kuchukuliwa na Shirika hili katika kutatua changamoto hiyo, hata hivyo, Kamati hii imelitaka Shirika hili kuzidisha kuchukua juhudi kwa kuwa tatizo hilo bado ni kubwa.

3.1.5 Kushindwa kufanya tathmini ya thamani ya mali za kudumu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Umeme lilifanya makubaliano na Kampuni ya M/s Trace Associate Ltd kwa ajili ya kufanya tathmini ya thamani ya mali za kudumu kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hata hivyo, ukaguzi umeshindwa kupata ripoti ya tathmini ya thamani ya mali za kudumu ambazo hazikuwahi kufanyiwa tathmini kwa kipindi hicho na zinahitaji muendelezo wa tathmini hiyo iweze kufanyika ambapo hadi ukaguzi unakamilika ripoti ya tathmini ya mali zifuatazo hazikupatikana kwa ukaguzi. Mchanganuo wa mali hizo unaonekana katika jadweli lifuatalo:

Aina ya Mali za kudumu	Thamani (Tsh) 30.6.2020	Thamani ya Uchakavu (Tsh) 30.6.2020	Thamani Halisi ya Sasa (Tsh) 30.6.2020
Ardhi	249,678,000	-	249,678,000
Majengo	2,631,511,402	1,222,349,756	1,409,161,646
Mitambo/Vifaa	139,729,355	8,150,879	131,578,476
Jumla	**3,020,918,757**	**1,230,500,635**	**1,790,418,122**

Kutokana na mchanganuo unao onekana hapo juu, jumla ya thamani halisi ya mali za kudumu za shilingi 1,790,418,122 zimekosa ripoti ya tathmini hiyo kupelekea thamani ya jumla ya mali za kudumu ya shilingi 274,648,029,694 iliyopelekea hesabu za mwisho wa mwaka kuripotiwa kimakosa.

Majibu ya Shirika

Shirika la Umeme Zanzibar tayari limekwishafanya tathmini ya thamani ya mali za kudumu, ambazo hazikufanyiwa tahmini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo ripoti ya tathmini hiyo kutoka kwa Mthamini Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshakabidhiwa kwa Shirika.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC imebaini kuwa Shirika la Umeme lilifanya tathmini ya baadhi tu ya mali zake kitu ambacho ni kinyume na utaratibu. Hivyo, Kamati hii inalishauri Shirika hili likifanya tathmini za mali zake basi lifanye kwa mali zake zote ili ipatikane tathmini halisi ya mali hizo.

3.1.6 Dosari katika mfumo wa urejeshwaji wa mikopo kwa wateja

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Umeme limeandaa sera ya utoaji wa huduma ya nishati ya umeme kwa wateja wapya kwa njia ya mikopo ambapo wateja hao hutakuwa kulipa mikopo hiyo kwa muda katika ya miezi sita, miezi kumi na mbili na miezi kumi na nane kulingana na makubaliano yaliyoingiwa baina ya Shirika na wateja waliokopeshwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya orodha ya wateja wapya waliounganishwa umeme kwa njia ya mkopo na kubainika kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2020 Shirika la Umeme lilitoa mkopo wenye thamani ya shilingi 300,941,190.

Ukaguzi ulibaini mwenendo wa urejeshwaji wa mikopo hiyo hauridhishi baada ya kukosa taarifa za urejeshwaji wa mikopo hiyo kutoka katika mfumo unaotumiwa na Shirika (SUPREMA SYSTEM). Mfumo huo umeshindwa kuonyesha deni la mteja mmoja mmoja, kiwango anachodaiwa, kiwango kilicholipwa na bakaa ya deni lililobakia, jambo ambalo limepelekea kusababisha ugumu wa kujiridhisha uwepo wa kiwango sahihi kinachodaiwa, kilicholipwa na kilichobakia kutokana na taarifa hizo kurikodiwa katika madaftari.

Kutokutumika kwa mfumo kwenye ukusanyaji wa madeni kunapelekea kushindwa kujiridhisha kwa uwepo na ulipwaji wa madeni hayo na hivyo kunaweza kulipelekea shirika kulikosesha mapato.

Majibu ya Shirika

Ni kweli kwamba Shirika la Umeme kwa kutumia mfumo wa SUPREMA ulikuwa ukitoa ripoti za mikopo kwa ujumla na sio kwa mteja mmoja mmoja, hivyo basi, liliweza kuwasiliana na mtaalam alieko Afrika Kusini na kuweza kurekebisha mapungufu hayo na hivi sasa ripoti inatoka kama inavyohitajika.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kwa kuwa kasoro hiyo imechukuliwa hatua baada ya Mkaguzi Mkuu kutoa Ripoti yake Kamati hii imeibakisha Hoja hii kama ilivyo na inalishauri Shirika hili kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa utaratibu ili kuepuka hoja zisizo za msingi.

3.1.7 Kushindwa kutumika kwa Mfumo wa Uhasibu wa kielektroniki wa USD 65,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Umeme lilifanya malipo ya

jumla dola za kimarekani 65,000 kwa ajili ya kununua mfumo wa Kielektroniki (SAP) ulionunuliwa Juni 2005 ambao umekusudiwa kushughulikia kazi za uhasibu, rasilimali watu, uhifadhi wa mali za kudumu na kazi za manunuzi. Ukaguzi umebaini Shirika la Umeme bado linaendelea kufanya shughuli za uhasibu ikiwemo utayarishaji wa hati za malipo, uwekaji wa taarifa za fedha kwenye madaftari ya kumbukumbu za fedha *(Manual System).*

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mwongozo wa uhasibu wa Shirika la Umeme *(Corporation Accounting Manual)* kifungu nambari 17.1 ambapo kinaelezea utengenezaji wa taarifa za kifedha zifanyike kwa kutumia njia ya mfumo wa kielektroniki (SAP Package).

Majibu ya Shirika

Shirika la Umeme Zanzibar linafanya shughuli za kihasibu zote ikiwemo kufanya hati za malipo (payment vouchers), ukusanyaji wa mapato (Revenue Collection) na uwekaji wa rekodi za rasilimali za kudumu (Fixed Assets Register) kwa kutumia Mifumo ya kielekroniki ambayo ni SAP, SUPRIMA na EQUILLIUM. Hata hivyo, kutokana na mifumo tofauti inayotumika katika uwekaji wa kumbukumbu za kifedha, Shirika linapata changamoto ya utengenezaji wa hesabu za mwaka (Financial Statement) kwa kutumia Mfumo wa SAP kutokana kutokuwa na muingiliano baina ya Mifumo hiyo.

Ili kutatua changamoto za ufungaji wa hesabu, Shirika la Umeme kupitia mradi wa ZESS limeweka kipengele cha kuunganisha mifumo hiyo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kwa kuwa kasoro hiyo imechukuliwa hatua baada ya Mkaguzi Mkuu kutoa Ripoti yake Kamati hii imeibakisha Hoja hii kama ilivyo na inalishauri Shirika hili kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa utaratibu ili kuepuka hoja zisizo za msingi.

3.2: BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA PBZ KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 31 JUNI, 2019

Kamati haikupokea majibu ya taarifa ya Mapato na Matumizi ya Benki ya Watu wa Zanzibar kama zinavyoelekeza Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 kwamba majibu ya Taasisi yanatakiwa yawasilishwe katika Kamati siku mbili kabla ya Kamati kukaa na kujadili taarifa hizo. Hata hivyo, Kamati imepatiwa

maelezo ambayo yameiwezesha Kamati kubaini mambo yafuatayo:

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya LAAC imegundua kwamba ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka za Benki ya Watu wa Zanzibar ni tofauti na ule unaotumiwa na Serikali kwa vile PBZ hufunga hesabu zake kuanzia mwezi wa Januari hadi Disemba kwa vile PBZ ni kampuni inayojitegemea ambayo inafanyakazi zake kwa kusimamiwa na Bodi chini ya maelekezo yanayotolewa na BOT.

Kwa mwaka 2019, mapato ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) yatokanayo na riba yameongezeka kutokana na uwezo wa benki kukopesha ulikuwa mzuri na wateja wake walirudisha mikopo ipasavyo. Aidha, kupungua kwa mapato yasiyo ya riba yameonekana kupungua kwa mwaka wa fedha 2019 kwa sababu wateja wengi kwenda kufuata huduma kwenye 'hall' (dirishani) kuliko kutumia njia nyengine.

Kadhalika, Kamati ilitaka kujua vyanzo vya mapato vya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na kuelezwa kwamba kuna vyanzo viwili yaan mapato yatokanayo na mikopo kwa benki zote mbili (Conventional na Islamic bank) pamoja na mapato yatokanayo na huduma na biashara ya ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni. Kamati imegundua kuna vyanzo vyengine vinavyotokana na uendeshaji wa Benki (other operating income) ambavyo vinajumuisha gawio, mapato kutoka kampuni ya umoja (Umoja Swift), benki ya mukopa na 'Afro Exim'.

Aidha, kuna mapato yanayopatikana kupitia huduma ambazo PBZ inazitoa na kupatiwa ujira wao (fee and commission) ambazo zinapatikana katika 'Note' 32 lakini Kamati ilishindwa kupata ufafanuzi wa kiwango halisi kilichochangiwa na ujira huo kwa mwaka 2019 na kuelezwa kwamba ufafanuzi wake unapatikana katika 'trial balance'. Sambamba na hilo, Kamati imegundua kuwa PBZ inakusanya mapato kwa niaba ya TRA ambayo huwa wanapata ujira wao.

Kadhalika, Kamati ilitaka kujua kwanini mapato ya uwekezaji hayajawekwa kama ni vyanzo vinavyojitegemea na kueleza kwamba hali hiyo inatokana na 'format' za mabenki zinavyotaka na vile vile mapato hayo sio vyanzo vya uhakika kupatikana. Kufanya hivyo, ndio kunatoa taswira halisi kwamba mabenki ni taasisi zinazo lenga zaidi katika utoaji wa huduma.

Kwa upande wa matumizi ya Benki ya Watu wa Zanzibar, Kamati imegundua yameongezeka kwa sababu ya kuongezeka kwa riba ya amana za wateja kulikotokana na wateja wengi kuweka fedha zao benki. Aidha, kulikuwa na vikao vingi vya Bodi vilivyofanyika kuhakikisha usimamizi mzuri wa uendeshaji wa shughuli za benki.

Kamati pia imebaini kuwa gharama za uendeshaji zimeongezeka kutokana na

kuongezeka kwa uwekezaji wa ujenzi katika maeneo tofauti ikiwemo ujenzi wa vituo vya huduma za ATM za Malindi shilingi 129,189,086.00, Mlandege shilingi 54,230,670.00 na shilingi 55,035,113.00. Wakati shilingi 374,672,420.00 zimetumika kwa ujenzi wa kituo cha huduma cha Tandahimba Mtwara na shilingi 82,660,038.40 zilitumika kulipia huduma za ulinzi kwa kampuni ya 'Soyuz Security Service Limited' kwa Tanzania nzima.

Kamati pia imebaini kwamba kuna baadhi ya maeneo gharama za matumizi ya wafanyakazi ziliongezeka wakati zilitakiwa zipungue kutokana na kuwepo kwa Uviko 19 na kuelezwa kwamba PBZ haikupunguza wafanyakazi katika kipindi hicho kama ilivyokuwa katika mahoteli bali walifanya kazi zaidi hadi muda wa kupindukia na kuna sehemu walifungua vituo vya kukusanyia mapato (collection centers) vilivyokuwa vinafanya kazi hadi muda wa usiku, hivyo kulihitajika posho za ziada zitumike.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

1. Kwa vile upitiaji wa taarifa za fedha za benki unatofautiana sana na taarifa nyengine, Kamati inaiomba PBZ iwe na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa Kamati ili waweze kuwa weledi katika upitiaji taarifa zao.
2. PBZ iiendeleze vyema miradi yake ya uwekezaji ili iwe endelevu na ilete tija zaidi kwa PBZ na nchi yetu.
3. PBZ iongeze juhudi katika ukusanyaji wa mapato yake ili iweze kuipatia Serikali gawio kubwa zaidi.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR

Kwa upande wa hoja za Ufanisi katika uendeshaji wa Benki na Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha, Kamati haikuwa na maelezo ya ziada kwenye hoja hizo kwa sababu majibu yake yanapatikana katika maelezo yaliyotolewa ufafanuzi awali yanayohusu mapato na matumizi.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.2.1 Kutokutekeleza muongozo wa Benki kuu (BOT)

Kutokana na muongozo wa BOT juu ya utekelezaji wa mfumo wa uhasibu (IFRS 9) unaeleza kwamba, mfumo wa upoteaji wa mkopo unaotarajiwa (expected credit loss - ECL) chini ya IFRS 9 kwa madhumuni ya udhibiti wa vifungu vya uhasibu, Benki pamoja na Taasisi za kifedha zinatakiwa kuhakikisha kwamba taratibu zote za kibenki zinafuatwa katika kuamua kiwango cha upotevu wa mkopo na kuhakikisha kuwa

nyaraka zinahakikiwa na kusainiwa mara kwa mara.

Ukaguzi umebaini kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar, bado haijaandaa kielelezo cha nyaraka kinachohusiana na hali hiyo.

Majibu ya Benki

Licha ya kujitokeza kwa kasoro hizo lakini kwasasa Benki ya Watu wa Zanzibar tayari imeshatekeleza muongozo huo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imegundua kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar ilikuwa nao muongozo huo mpya uliotolewa na BOT ambao ulikuwa katika nakala laini (Soft copy) isipokuwa hawakuwa na nakala ngumu (hard copy) ambayo Mkaguzi aliuhitaji ili kujiridhisha kama utaratibu wa kuamua kiwango cha upotevu wa mkopo unafuatwa kikamilifu. Hili limebainika baada ya Kamati kuoneshwa muongozo huo ambao ulitolewa baada ya Mkaguzi kumaliza kufanya kazi yake.

Mapendekezo ya Kamati

1. PBZ ihakikishe inaendelea kutumia miongozo yote inayotolewa na BOT ili iweze kutekeleza matakwa ya msimamizi wa shughuli za Mabenki Tanzania na kuepuka kasoro za ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti.

2. Kutokana na ugumu uliopo katika kukagua taarifa za fedha za Benki, PBZ iipatie mafunzo Kamati ya LAAC ili iweze kuchunguza kwa weledi wa hali ya juu taarifa zake na kuishauri vizuri Serikali.

3. PBZ itekeleze ushauri wa Mkaguzi kwa wakati ili kuepusha hoja kuainishwa katika ripoti ya Mdhibiti wakati tayari imeshaifanyia kazi.

TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA PBZ KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 31 JUNI, 2020

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umebaini mapato yatokanayo na riba yameongezeka kutoka shilingi 52,254,999,740 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019, ukilinganisha na shilingi 62,726,498,962 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020, kukiwa na ongezeko la shilingi 10,471,499,222 sawa na asilimia 167 ya ongezeko.

Majibu ya Benki

Mapato ya benki ya Watu wa Zanzibar yameongezeka kwa sababu kuongezeka kwa

mikopo kulikosababisha kuongezeka kwa riba ambapo mwaka 2019 jumla ya mikopo bilioni 376 ilikopeshwa wakati kwa mwaka 2020 kulikuwa na mikopo ya bilioni 469. Aidha, mapato yasiyokuwa ya riba (non interest income) yalipungua kutokana na kuwepo kwa virusi vya uviko 19 vilivyopelekea mapato ya ubadilishaji fedha za kigeni (foreign exchange) kupungua ambapo mwaka 2019 kulipatikana bilioni 6 wakati 2020 mapato yalipungua hadi bilioni 3.5

Uchunguzi na Mapendekezo wa Kamati

Kamati baada ya kupitia 'Financial Statement' ya PBZ imegundua kwamba ililipa fedha nyingi kwa kulipa posho za vikao vya Bodi. Kamati imetaka kupatiwa muongozo wa malipo hayo ambapo kupitia barua ya tarehe 17 Agosti, 2020 yenye kumbukumbu nambari CAB.40/158/01/15 iliyojibiwa na Katibu Mkuu (OR) - Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeainisha posho za baadhi ya Wajumbe wa Bodi ambayo Kamati iliridhika nayo.

Taarifa ya matumizi

Ukaguzi umebaini kupungua kwa matumizi ya riba kutoka shilingi 11,769,476,447 kwa mwaka unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 10,918,994,250 kwa mwaka unaoishia Disemba 2020, kukiwa na upungufu wa shilingi 850,482,197 sawa na asilimia 7.8 ya upungufu.

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020, imebainika gharama za uendeshaji zimeongezeka kutoka shilingi 36,906,940,131 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019, hadi kufikia shilingi 39,363,545,784 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020, kukiwa na ongezeko la shilingi 2,456,605,653 sawa na asilimia 6.2 ya ongezeko.

Majibu ya Benki

Mapato ya Benki ya Watu wa Zanzibar yameongezeka kutokana na maelekezo kutoka Benki Kuu ya kuanza kutumia mfumo wa IFRS 9 ambao uliwagharimu jumla ya shilingi bilioni 11. Aidha, Benki ilifuta (Written off) mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 2.5 ambayo imekidhi vigezo vya BOT ili isikuwemo katika ukaguzi unaofanywa na BOT kwa vile wateja wake wanaonekana hawana uwezo wa kurudisha mikopo hiyo.

Uchunguzi wa Kamati

Kufuatia majibu hayo, Kamati ilitaka kujua vigezo ambavyo BOT huamua mkopo ufutwe na kuelezwa kuwa ikifikia mteja kwa mwaka mmoja hajalipa kiasi chochote cha mkopo wake (mkopo wake unafutwa). Hata hivyo, kufutwa huko hakuizuii Benki husika kuendelea kufuatilia malipo ya mikopo hiyo ambapo PBZ kwa mwaka 2020 ililipwa jumla ya shilingi milioni 678 ambayo tayari ilikuwa imeshafutwa.

Aidha, Kamati iligundua kwamba mikopo iliyofutwa kwa mwaka 2019 ilikuwa milioni 884,615,000 wakati mwaka 2020 ilizidi zaidi ya mara mbili na kufikia jumla ya shilingi bilioni 1,625,661,000. Hali hiyo ilichangiwa na wafanyakazi askari kukopa zaidi ya sehemu moja ambapo kiwango cha vifo huwa vingi na sio kuibuka kwa virusi vya uviko 19 kama awali ilivyodaiwa na watendaji wa PBZ kwa vile Covid imekuja mwishoni mwa mwaka 2019. Kutokana na hali, wakopaji hao hushindwa kupatikana mikato ya mikopo yao.

Kamati baada ya kupitia barua ya tarehe 19 Septemba, 2020 iligundua kwamba ufutwaji wa mikopo hiyo ulifikia jumla ya shilingi 2.5 bilioni badala ya 1.6 kwa vile ilijumuisha na ufutwaji wa mikopo mingine iliyokuwa inamalizika miaka ya 2019, 2021, na 2022. Kamati ilipata wasiwasi kuona kiwango kilichofutwa kuwa kikubwa zaidi ya kile kilichoainishwa katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka 2020.

Kamati haikukubaliana na kitendo hicho maana inauelewa wa kutosha kwamba ufutwaji wa mikopo ndio miongoni mwa eneo kubwa linalotumiwa na watendaji wa benki kuchota fedha za umma ili kutimiza maslahi yao binafsi.

Kamati pia imegundua kuna 'Note' nambari 36 ambayo imeelezea vitu viwili tofauti ('charge'/recovery of ECL - loan and financing' na 'Recovery of ECL - other assets') kinyume na viwango vya kitaifa na kimataifa vya uandaaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

Kadhalika, Kamati ilitaka kufahamu ufafanuzi wa 'Note' 40 (other operating expenses) na 'Note' 39 (General and administrating costs) zinahusiana na vitu gani kwa vile zinaonekana zinafanana na kuelezwa kwamba 'Note' 39 inajumuisha vitu vingi vikiwemo 'Deposit insurance, vifaa vya kuandikia pamoja na gharama za Ofisi za usafirishaji fedha katika Matawi tofauti wakati 'Note' 40 imeelezwa haionekani moja kwa moja na inahusiana na fedha za 'donation' na 'social responsibility' na vitu vingine vingi ambapo kwa mwaka 2020, PBZ ilitumia shilingi milioni 600 kwa shughuli za 'social responsibility'.

Kamati haikukubaliana na majibu ya watendaji ya kuvitenganisha vitu hivyo katika 'Note' mbili tofauti wakati zinalingana. weka pamoja vitu hivyo katika 'Note' moja kwa vile vinatokana na maumbile tofauti.

Mapendekezo ya Kamati

1. Benki ya Watu wa Zanzibar ihakikshe inafuatilia ipasavyo mikopo ya wateja wake ili kuepuka kufutwa na BOT na kuikosesha Serikali gawio.

2. PBZ iache utaratibu wa kuchanganya pamoja madeni yaliyofutwa miaka tofauti badala yake kila mwaka yaonekane wazi madeni yaliyofutwa ili kutoa taswira halisi na sahihi ya fedha hizo.

3. PBZ itumie 'Note' moja kwa ajili ya ufafanuzi wa kitu kimoja kinachotofautiana na chengine kama zinavyoelekezwa katika viwango vya ufungaji wa hesabu vya kitaifa na kimataifa. Aidha, PBZ iviunganishe katika 'Note' moja vitu vinavyolingana.

Ufanisi katika Uendeshaji wa Benki

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa benki kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 na Disemba 2020.

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020, Benki ya Watu wa Zanzibar imepata faida ya shilingi 18,712,542,933 ukilinganisha na faida ya shilingi 32,066230,084 iliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 kukiwa na upungufu wa shilingi 13,353,687,151 sawa na asilimia 71.4.

Majibu ya Benki

Faida iliyopatikana imetokana na sababu zilizoainishwa katika majibu ya taarifa za mapato.

Uchunguzi na Mapendekezo wa Kamati

Katika uchunguzi wa hoja hii, Kamati imegendua kwamba kuna jumla ya shilingi bilioni 2.4 ambazo benki ya Watu wa Zanzibar imelipa Serikalini kama gawio lake kwa mwaka 2020 ambalo gaawio hilo litakuja kuonekana katika ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2021. Fedha hizo zimetokana na utoaji wa asilimia 20 ya faida yake kwa kila mwaka.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.2.2 Mapato ya ujira ambayo hayakupokelewa shilingi 395,889,294

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Mapato imeingia mkataba na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na walipa kodi. Kwa mujibu wa kifungu 8.2 cha makataba kimebainisha asilimia 0.1 ya kodi ilipaswa kukusanywa na kuwa ujira kwa PBZ. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 PBZ ilistahiki kulipwa jumla ya shilingi 395,889,294 kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) kupitia Benki kuu Tanzania (BOT). Hadi ukaguzi unafanyika, imebainika kujitokeza kwa kasoro mbali mbali za utekelezaji wa mkataba huo kama ifuatavyo:

- Kubainika kwa kumalizika muda wa makubaliano ya mkataba wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ujira tokea Februari.
- Benki ya Watu wa Zanzibar kuendelea kukusanya mapato hayo bila ya makubaliano ya mkataba kuanzia Febuari 2019 hadi 30 Juni, 2020 bila ya kupokea ujira kutoka TRA.

Majibu ya Benki

PBZ ilifanya mazungumzo ya kuingia mkataba mpya na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa lengo la kuendelea na huduma za ukusanyaji wa mapato katika vituo mbali mbali. Hata hivyo Mamlaka ya Mapato hawakuonesha nia ya kutaka kuendelea na mkataba huo kwa hoja kwamba kwa vile Benki inakusanya mapato ya Serikali hakuna haja ya kutoza gharama kwenye ukusanyaji huo.

Hii ilikuwa ni kwa benki zote Tanzania ambazo zinafanya makusanyo hayo na sio PBZ peke yake. Kuhusu deni la nyuma Mamlaka pamoja na benki zilikubaliana kufanyika malipo hayo kwa awamu ambapo hadi kufikia Disemba 2021, PBZ ilishapokea shilingi 339,416,793.94. PBZ inaendelea kufuatilia deni lililobakia kwa ukaribu ili kuhakikisha linalipwa lote.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imegundua kwamba ni kweli PBZ ilikuwa haina mkataba na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhusu ukusanyaji wa kodi kwani mkataba uliokuwepo ulimaliza muda wake tokea mwaka 2018 lakini wakati kamati inafanya ukaguzi wake, mkataba huo ulikuwa unaendelea kufanya kazi na tayari deni walilokuwa wakidai limelipwa na kubakia shilingi milioni 56,472,500.06.

Aidha, Kamati ilitaka kujua sababu za kutoendelea mkataba huo na kugundua kwamba benki zilikuwa zikitumia vibaya fedha hizo kwa kuziingiza katika biashara na kujinufaisha kinyume na utaratibu wakati benki hizo huwa zinapatiwa ujira wake.

Kutokana na hali hiyo, TRA ilivunja mkataba kwa mabenki yote lakini PBZ iliendelea kukusanya mapato hayo hadi TRA walipoamua kuingia tena mkataba mwengine na PBZ. Lakushangaza, PBZ iliyafanya hayo pasi na kuwepo kwa mkataba na bila kujua athari za baadaye iwapo TRA ingekataa kulipa kiasi hicho stahiki.

Kadhalika, Kamati imebaini kuwa kulikuwa na upotevu wa fedha uliosababishwa na mpango mbaya uliokuwa ukitumika kwani mwaka 2019 malipo ya ‘medical expenses’ yameongezeka ukilinganisha na mwaka 2020 licha ya kuwepo wafanyakazi waliokuwa wameajiriwa mwezi wa Oktoba kwa sababu PBZ ilikuwa ikilipa ‘premium’ ya ‘medical expenses’ lakini mwanzoni wa mwaka 2020 gharama hizo zilipungua kwa vile malipo

yalikuwa yakifanyika kwa mujibu wa matumizi halisi ya huduma iliyotolewa.

Mapendekezo ya Kamati

1. PBZ iwe na mipango mizuri itakayokuwa rafiki katika kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.
2. PBZ ihakikishe ina 'renew' mikataba yake mara tu inapomaliza muda wake ili kuhalalisha wanachokitekeleza.
3. PBZ ihakikishe inafuatilia madeni yake na yanalipwa kwa wakati.

UKAGUZI MAALUM WA KAMATI KATIKA MATAWI LA DODOMA, KIGAMBONI NA TANDIKA

Katika ufuatiliaji wa kilichogunduliwa na Kamati wakati ilipokuwa ikichunguza majibu ya hoja ya taarifa ya matumizi kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kuhusiana na ujenzi wa Matawi na Vituo mbali mbali vinavyotoa huduma za kibenki huko Tanzania Bara. Tarehe 7 Febuari, 2022, Kamati ilikwenda kuifuatilia miradi husika iliyotekelezwa ili iweze kupima kama inaendana na thamani halisi ya fedha. Kutokana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini yafuatayo:

A: Tawi la PBZ - Dodoma

1. **Uanzishwaji wa ujenzi huo umechelewa:** Ujenzi wa Tawi hilo ulitakiwa uanze tangu mwaka 2018 lakini ulianza rasmi Oktoba, 2021 na ukamilike mwezi wa Machi, 2022 (Miezi Sita) kwa gharama za shilingi bilioni 1.2. Lakushangaza, hadi Kamati inafanya ukaguzi katika jengo hilo, bado jengo halijaanza kutoa huduma zake zote za (Kiislamu na za Kawaida) kwa vile kulikuwa na kutokukamilika uwekaji wa mashine ya kielektroniki ya utoaji fedha (ATM).

   Kamati ilihoji kwamba kuna sababu gani zilizosababisha kutokuanza ujenzi huo tokea 2018 ambapo watendaji walishindwa kutoa jawabu lililoiridhisha Kamati na kuifanya kuwa na wasiwasi mkubwa kwamba utendaji wa PBZ haukuwa wa ufanisi kwa vile kila muda ukiwa mrefu katika ujenzi husababisha na gharama za ujenzi pia kuongezeka. Kwa mnasaba huo, ongezeko la gharama hizo limetokea pasi na kuwepo sababu za msingi na kuifanya PBZ kutumia gharama zaidi ukilinganisha na utofauti wa muda uliojitokeza. Kamati haikuridhika na kitendo hicho na PBZ inatakiwa iwe makini na mbinu kama hizo zinazotumiwa na watendaji kujifaidisha.

2. **Kutofahamika kwa Tawi na Wateja:** Kwa vile tawi ni jipya, hivyo watu wengi wa maeneo ya Dodoma na maeneo ya karibu hawajafahamu uwepo wa Tawi hilo.

3. **Mkataba wa ujenzi kutozingatia ujenzi wa eneo la wapita kwa miguu (pavement):** Kamati imegundua kwamba katika eneo la mbele ya benki hiyo kuna eneo ambalo halijajengwa 'pevement' na kusababisha Mkandarasi kuingia mkataba wa nyongeza (addendum) ili kurekebisha kasoro hiyo. Kamati haikufurahishwa na kuwepo kwa kasoro hiyo kwa vile ni jambo ambalo linatambulika tangu awali, linaiongezea PBZ kutumia fedha nyengine ambazo haikuzipanga pia inaongeza muda wa umalizaji wa ujenzi husika. Hali hiyo, imepelekea kutoondolewa kwa mabati yaliyozungushwa (uzio) na sehemu ya kutotumika ipasavyo.

4. **Kuwepo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo nje ya Tawi hilo:** Tawi linakabiliwa na changamoto ya kuvamiwa na wafanyabiashara hususan wakati wa jioni na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wateja wanaohitaji huduma kupitia Tawi hilo.

5. **Uwepo wa kasoro katika michoro ya jengo:**

   Kutokuwepo kwa njia za wateja wenye ulemavu wa miguu: Jengo lililojengwa halipo rafiki kuwawezesha wateja wenye ulemavu kupata huduma zao kwa urahisi. Hili limebainika baada ya Kamati kuona hakuna njia ya kupita gari zao wala 'lift' hususan kwa wale wateja watakaofuata huduma za benki ya Kiislamu ambayo Ofisi za Benki hiyo zipo juu (ghorofa ya kwanza). Kamati ilipohoji, ilijibiwa kwamba eneo la kujenga 'lift' ilikuwepo ila Mjenzi alipata maelekezo kutoka kwa Mjengewa (PBZ) aizibe sehemu hiyo.

   Kufuatia hoja hiyo, watendaji wa Benki walieleza kwamba kutakuwa na mtoa huduma za kiislamu atakayewekwa eneo la chini kwa ajili ya kuwapatia huduma wateja wenye ulemavu jambo ambalo halikukubaliwa na Kamati kwa vile kuna muongozo wa mindombinu rafiki haukuzingatiwa unaoyataka majengo ya Umma/Serikali inayotaka majengo mapya yanayojengwa yatengenezewe njia za kuwasaidia watu wenye ulemavu wa viungo hususan miguu.

   a) **Kutokuwepo kwa eneo maalum la kuwekea mashine za kielektroniki:** Kamati imekagua Tawi la Dodoma, Kogamboni na Kituo cha huduma cha Tandika kwamba michoro ya jengo husika haijaweka eneo maalum la kupitisha mashine ya kielektroniki ya utaji fedha badala yake Mkandarasi hujenga kwanza na baadaye hulazimika kuvunja ili kupata njia ya kupitisha mashine hiyo na hatimae kuziba eneo husika. Kamati imelingundua hilo baada ya kupata maelezo ya Mkandarasi wa jengo la Dodoma na kuona ujenzi wa ATM nyengine ambazo zote hazifanyi kazi kwa vile hazijakamilika.

   b) **Kutoingizwa kwa baadhi ya milango na vifaa vya kieletroniki katika mkataba wa ujenzi wa Tawi la Dodoma:**

Kamati imeelezwa kuwa mchoro ulionesha uwepo wa milango mitano itakayokuwa na vifaa vya kielektroniki vinavyotambua wafanyakazi wanaohitajika kuingia na kutoka ndani ya jengo. Lakushangaza, milango hiyo imeongezeka na kufikia zaidi ya kumi ambayo imesababisha mkataba wa awali kurekebishwa na gharama za ujenzi kuongezeka. Lakushangaza zaidi, Kamati ya LAAC imeshindwa kupata mkataba wa nyongeza ya ujenzi huo hadi muda wa uwasilishaji wa ripoti umefika.

6. Kamati imegundua kwamba umiliki wa jengo hilo ni wa ubia (partnership) ambapo PBZ imejenga katika eneo la mtu na kuwa na asilimia 70 ambayo Mjengewa atahitaji kuinunua kupitia faida itakayopatikana hadi kumalizika kwa jengo hilo na umiliki kurudi kwa Mjengewa.

   Kamati ilipokuwa inakagua kupitia taarifa zilizomo katika maelezo, ilipata picha kwamba PBZ wanajenga majengo watakayokuwa na umiliki nayo wa moja kwa moja lakini kiuhalisia katika majengo yote matatu iliyoyatembelea, kamati imegundua kwamba PBZ haikufanya ujenzi ila wameyafanyia matengenezo majengo ya watu hali ambayo itawalazimu kulipa kodi kila mwezi kwa mujibu wa muda waliyokubaliana na mwisho wa siku jengo linabakia katika umiliki wa mtu husika.

   Kamati ya LAAC haikulikubali kikamilifu suala hilo kwani imegundua PBZ bado itakuwa haijajikwamua na changamoto ya kufanyakazi katika majengo yaliyokuwa hayamilikiwi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwalazimu kuendelea kulipa kodi na kupunguza faida na gawio la Serikali.

7. **Kuwepo uwezekano mkubwa wa matumizi mabaya ya fedha za umma:** Kamati iligundua kwamba mradi wa ujenzi wa Tawi la Dodoma ulitakiwa ufanyiwe kazi mwaka wa fedha 2019 na fedha zilionekana kutumika lakini ujenzi rasmi ulianza mwezi wa Oktoba, 2020. Kamati haikuridhika na majibu ya watendaji ya kwamba kulikuwa na taratibu zilianza kufanyika. Kwa mnasaba huo, kuna uwezekano mkubwa kwamba fedha iliyoingizwa haikwenda yote kwenye mradi husika.

8. **Kutowiana kwa gharama za malipo ya mashine za kielektroniki (ATM):** Kamati ilihoji bei zote za ununuzi wa mashine hizo na kuelezwa kwamba mashine mbili za Tawi la Kigamboni na kituo cha huduma cha Tandika zilikuwa milioni 25,000,000 kwa kila moja wakati mashine ya Dodoma imegharimu takriban jumla ya shilingi milioni 75. Hali hiyo ilielezwa inawezekana inatokana na uwezo wa teknolojia yake. Hata hivyo, Kamati haikukubaliana na majibu hayo hasa ukizingatia fedha za ununuzi wa mashine moja ni kubwa zaidi ya mara mbili ya mbili tofauti. Aidha, uzoefu unaonesha ATM nyingi zinazonunuliwa huwa haziwezi kutumika kwa muda mrefu na teknolojia yake ni tofauti na zile ATM za benki nyengine.

9. **Kuwepo tofauti kubwa ya fedha zilizotumika kwa ujenzi:** Kamati imegundua kwamba fedha za ujenzi zilizooneshwa katika maelezo ya awali (kamati lipokutana na PBZ) ilikuwa ni jumla ya shilingi 1.2 bilioni wakati ilipolitembelea jengo hilo Mkandarasi alishindwa kueleza fedha ambazo zimegharimu ujenzi husika isipokuwa inajua Kampuni yake ya M$M. Hali hiyo iliipa Kamati wasiwasi na usahihi juu ya gharama halisi za mradi na kushindwa kupima thamani halisi ya fedha zilizotumika na utekelezaji wa mradi huo.

   Hata hivyo, baadaye Kamati ililetewa gharama hizo kuwa zimefikia shilingi 1.4 bilioni. Matumizi hayo yaliongezeka kwa vile kuliongezeka gharama za ununuzi wa 'ATM' na 'generator' lakini ilishindwa kuthibitishiwa kwamba taratibu za matumizi ya fedha hizo zilifuatwa zikiwemo kupitishwa na Bodi pamoja na mabadiliko hayo kuzingatiwa kupitia marekebisho ya mkataba.

10. **Kutotangazwa ipasavyo kwa huduma zinazotolewa na PBZ:** Kamati imegundua kwamba PBZ haitangazwi kikamilifu kama zinavyojitangaza benki nyengine, hali hiyo inaonekana kupitia matukio tofauti yanayojitokeza mfano matamasha na shughuli zinazofanyika katika Baraza na za kitaifa, PBZ huwa hawaonekani kuchangamkia fursa zilizopo badala yake huchukuliwa na benki nyengine.

11. **Kutokuwepo kwa mashirikiano ya karibu na Mashirika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yanayofanya kazi zake Tanzania bara:** Kamati imebaini kuwa SMZ inayo Mashirika mengi yanayofanya kazi Tanzania bara ambayo kama yatashirikiana ipasavyo yataweza kufanya biashara yenye tija kubwa kwao na Serikali kwa ujumla hasa ukizingatia yanazo fursa nyingi za kukuza mitaji yao. Hili limebainika baada ya Kamati kutembelea Shirika la Bima Zanzibar tawi la Dar - es - Salaam na kukuta kuna benki nne tayari zimeshaingia mkataba nao kwa ajili ya utoaji huduma za bima kupita benki hizo hizo PBZ sio miongoni mwa benki hizo. Hali hiyo husababisha mwanya kwa mabeki wengine kuutumia kuizorotesha PBZ.

    Kadhalika, kuna Mashirika ya Zanzibar kama Shirika la Meli na Uwakala (ZMA) pamoja na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) tayari wanazo nyumba za zamani tena zipo maeneo ya mjini ambazo wanahangaika kutafuta Taasisi itakayowasaidia kuzijenga. Hivyo, iwapo mashirika hayo yataunganisha nguvu yanaweza kuzijenga nyumba kisasa na kuzitumia kwa maslahi ya Taifa letu.

B: Tawi la PBZ - Kigamboni

1. Tawi hilo limeanza kujengwa tarehe 24 Juni, 2020 na lilitakiwa kumalizika tarehe 24 Oktoba, 2020 lakini mradi ulikabidhiwa PBZ tarehe 15 Aprili, 2021 na

ulifunguliwa rasmi tarehe 15 Juni, 2021. Kuchelewa huko kumesababishwa na kuchelewa kupatikana kwa vifaa vya ICT (Camera, UPS na router) kulikotokana na kuibuka kwa virusi vya uviko 19.

2. Mradi huo ulijengwa na 'Ben Bill Company' ambapo gharama zilizoainishwa awali wakati Kamati inapokea maelezo zilikuwa shilingi 452,997,608.98 lakini ilipofika katika eneo la ujenzi iligundua gharama hizo ziliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 604,496,958.98 ambazo zilijuimsha gharama nyongeza za 'Mshauri Elekezi (11,089,000/-), uwekaji wa mfumo wa usalama (36,738,180/-), ununuzi na ufungaji wa 'generator' (57,753,000/-), ununuzi na uwekaji wa 'UPS' (20,919,250/-) na gharama za mashine ya utoaji fedha ya ATM (25,000,000/-).

3. PBZ imekodi jengo hilo ambapo kila mwezi inatakiwa ilipe jumla ya shilingi milioni 81 kwa kipindi cha miaka kumi ya kodi husika. Kwa kodi na kipindi hicho cha kodi, PBZ itakuwa imelipia jengo kwa shilingi milioni 810,000,000/-. Jambo ambalo limeifanya Kamati kufikiri zaidi kwamba kama fedha hiyo ingekuwa inaingia PBZ, Serikali ingeweza kupata gawio kubwa litakalotumika kwa kuwapatia wananchi wetu huduma muhimu za afya, elimu na kadhalika.

C: Kituo cha huduma kwa Wateja wa PBZ - Tandika Mtaa wa Chiota

Ujenzi wa mradi huu unaotoa huduma za benki ya kiislamu pekee ulianza na kumalizika sambamba na mradi wa Kigamboni isipokuwa ulikabidhiwa tarehe 27 Aprili, 2021 na kugharimu jumla ya shilingi 500,056,080.02 ambao ulikuwa ukitekelezwa kupitia Mkandarasi BEN BILL COMPANY na Mshauri Elekezi wake ni M PLUS M ARCHITECTOR. Kupitia ukaguzi uliofanyika, Kamati ya LAAC imegundua mambo yafuatayo:

1. Mradi huo ulichelewa kukamilika kwa mujibu wa mkataba wake. Ukaguzi umebaini kwamba mbali sababu zilizoelezwa ambazo zimechangia kuchelewa kwa miradi ya PBZ, Kamati imebaini kuwepo kwa miradi mingi ambayo inafanyiwa kazi na Mkandarasi na Mshauri Elekezi mmoja kwa wakati mmoja kunachangia kwa kiasi kikubwa kunasababisha kuchelewa kwa miradi hiyo.

2. Kuwepo kwa vifaa vya usalama vinavyoruhusu watu waliosajiliwa tu kuingia ndani ambavyo havifanyi kazi kwa kipindi cha zaidi ya siku mbili. Hali hiyo ni hatari kwa usalama wa Benki na mali zake kwani wahalifu wanaweza kutumia mwanya huo kufanya hujuma. Kamati imeelezwa kasoro hiyo imetokea wakati wa uwekaji wa ATM.

3. Kuwepo kwa gharama tofauti za ujenzi wa mradi huo kwa vile awali Kamati

iliambiwa gharama zake ni shilingi 500,056,080.02 lakini baada ya kutembelea zilikuwa shilingi 500,056,276.02. Hali hiyo haitoi taswira nzuri na sahihi kiukaguzi.

4. Kuwepo kwa kasoro ndogo ndogo za kiujenzi, Kamati imebaini katika mlango wa nje kuna sehemu imeshaanza kufanya ukungu jambo linaloonesha maji ya mvua yanakuwa yanakaa. Hali hiyo ikiachiwa itapelekea kuoza kwa sehemu husika. Aidha, Kamati imebaini kuna kamera moja tu (CCTV CAMERA) upande wa mbele wa benki hiyo ambayo inaonesa upande mmoja lakini hakuna nyengine inayoonesha upande wa mwengine (yaan hazionani). Mazingira kama hayo yanaweza kutumiwa na wahalifu kuingia benki na kufanya wizi bila ya kuwatambua kirahisi.

Mapendekezo ya Kamati

1. PBZ ihakikishe inatekeleza miradi yake ya ujenzi ndani ya wakati unaotakiwa kwa mujibu wa mikataba husika.
2. PBZ ijitangaze zaidi na iwache kufanya kazi kwa mazoea ili waweze kufika sehemu tofauti mjii na vijijini.
3. PBZ iwe na mpango mzuri utakaowezesha kujenga ofisi zao wenyewe ili kuepusha upotevu wa fedha kwa kukodi na hatimae kuwanufaisha wamiliki wa majengo hayo.
4. PBZ ihakikishe michoro ya ujenzi wa Ofisi zake inakuwa imekamilika ipasavyo na ujenzi ufanyike kwa mujibu wa mchoro husika ili kuepusha kujenga na kuvunja baadaye.
5. PBZ ihakikishe inazifanyia kazi kasoro zote za ujenzi zilizogundulika ili kuyafanya majengo hayo yadumu kwa muda mrefu na yawe salama muda wote.
6. PBZ ihakikishe taarifa zake hususan za kifedha zinakuwa sawasawa wakati wowote. Hali hiyo itakuza imani na ufanisi wa Taasisi hiyo.
7. Ili kupatikane ufanisi, ni busara kwa wakati mmoja utekelezaji wa miradi ufanywe na Wakandarasi na Washauri Elekezi tofauti.
8. PBZ ishirikiane na Mashirika mengine ya SMZ yanayofanya kazi upande wa Tanzania Bara ili kutanua wigo wa biashara zao na kunufaika na kwa pamoja na fursa ziliopo katika maeneo hayo.
9. PBZ ihakikishe inajenga majengo yaliyokuwa rafiki na wateja wake wote hususan watu wenye ulemavu.

3.3: BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Taarifa ya Mapato

Bodi ya Mapato Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya bilioni 605.32 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya kodi na tozo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi bilioni 463.73 zimekusanywa sawa na asilimia 76.61 ya makadirio. Aidha, mapato ya Bodi ya Mapato yameonekana kuongezeka kutoka shilingi bilioni 439.08 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia bilioni 463.73 kwa mwka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi bilioni 24.65 sawa na asilimia 5.61.

Majibu ya Bodi

Bodi ya Mapato Zanzibar haikuweza kufikia lengo lake la makusanyo ililojipangia kutokana na kupungua kwa wageni walioingia Zanzibar mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2019/2020. Kwa mfano, mwezi wa Machi waliingia wageni 33,000 wakati mwezi wa Aprili waliingia 334. Hali hiyo ilisababishwa na kuibuka kwa maradhi ya Uviko 19 Ulimwenguni.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na kupungua kwa mapato ya Bodi ya Mapato Zanzibar, Kamati ilitaka kujua kwanini kulikuwa na ongezeko la mapato yaliyokusanywa ukilinganisha na mwaka 2019 na mwaka 2020 na kuelezwa kwamba katika miezi ya awali 2020, ZRB ilifanikiwa kukusanya vizuri zaidi kutokana na wageni wengi walioingia Zanzibar kuliko mwaka 2019 kwani maradhi yalianza kuonekana athari yake katika makusanyo yao katika miezi ya mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hata hivyo, Kamati iligundua kwamba kuna baadhi ya mapato yalipungua katika miezi ya mwisho wa mwaka wa fedha wa 2019/2020 kutokana na 'low session' ya wageni Zanzibar ambapo upungufu huo ulipelekea hoteli nyingi kufungwa na watu kukosa ajira.

Mapendekezo ya Kamati

ZRB ibuni vyanzo vyengine vya mapato ili chanzo kimoja kikianguka vyengine viviinue.

Taarifa ya Matumizi

Bodi ya Mapato ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 16,504,633,531 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Bodi ilitumia jumla ya shilingi 13,971,951,102 kwa ajili ya kazi za kawaida ikiwa ni sawa na asilimia 85 ya makadirio.

Matumizi ya Bodi yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 11,381,939,963 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 13,971,102 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 2,590,011,139 sawa na asilimia 22.75

Majibu ya Bodi

Matumizi ya Bodi ya Mapato Zanzibar yalionekana kuongezeka kutokana na mwezi Agosti, 2019, ZRB iliajiri wafanyakazi wapya na kusababisha fedha za malipo ya mishahara kuongezeka. Aidha, katika mwaka 2019/2020, wafanyakazi wa ZRB waliongezewa mishahara ambapo Kamati iliridhika na vielelezo vilivyooneshwa.

Uchunguzi wa Kamati

Mbali na kuchunguza matumizi ya ZRB, Kamati iliingia ndani zaidi na kugundua kwamba Mdhibiti katika ripoti yake ameainisha jumla ya shilingi bilioni 16.5 za makadirio ya matumizi ya kawaida lakini hakuonesha fedha za maendeleo ambazo ZRB ilitumia na kupelekea kufikia jumla ya shilingi bilioni 27.54. Kutokuonesha fedha za miradi katika kitabu cha Mdhibiti (CAG) kunaweza kuwanyima fursa Wajumbe kutambua matumizi halisi na sahihi ya Taasisi.

Sambamba na hilo, Kamati iligundua jumla ya shilingi 4,200,000 zilitumika kwa ajili ya kukodi nyumba za Ofisi zao za Mikoa. Hata hivyo, fedha hizo hazikutumika kwa vile hawakupata nyumba eneo la kusini na nyumba waliyoipata eneo la Kaskazini haikuwaridhisha ubora wake. Kadhalika, Kamati ilipochunguza matumizi katika kifungu cha 10 (note 10) iligundua kuna kifungu cha 'reward for information' kilikuwa na shilingi 40,117,000 kwa ajili ya ulipaji asilimia ya fedha kwa raia wema watakaotoa taarifa ya kukamatwa kwa kitu. Kamati imegundua kuwa fedha hizo ni kidogo ukilinganisha na matukio na muamko wa watu.

Kwa upande wa posho la vikao vya Bodi, Kamati imegundua kwamba kifungu cha posho hizo kinajumuisha na posho nyengine wakati uzoefu unaonesha Taasisi nyengine za SMZ huwa wanazitofautisha katika hesabu zao. Aidha, Kamati imegundua kwamba bajeti ya makusanyo ya Bodi ya Mapato na Matumizi huwa inapangwa na Wizara ya Fedha na Mipango tofauti na Taasisi nyengine. Hali hii hupelekea ugumu katika ufikiaji lengo la makusanyo kwa vile Taasisi husika ndio inayojifahamu uwezo halisi wa makusanyo yake kulingana na vyanzo vyake.

Mapendekezo ya Kamati

1. ZRB itoe uelewa zaidi kwa wananchi juu ya uwepo wa fedha ambazo zinatumika kuwalipa watu wanaotoa taarifa za ukwepaji au uvunjaji wa sheria za kodi.
2. Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe haiipangii ZRB kiasi cha makusanyo au matumizi yake badala yake isimamie ukusanyaji na utumiaji wa fedha zao.
3. Wizara ya Fedha na Mipango itoe muogozo uliokuwa wazi na wenye vifungu (codes) vinavyotenganisha upangaji wa mapato na matumizi ya Taasisi ili ziweze kuwiana na kuondosha tofauti iliyopo.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.3.1: Kushindwa kutenganisha Ardhi na Majengo katika hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 7,530,308,731

Kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu vya kimataifa (IPSAs 17) aya ya 74 inaeleza kwamba Ärdhi na Majengo ni mali zinazoweza kutengenishwa na kuhesabiwa kwa thamani tofauti, hata kama uwepo wa mali hizo zinapatikana kwa pamoja" ambapo Bodi imeripoti thamani ya ardhi na majengo kuwa ni shilingi 7,530,308,731 zinazomilikiwa Unguja na Pemba.

Kiwango cha mali za kudumu za muda mrefu kilichoainishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2020 hakikuzingatiwa matakwa ya viwango vya ufungaji wa hesabu vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Majibu ya Bodi

Bodi ya Mapato imefanya tathmini ya Majengo na Ardhi kama IPSAS 17 inavyoelekeza. Aidha, katika Hesabu ya mwaka 2020/2021 itaonesha Majengo na thamani yake na Ardhi na thamani yake.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilitaka kujua majengo ya Bodi ya mapato Zanzibar yapo maeneo gani na kuelezwa kwamba ZRB wanayo majengo yao katika maeneo ya Mazizini, Tibirinzi, Gombani, Shangani na Migombani ambayo yanatumika isipokuwa jengo la Ofisi ya ZRB liliopo Shangani walilolikabidhi Serikalini kwa zaidi ya miaka minne kwa ajili ya kutumika kwa shughuli za kiserikali (Kamati ilishindwa kupata barua ya makabidhiano ya jengo hilo). Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba kwa muda wa miaka miwili jengo hilo limekaa pasi na matumizi yoyote kama ilivyokusudiwa na limekuwa bovu na kuhitaji kufanyiwa matengenezo makubwa ili liweze kurudi katika hadhi yake ya awali.

Aidha, Kamati ilielezwa kwamba ZRB ilishindwa kutenganisha hesabu ya Ardhi na Majengo kutokana na mabadiliko ya mfumo yake ya ukusanyaji mapato iliyokuwa inaitumia pamoja na kutokuwa na uelewa kwamba taarifa mbili hizo hazitakiwa kuunganishwa pamoja.

Mapendekezo ya Kamati

1. Bodi ya Mapato Zanzibar iombe Serikalini kurudishiwa jengo lao ili waweze

kulifanyia matengenezo na kulitumia kama Ofisi ndogo ya kuwahudumia walipa kodi wadogo wadogo wa maeneo ya Mjini.

2. ZRB ihakikishe inatenganisha hesabu ya majengo na ardhi ili hesabu zao ziweze kutoa taarifa sahihi kwa watumiaji vitabu hivyo.

3.3.2: Taarifa za fedha ambazo hazikufanyiwa usuluhishi wa kibenki kwa muda mrefu

Ukaguzi umebaini uwepo wa taarifa za kibenki ambazo hazikufanyiwa usuluhishi (reconciliation) kwa muda mrefu kama ifuatavyo:

(a) uwepo wa madeni yanayodaiwa benki kwa muda mrefu hesabu nambari 021103000475 shilingi 127,887,545

Ukaguzi umebaini uwepo wa deni la muda mrefu tangu mwaka 2018 lenye thamani ya shilingi 138,108,385 ambayo yamepungua hadi kufikia shilingi 127,887,545 katika mwaka wa fedha 2020 zilizopo katika hesabu namba 021103000475 ya Bodi ya Mapato Zanzibar iliyopo katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Kutokana na kuwepo kwa taarifa hiyo, ukaguzi umebaini haukuweza kuona jitihada zilizochukuliwa na Bodi ya mapato katika kuhakikisha kuwa fedha hizo zinafanyiwa usuluhishi wa kibenki, ambapo katika taarifa ya hesabu hazikuweza kuonekana.

Majibu ya Bodi

Jumla ya shilingi 127,887,545.00 ni fedha ambazo zimeingia kimakosa kwenye hesabu nambari 021103000475 (hesabu nambari 021103000475 kwa sasa inajulikana kwa namba 0404003000) (retention account) iliyopo PBZ kutoka kwa walipa kodi mbali mbali ambazo ni malipo ya kodi. Fedha hizo hubakia kwenye hesabu hiyo mpaka pale walipa kodi wanapokuja kufanya uhakiki wa malipo yao ndio hutolewa kwenye hesabu hiyo na kuingizwa kwenye hesabu nambari 9928130504 iliyopo BOT au 0404003001 iliyopo PBZ. Hata hivyo, fedha hizo zimehaulishwa kutoka hesabu nambari 021103000475 iliyopo PBZ na kuingizwa kwenye hesabu nambari 9928130504 iliyopo BOT.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya LAAC imesikitishwa kwa Taasisi kubwa ya Bodi ya Mapato Zanzibar, kawaida hushindwa kufanya usuluhishi wa kibenki hadi pale anapotokezea mteja kulalamika kuwa amelipa deni lake au laa. Kutofanya usuluhishi wa kibenki kunaweza kuisababisha Bodi kushindwa kufahamu kwa wakati matatizo yaliyojitokeza katika ulipaji miamala tofauti na kuyapatia ufumbuzi haraka kabla ya kusababisha hasara kwa Bodi. Aidha,

Kamati imegundua kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar imefanya malipo ya kasoro zilizojitokeza nje ya wakati uliotakiwa wa mwezi wa Juni, 2020 badala yake imerekebisha kasoro hizo tarehe 3 mwezi wa Mei, 2021.

Mapendekezo ya Kamati

Bodi ya Mapato Zanzibar ijiwekee utaratibu wa kufanya usuluhishi wa taarifa zake za kibenki kila baada ya mwezi mmoja ili kujipatia hesabu sahihi na kamili ya fedha zake.

(b) Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha uwepo wa deni la wadai shilingi 4,520,873,299

Ukaguzi umebaini uwepo wa deni la shilingi 4,520,873,299 ambalo limeripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka lakini vielelezo vya kuweza kuthibitisha uwepo wa deni hilo havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha ukweli na usahihi wa kiasi kinachodaiwa. Orodha ya wadai hao wanaonekana katika Jadweli lifuatalo:

Nam.	Maelezo	Mwaka wa fedha 2019/2020 (Tzs.)
1.	Rahisi Solution Ltd.	71,486,995
2.	Advent Construction Ltd.	1,200,000,000
3.	BITZ Company Ltd.	49,386,304
4.	Norway Registers Devas	3,200,000,000
Jumla		**4,520,873,299**

Majibu ya Bodi

Jumla ya shilingi 4,520,873,299.00 ni deni linalodaiwa ZRB kutokana na huduma/bidhaa zilizotolewa kutoka kwa wadai. Baada ya kukamilika kazi kwa awamu na kutolewa stakabadhi (certificate) na kujiridhisha na kazi iliyofanywa, malipo hufanyika. Deni hili limeripotiwa kwenye hesabu za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa IPSAS, Financial Regulation na Accounting Manual ya ZRB. Hata hivyo, deni hili halikulipwa kutokana na kutokamilika kwa kazi kwa mujibu wa mikataba.

Uchunguzi wa Kamati

Kutokana na majibu yaliyotolewa na ZRB, Kamati ilitaka kujua utaratibu mzima wa ukusanyaji malipo kwa mtoa huduma, na kubaini kwamba kwa mujibu wa viwango vya ukaguzi vinamtaka Mshauri Elekezi kuwasilisha “invoice” ya deni analodai na ZRB kuweka kumbukumbu zake lakini malipo ya huduma iliyotolewa hufanyika baada ya kukamilisha mkataba. Hata hivyo, Kamati iliweza kupatiwa vielelezo hivyo kwa ukaguzi.

Pamoja na Kamati kuoneshwa vielelezo hivyo, Kamati ilitafakari zaidi na kushangazwa kwamba kwanini Mkaguzi alipopita hajaviona vielelezo hivyo hadi kufikia hoja hiyo kuingizwa katika ripoti cha Mdhibiti. Kutokana na hali hiyo, Kamati ilipata wasawasi juu

ya usahihi wa vielelezo husika na kushindwa kukubaliana navyo.

Mapendekezo ya Kamati
Bodi ya Mapato Zanzibar iwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi vielelezo ili vinapohitajika kwa ukaguzi viweze kupatikana kwa wakati.

3.3.3: Taarifa ya Madeni ya Kodi

(a) Madeni ya Kodi ya Muda Mrefu shilingi 27,322,335,187
Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 27,322,335,187 ni madeni ya muda mrefu ya walipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kati ya deni hilo shilingi 26,384,159,034 ni fedha zilizolipwa na walipa kodi kimakosa kwenda katika hesabu za TRA Dar - es - Salaam badala ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na shilingi 938,176,153 ni deni ambalo halijalipwa. Kushindwa kukusanya madeni ya kodi kunapekelea Serikali kukosa mapato yanayotokana na kodi.

Wadaiwa wa kodi za muda mrefu wa Bodi ya Mapato Zanzibar ni Dezo Construction (shilingi 897,388,659 hazijalipwa), Dullar Motors Limited (shilingi 40,787,494 hazijalipwa), MIC (Tigo - shilingi 14,500,000,000 kodi ya VAT iliyolipwa TRA DSM kimakosa) na VAT (shilingi 11,884,159,034 ikiwa ni kodi ya VAT iliyolipwa TRA DSM kimakosa.

Majibu ya Bodi
TRA tayari washalipa deni ambalo lilistahiki kulipwa kwa mujibu wa sheria. Hivyo, deni ambalo limebaki ambalo ZRB inaidai TRA ni deni la kampuni ya HTT ambapo ni Tzs.1.7 bilioni. Aidha, Hazina SMT imewaamuru TRA ililipe kwa utaratibu wa marejesho. Aidha, kuhusu deni la VAT la 11.8 bilioni TRA wameiandikia barua ZRB kwa mujibu wa sheria TRA hawana mamalaka ya kulilipa deni hilo kwa barua ya tarehe 9 Julai 2021 yenye kumbukumbu namba **BA.86/510/01A/84.**

Uchunguzi wa Kamati
Kamati imegundua kwamba kuna mgongano wa sheria zinazosimamia ulipaji wa kodi ya VAT kwa Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania ulioanza mwaka 2015, baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya marekebisho ya sheria ya VAT. Awali, kodi ilikuwa ikikusanywa kule eneo ambalo bidhaa husika inaenda kutumika lakini kutokana na mabadiliko ya sheria husika, hivi sasa kodi inayokusanywa Tanzania Bara kwa bidhaa zinazokuja kutumika Zanzibar zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa matumizi ya Tanzania bila ya

kuletwa Zanzibar kama ilivyokuwa awali.

Mwaka 2012, ZRB ilibadilisha sheria yake na kuzitaka Kampuni na Taasisi zinazolipa kodi kulipa kule sehemu ambayo huduma inatolewa. Kwa mnasaba huo, Kampuni ya simu ya Tigo haijalipa kodi yake ZRB tangu mwaka 2009 hadi 2012 kwa madai kwamba walikuwa hawana Ofisi Zanzibar.

Mapendekezo ya Kamati

1. Bodi ya Mapato Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inalipeleka suala la mgongano wa sheria za VAT katika Kamati Maalum inayoshughulikia kero za Muungano ili lipatiwe ufumbuzi wa haraka.

2. ZRB ihakikishe inatafuta mbinu muafaka zitakazowezesha madeni yote yanayodaiwa yanalipwa ili yaweze kuongeza mtaji wa ZRB.

(b) Madeni ya Kodi ya muda mrefu ambayo hayajasuluhishwa shilingi 20,515,860,319 na dola za kimarekani U$D 4,110,033

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 20,927,104,389 na dola za kimarekani 4,135,033 ikiwa ni madeni ya muda mrefu ya walipa kodi ambayo yapo katika malalamiko. Aidha, katika ufuatiliaji wa madeni hayo, jumla ya shilingi 411,244,070 na dola za kimarekani 25,000 zililipwa na wadaiwa hao.hata hivyo, tathmini ilionesha kwamba jumla ya shilingi 20,515,860,319 na dola za kimarekani 4,110,033 ikiwa ni bakaa la deni ambalo limeshindwa kulipwa na walipa kodi kwa wakati.

Majibu ya Bodi

Madeni ya kodi ya muda mrefu hayo ni madeni ambayo yalikuwa na migogoro na mengine yalikuwa na kesi mahakamani. Katika deni hilo tayari Tzs. 4.7 bilioni zishalipwa ambalo limetokana na deni la jumla la TZS 14.0 bilioni kutoka katika Kampuni ya MIC (T) Ltd. Kwa mujibu wa Sheria deni hilo halipo tena kutokana na barua ya tarehe 27 Oktoba, 2021 reference namba BA.86/510/01A/96. Katika deni lilikuwa mahakamani ambalo ni Deni la My blue lishafanyiwa mapitio na ishatolewa ripoti ya ukaguzi tarehe 1/11/2021. Deni la Dezo lishafanyiwa mapitio hatua za kuligomboa zimechukuliwa za kutumia njia ya payment by third party kama sheria inavyoelekeza katika njia za ugomboaji wa madeni. Aidha madeni yaliyobaki yamepoteza sifa kwa mujibu wa sheria ya Public Finance Act No. 12 ya mwaka 2016.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati haikufurahishwa kabisa na uwepo wa madeni ya muda mrefu tangu mwaka 2014 na yenye fedha nyingi ambazo kama zingepatikana zingekuza mtaji na kuimarisha utendaji wa ZRB. Aidha, Kamati imeendelea kujiuliza inakuwaje kwa Taasisi kubwa ya

ZRB kushindwa kufanikisha ulipwaji wa madeni hayo hadi yanafikia kupitwa na miaka mingi na kupelekea kuondolewa au kufutwa. Kwa kweli hicho ni kitendo cha aibu kwani kinaweza kuleta picha kwamba huenda kuna hujuma ya makusudi inafanywa ya kuchelewesha au kuzuia juhudi za ulipwaji wake ili wachache wajinufaishe kibinafsi.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kampuni zinazotoka Tanzania Bara kuja kufanya kazi Zanzibar ziwekewe utaratibu wa kuweka dhamana (guarantee) ya fedha ili zitakaporudi kwao ziweze kutumika kama fidia kwa Bodi ya Mapato.

2. Taasisi za Tanzania Bara zikifanya kazi Zanzibar ziwekewe utaratibu wa kulipa kodi ya mwaka mzima ili kuepusha madeni yasiyolipika zinapokimbia.

3. ZRB ifuatilie Tanzania Bara kampuni zote zilikuwa zinadaiwa na kukimbilia Dar-es -Salaam na kama Sheria zinaruhusu basi wawashitaki.

4. Kwa vile Kamati haikuridhishwa na majibu ya ZRB, bado inasisitiza madeni inayodai ihakikishe yanalipwa kwa maslahi ya Zanzibar.

UKAGUZI MWENGINE

Tarehe 29 Januari, 2022, Kamati ilipatiwa mafunzo na Bodi ya Mapato Zanzibar kuhusiana na Mfumo wa ukusanyaji wa mapato yao kutoka kwa walipa kodi waliosajiliwa (VFMS) na kubaini mambo yafuatayo:

1. Mfumo huo umeandaliwa na wafanyakazi wazalendo kutoka Bodi ya Mapato Zanzibar, Taasisi za Serikali pamoja na kijana mtaalamu binfsi ambaye bado hajaariwa.

2. Kuwepo kwa Mfumo huo, utaweza kuisaidia Wizara ya Fedha na Mipango na Serikali kwa ujumla kuweza kukadiria mapato kulingana na uhalisia ulivyo na kuondokana na desturi ya kufanya makadirio pasi na kuangalia mwenendo wa uchumi upo vipi.

3. Ili kuhakikisha mfumo unakuwa endelevu, Bodi inataka watendaji wa mfumo huo wote wawe wafanyakazi wa ZRB. Kuwepo kwa wafanyakazi wanaotoka nje ya ZRB kunasababisha ugumu katika utekelezaji na uendelezaji wa mfumo huo. Kutokana na hali hiyo, Mradi kutoka nchi ya Norway (Norway Tax Authority) ulikuwa tayari kuwasaidia kwa kuwapatia mafunzo timu hiyo ya wataalamu lakini ilishindikana kwasababu walitaka wafanyakazi wa kudumu kutoka ZRB ili iwe rahisi kwao kuwafundisha wengine walio chini yao.

4. ZRB imeshindwa kumuajiri kijana ambaye ni mtaalamu waliomtumia katika maandalizi ya mfumo huo. Kinachoshangaza, inafika mwezi wa 8 mchakato wa ajira bado haujakamilika ambapo hata GSO hajapelekwa wakati kuna Taasisi nyingi zinamuhitaji wakamuajiri.

5. ZRB waliandaa mfumo huo kwa gharama nafuu sana ambazo hazijafikia hata milioni 300 kwa kuwatumia wazalendo lakini mfumo kama huo ulitaka kuundwa ambao haukufanikiwa ulioandaliwa na wageni ulifikia dola za marekeni 1.3 bilioni na ambao usalama wake ulikuwa mdogo sana.

6. Wafanyakazi wanaoshughulikia mfumo huo wapo 6 ambao kutokana na majukumu waliyonao, hulazimika kufanyakazi kwa muda mrefu pasi na kupata nafasi ya kupumziko. Jadweli lifuatalo linaonesha idadi ya Wafanyakazi hao na shughuli wanazofanya:

Nam.	Idadi	Anachokifanya	Anapotoka
1.	1	'Back End Development'	Hana ajira
2.	1	POS	Shirika la Bandari
3.	1	'Tax Payer Portal'	Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma
4.	1	'Management Portal'	ZRB
5.	1	Úwekaji kumbukumbu	ZRB
6.	1	Usimamizi	ZRB

Aidha, wapo wafanyakazi wengine ambao wanasaidia wataalamu hao ambao nao pia wameazimwa kutoka katika Taasisi nyengine za Serikali ambapo mmoja anatokea TAMISEMI anayeshughulikia 'Back End Developer, mmoja kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) kwa ajili ya 'Management Portal' na mmoja anatoka Uchapaji ambaye anashughulikia 'POS'.

7. Wafanyakazi wanaotoka Taasisi nyengine wanatakiwa warudi katika Ofisi zao huku wakihitaji kutekeleza majukumu ya uendeshaji wa mfumo huo.

8. Mfumo huo ulikuwa umekamilika tokea Julai, 2021 ili haukuanza ukifanyakazi kwasababu vifaa vyake vilikuwa bado lakini kwasasa wameingia mkataba na kampuni tatu kwa ajili ya uletaji viaa hivyo na tayari kuna takriban vifaa mia tisa

wameshakuwa navyo.

9. Kukamilika kwa mfumo huo, utaondoasha baadhi ya changamoto zilizopo hususan za kutojisajiliwa kwa wageni hotelini.

10. ZRB ina mpango wa kuunganisha mfumo huo na uhamiaji Zanzibar ili kupata taarifa za wageni wanaoingia nchini na wapi wanaenda (wenyeji wao).

11. Mfumo unaweza kuona kodi zote zinazolipwa na walipa kodi waliosajiliwa.

Mapendekezo ya Kamati

1. Bodi ya ZRB ihakikishe inaharakisha kumuajiri mfanyakazi mtaalamu alokuwa hajaariwa ili kuepusha kuchukuliwa na Mamlaka nyengine.

2. ZRB ihakikishe inaupatia ulinzi wa hali ya juu mfumo wanaoutumia ili kuepusha upotevu wa fedha za walipa kodi.

3. ZRB iharakishe inakamilisha hatua za kuunganisha Mfumo huo na Mfumo wa Uhamiaji ili waweze kuwatambua wakwepaji kodi na kuongeza mapato maradufu.

4. ZRB ihakikishe inapeleka Serikalini maombi ya kuwafanyia uhamisho watendaji wa Serikali ili wahamie katika Ofisi yao kwa lengo la kuuendeleza na kuusimamia Mfumo.

3.4: SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR (ZIC)

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umefanya uchambuzi wa ukusanyaji wa mapato ya Shirika la Bima la Zanzibar na kubaini mapato hayo yameongezeka hadi kufikia 19,853,482,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 19,220,931,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 kukiwa na ongezeko la shilingi 632,551,000 sawa na asilimia 3.29 ya ongezeko.

Majibu ya Shirika

Mapato ya Shirika yanatokana na vionzio vyake mbali mbali ya mauzo ya Bima za magari, Bima za kinga ya moto, Bima mchanganyiko pamoja na faida zinazotokana na uwekezaji kama zinavyoonekana katika mchanganuo ufuatao:

Aina ya Bima	Makisio	Mapato halisi	Asilimia ya makusanyo 2019
Bima za magari	25,272,274,415	19,134,964,000	75%

Bima za kinga ya moto	1,187,260,205	1,184,843,000	99%
Bima za meli	881,745,950	2,050,007,000	232%
Bima mchanganyiko	673,945,744	951,698,000	141%
Bima za uwekezaji	863,966,759	1,316,426,000	152%
Jumla	**28,879,193,075**	**24,637,938,000**	**85%**

Mapato ya Shirika yameongezeka kutokana na sababu kwamba Shirika limechukua juhudi za kuzitangaza huduma zake katika vyombo vya habari na kupelekea wananchi wengi kupata uelewa, Aidha, kuongezeka kwa Bima katika meli, gari, uwekezaji pamoja na bima za moto kumekuza zaidi mapato hayo.

Uchunguzi wa Kamati

Awali, Kamati ilipatiwa na Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) taarifa ya mapato na matumizi ya miaka miwili inayoanzia mwezi wa Januari 2019 hadi Disemba 2020. Baada ya kuhoji kwanini kuna utofauti katika utoaji taarifa za ukaguzi, Kamati ilielezwa kwamba kuna Mashirika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yanafuata sheria zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wa majukumu yake. Sheria huzitaka Taasisi kutoa taarifa ya ukaguzi ya miaka miwili miwili inayoanzia mwezi wa Januari, kwa vile Shirika la Bima linafuata sheria ya Usimamizi wa Bima Tanzania ya mwaka 2009 iliyoanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) linalazimika kufuata utaratibu huo.

Katika mazingira hayo, Kamati imebaini kuwa utofauti uliopo katika kuripoti taarifa unaleta utata na unakwaza utekelezaji wa kazi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa vile hulazimika kuanzia mwezi wa tatu kuwasiliha kitabu kwa Rais.

Kamati pia imegundua Shirika halikufanya vizuri sana katika utoaji uelewa wa huduma ya bima za viwandani kwani mwamko wa suala hilo kwa wananchi wetu bado upo chini na kupelekea mapato yake kuwa machache sana. Kadhalika, Kamati imebaini tayari shirika limeshaiandikia barua Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusiana na ukataji wa bima kwa skuli mpya walizojenga ili kuzilinda na majanga iwapo yatatokea lakini hadi Kamati inamaliza ukaguzi wake bado barua hiyo haijajibiwa.

Katika hatua za kuzuia upotevu wa mapato, Kamati imegundua Shirika limeuimarisha mfumo wake wa utoaji huduma za bima kwa kutoa bima za kielektroniki kwa vyombo vya moto, ambazo hazitumii stika za kubandika kwenye kioo. Kufanya hivyo kutaliwezesha Shirika kuzuia udanganyifu kwa wafanyakazi na wananchi wanaokwepa kukata bima sahihi kwa Mawakala halali wa Shirika.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kuepusha changamoto zilizojitokeza, Kamati inapendekeza yafuatayo kwa Shirika letu la Bima la Zanzibar.

1. Taarifa za ukaguzi za Mashirika yanayoongozwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ziwe zinawasilishwa kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kutoa nafasi kwa Mkaguzi kupata muda wa kuzikagua ipasavyo.
2. Shirika litoe uelewa wa kutosha kuhusu ukataji wa bima katika viwanda ili waweze kukingwa na majanga yakitokea.
3. Vyanzo vilivyofanya makusanyo vizuri viimarishwe na viendelezwe ili vizidi kuzalisha faida zaidi.
4. Shirika lihakikishe mfumo wa ukataji bima unakuwa unapatikana wakati wowote.
5. Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar inashauriwa izikatie bima skuli zake mpya 19 katika Shirika la Bima la Zanzibar.

Taarifa ya Matumizi

Ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji zimepungua hadi kufikia shilingi 16,914,971,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia 2019 ukilinganisha na shilingi 17,109,002,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 ambayo ni ubungufu wa shilingi 194,031,000 sawa na asilimia 1.13.

Majibu ya Shirika

Kwa mwaka wa fedha 2019, Shirika limetumia jumla ya Tzs. 7.3 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya Tzs. 7.7 bilioni yaliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika.

Upungufu huo wa matumizi ya Shirika, ulisababishwa na biashara nyingi zilisajiliwa au kufanyika Makao Makuu ya Shirika badala ya kupitia kwa Mawakala na kupelekea kupunguza gharama za malipo kwao. Aidha, walilipa ujira mdogo kwa magari yaliyopata hitilafu kufikia jumla ya shilingi 12.5

Vile vile watendaji waliikumbusha Kamati kwamba mshahara wa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika ulipunguzwa kutokana na maelekezo ya Serikali ya kupunguza maslahi ya baadhi ya watendaji wa Mashirika ya Serikali.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kupitia majibu ya hoja za Mdhibiti, Kamati ilitaka kujua miradi ya maendeleo ya Shirika ambapo Mdhibiti hakuionesha katika kitabu chake. Shirika lilieleza kuwa lilitekeleza mradi wa ujenzi wa jengo jipya la Shirika katika eneo la Mkungu Malofa Chake chake - Pemba. Hata hivyo, ujenzi huo umesitishwa na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia barua nambari FH.101/237/01/2/4 ya tarehe 25 Agosti, 2020 iliyosainiwa kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuelezwa kuwa eneo hilo ni dogo halitoshi kwa ujenzi uliokusudiwa isipokuwa watapatiwa eneo jengine.

Kamati haikuridhishwa na jawabu ya kwamba eneo halitoshelezi kwa ujenzi wa Ofisi yao kwani ilipotaka ufafanuzi wa hilo ilielezwa kwamba eneo linatosha isipokuwa Serikali iliona ifanye maamuzi hayo kwasasa.Wakati Wizara ya Fedha na Mipango inatoka amri ya kusitisha, Shirika tayari limeshatumia shilingi 115 milioni kwa ajili ya gharama za awali za matayarisho ya ujenzi ikiwemo kulisafisha eneo na uchoraji wa ramani. Hatimaye barua ilielekeza kwamba watapatiwa eneo jengine na Afisa Mdhamini wa Wizara ya Fedha na Mipango katika maeneo ya Tibirinzi au Gombani ambapo hadi kamati inamaliza ukaguzi wake bado eneo hilo halijapatikana.

Kamati katika uchunguzi wake imebaini, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Shirika pia lilitekeleza mradi mwengine wa ununuzi wa mfumo wa Bima (CIMIS) kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wateja wake ambapo jumla ya shilingi 1,546,980,000 zilikuwa ni gharama zilizopangwa kutumika awali. Hata hivyo, Shirika lililazimika kuziongeza gharama hizo hadi kufikia shilingi 1,665,378,124. Kutokana na sababu zifuatazo:

1. Shirika lilikabiliwa na maelekezo na mahitaji kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya kuzitaka Mashirika ya Bima yote kuacha kutumia EFD mashine badala yake waunganishe mifumo yao na mfumo wa VFD;
2. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kutanua wigo wa taarifa wanazozihitaji na kulazimika Taasisi zote kufanya muunganiko na mfumo wa bima uitwao TIRA MIS na kulazimika bima zote kutoka kwa njia ya kielektroniki;
3. Kutumia mfumo wa kielektroniki kulipa mishahara ya wafanyakazi; na
4. Shirika lilipokea agizo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango la kufanya muunganiko wa mfumo wa malipo wa Serikali (ZanMalipo).

Mapendekezo ya Kamati

Katika jitihada za kuhakikisha Shirika linatekekeleza vyema majukumu yake na kupunguza matumizi, Kamati ilipendekeza yafuatayo:

1. Shirika ifuatilie ipasavyo kwa Afisa Mdhamini wa Wizara ya Fedha na Mipango ili

wapatiwe kiwanja cha kutosha kujenga Ofisi yao Pemba lakini eneo hilo liwepo eneo la kibiashara la mjini.

2. Shirika liharakishe kujenga katika eneo jipya ili kuepusha kufanya kazi katika majengo ya kukodi ambayo yanapunguza faida ya Shirika.
3. Ili kuendelea kupunguza matumizi, Shirika litafute njia bora zinazopunguza matumika katika utekelezaji wa majukumu yake.
4. Kwa vile Shirika lilikuwa liashatumia gharama katika maandalizi ya kiwanja cha zamani, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inalifidia Shirika kiasi cha fedha ilichokipoteza.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA SHIRIKA LA BIMA

(a) Ufanisi katika uendeshaji wa Shirika (Operating Performance)

Ukaguzi umepima utendaji wa Shirika kwa kufanya tathmini ya miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 na Disemba 2019, na kuonekana kuna faida ilipatikana kutoka shilingi 1,193,345 kwa mwaka 2018 hadi 2,112,944 kwa mwaka 2019.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa ukusanyaji mapato wa Shirika umeongezeka kufikia shilingi 19,853,482,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukulinganisha na shilingi 19,220,931,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 kukiwa na ongezeko la shilingi 632,551,000 sawa na asilimia 3.29 ya ongezeko.

Kwa upande wa matumizi, ukaguzi umebaini kupungua kwa gharama za uendeshaji kutoka shilingi 16,914,971,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 17,109,002,000 kwa mwaka wa fedha ulioishia Disemba 2018 ambao ni upungufu wa shilingi 194,031,000 sawa na asilimia 1.13.

Majibu ya Shirika

Kamati imegundua kwamba majibu ya hoja hii yanalingana na majibu ya awali kuhusu kuongezeka kwa mapato na kupungua kwa matumizi ya Shirika yanayopatikana katika hoja ya taarifa ya mapato pamoja na hoja ya taarifa ya matumizi yaliyoelezwa hapo juu. Hivyo, Kamati haikuwa na maelezo ya ziada.

(b) Ufanisi katika utendaji wa kifedha

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlingano wa msimamo wa mtaji (position of working capital) wa Shirika kwa muda wa

miaka miwili ambapo kwa mujibu wa vigezo vya khasibu mlingano huo unatakiwa ufikie wastani wa 2.01.

Kutokana na hali hiyo, ukaguzi umebaini kwamba uwezo wa Shirika kumudu kulipa madeni ya muda mfupi umepungua kufikia uwiano wa 1.06:1 kwa mwaka wa feha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na uwiano wa 1.2:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018. Kwa wastani huo, imebainika kuna upungufu wa uwezo wa Shirika kuweza kumudu kulipa madeni yake ya muda mfupi. Kama hali hiyo itaendelea, Shirika linaweza kushindwa kumudu kulipa madai ya bima (insurance claims) kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

Majibu ya Shirika

Watendaji wa Shirika walieleza kwamba Shirika lina mtaji wa kutosha kuhimili ulipaji wa madeni yake ya muda mfupi kwani mtaji uliopo unatosheleza. Hata hivyo, walieleza kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipokagua aliangalia zaidi uwezo wa fedha taslim lakini hakuzingatia uwezo wa mtaji unaotokana na thamani ya majengo na mali nyengine zilizowekezwa na Shirika. Aidha, biashara za bima kwa kipindi hicho zilitetereka na kupunguza faida iliyotarajiwa.

Kadhalika, Shirika lilieleza kwamba sababu zilizopelekea uwiano wa mtaji wao kushindwa kufikia wa 2.01, kumechangiwa na kutoa zaidi ya shilingi milioni 260 katika kampuni ya Uvuvi ambayo uendeshaji wake unasuasua.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na sababu zilizoelezwa na Shirika kuhusu upungufu wa mtaji wake, Kamati imebaini kuwa mtaji wa Shirika ulilazimishwa utumike kulipia gharama zisizostahiki za U$D 913,142 kwa ajili ya bima kwa MV. Mapinduzi II wakati Shirika la Meli halijalilipa Shirika la Bima U$D 100,000 kama walivyokubaliana huku tayari meli hiyo ilikuwa imeshapata ajali mara tatu tokea 2016 ilipopatiwa kinga na Shirika (barua nambari ZIC/A.98/W.F/VOL.XIV/57/20 ya tarehe 09 Oktoba, 2020 inahusika).

Kamati ilishitushwa na maelezo hayo na kugundua kwamba Shirika la Bima ni Shirika linalojitegemea katika utendaji wake lakini kujitegemea huko kumebakia katika maelezo tu na sio kivitendo kwa vile Serikali huingilia mipango na maamuzi Shirika na sio kulipatia mashirikiano ya kutosha ili liweze kuwa katika nafasi nzuri ya kutoa gawio kupitia faida itakayopatikana.

Aidha, kupitia barua niliyoitaja hapo juu Kamati iligundua kuwa hata Mashirika Mtawanyo walikataa kushirikiana na Shirika la Bima la Zanzibar kuikatia bima meli hiyo

kwa sababu zifuatazo:

(a) Taarifa ya 'renewal'inachelewa kuletwa katika Shirika la Bima jambo ambalo linapelekea kuchelewa kutolewa jibu la 'risk acceptance'.
(b) Madai ni mengi na makubwa kupelekea makampuni ya Bima kuendelea kupata hasara.
(c) Ada za malipo zinachelewa kulipwa na zinalipwa kwa vipingili na makubaliano ya ulipwaji haufuatwi, kwa mfano MV. Mapinduzi II hadi tarehe ya barua hiyo ilishindwa kuwasilishiwa kipingili cha pili.
(d) Gharama za madai zinazowasilishwa ni kubwa ukilinganisha na hasara.

Kamati imebaini zaidi kwamba Shirika lilikuwa likikataa kutoa fedha kwa ajili ya kinga ya meli isiyokuwa na sifa ila liliambiwa maagizo hayo yametoka juu na kuelekeza fedha zitolewe na Shirika kulipia meli hiyo.

Kupitia barua ya tarehe 9 Juni, 2020 yenye kumbukumbu nambari MOICT/M.120.C.2/VOL.VIII/115 iliyopelekwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima Zanzibar kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iliyoitaka Shirika kuzipatia kinga Meli za Serikali kutokana na maelekezo ya Serikali ikiwemo MT. Ukombozi. Kamati haikuridhishwa na utendaji wa aina hiyo ambapo mbinu kama hizo hutumiwa na wajanja kuingilia uhuru wa Mashirika ya Serikali kwa kuchukua fedha na hatimaye kuyaacha yanashindwa kutoa gawio Serikalini.

Kadhalika, Kamati imegundua Shirika la Bima linakwazika katika utekelezaji wa majukumu yake kutokana na kukosa ruhusa (Kanuni) ya kuanzisha Bima ya Kiislamu (Takkaful), ambapo kuna wateja wengi hususan Zanzibar wanashindwa kujiunga na huduma za Bima kwa sababu uendeshaji wake unakinzana na imani zao, hivyo hutoa ushauri wa kuanzishwa bima ya kiislamu. Hali hiyo inatokana na kukwama kwa Sheria ya Bima ya Kiislamu katika Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shirika linapotezea mapato mengi kutokana na kuwepo changamoto hiyo hasa ukizingatia zaidi ya asilimia 90 ya wakaazi wa Zanzibar ni Waislamu.

Sambamba na hilo, kuwepo agizo kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwamba vyombo vyote vya moto vya Serikali hususan gari zinatakiwa zikatiwe bima Shirika la Bima la Zanzibar lakini Kamati imegundua bado kuna vyombo vya moto vinashindwa kutii agizo hilo na kuamua kutokata bima katka Shirika. Kufanya hivyo ni njia moja ya kulikosesha mapato Sirika.

Mapendekezo ya Kamati

1. Miradi mikubwa ya uzalishaji faida (MV. Mapinduzi II) kabla ya kuanza utekelezaji wake iandaliwe mpango wa kibiashara ili iweze kufanyakazi kwa manufaa ya Taifa.

2. Miradi mikubwa inayofanyika Zanzibar ikiwemo uwekezaji katika rasilimali ya mafuta ukatiwe bima katika Shirika la bima la Zanzibar.
3. Serikali iyaachie huru Mashirika yake kiutendaji pasi na kuyaingilia katika madaraka yaliyonayo kisheria ili yaweze kuzalisha faida na kutoa gawio Serikalini.
4. Watendaji wa Serikali (Wakuu wa Idara/Taasisi na vitengo vya manunuzi) wanapoingia zabuni wahakikishe miradi hiyo inakatiwa bima katika Shirika la Zanzibar.
5. Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar ikutane na Wizara inayoshughulikia Fedha Tanzania ili kulipatia ufumbuzi suala la bima ya Kiislamu kwani likuwa la muda mrefu.
6. Kamati inaungana na Serikali kuendelea kuunga mkono agizo la Serikali la vyombo vya moto vya Serikali kukata bima Shirika a bima la Zanzibar na kuendelea kuisisitiza Serikali kuvichukulia hatua vyombo vyote visivyotii agizo hilo.

MATOKEO YA HOJA

3.4.1 Kuchelewa kuwasilishwa kwa taarifa za hesabu kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016 kifungu cha 119(1) kinaeleza wajibu wa Taasisi kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha husika.

Majibu ya Shirika

Kufuatia uwepo wa idadi kubwa ya Mawakala na Madalali walioenea Tanzania nzima. Kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa taarifa kwa wakati sahihi hivyo kupelekea kuchelewesha kuandaa hesabu kwa wakati na kuziwasilisha kwa Mkaguzi. Katika jitihada za kutatua changamoto hiyo, Shirika lililazimika kutafuta mfumo mpya wa kielektroniki utakaoweza kukidhi mahitaji ya Shirika ikiwemo kukamilisha zoezi la ufungaji wa hesabu na kuziwasilisha Afisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa vile Shiriki lilikiri juu ya hoja hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kueleza kuwa hatua za kuweka na kutumia mfumo mpya wa kielektroniki umeshaanza, Kamati ilitaka kujua kama kuna faida gani inayopatikana kwa kutumia mfumo huo, ni kwamba mfumo una unawawezesha wahasibu kuona makusanyo yaliyofanyika kiurahisi na kwa wakati bila ya kwenda eneo la kukusanyia. Hata hivyo, mfumo unakabiliwa na changamoto ya kujitokeza ‘delay’ katika ufanisi wake.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika lihakikishe inaifanyia kazi ipasavyo changamoto ya 'delay' ya mfumo ili kuepusha usumbufu kwa wateja na Mawakala.

3.4.2 Kushindwa kufanya ufuatiliaji wa malipo kwa wakati kutoka kwa Mawakala na Madalali.

Ukaguzi umebaini kwamba kupitia kitengo cha masoko makusanyo makubwa ya Fedha bado yanabakia mikononi mwa Madalali na Mawakala wa Bima katika Matawi yote ya Shirika la Bima la Zanzibar, jambo ambalo linaweza kupelekea kushindwa kulipa madeni ya muda mfupi na hatimae kushindwa kulipa madai ya Bima kwa wakati kwa mujibu wa Sheria. Ukaguzi umebaini kwamba kitengo cha masoko hakikuchukua jitihada kuhakikisha kwamba Fedha zote zilizopo mikononi mwa Mawakala na Madalali zinawasilishwa kwa wakati kwa mujibu wa sharia.

Majibu ya Shirika

Kutokana na changamoto zilizojitokeza katika ukusanyaji wa malipo ya ada ya Bima kwa wakati, hatua zifuatazo zilichukuliwa:

- Kuanzishwa kwa kitengo maalumu cha Shirika kitakachosimamia ukusanyaji wa madeni ya Mawakala na Madalali.
- Kuanza rasmi utaratibu wa malipo ya ada za Bima kwa njia za Kidigitali.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati haikufurahishwa na kitendo cha kubakia mapato mikononi mwa Mawakala na Madalali bila ya kuyawasilisha katika Shirika kwa wakati kwani kufanya hivyo kunaweza kutoa mwanya wa kutumika vibaya fedha za Shirika kwa maslahi binafsi hasa ukizingatia changamoto hiyo imetokana na kukosekana kwa ufuatiliaji wa karibu wa kitengo cha masoko cha Shirika. Kutokana na hali, Kamati ililazimika kuifuatilia kwa undani hoja hii kwa kufanya ziara ya kikazi Shirika la Bima Tawi la Dar - es - Salaam ili Kamati ikutane na kuwasikiliza Mawakala na Madalali hao.

Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na Shirika kuanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji mapato kutoka kwa Mawakala, Kamati imelishauri Shirika mambo yafuatayo:

1. Shirika liwe na mpango mzuri wa kuwafuatilia Mawakala na Madalali wao ili waweze kutambua changamoto zinazowakabili mapema na kuzisawazisha kabla hachelewa.
2. Kwa vile Shirika linahitaji kuwa na Mawakala, Shirika liweke utaratibu wa

kuwakata madeni yao katika malipo yao.

3. Kutokana na kubadilika kwa mfumo wa ukusanyaji mapato, Shirika lihakikishe linawapatia Madalali na Mawakala mafunzo ya kutosha ili kuepesha kurudi nyuma katika mfumo wa 'manual'.

3.4.3 Malipo ya madai yaliyolipwa kinyume na Sera ya Madai ya Shirika la Bima Tzs: 87,613,000

Katika ukaguzi uliofanyika kulifanyika tathmini ya madai yaliyolipwa na Shirika la Bima la Zanzibar kwa mwaka wa Fedha unaoishia Disemba 2019, ukaguzi umebaini kwamba malipo ya madai yaliyolipwa na Shirika kwa wateja mbali mbali waliopata ajali yalifanyika kinyume na Sera ya Bima ya Magari.

Aidha, imebainika Shirika limefanya malipo kwa mtu aliyepata ajali (third Party injuries/death to a pedestrial) ambayo hayakuoneshwa kwenye Sera ya Bima ya Magari.

Tawi la Dar - es - Salaam lilipa shilingi 57,500,000 ikiwa ni malipo ya uharibifu wa gari na ukokotaji gari namba T 218 CVF (Dai namba 020/080/9/162070/2010/2019 hati ya malipo nambari. 075341/2019 hundi nambari 277277), Tawi la Mwanza lilipa shilingi 5,000,000 ikiwa ni malipo kwa ajili ya kifo cha Abdoni Joviti Kalinjuna, kilichotokana na ajali ya gari nambari T181CEK (Dai nambari 020/088/9/157856/2019 hati ya malipo nambari 07533/2019 hundi nambari 977276).

Kwa mara nyengine Tawi la Dar - es - Salaam lilipa shilingi 25,113,000 ikiwa ni malipo ya madai baina ya Grace Sumailai V/S Taqwa bus Service kesi nambari 326 ya mwaka 2018 (Dai nambari 050/088/9/132317/2017 na vocha namba 067177/20 hundi namba 997876).

Majibu ya Shirika

1. Dai namba 020/080/9/162070/2010/2019 hati ya malipo nambari 075341/2019 hundi nambari 277277. Jumla ya Tzs. 87,613,000 ni kiwango kilichowekewa bima ''Sum insured''. Kiasi kilicholipwa kwa bima Tzs. 57,500,000 ambapo kiwango cha TZS 56,000,000 ni "own damage" na TZS 1,500,000 malipo ya "Towing charges''.
2. Dai nambari 020/088/9/157856/2019 hati ya malipo nambari 07533/2019 hundi nambari 977276 TZS. 25,113,000 zililipwa kutokana na kesi ya madai namba 326 ya 2018 baada ya kupata amri ya Mahakama na kutakiwa ZIC kulipa kiasi hicho.
3. Dai nambari 050/088/9/132317/2017 na vocha namba 067177/20 hundi namba 997876. TZS. 5,000,000 ililipwa kwa msimamizi halali wa mirathi (Abdoni Joviti Kalinjuna) baada ya kutokea kifo cha dai la upande wa tatu. Marehemu (Audax Joviti Kalinjuna) hakuwa abiria katika basi la abiria lililopata ajali lakini ni mtembea kwa miguu na mikataba yao ya bima haikuweka kikomo cha fidia ya

waenda kwa miguu kwa madai ya upande wa tatu (Pedestrian). Kama inavyoonekana katika jadueli:

S/n	Item	Private	Commercial	Motorcycle	Public
1	Property Damage	6,000,000	6,000,000	300,000	6,000,000
2	Bodily injured/Death	unlimited	unlimited	Unlimited	unlimited
3	Passenger Liability Injuries				3,000,000
4	Passenger liability Death				2,000,000
5	Passenger Liability (In Aggregate)				20,000,000
6	Excess Deductible	As Per Policy	As Per Policy	As Per Policy	As Per Policy

Uchunguzi wa Kamati

Hoja namba 1: Baada ya kupitia vielelezo na kumbukumbu tofauti, Kamati iliridhishwa na majibu ya Shirika kwani ilibaini kiwango kilichodaiwa kilikuwa kikubwa ukilinganisha na kiwango kilicholipwa. Hali hiyo inatokana na kwamba Sera ya Shirika inaweza kulipa malipo yasiyokuwa na kikomo kwa kifo au kuumia kwa Mali lakini Shirika lililipa si zaidi ya Tzs. 1,500,000 kwa kulivuta gari kutoka Sengerema lilipoharibika hadi Dar - es - Salaam lakini Shirika lililipa Tzs. 57,500,000 kufidia gharama zote dhidi ya Tzs. 87,613,000 zilizodaiwa. Hivyo, Shirika liliweza kuokoa jumla ya Tzs. 30,113,000.

Kamati pia imeridhishwa na majibu ya Shirika kuhusiana na malipo ya TZS. 25,113,000 kwa vile Mahakama ina uwezo wa kuamua kiwango cha malipo ya maumivu kulingana na mazingira ya ajali yalivyojitokeza wakati sera ya Shirika inaelekeza malipo ya juu kwa maumivu ya mtu aliyeathirika na ajali ni shilingi 3,000,000. Aidha, Kamati iliweza kuviona vielelezo ikiwemo maamuzi ya Mahakama kuhusiana na suala hilo.

Vile vile, Kamati ilikubaliana na majibu ya hoja namba 3 inayohusu malipo ya shilingi 5,000,000 ikiwa kama fidia kwa ndugu wa marehemu Abdon aliyefariki. Kamati ilibahatika kuona picha ya marehemu huyo na kukubali kwamba alikuwa ameumia vibaya mno na ndugu zake walistahiki kulipwa zaidi ya fedha hizo.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika liweke katika sera yao ukomo wa uwajibikaji wa malipo ya fidia kwa watu wa marehemu ambao wanatembea njiani.

3.4.4 Madai yatokanayo na wabia wengine wa Bima (Due to other reinsurance and treaty) Tzs. 1,784,659,276

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia kumbukumbu za Shirika kwa mwaka wa Fedha unaoishia Disemba 2019 imebainika kuwepo kwa madai yatokanayo na wabia wengine wa shughuli za Bima kama inavyoonekana katika mchanganuo wa madeni hayo ufuatao:

Nam.	Wabia wa Shirika la Bima – Znz.	Jumla ya Fedha (Shs).
1	Due to other Facultative Reinsurers	533,631,579
2	Due to JB Boarder	1,209,017,677
3	Due to Afro-Asian Treat Reinsurance	42,010,020
	Jumla	**1,1784,659,276**

Taarifa za hesabu za Shirika kwa mwaka wa Fedha unaoishia Disemba 2019 ziliripoti uwepo wa madai kama inavyoonekana hapo juu, madai ambayo yameonekana kuwa na dosari zifuatazo:-

- Kukosekana kwa taarifa za usuluhishi na uthibitisho wa uwepo wa usahihi wa salio la madai lililoripotiwa mwisho wa mwaka.
- Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha madai hayo ikiwemo Ankara (invoice), taarifa ya madai (debit notes), stakabadhi ili kuweza kuthibitisha uwepo wa usahihi wa salio la madai.
- Madai yanayotokana na mkataba wa Afro-Asian ni ya muda mrefu na ambayo yamekosa uthibitisho halali kwa zaidi ya kipindi cha miaka mitatu, ambayo yanatia shaka juu ya uwepo wake.

Majibu ya Shirika

Kamati ililezwa kwamba Shirika linatambua uwepo wa madeni hayo na kwasasa Shirika tayari limeshafanya ''reconciliation'' ya madeni hayo ambapo wabia wao waliochelewa kuwasilisha taarifa hizo ndani ya muda sahihi.

Katika kutatua changamoto hiyo, Muhasibu maalum ametayarishwa kwa ajili ya kufuatilia miamala na kufanya "reconciliation" kwa kila muda husika kuhusiana na madeni ya re insurance (Due to re insurance or treaty) .

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na Shirika kukiri kujitokeza kwa changamoto za kuwepo vithibitisho lakini Kamati ilitaka kujua sababu iliyopelekea hayo na kuelezwa kuwa Shirika linafanya kazi na Makampuni yaliyopo nje ya nchi ambayo kutokana na kuzuka ungonjwa wa Uviko - 19 walishindwa kuja nchini ili Shirika lipate uthibatisho wa deni wanalodaiwa na Wabia wao. Kuhusiana na Mkataba wa Afri-Asia, Kamati inakiri kupatiwa Mkataba huo na kuridhika nao.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika liwe na utaratibu wa kufanya usuluhishi wa madeni yake mara kwa mara ili kutambua kwa haraka kasoro zilizopo na kujipanga vizuri kwa utatuzi wake.

3.4.5 Madai ya Kodi (VAT) yaliyokosa uthibitisho Tzs. 772,343,656

Kwa mujibu wa taarifa za fedha za Shirika la Bima, imebainika jumla ya shilingi 772,343,656 ikiwa ni madai yanayohusiana na Kodi ya Ongezeko la thamani kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019, hata hivyo mchanganuo wa kina kuhusu madai ya kodi ya ongezeko la thamani yaliopaswa kulipwa kwa mwezi husika hayakuwasilishwa kwa ajili ya uthibitisho.

Ukaguzi umebaini kwamba gharama za kodi ya ongezeko la thamani na madai haya huoonyeshwa katika taarifa za kila mwezi, badala yake yameorodheshwa kiujumla katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ambapo maelezo na muda wa madeni ya kodi ya ongezeko la thamani hayakuoneshwa.

Kwa mujibu wa mapitio ya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT returns) kwa mwezi wa Disemba 2019 yaliyowasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalionesha Shirika lilikuwa na deni la kodi ya ongezeko la thamani la shilingi 279,442,395 kwa Matawi ya Shirika la Bima Tanzania Bara na kupelekea tofauti ya kiwango kilichoonekana katika taarifa za hesabu za Shirika.

Mchanganuo wa deni la kodi ya ongezeko la thamani inaonekana katika jadweli lifuatalo: -

Nam.	Jina la Tawi	Deni la VAT kwa	Deni la VAT kwa	Totauti iliyobainika

		mujibu wa hesabu (Shs)	mujibu wa Marejesho ya TRA (Shs)	(Shs)
1	Dar es Salaam	328,341,931	202,806,232	125,535,699
2	Mbeya	90,264,875	16,742,490	73,522,385
3	Arusha	128,547,106	19,447,260	109,099846
4	Mwanza	102,480,286	22,235,191	80,245,095
5	Kijitonyama	2,796,853	1,964,663	832,190
6	Mtwara	8,856,849	6,950,825	1,906,024
7	Dodoma	58,197,171	9,295,733	48,901,143
	Jumla	**719,485,071**	**279,442,395**	**440,042,382**

Aidha, ukaguzi ulichunguza zaidi na kubaini tofauti ya madai ya kodi ya ongezeko la thamani isiyo ya kawaida yenye jumla ya shilingi 79,483,826 kwa Tawi la Mbeya, shilingi 402, 544 kwa Tawi la Mtwara na Shilingi 1,122,595 kwa Tawi la Dodoma, ambapo maelezo ya kina pamoja na vielelezo vya kuthibitisha madai hayo havikuweza kupatikana kwa ukaguzi.

Ukaguzi unashauri kwamba Uongozi wa Shirika la Bima uhakikishe kwamba madeni na madai ya Kodi ya ongezeko la thamani linaendena na marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT Returns) ili kuhakikisha kunakuwepo na usahihi wa taarifa hizo.

Majibu ya Shirika

Kwa kipindi cha mwaka 2019, Shirika lilikuwa na wajibu “commitments” ya kulipa mahitaji mengi na makubwa jambo ambalo lilipelekea kuchelewa kulipa kodi iliyotajwa ya Tzs. 440,042,382. Shirika lilipa jumla ya shilingi 1,739,450,445 ambapo kati ya hizo Bakhresa alilipwa shilingi 993,600,000 na MV. Mapinduzi shilingi 745,850,445. Hata hivyo Shirika limeweza kulipa bakaa hiyo ndani ya mwaka 2020.

Aidha, Tzs. 81,008,965 iliyotajwa katika hoja hii ni kiasi ambacho kinadaiwa kati ya kanda ya pwani na kanda nyengine na sio deni kwa Mamlaka ya Mapato.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati haikufurahishwa kwa Shirika kubwa kama la Bima la Zanzibar kubainika na kadhia ya kutolipa kodi kwani ni jukumu la Taasisi kuhakikisha katika mipango yake kunakuwepo mpango wa kulipa kodi kwani ndio inayoisadia Serikali kuendesha shughuli zake za msingi. Kitendo cha Shirika kujikita na majukumu mengine na kuacha jukumu

lenye misingi ya kisheria ni ukiukwaji wa sheria za kodi. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba kodi hiyo imelipwa nje ya muda wa ukaguzi.

Mapendekezo ya Kamati

1. Shirika la Bima lihakikishe madeni na madai ya Kodi ya ongezeko la thamani yanalipwa kwa wakati.

2. Shirika lihakikishe linakuwa na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili zitakapohitajika ziweze kupatikana.

3.4.6 Malipo yasiyokuwa na tija kwa Shirika la Bima Tzs. 141,369,500.

Jumla ya Shilingi 141,369,500 zimeoneshwa katika hesabu ya madeni ya Shirika la Bima. Ukaguzi ulipitia taarifa ya madeni na kubaini kuwa Shirika kwa tarehe tofauti lilikataa madai yaliyowasilishwa na wadai ambayo yalilazimisha wadai kuwapeleka Mahakamani, aidha ukaguzi ulibaini kuwa Mahakama iliamuru kwa upande wa wadai kulipwa fidia kwa sababu ya Shirika la Bima kutohudhuria Mahakamani wakati wote tarehe za kesi ziliposikilizwa.

Kwa upande wa wadai, madai yao ya awali yalikua na jumla ya shilingi 1,800,000. Kutokana na Shirika la Bima kushindwa kuhudhuria vikao vya Mahakama, Mahakama iliamuru jumla ya shilingi 50,181,500 zilipwe kwa wadai na kupelekea Shirika kupata hasara kubwa kwa kulipa zaidi ya madai yaliyodaiwa hapo awali.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba kesi nambari 23/2016 iliyopelekea Mahakama kuamuru Shirika la Bima kufanya malipo ya shilingi 26,523,000 na shilingi 64,665,000 kwa hesabu ya Mahakama ya Iringa kupitia hesabu nambari 01J10400000100 CRDB. Ukaguzi haukuweza kupatiwa ufafanuzi wa uwepo wa deni hilo pamoja na vielelezo vilivyothibitisha Mahkama kuamuru malipo ya fedha hizo.

Ukaguzi unashauri kwamba Uongozi wa Shirika la Bima la Zanzibar kupitia kitengo cha sheria kinapaswa kutumia busara, hekima na tahadhari wakati wa kushughulikia madai ili kupunguza malipo ya ziada yanayoweza kujitokeza ambayo husababisha hasara kwa Shirika. Mchanganuo wa malipo ni kama inavoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Na	Tarehe ya Uhaulishaji	Fedha zilizohaulishwa (Shs)	Fedha zilizodaiwa na Mlalamikaji (Shs)	Nambari ya Hesabu	Aliyelipwa

1	13/05/2019	50,181,500	1,800,000	01J10400000100 CRDB Moshi Branch	Nickson Mutabirwa
2	11/12/2019	26,523,000			Iringa Judicial Deposit Account
3	11/12/2019	64,665,000			Iringa Judicial Deposit Account
Jumla		**141,369,500**			

Majibu ya Shirika

- Malipo haya yalifanyika kwa kesi mbili tofauti za madai zilizokuwa zimefunguliwa dhidi ya Shirika Mwanza na Iringa pamoja na kesi za gharama za mawakili (bill of cost).

    i. Kesi Ya Madai Nam. 12/2017 - Nickson Mtabirwa dhidi ya ZIC na Wengine Wawili; jumla ya madai yake Tzs. 250,000,000 kama gharama ya fidia.

    ii. Kesi ya Madai namba 23/2016 - Dominic Eric Kasisi dhidi ya ZIC na Wengine: jumla ya madai ni Tzs. 187,900,000.

    iii. Miscellaneous civil case no. 10/2018; jumla ya madai ni Tzs. 26,518,000 (bill of cost).

- Malipo yote hayo yaliamuliwa na Mahakama na vielelezo vya nakala za hukumu pamoja na Decree Order zipo.

- Kesi ya Madai nam. 12/2017 - Nickson Mtabirwa dhidi ya ZIC na Wengine Wawili ililipwa TZS 50,181,500 kwa amri ya Mahakama kwa kutolewa garnishee order benki ya kuzuia kiwango hicho na baadae kiwango hicho kilitolewa na kulipwa Mdai. Awali Mdai alipewa ofa ya Tzs. 1,800,000 na alikataa ndipo alipofungua kesi na sio kwamba ndio kiwango alichokidai. Nyaraka za Mdai alizoletea Madai zipo na hazioneshi kiasi hicho cha fidia kwamba ndicho anacho dai.

- Kesi ya Madai namba 23/2016 - Dominic Eric Kasisi dhidi ya ZIC na Wengine, malipo ya Tzs 90,867,000 yote hayo yalizuiwa kupitia hesabu ya benki za Shirika na kuingizwa katika “account” ya Mahakama kutokana na kesi hii ambapo Tzs. 26,518,000 gharama za Wakili (bill of cost) na Tzs. 64,665,000 ni fidia kwa Mdai.

Baada ya majadiliano na wadai na wakili wao Shirika lilifikia makubaliano katika fedha Tzs. 91,188,000 ambazo ziliingizwa Mahakamani zitumike kwa kesi hizi mbili na wakakubaliana:

- Kesi ya Madai namba 23/2016 - Dominic Eric Kasisi dhidi ya ZIC alipwe Tzs. 45 milioni.
- Miscellaneous Civil Case no. 10/2018; zilipwe TZS 23,000,000 (bill of cost) 03/2019; zilipwe Tzs. 2,000,000 (bill of cost)
- Kiwango cha Tzs. 21,188,000 walikubaliana kirejeshwe katika "account" za Shirika na makubaliano hayo yalishuhudiwa na Mahakama.
- Tayari TZS 18,028,000 zimesharudishwa kutoka Mahakamani na kuingizwa katika account ya Shirika.

- Uongozi ulichukua hatua kwa watendaji wake ambao kwa namna moja ama nyengine hawakutekeleza majukumu yao ipasavyo na kusababisha kulipa viwango vikubwa na ilimuachisha kazi Ndg. Abdulazizi Baisi mwanasheri ambaye alikuwa anashughulikia kesi hizo.

Uchunguzi wa Kamati

1. Kamati imesikitishwa sana na kitendo cha uzembe wa wanasheria wa Shirika kushindwa kuhudhuria Mahakamani kusimamia kesi zake na kusababisha gharama zisizo za lazima kwani Kamati imegundua wanasheria walihudhuria wakati wa kusomwa kesi hiyo, na kudai kwamba walikuwa hawashiriki kwa vile walikuwa hawapati wito wa Mahakama kuhusu muendelezo wa shauri lao. Kamati imebaini kuwa Shirika halikutimiza wajibu wake wa kufuatilia kilichokuwa kinaendelea Mahakamani hasa ukizingatia walikuwa wanajua kama kuna shauri dhidi yao.

2. Kuhusiana na madai ya kesi nam. 12/20017, Kamati ya LAAC pia imegundua dai la malipo ya awali ya shilingi 1,800,000 lilitolewa na Shirika kumlipa Mdai kama fidia yake kutokana na alivyoumia na baada ya kukataa malipo hayo ndio alikimbilia Mahakamani na Shirika kuamuriwa limlipe shilingi 50,181,500. Kwa mtazamo wa Kamati fedha hizo pia inaonekana kuwa ni kidogo maana Mdai aliumia vibaya na kuharibiwa mipango yake yote ya maisha maana Mdai alifikia hata kutolewa bandaba (figo).

Kwa upande wa vielelezo vya shillingi 26.5 milioni ambavyo Mdhibiti hakupatiwa, Kamati

imegundua kwamba Shirika halikuwa na utaratibu mzuri wa uwekaji kumbukumbu zake kwani baada ya huduma kukamilika kutolewa, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma inahitaji vielelezo vyake viwepo ambapo vikihitajika kwa ukaguzi vipatikane, lakini hadi Mdhibiti anakamilisha kazi yake havijapatikana kwa ukaguzi. Hata hivyo, Shirika limedai kuwa Mkaguzi hakupatiwa vielelezo hivyo kwa vile vilikuwa havijafika Ofisini.

Kamati haikukubaliana na sababu hiyo hasa ukizingatia mawasiliano ya siku hizi yanafanyika hata kwa njia ya mtandao. Hivyo, Shirika lingeweza kutafuta njia mbadala ya kuhakikisha vielelezo hivyo vinapatikana kwa wakati. Kamati haikushangazwa na Mdhibiti kukosa vielelezo hivyo kwani hata Kamati ilishindwa kupata baadhi ya vielelezo wakati wa kikao hadi muda mwengine wakati Kamati imeshamaliza kazi zake.

Vile vile, Kamati imegundua Shirika lina upungufu wa wanasheria kwani wapo watano wanaotakiwa kufanya kazi katika Matawi yao yote sita yaliyopo Zanzibar na Tanzania Bara.

Mapendekezo ya Kamati

1. Shirika la Bima Zanzibar liajiri wanasheria wengi ili liweze kuwakilishwa wanapokuwa na kesi zaidi ya moja.

2. Shirika liwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili kasoro zilizojitokeza zisijirudie.

3.4.7 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio ya Tzs. 83,884,000

Kifungu cha 83A na Aya 4(c) ya jadweli la kwanza kwenye sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2014 kinataka makato ya kodi yazuio ya asilimia 5 kwa huduma zinazotolewa na asilimia 2 kwa manunuzi ya bidhaa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Bima la Zanzibar limefanya malipo ya shilingi 83,884,000 kwa watoa huduma mbali mbali kwa ajili ya kazi za ushauri na huduma za kisheria walizotoa watoa huduma kwa Shirika bila kukatwa kodi ya zuio.

Kukata kodi ya zuio kunapunguza gharama za ukusanyaji wa kodi, kunasaidia kuzingatia sheria na kupunguza kukwepa kodi; vile vile kunasaidia Serikali kukusanya kodi mapema, kitu ambacho hakikufanyika.

Kushindwa kuzuia kodi kwa huduma mbali mbali zinazotolewa kunaweza kupelekea kuisababishia Shirika hasara zisizo za lazima zinazotokana na malipo ya adhabu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

Na	Tarehe	Nambari	Jumla ya	Maelezo	Tawi

		ya Hundi	Fedha (Shs)		lililofanywa malipo
1	13/09/2019	936707	6,000,000	Ikiwa ni malipo ya Mshauri mwelekezi kwa ajili ya kuboresha tozo za Bima (Premium rate proposal)	Dar es Salaam
2	23/08/2019	977146	21,911,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya TANSCAR ATTORNEYS	Dar es Salaam
3	16/05/2019	936490	7,150,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya TANSCAR ATTORNEYS	Dar es Salaam
4		977323	10,000,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Wakili Chanjarika & Company Advocates	Dar es Salaam
5		977334	8,275,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya usimamizi wa kesi nambari 169 ya mwaka 2017	Dar es Salaam
6		977299	14,300,000	Ikiwa ni malipo ya huduma za usimamizi wa kesi nambari 68 ya mwaka 2019 kwa Tanscar Attorneys	Dar es Salaam
7	20/02/2019	000009	4,680,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Pango la Nyumba za wafanyakazi wa Shirika la Bima	Kituo cha mauzo, Kijitonyama
8	13/02/2019	001380	2,365,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya Gari nambari Z 868 GZ.	Makao makuu, Zanzibar
9	03/04/2019	001429	3,903,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya Gari nambari SLS 104 A.	Makao makuu, Zanzibar
10	24/09/2019	001936	5,300,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya Gari nambari Z 164 JV.	Makao makuu, Zanzibar

Jumla	**83,884,000**		

Majibu ya Shirika

Shirika limepokea ushauri wa Mkaguzi na kwasasa linaendelea kukata kodi ya zuio kwa huduma zote kama inavyotakiwa kisheria.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na Shirika kukiri kwamba kweli hawakuzuia kodi ya shilingi 4,194,200 kutoka kwa washauri Elekezi waliofanya kazi na Shirika, kwa kutilia maanani kwamba kodi ndio msingi wa maendeleo ya kila nchi, Kamati haikufurahishwa na kitendo hicho na imeutaka uongozi mpya wa Shirika kuwa makini sana na masuala ya ulipaji kodi kwani ndio yanayoimarisha miundombinu ya kijamii.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika lihakikishe linazuia kodi zote za Washauri Elekezi.

3.4.8 Uwepo wa tuhuma za madai ya bima kwa muda mrefu Tzs. 104,300,000

Kwa mujibu wa taratibu za madai zilizowekwa na Shirika la Bima, uchunguzi wa tuhuma za madai zinapaswa kushughulikiwa na Idara ya Madai pamoja na kitengo cha sheria kwa kufanya kazi kwa karibu ili kuhakikisha uthibitisho wa madai yanaweza kufanyiwa kazi kwa haraka kwa lengo la kupunguza nafasi ya wadai kuweza kulishtaki Shirika.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa madai wa muda mrefu ikiwemo madai ya tuhuma, madai yaliyokosa uthibitisho wa kutosheleza ambayo yanahitaji uchunguzi zaidi ili kuepusha Shirika kufanya malipo kinyume na utaratibu.

Mchanganuo wa madai hayo ambayo ukaguzi umekosa vielelezo na uthibitisho wa kutosheleza wa uwepo wa Madai hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Madai ya Bima yaliyokosa uthibitisho.

Na	Namba ya dai	Jina la Mdai	Jumla ya fedha inayodaiwa (Shs)	Maelezo
1	010/070/9/168527/2019	Mr.	13,500,000	Ikiwa ni malipo ya

		Ramadhani Haji Juma		madai ya tuhuma ya ajali wakati muda wa Bima umeshamaliza (expiry of the insurance policy)
2	010/070/9/165958/2019	Mr. Omar Juma Budda	5,800,000	Ikiwa ni malipo ya madai ya tuhuma ya ajali wakati ajali haikutokezea (Non occurance of an accident)
3	010/070/9/165104/2019	Nassor Said Mohamed	85,000,000	Ikiwa ni malipo ya madai ya tuhuma ya ajali wakati ajali haikutokezea (Non occurance of an accident)
Jumla			**104,300,000**	

Majibu ya Shirika

Madai haya yalikuwa na mashaka ndio maana yakachelewa kulipa ili kujikinga kulipa madai yasiyokuwa halali na kusababisha upotevu wa fedha za Shirika.

Dai la Ndg. Ramadhani Haji Juma na Omar Juma Buda madai haya hayakulipwa na tayari yameshafungwa baada ya wahusika kukubali kwamba sio madai halali.

Dai la Ndg. Nassor Said Mohamed bado lipo kwa msuluhishi wa migogoro ya bima Tanzania baada ya Shirika kukataaa kulipa dai hilo kutokana na udanganyifu uliojitokeza.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilifuatilia hoja hii kwa kupitia vielelezo vya kukataa kulipa deni, iligundua kwamba kuna udanganyifu mkubwa unafanyika hususan wakati wa ajali inapotokezea na madai yanapowasilishwa kwa ajili ya malipo kwani wakaguzi wa magari huwasilisha madai ya vitu vingi ukilinganisha na uhalisia. Hali hiyo husababisha dai kuwa na gharama kubwa zinazoifanya Shirika kuchelewa kufanya malipo. Aidha, kuna

wadanganyifu wengi hujitokeza kwa kudai mali zao zimeathirika na kudai fidia kwa Shirika.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika liwe makini sana kuyachunguza ipasavyo madai yanayowasilishwa kwao ili kuepuka kuja kulipa madai hewa.

3.4.9 Kuchelewa kupelekwa kwa fedha benki Tzs. 186,637,556

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 186,637,556 kuwa ni mapato yanayokusanywa na madalali pamoja na mawakala wa matawi ya Dar es Salaam na Arusha kwa niaba ya Shirika la Bima hayakuwasilishwa benki kwa wakati. Kutokupeleka benki fedha za mapato zilizokusanywa kwa wakati ni kwenda kinyume na kanuni za Msimamizi wa Biashara za Bima Tanzania (TIRA).

Majibu ya Shirika

Fedha zilikuwa zikichelewa kupelekwa benki na baadhi ya Mawakala kutokana na kuwepo mtawanyiko mkubwa wa Mawakala na wengine kuwa na tatizo la kuwa mbali na mabenki na ndipo Shirika likafikiria njia ya kutumia “system” ya ‘’CIMIS’’ kwa ajili ya kuondoa tatizo hilo na kwa sasa fedha zote zinapelekwa kwa wakati kwani “system” hairuhusu kutoa bima bila malipo kuingia benki.

Uchunguzi wa Kamati

Kufuatia majibu hayo ya Shirika, Kamati haikukubaliana na kuwepo kwa mtawanyiko mkubwa kama ni sababu ya kuchelewa kupeleka fedha benki. Hili lilibainika baada ya Kamati kupitia orodha ya malipo ya Bima zilizochelewa kupelekwa Benki na kugundua kuwa kuna Mawakala wengi wamekaa na fedha kwa kipindi cha miezi miwili hadi mitatu wakati kiuhalisia hakuna umbali unaokwaza fedha kushindwa kuzifikisha Benki kwa muda wote huo. Hata hivyo, Kamati imekubaliana na Shirika kwamba kutokuwepo kwa mfumo wa malipo wa kidigital ambao hulazimisha Wakala kufanya malipo kwanza ndio aweze kufanya kazi yake kuwa ni sababu ya kuchelewesha malipo hayo.

Kutokana na utata wa majibu ya Shirika, Kamati iliamua kufanya ziara ya kikazi Tanzania Bara kwa lengo la kukutana nao na kuwasilikisha sababu hasa zilizowafanya wacheleweshe malipo ya mauzo ya Bima pamoja na changamoto za kazi zao kwa ujumla wake. Aidha, Kamati baada ya kupitia vielelezo iligundua kwamba tayari fedha hizo zimeshapelekwa Benki kwa nyakati tofauti ila zimewasilishwa nje wakati unaotakiwa.

Mapendekezo ya Kamati

1. Shirika linatakiwa kuwa makini sana na Mawakala maana huzingatia zaidi mapato yao kuliko maslahi ya Shirika.

2. Shirika lifuatilie utendaji wa Mawakala wake ili liweze kutambua ufanisi na ushirikiano uliopo baina yao.

3. Shirika lichukue hatua zifaazo kwa Mawakala wanaochelewesha kupeleka fedha benki ikiwemo hata kufuta usajili wake wa kuwa Wakala wao.

3.4.10 Uwepo wa mikopo ya muda mrefu na mapato ya ada ya bima (premium) yaliyokuwa hayajakusanywa kutoka kwa Mawakala na Madalali Tzs. 648,891,615

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa jumla ya shilingi 531,526,363 za mapato ya ada ya bima ambayo haikukusanywa kwa muda mrefu, ukaguzi pia umebaini uwepo wa jumla ya shilingi 117, 365,252 ya mikopo ambayo haikukusanywa kutoka kwa Mawakala. Katika kupitia vitabu vya Mawakala imebainika kwamba mikopo na mapato mengineyo hayakupatikana kwa wakati na kupelekea baadhi ya hesabu za Mawakala kuonekana kuwa hazifanyikazi kwa zaidi ya kipindi cha miaka mitatu.

Ukaguzi umeshindwa kuona jitihada zozote zilizochukuliwa na uongozi wa Shirika la Bima katika kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwa wakati. Uwepo wa madeni ya muda mrefu yanatia shaka juu ya uwepo wa Mawakala, aidha kushindwa kupata malipo kutoka kwa Mawakala kunaweza kusababisha hasara kwa hatua ambazo zitachukuliwa na uongozi wa Shirika la Bima katika kuyafuta madeni hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 72(2) na 137(2) cha sheria ya uanzishwaji wa Shirika la Bima la Zanzibar. Kiambatisho Nambari 3 cha kitabu cha Mdhibiti kinahusika.

Majibu ya Shirika

Shirika linaendelea kupunguza madeni ya Mawakala wanaodaiwa ada za bima kupitia ujira wao kwa kila mwezi. Kwa baadhi ya Mawakala wenye mikopo wanakatwa kama ilivyo katika mikataba yao walioingia na Shirika.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imebaini kuwa Shirika hutoa mikopo kwa lengo la kuwawezesha Mawakala kumudu gharama za kutengeneza vizuri Ofisi zao pamoja na gharama za kununua vitendea kazi. Aidha, kiasi cha mkopo wanachopewa huendana na faida wanayoiingiza

Shirika isipokuwa Kamati inakubaliana na hoja ya Mdhibiti kwamba mikopo hiyo huwa inacheleweshwa kurudishwa na kulifanya Shirika kuwa na madeni ya muda mrefu. Hali hiyo huzorotesha maendeleo ya Shirika kwa ujumla.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika lisimamie na kufuatilia ipasavyo mikopo hiyo ili iweze kurudishwa kwa wakati.

3.4.11 Uwepo wa wadaiwa na malipo ya Bima Tawi la Arusha Tzs. 55,721,830

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa wadaiwa wanaotokana na sera za bima (Insurance Policy) zinazouzwa kwa mkopo katika Ofisi ya Tawi la Arusha yenye jumla ya shilingi 55,721,830 ambazo bado hazijalipwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2019. Kwa vile wadaiwa hao ni wengi, ukaguzi umeonesha baadhi ya wadaiwa hao kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 23: Wadaiwa wa malipo ya Bima

Na	Tarehe	Jina la Mteja/Mdaiwa	Jumla ya Fedha (Shs)
1	24/12/2019	Daruni Delivers & Transport Ltd.	590,000
2	27/12/2019	Daruni Delivers & Transport Ltd.	590,000
3		Machame Safari Express Ltd.	8,070,500
4	01/07/2019	Mary Paul Mushi	1,020,110
5	24/07/2019	Sherali O. Mbowe	295,000
6	12/04/2019	Fausta Valeria/Machame	1,517,775
7	09/08/2019	Gideon Alfred Mwakibinga	531,000
8	16/08/2019	Charles N. Swai	531,000
9	06/12/2019	Chirstina S. Lukumay	413,000
Jumla			**13,558,385**

Majibu ya Shirika

Deni hili ni deni halali ambalo limetokana na wateja wetu wakubwa ambao hulipa kwa awamu ambapo Shirika hukubaliana na mteja kulipa kwa awamu ili kuweza kuendana

na ushindani wa soko. Kwasasa jumla ya Tzs. 41,207,055.00 sawa na asilimia 74 ya deni lote kwa kipindi cha mwaka 2020 tayari zimeshalipwa na kubakia bakaa ya Tzs. 14,514,775.00

Uchunguzi wa Kamati

Kwa vile Shirika limekiri juu ya uwepo wa utaratibu huo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

Mapendekezo ya Kamati

Shirika lihakikishe fedha zilizobakia zinalipwa katika Shirika kwa wakati.

3.4.12 Kukatiwa bima kwa chombo kilichokuwa katika haliisiyoridhisha.

Kwa mujibu wa Sera ya Shirika la Bima, ili chombo kiweze kuandikishwa kukatiwa Bima kinapaswa kuwa katika hali nzuri. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bima lilipokea maagizo ya kukatia Bima MT. Mkombozi ambayo haipo katika hali ya kuridhisha kwa barua yenye kumbu kumbu namba MOICT/M.120/C.120/C.2/VOL VIII/115 ya tarehe 09/05/2019 kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika lililazimika kuikatia Bima MT. Mkombozi wakijua ya kwamba MT. Mkombozi haina sifa ya kukatiwa Bima kwa mujibu wa Sera ya Shirika la Bima na kwa kuzingatia chombo hicho kilipata ajali ya moto mnamo tarehe 10/10/2019 na hakuna vielelezo vilivyopatikana na ukaguzi vinavyothibitisha kuwa chombo hicho kiliwahi kufanyiwa ukarabati, au kulipwa fidia kutokana na ajali hiyo ya moto na kwamba kipo katika hali ya kuridhisha kwa mujibu wa sera ya Shirika, hali ambayo imepelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa kufanya maamuzi hayo jambo ambalo huenda likapelekea hasara kubwa kwa Shirika kwani ukizingatia Shirika halina uwezo wa kukikatia Bima chombo hicho peke yake ililazimika kumtafuta mbia wakushirikiana nae katika kukikatia Bima chombo hicho.

Kukikatia Bima chombo ambacho hakina sifa kunaweza kupelekea Shirika la Bima kupoteza sifa yake ya kuwa ni Shirika la kibiashara badala yake huenda likawa Shirika la huduma jambo ambalo ni kinyume na sheria na kanuni za biashara za Bima.

Majibu ya Shirika

Pamoja na kupokea maagizo ya kutoa kinga kwa meli ya Serikali MT. Ukombozi kwa barua yenye kumbukumbu namba MOICT/M.120/C.2/VOL.VIII/115 ya tarehe 9/05/2019. Hata hivyo, Shirika halikutoa kinga hiyo baada ya kutoa “rate” ambazo zilikuwa kubwa na kuweka masharti magumu na hatimaye meli hiyo ikakosa kinga na kuwataka wafanye matengenezo ya meli hiyo ili ipate sifa za kukatiwa bima.

Uchunguzi wa Kamati

Baada ya kupata majibu kutoka Shirika, Kamati iliipitia barua hiyo na kujiridhisha kwamba Shirika la Bima Zanzibar kweli hawakutoa kinga kwa meli ya mafuta ya MT. Mkombozi kupitia barua namba MOICT/M.120/C.2/VOL.VIII/115 ya tarehe 9/05/2019 iliyotoka kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na usafirishaji ya wakati huo. Hata hivyo, Kamati ilikemea utaratibu unaotumika kwa Mashirika ya Serikali kupatiwa maagizo yanayokwenda kinyume na Sera na Sheria zao kwani huwarudisha nyuma na kuwavurugia mipango yao.

Mapendekezo ya Kamati

Serikali ihakikishe inafanya kazi na Mashirika yake pasi na kuyaingilia hususan katika utekelezaji wa majukumu yao.

3.4.13 Dosari katika ukataji wa bima kwa vyombo vikubwa

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba SMU/UU/3/7VOL.II/36 ya tarehe 27/10/2020 kutoka Shirika la Meli Zanzibar waliwataka Shirika la Bima la Zanzibar kuikatia Bima Meli ya MV. Mapinduzi II ambayo ilimaliza muda wake wa matumizi mnamo tarehe 14/02/2020. Kwa mujibu wa barua hiyo, Shirika la Meli lilijikubalisha kulipa jumla ya dola za Kimarekani (USD) 248,843.85 kwa vipindi vya awamu tatu tofauti kama inavyoonekana hapa chini:

Nam.	Awamu za Malipo	Kiwango cha malipo (USD)	Tarehe ya Malipo
1	Malipo ya awamu ya kwanza	100,000	13/02/2020
2	Malipo ya awamu ya pili	100,000	13/04/2020
3	Malipo ya awamu ya tatu	48,844	13/06/2020

Pamoja na barua za ukumbusho za kulitaka Shirika la Meli kufanya malipo ya Bima kwa meli yake, Shirika lilishindwa kufanya malipo hayo kwa mujibu wa Sera na badala yake ombi hilo la kuikatia Bima MV. Mapinduzi II lilikubaliwa na Shirika la Bima kupitia barua yenye kumbukumbu nambari ZIC/A.482/MTU.II/09/2020 ya tarehe 04/02/2020.

Dosari iliyobainika na Ukaguzi ni kwamba Shirika la Bima liliamua kuikatia Bima Meli hiyo kabla ya malipo hayo kukamilika jambo ambalo ni kinyume na Sera, sheria na kanuni zinazosimamia biashara ya Bima.

Majibu ya Shirika

Shirika lilitoa kinga kwa meli ya MV. Mapinduzi baada ya kuingia makubaliano ya kulipia ada ya meli hiyo kwa awamu tatu kama zilivyoainishwa katika Ripoti ya Mkaguzi, hata hivyo Shirika la meli lilishindwa kukamilisha makubaliano hayo kwani waliweza kulipa sehemu ya kwanza ya malipo hayo ambayo ni USD 100,000.00 na sehemu iliyobakia USD 148,844 hadi sasa zimeshinda kulipwa na kuliingiza Shirika katika madeni na mahusiano mabaya kwa Washirika wa bima mtawanyo wa meli hiyo. Shirika liliamua kukatia bima meli hiyo baada ya vikao vya watendaji wakuu wa Wizara na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango wa wakati huo, na hili lilifanyika baada ya Shirika kukataa kutoa kinga kwa meli za Shirika la meli kwani hazikuwa na sifa ya kupewa bima.

Uchunguzi wa Kamati

Kutokana na majibu ya Shirika la Bima la Zanzibar na vielelezo vya barua, Kamati imegundua Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango ya wakati huo ilililazimisha Shiriki kupitia Kampuni Washirika kuikatia kinga meli ya MV. Mapinduzi II wakati ilikuwa bado haijakamilisha vigezo vya kuweza kupatiwa huduma hiyo. Kuikatia bima meli hiyo kumeitia hasara Shirika na kuteteresha mtaji wake kwa vile gharama zake zilikuwa kubwa sana. Kamati imebaini kwamba kuna nguvu imetumika kwani kuna barua ya Mkurugenzi Mtendaji tarehe 09 Oktoba, 2020 yenye kumbu kumbu nambari ZIC/A.98/W.F/VOL.XIV/57/20 inayohusu kukataa kwake dhidi ya utoaji kinga kwa meli ya MV. Mapinduzi II.

Kamati imekemea sana utendaji wa aina hiyo wa kufuata amri kutoka juu usiofuata masharti wala taratibu za sera na sheria na kuiomba Serikali kuyaachia Mashirika yake yafanye biashara bila kuwepo vikwazo ili yaweze kutengeneza faida na hatimaye kutoa gawio kwa Serikali.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaendelea kuitaka Serikali kupitia watendaji wa Wizara zake kuacha kuyalazimisha Mashirika kutekeleza shughuli zake kinyume na utaratibu kwani kunayatia hasara na kuharibu taswira ya utendaji wao.

3,4,14 Bakaa ya Fedha katika hesabu ya FBME Tzs. 90,830,291

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu vya Shirika la Bima la Zanzibar imebainika uwepo wa bakaa la fedha katika hesabu za benki ya FBME ambapo bakaa hiyo ipo kwa muda mrefu na hakuna jitihada zozote zilizobainishwa na Shirika hilo juu ya ufuatiliaji wa bakaa hiyo ili iweze kupatikana jambo ambalo huenda likapelekea fedha hiyo kukosekana na kulisababishia Shirika hasara kubwa. Mchanganuo wa bakaa hiyo ya

fedha ambayo haijulikani hatima yake ni kama ifuatavyo:-

Bakaa ya Fedha katika hesabu ya FBME.

Nambari ya hesabu	Kiwango cha fedha kilichopo (Shs)	Jina la tawi la Shirika
030653 TZS, FBME	6,149,799	Makao Makuu (Unguja)
FBME Account	2,797,613	Tawi la Mwanza
FBME Account	5,547,046	Tawi la Arusha
Account number 030653 TZS – TCA-002	47,824,787	Tawi la DSM
Account number 030653 USD	28,511,053	Tawi la DSM
Jumla	**90,830,291**	

Majibu ya Shirika

Mara kadhaa Shirika limekuwa tukifuatilia kwa maandishi kwa msimamizi wa Bank hiyo (DEPOSIT INSURANCE BOARD) ambapo majibu yake ni kuwa wao wanaweza kurudisha Tzs. 1,500,000 kwa kila mmiliki wa Account na ndicho Shirika kilichopokea kwa muda wote huo.

Aidha tumemuandikia Governor wa BOT hivi karibuni bado hatujapata majibu kutoka kwake.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati baada ya kupitia kielelezo cha barua ya tarehe 1 Machi, 2021 yenye kumbukumbu nambari UB.56/458/01, ilithibitisha kuwa kweli Shirika limeweka zaidi ya shilingi milioni 50 katika benki ya FBME. Hata hivyo, kwa mujibu wa taratibu za ufilisi wa Benki, wateja hupatiwa shilingi 1.5 milioni kwa kila aliyeweka zaidi ya kiasi hizo. Kwa mantiki hiyo, uwezekano wa fedha hizo kurudishwa zote ni mdogo sana.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaendelea kuushauri uongozi wa Shirika la Bima kuzidi kufanya vikao vya mara kwa mara na Benki ya Tanzania kuwataka urudishwaji wa bakaa hiyo.

ZIARA YA KAMATI YA LAAC KATIKA TAWI LA SHIRIKA LA BIMA LILIOPO LUMUMBA DAR - ES - SALAAM

Tarehe 18 Novemba, 2021 Kamati ya Kuthibiti na Kukagua Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika ilifanya ziara ya kikazi katika Shirika la Bima Tawi la Dar - es - Salaam kwa ajili ya kufuatilia majibu ya Shirika hususan ya ucheleweshwaji wa kupelekwa fedha benki unaofanywa na Mawakala na Madalali wa Shirika. Aidha, Kamati pia ilipata fursa ya kufahamu changamoto za Shirika, Madalali pamoja na Mawakala hao katika utendaji wa kazi zao.

Awali, Kamati ilipatiwa maelezo kwamba Tawi la Shirika la Bima ni miongoni mwa Mashirika ya Serikali yanayofanya kazi zake Tanzania Bara (Matawi mengine yapo Mwanza, Dodoma, Mbeya, Arusha, Zanzibar na Dar -es - Salaam. Tawi hilo limeanza kazi zake mwaka 2000 ambapo kwasasa Tawi lina wafanyakazi 24 pamoja na Madalali na Mawakala 33.

Kabla ya mwaka wa fedha 2019/2020, Shirika lilikuwa likifanya kazi zake kwa kutumia mfumo wa 'manual' lakini hivi sasa Shirika linatumia mfumo wa kidigitali ambapo tayari Benki kadhaa zinashirikiana nao zikiwemo CRDB, NMB na TCB katika utoaji wa huduma zake. Kupitia Benki hizo, Shirika linategemea kutumia fursa iliyopo kuwakopesha Mawakala wake waaminifu ili waweze kufanya kazi zao kwa urahisi na umakini zaidi.

Kupitia maelezo ambayo Kamati imepatiwa, ilitaka kujua kwanini PBZ haijachangamkia fursa iliyopo katika Shirika na kuelezwa kwa masikitiko maubwa kwamba PBZ wao wamelala wakati wenzao wamechangamka kutafuta fursa popote zilipo. Hivyo, kuna kila sababu fursa hiyo kuchangamkiwa na PBZ.

Baada ya utangulizi huo, Kamati ilipata nafasi ya kukutana na baadhi ya Mawakala ili kuwasikiliza na kufahamu sababu zilizowafanya wachelewe kupeleka malipo ya Bima Benki pamoja na kutathmini utendaji kazi wao na Shirika la Bima la Zanzibar. Miongoni mwa Kampuni hizo ni:

1. Arson Insurance Company iliyopo Kibaha;
2. Madson Insurance Company iliyopo Kariakoo;
3. AIKA Insurance Company iliyopo Morogoro 'road';
4. Wastara Insurance Company iliyopo Kariakoo, Buguruni, 'Airport', Sinza na Zanzibar ; na
5. Bahassany Insurance Company iliyopo Kinondoni.

Kamati ilifanya majadiliano na wawakilishi wa Kampuni hizo na kubaini pamoja na mambo mengine, kwamba ucheleweshwaji wa fedha kupelekwa benki ulisababishwa na

mambo yafuatayo:

1. Kuchelewa kufanya malipo kwa wafanyabiashara wanaopatiwa huduma na Mawakala hao. Hili hutokezea kutokana na Mawakala hukubaliana na wafanyabiashara kulipa fedha nusu na kiasi chengine kuahidi kumaliza baadae. Iwapo wafanyabiashara hao watashindwa kulipa kwa wakati, ndio ucheleweshwaji unajitokeza.
2. Kuwepo kwa mashirikiano mazuri ya kiutendaji baina ya Shirika la Bima la Zanzibar na Mawakala wake.
3. Kuwepo kwa ushindani mkubwa katika biashara ya bima hususan kutoka Kampuni binafsi zinazofanya kazi Tanzania. Kamati ilielezwa kuwa yapo Makampuni mengine yanatoa ujira mkubwa kwa Mawakala jambo ambalo hutoa ushawishi kwa Mawakala wa Shirika.
4. Kubanwa au kuingiliwa kwa uhuru wa Shirika la bima la Zanzibar katika ufanyaji kazi wake. Hili limetokana na baadhi ya kazi za Shirika kukwamishwa na Serikali, mfano Shirika lililazimishwa kuiwekea kinga Meli za MT. Ukombozi II na MV. Mapinduzi II kinyume na utaratibu wa sera na sheria za uendeshaji wa bima.
5. Mawakala hawana huduma za kibenki Ofisini mwao jambo ambalo huwakosesha wateja kwani mteja akiondoka kwenda kufanya malipo huwa harudi tena.
6. Mabenki yamejiingiza katika utoaji wa huduma za bima na kupelekea kuwanyangánya Mawakala wateja wao kwa vile wao huwakopesha wateja.
7. Kuwepo kwa ugumu wa upatikanaji wateja kwa Mawakala. Hili linasababishwa na Taasisi nyingi kujihusisha na shughuli za bima.
8. Kuna Mawakala wengi wamefanya kazi na Shirika la Bima la Zanzibar kwa muda mrefu wakiwemo AIKA Insurance Company tokea mwaka 2012, Wastara mwaka 2003 na Bahassany mwaka 2008.
9. ‘Bonus’ wanayolipwa ni ndogo sana ukilinganisha na makampuni mengine. Mawakala wamependekeza ipandishwe angalau ifikie asilimia 5 ya faida wanayozalisha.
10. Kuwepo kwa mpango wa kuwanunua wateja kwa madalali. Hili hutokezea kwa Wakala hulazimika kumpatia kiasi fulani cha fedha dalali ili amletee wateja katika kampuni yake.
11. Mawakala hawawezeshwi vifaa vya kuandikia wala kukodiwa Ofisi na Shirika.
12. Kuna baadhi ya wakati kunatokezea ucheleweshwaji wa malipo ya Mteja kwani Wakala huambiwa vocha haijakamilika mpaka itoke Zanzibar (Makao Makuu).
13. Kampuni binafsi zinaonekana kuwa na motisha zaidi ya zile za Serikali kwani hutokezea wakawasaidia Mawakala wao Ofisi, vifaa vya kuandikia au mteja akipata ajali hupatiwa gari nyengine akisubiri kufanyiwa matengenezo gari yake.
14. Kuna wateja wamekanusha kwamba ndio walikuwa wanachelewa kuwasilisha fedha benki ila sio kwa muda wa miezi mitano kama ilivyoelezwa katika taarifa ya

Mdhibiti.

15. Kuna baadhi ya wakati mfumo huwa haupatikani au unakuwa unazorota.
16. Wateja wawe wanalipwa madai yao haraka na ikiwezekana hata huo ukomo wa kulipa wa siku 45 ulioainishwa na sheria upungunzwe.

Mapendekezo ya Kamati

1. Huduma za bima ziboreshwe ili wateja wavutike zaidi kukata bima katika Shirika la Bima la Zanzibar.
2. Shirika la Bima litoe mikopo kwa Mawakala wanaoliletea tija shirika na wenye uaminifu ili waweze kukuza mtaji wao.
3. Shirika lianzishe utaratibu wa kujitangaza zaidi kwa njia tofauti hususan katika stendi za mabasi.
4. Mawakala wapatiwe fursa ya kufungua wakala wa benki katika Ofisi zao ikiwezekana wapatiwe mashine za kuhesabia fedha au za kutolea risiti za malipo.
5. Kwa vile Shirika la Bima ni shirika la kibiashara, Serikali iondoe mkono na iliruhusu kufanya kazi zake kwa mujibu wa Sera na Sheria zake ili baadae liweze kutoa gawio.
6. Shirika lihakikishe linazidi kuuimarisha mfumo wake ili uweze kupatikana ukiwa na nguvu wakati wowote.
7. Shirika liwapatie motisha zaidi mawakala wao.
8. Serikali kupitia PBZ ichangamkie fursa ya utoaji wa mikopo kwa Mawakala waaminifu wa Shirika ili liweze kujiongezea faidia maradufu.

3.5: SHIRIKA LA BANDARI

Taarifa ya Mapato

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini Shirika limeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za uendeshaji kwa asilimia 7.14. Aidha, ukusanyaji wa mapato mengineyo imebainika kutokufikia kwa lengo la ukusanyaji wa mapato hayo kwa asilimia 32.18.

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo husika kwa mujibu wa makadirio ikiwemo na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili Shirika kuweza kujiendesha kwa ufanisi na tija.

Majibu ya Shirika

Ni kweli katika mwaka wa fedha 2019/2020 chanzo cha mapato yatokanayo na shughuli za uendeshaji (TSH. 27,100,747,874) yalipungua kwa asilimia 7.14 (TSH.

2,082,398,551.30) ukilinganisha na makadirio ya mwaka 2019/2020 (TSH. 29,183,146,425).

Mapato yatokanayo na shughuli za uendedhaji ni mapato ambayo hutokana na huduma zinazotolewa kwenye uhudumiaji wa mizigo (Mizigo mchanganyiko na makontena) ikwemo kazi za upakiaji na uteremshaji wa mizigo Bandarini (Cargo, Container, Wharfage Ship, Wharfage Dhow, labour Charges, lifting charges, Storage and Stuffing).

Sababu iliopelekea kupungua kwa mapato haya ni kupungua kwa uingizwaji na utoaji wa mizigo kutoka katika maeneo mbali mbali ya Bandari zetu kutokana na kupungua kwa ujaji wa meli za kigeni hii ilichangiwa na mripuko wa maradhi ya Covid 19, ugonjwa ambao ulianza katikati ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Jadweli liliopo hapo chini linaonesha Mchanganuo wa Mapato yatokanayo na shughuli za uendeshaji kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NAM.	MAELEZO	MAKISIO (BUDGET)	MAPATO HALISI
1.	Mapato yanayotokana na Uendeshaji (Operational Revenue	29,183,146,425	27,100,747,874
2.	Mapato yanayotokana na Huduma za Baharini (Marine Revenue)	5,798,450,160	7,222,362,250
3.	Mapato Mengineyo (Other Revenue)	1,260,658,149.9	880,295,667
4.	Bank Interest	61,406,808	66,928,104
5.	NON CAS REVENUE		946,553,489
JUMLA KUU		**36,303,661,542.9**	**36,216,887,383.27**

Ni kweli katika mwaka wa fedha 2019/2020 chanzo cha mapato yatokanayo na mapato mengineyo (TSH. 880,295,667) yalipungua kwa asilimia 32.18.

Mapato mengineyo ni mapato ambayo sio kati ya mapato yatokanayo na Shughuli za uendeshaji wala mapato yatokanayo na vyombo vya baharini. Mapato haya yamegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni kama zifuatazo:-

i. Mapato ya Meli ya LCT Jitihada

ii. Mapato ya Chelezo (SlipwayRevenue)

iii. Mapato mengineyo (Other Earnings)

Sababu iliyopelekea kupungua kwa mapato mengineyo ni kama zifuatazo:-

i. Kupungua kwa mapato yatokanayo na LCT Jitihada kwa asilimia 44 sawa na TSH. 260,124,028.76 ya makadirio ya mwaka (TSH. 588,000,000), ambapo mapungufu haya yamesababishwa na kutofanya kazi kutokana na sababu ya matenegezo mbali mbali ya meli katika vipindi tofauti vya mwaka wa fedha 2019/2020.

ii. Kupungua kwa mapato yatokanayo na Chelezo (Slip Way Revenue) kwa asilimia sawa 70 ambayo ni sawa na TSH. 116,726,277 ya makadiro ya mwaka (TSH.165,705,550), ambapo mapungufu haya yamesababishwa na upokeaji wa meli zinazokaa chelezoni zina muda mdogo, uzito na urefu mdogo kwa sababu mapato yetu yanatokana na uzito na urefu wa meli kwa mwaka 2019/2020.

Shirika limepokea ushauri wa Mkaguzi juu ya kuimarisha vyanzo vyake vya mapato na pamoja na kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa Shirika, kwa sasa Shirika limeimarisha chanzo chake cha mapato mengineyo kwa kuifanyia matengenezo Meli ya LCT Jitihada na pamoja na vyanzo vyengine.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini na kupendekeza yafuatayo:

Kamati ya LAAC baada ya kupitia hesabu ya mwisho wa mwaka ya Shirika la Bandari, iligundua kuna mapato yatokanayo na zabuni (tender income) Shirika iliyakusanya lakini hawakupanga katika bajeti yao, Kamati ilielezwa kuwa Shirika hufanya hivyo kwa vile hushindwa kujua kiasi cha fedha watakayoweza kupata. Kamati haikuridhishwa na hali hiyo na kupendekeza kwamba kwa vile Shirika linafahamu kuwa litahitaji kufanya zabuni, fedha za chanzo hicho kinatakiwa kioneshwe wazi ili Shirika liweze kujitathmini kwa kiasi gani imelifikia lengo hilo.

Hivyo, Kamati ya LAAC imelishauri Shirika lifanye utafiti mdogo wa kujua vyanzo vyake vyote na kuviingiza hesabu zao za mwisho wa mwaka kuwa ni vyanzo vinavyojitegemea.

Aidha, Kamati imegundua kwamba Shirika halijalifanyia marekebisho daftari la kumbukumbu za ghalani kwa kuingiza baadhi ya vifaa vilivyokosekana kama ilivyoelekezwa na Mdhibiti kwa vile Shirika lina mpango wa kuandaa mfumo wa

TEHAMA utakaokuwa na daftari la kumbukumbu za ghalani ili iwe rahisi kuweka kumbukumbu hizo na kuondokana na daftari la nakala ngumu (hard copy). Kamati imesikitishwa na kitendo cha Shirika kutoliboresha daftari la kumbukumbu za ghalani licha ya Mdhibiti kubainisha kasoro hiyo. Kwa mnasaba huo, hoja hiyo itaweza kujirudia tena katika mwaka wa fedha ujao iwapo Shirika litakuwa halijakamisha mfumo huo.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kwamba Shirika halina mpango wa kufanya marekebisho na matengenezo ya vifaa vyake (repair and mentenence register) badala yake hufanya kazi kwa mazoea katika utengenezaji wa vifaa vinavyoharibika. Kamati ilishitushwa na majibu ya Shirika na kueleza kwamba kwa Shirika kama la Bandari halitegemewi kukosekana kwa mpango huo.

Hivyo, Kamati imelitaka Shirika kuhakikisha kuwa linaandaa mpango wa marekebisho na matengenezo ya vyombo vyao ili uweze kuwa dira ya matengenezo ya vifaa vyao na kuondokana na mrundikano wa makachara.

Katika utekelezaji wa shughuli za Shirika za kila siku, Kamati imebaini kwamba kuna upotevu mkubwa wa mapato na matumizi ya fedha yanayosababishwa na urasimu unaosababishwa na taratibu ndefu za manunuzi (Sheria namba 11 ya 2016) ambazo zinakwaza ufanisi wa haraka wa Shirika. Kwa mfano, Shirika litahitaji kuzabuni, wafanyabiashara wachukue, wajaze na kurudisha zabuni hizo, zifunguliwe, zikaliwe na Kamati ya Tathmini, kutangazwa mshindi, hatua ya mikataba na hatimae utekelezaji. Hatua zote hizo zinahitaji muda ili kuingia katika hatua nyengine. Hivyo, kwa Shirika la Bandari mazingira hayo hayapo rafiki na utendaji wao.

Pamoja na sababu zilizoelezwa na Shirika la Bandari kuhusiana na Shirika hili kutokufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato, Kamati ya LAAC imebaini kuwa sababu nyengine ni uwepo wa mizani moja tu ya kupimia mizigo kwa Unguja na kutokuwepo kwa mizani kama hiyo kwa upande wa Pemba.

Ili kujiridhisha na utendani wa mizani hiyo, Kamati ya LAAC ilifanya ziara ya ukaguzi na katika mahojiano na Watendaji wa Shirika hili ilibaini kuwa kuna upotevu mkubwa wa mapato katika kianzio hicho cha mapato kutokana na sababu zifuatazo:

i. Baadhi ya gari haziwezi kupita juu ya mizani hiyo kutokana na maumbile ya mizani hiyo; na
ii. Asilimia kubwa ya gari zinazobeba mizigo kutokea eneo la Bandari ya Malindi

kwenye Majahazi haziendi kwenye mizani kwa ajili ya kupimwa.

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC ilitaka kujua Shirika la Bandari limejipanga vipi katika kutatua changamoto hizo na waiielezwa Kamati kuwa katika hatua ya awali katika mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika hilo limepanga kununua mizani nne ambapo Pemba itapelekwa mizani 1 na Unguja zitakuwepo mizani 3.

Pamoja na majibu hayo ya Shirika, Kamati ya LAAC imelishauri Shirika la Bandari kuzidi kuwa makini katika kukusanya mapato yake kwani nchi zilizozozungukwa na bahari hunufaika zaidi na mapato yanayotokana na bandari.

Taarifa ya Matumizi

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini Matumizi ya Shirika la Bandari Zanzibar yameonekana kupungua kutoka TSH. 31,129,110,374.66 kwa mwaka wa fedha 2018/2019hadi kufikia 29,801,710,959 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na na upungufu wa Tsh. 1,327,399,415.66sawa na asilimia 4.3.

Pia, ukaguzi umebaini kuwepo kwa upungufu wa asilimia 19.22(TSH. 6,922,576,863.87) ya matumizi halisi (TSH.29,089,905,366.12) kwa kulinganisha na makadirio ya matumizi (TSH.36,012,482,230) kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Majibu ya Shirika

Ni kweli matumizi yamepungua katika mwaka fedha 2019/2020 kama ukaguzi ulivyobaini ukilinganisha na Makadiro ya matumizi ya mwaka huo. Mapungufu haya yamesababishwa na mambo yafuatayo:

i. Kutolipwa mishahara iliyopangwa kutokana na kutopita kwa muundo mpya wa mishahara ambao kwa mwaka huu bajeti yake ilipangwa.
ii. Kupungua kwa gharama za shughuli mbali mbali za upakiaji na upakuzi bandarini ambazo zinatokana na kupungua kwa ujaji wa meli kubwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa Daftari la Kuhifadhia Mali (Asset Register) na ilibaini kuwa baadhi ya vifaa havikuingizwa katika Daftari hilo ingawa kwenye Taarifa ya Fedha (Financial Statement) vimetajwa.

Katika kutatua changamoto hiyo Kamati ya LAAC imelishauri Shirika hili kumteua mtu maalum ambaye atatunza mali za Shirika.

Vile vile, Kamati ya LAAC imebaini kuwa mfumo unaotumiwa na Shirika wa kuwekea kumbukumbu za mali ni wa zamani. Hivyo, Kamati hii imelishauri Shirika kufanya mawasiliano na Idara ya Mitaji ya Umma ili Shirika hilo liwe na Daftari la Kuhifadhia Mali ambalo linakwenda na wakati.

Aidha, Kamati ya LAAC imelishauri Shirika hili kuwa na Daftari la Kuhifadhia Mali ambalo litapatikana na njia ya "soft copy" ili iwe rahisi kuingiza taarifa pale wanapopata au wanapoiondoa mali.

Sambamba na hayo, Kamati ya LAAC imelishauri Shirika hili kuwa na "Repair and Maintanance Register" ili iwe rahisi kujua:

i. muda gani kifaa/chombo husika kinatakiwa kufanyiwa "service"; na
ii. ni kifaa/chombo kipi ambacho hutengenezwa mara kwa mara ili kiweze kuondoshwa "disposed".

Halikadhalika, Kamati ya LAAC imebaini ushirikiano mdogo baina ya Mtu wa Hesabu, Ufundi "Techinical" na Ununuzi jambo lililopelekea kununuliwa vifaa ambavyo viko kinyume na mahitaji yao.
Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imewashauri Watendaji hao kufanya kazi zao kwa karibu ili kuepuka kulitia hasara Shirika hili kwa kununuliwa vifaa/chombo ambavyo havina tija kwa Shirika.

Ufanisi katika uendeshaji wa Shirika la Bandari Zanzibar (Operating Performance)
Katika mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini kuwa mapato yatokanayo na Bandari (Port Income) yameongezeka kutoka Tsh. 33,313,879,874 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi Tsh. 34,323,110,123.27 kwa mwaka wa fedh 2019/2020 kukiwa na ongezeko la TSH. 1,009,230,249.27 sawa na asilimia 3, kwa ujumla ya mapato ya Shirika la Bandari kwa vyanzo vyote vya mapato yamepungua kutoka Tsh. 37,506,713,123.20 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ukilinganishana TSH. 36,216,887,383.90 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji wa zimepungua kutoka TSH. 31,129,110,374.7 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ukilinganisha na TSH. 29,089,905,366 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo gharama zimepungua kwa TSH. 2,039,205,008.80 sawa na asilimia 6.5.

Majibu ya Shirika

Shirika limepokea ushauri wa mkaguzi juu ya kuimarisha vyanzo vyake vya mapato pamoja na kubuni vyanzo vipya vya mapato. Kwa sasa Shirika limeimarisha chanzo chake cha mapato kwa kuiboresha kiutendaji meli ya LCT Jitihada.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC iliridhika na majibu hayo na ilizidi kusisitiza kufanyiwa kazi mapendekezo ya Kamati iliyoyatoa kwenye kipengele cha Taarifa za Mapato.

Ufanisi katika utendaji wa kifedha (Financial Performance)

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini uwezo wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi umeongezeka na kufikia uwiano wa 9:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2020 ukilinganisha na uwiano wa 6.9:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2019, uwezo wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi ni mkubwa zaidi ya kiwango kinachohitajika uwiano ambao si mzuri sana kifedha, fedha hizi zingeweza kuwekezwa katika hesabu za amana za kibenki na Shirika kuweza kupata faida ya malipo ya riba.

Kwa mujibu wa vigezo vinavyohitajika kiuhasibu vya uwezo wa Shirika kumudu dhima za mpito ni uwianowa 2:1 ambapo unaonesha uwezo mzuri wa kifedha wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi.

Majibu ya Shirika

Ushauri wa Mkaguzi umepokelewa, ambapo Shirika limeanza na taratibu za kutafuta uwezekano wa kuwekeza fedha za matumizi kwa muda mfupi kwa kutegemea kuongeza chanzo cha mapato yatokanayo na riba kwa fedha zilizowekezwa kwa muda mfupi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kuwaShirika la Bandari halina sera inayohusiana na masuala ya fedha jambo ambalo linapelekea Shirika hili kuwachukulia hatua wale wote ambao inawapa huduma.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ya LAAC imelishauri Shirika hili kuandaa sera hiyo ili liweze kuwachukulia hatua wale wote ambao watakwenda kinyume na sera hiyo.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.5.1 Madeni yasiyolipwa kwa muda wa mrefu TSH. 467,856,819.73

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa madeni ya muda mrefu jumla TSH. 467,856,819.73 fedha ambazo hakuna jitahada zozote zilizofanywa katika ufuataliaji wa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa, jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa Shirika kujiendesha kiufanisi.

Ukaguzi unashauri Shirika la Bandari Zanzibar, kuandaa mikakati na mbinu zitakazowezesha kukusanya madeni hayo kwa wakati pamoja na kuaandaa sera ya ufuatliaji wa madeni.

Majibu ya Shirika

Ni kweli kuwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Shirika hili linadaiwa kiasi hicho cha fedha, hata hivyo, taratibu zimeanza kuchukuliwa kwa kuwaandikia barua za ukumbusho wadaiwa na Shirika na uongozi umepanga taratibu za kuwatambua uwepo wao pia na kutizama taratibu za kisheria ya kufuta madeni yote yaliyokuwa hayawezi kulipika kutokana na kufilisika kwa taasisi zilizokuwa zikidaiwa na Shirika na pamoja kuomba muongozo wa Serikali kuu juu ya Taasisi za Serikali zilizodaiwa na Shirika.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

1. Bado juhudi zilizochukuliwa na Shirika za kudai fedha hizo haziridhishi, kwani kati ya Wadaiwa wote 24 ni Wadaiwa watatu tu waliopatiwa barua ya kukumbusha deni lao na Shirika.
2. Kampuni ya Mecco imepunguza deni lake, ambapo hadi Kamati hii inafanya ziara yake tarehe 18 Agosti, 2021 inadaiwa Tsh. 62,000/- tu badala ya Tsh. 6,970,035/- zilizoripotiwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu.
3. Shirika hili limerithi baadhi ya madeni kutoka Wharfage ndio mana kiwango cha deni hilo linaonekana kubwa.
4. Shirika la Bandari halina sera inayosimamia masuala ya fedha jambo ambalo linaliwia vigumu kuwachukulia hatua wale wote wanaoshindwa kulipia huduma wanayopatiwa na Shirika hilo.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro hizo zilizobainika Kamati ya LAAC imelitaka Shirika la Bandari kutekeleza yafuatayo:

i. Kuhakikisha kuwa Wanadaiwa hao wanalipa deni lao katika kipindi kifupi kijacho ili kulinda fedha za umma.
ii. Kuandaa sera maalum inayohusiana na masuala ya fedha ili kuwashukulia hatua wale wote watakaokwenda kinyume na sera hiyo.

3.5.2 Kukosekana kwa uhalisia wa bajeti

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari katika uhalisia wa bajeti ya mapato yaliyokadiriwa kukusanya kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Makadirio halingana na mapato halisi ya fedha yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 jambo ambalo limepelekwa kukosekana kwa uhalisia wa makadirio ya bajeti na kupelekea uwepo wa tofauti kubwa iliyobainika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari kutengeneza bajeti zinazozingatia uhalisia na kuweka mbinu madhubuti na endelevu zitakazotuhakikishia kupanda kwa makusanyo ya mapato.

Majibu ya Shirika

Vigezo vilivyotumika ni muelekeo halisi wa biashara kwa mwaka uliopita 2018/2019, huduma tulizotoa ni pamoja na muelekeo wa uchumi wa kitaifa na kimataifa kama inavyoonekana katika ripoti utekelezaji.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

1. Bajeti ya Shirika la Bandari imeonekana kupanda sana kwa kuwa Shirika hili lilifanya makisio ya bajeti yao kwa kipindi cha miezi 9 tu badala ya mwaka (miezi 12).

2. Baadhi ya shughuli hazikupangiwa bajeti kwa kuwa zilionekana ni shughuli za msimu.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeza tena katika siku zijazo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Shirika la Bandari ikipanga bajeti yake ipange bajeti ya mwaka mzima badala ya miezi 9.

2. Wahakikishe kuwa shughuli zote zinapangiwa bajeti ili kuepusha dosari zisizo za msingi.

3. Wanapopanga bajeti wahakikishe kuwa makisio wanayoweka ni makubwa ili

kupata ari ya kukusanya, kwani, endapo watakisia kidogo kuna uwezekano mkubwa wa kukusanya mapato kinyume na uhalisia wake.

3.5.3 Kutofuatwa kwa viwango vya kimataifa vya uandaaji na utayarishaji wa Taarifa za Hesabu kwa kipengele cha sera ya Uhasibu (IAS 8)

Ukaguzi umebaini Shirika la Bandari limefanya mabadiliko kadhaa katika sera ya uhasibu kuhusu tathmni ya mali za kudumu. Katika mabadiliko hayo Shirika limebadilisha mfumo wa gharama na kwenda kwenye mfumo wa uhakiki kutokana na zoezi la uhakiki lililofanyana Mthamini wa mali za kudumu kulingana na mahitaji ya viwango vya uhasibu, mabadiliko yoyote katika sera ya uhasibu yanapaswa kuhesibiwa na kuzingatiwa mwaka wa fedha ulipita. Ukaguzi umebaini Shirika la Bandari limekiuka utaratibu ulioweka kwa mujibu wa viwango vya uhasibu. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na viwango vya kimatifa vya uandaji na utayarishaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka (IAS 8).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari kufuatia viwango vya kimataifa vya uhasibu ili taarifa za uhasibu ziwezekuonesha sura halisi na sahihi.

Majibu ya Shirika

Kutokufuatwa kwa viwango vya kimataifa kumetokana na uelewa mdogo wa watendaji kuhusiana na viwango vya kimataifa. Uongozi wa Shirika la Bandari umepokea ushauri na kuahidi kuendelea kutumia vigezo vilivyowekwa katika uandaaji wa taarifa za hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa ili hesabu za Shirika ziweze kuonesha sura halisi na sahihi na kwa kufanya hivi Shirika limepatiwa mhasibu kutoka Afisi ya Raisi, Fedha na Mipango mwenye uelewa na ujuzi wa viwango vya kihasibu kitaifa na kimataifa.

Kwa kuhakikisha matumizi sahihi ya viwango vya kitaifa na kimataifa uongozi katika mwaka wa fedha imepangaa kuandaa “Accounting policies, Accounting manual” pamoja na fixed asset management Policies” za Shirika la Bandari ambazo zitasaidia kuhakikisha hesabu zinaandaliwa kulingana na matakwa ya viwango vya kitaifa na kimataifa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC imeridhika na majibu ya Shirika hili, hata hivyo, imemtaka Mtendaji huyo kutekeleza majukumu yake kama Sheria zinavyoelekeza.

3.5.4 Kutofautwa kwa viwango vya kimataifa vya uandaaji na utayarishaji wa Taarifa za hesabu kuhusu mahusiano ya pande mbili za mkataba (IAS 24).

Kukosekana kwa utoaji wa taarifa ya wazi ya mahusiano ya karibu baina ya Uongozi wa juu wa Shirika la Bandari ambao unatokana na Kikosi Maalum cha Kuzuwia Magendo (KMKM) na Kikosi cha KMKM (Disclosure for the related party).

Majibu ya Shirika

Kutofuatwa kwa viwango vya kimataifa kumetokana na uelewa mdogo wa watendaji kuhusiana na viwango vya kimataifa. Shirika limepatiwa Mhasibu kutoka Afisi ya Raisi, Fedha na Mipango mwenye uelewa na ujuzi wa viwango vya kihasibu kitaifa na kimataifa.

Hata hivyo, katika kitabu cha fedha kilichofanyiwa marekebisho kutokana na hoja za ukaguzi kimeweka wazi uhusiano huo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Licha ya kasoro zilizobainika na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, vile vile, katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa baadhi ya Vifungu havikuwekwa Nambari "Note" kama taratibu za fedha zinavyoelekeza. Kwa mfano vifungu vinavyohusiana na "Other Income" na "Other Expenses".

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC ililishauri Shirika hili kuwa makini katika kutekeleza majukumu yake, ingawa limepatiwa Mhasibu mwenye uelewa na ujuzi wa viwango vya kihasibu kitaifa na kimataifa.

Aidha, Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa maelezo zaidi juu ya kwa nini Shirika la Bandari limewapatia kazi Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo badala ya mtu mwengine?

Kutokana na swali hilo, Kamati hii ilielezwa kuwa Shirika lilikipatia Kikosi hicho kwa kuwa kazi zinazofanywa na KMKM ni nzuri na zinajitangaza.

Kamati ya LAAC imeridhika na majibu ya Shirika hili, hata hivyo, imewataka Watendaji wa Shirika kuwa wazi pale Mkaguzi Mkuu anavyotekeleza majukumu yake ili kuepusha hoja zisizo na msingi.

3.5.5 Mapungufu katika kuzingatia utaratibu wa ununuzi wa umma katika ujenzi wa ghala la Saateni TSH. 674,949,910.

Ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Bandari Zanzibar liliingia Mkataba na Kikosi Maalum cha Kuzuwia Magendo (KMKM) kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Ghala la kuhifadhia bidhaa Saateni kwa gharama za Shillingi 674,949,910. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokufuatwa kwa taratibu za ushindani za kumtafuta Mzabuni wa kazi hiyo na kutumika kwa gharama kubwa ukilinganisha na hali halisi ya ujenzi huo na kupelekea thamani halisi ya fedha (VFM) kushindwa kupatikana.

Majibu ya Shirika

Ni kweli Shirika la Bandari halikufuata taratibu za ushindani za kumtafuta Mzabuni kwa ajili ya kazi ujenzi wa ghala la kuhifadhia bidhaa Saateni, uongozi ulifanywa hivyo baada ya kupata agizo kutoka Baraza la Mapinduzi kupitia barua yenye kumbukumbu namba MOCIT/B.40/C.3/VOL.IV/19 ambapo Shirika liliagizwa kufanywa ujenzi kwa njia ya dharura kwa kuipa kazi hiyo vikosi. Hivyo, Shirika lilifanya maamuzi ya kuipatia kazi hiyo Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), kwa kuzingatia kuwa Kikosi cha KMKM ndio kikosi kinachotumiwa katika majengo ya kimkakati ya Serikali. Aidha, KMKM ni ndio kikosi chenye uwezo katika ujenzi kulinganisha na Vikosi vingine vya Idara Maalum za Serikali.

Kuhusu hoja ya kutofikiwa kwa viwango vya ujenzi wa ghala na kupelekea gharama kubwa kulinganisha na thamani na hali halisi ya ujenzi huo na kupelekea thamani halisi ya fedha kutopatikana. Shirika la Bandari baada ya kupokea agizo kutoka Baraza la Mapinduzi liliandaa design, michoro na BOQ ya jengo hilo ambalo litakuwa na uwezo wa kubeba uzito wa Tani kwa mita ya mraba 4tonnes/m^2 kama uwezo wa gati yetu ambapo jengo litaweza kuhudumia gari la kontena lenye mzigo kuingia ndani. Shirika liliiandikia Makao Makuu ya KMKM na kuwataka kuleta thamani ya ujenzi wa ghala hilo kulingana BOQ na mchoro uliotayarishwa na Shirika. Gharama za KMKM zilikuwa kubwa kwa asilimia 1.5 ambayo kimsingi inakubalika.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Shirika la Bandari halikuunda Kamati maalum ya kufuatilia ujenzi huo kama Sheria ya Ununuzi inavyoelekeza na badala yake ujenzi huo ulisimamiwa na Idara ya Ujenzi ya Shirika, jambo ambalo ni kinyume na Sheria ya Ununuzi.
2. Shirika la Bandari halikumtafuta Mshauri Elekezi wa kusimamia ujenzi huo kama Sheria ya Ununuzi inavyoelekeza na badala yake ujenzi huo ulisimamiwa na Idara ya Ujenzi ya Shirika, jambo ambalo ni kinyume na Sheria ya Ununuzi.
3. Afisa Manunuzi hakushirikishwa ipasavyo wakati wa ujenzi huo jambo ambalo ni kinyume na Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2016.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikupata muda wa kukagua ujenzi wa ghala la kuhifadhia bidhaa huko

Saateni kutokana na shughuli nyingi, hata hivyo, kutokana na kasoro hizo zilizozibaini ililishauri Shirika la Bandari kutekeleza majukumu yake kwa mujibu ya matakwa ya Sheria ili kuepusha kasoro zisizo na lazima.

3.5.6 Thamani ya mali za kudumu ambazo hazikuoneshwa katika hesabu za mwisho wa mwaka za Shirika la Bandari.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini kuwa hakuna ufafanuzi wa thamani za mali za kudumu hazikuoneshwa katika hesabu za mwisho wa mwaka za Shirika la Bandari ikiwemo majengo,ardhi na vyenginevo. Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba Shirika la Bandari limeshindwa kuonyesha hivyo ni kwenda kinyuma na viwango vya uandaaji na utayarishaji wa Taarifa za hesabu.

Majibu ya Shirika

Ni kweli ufafanuzi wa thamani za mali za kudumu hazikuoneshwa ni kutokana na makosa ya kiutendaji lakini katika kitabu cha fedha cha marekebisho taarifa hiyo tayari imeambatishwa ukurasa wa 45 wa ripoti ya fedha ya mwaka 2019/2020. Hata hivyo, Uongozi wa Shirika la Bandari katika kuhakikisha inaandaa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na kitaifa imejipanga katika mpango wa mwaka 2021/2022 kuwajengea uwezo watendaji wake wa Kitengo cha Fedha kuhusu uelewa wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya ufungaji wa hesabu za fedha.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na majibu hayo ya Shirika, Kamati ya LAAC imeibakisha hoja hii kama ilivyo. Hii ni kutokana na kuwa Shirika la Bandari limekiri kufanya marekebisho katika Kitabu chake cha fedha, hata hivyo, hadi Kamati hii inafanya ziara katika Shirika hilo Kitabu hicho hakijawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama taratibu zinavyoelekeza.

SHIRIKA LA BANDARI – PEMBA

3.5.7 Malipo Kinyume na Taratibu za Utumishi Tsh. 55,944,292.3

Jumla ya shiling 55,944,292.3 zimelipwa kwa siku za mapumziko na muda baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi wa Shirika la Bandari Pemba.

Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakuzingatia taratibu za utumishi wa umma juu ya uwepo wa barua ya kufanya kazi siku za mapumziko na muda baada ya saa za kazi kwenda kwa ofisa mdhamini Pamoja na uwepo wa fomu maalum ya malipo (overtime sheet) kwa wafanyakazi wa Wizara.

Majibu ya Shirika

Ni kweli kwamba wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa malipo ya muda baada ya saa za kazi "overtime" hayakuzingatia baadhi ya taratibu za utumishi wa umma juu ya uwepo wa barua ya kufanya kazi kwa siku za mapumziko na muda baada ya saa za kazi pamoja na fomu maalum za malipo (over time sheet). Hali hiyo imetokana na kufata utaratibu wa zamani wa Shirika ambapo Mkuu wa Bandari husika alipatiwa kitabu maalum cha Shirika cha kuwekea kumbu kumbu za masaa ya ziada pale ilipobidi kufanya hivyo kwa baadhi ya watendaji ama kwa siku za sikukuu na mwisho wa mwezi kuwaombea malipo kwa Mkurugenzi wa Tawi huku akiambatanisha na vielelezo vya kazi iliofanyika kwa kila mfanyakazi alieombewa, siku, tarehe na muda uliohusika "Overtime record".

Hivyo, kwa utaratibu huo, kulikuwepo na barua ya jumla kutoka kwa Wakuu wa Vituo na ufafanuzi wa kila mfanyakazi aliehusika, na baada ya Uongozi kuridhika na usahihi wa maombi hayo, hatua za malipo zilifanyika. Pamoja na hayo na kwa kuzingatia muongozo uliotolewa ndani ya Shirika na ambao umeenda sambamba na mapendekezo ya Ukaguzi kuhusiana na utaratibu wa kuomba kwa barua kabla, uhitaji wa wafanyakazi kwa kazi za muda baada ya muda wa kawaida ama sikukuu, tayari Tawi linafuata utaratibu huo ili kuenda sambamba na taratibu za kiutumishi.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kuifanyia kazi hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Ingawa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibaini kuwa kuna ukiukwaji wa baadhi ya taratibu za kazi katika Shirika hili, na ingawa Shirika limeahidi kufuata mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi kuhusiana na utaratibu wa kuomba kwa barua kabla. Hata hivyo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa kutokana na asili ya shughuli zao kuna uwezekano mkubwa wa taratibu hizo kushindwa kuzifuata. Hii ni kutokana na kuwa zipo baadhi ya shughuli wanazozifanya hazitoweza kusubiria kibali ndio zitekelezwe inawalazimu kwanza waokoe hali iliyokuwepo.
2. Baadhi ya watendaji hawana uelewa mpana kuhusiana na kazi zao.
3. Shirika la Bandari Pemba halina Mwanasheria, hivyo, wanategemea Mwanasheria kutoka Afisi ya Unguja ambae ni mmoja tu.
4. Shirika la Bandari Pemba haliandai taarifa za fedha za kwa ajili ya Pemba "segment report" tu, jambo ambalo linamnyima mtu kuweza kujua maendeleo au utendaji wa Shirika kwa upande wa Pemba pekee.
5. Shirika la Bandari Pemba lilitumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya mafunzo ya watendaji kwa kuwapatia mafunzo watendaji kinyume na taaluma au shughuli zao.
6. Shirika hili lina idadi kubwa ya watendaji ambapo asilimia kubwa ya watendaji hao ni Makuli na wachache wenye taaluma.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Shirika la Bandari liwe na utaratibu wa kuandaa taarifa ya fedha kwa upande wa Shirika la Bandari Pemba pekee ili kumuwezesha mtu kujua taarifa za kifedha za Pemba tu.
2. Shirika hili lihakikishe kuwa linawapatia mafunzo watendaji wake kwa mujibu wa fani zao ili ipatikane thamani halisi ya matumizi ya fedha hizo.
3. Shirika la Bandari Pemba lihakikishe kuwa linawapatia mafunzo watendaji wake ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuachana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea.
4. Shirika la Bandari Pemba liajiri Mwanasheria ili liweze kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria za nchi.
5. Kwa kuwa Shirika hili lina mpango wa kuanza kutoa huduma zake kwa kutumia mtandao (TEHAMA), na kwa kuwa Shirika hili lina idadi kubwa ya watendaji ambao kuna uwezekano mkubwa wa kupoteza ajira zao, na kwa kuwa watendaji hao wanategemewa na familia zao. Hivyo basi, Shirika la Bandari Pemba liandae utaratibu maalum wa kuwaweka kisaikolojia watendaji wake ambao watapoteza ajira zao, ili muda huo ukifika iwe rahisi kwao kujua wataendesha vipi maisha yao.

   Vile vile, kwa kuwa Shirika hili lina nia ya kutoa huduma zake kwa njia ya mtandao, Kamati ya LAAC inalishauri Shirika kutokuajiri watendaji wapya kwa zile nafasi za watendaji ambao wanastaafu ili kuepusha kustaafisha “redundance” idadi kubwa ya watendaji

3.5.8 Malipo Yaliokosa Kukatwa Kodi ya Zuio Shilingi 17,040,000

Jumla ya shilingi 17,040,000/- zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Bandari Pemba kwa Wafanyabiashara tofauti. Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakukatwa kodi ya zuio (TRA/ZRB) na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hio.Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Shirika

Ni kweli kuwa ukaguzi ulibaini tatizo la kutokukatwa kodi ya zuio katika manunuzi ya huduma yenye thamani ya Tsh. 17,040,000/= ambazo Tawi liliwalipa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa miezi tofauti. Hali hiyo ilitokana na kutokufahamu kuwa pamoja na kuwa JKU ni Taasisi ya Serikali, lakini pia ilihitajika kukatwa kodi hiyo kwani malipo

mengineyo yote yalikatwa kwa mujibu wa taratibu. Kutokana na maelekezo hayo tayari Shirika limeshaanza kufuata utaratibu huo mpya wa kukata kodi katika malipo yao yanayoendelea kila mwezi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC imekifanyia marekebisho Kitabu cha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kuitambua Hoja iliyoandikwa Namba 3.5.7 katika ukurasa wa 55 wa Kitabu hicho kusomeka kuwa Hoja Namba 3.5.8 na Hoja zinazoendelea zitafuata mpangilio huo. Hii ni kutokana na kuwa tayari Hoja Namba 3.5.7 inasomeka katika ukurasa wa 53 wa Kitabu hicho.

Kwa upande wa hoja husika, Kamati ya LAAC imeibakisha hoja hiyo kama ilivyo, kwa kuwa matakwa ya Sheria hiyo yapo tangu mwaka 2016. Kamati ya LAAC imefikia maamuzi hayo kwa kuwa, kwa kawaida Shirika la Bandari ndio linalopaswa kuizuia kodi hiyo na endapo litashindwa kufanya hivyo, basi Mamlaka ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ilipaswa kuzuia kodi hiyo.

3.5.9 Malipo kwa Wafanyabiashara ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi Shilingi 55,356,201

Jumla ya shiling 55,356,201/- zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Bandari – Pemba kwa Wafanyabiashara tofauti.

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyabiashara hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi ili kuweza kufanya biashara na taasisi za serikali.

Majibu ya Shirika

Ni kweli katika ukaguzi imebainika kuwa baadhi ya wafanyabiashara hawajasajiliwi na Mamlaka ya Ununuzi. Hata hivyo, baada ya Shirika hili kuwafuatilia zaidi, iligundulika kuwa baadhi yao tayari walishasajiliwa na kwa wale wachache ambao hawakusajiliwa walielekezwa juu ya utaratibu unaotakiwa ili waweze kufanya biashara na Taasisi za Serikali kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa pale itapohitajika na wanaendelea kujisajili. Pamoja na hayo, kwa sasa Shirika linafanya manunuzi na wafanyabiashara waliosajiliwa tu na kabla ya kufanya nao biashara Shirika hujiridhisha kuwa ni kweli mfanyabiashara huyo amesajiliwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC ilikubaliana na majibu hayo, hata hivyo, ililitaka Shirika hilo kuzidi kuwa makini pale wanapohitaji huduma kutoka kwa Wafanyabiashara. Kwani kwa mujibu wa

Sheria ya Ununuzi Wafanyabiashara hao wanatakiwa kukata leseni kwa Mamlaka husika kila mwaka.

3.5.10 Masurufu Yasiokuwa na Marejesho (Returns) Shilingi 25,220,260

Jumla ya Shilingi 25,220,260/- zimelipwa kwa matumizi madogo madogo ya Shirika la Bandari Pemba kupitia masurufu mbali mbali.

Ukaguzi umebaini kwamba kutokuambatanishwa kwa baadhi ya marejesho ya masurufu katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Majibu ya Shirika

Wakati ulipofanyika ukaguzi kulibainika kuna baadhi ya malipo ya masurufu yasiyokuwa na marejesho kiasi cha Tsh. 25,220,260/-. Hata hivyo, baada ya wahusika wa Kitengo cha Fedha kuangalia kumbukumbu za malipo ya masurufu hayo, walibaini kuwa marejesho yote yapo, isipokuwa kwamba, baadhi ya marejesho yalifunganishwa na vocha tofauti na mengine hayakufunganishwa na hati husika na kupelekea kuhifadhiwa katika mafaili mbali mbali. Kwa mantiki hiyo, marejesho yote yaliyokusudiwa yapo na hivi sasa yeshaambatanishwa vizuri katika hati husika na yako tayari kwa kufanyiwa ukaguzi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na maelezo ya Shirika waliyoyatoa mbele ya Kamati hii, Kamati ya LAAC imebaini kuwa kuna uwekaji mbaya wa kumbukumbu katika Shirika hilo jambo lililopelekea kuibuka kwa Hoja hiyo. Hivyo, Kamati ya LAAC imewataka Watendaji wa Shirika kufanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu ili kuepuka kasoro zisizo na msingi.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Shirika juu ya Hoja hiyo, hivyo, imebaki kama ilivyo.

Mengineyo

Baada ya majadiliano kumalizika kuhusiana na Hoja zilizomo katika Kitabu cha Mkaguzi Mkuu, Kamati ya LAAC ilibaini na kushauri yafuatayo:

1. Kamati iliomba ufafanuzi kwa baadhi ya vianzio vya mapato ambavyo vilikusanya kidogo na kupata ufafanuzi kama ifuatavyo:

    a. Kianzio cha “Hire of Equipment”, Shirika lilipata mapato madogo kwa kuwa Shirika hili kwa Pemba linamiliki ‘crane” moja tu ambayo hutumika zaidi katika shughuli za Serikali.

    b. Vianzio vya “Tug and Pilot Service” havikukusanya sana kwa kuwa meli za

kigeni hazikuwasili katika mwaka huo wa fedha.

2. Vifungu vya fedha vilivyoidhinishwa kutumika Pemba vitumike kama vilivyopangwa. Kamati ya LAAC imeshauri hivyo baada ya kubaini kuwa baadhi ya vifungu kama vile kifungu cha Sare "uniform" kilichotengewa Tsh. 11,950,000 na kifungu cha matumizi ya Bodi likichotegewa Tsh. 20,000,000 havikutumika kama vilivyokusudiwa.

3. Baadhi ya gari zinazopakia mizigo kutoka Bandarini zinapakia zaidi ya uwezo wake jambo linalopelekea kuharibika kwa barabara. Hivyo, Kamati ya LAAC inalishauri Shirika hili kuzidi kuona umuhimu wa kuweka mizani na kwa upande wa Pemba ili kunusuru hali hiyo.

4. Shirika la Bandari Pemba lisipange makadirio madogo ya bajeti kwa lengo la kuonekana kuvuka malengo.

5. Shirika la Bandari Pemba lihakikishe kuwa linadhibiti Bandari zote zisizo rasmi maarufu Bandari Bubu ili kuongeza mapato ya Bandari.

3.6: SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2019/2020

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umebaini kwmaba mapato ya Shirika la Biashara la Taifa yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 10,021,596,610.44 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi 56,795,231,494.32 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na ongezeko la mapato ya shilingi 46,773,634,883.88 sawa na asilimia 467.

Majibu ya Shirika

Shirika lilikubali kwamba ni kweli mapato yake yalionekana kuongezeka kwa asilimia 467, hali hiyo ilitokana na kuongezeka mauzo ya karafuu kutoka tani 215 zenye thamani ya shilingi 3,323,910,720.00 mpaka tani 4,685 zenye thamani ya shilingi 52,882,766,620. Kikawaida, mavuno ya karafuu huwa yanakuwa na mzao mkubwa kila baada ya miaka mitatu mabapo kwa mwaka 2019/2020, ilikuwa ndio mwaka uliozaliwa sana karafu na kuinua kiwango cha karafuu zilizouzwa.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika imebaini kwamba ubora wa karafuu za Zanzibar unaweza kuharibiwa iwapo kutaachiwa kuigia

kwa karafuu zinazotoka nje ya Zanzibar au wakulima kutodhibitiwa ipasavyo kuingiza vitu visivyotakiwa katika karafuu hizo.

Kwa upande wa chanzo cha mapato ya chakula na malazi, Kamati iligundua kuwepo kwa hasara inayotokana na huduma za chakula na malazi zinazotolewa katika nyumba za Makonyo - Pemba. Kamati ilipotaka kujua sababu ya kutokea kwa hasara hiyo, ilielezwa kwamba kuna changamoto katika uhalisia wa matumizi ya gharama za uendeshaji na utoaji wa huduma za chakula kwa wageni wanaofika kupatiwa huduma katika nyumba hizo. Kamati haikuridhishwa na majibu hayo kwa inafahamu faida inayopatikana kwa biashara za vyakula na vinywaji.

Kadhalika, Kamati yetu imegundua kwamba kuna tofauti ya jumla ya fedha za mapato zilizooneshwa katika kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (56,795,231,494.32) ukilinganisha na Ripoti ya utekelezaji wa mipango ya Shirika pamoja na ripoti ya Mkaguzi wa ndani iliyoonesha jumla ya shilingi 77.647,891,000 sawa na tofauti ya shilingi 20,852,659,506. Watendaji wa Shirika walieleza kwamba hali hiyo ilitokana na ripoti za utekelezaji huwa zinaandaliwa mapema kabla ya kuandaliwa ripoti ya fedha ya mwisho wa mwaka.

Taarifa ya matumizi

Kwa upande wa matumizi ya Shirika la Biashara la Taifa, yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 20,582,313,713.76 kwa mwaka 2018/2020 hadi kufikia shilingi 84,638,754,140.61 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na ongezeko la matumizi ya shilingi 64,056,440,426.85 sawa na asilimia 76.

Majibu ya Shirika

Shirika lilikubali kwamba ni kweli matumizi yake yameongezeka baina ya mwaka 2019 ukilinganisha na mwaka 2020. Hali hiyo ilisababishwa na kuongezeka matumizi ya fedha za kununulia karafuu katika mzao mkubwa kutoka 2,950,824,000 kwa ajili ya ununuzi wa tani 211.3 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi 62,908,204,500 kwa ununuzi wa tani 4,497.5 kwa mwaka 2019/2020 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 2028.5 za tani zilizonunuliwa.

Vile vile Shirika lilieleza kwamba liliweza kufanya matumizi ya kununua tani 190 za mchele kwa ajili ya hifadhi ya chakula kwa shilingi 403.18 milioni kutoka katika kampuni ya MW RICE MILLARS LTD.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilitaka kujua kwamba katika msimu huo mkubwa wa karafuu, mbona hakujaonekana uwekaji wa mageti ya kuzuia magendo ya karafuu hususan kisiwani

Pemba kama inavyokuwa wakati wa misimu wa uokoaji zao hilo. Shirika lilieleza kwamba katika hatua za kupunguza gharama, liliona ni vyema waondoe kikundi kazi (task force) na mageti ambayo yalikuwa yakitumia fedha nyingi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Shirika lihakikishe linaanda mikakati mizuri itakayoweza kutumika katika uokozi wa zao la Karafuu bila ya kutumia gharama nyingi.

Ufanisi katika uendeshaji wa Shirika la Biashara la Taifa (Operation performance)

Pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Shirika. ukaguzi umebaini kwamba gharama za uendeshaji nazo ziliongezeka hadi kufikia shilingi 84,638,754,140.61 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 20,582,313,713.76 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni ongezeko la shilingi 64,056,440,426.85 sawa na asilimia 76.

Katika tathmini ya vipindi viwili vya ufungaji wa hesabu, ukaguzi umebaini kwamba Shirika limeendelea kujiendesha kwa hasara, ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hasara hiyo imeongezeka hadi kufikia shilingi 27,843,522,646.29 ukilinganisha na hasara ya shilingi 10,560,717,103.32 ya mwaka 2018/2019 kukiwa na tofauti ya shilingi 17,282,805,542.97 sawa na asilimia 163.65.

Majibu ya Shirika

Shirika lilieleza kwamba ni kweli uchambuzi unaoonekana mapato na matumizi yameongezeka kwa mwaka 2019/2020 ukilinganisha na 2018/2019, hii imetokana na kuongezeka kwa manunuzi ya Karafuu kwa mwaka 2019/2020. Aidha, gharama za Uendeshaji kwa mwaka 2019/2020 ni 12,022,065,124.76 ukilinganisha na TZS 11,837,242,693.65 kwa mwaka 2018/2019 ikiwa ni ongezeko la TZS 184,822,431.11 sawa na asilimia 1.5. Hali hii inaonesha uongozi wa Shirika ulijitahidi kwa kiasi kikubwa kuweza kubana matumizi ukizingatia mwaka 2019/2020 kulikuwa na ongezeko kubwa la manunuzi na mauzo kiasi ambacho kilipelekea kuwa na gharama za moja kwa moja zinazohusiana na ongezeko hilo.

Hali ya hasara ya Shirika inachangiwa zaidi na uwepo wa gharama kubwa za mauzo (Cost of Sales) zinazotokana na bei kubwa ya karafuu aliyolipwa mkulima ukilinganisha na bei ya mauzo ya karafuu.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na majibu ya Shirika na hali halisi ya mfumo wa uendeshaji biashara ulivyo wa kununua na kuuza bidhaa, Kamati ilikubaliana na maelezo ya Shirika na kuendelea kuisisitiza Serikali kuliruhusu Shirika kununua karafuu kwa bei halisi ya soko la karafuu Ulimwenguni ili Shirika liweze kujiendesha na kufanya biashara yenye faida na sio

kupanga bei isiyozingatia soko linavyokwenda na kusababisha hasara za kiufanisi katika uendeshaji wa Shirika.

Ufanisi katika utendaji wa kifedha (Financial Performance)

Ukaguzi umebaini kwamba utendaji wa kifedha wa Shirika umedhoofika na kufikia uwiano wa mtaji wa 0.16:1 kwa mwaka 2019/2020 ukilinganisha na 6:1 kwa mwaka 2018/2019. Hali hiyo inaonesha kutokufikia kwa uwiano wa 2:1 (kwa mwaka 2019/2020) kama unavyohitajika na vigezo (Benchmark) vya uwiano wa mtaji kiuhasibu.

Aidha, kwa kipindi hicho cha miaka miwili ya fedha, inaonekana Shirika la Biashara la Taifa limedhoofika na halina uwezo wa kujiendesha kibiashara (halina uwezo wa kulipa madeni yake ya muda mfupi).

Majibu ya Shirika

Uongozi wa Shirika umejitahidi kutoa ripoti kwa Serikali kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi suala la Madeni makubwa yanayoikabili Shirika la Biashara la Taifa. Aidha, utendaji wa kifedha wa Shirika unaoonekana katika miaka miwili umetokana na maamuzi ya Serikali ya kulitaka Shirika kuendelea kununua Karafuu kwa bei ya juu wakati bei halisi katika soko la dunia imekuwa ikishuka.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati iliridhika na majibu yaliyotolewa na Shirika. Hata hivyo, imeishauri Serikali kwamba ili kuondoa ukwasi kwa Shirika, ni busara kwa Serikali itoe ruzuku kwa Shirika ili bei ya kununulia karafuu ibakie kama inavyopangwa hasa ukizingatia bei ya kununua na kuuza karafuu katika soko la duniani inakuwa inabadilika muda baada ya muda.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.6.1 Taarifa za Wadaiwa na Wadai wa Shirika

(a) Wadaiwa, shilingi 1,661,915,698.87

Ukaguzi umebaini uwepo wa madeni ya muda mrefu ambapo inaonekana jitihada hafifu zilizochukuliwa na kupelekea deni hilo kupungua kwa kiwango kidogo, jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa Shirika kujiendesha kibiashara. Aidha, ukaguzi umebaini deni linalodaiwa Shirika limepungua kwa kiwango kidogo kutoka shilingi 1,682,589,595.63 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi 1,661,915,698.87 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi 20,673,896.76 sawa na asilimia

moja ya deni hilo.

Sambamba na hilo, kutokuwepo kwa ufuatiliaji mzuri wa madeni kunapelekea uwepo wa madeni sugu ambayo hayatoweza kulipika na kusababisha hasara kubwa kwa Shirika na kuibebesha mzigo mkubwa Serikali. Miongoni mwa Wadaiwa wa Shirika ni pamoja na Rental Debtor-Rent Receivable Kitega Uchumi shilingi 426,920,461.54, staff loan shilingi 792,707,060.48 na shilingi 349,593,866.68 kwa Loan ZSTC - Dar es Salaam.

Majibu ya Shirika

Shirika limechukua jitihada mbali mbali kufuatilia madeni hayo na litaendelea kufuatilia ili kuhakikisha madeni yote yanalipwa kwa wakati. Aidha madeni hayo yamejumuisha Mikopo mbali mbali ambayo uhalisia wake inakatwa kila mwezi kama Mikopo ya Wafanyakazi na mikopo ya vespa kwa Masheha ambao kila mwezi wanakatwa katika mishahara yao. Mchanganuo wa upungufu wa madeni hayo ni kama ufuatao:

Nam.	Wadaiwa wa Shirika	Juni 2019 (Tzs)	Juni 2020 (Tzs)
1	Rental Debtors - Rent Receivables Kitega Uchumi	426,920,461.54	141,778,794.55
2	Provision for Trade Doubtful Debts	(263,084,964.91)	(263,084,964.91)
3	Dar es Salaam Trade Receivables	38,460,475.37	36,983,375.37
4	Staff Loan	792,707,060.48	547,557,142.48
5	Coolies Loan	90,046,496.30	90,046,496.3
6	General Receivable	339,092,443.72	339,590,443.72
7	Loan ZSTC DSM	347,593,866.68	347,593,866.68
8	Loan Clove for Famers	21,312,586.40	21,147,584.40
9	Vespa Loan	189,320,005.21	71,965,286.21
10	ZSTC Receivable Control	(320,452,696.92)	(320,452,696.92)
JUMLA		**1,661,915,698.87**	**750,040,332.97**

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati iligundua kwamba pamoja na Shirika kuchukua juhudi za kufuatilia madeni wanayodai lakini jitihada zaidi zinahitajika ili kuhakikisha madeni yaliyobakia yanalipwa ili kuliongezea mtaji Shirika. Hali hiyo imebainika baada ya kutathmini deni lililolipwa la shilingi 911,875,365.9 na kubakia shilingi 750,040,332.97.

Kamati ilishindwa kuthibitisha kupitia vielelezo deni la ununuzi wa vespa ambazo zilikopeshwa kwa ushirika wa Makuli pasi na kuwa na Mkataba ulio wazi kama taratibu za kukopeshana bidhaa au fedha inavyotaka. Kufanya hivyo kunapelekea Shirika kushindwa kuwa na mashiko ya kisheria kuwadai madeni hayo hasa ukizingatia muda wa Mkataba wao ulikuwa mwaka mmoja na tayari umeshamaliza.

(b) Wadai, shilingi 25,671,454,180

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika linadaiwa shilingi 25,671,454,180 na Taasisi na watoa huduma mbali mbali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, wakati hakujaonekana jitihada zinazochukuliwa na Shirika kuhakikisha deni hilo linalipwa na kupelekea taswira nzuri ya kujiendesha kibiashara. Kuendelea kuwepo kwa madeni hayo, kunaweza kusababisha hasara kubwa kwa Shirika kwa kupata tozo ya adhabu na riba ya ucheleweshwaji ulipaji deni hilo kwa wakati.

Miongoni mwa Wadai hao ni pamoja na shilingi 5,000,000,000 (ZSSF), shilingi 10,550,155,699.42 (Wanunuzi wa Karafuu), shilingi 377,000,000 (Wizara ya Vijana) na shilingi 8,067,331,747.83 (Benki ya Watu wa Zanzibar.

Majibu ya Shirika

Shirika limejitahidi kuchukuwa jitihada mbalimbali kuweza kulipa madeni hayo licha ya kutokuwa na fedha. Hadi sasa Shirika limeweza kulipa madeni ya kiinua mgongo na linatarajia kulipa madeni mengine yaliyobaki katika mwaka huu wa fedha.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati imegundua kwamba kuna utekelezaji mbaya wa matumizi ya fedha za Serikali kwani matumizi hufanywa bila ya kuzingatia mpango halisi wa fedha hizo. Hili limebainika kwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya mradi vijana wa Pilipili kupitia Wizara ya Vijana na kutumika kwa shughuli za ununuzi wa Karafuu. Hatimae, mradi wa pilipili ulishidwa kutoa tija iliyokusudiwa na vijana wengi kushindwa kunufaika na mradi huo. Aidha, Kamati haikuridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na Shirika la ZSTC kwa mwaka 2019/2020 kwani wameweza kufanikiwa kulipa deni la kiinua mgongo tu la shilingi 225,000,000 kati ya jumla ya deni lote la shilingi bilioni 25,671,454,180 sawa na shilingi

….. ambazo bado hazijalipwa.

Kutokana na ukaguzi huo, Kamati inalishauri yafuatayo kwa Shirika na Serikali kwa jumla:

1. Fedha za Serikali zitumike kwa mujibu wa Mpango kazi na malengo yakiyokusudiwa na vyombo vinavyopitisha bajeti husika.
2. Shirika lihakikishe linachukua juhudi stahiki ili kuhakikisha madeni yake yanalipwa kwa wakati.

3.6.2 Ucheleweshwaji wa fedha za mapato kupelekwa benki shilingi 140,565,900 na dola 20,783

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi milioni 140,565,900 na dola 20,783 zilikusanywa na Shirika kutoka vyanzo vyake vya uuzaji wa bidhaa mbali mbali katika maduka yake. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa fedha hizo kwa muda mrefu baina ya siku tatu hadi mwezi mmoja bila ya kupelekwa benki kwa wakati. Vielelezo vinaonesha kwamba fedha zilizocheleweshwa kwa duka la Maisara ni jumla ya shilingi 59,350,100, duka la Uwanja wa Ndege ni U$D 20,783 na duka la Malindi shilingi 79,141,800.

Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa

Shirika limekiri kwamba kumekuwepo uchelewaji wa fedha za mauzo kupelekwa benki kwa wakati na Kamati kuelezwa kwamba ucheweshwaji huo umetokana na maduka ambayo yanauza bidhaa ambazo kikawaida huhitaji kubakisha fedha kwa ajili ya kuwarejeshea wateja wanaokuja na pesa nyingi (chenji) hasa mauzo yanayofanyika kwa Dola katika Duka la Airport. Kwasasa hatua zimechukuliwa za kupunguza ucheleweshaji huo na kwa muda huu, fedha hizo zinapelekwa Benki kwa wakati.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati baada ya kujiridhisha na hoja hiyo na kwa vile Shirika limekubali na kuchukua hatua za kurekebisha kasoro hiyo, Kamati haikuwa na hoja za ziada kwa Shirika na kuwataka wawe makini na mauzo ya fedha za maduka yao na waendelee kuwa na utaratibu huo wa kuziwasilisha benki kwa wakati kwani ucheleweshwaji unaweza kutoa mwanya kwa watendaji wasio na maadili mazuri kuzitumia vibaya fedha hizo kwa maslahi binafsi.

3.6.3 Fedha zilizokopwa na Shirika kutoka kwa watu binafsi shilingi 6,771,848,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi bilioni 6,771,848,000 zimepokelewa (mkopo) kutoka kwa wafanyabiashara wa nchi tofauti kwa lengo la kununua karafuu ambazo hazikutumiwa kama ilivyokusudiwa wala wafanyabiashara hao hawajapatiwa bidhaa inayolingana na uhalisia wa kima cha fedha kilichozuiliwa na Shirika. Jumla ya tani 607

kutoka katika Kampuni la Unique Traders kutoka India tani 5,200 (1,592,448,000), Rashwel ya Dubai tani 75 (shilingi 817,800,000), Afcom la Dubai tani 200 (shilingi 2,180,000,000) na Atban la Tanzania tani 200 (shilingi 2,180,000,000).

Ukaguzi haukuweza kuthibitisha uhalali wa deni hilo kutokana na kukosekana vielelezo na nyaraka zinazothibitisha makabidhiano ya fedha hizo kwa ajili ya ununui wa karafuu kwa wafanyabiashara hao.

Majibu ya Shirika

Kamati imeelewa kwamba Shirika lilipokea fedha za utangulizi kutoka kwa Wateja wa Karafuu kwa lengo la kununua Karafuu na sio kuwakopa na fedha hizo zilitumika kama zilivyokusudiwa ingawa bei ya kununulia ilikuwa kubwa ukilinganisha na bei ya kuuzia. Sababu hiyo ilipelekea Shirika kushindwa kuwapatia karafuu zao. Aidha, Shirika limekanusha kwamba fedha hizo zimetolewa kwao kama unavyokuwa mkopo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ilipofuatilia hoja hiyo iligundua kwamba utaratibu wa utangulizaji fedha kwa lengo la kupatiwa karafuu unalingana na kusema kwamba Shirika limekopeshwa na wanatakiwa kulipa deni la karafuu zinazohijika. Aidha, Kamati pia imegundua kwamba ni kweli Shirika halikuwa na mikataba na Makampuni ya ununuzi wa karafuu ila lilikuwa na 'invoices' ambazo Shirika walizitumia kama kielelezo cha makubaliano yao.

Kwa vile 'invoice' haitoi taswira kamili ya makubaliano, Kamati imelitaka Shirika kuanzisha utaratibu wa kuingia nao mikataba (forward contract) ili liweze kuondoa utata au kutofahamiana juu ya biashara wanayoifanya ambapo mtu wa tatu (third party) ataweza kupata majibu ya lini mkataba unaanza na kumalizika, majukumu ya kila upande pamoja na uwajibikaji wao.

3.6.4 Ulipaji wa Mishahara kwa wafanyakazi wa muda bila kupewa Mikataba

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika linao wafanya kazi wengi ambao wanafanya kazi kwa mikataba ya muda mrefu kinyume na taratibu za utumishi Serikalini (idhini ya katibu Mkuu Kiongozi). Jumla ya wafanyakazi 33 kwa upande wa Unguja na 43 Pemba wanafanya kazi wamegundulika kufanya kazi na Shirika kwa muda mrefu.

Majibu ya Shirika

Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) lina jumla ya wafanyakazi 76 wa Mkataba kwa Unguja na Pemba. Wafanyakazi hao waliajiriwa kwa ajili ya kufanya kazi mbali mbali ikiwemo uzalishaji wa bidhaa za kilimo hai, kusafisha Karafuu, uuzaji wa bidhaa katika maduka ya Shirika, kusarifu Karafuu na bidhaa nyengine za kilimo na kuzifungasha katika ujazo mdogo, pamoja na uzalishaji wa mafuta ya mimea.

Mikataba ya wafanyakazi hao ilimalizika muda wake tarehe 30/09/2018 na Shirika lilichukua hatua ya kuwaombea Kibali cha uajiri kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011, Kifungu Nam. 60 - (1) (b)kwa barua ya Shirika Nam. SBT/Z.20/1/105/VOL XV ya tarehe 24/08/2018.

Shirika liliendelea kuwatumia wafanyakazi hao huku likisubiri majibu ya Kibali cha Uajiri kutoka Serikalini. Hata hivyo, majibu ya barua hiyo yalikawia sana kupatikana, ndipo Shirika likachukua hatua mbali mbali za ufuatiliaji kwa kukumbushia barua yetu.

Kutokana na Shirika kuendelea kuwalipa mishahara wafanyakazi hao bila kuwa na Mikataba ambapo ni kinyume na taratibu za malipo, pamoja na agizo la Serikali kuhusu kuzuia ajira kwa muda kufuatia Toleo Nam. Nam. CAB.40/158/01/5 la tarehe 08/12/2020 kutoka (OR)-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora linalohusiana na kusitisha ajira kwa muda na kusimamisha nyongeza ya muda wa utumishi kwa watumishi wa Umma waliofikia umri wa kustaafu kwa lazima (miaka 60) Shirika limepanga kufanya zoezi la kuwapunguza kazini wafanyakazi hao. Aidha, Shirika liliomba na kupatiwa muongozo wa utekelezaji wa zoezi hilo Kamisheni ya Kazi,na kuanza utekelezaji wake kwa mujibu wa Sheria ya ajira Nam. 11 ya 2005. Kifungu Nam. 121 cha Sheria hiyo Kinahusika.

Hadi hivi sasa Shirika limefikia 95% ya utekelezaji wa zoezi hilo na inatarajiwa hadi kufikia tarehe 31/08/2021 itakuwa ni mwisho wa ajira za mikataba. Hivyo, wafanyakazi hao watalipwa stahiki zao zote kwa kipindi chote cha utumishi wao kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na kwa mujibu wa muongozo uliotolewa katika Kibali cha Kukamilisha zoezi hilo kilichotolewa na Kamisheni ya Kazi kwa barua Nam. KK/24/04/VOL II/41 ya tarehe 03/08/2021.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na majibu ya Shirika, Kamati ilitaka kujua kwamba Shirika limechukua juhudi za kukaa na kuwaeleza wafayakazi hao kuhusu kusimamishwa kazi na vipi Shirika limejipanga kutekeleza majukumu yake wakati wana wafanyakazi kidogo. Shirika limeeleza kwamba tayari wameshakaa nao vikao na kuwataka wajikusanye kivikundi ili msimu wa karafuu ukifika waweze kuwatumia.

Kamati imelishauri Shirika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria za nchi na kuwa na mahitaji ya wafanyakazi hakuhalalishi uvunjwaji wa Sheria za Utumishi na za Kazi. Hivyo, Shirika lifuate Sheria kikamilifu.

3.6.5 Tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo

Katika kufuatilia na ujiridhisha hatua iliyofikia miradi ya maendeleo ya Shirika, ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya miradi bado haijatekelezwa na mengine imesimama na

kuchelewa kutekelezwa kutokana ukosefu wa upatikanaji wa fedha. Miongoni mwa miradi hiyo ni:

a) Ujenzi wa Ofisi na Kitega Uchumi Malindi

Shirika limeingia Mkataba wa ukarabati wa jengo la zamani la Shirika pamoja na nyumba mbili zilizopo Malindi kupitia mkataba kumbukumbu nambari ZSTC/W/CRMH/01/2016/2017 wa tarehe 10/6/2016 na Kampuni ya ZECCOM kwa thamani ya shilingi bilioni 2,888,885,522.60 ambapo jumla ya shilingi 1,991,807,131.97. Kupitia mradi huo, ukaguzi umebaini dosari zifuatazo:

1. Ukaguzi umebaini Shirika limeshindwa kulipa jumla ya shilingi 897,078,390.63 sawa na asilimia 31.
2. Ukaguzi haukupatiwa makubaliano yaliyofikiwa baina ya Shirika na Mkandarasi huyo juu ya uwepo deni hilo na namna au njia litakavyolipwa.
3. Kukosekana kwa ripoti ya awali ya utanuzi wa jengo hilo na namna ambavyo litakavyokuwa baada ya kukamilika.
4. Kukosekana gharama halisi ya fedha kwa mujibu wa makisio ya Muhandisi katika ukarabati.
5. Kufunga mkataba mmoja wenye aina mbili ya kazi (ukarabati wa ujenzi na ujenzi mpya).

Majibu ya Shirika

Kutokana na maelezo hayo ya ripoti, Shirika lilieleza yafuatayo:

1. Shirika kushindwa kulipa deni linalotokana na mradi huu, ni kutokana na kukosa fedha za kujiendesha hali iliyosababishwa na kushuka kwa bei ya kuuzia karafuu katika soko la dunia, wakati ZSTC ikiendelea kununua karafuu kutoka kwa wakulima kwa bei kubwa. Deni halisi ambalo Shirika linadaiwa na Kampuni ya ZECCON ni TZS 708,750,005.5, Aidha, hadi sasa Jengo hilo tayari limeshakodishwa na Shirika linategemea kutumia fedha hizo za kodi kupunguza deni hilo.
2. Shirika limepokea hati ya madai iliyoidhinishwa na Mshauri Elekezi ambae ni msimamizi wa mradi huo wa Mjenzi wa Ofisi ya Kitega Uchumi Malindi yenye thamani ya TZS 708,750,005.5 deni hili liliwasilishwa kwa wakaguzi kipindi cha ukaguzi.

3. Shirika liliweza kuwasilisha michoro inayoonesha jengo kongwe pamoja na majengo yaliyopendekezwa kujengwa na kufanyiwa ukarabati. Aidha, Shirika liliahidi kuwasilisha Hadidu Rejea (TOR) iliyowasilishwa kwa Mshauri Elekezi aliesanifu majengo hayo. Hivyo, michoro hiyo ilikuwa na vipimo vinavyoonesha ukubwa wa jengo.

4. Gharama zote za ujenzi zimewasilishwa katika hati ya madai ya malipo na iliwasilishwa wakati wa ukaguzi.

5. Shirika lilifunga mkataba mmoja kutokana na kazi zenyewe kuwa na uhalisia mmoja na kazi zote zilitakiwa kufanyika kwa pamoja. Majengo hayo yalitakiwa kuwa na muonekano mmoja na yaweze kutumika kwa pamoja (jengo moja liweze kuwa na muingilano na jengine). Aidha, Sheria ya manunuzi inaelekeza kuchanganya kazi (aggregation) ya kazi zenye kuendana.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika ukaguzi wake, Kamati ilipitia mkataba wa ujenzi ili kujiridhisha nao na ilitaka kujua ujenzi ulikamilika lini, mwezi gani jengo lilikodishwa pamoja na kwanini kumekuwa na tofauti ya deni linalodaiwa na Shirika baina ya Ripoti ya Mkaguzi (CAG) (shilingi 897,078,390.63) na majibu ya Shirika (shilingi 708,750,005.5) inayotokana na Mkaguzi kuingiza fedha za kodi wakati majibu yalitenganisha. Kwa upande wa jengo, lilianza mwaka 2020 na kumaliza Febuari, 2021 ambapo Shirika lilishindwa kumlipa Mkandarasi fedha zote bila ya kuwa na makubaliano hayo kwa vile walikuwa hawana chanzo chengine cha mapato zaidi ya uuzaji karafuu ambazo bei ya ununuzi kutoka kwa wakulima ilikuwa kubwa ukilinganisha na mauzo ila walikubaliana na Mkandarasi kwamba deni hilo litalipwa bila ya kuwepo ongezeko lolote.

Kuhusu kuchanganya ujeni na ukarabati, Kamati ilijirisha kwamba Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma chini ya kifungu cha…. kinaruhusu kitendo cha kuchanganya ujeni kama ilivyofanywa na Shirika isipokuwa gharama za kila ujenzi ziwe wazi ndani ya BOQ, hili lilifanyika ili kuepuka gharama mara mbii utangazaji zabuni na kumlipa Mkandarasi.

Kamati pia ilitaka kujua kwanini Shirika Baada ya kupitia mkataba, Kamati iliridhika na majibu ya shirika na moja.

Mbali na hayo, Kamati pia imegundua kutokuwepo mashirikiano mzuri kati ya watendaji wa Shirika na Mkaguzi aliyekagua katika kipindi hicho, Kamati imeligundua hili kutokana na kutofautiana majibu yao kwani CAG amesema hakupatiwa vielelezo alivyokuwa akivihitaji wakati Shirika lilieleza kwamba walimpatia vielelezo hivyo ila hakutaka kuvipokea kwasababu zake binafsi. Sambamba na hilo, Kamati imegundua barua

kutoka CAG ilichelewa kufika katika Shirika hasa ukizingatia Ofisi hizo zipo karibu.

Katika hoja hii, Kamati ulipendekeza mambo yafuatayo:

1. Kuwepo na madaftari maalum litakalotumiwa na watendaji wa CAG wanapohitaji kupatiwa vielelezo ili kuepusha lawama kutoka kila upande.
2. Ni vyema kwa makubaliano yoyote hususan yanayohusu ujenzi yakawekwa kwenye mikataba ya wazi ili kuhakikisha kila pande mamufaika nao.

b) Ujenzi wa Maghala ya Kununulia na Kuhifadhia Karafuu pamoja na Kitega Uchumi (Madungu) Pemba

Shirika limeingia mkataba wa ujenzi wa jengo la kitega uchumi (mkataba nambari SMZ/FO121/W/ICB/2018/2019/01 wa tarehe 12/12/2019) na Kampuni ya Selecom Construction Limited kwa thamani ya shilingi 6,923,355,649. Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 557,388,802.25 sawa na asilimia 8 zimeshalipwa kwa Mkandarasi kwa kazi ya ujenzi kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kusainiwa mkataba.

Ukaguzi umebaini ujenzi huo haujafikia katika hali ya kuridhisha na umekwama kuendelea kutokana na ukosefu wa jumla ya shilingi 6,365,966,846.75 sawa na asilimia 92 za kumalizia ujenzi huo. Kasoro zilizobainika ni:

- Shirika kushindwa kuendeleza ujenzi na kupelekea ujenzi kusimama.
- Shirika kushindwa kumlipa Mshauri Elekezi jumla ya shilingi 296,123,850.6 sawa na asilimia 92 ya malipo yote.

Majibu ya Shirika

1. Ujenzi wa maghala pamoja na Kitega Uchumi Madungu - Pemba umesimama kutokana na Shirika kukosa fedha za kujiendesha, hali iliyosababishwa na hasara iliyotokana na tofauti ya bei ya kuuzia karafuu na ile ya ununuzi kutoka kwa mkulima. Kwa kipindi chote hicho, Shirika lilikosa fedha kama ilivyojipangia. Shirika lipo katika jitihada za kutafuta vyanzo vya fedha ili liweze kuendeleza miradi yake, pamoja na jitihada za kupunguza gharama za miradi yake.
2. Shirika linatarajia kuendeleza miradi iliyoyaanzisha na kutaka ikamilike kwa wakati, kusimama kwa ujenzi kulitokana na ukosefu wa fedha uliyotokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wa Shirika. Hivyo, ni matarajio ya Shirika

kuendeleza miradi iliyoianzisha na kuikamilisha kwa wakati pamoja na kuzingatia gharama halisi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na Shirika kukiri kuhusu ucheleweshwaji na kusimama kwa ujenzi wa miradi yake ya maendeleo pamoja na fedha za malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi, Kamati imelishauri Shirika mambo yafuatayo:

1. Kuwa na mpango mzuri wa utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo ili iweze kuitekeleza kwa wakati.
2. Shirika liache desturi ya kuanzisha miradi mingi kwa wakati mmoja jambo ambalo linapelekea kushindwa kulipa madeni yake.

c) Upandaji wa mikaratusi katika maeneo ya Mamoja na Kashindeni kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi ya mafuta ya mimea.

Shirika limeshindwa kutekeleza baadhi ya miradi iliyotajwa hapo juu kutokana na ukosefu wa fedha unaolikabili Shirika, ukaguzi unashauri Shirika libuni miradi michache ambayo wataweza kuitekeleza kwa wakati na kuleta ufanisi na tija kwa jamii.

Majibu ya Shirika

Shirika limepokea ushauri ingawa hali iliyotokezea haikutarajiwa katika utekelezaji wa mipango ya miradi ya maendeleo iliyojipangia.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ililezwa na Shirika kwamba miradi wa Shamba la Mamoja umefikia katika hatua nzuri kwani miti imeshakuwa na ipo katika hatua ya kuvunwa lakini katika shamba la Kashindeni ndio wanaedelea na kuatika miche. Kamati ilitaka kujua kwanini Shirika halikufika lengo lake na kuelezwa sababu kuu ni kushuka kwa bei ya uuzaji karafuu jambo ambalo hawakutarajia kutokezea. Kama inaungana na ushauri wa CAG kwamba Shirika liwe linabuni miradi kidogo ili liwe na uwezo wa kuitekeleza ipasavyo.

3.6.6 Kutokuingizwa kwa taarifa za madeni katika hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 7,794,086,747.56

Ukaguzi umebaini uwepo wa madeni yenye jumla ya shilingi 7,794,086,747.56 ambayo hayajaripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka na kupelekea hesabu hiyo kutoonesha uhalisia na usahihi wake. Hali hiyo imepelekea dosari zifuatazo:

- Uwepo wa deni la shilingi 43,802,000 ambazo zimetumika kuwakopesha wanafunzi saba ambapo wengine walikuwa wakipatiwa mikopo mipya kabla ya kumaliza mkopo wa awali (kupandishia mikopo).
- Uwepo wa deni la Wakandarasi, Washauri Elekezi pamoja na tozo a kodi zenye jumla ya shilingi 7,750,284,747.56 ambazo hazikuripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

Majibu ya Shirika
Shirika tayari limesharipoti madeni hayo katika hesabu za mwaka.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati iltaka kujua kwanini wafanyakazi wanapandishiwa mikopo pasi na kumaliza mkopo wa awali na kuelezwa hilo lilikuwa likifanyika kutokana na huruma a kibinadamu ili kuwasaidia waweze kutatua changamoto zinazowakabili. Pamoja na Shirika kukiri na kurekebisha kasoro zilizzojitokeza, Kamati ililishauri Shirika liwe na mpango maalum wa mikopo kwa wafanyakazi wake na sio wafanyakazi kupandishiwa mikopo.

3.6.7 Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya shilingi 246,631,737

Ukaguzi umebaini Shirika limefanya uhaulishaji wa fedha kutoka katika hesabu 0404078000 yenye jumla ya shilingi 246,631,737 kwa ajili ya kumlipa mtoa huduma na msimamizi wa jengo la kitega uchumi - Kinazini (Knight Frank). Aidha, ukagui haukuweza kuthibitisha huduma inayotolewa na kampuni hiyo kutokana na kutokuwepo matumizi na vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa matumizi hayo.

Majibu ya Shirika
Shirika lilieleza kuwa vielelezo vya matumizi hayo vitaonekana katika Ofisi za Knight Frank ambapo Wakaguzi walitakiwa wakajiridhishe huko.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Kamati ilihoji kwamba ni sababu gani zilizosababisha vielelezo vya matumizi ya fedha za huduma katika jengo linalomilikiwa na ZSTC kushindwa kupatikana katika eneo la mmiliki wa jengo na kuelekeza ukaguzi ukaonane na mtoa huduma. Shirika lilieleza huo ndio utaratibu waliokuwa wakitumia awali ambapo hata mkaguzi wa ndani na nje hawajenda kukagua vielelezo vya huduma ailivyokuwepo kwa Knight Frank. Aidha, Kamati katika uchunguzi wake pia iligundua Shirika halina hata nakala za vielelezo halisi (origin) alivyonavyo mtoa huduma. Kamati ilishitushwa na majibu hayo na kutoa agizo kwamba Kamati kwa wakati wake itafuatilia na kuvikagua vielelezo hivyo ili iwe katika nafasi ya kuweza kushauri kitu halisi alichokikagua. Kupitia kadhia hiyo, Kamati ilishauri

mambo yafuatayo:

1. Shirika limruhusu mkaguzi wa ndani kukagua vielelezo vya huduma zinazotolewa na kampuni ya Knight Frank.

2. Kampuni ya Knight Frank iwasilishe nakala ya vielelezo vyote vinavyohusiana na matumizi ya utoaji wa huduma katika jengo alilokodi la ZSTC.

3.6.8 Madeni ya muda mrefu shilingi 543,605,532.33

Ukaguzi umebaini uwepo wa madeni ya muda mrefu ambapo Shirika limeonesha jitihada za kulipunguza ingawa bado Shirika linasumbuliwa na deni hilo linalotokana na ukodishwaji wa jengo la kitega uchumi liliopo Gulioni. Aidha, uwepo wa ulipaji usioridhisha kwa wadaiwa kunapelekea kujitokeza kwa madeni sugu ambayo hayataweza kulipwa na kusababisha hasara kubwa kwa Shirika utakaoibebesha mzigi mkubwa Serikali.

Kuongezeka kwa wadaiwa knachangiwa na kutokuwepo kwa umakini wa ukusanyaji wa madeni pamoja kukosekana na sera nzuri ya ukusanyaji wa madeni hayo ambapo katika kipindi cha ukaguzi wa Kamati deni hilo limefikia shilingi 543,605,532.33.

Majibu ya Shirika

Shirika lilieleza kwamba limeshirikiana na kampuni ya Knight Frank na linaendelea kufatilia na kuhakiki madeni ya wapangaji katika jengo la ZSTC Investment building na baadhi ya wapangaji wameshalipa madeni yao.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati haikufurahishwa na majibu hayo kwani Kaati ilitaraji kute tayari kasoro alizozieleza Mdhibiti ziwe zimeshafanyiwa kazi. Kushindwa kuzifanyia kazi kasoro hizo kunapelekea kukosa ufanisi wa Shirika.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA - PEMBA

KIWANDA CHA MAFUTA YA MAKONYO NA ARKI ZA MIMEA-PEMBA

3.6.9 Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda wasiokuwa na mikataba ya kazi shilingi 83,446,225.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 83,446,725 zimetumika kwa ajili ya kuwalipa mishahara wafanyakazi wa muda mfupi (daily pay) wanaofanya kazi mbali mbali katika kiwanda cha Makonyo lakini mikataba yao ya kazi ilikosekana kwa ukaguzi.

Majibu ya Shirika

Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) liliwasilisha majibu yanayolingana na majibu yaliyomo katika bullet namba 3.6.4 (rejea majibu hayo).

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Kwa vile Kamati imeshaitolea ushauri hoja kama hiyo isipokuwa imesisitiza yafuatayo:

1. Shirika litakapokuwa linaendesha zoezi la kuwasimamisha kazi watendaji hao, ni lazima lihakikishe linawapatia stahiki zao zote wanazolidai Shirika ikiwemo kiinua mgongo na mafao mwngine.

2. Kwa vile wafanyakazi hao wana uzoefu na ujuzi wa kutosha wa kutekeleza kazi za kiwandani, Shirika litakapopata nafasi za kuajiri, wawapatie nafasi ya upendeleo za kuwaajiri wale wote wenye sifa.

3. Shirika lichukue juhudi za kutosha kuwahamasisha wafanya kazi hao ili waweze kuanzisha au kujiunga katika vikundi ambavyo watakuwa na fursa ya kuwaajiri kwa muda.

3.6.10 Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda na vibarua kinyume na utaratibu shilingi 4,632,500

Kiwanda cha Makonyo – Pemba inao wafanyakazi wa muda (daily pay) kwa ajili ya kufanya kazi tofauti za kiwandani na kuwalipa shilingi 8,500 kwa mfanyakazi kwa siku aliyohudhuria kazini. Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 4,632,500 zililipwa kwa wafanyakazi wa muda na vibarua kwa siku ambazo hawakuhudhuria kazini. kufanya hivyo ni kinyume na sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011 pamoja na miongozo tofatuti iliyotolewa.

Majibu ya Shirika
Shirika lilieleza wafanyakazi hawakulipwa kinyume na sheria, ni kweli hawakuwemo kwenye daftari la mahudhurio ila walifanya kazi za nje ya kiwanda kama kwenye vyungu, shamba la mamoja na mtakata na waliweka mahudhurio kwenye sehemu zao kazi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Kamati katika uchunguzi wake ilielezwa na Shirika kwamba katika kiwanda kulikuwa na madaftari mawili ambapo moja lilikuwa Ofisini (ndio alilokagua CAG) na jengine lilikuwa shambani sehemu wanazozifanya. Kuna wafanyakazi hawakusaini daftari la Ofisini ila walisaini lile la shambani.
Kamati ilipopitia daftari la Ofisini iligundua kwamba halikuwa na saini za wafanyakazi hao lakini lakushangaza hati za majina husika katika daftari hilo zimeandikwa na hati zenye kufanana na kutambua kuwa zimeandika na mtu mmoja na kuleta wasiwasi mkubwa kwamba inawezekana limetengenezwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati ilishauri haya:

1. Shirika liwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbuumbu za Ofisi.

2. Shirika liache utaratibu unaotumika wa majina ya daftari la wafanyakazi kuandikwa na mtu mmoja na baadhi yao walishindwa hata kusaini katika eneo lao.

3.6.11 Deni la kiwanda kwa watoa huduma shilingi 8,114,990

Ukaguzi umebaini kuwa Kiwanda cha Makonyo kinadaiwa jumla ya shilingi 8,114,990 na watoa huduma wanne katika mwaka wa fedha 2019/2020. Deni hilo lilionekana kwa mtoa huduma Nassor Said Nassor (1,295,930), Tahfif Auto Works (1,399,480), Mbarouk Salim Ali (1,104,320) na Shirika la Bandari la Zanzibar (4,315,260).

Majibu ya Shirika la Biashara

Shirika halikuweza kulipa madeni hayo kutokana na ukosefu wa fedha katika kipindi cha mwaka 2019/2020, ila kwa sasa deni hilo limeshalipwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati imegundua kwamba kwa vile mwaka wa fedha 2019/2020 Shirika lilikuwa na mvuno mdogo wa Karafuu ambapo Shirika halikuweza kupata faida kubwa kukidhi mahitaji yake yote, hivyo lilishindwa kulipa madeni hayo lakini kwasasa tayari yameshalipwa. Kamati imeshauri ni vyema kwa Shirika kujipanga vizuri na kuhakikisha madeni yanalipwa kwa wakati ili kutoa sura nzuri kiutendaji kwa Shirika.

3.6.12 Hasara iliyosababishwa na uvujaji wa mafuta wakati wa uzalishaji shilingi 101,144,000

Kwa mujibu wa viwango vya uzalishaji kiufanisi, kilogramu 700 za makonyo zinatakiwa kuzalisha kilogramu 33 za mafuta ambapo kwasasa kiwanda kinazalisha chini ya kiwango. Ukaguzi umebaini hasara ya jumla ya shilingi 101,144,000 imepatikana kutokana na uzalishaji wa mafuta kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ikiwa bei ya kilogramu 1 ya mafuta ya makonyo ni shilingi 8,000.

Majibu ya Shirika

Kamati ilielezwa na Shirika kwamba kiwanda cha makonyo ni cha muda mrefu na chakavu kunakosababisha tatizo hilo la uvujaji wa mafuta, shirika linachukua jitihada mbali mbali kurekebisha ili kupunguza hasara hiyo. Aidha, hesabu za wakaguzi zimeangalia zaidi kwenye makisio ya kiwango cha Makonyo kinachotumika katika kuzalisha kilogramu moja ya mafuta wakati kiwanda kinapokua kipya. Uhalisia wa uzalishaji hauko hivyo ukizingatia kwamba hakuna mashine inayofanya kazi kwa asilimia 100.

Watendaji wa Shirika walikiri kuwa kweli kuna uvujaji wa mafuta kwa kueleza kitaalamu kwamba kiwanda kipya kinatakiwa kizalishe kwa 5% wakati uhalisia wa kiwanda hicho kwa sasa kinazalisha 4% hadi 4.7% (sawa na kilo 21 za makonyo zizalishe kilo 1 ya

mafuta).

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati katika uchunguzi wake imegundua kuwa kiwanda cha uzalishaji wa mafuta ya makonyo ni cha muda mrefu kwa zaidi ya miaka 40 kwasasa, hivyo uzalishaji wake utakuwa na mapungufu ukilinganisha na kiwanda kipya. Aidha, Kamati imebaini kwamba katika mwezi wa Aprili, kulikuwa na makosa katika kumbukumbu zilizochukuliwa na Mkaguzi za kilogramu 21,725 ambazo zilipelekwa kiwandani kutoka ghalani kwa ajili ya kuchakatwa kuwa mafuta lakini kiwanda kiliharibika na kiuhalisia kiwanda kilichakata kilogramu 3,687 na kuzalishwa kilogramu 177 za mafuta.

Kamati imelishauri Shirika kuweka vizuri kumbukumbu zake pamoja na kuwa na desturi ya kukaa pamoja kushughulikia hoja za awali anazowasilisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwao ili Wakaguzi wanapopita waweze kupata vielelezo na maelezo kamili yatakayoonesha ufanisi wa shughuli walizozitekeleza.

3.6.13 Mafuta ambayo hayakuingizwa katika daftari la ghalani shilingi 2,674,800

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 2,674,800 zimelipwa kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petroli na dizeli lakini hayakuingizwa katika daftari la ghalani ili kuweza kudhibitisha uhalali wa mapokezi na matumizi yake. Shirika lilinunua lita 400 kwa shilingi 1,770,800 za petroli na lita 400 kwa shilingi 904,000 za dezeli yote kutoka katika Kampuni ya Zanzibar Petroleum Limited.

Majibu ya Shirika

Shirika limekiri kuhusu ununuzi wa mafuta hayo na kueleza kwamba kulikuwa na makosa katika uingizwaji wake kwani mafuta hayo yalinunuliwa kwa ajili ya utengezaji wa kiwanda ila yaliweza kugundulika na kurikodiwa mwisho wa mwaka baada ya kufanyika 'reconciliation'.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Baada ya kufuatilia kwa undani hoja hiyo kwa kuchunguza daftari la ghalani la mafuta ya makonyo na mafuta ya vyombo vya moto, Kamati imengudua kulitokea makosa wakati wa uandishi kwani Mtunza ghala aliyaingiza mafuta hayo katika daftari la mafuta ya makonyo badala daftari la mafuta ya vyombo vya moto.

Kamati pia imebaini kuwa hakukuwa na mashirikiano mazuri kali ya Mkaguzi (CAG) na watendaji wa shirika hususan katika uwasilishaji majibu na vielelezo viliopo kwani imeonekana taarifa za kiukaguzi hazimfikii Afisa Masuul aliyopo Unguja. Kutokana na kuwepo changamoto hizo, kamati imeshauri yafuatayo:

1. Kutokana na utata unaojitokeza mara nyingi katika kikao cha Kamati, kuwepo na daftari maalum litakaloonesha vitu au mambo ambayo Mkaguzi amehitaji na kupatiwa na Shirika au Taasisi (yawe mawili la Taasisi na la Mkaguzi)

2. Watendaji wa Shirika Pemba wawe wanampatie Afisa Masuul taarifa zinazohitajika katika Shirika lake.

3. Kuwepo a mashirikiano ya kutosha kati ya watendaji wa Shirika na Mkaguzi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Kamati.

4. Mkaguzi anapokwenda kukagua katika maeneo yanayohitaj utaalamu maalum kwa mfano viwandani awe na taaluma husika ili kuepusha kutoa maelezo yanayoleta utata wakati Kamati inapitia hoja hiyo.

UKAGUZI MAALUM WA KAMATI KATIKA TAWI LA SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) DAR - ES - SALAAM

Katika ufuatiliaji wa hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na majibu ya Shirika la Biashara la Taifa kwa kufanya ziara ya kikazi ya siku moja katika Tawi la ZSTC Dar - es - Salaam. Kamati iligundua kuna umuhimu wa kuzikagua mali zinazomilikiwa na Shirika hilo ili kutambua kama zinatija na Serikali ama laa ili iweze kuishauri ipasavyo Serikali kabla ya kutokezea changamoto.

Lengo la Ukaguzi wa Kamati

kufanya ukaguzi katika Tawi la ZSTC ambalo linajumuisha duka liliopo Manzese, duka liliopo Lumumba, nyumba mbili za Shirika ziliopo Sinza pamoja na kufanya kikao na Watendaji wa Tawi la Shirika Dar - es - Salaam ili kuchunguza na kutathmini majibu yaliyowasilishwa na watendaji wa Shirika Zanzibar.

Ukaguzi katika ghala na Duka la Dar - es - Salaam

Duka la Dar - es - Salaam limeanzishwa mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 kwa lengo la kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar zinapatikana Tanzania Bara bila ya wafanyabiashara kuzifuata zinapozalishwa, wakati duka la Manzese limeanzishwa mwaka 2019 kuendeleza au kutanua wigo wa biashara.

Kwa upande wa mapato, kwa mwaka 2019/2020, Shirika lilikusanya jumla ya shilingi milioni 1,452.3 kutoka vyanzo vya mauzo ya bidhaa tofauti. na kutumia jumla ya shilingi milioni 1,514.7 kufanyia shughuli za kuuza bidhaa mbali mbali zikiwemo za vyakula na vifaa vya majumbani. Aidha, Tawi limetumia shilingi milioni 5.2 zilitumika katika matengenezo ya vifaa vya Ofisi zikiwemo ‘compyuter’. Tawi hilo limemaliza mwaka likiwa na hasara ya shilingi milioni 62.4 na bakaa ya bidhaa za mkopo zenye thamani ya shilingi 136,359,963.20 ambapo kati ya hizo shilingi milioni 11,260,000 ni thamani ya bidhaa na shilingi 84,067,067.01 ni fedha ziliopo benki.

Kwa upande wa nyumba za ZSTC Sinza imejengwa na Shirika miaka ya 1980's kwa lengo la kuwapatia makaazi wafanyakazi wa Shirika, lakini baadae walikodishwa watu tofauti na hatimae (mwaka 2019) nyumba ilikuwa haitumiki na kufanywa jaa la kutupia taka.

Hivi sasa nyumba kubwa yenye vyumba vitatu na maduka madogo matatu (ya ushoni, nguo na vitavunwa) imekodishwa na kodi inaingia katika Shirika wakati nyumba nyengine yenye vyumba vitano anakaa mfanyakazi wa ZSTC na familia yake.

Kikao na Wafanyakazi wa ZSTC

Meneja Tawi la Dar - es - Salaam aliieleza Kamati kwamba Tawi la hilo lina wafanyakazi saba wa kudumu na sita wa muda kwa maduka yote mawili ya Lumumba na Manzese. Duka la Dar - es - Salaam linamilikiwa na Shirika la Nyumba la Tanzania Bara (NHC) na kulipa kodi ya shilingi 2,6000,000 kwa mwezi. Kutokana na mapendekezo ya Kamati Maalum iliyoundwa na Shirika, ilipendekeza kwa vile duka lipo katikati ya mji imekuwa biashara imekuwa nzito, wafungue duka jengine nje ya mji na kuingiza mtaji ili kuendeleza biashara, ndio likatafutwa Duka la Manzese.

Duka la Manzese limetokana na kukodi jengo la mtu binafsi (shilingi 2,800,000 kwa mwezi) kwa ajili ya kuendeleza uuzaji wa bidhaa za Zanzibar nje ya mji. Kwa bahati mbaya Shirika halijaweza kuingiza mtaji wa biashara matokeo yake wanauza zaidi bidhaa wanazochukua kwa wafanyabiashara kwa njia ya mkopo na kuwauzia kwa faida ndogo.

Kutokana na hasara inayopatikana katika Tawi hilo, tayari uonogzi wa Shirika limeshaamua kodi yake ikimaliza mwezi wa Oktoba, duka hilo watalifunga ili waweze kubakia na duka moja tu la Dar es Salaam.

Mikakati ya Shirika kuhusu biashara Tanzania Bara

kuendelea kuliomba kwa Shirika la Nyumba la Taifa jengo la ZSTC ghala na duka la Dar - es - Salaam ili wapatiwe umiliki halisi kama walivyowahi kufanya awali wakati Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa Waziri wa Wizara ya Biashara Zanzibar.

Kulifunga duka la Manzese kwani limeonekana kutokuwa na tija kwasasa.

Kutafuta Taasisi au Mjenzi wa nyumba ya Shirika Sinza ili wakubaliane kuijenga ghorofa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Baada ya kupitia taarifa ya Meneja wa Shirika Tawi la Dar es Salaam na kufanya ziara katika Duka la Dar es Salaam, Manzese na nyumba ya Shirika - Sinza, Kamati iligundua

mambo yafuatayo:

Duka la Manzese

1. Duka linafanyabiashara kinyume na lengo la kufunguliwa kwake. Kamati imekuta ndani ya duka bidhaa za unga na juice za Bakhresa pamoja na bidhaa za karafuu kidogo.

2. Duka linaendeshwa kihasara na kunufaisha makampuni binafsi kwani duka limekuwa kama wakala wa kuuza bidhaa zao (mkopo wa mali kauli) badala ya zile za Serikali na kupata faida ndogo ambayo inagharamia usafiri na wachukuzi. Mfano Kamati ilielezwa kuwa duka liliuza zaidi ya shilingi milioni 110 au 111 kwa mwezi lakini fedha zote zinarudishwa kwa Makampuni.

3. Duka linafanya biashara kwa mauzo ya 'cash' bila ya kuwa na ulinzi wa aina yoyote na kuhatarisha usalama wa fedha hizo, mali zilizopo na wafanyakazi.

4. Duka halijawahi kuingiziwa Mtaji tokea lianze kazi kama malengo ya uongozi wa Shirika ulivyoelekeza.

5. Duka bado lina fursa nzuri ya kufanyabiashara iwapo litakuwa na mikakakati inayotekelezeka.

6. Meneja wa Tawi aliwhi kuandika barua ya tarehe … yenye kumbu …. kuuomba uongozi wa Shirika kuchukua maamuzi mazito ya kulifunga duka moja ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Duka la Dar - es - Salaam

1. Duka linafanyakazi katika nyumba ya Shirika la Nyumba la Taifa ambapo hulipa kodi kubwa waliyopangiwa kuliko nyumba zote ziliopo katika eneo hilo.

2. Shirika limeazimia kuandika barua ili kuomba wamilikishwe jengo hilo.

3. Duka halifanyi biashara kwa kusuasua kwa vile wateja wengi huja Zanzibar kununua bidhaa wanazouza wao kwa bei nafuu kuliko bei inayouzwa dukani hapo. Mfano kichupa cha 20 mililita za karafuu, Unguja inauzwa kwa shilingi 2,500 wakati dukani hapo 6,000.

4. Iwapo umiliki wa duka hilo utapatikana, duka litaweza kumudu na kujiendesha vizuri kibiashara

Nyumba ya Maakazi - Sinza

1. Nyumba ni ya zamani na kunajaa maji ya mvua. Meneja kachukua juhudi ya kuyatoa maji hayo kwa pampu maalum.

2. Nyumba haziwezi kujiendesha kujifidia gharama za kawaida na za matengenezo.

3. Kuna eneo la kutosha la kuweza kujenga ghorofa itakayotimiza lengo lililokusudiwa na kufanya biashara.

Kufuatia uendeshaji huo wa Tawi, Kamati inashauri yafuatayo:

1. Kuhusu kubakia au kuondolewa kwa Tawi, Kamati iliona bado haja ya kuliacha Tawi hilo liendelee kufanyakazi ipo. Hata hivyo, kunahitajika mpango mpya wa biashara na mabadiliko ya hali ya juu katika uendeshaji wake ili lengo la kuanzishwa kwake kuweze kufikiwa.

2. Kwa vile uendeshaji wa biashara hufanyika kwa hasara, ni vyema duka la Manzese likafungwa mara tu litakapomaliza Mkataba wake ili kutoa fursa kwa Shirika kushughulikia duka moja la Dar es Salaam hadi hapo hali itakapotengemaa na kuamua kutanua wigo wa biashara kwa mara nyengine.

3. Kamati pia inalitaka Shirika kufanya haraka ya kukumbushia barua yao maombi waliyofanya awali ili waweze kupatiwa na kumilikishwa jengo la Dar es Salaam. Kufanya hivyo kutalipunguzia kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji Shirika.

4. Kwa upande wa nyumba ya wafanyakazi iliopo Sinza, ni busara Shirika likatafuta Muwekezaji ili aweze kulijenga jengo hilo (ghorofa) kwa njia ya ubia ambapo watakubaliana kwa muda fulani mjenzi ajirudishie gharama zake.

Kiujumla, Kamati imegundua kwamba Tawi la ZSTC Dar - es - Salaam Mapato yake yameonekana kupungua kwa miaka mitatu mfululizo wakati gharama za matumizi zimeongezeka. Hivyo Kamati iliomba ipatiwe taarifa kamili ya vyanzo na mapato ya Tawi kwa muda wote wa miaka mitatu lakini hadi kamati inawasilisha ripoti hii leo hakuna taarifa yoyote iliyowasilishwa. Aidha, Kamati imebaini kuwa gharama ya uchakavu wa jengo haijaingizwa katika hesabu za mwisho wa mwaka na ripoti kushinwa kutoa picha halisi ya gharama za mali za Shirika Dar - es - Salaam.

3.7: SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA (ZMA)

Taarifa ya Mapato

Mapato ya Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka TZS 14,880,312,387.70 kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi kufikia TZS16,210,994,551.70 kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la TZS 1,330,682,164 sawa na asilimia 8.90.

Majibu ya Shirika

Mapato ya Shirika la Meli Zanzibar yanatokana na vyanzo vikuu vinne vya mapato yanayotokana na usafirishaji wa Abiria na mizigo, ukodishaji wa meli za mafuta, mapato ya uwakala wa meli za kigeni na mapato ya utoaji mizigo (Release). Aidha, katika hesabu za Shirika kuna mapato mengineyo ambayo yanatokana na mapato ya kodi ya vyumba katika jengo la Ofisi la Shirika la Meli liliopo Mkoani, mapato ya kodi ya sehemu ya ofisi katika jengo la Ofisi Kuu Unguja na mapato ya wanafunzi katika meli (sea time).

Tofauti ya mapato inayonekana hapo juu ya Shilingi 1,330,682,164 ni thamani ya ruzuku kwa kupewa Meli ya MT. Ukombozi II pamoja na mapato yake. Jadueli lifuatalo linaonesha mapato halisi kwa ulinganisho wa mwaka wa fedha 2019/20-2018/19.

CHANZO CHA MAPATO	2019/2020	2018/2019	TOFAUTI	%
M.V. Maendeleo	-	-	-	
M.V. Mapinduzi II	1,999,286,779	2,841,315,308	-842,028,528	-29.6
Charter Hire M.T.S.Ukombozi	2,654,315,194	1,873,754,520	780,560,674	41.6
Charter Hire M.T.S.Ukombozi II	287,495,145	-	287,495,145	-
Agency Revenue	5,761,344,323.29	6,142,016,171.04	1,160,077,381.09	-20
Release	667,523,700	721,338,773	-53,815,073	7.4
Other income	19,935,498	11,044,366	8,891,132	80.5
Amortization of government grant and provision	4,821,093,912.5	3,290,843,250.00	1,530,250,662.50	46.5
JUMLA	**16,210,994,551.79**	**14,880,312,388.04**	**1,330,682,163.75**	**8.9**

Uchunguzi wa Kamati

Katika kujadili hoja hii, Kamati ilitaka kujua sababu zilizopelekea mapato ya Shirika kuongezeka mwaka 2019/2020 ukilinganisha na mwaka 2018/2019 na kuelezwa kwamba hali hiyo ilitokana na ukodishwaji wa M.T.S.Ukombozi II pamoja na kuwepo kwa uchakavu wa meli za Serikali hasa ukizingatia Shirika linafunga hesabu zake za mwaka kwa mfumo wa ácrual basis'.

Aidha, kuhusu ufanisi wa meli za Serikali, Kamati ilielezwa kwamba M.V. Mapinduzi II

kwasasa ipo nangani inasubiri utaratibu wa kufuatwa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Lakushangaza, kuna wafanyabiashara tofauti wanaonekana nia ya kununua meli hiyo ambao wanakwenda katika Shirika lakini wanaelekezwa waende Wizara ya Fedha na Mipango suala ambalo inalifanya Shirika kubakia njia panda kuhusu hatma ya wateja hao.

Kwa upande wa M.V. Maendeleo, Shirikia ilitegemea itafanya kazi lakini kwasasa ipo katika chelezo cha Mombasa Kenya kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo. Lakusikitisha, pamoja na kuwa Serikali imeshaitolea maamuzi ya kuuzwa lakini kwa muda mrefu imekuwa ikiongeza gharama za kodi ya kuwepo katika chelezo ambapo inakadiriwa zaidi ya U$D 500,000 zipatikane ili kuigomboa meli hiyo na ndio maamuzi ya Serikali yaweze kufanyika wakati makisio ya gharama za mauzo yake yanakisiwa kufikia si zaidi ya U$D 500,000.

Katika kufuatilia sababu ya ubovu wa M.V. Maendeleo II, ilielezwa kwamba Shirika liliingiza mkataba wa uendeshaj wa meli hiyo na kuelezwa kwamba meli hiyo ilikodishwa kwa Kampuni ya Mkunazini kwa muda wa miaka mitatu (2016/2018) na kuirudisha katika ikiwa imechakaa hali ambayo ni kinyume na makubaliano nao. Hali hiyo iliisababisha Shirika kufungua kesi Mahakama Kuu ya Zanzibar mwaka 2018 na kuamuliwa kila upande wa kesi ibebe mzigo wake mwenyewe.

Hatimae, Shirika liliamua kupeleka maombi ya kukata rufaa lakini limeshindwa kwa vile Bodi ya Shirika kisheria ndio yenye uwezo wa kukata rufaa na wakati Kamati inafanya kazi zake za ukaguzi Mwenyekiti wa Bodi hiyo alikuwa bado hajateuliwa. Hivyo, Shirika iliiomba Mahkama waruhusiwe kuwasilisha rufaa yao nje ya wakati (Certificate of delay). Kwa bahati mbaya, hadi Kamati inawasilisha taarifa hii, Kamati ilishindwa kupatiwa hati hiyo kuthibitisha hatua zilizoanzwa kuchukuliwa na Shirika katika ukataji rufaa.

Kamati ya LAAC imegundua kwamba ukataji rufaa ulikwama kutokana na kukosekana kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika kwa ambapo uteuzi wa aluyekuwepo aliondolewa katika nafasi hiyo tangu mwezi tarehe 15 Desemba, 2020.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kamati imelitaka Shirika kuchukua hatua za haraka za kwenda Mombasa Kenya kufuatilia maendeleo ya meli ilivyo na mchakato mzima wa maandalizi ya uuzwaji wa meli hiyo.
2. Serikali kuchukua juhudi za makusudi za kutekeleza azma yake ya kufanya mauzo ya meli zake ili iliondolee Shirika mzigo wa gharama za uendeshaji.
3. Shirika lichukue hatua za haraka kukata rufaa ya kesi huko Mahakama ya Rufaa dhidi ya Kampuni ya Mkunazini ili iweze kupata haki yake.
4. Kamati ipatiwe nafasi ya kwenda Mombasa Kenya kuifanyia ukazi zaidi meli hiyo.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Shirika la Meli Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 15,602,644,040 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 16,759,823,599 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa ni ongezeko la shilingi 1,157,179,559 sawa na asilimia 7.4.

Majibu ya Shirika

Matumizi ya Shilingi 16,759,823,599 yanajumuisha matumizi mbali mbali ya Shirika la Meli pamoja na gharama za uchakavu (depreciations) ya meli. Sababu za kuongeza matumizi ni gharama za uendeshaji wa Meli ya MT. Ukombozi II ambayo takriban 2.4 bilioni zilitumika kulipa gharama za uendeshaji wake. Jadweli lifuatalo linaonesha matumizi halisi ya Shirika la Meli Zanzibar kwa ulinganisho wa makisio (budget) kwa Mwaka 2019/2020.

UTAWALA	BUDGET 2019/2020	ACTUAL 2019/2020	TOFAUTI	ASILIMIA
UTAWALA	4,210,506,657.03	2,874,088,709.66	1,366,417,947.37	68.26%
MT UKOMBOZI	2,111,333,402.95	1,283,922,768.34	827,410,634.61	60.81%
MV MAENDELEO	3,772,373,648.80	276,256,279.08	3,946,117,369.72	7.32%
MV MAPINDUZI II	6,777,945,188.80	3,972,511,917.8	2,805,433,271.00	58.61%
MT UKOMBOZI II	1,100,653,600.00	1,246,067,752.76	-145,414,152.46	113.21%
	17,972,812,497.58	**9,652,847,427.64**	**8,319,965,069.94**	**53.71%**

Matumizi Halisi ya Shirika la Meli Zanzibar kwa Ulinganisho wa Miaka 2020/2019 na 2019/2020

	2019/2020	2019/2018	TOFAUTI	%(ASILIMIA
UTAWALA	2,982,747,980,.08	2,607,642,134.45	375,105,845.63	14.38%
MT UKOMBOZI	1,474,736,184.34	1,295,255,291.57	179,480,892.77	13.86%
MV MAENDELEO	276,256,279.08	456,179,122.00	-179,922,842.92	-39.94%
MV MAPINDUZI	7,335,503,451.88	9,803,823,446.80	-2,468,319,994.92	-25.17%

II				
MT UKOMBOZI II	2,471,430,196.76	-	2,471,430,196.76	100%
Agency Expenses	2,219149,579.30	1,439,744,045.96	779,405,533.34	54.13
JUMLA	**16,759,823,671.00**	**15,602,644,040.78**	**1,157,179,630.66**	**7.42%**

Uchunguzi wa Kamati

Ukiacha majibu ya Shirika, kutokana na takwimu zilizowasilishwa Kamati ilitaka kujua kwanini matumizi ya MV. Mapinduzi II yamepungua ukilinganisha kwa kipindi cha mwaka 2018 na 2019 na kuelezwa kwamba hali hiyo ilitokana na kutofanya kazi kwa meli hiyo na kupelekea kutumia gharama ndogo za mafuta yasiyokuwa na tija. Kadhalika gharama za kodi za usafiri na bima hazikuwepo. Aidha, Kamati iligundua kwamba Shirika linadaiwa madeni yapatayo shilingi bilioni 10,613,722,819.77 kutoka kampuni/watoa huduma tofauti wakiwemo kampuni ya Gabco, Shirika la Bandari, TRA, Deman pamoja na Shipyards ambazo ni vigumu kwasasa kuweza kuyalipa madeni hayo kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa Shirika.

Kadhalika, Shirika linadai jumla ya shilingi bilioni 1,536,406,870.76 kutoka kwa wateja tofauti waliowapatia huduma na watu binafsi. Miongoni mwa wadaiwa ni pamoja na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Hali hiyo inazidi kulididimiza Shirika kimapato na kushindwa kujipatia faida katika uendeshaji wa shughuli zake.

Kamati ilisikitishwa na taarifa kuwa meli za Shirika haziingizi faida na zinakwenda kwa hasara isipokuwa meli MT. Mkombozi pekee na kwasasa MT. Mkombozi II tayari imeshafanyiwa matengenezo na inaonekana itawapatia faida Shirika. Hali hiyo imetokana na kuharibika mara kwa mara kwa MV. Mapinduzi na MV. Maendeleo iliyopo Kenya kimatengenezo. Aidha, Kamati ilishitushwa na maelezo kwamba wakati wa ununuzi wa MV. Mapinduzi II, wataalamu wa Shirika hawakushirikishwa ipasavyo katika utoaji mawazo yao na ufuatiliaji wa matengenezo ya meli hiyo tangu hatua za awali. Hali iliyopelekea kushindwa kufanyakazi kwa meli hiyo na Serikali kufanya maamuzi magumu ya kuuzwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati ilitaka ipatiwe ushauri wa wataalamu kuhusu meli ya MV. Mapinduzi II na MV. Maendeleo lakini hadi Kamati inawasilisha hotuba yake haijapatiwa.

Mbali na hayo, Kamati imegundua kuwa Shirika linakosa baadhi ya mapato yake kutokana na kushindwa kusimamia vizuri utekelezaji wa majukumu yake kwani kuna baadhi ya watoa mizigo (clearing and forwarding) huruhusiwa kuchukua mizigo yao kwa ahadi ya kulipa baada ya kufanya biashara zao jambo ambalo hupelekea kutotekeleza ahadi zao na kulisababishia hasara Shirika. Miongoni mwa Makampuni hayo ni pamoja

na Zubeid Abdalla, Juma Shaaban na Gapco Zanzibar.

Kamati pia imegundua miongoni mwa sababu inayopelekea Shirika letu kutofanya vizuri ni pamoja na kuwepo maslahi madogo wanayolipwa ukilinganisha na watendaji wa meli nyengine. Hali hiyo husababisha wataalamu wao kuhama kwani kipato wanacholipwa kinapungua kwa kiwango cha mara mbili zaidi ya kile wanacholipwa wafanyakazi wa makampuni mengine.

Mapendekezo ya Kamati

1. Shirika lihakikishe linalipa madeni inayodaiwa na inafuatilia kwa karibu madeni yote inayodai ili liweze kukuza kuongeza mapato na mtaji wake.
2. Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iwashirikishe wataalamu wa Shirika tangu katika hatua za awali za ununuzi wa meli mpya hadi katika uendeshaji wa meli hizo.
3. Serikali iwapatie Shirika meli mpya na zenye unafuu katika uendeshaji wake na ilikabidhi Shirika kuziendesha na Serikali ibakie kuwa msimamizi wa kupatiwa gawio lake.
4. Serikali ihakikishe inawalipa mishahara mizuri wafanyakazi wa Shirika angalau waweze kulingana na watendaji wa makampuni mengine ya meli.
5. Shirika liondokane na mazoea ya kuwaruhusu wafanyabiashara kutoa mizigo kabla ya kulipa gharama husika.

Ufanisi katika utendaji wa shIrika la Meli

Mwenendo usioridhisha wa hali ya kifedha

Kwa miaka miwili, Shirika limekuwa na mwenendo usioridhisha kwa kupata hasara mfululizo. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hasara iliyopatikana ilikuwa shilingi 548,829,047.17 na kwa hesabu za mwaka ulioishia Juni 2019, hasara ilikuwa shilingi 722,331,653.16. Mwenendo wa hasara umekuwa ukichangiwa na hali isiyoridhisha ya uendeshaji wa meli pamoja na ongezeko la gharama za uendeshaji wa meli. Mfululizo wa hasara hizo una athari kubwa kwenye Mtaji wa Shirika, hivyo kulifanya kutokopesheka ili kukidhi mahitaji yake ya kifedha.

Aidha, kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2020, madai yameongezeka kwa asilimia 28.75, hadi shilingi 10,613,722,819.77 kutoka shilingi 8,243,483,029.18 zilizoripotiwa kwenye hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2019. Kwa upande mwengine, thamani ya wadaiwa imeongezeka hadi shilingi 958,469,686.45 kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2020, kutoka shilingi 681,131,184.63 zilizoripotiwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2019.

Majibu ya Shirika

Kwa mwaka wa Fedha 2019/2021 Shirika la Meli Zanzibar, meli zake zilitumia fedha zaidi kuliko mapato yaliyoingia. Ukiondoa meli ya Ukombozi, meli zote za Shirika zilitumia zaidi kuliko kipato zilichoingiza jambo lililopelekea kupata hasara za mfululizo kama Jadweli lifuatalo linavyoonesha:

CHANZO CHA MAPATO	MAPATO	MATUMIZI	ZIADA/PINGUFU
M.V. Maendeleo	-	276,256,279.08	- 276,256,279.08
M.V. Mapinduzi II	1,999,286,779	7,335,503,451.88	- 5,336,216,672.53
Charter Hire M.T.S.Ukombozi	2,654,315,194	1,474,736,184.34	1,179,579,009.61
Charter Hire M.T.S.Ukombozi II	287,495,145	2,471,430,196.76	- 2,183,935,051.58
	4,941,097,118	**11,557,926,112**	**- 6,616,828,994**

Aidha kuongezeka kwa madeni ya Shirika kunatokana na kutumia mikopo zaidi katika kuendesha shughuli zake za kila siku na uendeshaji wa Meli. Hali hii imechangia ongezeko la Madeni kwa kuwa meli zao zilikuwa zikitumia fedha nyingi bila ya kutoa tija ambayo ingetumika kulipa gharama za uendeshaji.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa vile Serikali tayari imeshalitolea maamuzi suala la upatikanaji wa hasara zinazotokana na uendeshaji wa meli za Shirika kwamba imepanga kuziuza meli hizo na kununua meli nyengine na kwa kuwa majibu ya hoja hii yameguswa katika hoja ya matumizi. Hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi kwa Shirika.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.7.1 Kutowasilisha makato ya Kisheria shilingi 203,895,169

Ukaguzi kupitia taarifa ya Makato ya Kisheria wa Shirika la Meli na kubaini kwamba jumla ya kiasi kilichotajwa hapo juu kinajumuisha makato ya Kisheria ya kodi ya Mapato kutoka katika Mshahara (Payee) ya Shilingi 135.508,821 na kodi ya ujenzi na maendeleo yenye thamani ya Shilingi 68,386,374 hayakupelekwa katika Mamlaka ya Mapato (TRA) Madeni hayo yameendelea kuongezeka kwa miaka kadhaa. Hali hii hupelekea kulipa faini, riba na adhabu ambazo zitaathiri hali ya kifedha ya Shirika la Meli, hivyo kupelekea

kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa. Utolipa kwa kodi kunaweza kuathiri kiasi cha mapato ambayo Serikali ingelipata.

Majibu ya Shirika

Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2019/2020, Shirika lilikuwa linadaiwa kiasi kikubwa cha fedha ikiwemo malipo ya Makato ya Kodi kwa Mamlaka mbali mbali. Hali hii ilitokana na fedha ambazo zilitengwa kulipa makato ya kisheria kutumika katika kuokoa uendeshaji wa Shirika hasa kuzinusuru na uharibifu Meli zetu ambazo bila ya kuchukuwa hatua za dharura zingeweza kuwa katika hali mbaya zaidi.

Katika kukabiliana na kipindi hiki cha mpito, shirika liliandika barua kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuzijuilisha hali halisi ya mwenendo wa Shirika na kuwa halijakataa wala kukimbia dhima zake na mara litakapopata ufumbuzi wa changamoto zake litalipa madeni yake.

Jitihada zimefanyika na sasa hali ya kifedha imeanza kuimarika na hivyo Shirika la Meli Zanzibar limeanza kulipa Kodi zake kwa TRA na Mamlaka nyingine za mapato.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iligundua kwamba barua ya Shirika la Meli na Uwakala iliyoandikwa kupelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania iliandikwa nje ya muda wa ukaguzi na ndio maana hoja hii ikaingizwa kwenye kitabu cha Mdhibiti. Kamati ilitaka kujua shughuli ambazo fedha hizo za kodi zilifanyiwa matumizi gani na kuelezwa kuwa zilinunuliwa kifaa maalum cha MV. Mkombozi II kwa ajili ya matengenezo ya meli ambacho kilichelewa kufika kutokana na kuibuka kwa maradhi ya uviko 19 ambapo mwezi wa 6, 2020 kifaa hicho kilifika na kuingizwa na mwezi wa 7, 2020 meli hiyo ilianza kufanyakazi.

Kuhusu Mkataba wa matengenezo ya meli hiyo, Kamati ilielezwa kwamba Mkataba huo haukueleza baadhi ya mambo ya msingi ikiwemo mjenzi afanye matengenezo iwapo kutatokezea hitilafu badala yake Shirika lilifanya wenyewe.

Mapendekezo ya Kamati

1. Shirika linapoingia Mkataba wa kutengenezewa meli linatakiwa liingize kipindi cha dhamana (guarantee period) ambapo kukitokezea maharibiko Mjenzi awajibike kufanya matengenezo husika.

2. Shirika lihakikishe makato ya kisheria yanalipwa kwa wakati hususan kodi ambazo ndio zinazokwenda kuwaletea wananchi wetu maendeleo.

3. Watendaji wa Shirika hususan mafundi washirikishwe ipasavyo wakati Mjenzi wa meli anapoifanyia matengenezo meli husika ili kuwaongezea ujuzi wao.

3.7.2 Kukosekana kwa Ufanisi katika Meli ya Ukombozi II

Katika kipindi cha mwaka unaoishia Juni 2020, ukaguzi ulipitia taarifa za mapato na matumizi ya Meli ya MT. Ukomozi II kwa lengo la kuangalia ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa meli hiyo na kubaini kwamba jumla ya shilingi 2,471,430,196.76 zilitumika ikiwa ni sehemu ya gharama za uendeshaji wa meli za Ukombozi II ikilinganishwa na mapato halisi ya yaliyopatikana na meli hiyo ambayo ni shilingi 287,495,145.18. Aidha ukaguzi ulifuatilia zaidi na kubaini kwamba meli mpya ya mafuta MT. Ukombozi II tangu ilipowasili Zanzibar ilifanya safari moja tu baada ya Serikali kuikabidhi mnamo tarehe 01.10.2019. Kukosekana kwa ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa meli hii mpya kumepelekea kukosa mapato ambayo yangeweza kusaidia kumudu gharanma za uendeshaji na kulifanya shirika kujiendesha kiufanisi.

Majibu ya Shirika

Meli ya Ukombozi II ilikabidhiwa kwa Serikali kutoka kwa Mjenzi kampuni ya Darmen ya Uholanzi mwezi wa Septemba 2019 na ilikabidhiwa Shirika la Meli Zanzibar kwa ajili ya uendeshaji. Ili Meli ifanye kazi inapaswa kukamilisha taratibu zote za Kisheria. Itakumbukwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020, Meli ya MT. Ukombozi II ilifanya safari moja tu ya kibiashara, tarehe 05 Disemba 2019.

Safari hiyo ilikuwa ya majaribio ambayo Meli ya Ukombozi II ilikumbwa na changamoto mbali mbali. Miongoni mwa changamoto zilitokea ni kutokea hitilafu katika mfumo wa ushushaji wa mafuta zilizotokana na udhaifu wa baadhi ya vifaa katika mfumo huo. Maharibiko haya yaliwasilishwa moja kwa moja kwa mjenzi wa Meli kwani meli hii ilikuwa katika kipindi cha dhamana ya Mjenzi (guarantee).

Mjenzi alihitaji muda ili kuwasilisha na kukifunga kifaa kilichoharibika jambo ambalo lilisababisha meli kusita kufanya kazi zake za kawaida za kusafirisha mafuta na ililazimika kukaa nangani ikisubiri matengenezo. Ni wazi kuwa meli hii bado ilikuwa ikiendelea kutumia gharama kubwa ikiwa nangani ikiwemo mafuta ya majenereta. Hata

hivyo, mpaka unamaliza mwaka wa fedha 2019/2020 meli hiyo haikuweza kufanya safari nyengine ya kibiashara kwa sababu kifaa kilichokuwa kikisubiriwa kilikuwa hakijawasili. Jadweli lifuatalo linaonesha matumizi ya shilingi 2,471,430,196.76:

HUDUMA	MATUMIZI
Crew Salary & Allowances Ukombozi	54,163,529.50
Fuel (Bunker)	554,649,000.00
Lubricants	8,801,856.00
Insurance M.T.Ukombozi	512,259,298.58
Stevedoring, Port MT Ukombozi	12,621,907.70
Water Ukombozi	5,510,332.00
Survey & Certification MT. Ukombozi	25,990,028.83
Repair & Maintanances Ukombozi	42,173,800.15
Crews Food Ukombozi	24,809,000.00
Crews Uniforms MT. Ukombozi	1,489,000.00
Cleaning tools - Ukombozi	3,600,000.00
Depreciation MT Ukombozi	1,225,362,444.00
JUMLA	**2,471,430,196.76**

Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati
Kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa kasoro hiyo wakati Mkaguzi anafanya kazi zake katika Shirika hilo. Kamati haikuwa na hoja zaidi.

3.7.3 Kukosekana kwa mfumo wa usimamizi wa viashiria vya hatari kwa Taasisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Meli halijaandaa mfumo wa namna ya kufanya utambuzi wa viashiria vya hatari kwa Shirika jambo ambalo lingesaidia kuepukana na viashiria vinavyowea kupelekea kuathiri utendaji wa Shirika la meli katika uendeshaji wa meli pamoja na shughuli za uwakala ili kuweza kufika malengo yaliyokusudiwa.

Kukosekana kwa mfumo wa usimamizi wa viashiria vya hatari kwa Shirika kumepeleka kusita kwa utoaji wa huduma za meli kwa muda mrefu na kusababisha usumbufu kwa abiria ambao ni wananchi wanaotegemea huduma za meli za Serikali kwa kiwango kikubwa kutokana na gharama nafuu za tiketi za safari kwa upande wa wasafiri wa Unguja na Pemba.

Majibu ya Shirika

Shirika limepokea ushauri wa Mkaguzi na limeshaanza kuufanyia kazi ushauri huo, Shirika limejipanga kutoa elimu ya utambuzi wa viashiria vya hatari (risks) kwa watendaji wakuu wa Idara na vitengo.

Kabla ya kutengeneza mfumo kila mkuu wa Idara au kitengo atatakiwa kuainisha viashiria vya hatari katika Idara au kitengo chake, na baadae mfumo mmoja utatengenezwa kwa Shirika zima.

Shirika kwa sasa ingawa halijaweka mfumo rasmi kimaandishi lakini linatambua viashiria vyake vya hatari na udhibiti wa ndani (internal control) umewekwa ili kujikinga na hatari za baadae zinazoweza kutokea. Njia tofauti zinatumika katika kudhibiti hatari kwa kila Idara, miongoni mwa njia hizo ni:

1. Kuwepo kwa mfumo (electronic system) wa ufatiliaji wa utoaji wa makontena na mizigo mengine. Mfumo huu umeunganishwa moja kwa moja na benki na malipo yote yanapitia benki. Shirika limeondosha kabisa opokeaji wa fedha taslim na kupunguza janga au kiashirika cha upotevu, wizi na ucheleweshaji wa kupeleka fedha benki.

2. Kuondosha uwezo wa kusaini cheki na nyaraka nyengine za kibenki kwa baadhi ya watendaji (wahasibu).

3. Kuwepo kwa mfumo wa benki (online banking) ambapo Mkurugenzi Muendeshaji anaweza kuona taarifa zote za kibenki na miamala yote aliyoipitisha kila siku.

4. Kuwepo na mgawanyo wa majukumu (segregation of duties).

5. Kuwepo kwa kinga za bima za Shirika (Insurances), kinga hizi ni kwa ajili ya kufidia athari za uharibifu wa bahari, ajali kwa mabaharia na meli.

6. Kuwepo na watendaji maalum wanaosimamia usalama wa meli (DPA).

7. Kuwepo kwa kitengo cha ukaguzi wa ndani na kamati ya ukaguzi.

Kukosekana kwa mfumo wa usimamizi wa viashiria vya hatari sio sababu ya moja kwa

moja iliyopelekea kusita kwa utoaji wa huduma za meli kwa muda mrefu, miongoni mwa sababu kubwa zilizopelekea kuathiri utendaji wa Shirika ni:

1. Maharibiko ya mara kwa mara ya MV. Mapinduzi II na gharama kubwa za uendeshaji wa meli hii.
2. Uchakavu wa meli ya MT. Ukombozi na MV. Maendeleo.
3. Kusita kufanyakazi kwa MT. Ukombozi II kutokana na hitilafu za kiufundi. Meli hii ilinunuliwa na Serikali na kukabidhiwa Shirika la Meli mwezi Octoba, 2019. Dosari nyingi zilijitokeza baada ya kufanya safari yake ya kwanza na zilikuwa nje ya uwezo wa Shirika kuzitatua.

Uchunguzi wa Kamati

Kupitia majibu hayo, Kamati ilitaka kujua Shirika lina mpango gani wa kuwapatia utaalamu wafanyakazi wake na wanashirikiana vipi na mataifa mengine yaliyoendelea zaidi katika shughuli za uendeshaji wa meli na kuelezwa kwamba Shirika tayari limeshafanya mazungumzo na Barma kuja kuwafundisha wafanyakazi wao kuhusu uendeshaji bora wa meli kwa kipindi cha miaka miwili. Hata hivyo, uongozi wa Shirika umeeleza kwamba unakabiliwa na changamoto ya kuwepo mwitikio mdogo wanapotangaza nafasi za ajira kwa vile maslahi wanayolipwa ni madogo.

Mapendekezo ya Kamati

1. Shirika liharakishe kutengeneza mfumo wake ili hoja kama hiyo isijitokeze mara nyengine.
2. Shirika liendelee kuwapatia mafunzo tofauti wafanyakazi wake ili waweze kusimamia vyema viashiria hatarishi vyao.
3. Shirika iharakishe kufuatilia kwa karibu wahisani waliojitokeza kuwapatia mafunzo watendaji wa Shirika letu.

3.7.4 Kukosekana kwa ripoti ya kiufundi katika usimamizi wa matengenezo ya meli ya MV. Maendeleo uliyogharimu jumla ya shilingi 3,322,810,664.23

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 3,322,810,664.23 zilizotumika kuifanya matengenezo makubwa MV. Maendeleo iliyopo chelezoni Mombasa nchini Kenya.

Pamoja na gharama kubwa iliyotumika katika matengenezo hayo kumekosekana ripoti ya Kiufundi kutoka katika Idara ya Ufundi ya Shirika la meli Zanzibar ambayo ndio inayowajibika kutolea taarifa matengenezo ya meli zote za Shirika kutokana na uharibifu pamoja na pale chombo kinapohitajika kufanyiwa matengenezo mara kwa mara ili kutoa picha halisi ya vifaa pamoja na matengenezo husika yaliyofanyika kabla ya kufanya malipo.

Kukosekana ripoti hyo kumepelekea kutokuwepo kwa thamani ya mchango wa kiufundi kutoka Idara ya Ufundi ya Shirika la Meli pamoja na kutokuwepo kwa uwazi wa gharama kubwa zilizotumika katika matengenezo ya meli hiyo ambayo kwa kipindi kirefu zaidi ya mwaka mmoja ipo chelezoni Mombasa nchini Kenya.

Majibu ya Shirika

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Shirika la Meli Zanzibar liliipeleka meli ya (MV. Maendeleo) Chelezoni kwa ajili ya matengezo makubwa. Kabla ya Meli kupelekwa Mombasa nchini Kenya uongozi wa Shirika ulitoa maagizo kwa Mkurugenzi wa Idara Ufundi na Uendeshaji (ambaye aliambatana na meli kuelekea Mombasa) kuikagua meli hiyo na kuwasilisha ripoti yake kwa kila hatua ya ujenzi inayofikiwa.

Kwa bahati mbaya tarehe 02.12.2020 wakati meli ya MV. Maendeleo ikiwa katika Chelezo cha Africa Marine Mombasa nchini Kenya, Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirika la Meli Zanzibar alihamishiwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuendelea na kazi. Kwa kuwa kazi hii ilikuwa ya kitaalamu na kuondoka kwa Mkurugenzi ufundi lilikuwa ni jambo la ghafla. Shirika lilifanya jitihada ya kutafuta mtumishi mwengine kujaza nafasi ya Mkurugenzi ufundi bila yamafanikio.

Hivyo Baadhi ya Kazi ambazo zimeshafanywa zimeachwa na hazijathibitishwa zikisubiri ujio wa Mkurugenzi mpya au mtaalamu ambaye ataajiriwa na Shirika la Meli kwa ajili ya kazi hiyo ili hatua nyengine ziendelee.

Gharama ya shilingi 3,322,810,664.23 haikuwa gharama ya Chelezo pekee bali ilijumisha

gharama mbali mbali za ujenzi wa Meli ya MV. Maendeleo. Gharama hizo zilijumuisha matayarisho ya Msingi kabla ya Meli kuelekea chelezoni Mombasa. Baadhi ya vifaa na vipuri vilinunuliwa kabla ya meli haijapelekwa chelezoni.

Gharama hizo zilijumuisha unununzi wa Hydraulic Motor, unununzi wa Mashine na Generator za Meli (Main Engine Nigata and generators), uchomeaji na uzibaji wa ndani ya Meli (Underwater welding), kodi ya Generator la dharura, generator hilo lipo nchini Kenya, Meli ya MV. Maendeleo ilipelekwa Mombasa Kenya ikikokotwa na Tagi shwari iliyokodiwa kutoka Shirika la Bandari Zanzibar, gharama ya Wakala wa meli pamoja na gharama za Bandari nchini Kenya. Kulingana na miongozo ya masuala ya Bahari meli yoyote iliyo katika bandari ya kigeni ni lazima ihudumiwe na wakala kutoka katika nchi husika, posho la Mabaharia. gGharama za Mikopo (direct attributable), gharama za matengenezo makubwa ya kazi za chuma na Kodi ya Chelezo pamoja na umeme wa kufanyia kazi Melini (Shore power supply).

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati iligundua kwamba uhamisho wa Mkurugenzi Ufundi haukuwa uhamisho wa kawaida maana katika hali ya kawaida huwezi kumuhamisha mfanyakazi wakati kuna kazi anafanya na hakuna mtu ambaye anaweza kutekeleza kazi husika na hata kama yupo basi inatakiwa afike eneo la kazi husika ili kusitokee hitilafu yoyote. Aidha, Kamati imebaini kuwa wakati ukaguzi unafanyika Mkurugenzi Ufundi alikuwepo na kuthibitisha barua/ripoti ya matengenezo ya awali ya tarehe 3 mwezi wa 7, 2019 pamoja na 'invoice' yake yenye gharama za malipo ya dola za marekani 97,750.80 sawa na asilimia 30 ya Mkataba kwa Africa Marine Ltd. lakini Kamati imeshindwa kuona ripoti ya ufundi itakayohitajika kulipwa asilimia 70 iliyobakia kama ilivyoelezwa ktika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mapendekezo ya Kamati

1. Shirika linatakiwa kuwa makini sana wakati wanapoamua kufanya uhamisho wa wafanyazi mtaalamu ambaye hakuna mtu mfanyakazi mwengine anayeiweza kazi yake.
2. Shirika ihakikishe linaishirikisha Kamati ipasavyo kwenda kuona kuiona MV. Maendeleo na kushauri.
3. Shirika lihakikishe linaandaa ripoti ya kitaalamu wanapotaka kuzifanyia matengenezo meli zao.

UKAGUZI MAALUM WA KAMATI YA LAAC KWA SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA DAR - ES - SALAAM

Kwa vile Shirika linafanyakazi na linazo meli zake Dar - es - Salaam, Kamati iliona kwamba ili kupata taswira halisi na sahihi ya ukaguzi wake ni lazima ifanye safari kwenda kukagua meli na utendaji wa Shirika Dar - es - Salaam tarehe 19 Januari, 2021.

Katika ukaguzi huo, Kamati ilitembelea eneo zinazofunga gati meli za Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar katika bandari ya Dar - es - Salaam, nyumba za Shirika, Ofisi ya Shirika pamoja na kufanya kikao na watendaji wa Shirika. Kiujumla, Kamati iligundua mambo ya msingi yafuatayo:

1. Shirika linamiliki meli nyumba 2 ziliopo Magomeni; moja imenunuliwa 2015 ambayo ina vyumba 12 inayotumiwa na wanafunzi wa Shirika wakiwa masomoni na ya pili inamilikiwa na Shirika tangu 1996 yenye vyumba vinane ambavyo inatumiwa na Mabaharia.
2. Kwasasa, nyumba zote hizo hazitumiki kama ilivyokusudiwa kwa vile shughuli za uendeshaji wa meli zimepungua na hakuna wanafunzi wanaosoma.
3. Nyumba hizo zinasimamiwa na mstaafu wa Shirika ambaye analipwa shilingi 60,000/- kila mwezi. Lakushangaza, malipo hayo yanafanyika pasi na kuwepo Mkataba wowote wa ajira.
4. Shirika Dar - es - Salaam linao wafanyakazi watano ambao wote ni wakaazi wa Dar - es - Salaam ila wakati meli zilipokuwa zikifanyakazi waliongezeka kwa kufanya maombi ya wafanyakazi Zanzibar.
5. Shirika lina mpango wa kuzungumza na ZSSF ili kuzijenga ziwe za ghorofa nyumba hizo.
6. Shirika lilichukua juhudi za kutafuta wadhamini kutoka tanzania Bara kama vile Shirika la Nyumba Tanzania ili kuingia ubia wa kujenga eneo hilo lakini walieleza kwamba eneo hilo ni dogo halitoshi kwa ujenzi wa jengo la ghorofa. Kamati imelitembelea eneo hilo na kujiridhisha kwamba ni eneo kubwa ambalo linatosha kwa juenzi wa aina hiyo.
7. Kamati imegundua MV. Mapinduzi II inafunga gati eneo liliopo mbali ndani ya Bandari tofauti na meli za Makampuni mengine. Hali hiyo imesababishwa na muundo wa meli yenyewe kuwa na ‘draft’ ambao sio rafiki kufunga gati eneo la kawaida.
8. Kamati pia imegundua abiria wa MV. Mapinduzi II na MV. Maendeleo wanashuka mbali na geti namba 1 na kusababisha kupata usumbufu wa kutoka kwa kutembea sana hususan wakiwa na mizigo ambapo hata gari za binafsi (tax) haziruhusiwi kufika huko wanapoteremka.
9. Kamati ilishangazwa na taarifa kwamba wataalamu waliokuwa wanaiunda MV. Mapinduzi II walifika na kuangalia mazingira ya Bandari ya Dar - es - Salaam na kupatiwa ushauri na wataalamu wa Shirika kwamba meli itakayoundwa iwe rafiki katika ufungaji gati wake lakini meli iliyotengenezwa haikufuata ushauri wao.
10. Kamati imegundua kwamba kwasasa hakuna banda la kukaa abiria wanaosubiri kusafiri kwani banda lililokuwepo awali lilivunjwa kutokana na ujenzi wa utanuzi wa bandari ya Dar - es - Salaam. Hata hivyo, Shirika likishapatiwa meli litafanya mazungumzo ya kujengwa upya banda hilo na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).
11. Shirika linapata mashirikiano ya kutosha kutoka Shirika la Bandari la Dar - es - Salaam.

12. Kamati pia imebaini kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ilikuwa tayari kutoa msamaha wa gharama za ufungaji gati kwa meli ya Mapinduzi II ambayo hutolewa kupitia maombi maalum kutoka kwa kepteni wa meli husika. Lakushangaza na kusikitisha makepteni wa Shirika la Meli na Uwakala huwa wanashindwa kufanya maombi hayo na kupelekea kukosa msamaha.
13. Kamati imegundua kwamba bado kuna umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa Shirika hili la Meli na sio kuliondosha kutokana na fursa za uwezekano wa kujipatia mapato makubwa zaidi.
14. Kamati imegundua kwamba kwa kipindi hiki ambacho Shirika halikuwa na meli ya abiria, wafanyakazi wa Shirika waliopo Dar - es - Salaam huwa hawana kazi na kupekelea kulipwa mishahara pasi na kuwepo tija. Hili lilibainika wakati Kamati ilipokuwa ikipokea taarifa ya shughuli za Shirika Dar - es - Salaam ambapo Kamati haikuridhishwa na ripoti iliyowasilishwa na Meneja wa Shirika Dar - es - Salaam kwa vile haikuwa na taarifa zozote zenye takwimu za mapato na matumizi ya mwaka 2019/2020 ya Shirika (taarifa za fedha).

    Kutokana na hilo, Kamati ilitaka ipatiwe ripoti yenye takwimu na kuahidiwa kwamba itaandaliwa na kuwasilishwa lakini hadi Kamati inawasilisha ripoti yake katika Baraza, hakuna taarifa yoyote iliyopatikana, jambo linaloitia wasiwasi Kamati kwamba Shirika halikuwa na usimamizi mzuri katika uendeshaji wa majukumu yake.

Mapendekezo ya Kamati

1. Shirika lishirikiane na Taasisi za SMZ zinazofanya kazi Tanzania Bara ili waingie ubia wa kujenga jengo la ghorofa katika eneo hilo kwa maslahi ya Wabia hao.
2. Makepteni wa Shirika wanapopatiwa fursa za kupata msamaha, wafuate taratibu zilizowekwa kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama zisizostahiki.
3. Shirika liwasilishe maombi ya kujengewa Banda la Abiria karibu na sehemu zinapofunga gati meli zetu.
4. Shirika litafuatilie Shirika la bandari Dar - es - Salaam ili watengenewe njia ya kupita abiria wetu mara wanaposhuka ili kuwapunguzia umbali hususan abiria wenye mizigo na watoto.
5. Kamati inasisitiza utaalamu mzuri unaotolewa na watendaji wetu ufuatwe/utekelezwe ili tija ya kile kinachofanywa iweze kupatikana.
6. Mfanyakazi anayekaa katika nyumba hizo apatiwe mkataba wa malipo anayoyafanya.
7. Shirika liache tabia ya kuipatia taarifa zisizoridhisha Kamati na inalitaka Shirika liwasilishe taarifa ya mapato na matumizi yake kwa upande wa Dar - es - Salaam kama ilivyoelekeza Kamati.
8. Uongozi wa Shirika utafute njia mbadala kuhakikisha nyumba wanazomiliki zinatumika na kuliingizia mapato Shirika na sio kuziacha zikawa zinachakaa kwani hizo ni rasilimali muhimu iwapo zitatumika vizuri.
9. Serikali ilipatie nyenzo na wataalamu Shirika ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

3.9: MFUKO WA BARABARA (ZRF)

Taarifa ya Mapato

Mapato ya Mfuko wa Barabara yameongezeka kutoka TZS. 12,437,192,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia TZS. 13,530,051,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la TZS. 1,092,859,000 sawa na asilimia 8.8.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kama ukaguzi ulivyoonesha kuwa makusanyo ya mapato kwa mwaka 2019/2020 yalikuwa yamefikia TZS. 13,530,051,000 ukilinganisha na TZS. 12,437,192,000 ya mwaka 2018/2019. Mapato hayo yametokana na vyanzo vyake vya 'Roads Development Ley, Motor Vehicle Levy, Funds Received from TANROADS' na 'Rental income'.

Aidha, fedha zilizopokelewa kutoka TANROADS (20,508,000) zilikuwa ni kwa ajili ya kuendesha Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Mfuko ya Barabara wa Zanzibar ni Mwanachama katika Jumuiya hiyo.

Uchunguzi wa Kamati

Katika ufuatiliaji wa hoja hii, Kamati iligundua mambo yafuatayo:

1. Kuwepo kwa ongezeko la mapato ukilinganisha mwaka 2018/2019 na 2019/2020 kumetokana na ununuzi mkubwa wa mafuta ambayo ni moja kati ya vyanzo vyao viwili wanavyojitegemea. Hata hivyo, yakilinganishwa mapato (shilingi 13,530,051,000) na makisio yao (shilingi 15,139,416,000), Kamati imegundua kwamba mapato hayo yamepungua kwa shilingi 1,609,365,000) kutokana na kuibuka kwa maradhi ya Covid 19.

2. Mfuko haujazifanyia marekebisho tofauti ya fedha iliyoonekana katika Ripoti yao ya Fedha ya Mfuko wakati wa ukaguzi. Hilo limebainiwa na Kamati baada ya kuona kuna tofauti ndogo ya matumizi yanayoonekana katika ripoti ya Mdhibiti na taarifa ya fedha ya mwisho ya Mfuko.

3. Mfuko unategemea vyanzo vikuu viwili vya mapato ambavyo ni fedha za uuzaji wa mafuta zinazotolewa na TRA na ZRB pamoja na chanzo cha kodi ya jengo lao.

4. Fedha za tozo ya mafuta (shilingi 100 kwa kila lita) zinazokusanywa na ZRB

baada ya kukata asilimia 5, hazipelekwi zote katika hesabu ya hazina. Hili limebainika baada ya Mfuko kufuatilia na kugundua taarifa za matumizi ya mafuta hayo zilizokusanywa katika mfumo wa ZURA haziendani sambamba na zile zinazoonekana katika hesabu inayowasilishwa na ZRB (barua ya tarehe 9 Novemba, 2021 yenye kumbukumbu nambari ZRB/M.29/Vol. II/93 inahusika).

5. Aidha, Kamati imegundua kuna upotevu na ubadhirifu mkubwa wa fedha zinazowasilishwa katika Mfuko kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwani huwa hazilingani na kumbukumbu zilizowasilishwa na ZRB. Hili limebainika baada ya Kamati kupitia kumbukumbu ya nakala ya barua ya uwasilishwaji wa fedha hizo katika hesabu ya hazina kutoka ZRB kuwa ni tofauti na kiwango halisi wanachoingiziwa Mfuko na Wizara ya Fedha na Mipango.

6. Kamati imebaini kwamba Wizara ya Fedha haiziingizi fedha zote katika hesabu ya Mfuko kutoka hesabu ya hazina bila ya idhini ya Bodi, kitu ambacho ni kinyume na kifungu cha 3 cha Sheria ya Mfuko wa Barabara namba 2 ya mwaka 2001 kinachotaka fedha za Mfuko ziingizwe moja kwa moja katika Mfuko na zitumike kwa matumizi ya uendelezaji shughuli za Mfuko.

7. Kamati imepitia barua ya tarehe 23 Mei, 2019 yenye kumbukumbu nambari MRK/MT/MFB/F/VOL.IV/57 na kugundua kwamba, Mfuko huwaandikia barua Wizara ya Fedha kukumbushia bakaa ya deni lao lakini kwa bahati mbaya Wizara ya Fedha na Mipango haijawahi kujibu barua hizo na kupelekea hoja ya ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti (CAG). Lakushangaza, miongoni mwa wajumbe wa Bodi ya Mfuko yumo Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango ambaye aliwahi kuomba katika kikao cha Bodi kwamba deni hilo lifutwe.

8. Kamati imegundua pia Mfuko unaidai Wizara ya Fedha na Mipango jumla ya shilingi 3,272,603,000 kupitia barua namba MRK/MRK/MT/MFB/F/VOL.V/62 ya tarehe 14 Disemba, 2020 hadi Kamati inafanya ukaguzi wake.

9. Sambamba na hayo, Kamati imebaini Mwenyekiti na wajumbe wawili wa Bodi wameshamaliza muda wao na kusababisha ugumu katika utendaji kazi wa Mfuko.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mfuko wa Barabara uwe na mfumo wake wenyewe utakakuwa unaoana na mifumo ya ZRB na ZURA ambao utawezesha kutambua mapato halisi yaliyokusanywa na ZRB yanaendana na kumbukumbu zilizopo ZURA.
2. Mfuko uingiziwe fedha za mapato yake moja kwa moja katika hesabu (account) yake kama inavyoelekeza Sheria yao na sio fedha kwanza zipitie Wizara ya Fedha

na Mipango.

3. Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inalipa deni lote inalodaiwa na Mfuko ili Mfuko huo uweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

4. Mfuko upatiwe Mwenyekiti na wajumbe wake ili uweze kusimamia kikamilifu na kuboresha utendaji wa Mfuko.

5. Fedha zinazokusanywa na ZRB ziwe zinaendana na lita za mafuta zinazopatikana katika mfumo uliopo ZURA ili kuweza kutoa hali halisi na sahihi ya mapato hayo.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Mfuko wa Barabara yameongozeka na kufikia TZS. 15,881,486,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kutoka TZS. 11,669,313,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la TZS 4,189,109,000.

Majibu ya Mfuko

Kama, ukaguzi ulivyobaini, kumekuwa na ongezeko la matumizi kwa mwaka 2019/2020 ukilinganishwa na mwaka uliopita wa 2018/2019 kwa asilimia 35.9. Aidha, Kutokana na taratibu za ufungaji wa hesabu, matumizi haya yamejumuisha, matumizi ya uchakavu wa mali za kudumu (depreciation) ambayo ni TZS 72 milioni kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na TZS 80,671 kwa mwaka wa Fedha 2018/2019.

Uchunguzi wa Kamati

Baada ya kupitia taarifa ya matumizi, Kamati ya LAAC imegundua mambo yafuatayo:

1. Kuwepo kwa tofauti ya fedha za matumizi ya Mfuko ambapo Ripoti ya Mdhibiti imeainisha jumla ya fedha zilizotumika kuwa ni shilingi 15,881,422,000 wakati taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ya Mfuko imeonesha shilingi 15,881,486,000 kukiwa na tofauti ya shilingi 64,000 ambapo kiukaguzi, hata kama imepotea shilingi moja, basi kamati inahitaji kujua fedha hiyo ya umma imetumikaje. Hili limetokea baada Mdhibiti kugundua uwepo wa tofauti hiyo lakini watendaji wa Mfuko walichelewa kupeleka marekebisho yaliyofanywa katika fedha za baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na mfuko hadi muda Mdhibiti anachapisha kitabu chake.

2. Kadhalika, Kamati imegundua kuna tofauti ya fedha za makadirio zilizoainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka (shilingi 16,139,446 ukilinganisha na makadirio ya shilingi 13,668,214,790 zinazoonekana katika ripoti ya Mkaguzi wa Ndani. Hali hiyo iliipa mashaka Kamati kwa kuona kwamba kuna uwezekano wa kutokuwepo umakini au kuwepo kwa mchanganyiko katika uandishi wa fedha hizo.

Mapendekezo ya Kamati

1. Watendaji wa Mfuko wawe makini wanapoandika taarifa zao za kifedha kwani kukosea kuandika vizuri nambari moja kunaweza kusababisha makosa katika namba nyengine.
2. Watendaji wanatakiwa wafuate kikamilifu maelekezo wanayopatiwa na Mkaguzi anapopita katika maeneo yao kukagua.

Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance) Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wa msimamo wa mtaji (Position of Working Capital) wa Mfuko wa Barabara kwa muda wa miaka miwili na kubaini uwezo wa Mfuko wa Barabara kumudu madeni ya muda mfupi umepungua kufikia uwiano wa1.2:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2020 ukilinganisha na uwiano wa 2:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2019.

Kutokana na upungufu huo, ukaguzi umebaini kuna ufupungufu wa uwezo wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi. Hali hiyo kama ikiendelea, Mfuko unaweza kushindwa kumudu madeni ya muda mfupi.

Majibu ya Mfuko

Ni kweli, ukaguzi ulibaini kuwa mali za mpito (Current Assets) zinazidi dhima za mpito (Current Liabilities) kwa miaka yote miwili. Mali hizo za mpito zinajumuisha Akiba ya Benki wakati tunafunga hesabu, deni la tozo kwa mujibu wa sheria, malipo ya awali kwa wakandarasi na madeni ya mikopo ya Wafanyakazi. Dhima za mpito, zinajumuisha fedha za "Roll over" za matengenezo ya barabara, 'Provision' mbali mbali, 'Retention fee' na malipo ya bidhaa na huduma kwa wauzaji wa bidhaa na watoa huduma.
Sababu ya kushuka kwa kiwango hiki kumesababiswa na kiwango kikubwa cha deni linalotokana na tozo. Hali hii inaweza kubadilika endapo fedha hizo za deni zitaingizwa katika hesabu ya Mfuko.

Uchunguzi na Mapendekezo la Kamati

Kamati imebaini kwamba ufanisi wa Mfuko kifedha hauendi sambamba na kipimo cha uwiano kutokana na Mfuko kukabiliwa na deni la shilingi milioni 3,272,603,000 wanalodai Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, Mfuko ulipwe deni lake ili mtaji wake ukue na kuimarisha uwezo wake wa kulipa madeni.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.9.1 Ucheleweshaji wa utekelezaji wa kazi za ukarabati wa barabara

Mfuko Barabara Zanzibar (ZRF) ulisaini mikataba ya utendaji wa mwaka (Annual Performance Agreements) baina yake na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambapo ulipanga kutumia TZS. 14,553,985,000 kwa ajili ya kazi za matangenezo ya barabara.
Kwa upande wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi - Unguja ilipangiwa kutumia TZS. 8,926,984,751,000. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi - Pemba ilipangiwa kutumia TZS 1,786,506,899 na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilipangiwa kutumia TZS. 3,723,097,000.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 TZS. 4,632,742,734 kati ya TZS. 14,553,985,000 zimetumika na kubaki na bakaa ya TZS. 9,921,242,267 ya fedha ambazo hazikutumika sawa na asilimia 68 ya makadirio. Hii inatokana na ucheleweshaji wa utekelezaji wa kazi za ukarabati wa barabara zilizopangwa ambapo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020, kati ya miradi 16 iliyopangwa kutekelezwa, miradi 4 haikutekelezwa kabisa na 2 imechelewa kukamilishwa.

Kutokana na hali hiyo ya ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi husababisha kuongezeka kwa muda, matumizi ya fedha zaidi ya bajeti iliyopangwa, kukosekana kwa ubora wa miradi na wakati mwengine kutekelezwa kwa mradi.

Majibu ya Mfuko

Ni kweli kiwango cha utekelezaji kifedha upo chini ukilinganisha na fedha iliyopangwa kutumika kwa mwaka 2019/2020. Kiwango cha fedha kilichotumika ni asilimia 23 tu. Hata hivyo, kiwango halisi (physical works) kipo juu ukilinganisha na fedha iliyolipwa. Sababu zifuatazo zimechangia utekelezaji wa kiwango cha fedha kuwa kidogo:

Mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Fuoni Mambosasa - Mwera Wilayani yenye urefu wa kilomita 3.4 una gharama ya TZS. 3,289,995,700 kwa kiwango cha lami ulikuwa umefikia asilimia 75 ya utekelezaji, wakati Mkandarasi ameomba na amelipwa asilimia 18 tu ambayo ni TZS. 605,603,744 ya Mkataba wake. Hivyo imepelekea kiwango kikubwa cha fedha kubakia, hii ilitokana na Mkandarasi kuchelewa kuomba malipo ya kazi aliyoifanya kwa kipindi husika, ingawa hali halisi ya utekelezaji ulikuwa ushamalizika kwa asilimia 75 (physical performance).

TZS 151,740,000 zilipangwa kumlipa Mkandarasi ikiwa ni bakaa (deni) katika matengenezo ya barabara ya Msingini ambapo ilikuwa imeshakamilika tangu mwaka wa fedha 2017/2018. Mpaka kufikia Juni 30, 2020 malipo hayo yalikuwa hayajafanyika lakini utekelezaji halisi ulishakamilika.

TZS 20,000,000 ilipangwa kutumika kwa ajili ya kufanya “design” ya mtaro wa Fuoni Mambosasa kwa kutumia Mshauri Elekezi. Mpaka imefikia Juni 30, 2020, Fedha hizi zilikuwa hazijatumika kwani hatua za kumpata Mshauri Elekezi zilikuwa zinaendelea.

TZS 2,500,000 ni fedha zilizobakia baada ya kuvunjwa kwa Mkataba wa Kikundi cha usafi cha K/Samaki Tumekuja na TZS 5,157,500 ni fedha zilizobakia katika matumizi ya Afisi ambayo ni “Supervision”, “Capacity building” na “Administration”.

Kwa upande wa barabara zilizojengwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, jumla ya TZS. 10,830,888,000.00 zilitengwa kwa ajili ya matengenezo mbali mbali ya barabara na shughuli zinazohusiana na matengenezo ya barabara. Kati ya fedha hizo, Unguja zilitengwa kiasi cha TZS. 8,958,967,818.00 na Pemba Tsh. 1,721,920,182.00. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 TZS. 4,632,742,267 kati ya TZS. 10,830,888,000.00 zilitumika sawa na asilimia 43 ambapo wastani wa utekelezaji wa kazi zilizopangwa (physical performance not based on financial weight) ulikuwa wa asilimia 57.

Miradi ya matengenezo ya barabara iliyopangwa kwenye mwaka wa fedha 2019/2020 ilikuwa 12 kati yake miradi minane (8) Unguja na minne (4), kwa upande wa Pemba jumla ya TZS 8,441,591,524.00 zilitengwa kwenye miradi hiyo sawa na asilimia 78 ya bajeti. Aidha, TZS. 2,389,296,476.00 zilitengwa kwa ajili ya kugharimia kazi zinazohusiana na matengenezo ya barabara zilipangwa kwa kipindi hicho sawa na asilimia 22. Hakuna mradi uliofutwa.

Utekelezaji wa miradi ya matengenezo ya barabara iliyopangwa kwenye mwaka wa fedha 2019/2020 kulingana na fedha zilizotengewa hasa kwa miradi iliyopangwa kutekeleza na wakandarasi hazikuweza kutumika kwa sababu ya kuchelewa kwa mchakato wa kuwapata wakandarasi ambapo mikataba ilisainiwa mwishoni mwa robo ya nne, hivyo haikuwa rahisi wakandarasi kulipwa fedha hizo kwa sababu walikuwa kwenye maandalizi (mobilization) na baadhi yao walikuwa wakisubiri malipo ya awali (Advance payment). Miongoni mwa miradi hiyo ni:

1. Matengenezo ya barabara ya Sharifumsa-Mwanyanya-Skuli ya Bububu na Kinduni -Kichungwani-Kitope pamoja na ujenzi. Kwenye mwaka wa fedha 2019/2020 mradi huu ulitengewa kiasi cha TZS 4,765,492,182.00, ambapo mkataba ulisainiwa tarehe 23 Juni 2020;
2. Mradi wa ujenzi wa daraja kasha lenye milango mitatu eneo la Nguli barabara ya Upenja-Kiwengwa ambapo TZS. 726,630,558.20 zilitengwa;
3. Ujenzi wa misingi ya maji ya mvua barabara ya Nyerere (Kiembesamaki-Uwanja wa ndege wa kimataifa wa (AAKIA) zilitengwa TZS. 1,210,000,000.00. Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 26 Juni 2020; na
4. Mradi wa uchoraji wa mistari barabara ya Mazizini-Fumba (km18) ulipangiwa kiasi cha TZS 220,000,000.00 ambapo mkataba ulisainiwa tarehe 26 Juni 2020.

Kwa upande wa miradi iliyopangwa kutekelezwa na watendaji wa Wakala wa Barabara Zanzibar (ZANROADS) ilikuwa minne (4) kwa Unguja na minne (4) kwa upande wa Pemba na miradi minane (8) ya matengenezo mbali mbali ya dharura Unguja na Pemba.

Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2020 miradi miwili (2) ilikuwa haijaanza kutekelezwa kwa sababu fedha ziliingizwa mwishoni mwa robo ya nne. Miradi hiyo ni matengenezo ya barabara ya Mkiang'ombe (3 km) kwa kiwango cha kifusi na matengenezo ya maeneo yaliyoharibika kwa mvua eneo la Raha barabara ya Wete -Gando na Kuungoni barabara ya Wete-Konde.

Aidha, TZS. 700,000,000.00 zilizotengwa kwenye robo ya nne kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Kibonde Mzungu (Daraja la Dkt. Shein)-Jumbi sokoni (1 km) zilikuwa hazijaombwa na Wakala wa Barabara Zanzibar-Unguja kwa sababu fedha zilizoombwa awali zilikuwa hazijamaliza.

Uchunguzi wa Kamati

Katika ufuatiliaji wake, Kamati ilielezwa kwamba miradi hiyo ilitekelezwa kupitia mikataba tofauti ambayo ilikuwa ikifanyiwa marekebisho hususan katika utaratibu wa malipo ya fedha husika kwa Mkandarasi, Kwa mshangao mkubwa, Kamati iliomba ipatiwe nyongeza ya mkataba (addendum) wa ujenzi wa barabara ya Msingini Pemba na kuambiwa upo lakini hadi Kamati inawasilisha ripoti yake leo haijapokea kielelezo hicho. Kutowasilisha kwake kunaitia wasiwasi Kamati kwamba kuna uwezekano wa fedha za umma kutumika isivyotakiwa.

Kutokana na umuhimu wa ukarabati wa barabara, Kamati iligusia pia mambo muhimu yafutayo:

1. Ukosefu wa umadhubuti wa barabara zinazojengwa ambapo hazitumiki muda mrefu huwa zinaharibika na kupoteza fedha za Serikali ikiwemo barabara ya Msingini Pemba.
2. Kukosekana kwa mashirikiano ya karibu baina ya ZAWA na Mfuko wa Barabara kabla ya kuanza na baada ya ujenzi wa barabara. Hali hiyo imebainika wakati wa ujenzi wa barabara ya Msingini Pemba ambapo imedaiwa kuharibika kwa haraka kutokana na kufuja bomba kubwa la maji liliopo pembezoni mwake na kusababisha maji kuingia katika barabara hiyo.
3. Mfuko unakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosa wataalamu wa kutosha jambo ambalo hupelekea barabara nyingi kuharibika muda mchache baada ya matengenezo.
4. Wakandarasi wakubwa barabara huwa hawachukui zabuni za ujenzi wa barabara za Zanzibar kutokana na kuwepo gharama kubwa usafirishaji wa vifaa vyao

ambavyo huwa vinatakiwa vikae eneo husika ambapo vingine vikishatumika mara moja au mbili hutakiwa kwenda sehemu nyengine kwa vile huwa havitumiki tena labda kutokezee maharibiko kama kijiko (grader).

Kwa mnasaba huo, hoja imebakia kama ilivyoelezwa katika ripoti ya Mdhibiti kwani kamati haikuridhishwa na majibu ya Mfuko.

3.9.2 Kukosekana kwa ushahidi wa mapokezi ya vifaa shilingi 134,321,000

Ukaguzi umebaini kuwa Idara ya Ujenzi na Utengenezaji wa Barabara (UUB) iliwalipa wauzaji wa kokoto, mchanga na vifaa vyengine vya ujenzi vyenye jumla ya TZS 134,321,000. Hata hivyo, ukaguzi haukupata ushahidi wa daftari la kumbukumbu la mapokezi ya vifaa hivyo ili kuthibitisha kupokelewa kwa vifaa hivyo. Hii inatokana na kukosekana kwa usimamizi wa mkataba ili kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika kwa vifaa vilivyopokelewa tu.

Kukosekana kwa ushahidi wa mapokezi ya mchanga na kokoto kunaweza kupelekea malipo kufanyika kwa vitu ambavyo havikupokelewa jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 11 ya 2016.

Majibu ya Mfuko

Kwenye bajeti ya matengenezo ya barabara ya mwaka wa fedha 2019/2020, WUMU ilitenga fedha kwa ajili ya kazi za uzibaji wa mashimo barabarani na matengenezo/ujenzi wa barabara za ndani za Taasisi ya Sayansi na Tekinolojia ya Karume kwa kiwango cha lami pamoja na upandishaji wa lami ya kupika kwenye maeneo tofauti ya barabara ya Kiembesamaki-Mnazimmoja. Ili kufanikisha kazi hizo, Wakala wa Barabara Zanzibar ambayo ndiyo mtekelezaji wa kazi hizo ilitumia kiasi cha TZS. 86,600,000 kununua mawe magumu kutoka kwa ndugu Salum Ali Mussa kwa ajili ya kusaga kokoto za miradi iliyotajwa hapo juu.

Kumbukumbu za idadi ya kiwango cha mawe yaliyonunuliwa zilinakiliwa kwenye madaftari na msimamizi wa Kanda ya Kusini na kuhifadhiwa. Aidha TZS. 48,321,000 zilitumika kugharamia mchanga ulioletwa na kampuni ya ZINAMOLA General Traders. Mchanga ulipelekwa Kibele kwenye mitambo ya kupika lami. Wakala wa Barabara Zanzibar imezipatia ufumbuzi Changamoto ya kununua mawe magumu kutoka kwa watu binafsi baada ya kupata kwari yenye mawe magumu huko Kandwi.

Uchunguzi na Pendekezo la Kamati

Pamoja na Kamati huoneshwa kumbukumbu la daftari husika, kwa vile kielelezo hicho ni rahisi kwa watendaji kukiandaa Kamati ya LAAC ilijikita na hoja kwamba kwanini Mkaguzi alipopita hajakiona na kujiridhisha kwamba kuna wasiwasi wa kuwepo

udanganyifu. Hivyo, hoja imebakia kama ilivyo katika ripoti ya Mkaguzi.

3.9.2 Mikataba iliyosainiwa na Wakandarasi walio na leseni zilizomaliza muda na wasio na leseni

Ukaguzi umebaini kwamba WUMU ilisaini mikataba ya ujenzi kwa wakandarasi yenye jumla ya TZS. 282,549,640 ambazo leseni zao za biashara zilikwisha muda na wengine hawakuwa na leseni.

Kutoa zabuni kwa wakandarasi ambao leseni zao za biashara zilikwisha muda na wengine kutokuwa nazo kabisa kunapelekea kutoa zabuni kwa wakandarasi wasio na sifa na ambazo hawajasajiliwa.

Majibu ya Mfuko

Miongoni mwa sifa/vigezo ambavyo Kikundi/Mkandarasi anatakiwa kuwa navyo ili apewe kazi ni pamoja na leseni hai ya biashara. Vikundi na Mkandarasi walioshinda zabuni za matengenezo mbali mbali ya barabara wakati wa kufanya tathimini ya nyaraka zabuni walizowasilisha leseni zao zilikuwa hai na kukidhi vigezo vyote. Leseni ambazo zilimaliza muda wakati wakitekeleza miradi walilazimika kuziongezea muda kwa kuzilipia kwenye taasisi husika na nakla zake kuwasilishwa kwa msimamizi wa miradi Wakala wa Barabara Zanzibar.

Kwa upande wa Unguja kampuni ya Edge Point Company ya Limited ilishinda na kupewa mradi wa uchoraji wa mistari (road marking) barabara ya Mazizini-Fumba (18 km). Wakati wa kufanya tathimini mwezi Aprili 2020, leseni ya biashara ya kampuni hiyo ilimalizika tarehe 5 Julai, 2020. Kutokana na kuchelewa kusaini mkataba wakati wa utekelezaji leseni ilimaliza muda wake na Mkandarasi kulazimika kukata leseni nyengine na kuwasilisha nakla yake kwa Wakala wa Barabara Zanzibar ambayo uhai wake ulianza tarehe 6 Julai 2020.

Kwa upande wa Pemba kampuni ziliyopewa kazi za usafi wa barabara (routine maintenance for paved roads) zilikuwa ni Chake Chake Youth Co. Ltd ambapo leseni yake ilimalizika tarehe 31 Disemba 2019, Kmpuni ya Hifadhi ya Mungu Co. Ltd. nakla ya leseni yake ya biashara, Cleaning Services Co. Ltd, nakla ya leseni yake ya biashara. Bright Security Co. Ltd pamoja na nakla ya leseni yake ya biashara. Renew yake.

Uchunguzi na Pendekezo la Kamati

Kamati ilipokutana na watendaji wa Mfuko ilipatiwa vielelezo vingi vya usajili wa Wakandarasi. Kamati ilifikiria zaidi kwamba kwanini alipopita Mkaguzi ambaye hutumia muda mkubwa kukagua asipatiwe. Aidha, Kamati pia ilihoji kwamba sheria za fedha inazitaka Taasisi tekelezaji mradi kuambatanisha vielelezo vyote kuthibitisha matumizi

ya fedha jambo ambalo halikufanyika na kupelekea Mkaguzi kushindwa kuoneshwa vielelezo husika.
Kwa mnasaba huo, hoja imebakia kama ilivyo kwa vile Kamati haikuridhishwa na majibu ya watendaji wa Mfuko.

3.9.3 Utekelezaji wa kiwango cha chini wa kazi zilizopangwa za matengenezo ya barabara

Makubaliano ya utendaji kazi yaliyoidhinishwa ya tarehe 23 Aprili 2020 kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2020 ilikuwa TZS 3,723,097,000. Ripoti ya kila mwaka kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuwa jumla ya TZS. 859,015,544 zilitumika katika kazi za matengenezo ya barabara ambayo ni sawa na asilimia 23 ya shughuli zilizopangwa.
Aidha gharama za usimamizi zilitumika kwa kiwango cha asilimia 54 na gharama za uendeshaji zilitumika kwa asilimia 100. Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa ushahidi wa wahandisi kutembelea maeneo ya miradi ukaguzi haukupatiwa ushahidi unaothibitisha wahandisi kutembea maeneo ya miradi.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, utekelezaji halisi ulikuwa kwa asilimia 83 lakini hakukupatikana vyeti vya kazi zilizokamilishwa alizopelekewa mkandarasi.

Kuchelewa kutoa vyeti na ushahidi wa kazi iliyofanywa kwa malipo husababisha fedha kutokulipwa kwa mwaka wa fedha husika na kupelekea matumizi hayo kuonekana katika kipindi tofauti cha mwaka wa fedha. Aidha kunapelekea wananchi kukosa huduma za maendeleo kwa wakati.

Majibu ya Mfuko

Utekelezaji wa kiwango cha chini wa kazi zilizopangwa za matengenezo ya barabara:

- Gharama za usimamizi zimetumika kwa asilimia 54 kwani gharama hizo hutumika kuwalipa Wahandisi katika usimamizi na ununuzi wa mafuta kwa ajili ya gari ya Kitengo cha Uhandisi, Gharama hizi hutumika pale tu kama kuna mradi unaendelea.

- Watendaji wa ORTMSMIM kupitia kitengo cha Uhandisi wamekuwa wakiandika ripoti za utekelezaji na kuziwasilisha kwa Katibu Mkuu kwa kila mwezi na kuambatanishwa ripoti hizo pamoja na sheet za muda wa ziada wakati wa usimamizi wa kazi hizo.

- Kwa kawaida vyeti kwa mkandarasi hutolewa katika muda maalum kama ulivyoelezwa ndani ya Mkataba husika. “Site Position Certificate” hutolewa mwanzo wa mradi na vyeti vyengine ambavyo ni ‘Substantial Completion

Certificate' na 'Taking Over certificate' huwasilishwa kwa Mkandarasi atakapomaliza kazi yake au kufikia asilimia iliyoainishwa kwenye mkataba, mpaka tarehe 30 Juni, 2021 hakukuwa na kazi iliyokamilika.

Uchunguzi na Pendekezo la Kamati

Kupitia hoja hii, Wajumbe wa Kamati wao wenyewe walikuwa mashuhuda kwani walieleza kwa undani kwamba inasikitisha na ni aibu barabara inatengenezwa kwa muda mchache na kuanza kufanya mashimo. Lakusikitisha zaidi ni kwamba kuna baadhi ya barabara huondolewa lami yote hususan katika kipindi cha mvua jambo linalothibitisha Mfuko hauna utaalamu wa kazi inazozifanya au wanashindwa kuwasimamia ipasavyo wajenzi. Hivyo, Kamati inaungana na Mkaguzi (CAG) na hoja imebakia kama ilivyo kwa vile Kamati haikuridhishwa na majibu ya watendaji wa Mfuko.

3.9.4 Kukosekana kwa ushahidi wa ukaguzi uliofanywa kwa bidhaa zilizonunuliwa shilingi 86,890,900

Kwa mwaka 2019 UUB Pemba ilinunua bidhaa zenye jumla ya TZS 86,890,900 kutoka kwa wauzaji tofauti, hata hivyo ukaguzi haukuweza kupewa ushahidi kwamba bidhaa zilizonunuliwa zilikaguliwa mara tu baada ya kupelekwa UUB.
Ukaguzi umetia shaka kwamba, bidhaa zinzowasilishwa bila kukaguliwa zinaweza kuwa sio kulingana na mahitaji ya mtumiaji kwa idadi na ubora.

Kutokufanya ukaguzi wa bidhaa mara zinapowasilishwa kwa ajili ya kuhifadhiwa ghalani ni kwenda kinyume na sharia ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma Nam. 11 ya 2016.

Majibu ya Mfuko

Ni kweli kama ukaguzi ulivyobaini, kuwa hakukuwa na Ushahidi wa kimaandishi unaoonesha kuwa bidhaa zilikaguliwa (Inspection Report) hata hivyo kiuhalisia, bidhaa zinazonunuliwa huwa zinakaguliwa na wataalamu kila zinapofikishwa ghalani wakati wa kuzipokea. Hata hivyo kwa sasa, Wakala wa Barabara wameshaandaa utaratibu wa kuunda "inspection team" kwa ajili kukagua bidhaa zinazonunuliwa na kuandaa ripoti ya ukaguzi (inspection report).

Uchunguzi na Pendekezo la Kamati

Hoja imebakia kama ilivyo kwa vile Kamati haikuridhishwa na majibu ya watendaji wa Mfuko.

3.10: SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)

Taarifa ya Mapato

Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020 limepangiwa kukusanya jumla ya Tsh. 1,500,000,000.00 kutoka katika vyanzo vyaka vya ndani na kutarajiwa kupata Tsh. 4,120,900,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka katika mfuko mkuu wa Serikali.

Hadi kufikia tarehe 30 June, 2020 jumla ya Tsh. 793,735,630.94 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ambayo ni sawa na asilimia hamsini na mbili nukta tisa (52.9) ya makadirio na kupata Tsh. 3,441,852,125 ambayo ni Ruzuku kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ambayo ni sawa na 83.5 ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Ni kweli kwamba katika mwaka huo wa fedha Shirika hili lilikusanya kiwango hicho cha fedha kupitia vyanzo vyake kama ifuatavyo:

Nam.	Chanzo cha Mapato	Makadirio	Mapato halisi	Asilimia ya Mapato
1.	Ruzuku kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali	4,120,900,000	3,441,852,125	83.5%
2.	Makusanyo ya vyanzo vya ndani	1,500,000,000	793,735,630.94	52.9%
Jumla		**5,620,900,000**	**4,235,587,755.94**	**75.4%**

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalijitokeza:

1. Kamati ya ilitaka kujua sababu zilizopelekea Shirika hili kushindwa kufikia malengo iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2019/2020, ambapo, ilielezwa kama ifuatavyo:
    a. Shirika lilipendekeza kukusanya jumla ya Tsh. 800,000,000, hata hivyo, Wizara inayohusiana na masuala ya Fedha ililitaka kukusanya Tsh. 1,500,000,000 kiwango ambacho hakiendani na uhalisia wa vianzio vyake vya mapato.

b. Shirika halikurusha vipindi vingi kwa njia ya mubashara “live” kutokana na maradhi ya uviko 19. Hii ni kutokana na kuwa watu wengi walishindwa kutoa mashirikiano kutokana na masharti yaliyowekwa juu ya maradhi hayo. Vipindi vinavyorushwa kwa njia hii ndio vyenye tija zaidi.
c. Shirika lilishindwa kuwafikia Washirika wao wa maendeleo kwa ajili ya kufanya “lobbing” kutokana na maradhi ya uviko 19.

2. Taarifa za Hesabu za Mapato na Matumizi zilizoelezwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani wa Shirika zimetofautiana na taarifa zilizoelezwa kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) ya Shirika.
3. Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani wa Shirika ilikuwa haiwasilishwi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama kifungu cha 117(6) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kinavyoelekeza.
4. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikuwa haifanyii kazi taarifa ya Mkaguzi wa Ndani wa Shirika kwa kuwa taarifa yake ilikuwa haijadiliwi kwenye Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya Shirika.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro zilizobainika Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Kitengo cha Mapato ihakikishe kuwa inavifanyia uhakiki vianzio vya ndani vya mapato vya kila Taasisi kabla ya kuzipangia kiwango cha kukusanya ili kuepusha malalamiko yasiyo ya lazima sambamba na kutozitia dosari Taasisi hizo kwa kuonekana kuwa hazikufikia malengo.
2. Wakaguzi wa Ndani wa Taasisi mbali mbali wahakikishe kuwa wanaziwasilisha taarifa za ukaguzi za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama Sheria ya Fedha inavyoelekeza.
3. Wakaguzi wa Ndani wa Taasisi mbali mbali wahakikishe kuwa taarifa za fedha wanazozieleza kwenye taarifa zao zimetolewa na mtendaji au chanzo sahihi ili kuwa na taarifa zinazofanana katika Taasisi moja.
4. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali azichukulie hatua Taasisi zote ambazo haziwasilishi taarifa za ukaguzi wa ndani kama Sheria inavyoelekeza.

Taarifa ya Matumizi

Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha Tsh. 5,620,900,000 kwa kazi za kawada pamoja na mishahara. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020, Shirika limeingiziwa Tsh. 4,181,912,094.49 ambayo ni sawa na 74.4% ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Ni kweli kwamba katika mwaka wa fedha husika Shirika hili lilitumia jumla ya kiasi hicho cha fedha ikiwa ni upungufu wa Tsh. 1,438,987,906.51 ambayo ni sawa na 25.6% ya makadirio.

Upungufu huo umeleta usumbufu kwa baadhi ya kazi kutokamilika kwa wakati. Kazi zenyewe ikiwemo:

(v) Ukarabati wa minara;
(vi) Ukarabati wa baadhi ya majengo na ofisi za Shirika;
(vii) Ukarabati wa uzio wa Masingini;
(viii) Upatikanaji wa hatimiliki kwa baadhi ya maeneo ya Shirika.

Pamoja na upungufu huo, Shirika liliweza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mpango kazi wake ili kukwepa kuachwa nyuma katika ushindani wa soko la habari ambalo kwa sasa limevamiwa na vyombo vingi vya habari.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalibainika:

1. Umoja wa Maaskari Wastaafu (UMAWA) walifunga mkataba na Shirika hili kwa kazi ya ulinzi kwa thamani ya Tsh. 35,280,000. Hata hivyo, Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka inaonesha kuwa matumizi yaliyofanywa kwa mwaka huo ni Tsh. 46,576,517. Hii ni kutokana na kuwa Shirika hili lilikuwa linadaiwa na Umoja huo katika mwaka uliopita. Hivyo, kwa kuwa Shirika linafunga hesabu zake kwa kutumia mfumo wa “Cash” imebidi malipo hayo yajumuishwe pia kwenye taarifa hiyo.
2. Watendaji wa Shirika hawaelewi sababu iliyopelekea Umoja huo ukawa unalidai Shirika hili hasa ikizingatiwa kuwa fedha za ulinzi zilipaswa kulipwa kwa mujibu wa masharti yaliyoelezwa kwenye mkataba huo.
3. Baadhi ya matumizi hufanyika kila mwaka isipokuwa kwamba, Shirika halitengi bajeti kwa ajili ya shughuli hizo. Kwa mfano; Tukio la kusherehekea mwaka.
4. Kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC ililishauri Shirika kutenga bajeti kwa kila shughuli ambayo inatekelezwa ndani ya Shirika hilo ili kuepuka kuwa na dhana mbaya juu ya matumizi inayoyafanya.

3.10.1 Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani

Kwa mujibu wa kifungu cha118(1) cha Sheria ya fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, inataka kila Taasisis inayohusika na bajeti ya Serikali kuwa na Kamati ya Ukaguzi

wa Ndani itakayoteuliwa na Afisa Mhasibu kwa kushauriana na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Utangazaji Zanzibar halina Kamati ya Ukaguzi wa Ndani.

Kukosekana kwa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kunapelekea kutokuwepo kwa chombo kitakachosimamia na kuleta mawasiliano ya vihatarishi na kutoa taarifa kwenye maeneo husika kwa Shirika pamoja na kutoa ushauri kwa Afisa Mhasibu juu ya hatua za kuchukuliwa kutokana na mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti ya ukaguzi wa ndani au kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali.

Majibu ya Shirika

Shirika la Utangazaji Zanzibar tokea kuanzishwa kwake lilikuwa likitumia Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo. Kamati hiyo ilitumika kutokana na kukosekana kwa Kamati ya Shirika. Hali hii ilitokana na kuchelewa kukamilika kwa muundo wa Shirika ambao hadi kufikia Juni, 2020 baadhi ya Wakurugenzi wa ndani walikuwa bado hawajateuliwa na baadhi ya walioteuliwa kuchelewa kuthibitishwa na Ofisi ya GSO. Kwa sasa Shirika linayo Kamati yake ya ukaguzi wa ndani ambayo inaendelea na majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha ili kuimarisha usimamizi wa ndani.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Shirika hasa ikizingatiwa kuwa Shirika hili liliundwa tangu mwaka 2013 hivyo, Kamati hiyo ilipaswa kuundwa tangu mwaka huo ili kuheshimu matakwa ya Sheria husika. Vile vile, kutokukamilika kwa muundo wa Shirika hakuzuwii Shirika hili kushindwa kuunda Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kwa kuwa Wakurugenzi waliokuwa hawajateuliwa hawahusiki moja kwa moja na Kamati hiyo. Kwa mnasaba huo, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

3.10.11 Mapungufu katika matumizi ya mafuta ya Shilingi 151,517,080

Ukaguzi ulipitia taarifa za usimamizi wa mafuta na kufanya ulinganisho wa rekodi zilizo kwenye madaftari la kuhifadhia kumbukumbu za mafuta.

Jumla ya shilingi 151,517,080 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta, malipo ambayo yalilipwa kwa wasambazaji wa kampuni ya United Group Limited shilingi 133,517,080 na shilingi 18,000,000 kutoka Zanzibar Petroleum kwa ajili ya matumizi ya Shirika. Aidha, ukaguzi umebaini kujitokeza kwa mapungufu mbali mbali ya kiutendaji katika uwekaji wa kumbukumbu za mafuta hayo, kasoro zenyewe ni kama hizi zifuatazo:

-

1. Kutokuwepo kwa daftari la kuonyesha mapokezi na matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa na Shirika.
2. Kutokuwepo na taarifa za ulinganishaji wa kumbukumbu za matumizi ya mafuta katika daftari la kurikodiwa mafuta ya Shirika na Kampuni ya Mafuta ili kuweza kuangalia taarifa za usuluhishi wa mafuta.
3. Kukosekana kwa mkataba wa manunuzi baina ya Shirika na Kampuni ya Mafuta.

Matumizi ya mafuta kwa Shirika yanagharimu fedha nyingi sana, hivyo basi, kutakuwa na uwekaji na utunzaji mzuri wa kumbukumbu za mafuta huweza kupelekea mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, kutokuwepo kwa taarifa za usuluhishi wa mafuta yaliyonunuliwa na kutumika kulipelekea kushindwa kutambua matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa matumizi yasiyofaa ya mafuta.

Katika kufuatilia hoja hizi yafuatayo yalijitokeza:

1. **Kutokuwepo kwa daftari la kuonyesha mapokezi na matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa na Shirika**

Majibu ya Shirika

Shirika la Utangazaji Zanzibar lilitumia fedha hizo kwa ununuzi wa mafuta kwa kazi za Shirika. Kazi hizo zikiwemo kazi za utafutaji na ufuatiliaji wa habari na kurusha matangazo ya moja kwa moja kwa kazi za Serikali kutoka katika maeneo tofauti Unguja na Pemba. Katika kutunza kumbukumbu za uingizaji na utoaji wa mafuta Shirika lilitumia daftari maalum kwa ajili ya udhibiti wa mafuta. Daftari hilo lilikuwa na mapungufu katika rekodi zake.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea Shirika hili kutokuwa na daftari hilo katika mwaka huo wa fedha, ambapo Watendaji wa Shirika waliieleza Kamati hii kuwa daftari lilikuwepo isipokuwa kwamba, katika daftari hilo kulikuwa na mapungufu mbali mbali kutokana na kutokuwepo kwa Mtunza Ghala kwa wakati ule.

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu hayo, kwa kuwa wakati Kamati hii inafuatilia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2017/2018 tarehe

13 -14 Januari, 2021 ilihoji kuhusiana na daftari la kutunzia mali ambapo, Shirika hili liliieleza Kamati kuwa mapungufu yaliyobainika kwenye daftari hilo yalijitokeza kwa kuwa Shirika halina Mtunza Ghala, hata hivyo, tayari Shirika limeshaomba mtendaji huyo kunakohusika.

Sambamba na maelezo hayo, Kamati ya LAAC ilitaka kujiridhisha na maelezo ya Shirika kwa kulikagua daftari hilo ambapo, Shirika liliipatia Kamati ya LAAC daftari hilo na kulikagua. Cha kushangaza wakati Mdhibiti anafanya ukaguzi wake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 daftari hilo hakupatiwa na kuandika hoja hiyo kama inavyojieleza.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea Watendaji wa Shirika wasimpatie daftari hilo Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alivyofanya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2019/2020 wakati daftari hilo lilikuwepo. Vile vile, Kamati ilitaka kujua Mtunza Ghala huyo alianza lini kazi katika Shirika hilo?.

Watendaji wa Shirika hawakuwa na majibu juu ya maswali yote hayo ya Kamati, hali hii ilipelekea Kamati hii kuwa na mswali mbali mbali juu ya Watendaji wa Shirika na hata ilidiriki kuwaambia kuwa inawezekana waliipatia Kamati daftari hilo lilipofika ofisini hapo tarehe 13 -14 Januari, 2021 wakifikiria kuwa Kamati hiyo haina uweledi juu ya suala hilo na Afisa wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yeye hakupewa kwa kuwa ni mtaalamu na anaweza kutoa dosari mbali mbali ndani ya daftari hilo.

Vile vile, Kamati ya LAAC baada ya kulipitia daftari hilo ilibaini yafuatayo:

iv. Baadhi ya gari huingiziwa mafuta kila siku tena kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano; gari yenye namba ya usajili SMZ 475B iliingiziwa mafuta katika mtiririko ufuatao:

Namba	Tarehe	Idadi ya Litre
1.	10/03/2020	30
2.	11/03/2020	40
3.	12/03/2020	30
4.	13/03/2020	30

v. Hakuna “log book” lililothibitisha matumizi ya gari hiyo, hali hii ilizidi kuitia mashaka Kamati juu ya matumizi ya mafuta ya gari hii.

vi. Shirika huingiza mafuta kwenye gari za Watendaji wake jambo ambalo ni kinyume na utaratibu. Hata hivyo, Shirika liliieleza Kamati kuwa hali hiyo

imefikiwa kutokana na tatizo la uhaba wa gari lililokuwa linalikabili Shirika hili.

vii. Kamati haikuona taarifa za utokaji wa mafuta kutoka tarehe 14 Machi, 2020 hadi tarehe 06 Mei, 2020.

Kiujumla Kamati ya LAAC haikupendezewa na hali hiyo na iliwataka Watendaji wa Shirika kutekeleza majukumu yao vyema pamoja na kumheshimu mtu yeyote anayefika ofisini hapo.

2. **Kutokuwepo na taarifa za ulinganishaji wa kumbukumbu za matumizi ya mafuta katika daftari la kurikodiwa mafuta ya Shirika na Kampuni ya Mafuta ili kuweza kuangalia taarifa za usuluhishi wa mafuta**

Majibu ya Shirika

Kampuni ya United Group LTD haina utaratibu wa kutoa '*Statement*' ya mafuta jambo ambalo lilipelekea Shirika hili kushindwa kufanya upatanisho (reconciliation) wa matumizi mafuta. Kutokana na hali hiyo, Shirika liliamua kuchukua mafuta katika Kampuni ya United Group LTD.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC ililishauri Shirika hili kabla ya kuingia mkataba na mtu mwengine kufanya utafiti wa kina juu ya utendaji wa mtu huyo ili kuepuka usumbufu usio wa lazima pamoja na kuweza kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za nchi.

Kamati ya LAAC haikuwa na maelezo zaidi na kutokana na majibu ya Shirika hoja hii imebaki kama ilivyo.

3. **Kukosekana kwa mkataba wa manunuzi baina ya Shirika na Kampuni ya Mafuta**

Majibu ya Shirika

Kwa upande wa mikataba na watoa huduma, Shirika lilikuwa likichukua mafuta yake kutoka katika Kampuni ya United Group LTD ambapo baada ya kuona Kampuni hiyo haitoi '*Statement*' ya mafuta kwa ajili ya kufanya upatanisho (reconciliation) wa matumizi mafuta. Uongozi wa Shirika uliamua kuhama kwenye Shirika hilo na kuanza makubaliano mapya na Kampuni ya Zanzibar Petroleum.

Kampuni hiyo ina utaratibu wa kutoa mikataba kwa wateja, lakini hadi kufikia Juni, 2020 Kampuni ya Zanzibar Petroleum walikuwa hawajatoa mkataba wa kazi hiyo kwa Shirika. Kwa sasa, Shirika linaendelea na mkataba wa mafuta na Kampuni ya Zanzibar Petroleum katika Kituo kilichopo Kijangwani.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikuwa na maelezo zaidi juu ya majibu ya Shirika na kutokana na majibu ya Shirika, hata hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

3:11: SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC) - UNGUJA
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2019/2020

Kamati ilifika Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) tarehe 10 Agosti, 2021 kufuatilia hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lakini haikufanikiwa kutekeleza majukumu yake kutokana na kugundua kwamba taarifa ya fedha iliyokabidhiwa Kamati hailingani na taarifa kama hiyo iliyowasilishwa na SHirika katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hili lilisababishwa na Shirika kuipatia Kamati taarifa ya fedha iliyorekebishwa taarifa zake na kuwasilishwa kwa Mdhibiti kinyume na muda ulitakiwa kisheria badala ya ile aliyoifanyia ukaguzi Mdhibiti.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati pia iligundua kwamba mapato na matumizi yaliyoainishwa katika taarifa mbili hizo zilikuwa zikitofautiana hali ambayo Shirika liliiomba Kamati ipangiwe siku nyengine ili kurekebisha kasoro hizo. Hivyo, Kamati ilikutana tena na Shirika tarehe 13 Septemba, 2021.

Taarifa ya Mapato

Shirika la Nyumba Zanzibar lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,035,000,000 kwa mwaka 2019/2020 ambapo hadi kufikia Juni, 2020 Shirika hilo limekusanya jumla ya shilingi 2,091,811,601.41 sawa na asilimia 68.92 ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Shirika halikuweza kufikia lengo la makusanyo kutokana na kuwepo kwa janga la Uviko 19 lililoathiri wapangaji wao wakubwa kusimamisha biashara zao kwa kipindi hicho, na kuomba kuchelewesha kulipa Kodi. Miongoni mwa wateja walioomba kusogezwa mbele kwa kipindi cha miezi mitatu madeni yao ni pamoja na Hoteli ya Serena na Emerson. Kwa wakati ambao Kamati inafanya ukaguzi, Wadaiwa hao tayari walikuwa wameshalipa madeni yao.

Shirika pia lilizuiliwa kutumia Sheria inayoruhusu kumtumia Dalali wa Mahakama (KUMEKUCHA) kwa kuwatoa wadaiwa sugu katika nyumba zao. Shirika lilieleza kwamba kufuatia kikao kilichofanyika tarehe 16 Mei, 2019 baina ya aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati Mheshimiwa Salama Aboud Talib, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Waziri huyo aliiagiza Bodi kutomtumia Dalali huyo badala yake kutumia njia mbadala ya kuondoa changamoto hiyo.

Kuhusu vyanzo vyao vikuu vya mapato, Shiriki linategemea kupata mapato yake kupitia vyanzo vinne vya kodi, mikataba, faini na vyanzo mbalimbali.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya LAAC kufuatia maelezo na vielelezo ilivyokagua, ilibaini kwamba pamoja na sababu zilizoelezwa na Shirika za kutofikia lengo la makusanyo ililojipangia, kuna sababu nyengine ya kutokuwepo uelewa na utayari wa wapangaji kunakotokana na Shirika kushindwa kuziendeleza nyumba hizo kwa kuzifanyia mategenezo muda baada ya muda hali iliyopelekea nyumba nyingi kuchakaa na kuanguka na kupelekea hasara ya kukosa mapato stahiki Shirika.

Aidha, Kamati ilibaini kwamba kuna vyanzo vyengine vya Ushauri Elekezi na Ujenzi wa nyumba ambavyo Shirika bado halijaanza kuvifanyia kazi. Vyanzo hivyo ni muhimu na iwapo Shirika itajipanga vizuri na kuvitekeleza ipasavyo, inaweza kuongeza mapato yake maradufu.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kamati ya LAAC imelitaka Shirika kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha inazifanyia matengenezo nyumba zao ili kupunguza uchakavu na uharibifu wa nyumba hizo. Kufanya hivyo, kutalisadia Shirika kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato yake na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

2. Shirika liendelee kufuatilia kwa karibu madeni inayodai kwa wapangaji wake ili kukuza pato la Shirika na kutoa huduma zinazoendana na hadhi yake.

Taarifa ya Matumizi

Kwa mwaka 2019/2020, Shirika lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,011,062,790 kwa matumizi ya kawaida ambapo hadi kufikia Juni, 2020 Shirika limetumia jumla ya shilingi 1,980,203,734 ambazo ni sawa na asilimia 65 ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Matumizi ya Shirika yameonekana kupungua kiwango kilichokadiriwa kutumia kutokana na baadhi ya hatua za kiutendaji zinazoshirikisha Mamlaka na Taasisi nyengine hayajafanyika kwa wakati kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mamlaka aHifadhi na Usimamizi wa Mji Mkongwe.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Baada ya Kamati kupitia taarifa ya ufungaji wa Hesabu za mwisho wa mwaka wa 2019/2020 ya Shirika, iligundua kwamba taarifa za matumizi za Shirika zinatofautiana

na zile zilizomo ndani ya taarifa ya fedha, Watendaji wa Shirika walieleza kwamba matumizi waliyowasilisha yalieleza uhalisia uliopo (cash basis) wakati taarifa za fedha zilijumuisha na uchakavu wa mali zinazomilikiwa na Shirika "depreciation". Kutokana na hali hiyo, Kamati ililishauri Shirika wanapofunga Hesabu zao za mwisho wa mwaka (Final account) zioneshe na uchakavu wa mali zao ili ukaguzi upate kuona uhalisia wa mtaji na rasilimali za Shirika na vipi watakavyoweza kuzitumia.

Aidha, Kamati ilibaini kwamba kuna uchakavu wa majengo ya Shirika (depreciation and amortization) na fedha za uwekezaji hazikutofautishwa na Shirika katika ufafanuzi wa fedha za Shirika (Note) badala yake zimeunganishwa katika nambari moja (Note 09). Kufanya hivyo, ni kwenda kinyume na taratibu za mifumo ya Uhasibu ya ufungaji wa Hesabu za kitaifa na kimataifa ambzo zinaelekeza vitu hivyo tofauti viainiswe tofauti. Kamati ilishauri uchanganuzi wa vitu viwili visivyolingana kila moja iwe inajitegemea.

Sambamba na hilo, Kamati iligundua kwamba kuna nyumba za maendeleo za Shirika ziliopo Michenzani ambazo zimeungana na nyumba zinazomilikiwa na watu binafsi zimefanyiwa matengenezo kwa fedha za Shirika bila ya wananchi hao (wamiliki binafsi) kuchangia gharama yoyote. Jambo hilo linapunguza uwezo wa wa Shirika kuwa na fedha za kutosha za kuzifanyia matengenezo nyumba zake nyingi zilizopo katika maeneo tofauti ambazo bado zinaonekena kuwa katika hali mbaya ya uchakavu.

Kuepuka kujitokeza tena changamoto kama hiyo, Kamati ililishauri Shirika kuanzisha sera na mpango maalum wa kuzifanyia matengenezo nyumba zake na zile zinazomilikiwa na watu binafsi ili ziweze kuwa na mazingira mazuri yanayoendana na hadhi ya nyumba za Serikali.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.11.1 Kuripotiwa kwa mapato pungufu ya shilingi 586,000,000

Ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umebaini taarifa ya fedha ya mwisho wa mwaka haikujumuisha sehemu ya mapato yatokanayo na kodi ambazo huduma ilikwishatolewa na Shirika lakini fedha hazikuweza kukusanywa mpaka kufikia mwisho wa mwaka. Jumla ya shilingi 2,617,841,101.4 zilipaswa kukusanywa na Shirika lakini jumla ya shilingi 2,031,841,101.4 ndizo zilizooneshwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka na kuwepo tofauti wa shilingi 586,000,000 ambazo hazikurikodiwa katika taarifa ya hesabu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti.

Majibu ya Shirika

Menejimenti ya Sherika imekiri kwamba haikuripoti makusanyo yasiyopokelewa kama mapato (receivables) lakini baada ya ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Menejimenti imekubali na kuripoti mapato yote kama inavyotakiwa na viwango vya kimataifa vinavyoongoza uandaaji wa hesabu.

Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati iligundua kwamba Shirika lilifanya marekebisho katika ripoti yake ya fedha baada ya kupata maoni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lakini walichelewa kuwasilisha majibu yao ndani ya wakati unaotakiwa kisheria. Kamati ilipatiwa barua inayotoka Ofisi ya Mdhibiti inayoeleza kwamba Shirika lilipelea majibu ya maoni yaliyotolewa na Mdhibiti wakati tayari ameshaanza kuandaa kitabu ha ripoti yake.

Kwa vile Shirika lilikiri kufanya makosa ya kutofuata taratibu za sheria za kimataifa za uaandaji na ufungaji wa hesabu kwa Taasisi za Umma (IPSAS). Kamati imelishauri Shirika wanapofanya marekebisho ya taarifa zao za fedha kulingana na maoni yaliyowasilishwa kwao kupitia ripoti ya awali ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, wahakikishe wanafanya marekebisho hayo ndani ya wakati unaotakiwa kisheria (mwezi mmoja baada ya ukaguzi) ili hoja hiyo ifutwe na isiweze kuonekana katika kitabu cha ripoti ya mwisho Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

3.11.2 Ufanisi katika uendeshaji wa Shirika la Nyumba.

Ukaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umebaini kwamba makusanyo yanayotokana na kodi za nyumba na vyanzo vyengine yameshuka kutoka shilingi 2,878,682,812.3 kwa mwaka 2019 na kufikia shilingi 2,091,811,601.14 kwa mwaka unaoishia Juni, 2020 ikiwa na tofauti ya shilingi 786,871,210.90 sawa na asilimia 10.8.

Aidha, Shirika limeendelea kujiendesha kwa hasara kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo pamoja na kwamba hasara hiyo imepungua kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2020 ukilinganisha na mwaka wa fadha ulioishia Juni 2019.

Majibu ya Shirika

Shirika limekiri kwamba ni kweli makusanyo yameonekana kupungua kutoka mwaka 2019 ukilinganisha na mwaka 2020. Hali hiyo, imesababishwa na kuwepo kwa janga la Uviko 19 (Covid 19) lililopelekea baadhi ya wateja wao wakubwa wanaojishughulisha na biashara ya utalii waliomba kusogezwa mbele muda wa kulipa deni lao la kodi la mwaka unaofuata. Mfano wa hoteli hizo ni Serena na Emerson.

Shirika iliwakubalia ombi hilo na kuhakikisha wanalipa deni lao kama walivyokubaliana kulingana na maombi ya barua husika ambapo wote walikamilisha kulipa madeni yao pasi na kujitokza usumbufu wowote.

Sababu nyengine ya kupungua kwa mapato ya Shirika ni kuongezeka kwa wadaiwa sugu hususan wanaokaa katika nyumba zao.

Kuhusu suala la kujiendesha kihasara, watendaji wa Shirika walieleza kiuhalisia Shirika

lao halikujiendesha kihasara kwani kiasi cha hasara kinachoonekana katika taarifa ya fedha za mwisho wa mwaka (Financial Statements) yanatokana na matumizi ambayo uhalisia wake hautumii fedha taslimu (non - cash transactions). Kwa mfano, hasara iliyotokana kupungua thamani na uchakavu wa majengo pamoja na kupungua thamani ya samani ya mali za Ofisi kunakotokana na uchakavu wake (depreciation).

Kiufupi, Shirika limekanusha kuhusu hoja ya kujiendesha kihasara kwa maelezo kwamba ukaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umethaminisha upungufu wa thamani ya majengo kutokana na uchakavu wake lakini haukuzingatia thamani halisi ya ardhi ambayo mali hiyo ilipo. Watendaji wa Shirika walieleza kwamba wanazo mali nyingi zinazopatikana katika maeneo ya mjini ambayo thamani halisi ya ardhi huwa inaongezeka kila baada ya muda kupita. Hivyo, kama ukaguzi ungezingatia thamani halisi ya ardhi pamoja na mali iliyopo juu ya ardhi hiyo, hakutoonekana kuwepo kwa hasara katika uendeshaji wa Shirika.

Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati

Ukaguzi wa Kamati umebaini kwamba kuna mali nyingi za Shirika hususan nyumba ambazo zipo katika hali mbaya inayotokana na uchakavu wa kutofanyiwa matengenezo kwa wakati na kwa muda mrefu. Hali hiyo husababisha upungufu wa mapato na uwezo wa Shirika kumudu kujiendesha ipasavyo. Sambamba na hilo, malalmiko kwa wakaazi wanaoishi katika nyumba hizo hudai kwamba kodi wanayolipa haina thamani halisi ya huduma inayopatikana katika nyumba hizo.

Kamati ilikubliana na hoja ya Mdhibiti kuhusu Shirika kujiendesha kibiashara na kulishauri Shirika kwamba iwe na mpango mzuri wa kuzifanyia matengenezo nyumba zake ili ziendane na wakati, ziongeze tija (kodi) pamoja na kutoa taswira halisi kwamba kweli nyumba hizo zinazomilikiwa na Serikali.

SHIRIKA LA NYUMBA - PEMBA

3.11.3 Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 2,243,400

Ukaguzi ulibaini kwamba jumla ya shilingi 2,243,400 zilitumiwa na Shirika kununlia vifaa mbali mbali lakini hazikuripotiwa katika daftari la ghalani. Vifaa na gharama zake ni shilingi 1,425,000 zilitumika kwa ajili ya ununuzi APC Back Up, shilingi 666,500 kwa ununuzi wa Tangi la maji, zulia, busati, feni na ndoo za maji na shilingi 151,000 kwa ununuzi wa vifaa vya usafi

Majibu ya Shirika

Menejimenti ya Shirika imekiri kwamba kulikuwa na kasoro za kutorikodiwa kwa wakati kwa vifaa vilivyonunuliwa na havikuwekwa katika daftari la ghalani. Hali hiyo, imetokana na upungufu wa wafanya kazi. Hata hivyo, Shirika tayari limeshachukua hatua kwa kumuweka mfanyakazi maalum anayeshughulikia ghala ambaye tayari ameshaviorodheshakatika vifaa hivyo katika daftari hilo. Kutokana na upungufu wa wafanyakazi, Shirika lilimuhamisha mfanyakazi aliyekuwa akifanyakazi za tarishi kuwa Mtunza ghala baada ya kumpatia mafunzo yaliyomuwezesha kumudu kutekeleza kazi zake.

Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati

Pamoja na Watendaji wa Shirika kukiri kwamba kulikuwa na mapungufu yaliyojitokeza na tayari wameshamuweka mfanyakazi kurekebisha kasoro hizo. Kamati imegundua kwamba mfanyakazi huyo bado hajabadilishwa kada ya Mtunza ghala (nafasi anayoifanyia kazi) suala ambalo linaenda kinyume na taratibu za kiutumishi.

Kamati ililishauri Shirika ama lifuatilie Tume ya Utumishi Serikalini ili liweze kumbadilisha kada mtumishi huyo kutoka Tarishi kuwa Mtunza ghala au kuhamisha Mtunza ghala kutoka katika Taasisi nyengine za Serikali na kumuhamishia katika Shirika kuendelea na majukumu yake.

3.11.4 Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslim shilingi 1,430,000

Jumla ya shilingi 1,430,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika. Ukaguzi umebaini kuwa malipo hayo yamefanywa kwa njia ya fedha taslim ambapo ni kinyume na taratibu za malipo. Mchanganuo wa vitu vilivyotumika kwa fedha taslim ni malipo ya mwanzo ya matengenezo ya nyumba Nam. 31A, B na 17 zilizopo Wete (shilingi 550,000), fedha za gharama ya matengenezo ya nyumba iliyopo Madungu (shilingi 480,000) na malipo ya fedha za mwisho kwa ajili ya matengenezo ya nyumba Nam. 31A, B na 17 ziliopo Wete (shilingi 400,000).

Majibu ya Shirika

Shirika lilikubaliana na hoja hiyo na kueleza kwamba hali hiyo ilisababishwa na mambo yafuatayo:

- Ofisi ilikuwa inawatumia mafundi wadogo kwa matengenezo madogo madogo ya nyumba zake;
- Matengenezo hayo yalikuwa yanafanyika kuhami hali ya dharura zilizokuwa zikijitokeza;
- Malipo hayo yalilipwa kwa mafundi tofauti na kwa kazi mbali mbali; na

- Wakandarasi walikuwa hawakubali kazi zenye kiasi kidogo cha fedha ambao malipo yao huwa yanalipwa kwa hundi.

Aidha, watendaji wa Shirika waliihakikishia Kamati kwamba kasoro zilizogundulika za ulipaji wa fedha taslim hazitojikeza tena na kwa kipindi ambacho kamati ililitembelea Shirika hilo, malipo yote yalikuwa yakifanywa Benki.

Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati

Kwa vile Watendaji wa Shirika walikubali kwamba walifanya makosa ya kutofuata taratibu za malipo kwa kuruhusu fedha za Shirika kulipwa kwa fedha taslim (Cash payment) badala ya kutumia Benki. Kutokana na umuhimu wa malipo ya fedha kupitia benki ambapo Serikali hupata mapato na huhakikisha usalama katika uhifadhi na matumizi ya fedha za Serikali, Kamati ililishauri Shirika kuwa na utaratibu wa kutumia 'sub voucher' ambapo fedha tayari zitakuwa zimeshapitia benki baada ya kuidhinishwa na Bodi kupitia kanuni zao za fedha (financial regulations).

Utaratibu huo utaisaidia Shirika kuweza kuwa na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli ndogondogo zinazohitaji kurekebishwa kwa haraka hadi hapo Serikali itakapoweka utaratibu mwengine wa matumizi ya fedha kwa mambo makubwa yanayojitokeza hafla (emergency) bila kuwemo ndani ya mpango wa Shirika.

Hoja namba 3.11.5 Malimbikizo ya madeni ya wapangaji wa nyumba za Shirika shilingi 235,867,500

Shirika la Nyumba - Pemba linadai jumla ya shilingi 235,867,500 zinazotokana na ukodishaji wa nyumba zake za maendeleo na milango ya biashara. Kati ya hizo deni la jumla ya shilingi 75,519,000 linadaiwa kwa Wizara ya Afya na watu binafsi katika eneo la Chake chake, jumla ya shilingi 10,238,500 kwa Katibu wa CCM Mkoa, Mfanyabiashara, katibu wa UVCCM, na watu binafsi wanaopatikana katika Wilaya ya Mkoani, jumla ya shilingi 116,540,000 zinadaiwa kwa KMKM, Wafanyabiashara na Watu binafsi waliopo katika Wilaya ya Wete wakati jumla ya deni la shilingi 235,867,500 linadaiwa kwa ZIPA, Uhamiaji, Katibu wa CCM Micheweni, Usalama wa Taifa na Watu binafsi katika WIlaya ya Micheweni.

Majibu ya Shirika

Shirika lilikiri kuhusu kuwepo kwa malimbikizo ya deni hilo kwa kipindi hicho, ila Shirika limeshaanza kuchukua hatua mbali mbali kuhakikisha madeni hayo yanalipwa na kupungua. Hatua zenyewe ni:

- Kutoa elimu kwa wapangaji wake na jamii kwa ujumla kupitia Redio, Televisheni,

Baruapepe ya Shirika, Magazeti, Mitandao ya kijamii, Mikutano mbali mbali na wapangaji na kubandika katika mbao za matangazo kuhusu ulipaji kodi.

- Kuwaandikia barua za ukumbusho wa kulipa deni, kutuma ujumbe mfupi wa simu za mkononi, kutoa notisi ya kufuta Mkataba wa upangishwaji, kufungwa kwa milango ya biashara na nyumba pamoja na kumtumia dalali wa Mahakama kwa ajili ya kuwatoa wadaiwa sugu.

- Kwa upande wa Taasisi za Serikali zinazodaiwa, Shirika limeziandika barua Taasisi husika na kupeleka orodha ya madeni Wizara ya Fedha na Mipango ili zilipwe moja kwa moja kupitia kasma zao. Aidha, Shirika linakabiliwa na changamoto ya kuwepo kwa madeni yasiyolipika ambayo huikosesha mapato makubwa Serikali. kwa mfano, kuhamishwa kwa wafanyakazi katika Jumba la Treni kumelikosesha Shirika jumla ya shilingi zaidi ya milioni 80 kwani wapangaji wao waliondoka na madeni yao.

Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika ukaguzi wa hoja hii, Kamati iligundua kwamba Shirika inazo nyumba nyingi zilizochakaa hususan za vijijini ambazo ushughulikiaje wake huhitaji gharama kubwa kutokana na matengenezo yanayohitajika; kuna nyumba zinaonekana zinamilikiwa na Serikali lakini wanakaa watu binafsi; kuna utaratibu wa kuuza nyumba zinazopatikana maeneo tofauti kwa bei ya aina moja; na kwa vile Shirika lina sehemu mbili kiutendaji (Unguja na Pemba) kuwepo na utaratibu kwa upande wa Pemba kuandaa taarifa yake ya fedha (segement financial report) na baadae ndio ziwepo taarifa jumuishi za fedha (consolidated financial report).

Kutokana na uchambuzi huo, Kamati ililishauri Shirika mambo yafuatayo:

- Shirika liepuke gharama zisizokuwa za lazima kwa kuchukua maamuzi magumu ya kuziuza nyumba zake zilizochakaa hususan zilizopo vijijini ili kulipunguzia mzigo na gharama za uendeshaji Shirika;

- Shirika linapoamua kuuza nyumba zake, liuze kwa bei stahiki kulingana na utofauti wa eneo ambalo nyumba husika ipo;

- Shirika linapoamua kuongeza bei nyumba zake, ihakikishe inazifanyia matengenezo nyumba hizo;

- Shirika liandae taarifa maalum ya fedha kwa upande wa Pemba; na

- Katika nyumba ambazo Shirika inazimiliki lakini pia kuna nyumba nyingi zinamilikiwa na watu binafsi, Shirika liwauzie wananchi nyumba hizo ili kuondosha changamoto ya ugumu wa kuzifanyia kazi nyumba hizo.

3.14 SHIRIKA LA MAGAZETI

Taarifa za Mapato

Shirika la Magazeti lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 838,900,000/= katika kipindi cha mwaka 2019/2020 kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato na shilingi 845,192,395/= ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia tarehe 30 June, 2020 jumla ya shilingi 935,260,525 zilikusanywa ambapo ni sawa na asilimia 111.5 ya makadirio na shilingi 632,994,425/= ya Ruzuku ilipokelewa kutoka Serikalini sawa na asilimia 75 ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Ongezeko hili la shilingi 96,360,525 ambalo ni sawa na asilimia 11.5 za makadirio lilitokana mrundikano wa madeni ambayo yalikuwepo kipindi cha mwaka 2018/2019 kwa taasisi mbali mbali hasa Taasisi za Serikali ambayo yalishindikana kulipwa mwaka huo wa fedha na kupelekea baadhi ya madeni hayo kulipwa ndani ya mwaka wa Fedha 2019/2020.

Pia, ongezeko hilo limetokana na makusanyo ya mauzo ya magazeti na matangazo katika matoleo maalum ya kupongeza maendeleo ya Rais Dk. Shein (1 Oktoba, 2019), Toleo maalum la miaka Tisa ya Dkt Shein, (30 Machi, 2020), Miaka 56 ya Muungano (26 Aprili, 2020), toleo la kumbukumbu ya Mzee Abeid Aman Karume (7 Aprili, 2020) na Toleo la Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar (12 Januari, 2020).

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Taarifa ya mapato ya Mkaguzi wa Hesabu za Ndani inafotautiana na Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement). Hii ni kutokana na kuwa Mkaguzi wa Hesabu za Ndani taarifa zake alizipata kupitia bango kitita lililowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
2. Shirika lilianzisha kianzio kipya cha mapato katikati ya mwaka, ambapo Shirika lilikifanyia makadirio kianzio hicho na wakayajumuisha na makadirio ya awali ya mapato jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa kibajeti.
3. Mkaguzi wa Hesabu za Ndani hana uhakika kama taarifa yake aliwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama Sheria ya Fedha inavyoelekeza.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kutatua kasoro zilizobainika na Kamati hii, yafuatayo yalipendekezwa:

i. Mkaguzi wa Hesabu za Ndani ahakikishe kuwa anapata taarifa za fedha kwenye vianzio vya uhakika ili apate taarifa sahihi.
ii. Mkaguzi wa Hesabu za Ndani ahakikishe kuwa anatekeleza majukumu yake kama Sheria na Kanuni za nchi zinavyoelekeza.
iii. Endapo Shirika litapata kianzio kipya cha mapato katikati ya mwaka, basi kianzio hicho makadirio yake ya mapato yasijumuishe kwenye makadirio ya awali ya mapato na badala yake mapato halisi ya kianzio hicho yajumuishwe kwenye mapato mengineyo, na ikiwa kianzio hicho kitaendelea kuwepo kwenye mwaka unaofuata basi kianzio hicho kitapaswa kupewa kifungu chake.

Taarifa za Matumizi

Shirika la Magazeti lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,559,592,395 kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya 1,297,644,216.6 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 83 ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Matumizi ya Shirika la Magazeti yameonekana kupungua kutoka shilingi 1,559,592,395 iliyoidhinishiwa kwa kazi za kawaida, ambapo hadi kufikia Juni, 2020 shilingi 1,297,644,216.6 zilitumika sawa na asilimia 83 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 261,948,178.6 sawa na asilimia 17 ya mapungufu. Hii ni kutokana na kupungua kwa Ruzuku kutoka Serikalini.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ina mapungufu mbali mbali kwa mfano; kifungu cha “Other Payment” kina maelezo “Note” zaidi ya moja ndani ya Taarifa moja ya Hesabu jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa ufungaji wa hesabu. Kifungu hiki kimeelezwa kama ni “Note” 5, 11 na 12.
2. Kamati ya LAAC ilishitushwa na hali hiyo na hasa ikizingatiwa kuwa Taarifa hiyo pia huwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama kifungu cha 121(1) cha Sheria ya Fedha kinavyoelekeza na endapo Mdhibiti atagundua kasoro yoyote basi huitaka Taasisi husika kufanya marekebisho juu ya Taarifa hiyo. Hata hivyo, Kamati ya LAAC bado ilibaini kasoro mbali ya Taarifa

hiyo husika ingawa ilipitia katika maeneo tofauti.

3. Taarifa ya mwaka ya Mkaguzi wa Hesabu za Ndani haikuelezea taarifa za matumizi za Shirika na badala yake ilielezea mapato ya Shirika tu.

Kasoro hii imeitia mashaka Kamati hii hasa ikizingatiwa kuwa taarifa za Mkaguzi wa Hesabu za Ndani wa Taasisi husika huwasilishwa Hazina (Treasury) ambaye ni kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mujibu wa kifungu cha 117(6) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016 ambaye kwa utaratibu wao wa ndani huiwasilisha taarifa hiyo kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani "Internal Auditor General" ambaye kwa mujibu wa kifungu cha 116(2)(f) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 ana jukumu la kuishauri Serikali juu ya hatua za kuchukua kuhakikisha thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali.

Sambamba na hilo, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kwa mujibu wa kifungu cha 11(2)(h) ana jukumu la kupitia, kutathmini na kupendekeza juu ya mfumo wa usimamizi na ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali.

Hivyo, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kupatiwa taarifa ambazo hazina matumizi au taarifa zake zinatofautiana na uhalisia uliopo kunaweza kumpelekea kutoa ushauri ambao sio sahihi kwa Serikali na kunaweza kutia hasara Serikali.

i. Mhariri Mtendaji wa Shirika alikuwa Mjumbe na Katibu wa Bodi ya Shirika hili, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.
ii. Kutokana na majukumu mengi na mazito ya Mhariri Mtendaji kumbukumbu za Vikao vya Bodi zilikuwa haziandikwi kwa usahihi wake.
iii. Mhasibu wa Shirika hana msaidizi.
iv. Shirika linatumia fedha nyingi kuchapisha gazeti hilo.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro zilizobainika Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Shirika lihakikishe kuwa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka inaandaliwa kama taratibu za ufungaji hesabu zinavyoelekeza kitaifa na kimataifa.
2. Mkaguzi wa Hesabu za Ndani ahakikishe kuwa taarifa zake anazoziandaa zinakidhi vigezo vyote vilivyokusudiwa kwa lengo la kuisaidia Serikali katika kusimamia rasilimali zilizopo katika Taasisi husika
3. Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani ahakikishe kuwa anazifanyia kazi ipasavyo taarifa zote zinazowasilishwa kwake na Wakaguzi wa Hesabu za Ndani kutoka katika Taasisi mbali mbali ili tija ya kuanzisha Kitengo hicho kiweze kupatikana.

4. Bodi za Wakurugenzi za Shirika na Taasisi Zinazojitegemea zihakikishe kuwa inatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo na sio kutekeleza shughuli zao kwa maslahi yao binafsi.
5. Serikali ilinunulie Shirika mtambo wa kuchapia magazeti ili kupunguza gharama za uchapaji.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA SHIRIKA LA MAGAZETI

Shirika la Magazeti ya Serikali limebadilisha namna ya ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kutoka katika Mfumo wa "Accrual Basis" na kuingia katika mfumo wa "Cash Basis", jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shuhuli za Shirika kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyopo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa Shirika kifaida au hasara.

Majibu ya Shirika

Shirika la Magazeti ya Serikali limeundwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii na sio kwa ajili ya biashara. Hata hivyo, kufuatia miongozo mbali mbali kutoka Serikali Kuu, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Shirika lilipokea agizo la kuingia katika Mfumo wa "Cash Basis" katika ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ili tuwe na uwiano na mfanano wa ufungaji wa hesabu kwa Taasisi zote za Serikali, barua yenye kumbukumbu Namb. AD.5/184/01/07/18 inahusika.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikubaliani na agizo la Serikali kupitia Afisi ya Rais, Fedha na Mipango la kuzitaka Taasisi zake kufunga hesabu kwa kutumia mfumo wa "Cash Basis" badala ya mfumo wa "Accrual Basis".

Kamati hii haikubaliani na agizo hili kwa kuwa endapo utafunga hesabu kwa kutumia mfumo wa "Accrual Basis" kuna fursa ya kuonekana hali halisi ya kifedha iliyopo katika Taasisi husika. Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kulifuta agizo hilo na kuzitaka Taasisi zake kufunga hesabu zao kwa kutumia mfumo wa "Cash Basis" kutokana na sababu tulizozieleza hapo kabla. Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

3.14.1 Kutokufanya Kazi kwa Kamati ya Ukaguzi

Shirika la Magazeti bado halijaanzisha Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu (Audit Committee) na hivyo kutumia Kamati ya Ukaguzi iliyoanzishwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo jambo ambalo ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari ya kutokufanya kazi kwa Kamati hiyo na kupelekea kubainika mapungufu mbali mbali katika usimamizi wa ndani wa Shirika la Magazeti ya Serikali kama ifuatavyo:-

- Kutokujadili na kuidhinisha mpango mkakati wa mwaka wa ukaguzi wa ndani
- Kutokupitia taarifa za hesabu za Shirika la Magazeti ya Serikali
- Kutobainisha mapungufu ya ripoti ya ukaguzi wa hesabu wa Nje kwa lengo la kufanyia kazi mapungufu yaliyobainika na kulishauri Shirika ili liweze kujiendesha kwa tija.

Majibu ya Shirika

Shirika la Magazeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 liliendelea kutumia Kamati ya Ukaguzi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Mambo ya Kale, isipokuwa kwamba, Kamati hiyo haikuwahi kupitia taarifa za Ripoti za Mkaguzi wa Ndani. Changamoto hii ilifanya Shirika kuanza mchakato wa kufuatilia utaratibu wa kuunda Kamati ya Ukaguzi ya Shirika kama lilivyopokea ushauri kutoka kwa Mkaguzi wake wa ndani juu ya kuwepo kwa Kamati ya Ukaguzi ili kuweka ufanisi nzuri wa kupitia ripoti za Mkaguzi na kupelekea kuweka ufanisi nzuri wa kiutendaji.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Shirika na hasa ikizingatiwa kuwa mara tu baada ya Shirika hili kuanzishwa lilipaswa kuwa na Kamati yake na sio kuitegemea Kamati ya Wizara.

Kutokana na maelezo yake hayo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa zinafuata Sheria na Kanuni za nchi ili kuepusha kasoro zisizo na msingi. Kwa mnasaba huo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

3.14.2 Manunuzi ambayo yamekiuka utaratibu Tsh, 102,364,625

Shirika la Magazeti limekuwa likigawa manunuzi ya bidhaa za vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ajili ya kuzuia kutumia njia sahihi ya ununuzi kama zilivyoelekezwa katika Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Hii imejitokeza wakati Shirika likifanya manunuzi ya vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano vilivoharimu shilingi 102,364,625.

Kufanya hivyo, ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:

Nam.	Nambari ya Hati ya	Aliyelipwa	Fedha zilizolipwa	Maelezo

	Malipo		(Tsh)	
1.	13/12, 18/12/2019	TLM Computer Service	11,970,000	Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kompyuta
2.	14/12, 18/12/2019	TLM Computer Service	27,930,000	Malipo ya ununuzi wa kompyuta
3.	15/12, 18/12/2019	TLM Computer Service	29,925,000	Malipo ya ununuzi wa kamera
4.	16/12, 18/12/2019	TLM Computer Service	13,965,000	Malipo ya ununuzi wa HP
5.	44/12, 18/12/2019	FTN Computer Service	10,124,625	Malipo ya ununuzi wa kompyuta saba
6.	1/11, 18/12/2019	FTN Computer Service	8,450,000	Malipo ya ununuzi wa HP laptop i5 3 GH1 TB 8 GB
JUMLA			102,364,625	

Majibu ya Shirika

Kufuatia agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia iliyokuwa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale ilionekana ipo haja ya kuanzishwa kwa gazeti la kiengereza. Hii ni kutokana na kuwa wageni kutoka Mataifa mbali mbali nje ya Nchi wanaotembelea na kukaribishwa Zanzibar hawapati habari sahihi kuhusiana na Zanzibar, ikiwemo habari za Kiuchumi, Siasa, Utamaduni, na Uwekezaji.

Kutokana na uharaka wa uzinduzi na uanzishwaji rasmi wa Gazeti la Zanzibar Mail pamoja na gharama kidogo zitakazotumika endapo Shirika hili halitofanya shughuli hiyo kwa kutoa zabuni. Shirika la Magazeti ya Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale iliomba muongozo kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali ya Serikali juu ya njia sahihi ya kununua vifaa hivyo kama Sheria ya Ununuzi inavyoekeleza. Kwa msingi huo, Mamlaka ya Ununuzi iliishauri Shirika kununua vifaa hivyo kwa njia ya “quotation” ili kuliwezesha Gazeti la Zanzibar Mail kuzinduliwa na kuanzishwa rasmi ndani ya muda uliopangwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

i. Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ililiridhia Shirika hili kufanya ununuzi wa vifaa vya Gazeti la Zanzibar Mail kwa njia ya nukuu iliyogharimu jumla ya Tsh. 88,000,000 kufuatia barua ya tarehe 13 Novemba, 2019 yenye kumbukumbu Namba MMUM BA.370/383/02/27. Vifaa hivyo, ni kama vinavyoonekana kwenye jadweli la hapo juu kuanzia kipengele nambari 1 hadi 4.

ii. Ununuzi mwengine uliofanywa ulikuwa ni ununuzi wa vifaa vya matumizi ya kawaida ya Gazeti la Zanzibar Leo kama vinavyoonekana kwenye jadweli kuanzia kipengele nambari 5 hadi 6. Ununuzi huu unaweza kufanyika kwa njia ya nukuu kwa kuwa haukufikia kiwango cha kuitisha zabuni.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hii kwa kuwa ununuzi wote uliofanyika umefuata taratibu.

3.15: MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 7,200,000,000 kupitia vyanzo vyake ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Mamlaka imekusanya jumla ya shilingi 3,396,047,461.10 ambazo ni sawa na asilimia 47 ya makadirio.

Mamlaka imeshindwa kufikia malengo ya bajeti ya makusanyo lupitia vyanzo vyake vya ndani kwa asilimia 53.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka imepata asilimia 47 ya makadirio kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kutofikia lengo hilo kumetokana na sababu kuu zifuatazo;

- Kwa mwaka husika, sababu kuu iliyopelekea mapato yasifikie malengo ni kuwepo kwa ugonjwa wa virusi vya Korona (Uviko - 19) ambao umepelekea wateja wengi wakubwa wa Mamlaka kufunga biashara zao.
- Kusitishwa kwa zoezi la uhamasishaji kwa wateja ambao husaidia kwenye kukuza makusanyo ya Mamlaka kutokana na kuwepo kwa ugonjwa wa virusi vya Korona (Uviko - 19).

- Mbali na juhudi za utoaji wa elimu kwa wananchi, lakini bado muamko ni mdogo kwa wateja kwenye kulipia huduma ya maji safi na salama

Uchunguzi wa Kamati

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:

1. Mamlaka inategemea zaidi mapato kutoka katika hoteli ambazo tayari Mamlaka imeshazifungia mita zinazosoma kiwango cha maji wanayotumia. Kufungwa au kupunguza matumizi ya maji kwa hoteli hizo kuliwakosesha mapato Mamlaka kwa kiasi kikubwa.
2. Kuondolewa (kufutwa uteuzi) kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka mwezi wa Disemba na Makamo Mwenyekiti kufariki kuliifanya Bodi isite kutekeleza majukumu yake hususan ya kiufuatiliaji na kuzorotesha upatikanaji wa mapato kwa mamlaka kwa vile vikao vya Bodi vilishindwa kufanyika na mkazo katika utekelezaji wa malengo ya makusanyo ulikosekana.
3. Kukosekana mapato mengi kunakotokana na kuwepo miundombinu mibovu ya maji inayosababisha uvujaji wa mara kwa mara wa maji katika maeneo tofauti.
4. Kuwepo wateja wenye viwanda vya matofali ambao ni watumiaji wakubwa wa maji lakini imesikitishwa na juhudi ndogo zinazofanywa na Mamlaka za kuwafungia mita zinazosoma kiwango cha maji wanayotumia kunakopelekea kuikosesha Mamlaka mapato. Hata hivyo, Mamlaka huwalipisha shilingi 500,000 kwa mwaka.
5. Kuwepo wateja wengi wadogo ambao hawajafungiwa mita lakini wanatumia kiwango kikubwa cha maji ukilinganisha na wanachokilipa kwa mwezi (4,000). Hata hivyo, Mamlaka ina mpango wa kuwafungia mita za malipo ya awali wateja wao (Pre-paid and Smart meters) pamoja na kwamba uwezo wao ni mdogo wa kuutekeleza mpango huo.

6. Kuwepo kwa madeni kadhaa inayodai Mamlaka kutoka katika Taasisi tofauti za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

7. Matumizi ya mfumo wa ‘cash basis’ katika ufungaji wa hesabu za mwisho badala ya ‘accrual basis’. Hivyo, Mamlaka hushindwa kuonesha taswira halisi ya madeni yao.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza mambo yafuatayo:

1. Mamlaka ifanye ubunifu wa kutafuta vyanzo vipya vya mapato na kuviimarisha vyanzo walivyonavyo ili kuepusha kukosekana mapato kutokana na chanzo kimoja kukosa kufanya makusanyo.
2. Mamlaka ihakikishe inafanyia matengenezo miundombinu yake pamoja na

kuharakisha matengenezo pale inapotokea uharibifu wa aina yoyote.

3. Mamlaka ihakikishe inakuwa na mpango mzuri wa kuwafungia mita wateja wake wanaotumia sana maji ili waweze kukuza mapato yao.
4. Serikali kupitia Wizara ya fedha na Mipango izikate fedha Taasisi zinazodaiwa maji na mamlaka kabla ya fedha zao za matumizi ya kawaida kuingizwa katika hesabu zao.
5. Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itoe muongozo utakaoiruhusu Mamlaka kutumia mfumo wa 'Accrual basis' katika ufungaji wa hesabu zake za mwisho wa mwaka ili ziweze kuonesha uhalisia wa mapato na matumizi wanayoyafanya.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya maji Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 15,069,040,459 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 117,286, 991,843 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Juni, 2020 Mamlaka ilitumia jumla ya shilingi 6,673,150,626.60 kwa kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia 44 ya makadirio na shilingi 17,026,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa sawa na asilimia 15 ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka imetumia asilimia 44 ya makadirio kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Punguzo la matumizi hayo kwa asilimia 56 limetokana na sababu kuu zifuatayo;

- Kupungua kwa matumizi ya kawaida ya Mamlaka "Other Charges", kumetokana na kupungua kwa makusanyo ya ndani ambayo yamefikia asilimia 47 ya makadirio yanayotokana na sababu kama zilivyoelezwa hapo awali.

- Mamlaka imetumia asilimia 15 ya makadirio kwa ajili ya kazi za maendeleo. Punguzo la matumizi hayo kwa asilimia 85 limetokana na sababu kuu zifuatazo.

- Mradi wa Uimarishaji na Uhuuishaji wa Mfumo wa Usambazaji wa Maji (India 92m) haukufanya utekelezaji kutokana na Uviko 19 na kupelekea lockdown nchini humo.

- Mradi wa Uchumbaji wa Visima (RAK) ulipata fedha pungufu kutokana na Uviko 19.

Kupungua kwa matumizi ya maendeleo ya Mamlaka "Development", kumetokana na kupungua kwa makusanyo ya ndani ambayo yamefikia asilimia 47 ya makadirio yanayotokana na sababu kama zilivyoelezwa hapo awali.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na kuwepo punguzo katika matumizi ya Mamlaka, Kamati iligundua mambo

yafuatayo:

1. Kuwepo kwa matumizi makubwa ya fedha za Mamlaka kwenye baadhi ya vifungu kinyume na bajeti iliyopangwa. Hili linatokana na kukosekana kwa Bodi yenye jukumu la kupitisha na kufanya marekebisho ya Bajeti ya Mamlaka.
2. Kuna pampu nyingi za visima zimeharibika na visima hivyo kushindwa kutoa huduma ipasavyo kwa wananchi wetu.
3. Mamlaka haina vifaa vya kutosha vya akiba vilivyopo ghalani kuwezesha matengenezo ya miundombinu ya maji kufanyika kwa wakati pindi itakapoharibika ghafla.
4. Kuna visima vingi havina pampu za maji.
5. Kuna ukosefu wa maji katika maeneo mengi ya Zanzibar jambo linalopelekea wananchi wenye uwezo kuamua kuchimba visima na kuacha kutumia maji ya ZAWA.
6. Jumla ya gari 14 za Mamlaka zimechukuliwa na Ofisi ya Rais, Ikulu bila ya idhini ya uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, Mamlaka ilimuandikia barua Katibu Mkuu - Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia barua ya tarehe 04 Machi, 2021 yenye kumbukumbu Namba ZAWA/A.10/15/20 na kujibiwa kuwa iendelee kuruhusu gari hizo kuchukuliwa.

   Kutokana na kadhia hiyo, Kamati ya LAAC iliamua kufanya kikao cha pamoja kilichowakutanisha Kamati, Watendaji wa Mamlaka ya Maji, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Ikulu, Shirika la Umeme Zanzibar na Mkuu wa Magari Ikulu tarehe 02 Februari, 2022 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi ili kulipatia ufumbuzi suala hilo na matokeo ya kikao hicho ni kama ilivyoelezwa kwenye ukurasa wa 156 hadi 163 wa Ripoti hii.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ya Maji Zanzibar ifanye matumizi ya fedha zake kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bodi ya Mamlaka.
2. Mamlaka izifanyie matengenezo pampu zilizoharibika na pamoja na kununua mpya ili kuondosha changamoto ya ukosefu wa maji kwa wananchi wa Zanzibar.
3. Mamlaka ihakikishe inanunua vifaa vingi na bora na kufihifadhi katika ghala lake ili kuifanyia matengenezo kwa wakati miundombinu ya maji pindi inapoharibika.
4. Mamlaka ichukue juhudi za makusudi kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata maji ya uhakika.

3.15.1 Manunuzi ya Mashine na Pampu za maji yaliyokiuka utaratibu wa manunuzi shilingi 126,766,686.00.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Maji Zanzibar imekiuka taratibu za kwa kwenda

kinyume na kifungu cha 42(2)(b)(c) cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kinachoitaka Taasisi ya umma kupanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika pamoja na mikataba maalum kwa namna inavyokubalika.

Aidha, kifungu cha 42(2)(c) cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kinakataza kutokugawa ununuzi na uondoshaji kwa lengo la kutokutumia utaratibu wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma. Jumla ya shilingi 126,766,686.00 zimetumika kuwalipa wasambazaji na makampuni zaidi ya sita tofauti kwa ajili ya ununuzi wa pampu za visima kinyume na utaratibu.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakiri kufanya matumizi hayo yaliyokiuka utaratibu kutokana na Mamlaka kutokuwa na fedha ya kutosha kwa ajili ya kuitisha zabuni, hivyo ilikuwa inanunua pampu kila dharura inapojitokeza.

Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha (2021/2022), Mamlaka imeandaa utaratibu wa kutumia “framework Contract” kwa lengo la kufuata taratibu za manunuzi ambapo malipo hufanyika wakati wa kupokea huduma. Utaratibu huu utatumika kwenye manunuzi ya pampu, bomba, vifaa vya umeme pamoja na vifaa vya magari na uchimbaji.

Uchunguzi wa Kamati

1. Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilielezwa fedha yote iliyopangwa kwa ajili ya kazi ya ununuzi wa pampu ilikuwa shilingi 183,401,530 kati ya hizo shilingi 126,766,686 ndio zilizokuwa hazikufuata utaratibu wa sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma. Kamati ilipohoji kwa nini hilo lilifanyika ilielezwa kwamba Mamlaka ilikuwa haina fedha za kuitisha zabuni. Kutokana na ukaguzi wake, Kamati haikuridhishwa na jibu hilo kwa kugundua yafuatayo:
2. Kuwepo kwa ukiukwaji wa makusudi wa Sheria kwani kila Mkuu wa Taasisi anaelewa kwamba kifungu cha 26(1)(g) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinamtaka kabla hajatangaza zabuni athibitishe upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli husika. Aidha, kifungu cha 43(2) cha Sheria hiyo kinamtaka Mkuu wa Taasisi kuanzisha ununuzi baada ya kuthibitisha kwamba fedha zote kwa kiwango kamilina kwa muda wote zitakuwepo wakati wa kuingia mkataba.
3. Vile vile, Mamlaka kupitia Bodi yake inayo fursa ya kuufanyia marekebisho mpango wake ili kusubiria fedha za kufanya manunuzi zikamilike, hili limebainikwa baada ya Kamati kupitia muda ambao vifaa hivyo vimenunuliwa na kuona kwamba kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kusubiria fedha, kununua

vifaa na vitu kuvihifadhi ghalani kwa matumizi ya baadae.

3.15.2 Ongezeko la gharama za matumizi ya mafuta

Ukaguzi ulipitia taarifa za usimamizi wa mafuta kwa kuangalia gharama za matumizi ya mafuta kwa mwaka 2019/2020 ukilinganisha na matumizi hayo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kubaini uwepo wa tofauti kubwa ya gharama za mafuta isiyo ya kawaida ya shilingi 260,597,019.00 ikiwa ni ongezeko.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakiri kwa kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa madaftari ya kuratibu safari za magari ambako kunaweza kupelekea mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Hata hivyo, ongezeko la mafuta kwa shilingi 260,597,019 limetokana na sababu nyengine zikiwemo;

1. Katika kupambana na Uviko 19, Shirika la Kimataifa la UNICEF liliipa Mamlaka jumla ya shilingi 24 milioni kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa lengo la kusambaza maji kwa magari.
2. Mamlaka ilitumia mafuta mengi kwa ajili ya kuunganisha bomba la chemchem la inchi 26 kwenye kulihudumia “excavator”.
3. Mamlaka pia imetumia mafuta kwa ajili ya magari ya UUB kwenye kujaza mawe kwenye shimo la Welezo kwa lengo la kunganisha bomba la inchi 24.

Kwa mwaka huu, Mamlaka imerekebisha dosari zote ilizokuwa nazo na kwa sasa imekuwa na uwekaji mzuri taarifa katika leja za mafuta pamoja na kuwa na madaftari la kuratibu safari za magari (log book).

Uchunguzi wa Kamati

Licha ya Mamlaka kukiri juu ya ongezeko la matumizi ya mafuta bila ya kuingizwa katika daftari la ghalani, Kamati ilitaka kujua sababu zilizopeleka kutofuata taratibu katika matumizi ya mafuta hayo na kujibiwa kwamba makosa yalitokea baada ya Mamlaka kufanya matumizi na baadae ndipo walipopeleka taarifa ya matumizi hayo Bodi.

Kamati haikuridhishwa na kitendo hicho cha Mamlaka na kueleza kwamba huo ni ukiukwaji wa taratibu unaoweza kutoa mwanya kwa watendaji wasiokuwa waadilifu kujinufaisha kwa fedha za umma.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kunusuru jambo kama hilo lisijitokeze tena, Kamati imeshauri yafuatayo:

1. Mamlaka ifuate utaratibu uliowekwa na sheria yake kwa kupeleka katika Bodi mapendekezo yote ya bajeti yao kwa kuidhinishwa kabla ya kufanya matumizi.

2. Mamlaka iweke utaratibu mzuri wa uwekaji kumbukumbu za mafuta yanayonunuliwa ili kudhibiti udanganyifu katika matumizi yake.

3. Mamlaka ifutate utaratibu wa uwekaji mzuri wa kumbukumbu za safari za gari zao katika daftari la kuratibu safari za magari (log book) ili kuepusha matumizi holela ya mafuta.

3.15.4 Ufanisi katika uendeshaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar

Ukaguzi ulibaini kuwa makusanyo yanayotokana na mauzo ya maji yameshuka kutoka shilingi 3,137,452,685 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019 na kufikiia shilingi 2,799,196,832 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kwa tofauti ya shilingi 338,255,853 sawa na asilimia 10.8.

Majibu ya Mamlaka

Ufanisi katika uendeshaji wa Mamlaka ya Maji umeshuka kutokana na sababu zifuatazo:

1. Kwa mwaka husika, sababu kuu iliyopelekea mapato yasifikie malengo ni kuwepo kwa ugonjwa wa virusi vya Uviko - 19 ambao umepelekea wateja wengi wakubwa wa Mamlaka kufunga biashara zao.
2. Kusitishwa kwa zoezi la uhamasishaji kwa wateja ambao husaidia kwenye kukuza makusanyo ya Mamlaka kutokana na kuwepo kwa ugonjwa wa virusi vya Uviko - 19.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilibaini kwamba bado Mamlaka ina uwezo mkubwa wa kuongeza mapato yatakayokuza ufanisi wake iwapo wataacha kufanya kazi kwa mazoea. Hili limebainika kwa kutathmini uvujaji wa maji katika majimbo tofauti ya Waheshimiwa Wajumbe kunakotoa taswira kwamba Mamlaka haifanyi kazi zake ipasavyo.

Mapendekezo ya Kamati

Ili Mamlaka iweze kuimarisha ufanisi wake, kamati ilishauri yafuatayo:

1. Mamlaka iimarishe vyanzo vyake vya mapato.
2. Mamlaka ihakikishe miundombinu ya maji inafanyiwa matengenezo haraka kila inapotokea hitilafu ili kuzuia uvujaji wa maji.
3. Mamlaka ipunguze matumizi yasiyo ya lazima.

MAMLAKA YA MAJI – PEMBA

3.15.5 Hati za malipo zilizokosa vielelezo shilingi 6,899,290

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 6,899,290 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Maji (ZAWA) – Pemba lakini vielelezo husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wake wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi za Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Malipo Yaliyokosa Vielelezo

Nam.	Nambari ya Hati ya Malipo	Fedha zilizolipwa	Aliyelipwa	Maelezo
1.	15/8 15/8/2019	1,455,700	Mamlaka ya Maji Pemba	Malipo ya fedha za marejesho kwa matumizi mbali mbali ya dharura
2.	42/9 27/9/2019	2,281,000	Sharif Petrol Station	Malipo ya fedha za sehemu ya mwanzo ya ununuzi wa mafuta
3.	2/10 3/10/2019	200,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya dharura
4.	35/11 27/11/2019	320,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Malipo ya fedha za marejesho kwa ajili ya ununuzi wa

				chakula
5.	15/3 17/3/2020	2,100,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya Walinzi ambao si waajiriwa
6.	2/4 9/4/2020	142,590	Samail Collage of Science and Technology	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya chakula kwa Washiriki wa kikao
7.	43/6 25/6/2020	400,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Malipo ya fedha ya awamu ya mwisho kwa ajili ya gharama za masomo
JUMLA		**6,899,290**		

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwamba kuna baadhi ya Hati za Malipo hazikukamilika vielelezo vya malipo hadi wakati wa ukaguzi wa mahesabu wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 unafanyika. Hata hivyo, Kitengo cha Hesabu cha Mamlaka ya Maji kimechukua hatua za kukamilisha vielelezo vinavyohusika kwa hati hizo za malipo na kuviambatanisha pamoja na Hati za Malipo zinazohusika.

Nam.	Nambari ya Hati ya Malipo	Fedha zilizolipwa	Aliyelipwa	Kilichokosekana
1.	15/8 15/8/2019	1,455,700	Mamlaka ya Maji Pemba	Barua ya maombi ya kitangulizi
2.	42/9 27/9/2019	2,281,000	Sharif Petrol Station	Barua ya maombi kutoka kwa Mtumiaji
3.	2/10 3/10/2019	200,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Marejesho ya fedha hizo
4.	35/11 27/11/2019	320,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Marejesho ya fedha zilizotumika
5.	15/3 17/3/2020	2,100,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Mkataba
6.	2/4 9/4/2020	142,590	Samail Collage of Science and Technology	Orodha ya Washiriki

7.	43/6 25/6/2020	400,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Risiti ya malipo
JUMLA		**6,899,290**		

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia majibu ya Hoja hii Kamati hii ilibaini yafuatayo:

1. Taarifa zilizokosa vielelezo wakati Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanya ukaguzi zilikuwa nyingi, hata hivyo, baada ya Mkaguzi kuwasilisha barua kwa uongozi "Management letter" baadhi ya vielelezo vilipatikana na vielelezo vyengine vimepatikana wakati Kamati hii ilivyofanya ukaguzi katika Mamlaka hii na viliwasilishwa kwa ukaguzi.

   Pamoja na uwasilishwaji huo, Kamati ya LAAC haikukubaliana na vielelezo hivyo kwa kuwa Mamlaka ilipewa muda wa mwezi mmoja na Mkaguzi Mkuu wa kuvitafuta vielelezo hivyo, isipokuwa kwamba, ilishindwa kuviwasilisha vielelezo hivyo kwa wakati. Kwa mnasaba huo, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

2. Mikataba inayofunga Mamlaka huhifadhiwa sehemu ya Utumishi kitendo ambacho ni kinyume na taratibu za kazi.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Mamlaka ya Maji ihakikishe kuwa inahifadhi vyema kumbukumbu zake ili wakati wowote zikihitaji ziweze kupatikana.

2. Mikataba inayofungwa na Mamlaka ihifadhiwe Masjala kama taratibu za kazi zinavyoelekeza na sio kuwekwa sehemu ya Utumishi.

3.15.6 Malipo kwa wafanyabiashara waliokuwa hawajasajiliwa Shilingi 34,237,762.60

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 34,237,762.6 zimelipa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Mji Pemba kwa wafanya biashara tofauti. Ukaguzi umebaini kwamba wafanya biashara hao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Kutokusajiliwa kwa wafanyabiashara na Mamlaka ya Ununuzi ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Zanzibar

nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Malipo ya Wafanyabiashara waliokuwa hawajasajiliwa

Nam.	Jina la Mfanyabiashara	Fedha zilizotumika (Tsh.)	Maelezo
1.	Nasor Ali Abdalla	846,034	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali
		912,576	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa cable wire 4
		1,368,864	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme
		8,579,165	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ufungaji mita za maji
		5,637,058	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji safi
		598,878	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji
		736,715	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kamba pamoja na dawa
2.	Masim Building Contractor	3,528,000	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa changarawe
3.	Soud Talib Juma	1,176,000	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari
		5,880,000	
4.	Khamis Yussuf Hamad	224,341.60	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viti vya plastiki
5.	Khamis Sultan Said	1,725,339	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa
6.	Midodoni Hadware	2,352,000	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji safi
7.	Samail Collage of Science and Technology	304,192	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya chakula na vinywaji
8.	Khamis Hassan Mgau	368,600	Malipo ya fedha kwa ajili ya uekezaji

Majibu ya Mamlaka

Katika kipindi hicho cha ukaguzi wa mahesabu ya fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Maji Ofisi ya Tawi la Pemba ilifanya biashara na wafanyabiashara mbali mbali. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma. Hii ilitokana na kutokuwa na orodha ya wafanyabiashara kutoka katika Ofisi ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ambao ni halali kwa Taasisi za umma kufanya nao biashara.

Hata hivyo, jitihada tayari zimeshachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwafuatilia wafanyabiashara husika pamoja na kwenda katika Ofisi ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara ambao watafanya miamala ya manunuzi na Mamlaka ya Maji watakuwa wamesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.

Baada ya Mamlaka ya Maji kufuatilia kwa wafanyabiashara hao pamoja na kwenda katika Ofisi ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Mamlaka ya Maji imebaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara hao wanao usajili halali kutoka katika Ofisi ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kama wanavyoonekana hapo chini pamoja na tarehe zao walizojisajili katika.

Nam.	Jina la Mfanyabiashara	Tarehe na Nambari ya Usajili	Maelezo
1.	Nasor Ali Abdalla	Tarehe 01/02/2021 Usajili ZPPDA/G/0213/2021	Amesajiliwa 2018 na 2021
2.	Masim Building Contractor	Tarehe 06/04/2021 Usajili ZPPDA/W/0625/2021	Amesajiliwa 2021
3.	Soud Talib Juma	Tarehe 30/04/2021 Usajili ZPPDA/G/0504/2021	Amesajiliwa 2021
4.	Khamis Yussuf Hamad	Tarehe 07/02/2020 Usajili ZPPDA/P/08/G/2020	Amesajiliwa 2020
5.	Khamis Sultan Said	Tarehe 27/02/2019 Usajili ZPPDA/P/037/2019	Amesajiliwa 2019

6.	Midodoni Hadware	Tarehe 13/08/2021 Usajili G000016	Amesajiliwa 2021
7.	Samail Collage of Science and Technology	-	Bado hajajisajili
8.	Khamis Hassan Mgau	Tarehe 04/08/2021 Usajili ZPPDA/W/0789/2021	Amesajiliwa 2021

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilitaka kujiridhisha na kauli iliyotolewa na Mamlaka ya Maji kuhusiana na Mamlaka hii kufuatilia usajili wa wafanyabiashara hao katika Ofisi za Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa barua itakayothibitisha kwamba kulikuwa na mawasiliano baina ya Taasisi mbili hizi. Hata hivyo, Mamlaka ya Maji Pemba haikuwasilisha barua hiyo, kitendo ambacho kimeitia mashaka Kamati hii juu ya kauli yao hiyo.

Sambamba na hilo, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa orodha ya wafanyabiashara aliyokabidhiwa Mkaguzi Mkuu wakati wa ukaguzi ilionesha kuwa wafanyabiashara hao walikuwa hawajasajiliwa, ingawa watendaji wa Mamlaka ya Maji wameielezea Kamati kuwa walikuwa wamesajiliwa. Kamati ya LAAC imethubutu kutoa kauli hiyo baada ya kujiridhisha kuwa Mkaguzi Mkuu wakati wa ukaguzi wake aliomba kupatiwa hati za usajili za wafanyabishara hao, hata hivyo, Mamlaka ya Maji ilishindwa kuwasilisha hati hizo.

Aidha, katika orodha ya wafayabiashara iliyowasilishwa mbele ya Kamati hii na Mamlaka ya Maji ni wafanyabiashara wawili tu waliosajiliwa kati ya wafanyabiashara 8.

Kiujumla Kamati ya LAAC inakubaliana na Hoja ya Mkaguzi Mkuu inayohusiana na Mamlaka hii kufanya kazi na wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC inazishauri Taasisi za Umma kuhakikisha kuwa zinatekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Sheria.

Vile vile, Mamlaka ya Maji na Taasisi zote za Serikali zielewe kuwa wafanyabiashara wanatakiwa kusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kila mwaka, hivyo, ni vyema wakafuatilia taarifa za mfanyabiashara kwanza kwa

Mamlaka husika kabla ya kuomba huduma kwake.

3.15.7 Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 276,118,668

Mamlaka ya Maji – Pemba huingia katika makubaliano ya ununuzi wa bidhaa na huduma mbali mbali kutoka kwa wafanyabiashara pamoja na Taasisi za Serikali kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Maji – Pemba inadaiwa na wafanyabiashara hao, wafanyakazi pamoja na Taasisi za Serikali jumla ya shilingi 276,118,668 kutokana na kupatiwa bidhaa na huduma mbali mbali. Aidha madeni haya ni ya muda mrefu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(2)(b) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba imekiri kuwa ina madeni ya ndani ya Wafanyakazi na madeni ya nje ya Wafanyabiashara. Deni hilo ni jumla ya shilingi za Kitanzania Milioni Mia Mbili Sabini na Sita Laki Moja Kumi na Nane Elfu Mia Sita na Sitini na Nane (Tsh. 276,118,668.00). Hii inatokana na Mamlaka ya Maji Ofisi ya Tawi la Pemba kuwa na uchache wa fedha za makusanyo.

Pia, Mamlaka ni taasisi inayoshughulikia huduma ya usambazaji wa maji kwa wananchi, hivyo basi, matumizi yake muda mwengine hujitokeza kinyume na matarajio ambapo hulazimika kununua vifaa tofauti kwa njia ya mkopo kutokana na uchache wa fedha za makusanyo. Hali hio hupelekea kuongezeka kwa madeni ya Taasisi.

Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba imechukua jitihada za kupunguza madeni hayo kila hali ya kifedha inaporuhusu ambapo kwa mwaka wa fedha ulioishia 2019/2020 imetayarisha bajeti ya jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni Mia Moja Tisini na Tano na Laki Nane (TSH. 195,800,000.00) ili kupunguza madeni hayo. Hata hivyo, Mamlaka imejitahidi kupunguza madeni hayo kwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni Arubaini na Moja Laki Moja Elfu Saba na Mia Mbili Sitini na Nne (TSH. 41,107,264) sawa na asilimia 15 ya deni lote kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini.

Nam.	Jina la Mfanyabiashara	Deni hadi Juni, 2020	Kilicholipwa hadi Juni, 2021	Kilichobaki hadi Juni, 2021

Nam.	Jina la Mfanyabiashara	Deni hadi Juni, 2020	Kilicholipwa hadi Juni, 2021	Kilichobaki hadi Juni, 2021
1.	Sapphire Engineering (T) Limited	56,111,000	0	56,111,000
2.	Wizara ya Fedha na Mipango – Pemba	2,440,000	0	2,440,000
3.	Zanzibar Petroleum Ltd	2,529,250	0	2,529,250
4.	Commissioner of Income Tax	37,259,694	0	37,259,694
5.	Misufini Stationery Centre	6,849,000	0	6,849,000
6.	Broad Mind Company Ltd	20,650,000	0	20,650,000
7.	Nassor Said Nassor	8,331,680	0	8,331,680
8.	Khamis Sultan Said	3,120,400	0	3,120,400
9.	Salim Hamdan Maalim	6,707,500	0	6,707,500
10.	Nassor Ali Abdalla	10,882,500	5,416,500	5,466,000
11.	Suleiman Seif Rashid	11,615,000	0	11,615,000
12.	Khamis Ali Makame	4,648,000	0	4,648,000
13.	Rashid Moh'd Soud	920,000	920,000	0
14.	Nourbhai Auto Services	6,555,000	6,555,000	0
15.	Kikwajuni Zanzibar Solar	2,100,000	0	2,100,000
16.	Issa Sarhani Said	3,080,000	0	3,080,000
17.	Rahisi Auto Spares	4,908,210	2,462,660	2,445,550
18.	Ali Moh'd Mvinja	5,855,000	0	5,855,000
19.	Efficient Plumbers	7,794,300	0	7,794,300
20.	Suleiman Nassor Suleiman	10,000,000	0	10,000,000
21.	Ali Sarhani Said	1,395,000	0	1,395,000
22.	Juma Faki Salim	487,104	487,104	0
23.	Omar Hamad Kombo	1,242,000	0	1,242,000

Nam.	Jina la Mfanyabiashara	Deni hadi Juni, 2020	Kilicholipwa hadi Juni, 2021	Kilichobaki hadi Juni, 2021
24.	MUUMU Pemba	360,000	0	360,000
25.	Malipo ya kuwaaga Wastaafu 17 - 2017	8,500,000	8,500,000	0
26.	Malipo ya kuwaaga Wastaafu 7 - 2018	3,500,000	0	3,500,000
27.	Malipo ya kuwaaga Wastaafu 12 - 2019	6,000,000	0	6,000,000
28.	Malipo ya kuwaaga Wastaafu 5 - 2020	2,500,000	0	2,500,000
29.	Deni Posho la Wafanyakazi – 2016/2017	6,210,000	6,210,000	0
30.	Deni Posho la Wafanyakazi – 2019/2020	2,340,000	2,340,000	0
31.	Deni Posho la Wafanyakazi Uchimbaji – 2017/2018	1,500,000	0	1,500,000
32.	Deni Posho la Wafanyakazi wa Chuo – 2018/2019	2,656,000	896,000	1,760,000
33.	Deni Posho la Wafanyakazi wa Chuo – 2019/2020	3,112,000	0	3,112,000
34.	Deni Posho Likizo 2018/2019	12,960,000	7,320,000	5,640,000
35.	Deni Posho Likizo 2019/2020	5,520,000	0	5,520,000
36.	Deni Posho Wafanyakazi Bora 5 - 2018	2,750,000	0	2,750,000
37.	Deni Posho Wafanyakazi Bora 5 - 2019	2,750,000	0	2,750,000
	JUMLA	**276,138,638**	**41,107,264**	**235,031,374**

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

1. Mamlaka inafunga hesabu za mwaka kwa kutumia mfumo wa 'Cash basis' mfumo ambao hauruhusu kukopa wakati Mamlaka ya Maji inakopa.
2. Mamlaka ya Maji Pemba ina deni la Income Tax jumla ya Tsh. 37,259,694. Kamati ya LAAC ilishtushwa na jambo hilo hasa ikizingatiwa kuwa fedha za Income Tax zinatokana na mishahara ya watendaji hivyo inakuwaje fedha hizo zisilipwe kwa wakati. Kutokana na hali hiyo Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea deni hilo kutokea, ambapo, Mamlaka ya Maji iliieleza Kamati hii kuwa deni hilo limetokea baada ya Mamlaka ya Maji kupunguziwa Ruzuku na Serikali jambo lililopelekea Mkurugenzi Fedha wa Mamlaka hiyo aielekeza Mamlaka ya Maji Pemba kutokulipa fedha hizo hadi pale hali ya fedha itakaporuhusu.

   Kamati ya LAAC ilisikitishwa sana na kauli hiyo na iliomba kupatiwa barua iliyoelekeza hivyo ili ijiridhishe na kile kilichosemwa, hata hivyo, Mamlaka ya Maji Pemba iliieleza Kamati hii kuwa maelekezo hayo yalitolewa kwa mdomo.

3. Mamlaka ya Maji Pemba kuanzia mwaka 2017 hadi mwezi wa Disemba, 2020 ilitakiwa na Mkurugenzi Mkuu kuwasilisha fedha zote za mapato inazokusanya Afisi Kuu Unguja na baadae asilimia 50 ya makusanyo hayo ndio yanarudishwa Pemba.

   Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa barua iliyoelekeza hivyo, hata hivyo, Mamlaka ya Maji Pemba iliieleza Kamati hii kuwa maelekezo hayo yalitolewa kwa mdomo kwenye kikao cha pamoja cha Watendaji wa ZAWA. Kamati ya LAAC, haikuridhishwa na maamuzi hayo ya Mkurugenzi Mkuu hasa ikizingatiwa kuwa Afisi Kuu ya Mamlaka ya Maji ilikuwa na bajeti yake ya matumizi. Hivyo, Mkurugenzi Mkuu kufanya maamuzi kinyume na bajeti ilivyoidhinishwa ni kuvunja masharti ya Sheria za fedha.

Mapendekezo ya Kamati

Ili Mamlaka ya Maji Pemba iweze kutatua kasoro zilizobainika, Kamati ya LAAC

ilipendekeza mambo yafuatayo:

1. Hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka zifungwe kwa kutumia mfumo wa 'Accrual basis' kwa kuwa mfumo huu unaruhusu kukopa.
2. Mamlaka ya Maji Pemba iachane na tabia ya kutekeleza shughuli zake kwa kufuata amri zinazotolewa kwa mdomo kwa kuwa mawasiliano ya kiutendaji ya Serikali hufanywa kwa maandishi.
3. Kwa kuwa fedha za makusanyo za Mamlaka ya Maji Pemba zilikuwa zinatumika pia Afisi Kuu Unguja, na kwa kuwa Mamlaka ya Maji Pemba haina fedha za kutosha, hivyo basi, Afisi Kuu Unguja ilipe deni la Income Tax pamoja na deni la wafanyakazi linalodaiwa Mamlaka ya Maji Pemba.
4. Mamlaka ya Maji Pemba ipunguze idadi ya wafanyakazi bora kwa mwaka pamoja na kuachana na utaratibu wa kuwaaga watendaji wanaostaafu kwa kuwa Mamlaka hii haina uwezo wa kufanya hivyo.

   Kamati ya LAAC inashauri hivyo kwa kuwa, kanuni ya 131 ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 haikumlazimisha Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi kufanya sherehe ya kuaga na kumpatia zawadi.
5. Watendaji wa Mamlaka ya Maji watekeleze shughuli zao kwa kufuata matakwa ya Sheria za nchi.

3.15.8 Malipo kwa wafanyabiashara waliokuwa hawajasajiliwa Shilingi 37,163,447.44

Majibu ya Hoja hii ni kama yalivyoelezwa kwenye Hoja Namba 3.15.6.

3.15.9 Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji mapato Shilingi 6,866,873,986.55

Mamlaka ya Maji – Pemba (ZAWA) ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 6,866,873,986.55 kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka imeweza kukusanya jumla ya shilingi 991,096,969.88 sawa na asilimia 14.43 ya makadirio ambapo hati hii inaonyesha Mamlaka imeshindwa kufikia lengo la makusanyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 32(1)(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Maji haikuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa asilimia Mia Moja kama ilivyojiwekea. Hali hii imetokana na sababu zifuatazo;

1. Kuwepo kwa ugonjwa wa virusi vya korona (Uviko-19) ambao umepelekea wateja wengi wa huduma ya maji wa Mamlaka kufunga biashara zao.
2. Kusitishwa kwa zoezi la uhamasishaji kwa wateja ambao husaidia kwenye kukuza makusanyo ya Mamlaka kutokana na kuwepo kwa ugonjwa wa virusi vya korona (Uviko-19).
3. Mbali na juhudi za utoaji wa elimu kwa wananchi, lakini bado muamko ni mdogo kwa wateja kwenye kulipia huduma ya maji safi na Salama pamoja na kuwa wateja wanafuatwa katika majumba yao.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yamebainika:

1. Mbali ya sababu hizo zilizoelezwa na Mamlaka hii, Kamati ya LAAC imebaini kuwa sababu yengine inayochangia Mamlaka ya Maji kukusanya mapato chini ya kiwango ni pamoja na Mamlaka hiyo kushindwa kufika baadhi ya maeneo ingawa huduma wanayoitoa inahitajika katika maeneo hayo.
2. Wakati wa ukaguzi, Mkaguzi Mkuu hakupatiwa nakala ya taarifa ya fedha (Financial Statement) ya mwaka husika na badala yake alipatiwa taarifa hizo kwa mdomo tu jambo ambalo limepelekea kupatikana kwa taarifa ambazo zina mapungufu.
3. Idadi ndogo ya mafundi, hali hii inapelekea kushindwa kuzitatua changamoto mbali mbali zinazojitokeza kwa wakati.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na mapungufu hayo Kamati ya LAAC imependekeza yafuatayo:

1. Mamlaka ya Maji izidishe juhudi ya kuyapatia huduma ya maji maeneo yote ambayo huduma hiyo haijafika ili kuwaondoshea usumbufu.
2. Mamlaka hii isiwatoze fedha wananchi ambao hawajanufaika na huduma ya maji ili kuepusha mivutano isiyokuwa ya lazima.
3. Mamlaka ya Maji iwe na kawaida ya kufanya zoezi maalum la kukusanya fedha kwa wateja wao ili iweze kufikia malengo iliyojipangia.
4. Afisi Kuu Unguja iipatie Afisi yake ya Pemba nakala ya taarifa ya fedha (Financial Statement) ya mwaka husika ili watendaji wa Afisi hiyo waweze kutoa taarifa sahihi zinapohitajika pamoja na kumuwezesha Mkaguzi Mkuu kufanya kazi zake bila ya usumbufu wowote.
5. Katika kuhakikisha kuwa wateja wa Mamlaka hii wanailipia huduma wanayopatiwa kwa wakati ni vyema Mamlaka ikaanzisha mfumo wa kulipia huduma hiyo kwanza (Pre paid) pamoja na kuendelea na zoezi la kuwafungia

mita wateja hao. Zoezi hilo lianze kwa wateja wa kwenye viwanda na hoteli.

6. Kuongeza idadi ya mafundi ili kuweza kushughulikia matatizo mbali mbali yanayojitokeza kwa wakati.

3.15.10 Madeni ya huduma ya maji ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu shilingi 16,007,884,152.98

Katika ukaguzi ulifanyika imebainika uwepo wa madeni ya maji yenye jumla ya shilingi 16,007,884,152.98 ambayo yanadaiwa na Mamlaka ya Maji – Pemba kwa Taasisi za Serikali, Wafanya biashara na watu binafsi ambapo madeni hayo ni muda mrefu. Aidha uongozi wa Mamlaka ya Maji – Pemba umeshindwa kuchukua hatua zinazostahiki kwa wadai husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Maji Pemba inadai kiasi kikubwa cha fedha ambacho ni madeni ya muda mrefu yatokanayo na utumiaji wa huduma ya Maji kwa wateja wake. Sambamba na hilo, Mamlaka ya Maji imechukua jitihada za lazima ili kuhakikisha kuwa inafanikiwa kukusanya fedha zitokanazo na utaumiaji wa huduma ya maji kama ilivyojipangia kutoka kwa wateja wake tofauti.

Miongoni mwa jitihada ambazo Mamlaka inachukua ili kuhakikisha malipo ya huduma ya Maji inafanikiwa ni pamoja na kutoa ankara kwa wateja wake wote kwa kila mwezi, kuwafuatilia wateja wake nyumba hadi nyumba kukusanya mapato hayo, pia Mamlaka hutumia njia ya uondoaji wa huduma ya Maji ikibidi kwa mteja husika.

Vile vile, Mamlaka hutumia njia ya mazumgumzo na matangazo kuwahamasisha wateja kuweza kusawazisha madeni yao ya huduma ya Maji. Pamoja na jitihada hizo, Mamlaka bado inabakia kuwa na jukumu la kutoa huduma ya maji safi na salama kama ambavyo Sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaelekeza.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na kiwango hicho cha fedha kilichoripotiwa kudai Mamlaka hii. Hii ni kutokana na kuwa Mamlaka ya Maji haina takwimu halisi ya wateja wao ambao wanapata huduma hiyo na badala yake ina orodha ya wateja ambao imewasajili tu.

Kwa kuwa vyombo vinavyopitisha bajeti za Taasisi hupitisha na bajeti ya malipo ya maji, hivyo, Kamati ya LAAC inaitaka Wizara ya Nchi, (OR), Fedha na Mipango

kuzikata fedha za Matumizi Mengineyo (OC) moja kwa moja Taassi zote ambazo zinadaiwa na Mamlaka hii.

MENGINEYO

Pamoja na kufuatilia hoja hizo Kamati ya LAAC imeagiza mambo yafuatayo:

1. Mamlaka ya Maji Pemba kuzifanyia ukarabati gari za Mamlaka zilizotelekezwa ofisini hapo ili zisizidi kuharibika.
2. Kuwe na mashirikiano ya karibu baina ya Taasisi za Serikali pale zinavyotekeleza majukumu yao ili kuepusha kujitokeza hasara miongoni mwa Taasisi hizo. Kwa mfano, Mamlaka ya Maji inavyolaza mabomba ya maji karibu na barabara ni vyema ikawasiliana na Taasisi inayohusiana na barabara ili kutekeleza shughuli zao bila ya kukwazana.
3. Mamlaka ya Maji ihakikishe kuwa inaweka katika ghala lake vifaa vya kutosha ili kuepusha usumbufu kwa watendaji pamoja na kwa wateja wao.

3.16: MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

Taarifa za Mapato

Mapato ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka Shilingi 16,424,630,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia Shilingi 16,734,169,912 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la Shilingi 309,539,912 sawa na asilimia 1.8.

Majibu ya Mamlaka

Ongezeko la mapato limetokana na kuongezeka kwa makusanyo ya tozo la usimamizi wa sekta ya mafuta (Regulatory levy) kwa Shilingi 292,496,000 pamoja na kuongezeka kwa mapato mengineyo yatokanayo na adhabu na uuzaji wa nyaraka za zabuni (tender documents) kwa shilingi 17,044,000.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalibainika:

1. Katika Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka haikujumuishwa Taarifa ya Mlinganisho “Statement of Comparison” wa miaka kwa madai kuwa Watendaji wa Mamlaka walifikiria kuwa Taasisi zinazoweka taarifa hiyo ni zile zinazofunga hesabu kwa kutumia njia au mfumo wa “Cash”.
2. Mapato mengi yamejumuishwa kwenye kifungu cha Mapato Mengineyo “Other Receivable” jambo ambalo halimpi fursa msomaji wa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka kujua kwa kina kifungu hicho kimejumuisha vianzio vipi.

3. Kifungu cha “Exchange Gain/Loss” hukadiriwa kwa kutumia fedha za Kimarekeni, ingawa, katika Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka mapato hayo huandikwa kwa kutumia fedha za Tanzania. Kitendo hiki hakioneshi uhalisia wa mapato husika hasa ikizingatiwa kuwa fedha ya Tanzania hupanda kila baada ya muda. Hivyo, kifungu hiki kitaonekana kinapata hasara tu.
4. Serikali imewataka kuwasilisha gawio kila mwezi na katika kipindi hiki wanatakiwa kuwasilisha Tsh. 500,000,000. Jambo hilo linapunguza ufanisi wa kiutendaji wa Taasisi hii kwani kiwango wanacholipa ni kikubwa sana na kwa kukisia kinafikia 40%.
5. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar inashindwa kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuthibiti maji na umeme kwa kuwa Mamlaka ya Maji (ZAWA) na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) haziwasilishi taarifa zinazotakiwa na Mamlaka hii. Jambo la kusikitisha Mamlaka hii imeshatoa indhari “notice” mara mbili kwa Taasisi hizi, hata hivyo, hakuna juhudi yoyote iliyochukuliwa na viongozi wa Taasisi hizi. Kitendo hiki kinarudisha nyuma dhamira ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na mambo hayo yaliyojitokeza Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Watendaji wa Mamlaka wahakikishe kuwa katika Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka wanaijumuisha Taarifa ya Mlinganisho “Statement of Comparison” ili kuweza kupima mambo au shughuli za miaka miwili zilivyotekelezwa.
2. Kila kianzio cha mapato taarifa zake zioneshwe katika Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ili kuweza kujua na kupima kila kianzio katika mwaka husika kimekusanya kiasi gani cha fedha.
3. Mamlaka ilipe gawio lake kwa mwaka na kwa asilimia kama zinavyofanyiwa Taasisi nyengine ili iweze kunufaika na mapato inayokusanya badala ya utaratibu unaotumika hivi sasa.
4. Mamlaka izichukulie hatua zinazostahiki Mamlaka ya Maji na Shirika la Umeme Zanzibar endapo zitashindwa kutoa mashirikiano yanayotakiwa ili Mamlaka iweze kutekeleza vyema shughuli zake.
5. Mamlaka ya Maji na Shirika la Umeme Zanzibar zitoe taarifa zinazotakiwa kwa Mamlaka ili Mamlaka hii iweze kujua kasoro mbali mbali inazozikabili Taasisi hizi na kuweza kutoa msaada au ushauri wake juu ya kasoro hizo.

Taarifa za Matumizi

Matumizi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 13,554,813,036 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 14,008,586,980 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 453,773,944 sawa na asilimia 3.35.

Majibu ya Mamlaka

Ongezeko la matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 limetokana na kuongezeka kwa gharama zinazohusu maslahi ya wafanyakazi (staff cost) kwa Shilingi 841,199,265 kulikosababishwa na kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi wa kudumu pamoja na wale wa kuazimwa kutoka Taasisi nyengine za serikali.

Vile vile, ongezeko la matumizi limesababishwa na kuongezeka kwa gharama zinazotokana na uchakavu wa rasilimali za Mamlaka (Depreciation and Armotization of assets) pamoja na kuongezeka kiasi kwa mchango wa Serikali kwa fedha zinazoingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC iliridhika kwa kiasi kikubwa na matumizi yaliyofanywa na Mamlaka hii, hata hivyo, Kamati hii haikuridhika na matumizi yaliyofanywa na Mamlaka ya kuzifanyiya matengenezo “service” gari zake 8 katika mwaka huo wa fedha, ambapo, jumla ya Tsh. 40,882,000 zilitumika. Kamati hii imeona kwamba kiwango hicho ni kikubwa sana ukilinganisha na uhalisia kazi halisi iliyofanywa.

Hivyo, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka kuhakikisha kuwa inafanya matumizi yake kwa kuzingatia kuwa kazi iliyofanywa inaendana na thamani halisi ya fedha.

HESABU ZA MWISHO WA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Taarifa ya Utendaji wa Kifedha

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini kwamba utendaji wa kifedha wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar umeimarika kwa kutoa huduma na kuongezeka kwa ufanisi katika utendaji wa shughuli zake. Kutokana na taarifa za kihesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi imebainika kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar inaendelea kupata faida.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar ilipata faida ya shilingi 2,725,582,932. Hata hivyo, faida ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar imeonekana kupungua kutoka Shilingi 2,869,816,964 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 2,725,582,932 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi 144,234,032 sawa na

asilimia 5.

Majibu kwa taarifa ya utendaji

Utendaji wa kawaida wa shughuli za Mamlaka umeendelea kuimarika kwa Mamlaka kuzidi na kuendelea kutoa huduma pamoja na kuongezeka kwa ufanisi katika utendaji wa shughuli zake za udhibiti. Hali hii imechangiwa na Mamlaka kuendelea kuajiri watendaji wenye uwezo na uelewa mkubwa na sifa zinazostahiki.

Vile vile, Mamlaka imeendelea kuwapatia mafunzo mbali mbali watendaji wake yakiwemo mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Majibu ya Mamlaka

Kama taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilivyoelezea kwamba Mamlaka imeendelea kupata faida kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa Shilingi 2,725,582,932 ikiwa ni pungufu kwa shlingi 144,234,032 sawa na 5% kwa kulinganisha na mwaka wa fedha 2018/2019.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar ikiwa ni Taasisi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina jukumu mama la kudhibiti huduma za maji na nishati kwa upande wa Zanzibar kwa kuhakikisha kwamba huduma hizo zinapatikana kwa uhakika, ubora na ufanisi wa kiwango cha juu bila ya kutarajia kupatikana faida kama zilivyo Taasisi nyengine. Faida yoyote ile itakayopatikana na Mamlaka ni matokeo tu ya uendeshaji wa shughuli za Mamlaka kwa kuwepo na tofauti baina ya fedha iliyokusanywa na ile iliyotumika. Hata hivyo, Mamlaka inaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba ukusanyaji wa mapato unaimarika na mapato yanaongezeka na gharama za uendeshaji (matumizi) zinapungua kwa kadiri ya hali itakavyoruhusu bila kuathiri shughuli na ufanisi wa huduma za Mamlaka.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka hii kuhakikisha kuwa inaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuanzishwa kwake ili Taasisi zilizopo chini yake pamoja na wananchi kwa ujumla kuweze kujua lengo la kuanzishwa kwa Mamlaka. Jambo hili linaweza kuisaidia Mamlaka kutekeleza shughuli zake kwa wepesi na kwa ufanisi mkubwa na hatimae kuleta tija iliyokusudiwa.

Vile vile, kwa kuwa Mamlaka hii ina jukumu la kudhibiti huduma ya maji na nishati Zanzibar, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka hii kutafuta Watendaji wenye taaluma ya kutosha juu ya shughuli zake ili watendaji hao waweze kubaini kasoro mbali mbali zitakazokuwepo kwenye Taasisi inazozisimamia pamoja na kutoa ushauri

utakaokubalika kwa lengo la kuleta ufanisi uliotarajiwa.

Pamoja na maelezo hayo, katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini na kupendekeza yafuatayo:

1. Jumla ya Wizara tatu ambazo ni: Wizara ya Uchumi wa Bluu, Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi na Taasisi mbili za Serikali ambazo ni ZPRA, ZPDC zinatumia jengo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati bila ya kulipa kodi wakati baadhi ya Taasisi za Serikali hutumia majengo ya Taasisi nyengine kwa kukodi.

   Mfano wa Taasisi ya Serikali ambayo inakodisha jengo lake kwa Taasisi nyengine ya Serikali ni Mfuko wa Barabara ambapo Mamlaka hii kabla ya kujenga jengo lake ilikodi ofisi katika jengo hilo na hivi sasa Mfuko wa Barabara umeikodisha ofisi ya Mkaguzi Kuu wa Hesabu za Ndani.

2. Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023 kuiruhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati kuzikodisha Taasisi zote zinazotumia jengo hilo, ili Mamlaka nayo iweze kukusanya mapato kupitia jengo lake kwa nia ya kuimarisha utendaji wa Mamlaka, kuepusha usumbufu wa malipo katika huduma zinazotolewa, kuendeleza muonekano mzuri wa jengo na haiba yake (Maintance and services) pamoja na kuongeza mapato yanayowasilisha Serikali Kuu.

3. Kamati ya LAAC inashauri hilo kwa kuwa endapo Mamlaka hii itakodisha jengo lake itakusanya jumla ya Tsh. 70,560,000 sawa na USD 29,400 kwa mwezi. Mchanganuo unafuata unaonesha namna Taasisi hizi zitakavyolipa:

NO.	TAASISI	SQUARE METRE	GHARAMA (USD)	TZ SHILINGS
1.	WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI	1,400	1,400 X 7 (USD) = 9,800	23,520,000
2.	ZPRA	600	600 X 7 (USD) = 4,200	10,080,000
3.	ZPDC		400 X 7 (USD) = 2,800	6,720,000

		400		
4.	WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI	1,000	1,000 X 7 (USD) = 7,000	16,800,000
5.	WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI	800	800 X 7 (USD) = 5,600 (USD)	13,440,000
	JUMLA KUU		**29,400**	**70,560,000**

4. Wizara na Taasisi zinazotumia jengo hilo hazilipi ipasavyo huduma inazotumia kama vile ulinzi, umeme, kodi ya ardhi, mafuta ya jenereta, usafi na maji jambo ambalo linaligharimu Mamlaka hii kutumia fedha nyingi kwa mambo ambayo hayahusu Mamlaka moja kwa moja, isipokuwa kwamba, Mamlaka inalazimika kulipia gharama hizo kwa kuwa ndio mmiliki wa jengo na gharama hizo huwasilishwa moja kwa moja kwake. Jadweli lifuatalo linaonesha matumizi ya uendeshaji wa jengo kuanzia mwezi wa Oktoba hadi Disemba, 2021. Matumizi ambayo yamevuka makisio ya bajeti husika.

NO.	MATUMIZI	GHARAMA
1.	UMEME WA KISIMA	1,000,000
2.	UMEME WA JENGO	11,093,678
3.	USAFI WA JENGO	16,305,119
4.	MATENGENEZO YA LIFTI &AC	33,879,890
5.	BILI YA MAJI	200,723
6.	ULINZI WA JENGO	6,912,000

7.	MAFUTA JENERETA	5,584,400
	TOTAL	**74,975,810**

Kutokana na hali hiyo, gharama za madeni huzidi kila mwezi kutokana kutokulipwa kwa huduma zinazotumika kwa muda uliopangwa. Lifuatalo ni jadweli linaloonesha madeni kwa baadhi ya Taasisi zinazotumia jengo hilo hadi Disemba, 2021.

NO.	MATUMIZI	GHARAMA
1.	UMEME WA JENGO	68,849,849.
2.	MATENGENEZO YA LIFTI &AC	WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI 10% = 3,387,989
3.	MAFUTA YA JENERETA 31/01/2022	1. ZPDC 15% = 416,700 2. ZPRA 15% = 416,700 3. WMNM 10% = 277,800 4. WANM 10% = 277,800 5. WUBV 10% = 277,800

Kamati ya LAAC inazitaka Wizara na Taasisi zote zilizopo katika jengo hilo kulipia gharama mbali mbali zinazotumia ili kuiondoshea Mamlaka mzigo uliokuwa hauna msingi.

5. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati inalipa kodi ya ardhi (Lease) kwa Serikali jumla ya USD 1000 kila mwaka wakati eneo au jengo husika linatumiwa pia na Taasisi nyengine za Umma.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kutoitoza kodi Mamlaka

hii kwa kuwa na Taasisi nyengine za umma zinanufaika na jengo hilo.

6. Kwa kuwa jengo hilo linatumiwa na Taasisi mbali mbali Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati imekuwa inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa nafasi za ofisi kwa wafanyakazi wake na kupelekea kugawa maeneo mengine ambayo yalipangiwa kazi nyingine pamoja na eneo la maegesho ya gari ya wafanyakazi na wanaofuata huduma.

7. Mamlaka imeweka kiwango maalum cha malipo kwa ajili ya kodi za kutumika Kumbi za Mamlaka kwa taasisi zote, hata hivyo, Wizara ya Maji, Nishati na Madini (WMNM) inatumia kumbi hizo bila kulipa kodi yoyote. Jadweli linalofuata linaonesha matumizi hayo ya ukumbi:

NAMBA	TAREHE	UKUMBI	TUKIO
1.	13-15/07/2021	BOARD ROOM	WMNM
2.	15/07/2021	BOARD ROOM	WMNM
3.	27-28/07/2021	BOARD ROOM	WMNM
4.	09 /08/2021	MAFUTA HALL	WMNM
5.	11/08/2021	MAFUTA HALL	WMNM
6.	12/08/2021	MAFUTA HALL	WMNM
7.	18/08/2021	MAFUTA HALL	WMNM
8.	30/08/2021	MAFUTA HALL	WMNM
9.	30/08/2021	BOARD ROOM	WMNM
10.	07/09/2021	BOARD ROOM	WMNM
11.	31/08/2021	BOARD ROOM	WMNM
12.	08/09/2021	MAFUTA HALL	WMNM
13.	09/09/2021	MAFUTA HALL	WMNM
14.	11/09/2021	DKT SHEIN HALL	WMNM
15.	20/09/2021	DKT SHEIN HALL	WMNM
16.	21/09/2021	DKT SHEIN HALL	WMNM

17.	22/09/2021	DKT SHEIN HALL	WMNM
18.	23/09/2021	DKT SHEIN HALL	WMNM
19.	24/09/2021	DKT SHEIN HALL	WMNM
20.	29/09/2021	BOARD ROOM	WMNM
21.	05/10/2021	BOARD ROOM	WMNM
22.	06/10/2021	BOARD ROOM	WMNM
23.	06/10/2021	BOARD ROOM	WMNM
24.	09/09/2021	DKT SHEIN HALL	WMNM
25.	15/10/2021	BOARD ROOM	WMNM
26.	18/10/2021	BOARD ROOM	WMNM
27.	22/10/2021	BOARD ROOM	WMNM
28.	27/10/2021	BOARD ROOM	WMNM
29.	05/11/2021	BOARD ROOM	WMNM
30.	05/11/2021	BOARD ROOM	WMNM
31.	07/11/2021	DKT SHEIN HALL	WMNM

Kwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati inatozwa kodi ya ardhi, na kwa kuwa Wizara na Taasisi za Serikali zinazotumia jengo hilo zinakaa bure, hivyo basi, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kutoilipisha Mamlaka hiyo kodi ya ardhi hadi hapo Wizara na Taasisi zinazotumia jengo hilo zitaanza kulipa kodi ya pango.

8. Mamlaka imekuwa ikiazimwa gari zake mara kwa mara kusaidia Taasisi nyingine katika shughuli za kila siku za ofisi hizo ikiwemo Idara ya Nishati, Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Kitendo hiki kimepelekea kuongezeka kwa gharama za kuzishughulikia gari hizo ikiwa ni pamoja na gharama za kuzifanyia “service” za kawaida na ununuzi wa “spea” mara kwa mara.

Kwa ujumla, Kamati ya LAAC haikuridhika na namna Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati inavyotumia gharama kubwa kwa ajili ya kulisimamia na kuliendeleza jengo lake kwa maslahi ya Taasisi nyengine, Taasisi ambazo pia huingiziwa fedha kwa

matumizi hayo. Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuyatekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Kamati hii kwa maslahi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati.

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA) – PEMBA

3.16.1 Vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la ghalani Shilingi 615,000

Ukaguzi umebaini kuwa kwamba jumla ya shilingi 615,000 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali lakini vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.

Kutokuingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunza vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Nambari ya Hati ya malipo	**Nambari ya Hundi**	**Fedha zilizolipwa (Tsh)**	**Aliyelipwa**	**Maelezo**
12/1 31/12/19	183	490,000	ZURA	Air cleaner 4pcs, Bearing 2pcs, Battery 1pc, Plug 1pc, Coil ya nje 1pc, Coil ya ndani 1pc, Locks 1pc, Seat cover 1 set.
6/3	183	125,000	ZURA	Air cleaner, Oil, hydrolic shokup, fore disk, roller, bolt and service charge.
Jumla		**615,000**		

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakiri kufanya malipo hayo halali na ilifuata taratibu zote za kisheria. Kwa hivi sasa Mamlaka imekuchukua jitihada za kuhakikisha kuwa vifaa vyote vilivyonunuliwa vimeingizwa katika daftari la Mtunza Ghala pamoja na kuhakikisha kuwa kosa hilo halitojirejea kwa mara nyengine.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hiyo Kamati ya LAAC ilibaini mambo yafuatayo:

1. Katika kipindi cha mwaka wa fedha husika hadi Kamati hii inafanya shughuli zake tarehe 25 Novemba, 2021, Mamlaka haina Mtunza Ghala (Storekeeper). Hivyo, shughuli za ghalani zinafanywa na mtu wa Utawala ambaye hana taaluma na masuala ya kutunza ghala.

2. Mamlaka inakabiliwa na tatizo la ufinyu wa nafasi, jambo ambalo limepelekea Mamlaka hiyo kushindwa kuajiri watendaji wa fani mbali mbali ambao wanahitajika kwa kuwa watendaji hao wakiajiriwa watakuwa hawana sehemu ya kukaa. Kutokana na kasoro hiyo watendaji waliopo hulazimika kutekeleza majukumu mbali mbali ingawa hawana taaluma nayo.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na changamoto zilizobainika Kamati ya LAAC imeishauri Mamlaka mambo yafuatayo:

1. Kuendelea na dhamira iliyonayo ya kujenga ofisi yake ili iweze kutekeleza malengo yake iliyokusudia pamoja na kufanya shughuli zao kitaalamu.

2. Kumtumia Mtunza Ghala aliyepo Unguja kufanya kazi na Pemba kwa kuwa kwa hivi sasa ni vigumu kwa Mamlaka kumuajiri Mtunza Ghala kutokana na ufinyu wa nafasi ya ofisi, sambamba na kuhakikisha kuwa hoja ya kutokuingiza vifaa katika daftari la ghalani kutokujirejea tena katika mwaka wa fedha 2020/2021.

3.16.2 Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslimu Shilingi 1,205,000

Jumla ya shilingi 1,205,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati. Ukaguzi umebaini kuwa malipo hayo yamefanywa kwa njia ya fedha taslim ambapo ni kinyume na taratibu za malipo.

Kufanya malipo kwa fedha taslim ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
07/08 05/08/2019	152	715,000	ZURA	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya vyombo vya moto.

12/1 31/12/2019	183	490,000	ZURA	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya vyombo vya moto.
Jumla		**1,205,000**		

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwamba Mamlaka hii ilifanya malipo ya matengenezo ya vyombo vya moto yaliyolipwa taslim, hata hivyo, Uongozi wa Mamlaka unaahidi kukakikisha kuwa malipo yote yatakayolipwa kwa wauza bidhaa na watoa huduma (suppliers) yatalipwa kwa njia ya "cheque" na "transfer".

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini mambo yafuatayo:

1. Malipo ya fedha yalifanyika baada ya Wahusika kupatiwa huduma husika, jambo ambalo ni kinyume na taratibu za fedha.
2. Gharama za fedha zilizotumika ni kubwa ukilinganisha na uhalisia wake. Hii ni kutokana na kuwa vyombo vilivyofanyiwa matengenezo (service) ni vitatu tu ambavyo ni vespa 1 na honda (kliki) 3. Aidha, vyombo hivyo vilikuwa ni vipya.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena, Kamati ya LAAC imeishauri Mamlaka kuhakikisha kuwa vyombo vya Serikali vinafanyiwa matengenezo katika Karakana ya Serikali.

3.17: MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali ya Mitaa na Mashirika ya Swerikali ya Mapinduzi Zanzibar (LAAC) ilipanga kufanya kazi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar tarehe 15 Novemba, 2021 hapo katika ukumbi wa mikutano uliopo katika jengo la 'Terminal Three'. Kwa bahati mbaya kazi hiyo haikufanyika kama ilivyopangwa katika ratiba ya Kamati kwa vile Wajumbe wa Kamati walichelewa kupatiwa majibu ya hoja zilizoelezwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya Serikali siku mbili kabla ya kikao ili waweze kupata muda wa kutosha kuipitia na hatimae kutoa mapendekezo muafaka (constructive recommendations) kwa Mamlaka kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Baraza, Toleo la 2020.

Kutokana na busara za Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC na Mwenyekiti wa Bodi wa Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, walijadiliana na kukubaliana kuipanga kazi hiyo ifanyike siku ambayo Kamati itakutana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba

tarehe 22 Novemba, 2021.

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umebaini mapato ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege yameongezeka hadi kufikia 17,372,432,528.56 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 14,542,276,472.72 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la shilingi 2,830,156,055.84 sawa na asilimia 16.29.

Majibu ya Mamlaka

Ongezeko hili la mapato limesababishwa na kuanzishwa kwa chanzo kipya cha mapato yatokanayo na ada ya ulinzi wa kiwanja (security fees) ambacho kilichangia jumla ya shilingi 1,709,835,966.05, Mchango wa Serikali kusaidia mishahara na gharama za uendeshaji kipindi cha mripuko wa maradhi ya Corona Tshilingi 1,437,448,944 na kuanzishwa ada ya utumiaji nyumba ya Mamlaka kwa upande wa Pemba (Pemba hospitality inn fees) ambayo ilitengeneza jumla ya shilingi 9,540,000.

Vianzio vyengine vya mapato vilishuka kutokana na athari ya mripuko wa maradhi ya corona. Jadweli lifuatalo linaonesha mchanganuo halisi wa mapato hayo:

Aeronautical Revenues:	2019/2020	2018/2019	VARIANCE
Cupps Revenues	1,085,401,640.00	1,073,334,616.40	12,067,023.60
Concession	568,914,039.12	616,505,454.80	(47,591,415.68)
Landing & Parking Fees	8,101,724,748.10	8,228,157,628.82	(126,432,880.72)
Safety Fees	484,134,000.00	396,318,000.00	87,816,000.00
Security Fees	1,709,835,966.05	-	1,709,835,966.05
Aeronautical Sub total	**11,950,010,393.27**	**10,314,315,700.02**	1,635,694,693.25
Non aeronautical Revenues:			
Advertisement charge	8,667,942.80	95,954,834.00	(87,286,891.20)
Airport car Parking	138,042,550.00	148,556,600.00	(10,514,050.00)
Concession Fees	138,821,405.00	195,554,692.88	(56,733,287.88)
ID Revenues	169,768,000.00	126,941,855.60	42,826,144.40
Interest Revenues	-	36,890,532.35	(36,890,532.35)
Misceleneous Revenues	180,671,605.00	104,368,820.99	76,302,784.01
Rental Fees	999,224,244.81	1,053,644,492.13	(54,420,247.32)
VIP charge	117,430,500.00	143,710,884.00	(26,280,384.00)
Pemba Hosspitality charge	9,540,000.00	-	9,540,000.00
Government grants	3,650,986,700.60	2,294,655,945.60	1,356,330,755.00
Other Income	229,187.08	27,682,115.15	(27,452,928.07)
Non aeronautical sub total	**5,413,382,135.29**	**4,227,960,772.70**	**1,185,421,362.59**
Total	**17,363,392,528.56**	**14,542,276,472.72**	**2,821,116,055.84**

Uchunguzi wa Kamati

Kamati baada ya kupitia hesabu ya mwisho wa mwaka ya Mamlaka, ilibaini sababu nyengine iliyosababisha kuwepo kwa tofauti katika mapato ya Mamlaka ni kuwepo kwa 'fixed deposit' ya milioni 24 na kupata riba ya shilingi 229,187.08 (other income) kwa

mwaka 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 27,682,115.15 kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
Kadhalika, Kamati ilihoji upungufu wa mapato katika chanzo cha matangazo ya kibiashara ambacho kiliporomoka kutoka 95.9 milioni kwa mwaka 2018 hadi 8.6 milioni kwa mwaka 2019 na kuelezwa kwamba hali hiyo ilitokana unafanywa na Mamlaka wa utengenezaji wa njia ya 'Terminal III' ulioharibu matangazo ya wafanyabiashara hao na Makampuni kukataa kulipa kodi stahiki. Aidha, Kamati iligundua kwamba changamoto hiyo imetokana na ukweli kwamba mikataba iliyopo haikuzingatia uharibifu wa matangazo ya wafanyabiashara hao jambo ambalo limeisikitisha kamati kwani kasoro hiyo inaweza kuisababishia Mamlaka/Serikali kulipa gharama nyingi zaidi iwapo ingeshitakiwa.

Vile vile Kamati ilitaka kujua kwanini mapato ya vitambulisho vya wafanyakazi wanaoingia katika Mamlaka kuwa yameongezeka kutoka shilingi 126.9 milioni (2018) hadi shilingi 169.7 milioni wakati mamlaka ilidai kukabiliwa na changamoto ya corona. Mamlaka ilieleza kwamba ongezeko hilo lilitokana na utaratibu uliopo wa vitambulisho hivyo kukatwa na makampuni mapema. Hivyo ilipoanza Corona tayari mapato yalikuwa yameshalipwa.

Kwa upande wa ongezeko la chanzo cha ukodishwaji wa mabasi ya kuwapeleka abiria katika ndege (Misceleneous Revenues). Watendaji wa Mamlaka walieleza kwamba awali huduma hiyo ilikuwa inatolewa na Mamlaka lakini kutokana na malalamiko na ushauri wa makampuni na wadau wengine ililazimika kukiondoa chanzo hicho kwa vile makampuni ya ndege yalitishia kuongeza nauli za ndege. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa kwa kuona nauli bado hazijapungua licha ya kuondolewa chanzo hicho na kuendelea kuwaumiza wananchi wanyonge wanaotumia usafiri wa ndege. Kamati ilichunguza zaidi na kubaini usafiri huo haupo badala yake ndege ndogo (za ndani) hivi sasa zinaegesha karibu na VIP ili kuepusha abiria kutembea masafa marefu.

Kamati ilihoji kwamba kukiondosha chanzo hicho cha mapato hakitaiingiza Mamlaka katika makosa kwa mujibu wa sheria zinavyoelekeza, na kuelezwa kuwa kimataifa usafirishaji wa abiria na mizigo yao hufanywa na makampuni na Serikali hubakia kutonza kodi tu, hivyo haitokuwa na athari katika utekelezaji wa sheria.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inakuwa makini inapoandaa mikataba yake ili kuepusha kukwazika katika utekelezaji wa majukumu yake.
2. Kwa vile usafiri wa mabasi hautumiki tena, Mamlaka ikae na Makampuni ya ndege kuangalia uwezekano wa kupunguza nauli ya ndege kwa abiria wetu.
3. Mamlaka ifuate sera, sheria na miongozo mbali mbali iliyopo katika utekelezaji wa majukumu.
4. Kutokana na unyeti wa Mamlaka katika upatikanaji wa mapato ya Zanzibar,

ihakikishe inabuni vyanzo bora vitakavyoongeza mapato zaidi.

Taarifa ya Matumizi

Ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia shilingi 17,947,277,332 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 17,539,920,118.14 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni ongezeko la shilingi 407,357,213.86 sawa na asilimia 2.3.

Majibu ya Mamlaka

Matumizi mengi yamefanyika chini ya makadirio isipokuwa kwa baadhi ya mafungu kama ifuatayo:

1. Gharama za usafiri (travelling cost) ambayo ilizidi bajeti kwa asilimia 11%, miongoni mwa sababu zilizopelekea kuongezeka kwa matumizi ya kifungu hiki ni malipo ya nauli na posho kwa walimu kutoka Tanzania bara kuja kufanya mafunzo ya ulinzi wa kiwanja, pamoja na gharama za wakaguzi kutoka Mamlaka ya Safari za Anga Tanzania kwa ajili ya ukaguzi wa kutoa vibali (Certification ya Kiwanja cha Kigunda).

2. Gharama za Thamani (Office furniture): kifungu hiki kimezidi bajeti kwa asilimia 65%, sababu iliyopelekea kuzidi huko ni kununuliwa kwa viti vya abiria kulikusababishwa na kuongezeka wageni kutoka Mashariki ya Ulaya.

3. Gharama za Bodi ya Wakurugenzi (Board facilitation cost): kifungu hiki kilizidi bajeti kwa asilimia 168% ukilinganisha na makadirio, sababu iliyopelekea kuzidiwa ni tatizo la mgawanyiko wa vifungu (code allocation), kwa kujumuishwa gharama nyengine za Bodi kama vile posho la wajumbe, gharama za chakula katika kifungu cha ada ya mwaka ya wajumbe wa Bodi (Director annual fees) iliyokuwa na bajeti ya Tzs. 12,000,000 badala ya kuingizwa kwenye vifungu vya posho na chakula. Hii imechangiwa na kuanza kutumia mfumo wa “Program base budget” na kutumia vifungu vya “GFS code” ambapo hapo awali hawakuwa wakitumia vifungu hivyo.

4. Msaada wa Kijamii (social support), kifungu hiki kilizidi bajeti kwa asilimia 106%, sababu zilizopelekea ni kufanyika sherehe ya kuzaliwa siku ya Mamlaka (Mamlaka day) pamoja na gharama za kushiriki kwenye michezo na kutoa misaada kwa wafungwa na watu wenye mahitaji katika kusherehekea siku ya kuzaliwa Mamlaka.

Uchunguzi wa Kamati

Baada ya kupitia taarifa za Mamlaka, Kamati iligundua kuwa bajeti yake imeongezeka maradufu ukilinganisha na uhalisia. Lakushangaza, Kamati haikufanikiwa kupata ithibativielelezo vya ongezeko hilo kitu ambacho kiliipa kamati wasiwasi katika

matumizi ya fedha zilizoongezeka kama ilivyoeleza mamlaka katika majibu yake. Hata hivyo, Kamati iligundua kuna tofauti ya fedha ilichangiwa na 'valuation report' yaan uchakavu wa mali za Mamlaka ambapo awali tathmini ilionesha uchakavu huo una thamani ya shilingi bilioni 6 lakini alipokuja Mdhibiti hakukubaliana na kiasi hicho. Hatimaye Mamlaka ilimtuma Mtathmini mwengine aliyebainisha kufikia shilingi bilioni 52

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inapofanya marekebisho ya bajeti yake inaishirikisha ipasavyo Bodi ya Mamlaka.

2. Mamlaka inapofunga hesabu zake za mwisho iingize tathmini sahihi ya gharama za mali zake.

Ufanisi katika uendeshaji wa Viwanja vya Ndege Zanzibar (Operating Performance)

Ukaguzi ulifanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka kwa kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa kuangalia taarifa za fadhe kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2019/2020.

Mamlaka imeendelea kujiendesha kwa hasara na kufikia kiasi cha shilingi 46,620,728,123 ukulinganisha na hasara ya shilingi 2,997,643,645.4 ya mwaka wa fedha ulioishia Juni 2019. Ukaguzi umebaini kuwa hasara ya shilingi 46,620,728,123 imeripotiwa kimakosa katika hesabu za fedha zinazoishia Juni, 2020 kutokana na makosa katika utiaji thamani wa majengo ya Mamlaka.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar inaendelea kujiendesha kwa hasara na kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilitengeneza hasara yenye jumla ya Shilingi 46,620,728,123.32, ongezeko la hasara limetokana na tathmini ya mali za Mamlaka (assets valuation), tathmini ambao ilifanywa katika mwaka wa fedha 2029/2020 kwa lengo la kutambua mali za Mamlaka pamoja na thamani zake.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa vile Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekiri kwamba kulikuwa na hasara katika uendeshaji wa shughuli zake. Kamati haikuwa na hoja zaidi.

Ufanisi katika uendeshaji wa kifedha (Financial Performance)

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlingano wa msimamo wa mtaji (Position of working Capital) wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar.

Ukaguzi umebaini uwiano kati ya mali za muda mfupi na madeni ya muda mfupi

umepungua kufikia 0.69:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2020 kutoka 1:4:1 kwa mwaka unaoishia Juni 2019.

Majibu ya Mamlaka

Ufanisi wa kifedha unaonesha kwamba uwiano wa mali za muda mfupi umepungia kutoka uwiano wa 1.42:1 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia uwiano wa 1.04:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia 2019/2020.

Uwiano huu, unaonesha kwamba bado Mamlaka inaweza kulipa madeni yake ya muda mfupi katika kipindi cha miezi 12 ijao.

Mamalaka inaendeleza juhudi za kukuza mapato ya Mamlaka na katika kutekeleza hayo, hatua zifuatazo zilichukuliwa:

1. Kuanzisha tozo mpya kwa ya "Airport security fees" ambayo inatarajiwa kuengeza mapato/makusanyo kwa zaidi ya asilimia 25% kwa mwaka.
2. Kuboresha vifaa vya usalama na miundo mbinu ya Mamlaka ili kuzishawishi Mashirika ya ndege kuongezeka safari zake katika viwanja vya Zanzibar na kupanuwa wigo wao katika utoaji huduma ikiwemo kuanza kuchukuwa mizigo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iliridhishwa na majibu ya Mamlaka na haikuwa na hoja zaidi.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.17.1 Kukosekana kwa mikataba ya ukusanyaji wa mapato

Mamlaka imeingia mikataba na watoaji huduma mbali mbali kwa lengo la kutoa huduma hizo na Mamlaka kupata mapato kupitia huduma hizo. Kutokana na mikataba ya makubaliano yao imebinika kukosekana kwa mapato yatokanayo na kodi pamoja na ada mbali mbali za viwanja vya ndege.

Ukaguzi haukuweza kupatiwa mikataba hiyo pamoja na jitihada mbali mbali zilizochukuliwa na kuitaka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuwasilisha mikataba hiyo kwa ajili ya ukaguzi.

Kushindwa kuwasilisha makubaliano ya mikataba iliyofungwa baina ya Mamlaka na watoa huduma hao, kumepelekea kutokujiridhisha juu ya usahihi wa mikataba hiyo, kima kinachopaswa kutozwa na kukusanywa, muda wa kuanza na kumalizika kwa makubaliano hayo na thamani halisi ya fedha inayopaswa kukusanywa kupitia mikataba hiyo.

Jumla ya watoa huduma 15 walilipwa bila ya mikataba. Mingoni mwao ni Arkia Israel,

Kenya Air Ways, Blue Panorama, Tui Fly Netherland, Air Italy pamoja na Smart Wings.

Majibu ya Mamlaka

Katika orodha ya wateja 15, wateja 14 hawastahiki kuwa na mkataba wa kodi ya pango (Rental lease agreement) kwasababu wateja hawa ni Mashirika ya ndege za kukodi (Charter flight) ambazo hawana ofisi katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume (AAKIA), wengi wao hupatiwa huduma aidha na Kampuni ya ZAT au Baadhi ya Kampuni za "Tour operator" kama vile Maha travel and Safris, Zanzibar Travel & Services, Flash tour na nyenginezo.

Kampuni ya Precession Air mkataba wake upo na uliwasilishwa kwa mkaguzi kwa ajili ya ukaguzi (Mkataba husika umeambatanishwa na ripoti hii).

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iliridhishwa na majibu yaliyoelezwa na Mamlaka. Hata hivyo haikurishishwa na mapungufu iliyoyabaini katika Mkataba wa Mamlaka na kampuni ya Precession Air hususan yakutotiwa saini na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka. Kamati baada ya kuupitia kwa undani mkataba huo, iligundua kwamba mkataba umesainiwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Biashara na masoko tarehe 10/2/2020 kinyume na Sheria ya Usimamizi wa fedha za umma ambayo inamtaka Mkuu wa Mamlaka (accounting Officer) ndio asaini kwa niaba ya Mamlaka.

Aidha, Kamati ilipohoji kuhusu kutopatiwa Mdhibiti mkataba huo kama inavyojiainisha katika hoja yake. Mamlaka ilithubutu kudanganya kwa kudai kuwa barua kutoka kwa Mdhibiti ya kutaka kuwasilisha majibu ya hoja (Management letter) ilichelewa kuwafika badala yake walipatiwa nakala ya barua waliyoifuata Ofisini kwa Mdhibiti ya tarehe 10/3/2021 yenye kumbukumbu nambari ZAA/FE/04/06 VOL.17 wakati Mdhibiti alieleza barua ilifika ndani ya wakati unaotakiwa.

Kutokana na utata huo, Kamati ilifuatilia barua halisi (original letter) pamoja na 'dispatch' ya uletwaji wa barua hiyo na kugundua kwamba maelezo ya Mamlaka hayakuwa na ukweli wowote kwani barua iliwafika mapema tarehe 14 January, 2021 yenye kumbukumbu nambari AUD/UMU/MVN/16/1/VOL.I/1.

Kamati haikuridhishwa na majibu hayo ya udanganyifu yaliyotolewa na Watendaji wa Mamlaka kwani imeipa shaka Kamati juu ya usahihi wa majibu wanayoipatia Kamati.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inapohoji watendaji wa Mamlaka wanatakiwa watoe majibu yaliyosahihi kinyume na hivyo kunaweza kumtia hatiani Mtendaji kwa kosa la jinai la kuidanganya Kamati kwa mujibu wa sheria ya kinga, Uwezo na Fursa za Wajumbe namba 4 ya mwaka 2007.

3.17.2 Kutowasilishwa mikato ya kodi na michango ya ZSSF ya wafanyakazi kwa wakati shilingi 639,932,727

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ukaguzi umebaini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetayarisha malipo ya mishahara ya wafanyakazi wake kwa mwezi unaoishia tarehe 30 Juni, 2020. Mamlaka imefanya zuio la makato wa wafanyakazi wake yanayokatwa kutoka katika mishahara yao kwa lengo la kulipwa kodi pamoja na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Ukaguzi umebaini dosari ya malipo hayo kutokulipwa kwa wakati, jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha 7 na 81 cha Sheria ya Kodi ya mwaka 2004 pamoja na kifungu cha 9(1)(a)(c) cha sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakubaliana na Mkaguzi hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya Shilingi 398,985,027 ya Kodi ya Mshahara na Shilingi 240,947,700 Michango ya ZSSF haikulipwa kutokana na tatizo la ukosefu wa fedha.

Hata hivyo, mpaka kufikia tarehe 16 Juni, 2021 Mamlaka imeshafanya malipo yenye jumla ya Shilingi 141,669,381.70 kwa deni linalotokana na kodi ya mishahara pamoja na kufanya malipo yote ya kila mwezi (Julai, 2020 hadi Juni, 2021) na kwa upande wa ZSSF jumla ya Shilingi 206,246,900 zimelipwa kupunguza deni pamoja na kulipa michango iliyofuata ndani ya muda stahiki. (Nakala za stakbadhi za malipo zimeambatanishwa na ripoti hii).

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na Mamlaka kukiri kutokezea kwa kasoro kama ilivyoeleza Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo Kamati ilipitia vielelezo na kujiridhisha kufanyika kwa baadhi ya malipo hayo nje ya wakati wa ukaguzi na haikuwa na hoja zaidi.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inalipa deni lililobakia linalotokana na kodi ya mishahara pamoja na michango ya ZSSF.

2. Mamlaka iwe na mpango mzuri wa kulipa huduma inazopatiwa kwa wakati.

3.17.3 Kukosekana kwa nyaraka za uthibitisho wa mapokezi ya bidhaa zenye thamani ya shilingi 251,935,641

Ukaguzi umebaini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetumia jumla ya shilingi 251,935,641 kuwalipa watoa huduma mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa zinazotumiwa na Mamlaka. Dosari iliyobainika na wakaguzi ni kutokupatikana uthibitisho wa nyaraka (GRN) za upokeaji wa bidhaa hizo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma namba 11 ya mwaka 2016.

Kutokuwepo kwa nyaraka za uthibitisho wa mapokezi ya vifaa kumetokana na uwepo wa mazingira dhaifu ya udhibiti yaliyotajwa hapo juu yanaweza kutoa fursa ya udanganyifu.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imethibitisha kupokea kwa bidhaa na ufafanuzi wake unaoneshwa katika Jadweli lifuatalo:

Nam	Tarehe	Nambaya Vocha	Supplier	Fedha (Tzs)	Uthibitisho wa kupokelewa bidhaa
1	15/2/2020	73/2	Chituli	19.25m	D/O No. 1051
2	2/3/2020	20/3	Chituli	11.55m	D/O No. 1051
3	16/3/2020	101/04	Said Abdalla	12.651m	D/O No. 0668 & 0667
4	19/3/2020	116/03	Chituli	15.4m	D/O No. 1051
5	9/7/2019	54/8	Davot	16.89m	D/O No. 351
6	6/11/2019	42/11	Mohasha	10.7m	D/O No. 0262
7	5/1/2020	36/1	CM Electric	25.628m	D/O No.0205
8	30/6/2020	June	7stars	16.5m	
9	7/8/2019	43/8	Almas	14m	D/O No. 071
10	30/6/2020	June 2020	Almas	11.2	D/O No. 007
11	30/6/2020	107/4	Binyange	9.28m	D/O No. 030
12	26/4/2020	123/4	Binnyange	8.725m	D/O No. 035
13	9/7/2019	54/7	Binyange	11.93m	D/O No. 020
14	12/7/2019	65/7	Wazalendo	8.205m	
15	2/2/2020	2/12	mohasha	28.7m	D/O No.0266
16	28/2/2020	198/2	Mohasha	31.329m	D/O No.0267
Jumla				**251.936m**	

Uchunguzi wa Kamati
Kwa vile Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar ilikubaliana na hoja iliyoelezwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati haikuwa maelezo zaidi.

Mapendekezo ya Kamati
Mamlaka ihakikishe inafuata taratibu zote za kisheria zinazosimamia upokeaji, uingizaji na uondooaji wa mali za umma ili kuepusha upotevu wa mali hizo na hasara kwa Mamlaka.

3.17.4 Dosari katika uwasilishaji wa taarifa za Mamlaka shilingi 46,620,728,123

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha za Mamlaka na kubaini kufanyika kwa makosa katika tathmini ya majengo ya Mamlaka ambapo thamani yake iliporomoka kutoka shilingi 52,633,008,901 mpaka kufikia shilingi 7,347,669,639 kwa mujibu wa Ripoti ya Mtathmini wa Mali.
Aidha, ukaguzi ulifuatilia kwa kina mabadiliko hayo ya utiaji thamani na kubaini kwamba thamani ya jengo la awali ilikuwa 52,633,008,901 baada ya kutoa gharama za uchakavu ambayo pia ilikuwa na makosa kwa kujumuisha mali za kudumu nyengine zisizohusiana na jengo na kupelekea makosa katika ufananishaji wa vitu viwili visivyofanana.

Makosa hayo kwa kiwango kikubwa yamepelekea uwepo wa hasara inayotokana na kushuka kwa thamani kwa jengo na kuzifanya hesabu za Mamlaka kutoonesha sura halisi na sahihi.

Majibu ya Mamlaka
Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilitumia Idara ya Mitaji ya Umma iliopo kwenye Wizara ya Fedha na Mipango katika kufanya Tathmini ya Mali za Mamlaka, katika Ripoti ya Tathmini iliyowasilishwa na Idara husika ilionesha thamani kwa kila mali ya Mamlaka. Baada ya kupokea ripoti husika, Mamlaka ilifanya mlinganisho baina ya kumbukumbu za mali zinazooneshwa kwenye taarifa za fedha kabla ya tathmini na thamani ilioneshwa na mtathmini na tofauti zilizojitokeza zilihamishiwa kwenye ripoti ya fedha (Income and expenditure) ikiwa tathmini ya mali imeonesha hasara na kuhamishiwa katika ripoti ya mitaji ikiwa imeonesha faida, ufanyaji huu, umezingatia miongozo ya kimataifa ya kiuhasibu, kwa hivyo jumla ya shilingi 46,620,728,123 zilioneshwa kama ni hasara kwa Mamlaka kwa kufuata miongozo husika.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Mamlaka ilikiri kujitokeza kwa changamoto hiyo ya kufanyika tathmini iliyokuwa na kasoro. Hata hivyo, Kamati ilihoji kwamba kwanini wasifanye wenyewe tathmini ya mali zao na kujibiwa kuwa Mamlaka ilikuwa haina mtaalamu wa kufanya tathmini hiyo.

Kutokana na majibu hayo, Kamati haikuwa na hoja ya ziada.
Aidha, Kamati imeielekeza Mamlaka ijipange vizuri kuajiri Mtathmini wa mali za Mamlaka ili kujiepusha na hoja kama hiyo kujirudia tena katika kipindi chengine.

3.17.5 Kukosekana kwa mikataba ya ujenzi na utoaji huduma yenye thamani ya shilingi 382,649,624

Ukaguzi umebaini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanya malipo ya jumla ya shilingi 125,531,200 kwa ajili ya kumlipa mkandarasi Ockra Constructuion Company Ltd. Kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kushukia na kurukia ndege (Airstrip) ya Uwanja mdogo wa ndege uliopo Nungwi (Kigunda).
Aidha, ukaguzi umebaini Mamlaka imefanya malipo ya jumla ya shilingi 257,118,424 kwa ajili ya kumlipa "Mohasha General Supplier" mtoa huduma za usambazaji wa vifaa na vitu mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka bila ya kuwepo kwa mkataba uliosainiwa kwa ajili ya usambazaji wa vifaa hivyo.

Majibu ya Mamlaka
Mamlaka inakubaliana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwamba kampuni ya Ocra Construction Company Ltd (Shilingi 125,531,200) haikuwa na mkataba na Mamlaka, kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha ndege cha Nungwi, sababu iliyopelekea hivyo ni kwamba, Mkandarasi Mkuu wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Nungwi alikuwa Kampuni ya Cosmo Map ambayo ilipatiwa zabuni kwa njia ya dharura (emergency procurement) ambapo, baadhi ya kazi, ziliilazimisha Mamlaka kutumia Wazabuni wengine kama Ocra Construction kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa kiwanja ambao ulitakiwa kukamilika kabla ya kuanza sherehe za Mapinduzi za Januari, 2020.

Kuhusiana na malipo ya Kampuni ya Mohasha General Supplies yenye jumla ya Shilingi 257,118,424 ni kweli kwamba malipo hayo kwa ujumla yake hayakuwa na mkataba wenye thamani ya malipo hayo kwasababu fedha zenye thamani ya shilingi 257,118,424 zililipwa kwa kazi na huduma tofauti na wakati tofauti kwa mwaka mzima wa fedha 2019/2020.

Hivyo, utaratibu wa manunuzi uliokuwa ukifuata kwa muamala mmoja mmoja kwa wakati husika iliokuwa ni ununuzi kwa njia ya "Local Purchase Order" ambao hauhitaji kuwa na mkataba wa kila muamala isipokuwa kunatakiwa kuwepo na "quotation 3" kutoka kwa watoa huduma, vigezo husika vilitimizwa kwa sehemu ya malipo yaliyofanyika ambao kwa ujumla wake kwa mwaka yalikuwa na thamani kama ilivyoanishwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati
Kwa vile Mamlaka ilikubaliana na hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

Serikali, Kamati haikuwa na hoja kuhusiana na majibu ya Mamlaka.

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE - PEMBA

3.17.6 Kushindwa kufikia malengo ya kukusanya mapato shilingi 618,378,900

Jumla ya shilingi 618,378,900 zilikadiriwa kukusanywa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ukaguzi umebaini kwamba makadirio hayo ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 324,089,485 zilikusanyw sawa na asilimia 52.4 ya makadirio ambapo hali hiyo inaonesha Mamlaka imeshindwa kufikia lengo la makusanyo.
Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 32(1)(2) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka
Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba ilipangiwa kukusanya mapato ya Shilingis 618,378,900 lakini hadi kufikia tarehe 30 June, 2020 Mamlaka ilikusanya mapato ya Shilingi 324,089.485 ambazo ni sawa na asilimia 52.4%. Upungufu wa mapato umetokana na kushindwa kukusanya mapato kutoka vianzio vipya vya mapato ikijumuisha ada ya ulinzi na tozo ya mfumo wa abiria na vile vile kupungua kwa safari za ndege kwa upande wa Pemba kulikosababishwa na athari ya janga la maradhi ya ‘corona’ pamoja na kupungua safari za ndege za Kampuni ya Tropical na Zan air ambazo zinaonesha dalili za kushindwa kuendelea na kutoa huduma za usafiri wa anga.

Uchunguzi wa Kamati
Kamati ilitaka kujua kulikuwa hakuna sababu nyengine iliyosababisha makisio kuwa makubwa zaidi na kuelezwa kwamba Mamlaka ilifanya makisio makubwa ya chanzo cha mapato ya ‘hospitality charge’ ya shilingi 324,089,485 (iliyooneshwa katika kitabu cha Mdhibiti) dhidi ya shilingi 241,521,675.00 ilizodai Mamlaka. Kutokana na hilo, Kamati ilitaka uthibitisho wa kuwepo kwa tofauti ya makisio hayo, hata hivyo ilishindwa kuithibitishia Kamati usahihi wa shilingi 241.5 milioni kuwa ndio fedha sahihi. Kuwepo kwa tofauti hiyo ilisababisha makosa katika uandaaji wa hesabu ya mwisho na kushindwa kutoa hesabu sahihi na halisi ya Mamlaka.

Mapendekezo ya Kamati
Mamlaka iwe na utaratibu mzuri wa kuandaa makisio ya makusanyo yake kuepusha ubabaifu katika utekelezaji wake.

3.17.7 kukosekana kwa uthibitisho wa uletwaji wa vitabu vya kukusanyia mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba inapaswa kukusanya mapato katika maeneo ya Mamlaka kwa mujibu wa sheria. Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka imepokea vitabu vya mapato kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar bila ya kuwepo kwa uthibitisho wa uletwaji na mapokezi ya vitabu hivyo, aidha ukaguzi umeshindwa kujua jumla ya vitabu halisi vya mapato vilivyopokelewa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.
Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka
Utaratibu wa kupokea vitabu vya risiti unatekelezwa kwa mujibu wa taaratibu na sheria za fedha. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa upande wa Pemba, ina utaratibu wa kusajili vitabu vya risiti na kuingiza kumbukumbu zake katika daftari maalum (Counterfoil Register) ambazo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya vitabu 40 vilipokelewa na kusajiliwa kwenye daftari.

Uchunguzi wa Kamati
Pamoja na Mamlaka kukiri kuhusu kutokuwepo kwa uthibitisho unaoonesha vitabu vya risiti vilivyopokelewa, Kamati ya LAAC imeungana na hoja hii iliyomo katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali na kukubali kwamba hoja haijajibika. Hata hivyo, Kamati imegundua kuna uwekwaji mbaya wa kumbukumbu usiozingatia maelekezo ya sheria.

Mapendekezo ya Kamati
Mamlaka iweke kumbukumbu zake vizuri ili wakaguzi wanapopita waweze kuzikagua.

3.17.8 Mamlaka kushindwa kukusanya mapato ya shilingi 65,609,020

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba hutoa huduma kwa kampuni mbali mbali za ndege ambapo hulazimika kukusanya mapato kutoka kwa kampuni hizo. Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka imeshindwa kukusanya jumla ya shilingi 65,609,020 kutoka kwa kampuni za ndege mbali mbali ambazo zilipatiwa huduma katika uwanja wa ndege wa Pemba. Jadweli lifuatalo linaonesha:

Nam.	Mtoa huduma	Jumla ya Fedha (Tzs.)
1.	Assalaam Air	47,804,380
2.	Zan Air	10,785,440
3.	Coastal Air	7,019,200
	Jumla	**65,609,200**

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka kupitia kiwanja cha Ndege cha Pemba kinaendelea na juhudi za kukusanya madeni kutoka kwa wateja waliopatiwa huduma na Mamlaka. Hatua hizi zimeonesha mafanikio kwani jumla ya shilingi 37,804,640 zimeshakusanywa kutoka kwenye deni lililoorodheshwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu na deni lililobakia ni shilingi 27,804,380 ambalo Mamlaka inaidai Kampuni ya Assalam Air.

Mamlaka imefikia makubaliano na kampuni husika kufanya malipo ya shilingi 3,500,000 kwa wiki.

Uchunguzi wa Kamati

Mbali na juhudi zilizochukuliwa na Mamlaka kuhakikisha baadhi ya deni linalipwa lakini Kamati imegundua kwamba deni hilo limelipwa nje ya mwaka wa ukaguzi (2019/2020) na Kamati haikupata sababu za msingi zilizoonesha juhudi za Mamlaka kufuatilia deni hilo kwa wakati huo pamoja sababu za kushindwa kampuni hizo kulipa madeni yao.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka ihakikishe inafuatilia madeni yake na hatimaye yanalipwa ndani ya wakati husika.

3.17.9 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu bila ya kulipwa shilingi 130,542,607

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba huingia katika makubaliano ya ununuzi wa bidhaa na huduma mbali mbli kutoka kwa wafanyabiashara tofauti na Taasisi za Serikali kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba inadaiwa na wafanyabiashara na Taasisi za Serikali jumla ya shilingi 130,542,607 kutokana na kupatiwa bidhaa na huduma mbali mbali. Aidha, madeni hayo ni ya muda mrefu. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika Jadweli lifuatalo:

Nam.	Jina la Mdai	Fedha anazodai (Tzs.)
1.	AKB Cleaning Enterprises	15,200,000
2.	RK General Supplier	25,000,000
3.	Nassor Said Nassor	15,481,000
4.	Fatah Moh'd Ali	5,000,000
5.	Rashid M. Soud	22,573,000
6.	Mbarouk Salim Ali	5,263,980

7.	Adam Store	3,268,000
8.	Asaa Kheri Asaa	1,495,070
9.	Misufini Stationary	4,562,000
10.	Juma Enterprises	907,500
11.	Ali Sarhan	362,500
12.	Rashid Auto Spares	826,000
13.	ZECO	7,752,775
14.	ZAWA	22,850,782
Jumla		**130,542,607**

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka hadi kufikia tarehe ya kuandaa hesabu ilikuwa na deni husika lenye thamani ya shilingi 130,542,607 lakini hadi kufikia mwezi wa Julai 2021, Mamlaka imeshalipa jumla ya shilingi 72,377,607 na limebakia deni lenye thamani ya shilingi 58,165,000, Deni hili linakusudiwa kulipwa katika kipindi cha miezi 3 kuanzia mwezi Agosti, 2021.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati imegundua kuwa deni kweli limelipwa nje ya wakati wa ukaguzi na bado deni halijamalizika hadi Kamati inakamilisha ukaguzi wake. Aidha, Kamati imebaini kuna makosa katika kuripoti jumla ya deni linalodaiwa kwani Mdai Rashid M. Soud hakuwa anadai shilingi 22,573,000 kama ilivyoripotiwa badala yake alikuwa anadai shilingi 12,572,000 na kufanya jumla ya fedha inayodaiwa na Mamlaka kuwa shilingi 120,542,607 badala ya shilingi shilingi 130,542,607. Kamati haikukubaliana na maelezo hayo kwa vile haikupokea kielelezo chochote kinachothibitisha usahihi wa wanachokieleza.

Mapendekezo ya Kamati

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) awe makini anaporiti hesabu zake ili kuondoa mgongano baina ya Mkaguzi huyo na Mkaguliwa zinapopita Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Mamlaka ihakikishe inakamilisha malipo ya madeni yake ndani ya wakati stahiki.

3.17.10 Hati za malipo zilizokosa vielelezo shilingi 95,636,945

Jumla ya shilingi 95,636,945 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba. Ukaguzi umebaini kwamba kutokuambatanishwa kwa baadhi ya vielelezo vya matumizi katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.
Miongoni mwa malipo yaliyokosa vielelezo ni shilingi 6,000,000 alizolipwa RK General Traders Co. Ltd. kwa ajili ya malipo ya awamu ya mwanzo ya ukarabati ya ukumbi wa mikiutano, jiko na vyoo, shilingi 10,000,000 alizolipwa Ibrahim Mkubwa Abdalla kwa ajili ya malipo ya awamu ya pili na ya mwisho ya matengenezo ya nyumba ya wafanyakazi pamoja na shilingi 2,500,000 zilizolipwa kwa M/V/Ndege Pemba ikiwa ni malipo ya usafishaji wa maeneo mbali mbali ya kiwanja cha ndege uliofanywa na na kikundi cha Nguvu kazi cha Mfikiwa Chake chake.

Majibu ya Mamlaka
Vielelezo vya marejesho ya gharama viliwasilishwa kwa wakaguzi lakini kutokana na tatizo la kutokurejea kwa mara ya pili kufanya uhakiki wa hoja za ukaguzi, kulipelekea hoja hii kubakia katika kitabu cha hoja.

Uchunguzi wa Kamati
Pamoja na Mamlaka kukiri juu ya kutowasilishwa vielelezo wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua kwanini suala hilo lilitokezea na kuelezwa kwamba Mamlaka ilipitikiwa. Hivyo, Kamati ilishitushwa na haikuridhishwa na jawabu hilo kwani linaweza kutoa mwanya kwa wafanyakazi wasiokuwa waaminifu kutumia fursa hiyo kujinufaisha wao wenyewe.

Mapendekezo ya Kamati
Kamati iandae mfumo mzuri wa uhifadhi wa kumbukumbu zake kwani taratibu zinataka vielelezo ipatikane mara tu baada ya kukamilika utoaji huduma.

3.17.11 vifaa ambavyo havikurikodiwa ghalani shilingi 16,524,383

Jumla ya shilingi 16,524,383 zimelipwa kwa ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba. Ukaguzi umebaini kwamba vifaa vilivyonununuliwa havikuingizwa katika daftari kwa kutunzia vifaa ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Miongoni mwa vifaa ambavyo havikurikodiwa ghalani ni pamoja na vifaa vya ujenzi, ununuzi wa vifaa vya kuandikia, ununuzi wa kioo cha basi SMZ 127A, ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya trekta SMZ 129B, mafuta, vifaa vya usafi pamoja na matengenezo ya mashine.

Majibu ya Mamlaka

Vielelezo vya marejesho ya gharama viliwasilishwa kwa wakaguzi lakini kutokana na tatizo la kutokurejea kwa mara ya pili kufanya uhakiki wa hoja za ukaguzi, kulipelekea hoja hii kubakia katika kitabu cha hoja.

Uchunguzi wa Kamati

Mamlaka haikukubaliana na majibu hayo kwa vile Mamalaka ilitakiwa kuchukua juhudi za kutosha kuhakikisha vielelezo hivyo vinamfika Mkaguzi ndani ya muda wa mwezi mmoja baada ya kumaliza ukaguzi wake hasa ukizingatia tayari ameshaionesha Mamlaka kasoro zilizojitokeza, hata hivyo Kamati iligundua kwamba kwasasa changamoto hiyo Mamlaka imeshairekebisha kwa kuviingiza vifaa vyote vilivyoorodheshwa kuwa havikuingizwa katika daftari la ghalani nje ya muda wa ukaguzi.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka ifuate sheria zinavyoelekeza sio katika uingizaji wa vifaa tu ghalani lakini hata katika utoaji wa vifaa hivyo.

3.17.12 malipo ya fedha kwa wafanyakazi ambao hawakusajiliwa shilingi 74,525,422

Jumla ya shilingi 74,525,422 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Pemba kwa wafanyabiashara tofauti. Ukaguzi umebaini kwamba wafanyabiashara hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya Zanzibar ili kuweza kufanya biashara na taasisi za Serikali.

Miongoni mwa wafanyabiashara hao waliokuwa hawajasajiliwa ni pamoja na RK General Traders Co. ltd, Jumsa Enterprises, Hafka Company Ltd, Suleiman Seif Rashid, Ibrahim Mkubwa Abdalla, Kassim Ali Suleiman, M/V/Ndege - Pemba, Issa Hababu Khalfan pamoja na Sheby Enterprises.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar namba 11 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Manunuzi yaliyofanyika kwa wafanyabiashara waliokuwa hawajasajiliwa kwa mujibu wa taratibu, tatizo hili zaidi ya asilimia 90% limetokana na kuwatumia wajasiriamali wadogo na wasanii ambao walishiriki katika shughuli za kutoa burudani katika kipindi cha kusheherekea siku ya kuzaliwa Mamlaka (Mwezi Agosti, 2020). Hata hivyo, Mamlaka inakusudia kuweka utaratibu maalum wa kuondosha/kupunguza utumiaji wa wajasiriamali wadogo na wasanii ambao hawatakuwa wamesajiliwa kwa mujibu wa sheria za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na Mamlaka kukiri kuwa waliwatumia wafanyabiashara waliokuwa hawajasajili na Mamlaka husika, Hata hivyo Kamati ilitaka kujua sababu iliyopelekea Mamlaka kufanya hivyo na kuelezwa kwamba Mamlaka walikuwa hawana uelewa wa matakwa ya sheria juu ya kuwatumia wafanyabiashara waliokuwa wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Kamati ilishangazwa na kutofurahishwa na kitendo hicho hasa ukizingatia kwamba Mamlaka inaye Mwanasheria na Sheria ya Manunuzi ipo takea 2016. Sambamba na hilo, kuna kodi ambayo Serikali ingeweza kuipata kwa kuwatumia wafanyabishara waliosajiliwa ila Mamlaka imesababisha mapato hayo kukosekana. Aidha, Kamati ilibaini kuwa wajasiriamali waliokuwemo katika orodha hiyo bado hawajapatiwa usajili hadi Kamati inamaliza ukaguzi hususan vikundi vya sanaa.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inatumia wafanyabiashara waliosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili Serikali ipate kodi itakayotumika kuwaletea maendeleo wananchi wetu.

2. Mamlaka iwe na desturi ya kuipitia barua pepe 'website' ya Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili kufahamu wafanya biashara waliosajiliwa kila wanapotaka kuingia nao mikataba.

UKAGUZI WA MRADI WA MAENDELEO WA UJENZI WA UWANJA WA NDEGE WA NUNGWI.

Wakati Kamati ya LAAC inafanya ukaguzi wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tarehe 24 Januari, 2022 iliona kuna haja ya kuutembelea na kuukagua mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege uliopo Nungwi ili kujionea kama thamani halisi ya matumizi ya fedha za Serikali imepatikana (value for money). Katika ukaguzi wake, kamati iligundua mambo yafuatayo:

1. Mradi huo ulianza mwaka 2019 na kuzinduliwa tarehe 10 januari, 2020 ambao awali ulikuwa ukiitwa Uwanja wa ndege wa Kigunda ambao ulikuwa unagharamiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ila kwasasa mradi huo unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

2. Kuna jumla ya shilingi bilioni 2,752,319,873.15 zilitumika kwa ujenzi kwa awamu tatu, ambapo awamu ya kwanza ilitumia shilingi bilioni 1,361,760,769.04 kwa kazi ya za usafishaji na ujenzi wa barabara kutoka barabara kuu hadi katika kiwanja wakati awamu ya pili ilitumia shilingi bilioni 1,050,646,450.00 kwa kazi ya huduma za usimamizi wa mradi, kumalizia kazi zilizobakia katika awamu ya

kwanza pamoja na ununuzi wa taa za 'solar' na awamu ya tatu ilitumia shilingi milioni 339,912,654.11 kwa kufanya ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka, kibanda cha walinzi, kituo cha Zimamoto, uvutaji umeme na gharama za fidia.

3. Bado Mradi haujapatiwa hatimiliki ya eneo lake ambapo awali Mradi ulikuwa na urefu wa kilomita mbili na nusu (2.5 km) na upana wa mita 40 na kuahidiwa kuongezwa

4. Mradi huu unahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa aina ya code 3C kwa kuzingatia mpango wa maendeleo ya uwanja na unatarajiwa kuwa na maegesho ya ndege mawili (apron) yatakayoweza kuhudumia ndege kumi na tano (15) kwa wakati mmoja, njia tatu za kupitia ndege (taxiway), jengo la abiria lenye uwezo wa kuhudumia abiria 1,100 kwa wakati mmoja na abiria 600,000 kwa mwaka, na huduma nyengine muhimu kwa mujibu wa viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

5. Kamati imegundua kwamba kuna eneo dogo tayari limeshatiwa lami laini na eneo kubwa bado halina lami yoyote.

6. Kamati pia imebaini kwamba uwanja hauna baadhi ya miundombinu muhimu itakayosaidia kutekeleza majukumu yake ipasavyo yakiwemo majengo na vifaa.

7. Kamati imebaini kuwa Mradi unakabiliwa na changamoto ya wananchi kupita katika eneo la uwanja licha ya juhudi zilizochukuliwa na uongozi wa kiwanja ya kuwatengenezea njia mbadala.

8. Kamati imegundua kuna ujenzi unaendelea na harakati za kilimo zinafanyika karibu na eneo la kiwanja, jambo ambalo linatishia kuvamiwa kwa kiwanja hicho na kuondoa taswira ya kuwa na kiwanja bora chenye sifa zote.

9. Kamati imegundua kwamba Uwanja huo haujitegemei unasimamiwa na Uwanja wa ndege wa Amani Abeid Karume kwani malipo yanafanywa kupitia. Aidha, mawasiliano na ruhusa ya kutua au kuruka ndege nayo yanatoka Makao Makuu yao.

10. Kamati imegundua kwamba uwanja unatoa huduma masaa 12 lakini eneo lake halina ulinzi wa uhakika kama inavyotakiwa kwa viwanja vya ndege vya kitaifa na kimataifa jambo ambalo linaweza kupelekea kufanyika kwa uhalifu.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ilitaka ipatiwe vielelezo vya Mikataba na uchambuzi wa matumizi ya fedha zote zilizotumika kwa mwaka 2019/2020 ili kujiridhisha na matumizi ya mradi huo.

Mapendekezo ya Kamati

1. Uongozi wa Uwanja uhakikishe unaharakisha kukamilisha ujenzi wa uwanja huo ili uweze kukamilika na kutoa huduma hususan kwa watalii.
2. Kamati iendelee kutoa elimu kwa wananchi wanaokaa karibu na maeneo hayo ili kuzuia wasiwe wanaingia katika uwanja.
3. Uongozi wa Uwanja uhakikishe unalidhibiti ipasavyo eneo lao ili kuepusha uvamizi kutoka kwa watu wa nje.
4. Uongozi ufuatilie hatimiliki ya eneo wanalolimiliki katika Taasisi husika.
5. Uongozi wa uwanja wa ndege uhakikishe kunakuwa na ulinzi wa uhakika kwa abiria na mali zao katika muda wote wa huduma.
6. Serikali iupatie Uwanja miundombinu itakayousaidia kutekeleza majukumu yake.

3.14: SHIRIKA LA MAGAZETI

Taarifa za Mapato

Shirika la Magazeti lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 838,900,000/= katika kipindi cha mwaka 2019/2020 kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato na shilingi 845,192,395/= ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia tarehe 30 June, 2020 jumla ya shilingi 935,260,525 zilikusanywa ambapo ni sawa na asilimia 111.5 ya makadirio na shilingi 632,994,425/= ya Ruzuku ilipokelewa kutoka Serikalini sawa na asilimia 75 ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Ongezeko hili la shilingi 96,360,525 ambalo ni sawa na asilimia 11.5 za makadirio lilitokana mrundikano wa madeni ambayo yalikuwepo kipindi cha mwaka 2018/2019 kwa taasisi mbali mbali hasa Taasisi za Serikali ambayo yalishindikana kulipwa mwaka huo wa fedha na kupelekea baadhi ya madeni hayo kulipwa ndani ya mwaka wa Fedha 2019/2020.

Pia, ongezeko hilo limetokana na makusanyo ya mauzo ya magazeti na matangazo katika matoleo maalum ya kupongeza maendeleo ya Rais Dk. Shein (1 Oktoba, 2019), Toleo maalum la miaka Tisa ya Dkt Shein, (30 Machi, 2020), Miaka 56 ya Muungano (26 Aprili, 2020), toleo la kumbukumbu ya Mzee Abeid Aman Karume (7 Aprili, 2020) na Toleo la Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar (12 Januari, 2020).

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Taarifa ya mapato ya Mkaguzi wa Hesabu za Ndani inafotautiana na Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement). Hii ni kutokana na kuwa Mkaguzi wa Hesabu za Ndani taarifa zake alizipata kupitia bango kitita lililowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
2. Shirika lilianzisha kianzio kipya cha mapato katikati ya mwaka, ambapo Shirika lilikifanyia makadirio kianzio hicho na wakayajumuisha na makadirio ya awali ya mapato jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa kibajeti.
3. Mkaguzi wa Hesabu za Ndani hana uhakika kama taarifa yake aliwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama Sheria ya Fedha inavyoelekeza.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kutatua kasoro zilizobainika na Kamati hii, yafuatayo yalipendekezwa:

1. Mkaguzi wa Hesabu za Ndani ahakikishe kuwa anapata taarifa za fedha kwenye vianzio vya uhakika ili apate taarifa sahihi.
2. Mkaguzi wa Hesabu za Ndani ahakikishe kuwa anatekeleza majukumu yake kama Sheria na Kanuni za nchi zinavyoelekeza.
3. Endapo Shirika litapata kianzio kipya cha mapato katikati ya mwaka, basi kianzio hicho makadirio yake ya mapato yasijumuishe kwenye makadirio ya awali ya mapato na badala yake mapato halisi ya kianzio hicho yajumuishwe kwenye mapato mengineyo, na ikiwa kianzio hicho kitaendelea kuwepo kwenye mwaka unaofuata basi kianzio hicho kitapaswa kupewa kifungu chake.

Taarifa za Matumizi

Shirika la Magazeti lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,559,592,395 kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya 1,297,644,216.6 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 83 ya makadirio.

Majibu ya Shirika

Matumizi ya Shirika la Magazeti yameonekana kupungua kutoka shilingi 1,559,592,395 iliyoidhinishiwa kwa kazi za kawaida, ambapo hadi kufikia Juni, 2020 shilingi

1,297,644,216.6 zilitumika sawa na asilimia 83 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 261,948,178.6 sawa na asilimia 17 ya mapungufu. Hii ni kutokana na kupungua kwa Ruzuku kutoka Serikalini.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ina mapungufu mbali mbali kwa mfano; kifungu cha "Other Payment" kina maelezo "Note" zaidi ya moja ndani ya Taarifa moja ya Hesabu jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa ufungaji wa hesabu. Kifungu hiki kimeelezwa kama ni "Note" 5, 11 na 12.
2. Kamati ya LAAC ilishitushwa na hali hiyo na hasa ikizingatiwa kuwa Taarifa hiyo pia huwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama kifungu cha 121(1) cha Sheria ya Fedha kinavyoelekeza na endapo Mdhibiti atagundua kasoro yoyote basi huitaka Taasisi husika kufanya marekebisho juu ya Taarifa hiyo. Hata hivyo, Kamati ya LAAC bado ilibaini kasoro mbali ya Taarifa hiyo husika ingawa ilipitia katika maeneo tofauti.
3. Taarifa ya mwaka ya Mkaguzi wa Hesabu za Ndani haikuelezea taarifa za matumizi za Shirika na badala yake ilielezea mapato ya Shirika tu. Kasoro hii imeitia mashaka Kamati hii hasa ikizingatiwa kuwa taarifa za Mkaguzi wa Hesabu za Ndani wa Taasisi husika huwasilishwa Hazina (Treasury) ambaye ni kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mujibu wa kifungu cha 117(6) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016 ambaye kwa utaratibu wao wa ndani huiwasilisha taarifa hiyo kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani "Internal Auditor General" ambaye kwa mujibu wa kifungu cha 116(2)(f) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 ana jukumu la kuishauri Serikali juu ya hatua za kuchukua kuhakikisha thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali.

Sambamba na hilo, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kwa mujibu wa kifungu cha 11(2)(h) ana jukumu la kupitia, kutathmini na kupendekeza juu ya mfumo wa usimamizi na ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali.

Hivyo, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kupatiwa taarifa ambazo hazina matumizi au taarifa zake zinatofautiana na uhalisia uliopo kunaweza kumpelekea kutoa ushauri ambao sio sahihi kwa Serikali na kunaweza kutia hasara Serikali.

1. Mhariri Mtendaji wa Shirika alikuwa Mjumbe na Katibu wa Bodi ya Shirika hili, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

2. Kutokana na majukumu mengi na mazito ya Mhariri Mtendaji kumbukumbu za Vikao vya Bodi zilikuwa haziandikwi kwa usahihi wake.
3. Mhasibu wa Shirika hana msaidizi.
4. Shirika linatumia fedha nyingi kuchapisha gazeti hilo.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro zilizobainika Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Shirika lihakikishe kuwa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka inaandaliwa kama taratibu za ufungaji hesabu zinavyoelekeza kitaifa na kimataifa.
2. Mkaguzi wa Hesabu za Ndani ahakikishe kuwa taarifa zake anazoziandaa zinakidhi vigezo vyote vilivyokusudiwa kwa lengo la kuisaidia Serikali katika kusimamia rasilimali zilizopo katika Taasisi husika
3. Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani ahakikishe kuwa anazifanyia kazi ipasavyo taarifa zote zinazowasilishwa kwake na Wakaguzi wa Hesabu za Ndani kutoka katika Taasisi mbali mbali ili tija ya kuanzisha Kitengo hicho kiweze kupatikana.
4. Bodi za Wakurugenzi za Shirika na Taasisi Zinazojitegemea zihakikishe kuwa inatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo na sio kutekeleza shughuli zao kwa maslahi yao binafsi.
5. Serikali ilinunulie Shirika mtambo wa kuchapia magazeti ili kupunguza gharama za uchapaji.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA SHIRIKA LA MAGAZETI

Shirika la Magazeti ya Serikali limebadilisha namna ya ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka kutoka katika Mfumo wa “Accrual Basis” na kuingia katika mfumo wa “Cash Basis”, jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shuhuli za Shirika kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyopo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa Shirika kifaida au hasara.

Majibu ya Shirika

Shirika la Magazeti ya Serikali limeundwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii na sio kwa ajili ya biashara. Hata hivyo, kufuatia miongozo mbali mbali kutoka Serikali Kuu, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Shirika lilipokea agizo la kuingia katika Mfumo wa “Cash Basis” katika ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ili tuwe na uwiano na

mfanano wa ufungaji wa hesabu kwa Taasisi zote za Serikali, barua yenye kumbukumbu Namb. AD.5/184/01/07/18 inahusika.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikubaliani na agizo la Serikali kupitia Afisi ya Rais, Fedha na Mipango la kuzitaka Taasisi zake kufunga hesabu kwa kutumia mfumo wa "Cash Basis" badala ya mfumo wa "Accrual Basis".

Kamati hii haikubaliani na agizo hili kwa kuwa endapo utafunga hesabu kwa kutumia mfumo wa "Accrual Basis" kuna fursa ya kuonekana hali halisi ya kifedha iliyopo katika Taasisi husika. Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kulifuta agizo hilo na kuzitaka Taasisi zake kufunga hesabu zao kwa kutumia mfumo wa "Cash Basis" kutokana na sababu tulizozieleza hapo kabla. Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

3.14.1 Kutokufanya Kazi kwa Kamati ya Ukaguzi

Shirika la Magazeti bado halijaanzisha Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu (Audit Committee) na hivyo kutumia Kamati ya Ukaguzi iliyoanzishwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo jambo ambalo ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari ya kutokufanya kazi kwa Kamati hiyo na kupelekea kubainika mapungufu mbali mbali katika usimamizi wa ndani wa Shirika la Magazeti ya Serikali kama ifuatavyo:-

- Kutokujadili na kuidhinisha mpango mkakati wa mwaka wa ukaguzi wa ndani
- Kutokupitia taarifa za hesabu za Shirika la Magazeti ya Serikali
- Kutobainisha mapungufu ya ripoti ya ukaguzi wa hesabu wa Nje kwa lengo la kufanyia kazi mapungufu yaliyobainika na kulishauri Shirika ili liweze kujiendesha kwa tija.

Majibu ya Shirika

Shirika la Magazeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 liliendelea kutumia Kamati ya Ukaguzi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Mambo ya Kale, isipokuwa kwamba, Kamati hiyo haikuwahi kupitia taarifa za Ripoti za Mkaguzi wa Ndani. Changamoto hii ilifanya Shirika kuanza mchakato wa kufuatilia utaratibu wa kuunda Kamati ya Ukaguzi ya Shirika kama lilivyopokea ushauri kutoka kwa Mkaguzi wake wa ndani juu ya kuwepo kwa Kamati ya Ukaguzi ili kuweka ufanisi nzuri wa kupitia ripoti za Mkaguzi na kupelekea kuweka ufanisi nzuri wa kiutendaji.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Shirika na hasa ikizingatiwa kuwa mara tu baada ya Shirika hili kuanzishwa lilipaswa kuwa na Kamati yake na sio kuitegemea

Kamati ya Wizara.

Kutokana na maelezo yake hayo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa zinafuata Sheria na Kanuni za nchi ili kuepusha kasoro zisizo na msingi. Kwa mnasaba huo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

3.14.2 Manunuzi ambayo yamekiuka utaratibu Tsh, 102,364,625

Shirika la Magazeti limekuwa likigawa manunuzi ya bidhaa za vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ajili ya kuzuia kutumia njia sahihi ya ununuzi kama zilivyoelekezwa katika Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Hii imejitokeza wakati Shirika likifanya manunuzi ya vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano vilivoharimu shilingi 102,364,625.

Kufanya hivyo, ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:

Nam.	Nambari ya Hati ya Malipo	Aliyelipwa	Fedha zilizolipwa (Tsh)	Maelezo
1.	13/12, 18/12/2019	TLM Computer Service	11,970,000	Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kompyuta
2.	14/12, 18/12/2019	TLM Computer Service	27,930,000	Malipo ya ununuzi wa kompyuta
3.	15/12, 18/12/2019	TLM Computer Service	29,925,000	Malipo ya ununuzi wa kamera
4.	16/12, 18/12/2019	TLM Computer Service	13,965,000	Malipo ya ununuzi wa HP
5.	44/12, 18/12/2019	FTN Computer Service	10,124,625	Malipo ya ununuzi wa kompyuta saba
6.	1/11, 18/12/2019	FTN Computer Service	8,450,000	Malipo ya ununuzi wa HP laptop i5 3 GH1 TB 8 GB
JUMLA			**102,364,625**	

Majibu ya Shirika

Kufuatia agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia iliyokuwa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale ilionekana ipo haja ya kuanzishwa kwa gazeti la kiengereza. Hii ni kutokana na kuwa wageni kutoka Mataifa mbali mbali nje ya Nchi wanaotembelea na kukaribishwa Zanzibar hawapati habari sahihi kuhusiana na Zanzibar, ikiwemo habari za Kiuchumi, Siasa, Utamaduni, na Uwekezaji.

Kutokana na uharaka wa uzinduzi na uanzishwaji rasmi wa Gazeti la Zanzibar Mail pamoja na gharama kidogo zitakazotumika endapo Shirika hili halitofanya shughuli hiyo kwa kutoa zabuni. Shirika la Magazeti ya Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale iliomba muongozo kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali ya Serikali juu ya njia sahihi ya kununua vifaa hivyo kama Sheria ya Ununuzi inavyoekeleza. Kwa msingi huo, Mamlaka ya Ununuzi iliishauri Shirika kununua vifaa hivyo kwa njia ya "quotation" ili kuliwezesha Gazeti la Zanzibar Mail kuzinduliwa na kuanzishwa rasmi ndani ya muda uliopangwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ililiridhia Shirika hili kufanya ununuzi wa vifaa vya Gazeti la Zanzibar Mail kwa njia ya nukuu iliyogharimu jumla ya Tsh. 88,000,000 kufuatia barua ya tarehe 13 Novemba, 2019 yenye kumbukumbu Namba MMUM BA.370/383/02/27. Vifaa hivyo, ni kama vinavyoonekana kwenye jadweli la hapo juu kuanzia kipengele nambari 1 hadi 4.
2. Ununuzi mwengine uliofanywa ulikuwa ni ununuzi wa vifaa vya matumizi ya kawaida ya Gazeti la Zanzibar Leo kama vinavyoonekana kwenye jadweli kuanzia kipengele nambari 5 hadi 6. Ununuzi huu unaweza kufanyika kwa njia ya nukuu kwa kuwa haukufikia kiwango cha kuitisha zabuni.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hii kwa kuwa ununuzi wote uliofanyika umefuata taratibu.

3.19: MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA (ZPPDA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 300,000,000 laki hadi kufikia Juni, 2020, mamlaka imekusanya jumla ya shilingi 194,190,497.28 sawa na asilimia 64.73 ya makadirio.

Majibu ya Mamalaka

Kamati haikupokea majibu yoyote yanayohusu taarifa ya mapato ya Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kama zinavyoelekeza Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020. Hata hivyo, Kamati ilipatiwa maelezo ndani ya kikao na Mamlaka ambapo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:

1. Mamlaka haiuweza kufikia lengo la makusanyo kwa vile makisio waliyopangiwa na Wizara ya Fedha na Mipango ni makubwa sana ukilinganisha na uhalisia wa mapato yenyewe.

2. Kamati iligundua kwamba usajili wa Kampuni katika Mamlaka sio jambo la lazima kwa mujibu wa Sheria yao, isipokuwa ulazima unatokea iwapo Kampuni husika itataka kufanya biashara na Seriakali na Taasisi zake zote.

3. Mamlaka inategemea mapato yake kupitia vyanzo vyake viwili kwa mwaka 2019/2020, vinavyotokana na ada ya usajili wa wafanyabiashara na ruzuku kutoka Serikalini (OC) ambavyo Kamati imegendua havijaorodheshwa kama zinavyotaka vigezo vya uandaaji hesabu wa mwaka kwani chanzo cha usajili wa wafanyabiashara ni chanzo ambacho Mamaka inakitambua lakini wamekiorodheshwa kama ni mapato mengineyo (other revenue).

4. Kamati imegundua kwamba Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma haikuwazingatia wafanyabiashara wenye mtaji mdogo (minor value businessman) wawe wanasajiliwa na Mamlaka. Hali hiyo inapelekea Taasisi nyingi za Serikali kupata hoja ya kujibu kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

5. Kuna tofauti ya mapato yaliyokusanywa yaliyoainishwa na Mdhibiti shilingi milioni 180 wakati taarifa ya fedha za mwisho wa mwaka zimeonesha shilingi milioni 194.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,857,400,000 ambapo hadi kufikia Juni, 2020 Mamlaka ilitumia jumla ya shilingi 1,601,175,791.47 sawa na asilimia 86.21 ya makadirio.

Majibu ya Mamalaka

Kamati haikupokea majibu yoyote yanayohusu taarifa ya matumizi ya Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kama zinavyoelekeza Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020. Hata hivyo, Kamati ilipatiwa maelezo ndani ya kikao na Mamlaka ambapo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:

1. Kuna tofauti ya Matumizi halisi baina ya kitabu cha Mdhibiti ambaye ameonesha 1.601 bilioni wakati ripoti ya hesabu ya mwisho wa mwaka ilionesha shilingi

1.604 bilioni.

2. Kukosekana kwa mapato kumeipekelea Mamlaka kushindwa kutekeleza baadhi ya shughuli ilizojipangia zikiwemo ukaguzi wa wafanyabiashara, mafunzo kwa wajumbe wa Bodi pamoja na Wahasibu hayakuweza kufanyika kama ilivyo kawaida.

3. Kamati imegundua kwamba Mamlaka haina jengo lake mwenyewe badala yake wamekodi kupitia jengo la Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa malipo ya shilingi milioni 5 kwa mwezi. Hata hivyo, baadhi ya wakati hushindwa kulipa kiwango hicho kutokana na uhaba wa fedha.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.19.1 Kutofanyakazi kwa kamati ya ukaguzi

Ni kweli mwanzo wa kuundwa kwa Mamlaka kamati hii haikufayakazi kutokana na sababu zifuatazo:

Mamlaka haikuwa na Mkaguzi wa Ndani kwa kipindi hichi. Tarehe 4/2/2019 ndipo Wizara ya Fedha na Mipango ilipotupatia Mkaguzi wa Ndani lakini pia Mkaguzi huyo hakukaa sana kwani mnamo tarehe 20/5/2029 alipata uhamisho wa kuwa msaidizi Mkurugenzi wa Idara ya Mipango, Utawala na Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A". Tarehe 2/9/2019 Wizara ya Fedha na Mipango ilimpeleka Mkaguzi mwengine wa ndani na alipofika tu alipata mapumziko ya kujifungua ya miezi mitatu na baada ya kurudi ndipo akaandaa ripoti hiyo. Hali hii ndiyo iliyopelekea kuchelewa kutoka ripoti ya ukaguzi na kuwasilishwa katika Kamati ya Ukaguzi.

Kamati ya ukaguzi iliipitia na kuijadili ripoti hiyo katika kikao chake cha tarehe 11/1/2021. Ripoti ya kikao hicho ipo ikihitajika.

Uchunguzi wa Kamati

1. Katika kufuatilia hoja hii, ilitaka kujua Mkaguzi wa Ndani baada ya kupata ujauzito alirejea lini Kazini na kujulishwa Mfanyakazi huyo alirudi kazini mwezi wa Disemba, 2019 kipindi ambacho angemudu kuandaa ripoti hizo kwa vile Mkaguzi wa nje wa Serikali alikuwa hajatoa ripoti yake.

2. Kamati iligundua kwamba Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ilikuwepo isipokuwa wajumbe wake walikosa uelewa wa sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Hali hiyo imejitokeza kwa vile walishindwa kufanya kikao kwa sababu ati Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani haipo jambo ambalo liliisikitisha sana Kamati kwa kutoa taarifa zisizo sahihi kwa vile sheria hiyo inawataka wafanye vikao vinne vya lazima kwa mwaka kujadili mambo tofauti yanayohusu utendaji wa Mamlaka na sio kusubiri ripoti ya Mkaguzi wa Ndani pekee. Kwa mantiki hiyo, hoja hiyo

imebakia kama ilivyo.

3. Aidha, Kamati imegundua Bodi ya Mamlaka imemaliza muda wake tokea Mei, 2021.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ihakikishe inavifanya vikao vyake kwa mujibu wa sheria.
2. Mamlaka ihakikishe inawapatia uelewa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi wa ndani ili wawe na ufahamu wa vifungu vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.
3. Mamlaka husika ihakikishe Bodi na Wajumbe wake wanateuliwa kwa wakati.
4. Mkaguzi wa Ndani aandae ripoti zake kwa wakati ili udhibiti wa ndani wa Mamlaka upatikane.

Hoja namba 3.19.2 Mapato ambayo hayakuwasilishwa benki shilingi 4,900,000

Tunathibitisha kwamba pesa hizo ziliwasilishwa benki kwa kufuata taratibu zote. Hata hivyo, zilitokea dosari za ukusanyaji wa mapato katika taarifa za usuluhisho wa kifedha (bank reconciliation) katika hesabu nambari 0406588000. Dosari hii ilitokea kwa kutowiana kwa majina baina ya "slip" ya benki na jina lililoandikwa kwenye risiti wakati wa kufanya malipo Pemba. Dosari hii ilifanyiwa kazi kwa kufanyiwa marekebisho kwa mujibu wa taratibu na kwamba tatizo hilo halipo tena.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati iligundua kwamba wafanyabiashara wengi hawana uelewa wa athari ambazo zinaweza kujitokeza iwapo kutatokea tofauti ya majina yaliyorikodiwa katika 'slip' na risiti husika na ndio maana hukosa umakini katika uandishi wa majina yao. Aidha, Kamati imebaini kasoro hiyo imerekebishwa na fedha hizo ziliingia Benki kwa Mamlaka kufanya mawasiliano na watendaji wa Mamlaka Pemba ili waweze kuangalia 'slip' husika pamoja na kumbukumbu za kambuni na kupata usahihi wa majina husika.

Kadhalika, Kamati imegundua kasoro hizo hazitojitokeza tena kwa vile Mamlaka inatumia mfumo wa 'Zan Malipo' ambao mtu anapewa 'control number' ya kulipia ambapo majina ya Kampuni tayari yanakuwa yameshasajiliwa.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inatoa uelewa kwa wafanyabiashara hususan wa Pemba ili wawe na uelewa wa kutumia majina yao sahihi ya kampuni zao.
2. Mamlaka ifanye upatanishi wa taarifa zake muda baada ya muda ili kutambua na kurekebisha mapema kasoro kama hizo.

3.21: MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Usafiri Baharini katika mwaka wa fedha 2019/2020, ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 4,491,804,899. Hadi kufikia Juni, 2020 Mamlaka imekusanya jumla ya shilling 2,286,469,743 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali sawa na asilimia 51 ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Usafiri Baharini haikufanikiwa kukusanya mapato yake kama ilivyopanga kufuatia agizo lililotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kutangaza rasmi kusitishwa usajili wa Meli za Kimataifa.

Kabla ya tangazo hilo, Mamlaka ilikuwa tayari ishaanza kuiendesha na kusimamia wenyewe usajili wa meli Kimataifa suala ambalo lilipelekea Kampuni na wamiliki wa meli kuwa na imani na kuvutiwa na kusajili meli zao katika taasisi yetu.

Jadweli lifuatalo inaonesha makadirio na mapato halisi ya Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2019/2020

NA	VIANZIO VYA MAPATO	MAKADIRIO (Tsh.)	MAPATO HALISI (Tsh.)	ASILIMIA
1.	Usajili wa meli za ndani	637,436,278	404,088,816	63
2.	Usajili wa meli za kimataifa	1,360,450,000	802,436,972	59
3.	Huduma za Bandarini	2,493,918,621	1,079,943,955	43
JUMLA KUU		**4,491,804,899**	**2,286,469,743**	**51**

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatay:

1. Katika mwaka wa fedha 2019/2019, Kifungu cha Mapato Mengineyo kimekusanya fedha kidogo (i.e Tsh. 61,998,930) ukilinganisha na mwaka wa fedha 2018/2019 (Tsh. 132,470,000).

   Hali hii imejitokeza kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 Kifungu hicho kilikusanya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (DANOUS) kwa ajili ya kuazimisha Siku ya Mabaharia Duniani pamoja na kupokea msaada kutoka Serikali Kuu tu.

2. Licha ya Zanzibar ilikuwa imezuiliwa kusajili meli za kigeni katika kipindi hicho, hata hivyo, Kifungu cha Mapato ya Kimataifa (International Revenue) kimekusanya jumla ya Tsh. 802,436,972. Fedha hizo zimetokana na huduma zilizokuwa zinatolewa kwa zile meli ziliokuwa zimesajiliwa kabla.

   Kwa kuwa hivi sasa zoezi la kusajili meli za kigeni limeruhusiwa tokea mwezi wa Oktoba, 2021, na kwa miongoni mwa vianzio vya mapato vya Mamlaka hii ni kusajili meli za kigeni, na kwa kuwa Mamlaka iliona jinsi ilivyozorota kiutendaji baada ya kuzuiliwa kutekeleza shughuli hii kwa kukosa kiasi kikubwa cha fedha.

   Hivyo basi, Kamati ya LAAC imeishauri Mamlaka kuhakikisha kuwa inakuwa makini katika kutekeleza shughuli zake ili kosa kama lile lisijitokeze tena kwa maslahi ya Mamlaka na Taifa kwa ujumla.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 4,577,364,860 kwa matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 Mamlaka imetumia jumla ya Tsh. 2,312,192,538 ambazo ni sawa na asilimia 51 ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Mamlaka ilipanga shughuli zifuatazo pamoja na utekelezaji wake:

NAM.	MAELEZO	MAKISIO (Tsh.)	HALISI (Tsh.)	ASILIMIA
1.	Fedha na utawala	3,019,584,860	2,209,807,738	69
2.	Mipango, Masoko na Utafiti	154,000,000	12,027,540	8
3.	Ukaguzi wa vyombo vya baharini, kampuni na bandari	118,260,000	9,017,925	8
4.	Usajili na utoaji wa leseni na vibali	311,024,000	52,276,719	17
5.	Utafutaji na uokozi	26,150,000	14,256,578	55
6.	Uhifadhi wa mazingira ya baharini	37,550,000	1,140,000	3
7.	Usimamizi wa masuala ya usalama wa vyombo vya baharini	16,500,000	13,216,038	80
8.	Miradi ya maendeleo	550,000,000	0	
	JUMLA KUU	**4,577,364,860**	**2,312,192,538**	**51**

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalibainika:

1. Kutokana na barua ya Mwenyekiti wa Mamlaka ya tarehe 27 Mei, 2019 yenye kumbukumbu Namba ZMA/WMUU/255/1/VOL.IX aliyoituma kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuhusiana na Ombi la kuidhinishiwa bajeti ya Mamlaka, Mamlaka ilikadiria kutumia jumla ya Tsh. 4,433,436,860 badala ya Tsh. 4,577,364,860 zilizoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

   Hivyo, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka kuwa makini na taarifa inazozitoa ili kuepusha usumbufu kwa wadau wake.

2. Kwa kuwa Mamlaka ilipata asilimia 51 ya makadirio ya matumizi iliyojipangia, Kamati ya LAAC iliomba kuelezwa athari ilizozipata Mamlaka hiyo kutokana na upungufu huo wa fedha, ambapo, ilielezwa kuwa baadhi ya mambo hayakuweza kutekelezwa ikiwemo yafuatayo:
   a. Ununuzi wa boti za doria
   b. Ujenzi wa uzio wa Afisi ya Mamlaka Pemba
   c. Ujenzi wa Afisi ya Mamlaka Kibweni
   d. Mfumo wa ufuatiliaji wa nyenendo za meli
   e. Mfumo wa usajili wa meli

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC iliiomba Serikali kuipatia Mamlaka fedha za kutosha ili iweze kutekeleza vyema shughuli ilizojipangia.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI

Katika utendaji wa kifedha wa Mamlaka (Financial Performance) na kiutendaji (Opearting performance) ni kipimo kinachoonesha namna Mamlaka inavyoweza kutumia mali zake kutokana na msingi wa biashara na namna ya ukusanyaji wa mapato kutokana na vyanzo vyake mbali mbali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka hii imebadilisha namna ya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kutoka katika mfumo wa “Accrual Basis” na kuingia katika mfumo wa “Cash Basis”, jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Mamlaka kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyomo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinaonesha katika uendeshaji wa Mamlaka Kifaida au hasara.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka iliieleza Kamati kuwa imepokea agizo kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kufunga hesabu kwa kutumia mfumo huo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikubaliani na agizo la Serikali kupitia Afisi ya Rais, Fedha na Mipango la kuzitaka Taasisi zake kufunga hesabu kwa kutumia mfumo wa "Cash Basis" badala ya mfumo wa "Accrual Basis".

Kamati hii haikubaliani na agizo hili kwa kuwa endapo utafunga hesabu kwa kutumia mfumo wa "Accrual Basis" kuna fursa ya kuonekana hali halisi ya kifedha iliyopo katika Taasisi husika. Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kulifuta agizo hilo na kuzitaka Taasisi zake kufunga hesabu zao kwa kutumia mfumo wa "Cash Basis" kutokana na sababu tulizozieleza hapo kabla

MATOKEO YA UCHUNGUZI

3.21.1 Vitabu vya mapato ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi

Ukaguzi umebaini kukosekana kwa vitabu vya ukusanyaji wa mapato kumepelekea kushindwa kufahamu idadi ya fedha iliyokusanywa na taratibu za fedha hizo zilivyotumika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, uchambuzi wa vitabu hivyo ni kama vinavyonekana katika jadweli lifuatalo:

Nam.	Mtiririko wa nambari za stakabidhi	Aliyepewa Huduma
1.	14751-14800	Pandu(Mkokotoni)
2.	15151-15200	Pandu(Mkokotoni)
3.	205401-205500	Abubakar Ali Haji
4.	205851-205900	Abubakar Ali Haji
5.	291901-291950	Abubakar Ali Haji

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alivyofanya ukaguzi katika Mamlaka hakupatiwa Vitabu hivyo, hata hivyo, hivi sasa Vitabu viko tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Mamlaka iliipatia Kamati Vitabu hivyo vya mapato kwa ukaguzi na ilielezwa kuwa wakati Mkaguzi Mkuu anatekeleza jukumu lake vitabu hivyo vilikuwepo,

isipokuwa kwamba, ilikuwa havijulikani vilipo.

Kutokana na ufinyu wa muda, Kamati ya LAAC ilikikagua kitabu kimoja tu chenye Risiti kuanzia Namba 205401 – 205450 kati ya vitabu vilivyowasilishwa kwake na kubaini mapungufu yafuatayo:

a. Risiti namba 205415 haikujazwa, isipokuwa kwamba, ilijazwa risiti ya mbeleyake ingawa nakala tatu za risiti hiyo zimebaki ndani ya kitabu hicho.
b. Risiti namba 205419 ambayo kwa kawaida hupelekwa benki risiti hiyo imebaki kwenye kitabu. Malipo hayo yaliyofanywa tarehe 7 Januari, 2020 na Ndg. Juma Kombo Ali, ambapo jumla ya Tsh. 35,000 zililipwa.
c. Asilimia kubwa ya risiti hizo kwa upande wa karatasi inayobakia kwenye kitabu hicho hazikuandikwa kwa madai kuwa karatasi hizo zilikuwa haziandikiki. Kamati ya LAAC haikukubaliana na maelezo hayo kwa kuwa Watendaji wa Mamlaka baada ya kubaini kasoro hiyo walipaswa kutumia "carbon paper".

Kwa ujumla, Kamati ya LAAC haikuridhika na matumizi ya vitabu hivyo na kutokana na mapungufu hayo iliyoyabaini ilihisi ndio sababu iliyopelekea Mkaguzi Mkuu asipatiwe vitabu hivyo. Kwa mnasaba huo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

2. Kwa kuwa Mamlaka imeshanunua mashine kwa ajili ya kufanya malipo kwa njia ya elektroniki, na kwa kuwa Mamlaka imeshaomba muongozo na ruhusa ya utoaji wa risiti kwa njia ya kielektroniki kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kufuatia barua ya Mamlaka ya tarehe 22 Julai, 2021 yenye kumbukumbu Namba ZMA/(OR) FNM/255/4/VOL. II ingawa Katibu Mkuu huyo hajaijibu barua hiyo muhimu kwa maslahi ya Mamlaka na taifa kwa ujumla.

   Hivyo basi, Kamati ya LAAC inamtaka Katibu Mkuu huyo kuijibu barua hiyo ili Mamlaka iweze kutumia mashine hizo na iachane na utaratibu wa kutumia vitabu.

3.21.2 Kukosekana kwa Mapato yatokanayo na usajili wa vyombo vya uvuvi

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali zinazopelekea kuikosesha Serikali mapato kwa kutokuvifanyia kazi kwa vifungu vya sharia tulivyovinakili hapo juu, dosari hizo ni kama zifuatazo: -

- Kutokuvifanyia usajili vyombo vya uvuvi katika maeneo tofauti ya bahari ikiwemo Mkokotoni, Kisakasaka n.k

- Kutokusanya mapato yanayotokana na vyombo vinavyofanya shughuli mbali mbali baharini zinazofanyika kupitia bandari ndogo ndogo kwa

mfano Donge Muanda, Kisakasaka n.k.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka tayari imeshalifanyia kazi suala hili kwa kuongeza nguvu ya rasilimali watu katika ofisi yetu iliyopo Mkokotoni, ambayo imepelekea kusajili kwa wingi vyombo vidogo vidogo katika bandari za Donge Muanda, Mkokotoni.

Aidha, Mamlaka imeunda kikosi kazi kwa ajili ya kufuatilia suala la usajili wa vyombo vidogo vodogo kwa Wilaya zote za Unguja na kwa upande wa Pemba, Mamlaka imeongeza nguvu kwa kumpeleka Afisa Mratibu, ambaye ndiye anayeongoza Ofisi hiyo ya Pemba.

Vile vile, Mamlaka kwa sasa imefanikiwa kuwajengea uelewa wadau wa sekta ya usafiri baharini kwa wanaotumia vyombo vidogo vidogo kwa kufanya ziara mbalimbali kwa kutoa elimu juu ya usafiri salama wa vyombo vidogo vidogo, umuhimu wa utunzaji wa mazingira baharini na umuhimu wa usajili wa vyombo, ambapo wadau hao waliweza kujishajihisha kwa kusajili vyombo vyao kwa wingi.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Mamlaka iendelee kutoa elimu kwa Wamiliki wa vyombo vya baharini juu ya umuhimu wa kusajili vyombo hivyo na waelezwe kuwa miongoni mwa sababu zinazopelekea vyombo hivyo kusajiliwa ni pamoja na kulinda usalama wao.
2. Taasisi inayohusika na masuala ya utoaji wa vibali vya uvuvi isitoe leseni ya uvuvi kwa Mhusika hadi Mhusika huo awe amesajiliwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini. Hivyo, ni lazima kwa Taasisi za Serikali kutekeleza majukumu yao kwa mashirikiano ili kila Taasisi iweze kutekeleza vyema shughuli zake na bila ya usumbufu wowote.

3.22: MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR (VTA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 407,430,000. Hadi kufikia 30, Juni 2020 Mamlaka ilikusanya jumla ya shilingi 1,253,763,608 sawa na asilimia 307.72 ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mamlaka ilikusanya Jumla shilingi. 1,253,763,608 kutokana na vyanzo vyake vya ndani makusanyo hayo yameongezeka

limetokana na sababu zifuatazo:-

1. Kuongezeka kwa vyanzo vya mapato ambavyo awali vilikuwa havijaingizwa katika bajeti ya mwaka 2019/2020, Makadirio ya makusanyo ya vyanzo hivi vilikuwa havijaingizwa katika makadirio ya makusanyo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Mamlaka ambazo ni shilingi 679,471,500/- ambazo ni sawa na asilimia 54.2% ya makusanyo halisi katika mwaka 2019/2020.

2. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliodahiliwa kwa mwaka wa masomo 2019/2020 kwa kozi mbali mbali zinazotolewa na Vituo vilivyo chini ya Mamlaka ya Elimu ya Amali.

Uchunguzi wa Kamati

Kufuatia majibu hayo, Kamati ilihoji ibainishiwe vyanza ambavyo Mamlaka haikuviingiza katika makadirio ya mapato na kuelezwa kwamba kulikuwa na zabuni kutoka Wizara inayoshughulikia vijana pamoja na kikosi cha Polisi Tanzania ambavyo Mamlaka ilishinda na kupatiwa kazi ya utoaji mafunzo ya ujasiriamali ya kwa vijana na kupelekea kuwaingizia jumla ya shilingi 400,780,000 kwa mwaka 2019/2020.

Aidha Kamati ilibaini kuwa pamoja na kuvuka lengo la makusanyo hadi kufikia asilimia 307.07. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba fedha hizo hazikukatwa kodi kwa mujibu wa sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ili kodi hiyo iweze kuisaidia Serikali kutelekeza majukumu yake ipasavyo.

Kadhalika, Kamati iligundua kuwa mbali na sababu zilizoelezwa na Mamlaka zilizosababisha mapato kuongezeka, pia kulikuwa na sababu ya upatikanaji wa zabuni ya useremala katika chuo cha Daya na Makunduchi ambapo jumla ya shilingi 278,691,500 zilipatikana. Ongezeko hili ni fedha za Mradi wa Vijana na Ajira na fedha zilizoingizwa na Baraza la Mitihani kwa ajili ya utoaji wa huduma ya chakula kwa walimu wanaosahihisha Mitihani ya Taifa ya Zanzibar na fedha za Mradi wa Vitanda vya Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inapendekeza kwamba vyanzo vyote vya mapato vya Mamlaka ambavyo ina uwezo wa kuvikusanya viingizwe katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ili yaweze kuondoa mwaya kwa baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu kujinufaisha.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,168,630,000. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 6,174,273,998 ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 1,994,356,002.00 ikiwa ni matumizi ya maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni, 2020 kiasi cha shilingi 5,945,945,275.000

zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 96.30 ya makadirio na shilingi 1,082,127,320 zilitumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 54.25 ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwamba matumizi ya Mamlaka yanaonekana ni makubwa kulingana na kilichopatikana kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ambapo Mamlaka ilianza matumizi yake ikiwa na bakaa ya shilingi 436,310,593.05. Hata hivyo, makadirio ya makusanyo yatokanayo na ruzuku ya matumizi mengineyo (Other Charge - O/C) yamepungua kwa asilimia 30.39 ya makadirio kwa mwaka kutoka Serikali Kuu ndio yaliyopelekea Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya matumizi yake yaliyopangwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 kutokana na kuibuka kwa ungonjwa wa UVIKO 19 ambao umeathiri shughuli za kiuchumi katika Taasisi mbali mbali.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya LAAC imebaini kuwa jumla ya shilingi 436,310,593.05 zimetumika kinyume na taratibu na maelekezo matumizi ya fedha za umma zanavyotaka. Utaratibu unataka, Taasisi inapobakisha fedha katika mwisho wake wa mwaka zinatakiwa kuwasilishwa katika hesabu ya hazina na baada ya mwaka mpya wa fedha kuanza, Mamlaka ilitakiwa iziombe ziingizwe katika hesabu ya Mamlaka tofauti na walivyofanya Mamlaka.

Vile vile, Kamati pia imegundua kuna ukiukwaji wa matumizi ya holela ya fedha za umma kwani matumizi katika kifungu cha posho maalum kilichoonekana katika hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka (Financial Statements) matumizi yake yalizidi bajeti iliyopangwa kwani jumla ya shilingi milioni 30 zilipangwa na kutumika shilingi 124,510,445. Mbali na hilo, Kamati iligundua kwamba Mamlaka inafanya kazi zake katika jengo la kukodi kutoka kwa mtu binafsi kwa shilingi milioni 26.3 kwa mwaka na tayari wameshapatiwa eneo liliopo karibu na Wizara ya Elimu lakini bado ujenzi kamili haujaanza.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inapofungua ‘deposit account’ kwa ajili ya kuweka fedha zilizokuwa hazijatumika hadi zikafikiwa na mwaka mwengine wa fedha.
2. Mamlaka ifanye matumizi yake kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bodi ya Mamlaka.
3. Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu iharakishe ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ili ipunguze upotevu wa fedha nyingi zinazotumika kwa kulipia kodi.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.22.1 Tofauti iliyojitokeza baina ya makusanyo halisi na kilichoripotiwa katika taarifa ya fedha shilingi 283,171,319.44

Katika kupitia stakabadhi za makusanyo ya mapato, taarifa za kibenki na daftari la fedha. Ukaguzi umebaini kwamba kuna tofauti ya upungufu wa shilingi 283,171,319.44 zilizoainishwa katika taarifa ikilinganishwa na iliyoripotiwa katika taarifa za makusanyo

halisi yaliyopatikana vituoni na Afisi Kuu ya Mamlaka. Kuwepo kwa tofauti baina ya makusanyo halisi kutoka vituoni na Afisi kuu kunapelekea taarifa zote za fedha kutotoa sura nzuri na sahihi kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

Bajeti	Taarifa za kifedha	Makusanyo halisi	tofauti
214,800,000	1,245,036,512.56	1,528,207,832	283,171,319.44

Majibu ya Mamlaka

Kwa kuwa Mamlaka inatumia Mfumo wa Uandaaji wa Taarifa zake kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IPSAS Cash Basis), Sheria na Kanuni za Fedha za Ndani (Public Finance Managent Act ya Zanzibar) pamoja na Miongozo mbali mbali ya uandaaji wa hesabu inayotolewa na Ofisi ya Fedha na Mipango Zanzibar juu ya utayarishaji wa Hesabu, ambayo imeitaka Mamlaka kuandaa taarifa za fedha za mwaka kwa kuangalia kiwango cha fedha halisi zilizokusanywa katika hesabu za kibenki pamoja na matumizi halisi yaliyofanyika katika mwaka wa fedha husika bila ya kuzingatia kiwango cha fedha zitokanazo na madeni kwa kipindi cha Julai hadi Juni ya kila mwaka.

Kwa maelezo haya taarifa zilizowasilishwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa wakaguzi zilikuwa ni sahihi kwa mujibu wa vielelezo vya ''Bank Statement''. Hii ni kutokana na michango yote ya wanafunzi na Fedha zinazotoka kwa Wahisani wa Maendeleo zinawasilishwa kupitia Benki. Hivyo ukusanywaji wa fedha unategemea miamala ya Benki ambayo ipo sahihi.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipofuatilia hoja hii na kufuatilia majadiliano na malumbano yaliyokuwa yakitolewa na watendaji wa Mamlaka kwa watendaji wa Mdhibiti (CAG) kwamba taarifa zote zilizowasilishwa mbele ya Kamati walipatiwa CAG ila wanashangaa taarifa iliyotolewa dhidi yao. Kamati iligundua kuwa kulikosekana mashirikiano ya karibu baina ya pande mbili hizo. Hali hiyo, hupelekea kutofikia ipasavyo lengo la ukaguzi husika.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kuwepo mashirikiano ya karibu baina ya wakaguzi na wakaguliwa ili kuweza kufanikisha lengo la ukaguzi la kupata taarifa na vielelezo sahihi.
2. Kuwepo na madaftari mawili (la CAG na la Taasisi) yatakayosaidia kuweka kumbukumbu za vielelezo na taarifa kamili za Mkaguzi na Taasisi inayokaguliwa.

3.22.2 Kukosekana kwa uhalisia wa makisio ya makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi.

Ukaguzi ulipitia taarifa ya makisio ya makusanyo yasyo ya kodi pamoja na uhalisia wa makusanyo katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwka 2020 za Mamlaka na kubaini uwepo wa tofauti ya shilingi 1,313,407,832 iliyotokana na makusanyo halisi kuwa makubwa zaidi ya makisio na kupelekea uwepo wa tofauti isiyo ya kawaida. Ufafanuzi wa makusanyo hayo ni kama yanavyoonekana katika Jadweli:

Bajeti ya Mapato ya kodi (Tzs.)	Makusanyo halisi ya Mapato (Tzs.)	Tofauti
214,800,000	1,313,407,832	1,313,407,832.00

Majibu ya Mamlaka

Katika mwaka wa 2019/2020 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ilikuwa na makusanyo yasio na kodi ya aina mbili kuu ambayo ni ada ya wanafunzi na fedha kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo. Kwa ujumla wake zilikadiriwa kuwa shilingi 407,430,000 ambazo makusanyo halisi zilikuwa ni shilingi 1,245,036,512.56.

Ni kweli katika mwaka wa fedha 2019/2020 kulikosekana uhalisia wa makisio ya makusanyo pamoja na makusanyo halisi ambayo yalisababishwa na kutokuwepo kwa matarajio ya makusanyo mpaka bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Kusababishwa kutokuwepo katika mipango ya Mamlaka kwa kipindi hicho. Hata hivyo kwa kuwa fedha hizo ziliingizwa katikati ya mwaka wa fedha ziliweza kutumika kwa mahitaji ya shughuli zilizopangiwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Ongezeko hili ni fedha za Mradi wa Vijana na Ajira na fedha zilizoingizwa na Baraza la Mitihani kwa ajili ya utoaji wa huduma ya chakula kwa walimu wanaosahihisha Mitihani ya Taifa ya Zanzibar na fedha za Mradi wa Vitanda vya Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imegendua kwamba uchunguzi wa hoja hii unafanana na hoja ya mwanzo ya ongezeko la Mapato. Hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

3.22.3 Vifaa vilivyohifadhiwa muda mrefu bila matumizi vyenye thamani ya shilingi 118,901,079

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imenunua vifaa mbali mbali kutoka kwa Mzabuni Furniture Centre Ltd. kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mamlaka inayotarajiwa kujengwa. Vifaa hivyo vimenunuliwa tarehe 3/4/2014 kupitia Mradi wa ALDL ambao ndio Mradi uliojenga kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni. Lakini ukaguzi umebaini vifaa hivyo vimehifadhiwa katika vyumba viwili vya dahalia ya wanawake kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita bila ya matumizi.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba vifaa vimekosa ushahidi wa nyaraka za kupokelewa mali ghalani. Vifaa hivyo vilikuwa na jumla ya shilingi 118,901,078.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli mradi wa ALSD II ulinunua vifaa mbali mbali vya kiofisi kupitia Mzabuni wa Furniture Center kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mamlaka inayotarajiwa kujengwa kupitia mradi huo. Ujenzi haukufanyika kutokana na uhaba wa fedha kwa kipindi hicho

cha Mradi. Hata hivyo, baadhi ya vifaa hivyo vinatumiwa na Ofisi kuu na Maktaba iliyopo Chuo cha Mafunzo ya Amali Mwankwerekwe na vichache vilivyobaki vinatarajiwa kutumika katika majengo mapya yaliyojengwa katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni. Aidha, Vifaa hivyo vilipokelewa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na Kamati kukiri kununuliwa na kupelekwa Mkokotoni kuhifadhiwa vifaa hivyo, Kamati imebaini kwamba Mradi huo ulitekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha Amali Makunduchi, Daya na ujenzi wa Afisi Kuu ya Mamlaka kwa awamu tofauti pasi na kuwepo ushirikishwaji wa karibu kutoka kwa watendaji wa Mamlaka. Hili limethibitika kwamba wakati Mkaguzi amefika Mamlaka kwa ajili ya ukaguzi hakuweza kupatiwa vielelezo hivyo ambavyo vyengine vilikuwepo Wizarani kwa vile ndio waliokuwa wasimamizi wakuu wa mradi huo. Hata hivyo, Kamati ilipatiwa vielelezo hivyo kwa ukaguzi.

Aidha, Kamati imebaini kwamba Wizara au Mamlaka haikuwa na mpango mzuri wa matumizi ya fedha hizo kwani waliamua kununua vifaa (viti) pasi na kumaliza majengo ya kuingiza viti hivyo. Hali hiyo inapelekea kuwepo matumizi mabaya wa mali za umma.

Mapendekezo ya Kamati

1. Wizara au Mamlaka inapokopa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi fulani iwe na mpango na mikakati mizuri ya kujikita katika utekelezaji wa mradi huo na sio vyenginevyo.
2. Utekelezaji wa Miradi ufanywe na Mamlaka husika na sio kuchukuliwa na kutekelezwa na Wizara husika.
3. Kuwepo utaratibu mzuri wa uwekaji kumbukumbu na ziwe zinapatikana wakati vinapohitajika.

3.22.4 Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika Dakhalia kulinganisha na uwezo wa Dakhalia (Hostel)

Ukaguzi umebaini kwamba kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni kina upungufu wa dakhalia usiokidhi mahitaji ya wanafunzi, hivyo husababisha mrundikano wa wanafunzi katika vyumba vya dakhalia hizo. Mapitio ya ukaguzi yamebaini kwamba chumba kimoja chenye uwezo wa kulaza wanafunzi wa 4 kinalaza wanafunzi 10 hali inayohatarisha afya na usalama wa wanafunzi. Aidha, dakhalia hizo haina viingiza hewa vya kutosha ikiwemo madirisha na mafeni.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa hivi sasa ina matatizo ya uhaba wa majengo ya dakhalia kulinganisha na mahitaji ya wanafunzi wanaotaka kuishi katika dakhalia hizo. Mamlaka imeliona tatizo hilo na imeshaanza juhudi ya kuandaa michoro ya dakhalia mpya. Hata hivyo, kuanza kutumika kwa vyuo vipya vya Daya na Makunduchi itasaidia kupunguza ukali wa tatizo hilo.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hiyo, Kamati iligundua uwepo wa utata kwa vile watendaji wa Mamlaka walikiri kuwepo kwa upungufu wa dakhalia za wanafunzi isipokuwa walikanusha hoja ya Mkaguzi kwamba kulikuwa na mrundikano wa wanafunzi hadi kufikia chumba kimoja kutumiwa kulaza wanafunzi 10. Kutokana na mkanganyiko huo, Kamati ilipanga kufanya ziara ya kushitukiza katika chuo cha Mkokotoni na Dakhalia yake ili kuweza kupata tswira kamili juu ya ukweli wa jambo hilo.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kwa vile mpango wa uendelezaji wa vyuo vya Amali upo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali iwaingizie fedha za kutosha ili Mamlaka iweze kutekeleza miradi yake.

2. Mamlaka iruhusiwe kuitekeleza Miradi yake wenyewe.

3.22.5 Dosari iliyobainika katika malipo ya mikataba ya zabuni yenye jumla ya shilingi 332,376,974

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari inayotokana na malipo ya mikataba ya zabuni ya wanaotoa huduma, kwa mujibu wa makubaliano ya pande zote mbili, malipo ya mikataba yote yatafanywa kwa awamu mbili ambayo ni asilimia 90 na asilimia 10 baada ya kumalizika kwa kazi. Mamlaka imekiuka masharti hayo kwa kulipa asilimia 100 kwa kila mkataba wa zabuni uliofungwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 31(f) cha sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Miongoni mwa watoa huduma waliogundulika kuwa na dosari katika mikataba yao ni Diamond Motor Ltd, Greenland General Supply Company Ltd na Visiwani General Supplies.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakubaliana na ushauri ulitolewa na Mkaguzi, ni kweli kiutaratibu malipo yalitakiwa kufanyika kwa awamu mbili, Awamu ya kwanza wakati anaposaini Mkataba kwa asilimia tisini (90%) na asilimia kumi (10%) baada ya kukamilika kwa kazi kama terms za mkataba zilivyotaka. Kwa kuwa Mamlaka ilishindwa kutekeleza mkataba katika kipengele cha malipo kwa muda na ni kwasababu ya kukosekana kwa fedha ndio ilipopelekea kulipwa kwa asilimia Mia Moja baada ya kumalizika kwa Kazi.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa vile Mamlaka ilikiri kutokezea kwa kosa hilo, na Kamati imejiridhisha kupitia Mkataba husika na kugundua kweli kosa lilifanyika na hatimae Kamati ilitoa mapendekezo yake.

Mapendekezo ya Kamati
Mamlaka itekeleze mikataba yake kama inavyojieleza.

MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI (MMA) - PEMBA

3.22.6 Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya kukusanya mapato ya shilingi 51,620,000

Jumla ya shilingi 51,620,000 zilikadiriwa kukusanywa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio hayo ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 42,699,398 zilikusanywa sawa na asilimia 82.7 ya makadirio ambapo hali hii inaonesha Mamlaka imeshindwa kufikia malengo ya makusanyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 32(1)(2) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka
Makusanyo ya Mamlaka/Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji yanategemea ada za wanafunzi, ruzuku kutoka Serikali kuu na miradi midogo midogo ya ndani ikiwemo kodi za ukumbi, mauzo ya fomu za kujiunga na Chuo kwa kila mwaka.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Taasisi imeshindwa kufikia malengo ya makusanyo ya Tsh 51,620,000 na kufanikiwa kukusanya Tsh 42,699,398 ambayo ni sawa na 82.7% ya makadirio. Hii imetokana na changamoto kubwa ya kuibuka kwa maradhi ya Uviko 19, ambayo yalipelekea Chuo kufungwa na kusitisha njia zote za mapato, jambo hili lilipelekea kuzorota kwa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na shughuli walizozianisha hapo juu na kupelekea kuto kufikia malengo. Pia chuo kilitumika kama ni kituo cha kuhifadhia wagonjwa wa Uviko 19 kwa Pemba, na kupelekea shughuli zote za Chuo kusimama kwa muda.

Uchunguzi wa Kamati
Kamati iliridhishwa na majibu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba isipokuwa ilitaka kujua Wizara ya Afya ilichangia chochote katika kipindi chote waipokuwa wakilitumia eneo hilo na kuelezwa kwamba hawakuchangia kwa kutoa fedha taslim ila walikarabati jeng hilo.

3.22.7 Kukosekana kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba haina Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kuweza kusimamia shughuli za ukaguzi wa ndani na utoaji wa taarifa juu ya makusanyo na matumizi ya fedha za Serikali.

Kutokuwepo kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani inaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha na mali za umma, aidha ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa Fedha

za Umma Zanzibar namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ina mfumo wa ukaguzi wa ndani ambao unajitegemea, ambapo kila ifikapo mwisho wa kota wakaguzi wa Mamlaka kutoka Makao Makuu Unguja hukagua na kufunga mahesabu ya Idara zote za Mamlaka Unguja na Pemba, na huwasilisha ripoti ya ukaguzi kwenye vikao vya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka.

Suala hili limeonekana kua ni changamoto katika utendaji na tayari Ofisi imeshafanya juhudi mbali mbali za kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani Pemba, ikiwemo kuandika barua za maombi ya kupatiwa mkaguzi wa ndani, kufanya mazungumzo ya ana kwa ana na Afisa Mdhamini Wiraza ya Fedha - Pemba ya kumshawishi kutupatia watendaji wa ukaguzi wa ndani, pia Ofisi imeshaliwasilisha suala hili kwa Mkurugenzi Mtendaji na Bodi ya wakurugenzi kupitia ripoti za utekelezaji za robo mwaka.

Uchunguzi wa Kamati

Katika uchunguzi wake, Kamati imebaini kuwa barua za kuomba Mkaguzi wa ndani kweli zilikuwepo ila hazikuwa zikijibia kwa maandishi na Ofisi ya Afisa Mdhamini wa Wizara ya Fedha na Mipango - Pemba ili kupata kujua kwa kiasi gani suala hilo linafanyiwa kazi.

Mapendekezo ya Kamati

1. Wizara ya Fedha na Mipango iharakishe kuipatia Muhasibu Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba ili kupunguza gharama za kiutendaji.

2. Ofisi ya Afisa Mdhamini ijibu barua za maombi ya watendaji zinazoelekezwa kwao.

3.22.8 Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa Mamlaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka - Pemba haina Mpango wa Manunuzi wa Mwaka ili kuweza kuthibitisha Mpango wa Manunuzi mzima wa Mamlaka na utekelezaji wake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 29(e) cha sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma namba 11 ya mwaka 2016 pamoja na kifungu cha 46(1)(2) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Zanzibar namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba ni sehemu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mamlaka Pemba hupata fedha za kuendeshea shughuli za kiutendaji kutoka Makao Makuu ya Mamlaka Unguja. Aidha, Utaratibu unaofuatwa ndani ya Mamlaka ni kutumia mpango mmoja wa manunuzi Unguja na Pemba.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa vile Mamlaka imekiri kutokezea kwa kasoro hiyo na kuomba kujirekebisha kwani walikuwa hawana uelewa kwamba wanahitajika kuwa na mpango wao unaojitegemea kama zilivyo Mamlaka nyengine ziliopo Pemba. Kwa hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

3.22.9 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 13,296,979

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 13,296,979 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba lakini vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo.

Kutoambatanishwa vielelezo katika hati ya malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

1. Vocha nambari 1/7 ya malipo ya fedha za posho na chakula kwa usimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali. Barua ya maombi hayo ipo yenye tarehe 02/07/2019 na risiti namba 0786. Kuhusu kukosekana kwa barua ya maombi kutoka kwa Mkuu wa Chuo ni kuwa, Mkuu wa chuo siye anayeratibu mitihani ya Taifa ya Mamlaka na kwamba mitihani hiyo huratibiwa na Mratibu wa Mafunzo Ofisi kuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba ambae ndie aliyeandika barua ya Maombi.
2. Vocha namba 1/1,19/1, 4/2, 1/3, 4/3, na 22/3 malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa Mamlaka. Kukosekana kwa muongozo unaohusu ulipajiwa nauli za wafanyakazi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Ni kweli kuwa kwasasa Mamlaka haina muongozo wake wenyewe unaotumia kulipia nauli za wafanya kazi, ila inatumia muongozo wa Wiraza ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kulipa nauli hizo.
3. Vocha namba 2/2 kukosekana kwa risiti ya malipo ya fedha kwa ajili ya usanifu wa mchoro na utayarishaji wa makadirio ya ujenzi wa nyumba ya wageni. Ni kweli kuwa wakati wa ukaguzi risiti ya malipo hayo haikuwepo, hii ni kutokana na kuwa risiti aliyoleta supplier ilikuwa na makosa ya jina la Taasisi, ambapo Ofisi iliirejesha kwa muhusika ili aifanyie marekebisho na kwamba hadi ukaguzi unakamilika risiti haikuwa imepatikana. Ofisi ilifanya jitihada za kuifatilia risiti hiyo na kwa sasa risiti hiyo ipo.
4. Kwa upande wa ramani na BOQ ni kuwa wakati wa ukaguzi ramani na BOQ ya jengo zilikuwepo ila kutokana na mapungufu ya kibinadamu vitu hivi havikuweza kuwasilishwa, kwa sasa vitu hivyo vipo na vipo tayari kukaguliwa.
5. Vocha namba 22/2 malipo ya fedha za posho la usimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali. Barua ya maombi hayo ipo yenye tarehe 26/02/2020 na orodha wa Mahudhurio ya wasimamizi wa mitihani. Kuhusu kukosekana kwa barua ya maombi kutoka kwa mkuu wa Chuo ni kuwa, Mkuu wa chuo siye anae ratibu mitihani ya Taifa ya Mamlaka na kwamba mitihani hiyo huratibiwa na Mratibu wa Mafunzo Ofisi kuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba ambae ndie alie andika barua ya Maombi hayo. Kuhusu Orodha wa mahudhurio ni kuwa orodha hizo zilikuwepo na mkaguzi

alizipitia na kuziweka alama ya vyema.

6. Vocha namba 23/2 marejesho ya fedha zilizotumika kwa chai na chakula kwa wasimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali. Barua ya maombi hayo ipo yenye tarehe 26/02/2020 na orodha wa Mahudhurio ya wasimamizi wa mitihani. Kuhusu kukosekana kwa barua ya maombi kutoka kwa Mkuu wa Chuo ni kuwa, Mkuu wa chuo siye anae ratibu mitihani ya Taifa ya Mamlaka na kwamba mitihani hiyo huratibiwa na Mratibu wa Mafunzo Ofisi kuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba ambae ndie alie andika barua ya Maombi hayo. Kuhusu Orodha wa mahudhurio ni kuwa orodha zilikuwepo.
7. Vocha namba 3/3 malipo ya fedha za imprest kwa matumizi madogo madogo ya Chuo cha Mafunzo ya Amali. Marejesho yapo na mkaguzi alikuja kuyahakiki na kuweka alama ya vyema baada ya uhakiki huo
8. Vocha namba 5/2 kuhusu malipo ya fedha za kodi ya TRA iliyokatwa kwa wafanyabiashara kwa mwezi wa Januari, 2020. Risiti ipo yenye nambari ZN21453341, tayari imefanyiwa verification.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kamati iliridhika na majibu ya vocha nambari 1/7 yaliyotolewa na Watendaji wa Mamlaka pamoja na kielelezo cha barua kilichokaguliwa. Kwa hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.
2. Kwa upande wa majibu ya vocha nambari 1/1,19/1, 4/2, 1/3, 4/3, na 22/3, Kamati imegundua kwamba Mkaguzi alipopita kwa ukaguzi, Mamlaka haikuwa na muongozo wa Wafanyakazi kwa vile uliwasilishwa katika Bodi kupitia waraka nambari 16.16.1 ikiwa ni agenda ya 16 ya barua ya tarehe 27 Septemba, 2021. Kwa maana hiyo, Muongozo huo uliandaliwa na kuwasilishwa nje ya muda wa ukaguzi wa 2019/2020.
3. Kwa upande wa majibu ya Vocha nambari 2/2, Kamati iliridhika na jibu la kutokuwepo kwa risiti ya usarifu wa mchoro wa jengo la nyumba ya wageni wakati wa ukaguzi ila haikuridhishwa na jibu la kutokuwepo kwa BOQ kwa vile hiyo ni kielelezo ambacho kinatakiwa kiwepo katika eneo la kazi ambalo Mkaguzi alikwenda kwa ajili ya ukaguzi lakini hakuikuta.
4. Kuhusu majibu ya vocha nambari 22/2, Kamati iliridhishwa na majibu na haikuwa na hoja zaidi.
5. Kuhusu majibu ya vocha nambari 23/2, Kamati iliridhishwa na majibu ya watendaji isipokuwa ilishangazwa na maelezo kwamba risiti za vielelezo zilikuwepo wakati wa Ukaguzi lakini hoja imeingia kwenye kitabu.
6. Kuhusu majibu ya vocha nambari 3/3, Kamati ilishangazwa na kwamba Mkaguzi alihakiki marejesho ya 'imprest' na kuyawekea alama ya vyema ambazo Kamati imeziona lakini hoja imeingizwa kwenye kitabu.
7. Kwa upande wa majibu ya vocha nambari 5/2, kuhusu malipo ya fedha za kodi ya TRA, Kamati imeridhishwa na majibu kwa vile imeweza kuona vielelezo vya malipo hayo ila ilishangazwa na uwepo wa hoja hii wakati kuna maelezo kwamba Mkaguzi alioneshwa vielelezo hivyo.

Uchunguzi wa Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inakamilisha muongozo wa wafanyakazi wake ili iwe dira katika utekelezaji wa majukumu yake.
2. Mamlaka ihakikishe inafuata kikamilifu sheria ya Usimamizi wa Fedha ili wanapotekeleza miradi yao kuwepo na vielelezo vyote vinavyohitajika kwa ukaguzi ikiwemo BOQ.
3. Kuondosha utata katika utekelezaji wa kazi za ukaguzi, Mkaguzi na Mkaguliwa kila mmoja aandae daftari la makabidhiano ya mahitaji yote ya ukaguzi ambapo daftari la Mkaguzi litajazwa na Mkaguliwa na la Mkaguliwa litajazwa na Mkaguzi.

3.22.10 Kukosekana kwa zabuni ya Mkandarasi wa Ujenzi wa Jengo la Maabara katika Chuo cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba.

Jumla ya shilingi 107,147,338.78 zimelipwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba kwa Mkandarasi wa ujenzi wa jengo la Maabara katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji. Ukaguzi umebaini kwamba malipo ya Mkandarasi huyo hayakuzingatia uwepo wa zabuni kulingana na kiwango cha fedha alicholipwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 68(1)(2)(3)(4) cha sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar namba 11 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Ujenzi wa jengo hili ulidhamiriwa kuwa sehemu ya kuwajengea uwezo walimu na pia kuwapatia wanafunzi fursa ya kufanyakazi za vitendo kupitia 'live projects', kwa sababu hiyo, Mkurugenzi Mtendaji kwa nia njema alitoa agizo la kuwa, kazi ya ujenzi wa Jengo la Maabara ifanywe na Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji kupitia Idara zake. Kwa utaratibu huo kila Idara ilishiriki katika ujenzi huo kulingana na kazi/fani zao. Kitendo cha kukipatia Chuo kazi kama hizi kinapelekea kukitangaza chuo, kuwajengea uzoefu walimu pamoja na wanafunzi kupata uzoefu mkubwa wa kazi, jambo ambalo litawawezesha wanafunzi wanapohitimu kujiajiri wenyewe.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iliridhika na majibu ya hoja hiyo yaliyotolowa na watendaji kwa vile kufanya hivyo kunanusuru fedha nyingi za Serikali ambazo zilitakiwa zitolewe ili Mamlaka iweze kununua vifaa vya kuwafundishia kivitendo wanafunzi wao lakini pia inawapatia uzoefu (mazoezi) wa kutosha walimu na wanafunzi wao. Sambamba na hayo, inaimarisha mazingira ya chuo kwa kuwapatia majengo ya kisasa kwani Kamati ilipata fursa ya kuyaona majengo hayo na kuridhika na ujenzi wake.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka iiandikie barua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kupata ufafanuzi na muongozo

wa kufanyakazi za ujenzi kama ni sehemu ya mafunzo lakini kwa upande mwengine kunatokea ukiukwaji wa sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar namba 11 ya mwaka 2016.

3.22.11 Kukosekana kwa zabuni ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi shilingi 236,296,842.1

Jumla ya shilingi 236,296,842.1 zimelipwa na Mamlaka - Pemba kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya ujenzi wa jengo la Maabara katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji.

Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakuzingatia uwepo wa zabuni kulingana na kiwango cha fedha kilichotumika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 68(1)(2)(3)(4) cha sheria ya Ununuzi na Uondoji wa mali za Umma Zanzibar namba 11 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Utaratibu kujenga kwa kutumia nguvu kazi ya walimu na wanafunzi katika ujenzi ulipelekea mfumo wa manunuzi ya vifaa kufanyika kwa mujibu wa mahitaji ya mafundi kwa wakati husika, na kwamba kama kungefanyika manunuzi ya vifaa kwa wingi kungepelekea vifaa kuharibika, hasa ukizingatia kuwa Chuo kina changamoto kubwa ya ufinyu wa nafasi ya ghala. Hivyo manunuzi yalikuwa yakifanyika pale inapotokezea mahitaji tu kwa wakati husika.

Ofisi ya Mamlaka Pemba iliingiziwa fedha kutoka Makao Makuu ya Mamlaka Unguja na kutakiwa kufanyakazi ya ujenzi kwa mujibu wa taratibu za manunuzi za kawaida, ambapo Ofisi ya Mdhamini Pemba ilifanya hivyo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipofuatilia hoja hii ilibaini kweli kuna ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa vile taratibu za zabuni hazikufuatwa ipasavyo. Hata hivyo iliridhishwa na vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa na ujenzi wake kwa vile kama kungetumika utaratibu wa zabuni ingeilaziu Mamlaka kutumia fedha zaidi.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka ihakikishe inaandaa muongozo wake utakaopelekwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa ajili ya kuthibitishwa ili uwe ndio dira ya utekelezaji wa kazi zake.

3.22.12 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 21,225,000

Jumla ya shilingi 21,225,000 zimehaulishwa kutoka hesabu ya Vitongoji Development

kwenda hesabu nyengine tofauti na baadhi ya fedha hizokulipwa kwa watoa huduma mbali mbali kwa matumizi ya Chuo cha Mafunzo ya Amali - Pemba. Ukaguzi umebaini kwamba vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati ya malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanishwa vielelezo katika hati ya malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

1. Vocha namba 3/7 uhaulishwaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0404447000 ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba. Risiti ipo yenye namba 03337 ya tarehe 27/06/2019
2. Vocha namba 1/8 yenye thamani ya shilingi 3,600,000/- uhaulishwaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0511030000 ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Zanzibar. Risiti ipo yenye namba 13405 ya tarehe 30/08/2019.
3. Vocha namba 1/3 yenye thamani ya shilingi 6,155,000/- uhaulishwaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0404163000 ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba. Risiti ipo yenye namba 13406 ya tarehe 2/04/2020.
4. Vocha namba 1/5 yenye thamani ya shilingi 140,000/- malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya kusafirisha matufali kutoka kiwandani Vitongoji kwenda katika sehemu ya ujenzi wa vyoo na mashimo ya corona. Malipo hayo yalifanyika kwa kutumia subvoucher ya tarehe 4/5/2020, wakati wa ukaguzi hati hiyo haikuonekana kutokana na mapungufu ya kibinadamu, wakati wa uhakiki hati hiyo ilionekana na kuwekewa alama ya vyema.
5. Vocha namba 1/6 malipo ya fedha kwa ajili ya ushonaji wa barakowa kwa ajili ya matumizi ya Kituo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji (200pcs). Malipo hayo yalifanyika kwa kutumia risiti namba 5503 ya tarehe 30/6/2020. Wakati wa ukaguzi risiti hiyo haikuonekana, wakati wa uhakiki risiti hiyo ilionekana na kuwekewa alama ya vyema.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia ukaguzi wa hoja hiyo pamoja na majibu yake, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Mkaguzi hakupatiwa vielelezo wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, vielelezo hivyo viliwasilishwa nje ya muda wa ukaguzi na ndio maana baadhi ya hoja hizo zikaingizwa kitabuni.

Sambamba na hilo, Kamati imegundua kwamba Mamlaka haikuwa makini katika utekelezaji wa sheria ya Fedha za Umma na sheria nyengine kwani ilishindwa kuambatanisha vielelezo vya malipo mara tu baada ya malipo kukamilika pamoja na kuhifadhi vizuri vielelezo vya matumizi yake.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inafuata sheria na taratibu za malipo kwa kuambatanisha vielelezo vya malipo mara tu inapokamilisha malipo ili kumuwezesha Mkaguzi kufanya kazi yake kwa mujibu wa sheria ziliopo.
2. Mamlaka ihakikishe inaweka vizuri kumbukumbu za matumizi yake ili zinapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati.

3.22.13 Vifaa ambavyo taratibu za mapokezi hazikuthibitishwa shilingi 16,323,817.20

Jumla ya shilingi 16,323,817.20 zimelipwa kwa ajili ya usambazaji wa chakula na vifaa mbali mbali katika kambi ya usahihishaji wa mitihani ya STD IV katika skuli ya Fidel Castro. Malipo hayo yalifanywa kwa kutumia hati nambari 4/1 ya tarehe 23/1/2020 kwa kutumia hundi 000404 ambayo alilipwa Ndugu Farouk Salim Said kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba vifaa vilivyonunuliwa havikuingizwa katika daftari la kutunzia vifaa ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi na matumizi ya vifaa hivyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar Namba 11 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwamba wakati wa ukaguzi utaratibu wa uingizaji vifaa katika daftari la kurekodia vifaa ghalani vya kambi ya usainishaji mitihani ulikuwa haujakamilika, kwa sasa vifaa vyote tayari vimeshaingizwa katika daftari la kumbukumbu kama ulivyo utaratibu.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iligundua kwamba kukosekana kwa uelewa wa kuwepo mtendaji anayefahamu taratibu za kuweka kumbukumbu za vifaa vinavyoingia ghalani ilikuwa pia ni sababua nyengine iliyosababisha kuwepo kwa hoja hii. Kamati imelijua hili baada ya kuambiwa kwamba watendaji waliokuwepo walikuwa hawana ujuzi wa kutekeleza kazi hizo.

Mapendekezo ya Kamati
Mamlaka ihakikishe kunakuwepo daftari maalum la uhifadhi wa kumbukumbu za vifaa vinavyoingizwa na kutolewa ghalani.

3.22.14 Kukosekana kwa muongozo wa ulipwaji wa posho na gawio la faida shilingi 23,962,398
Jumla ya shilingi 23,962,398 zimelipwa na Chuo cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba kwa ajili ya posho pamoja na gawio la faida kwa watendaji walioshiriki katika kazi ya kutoa huduma kwa wasahihishaji wa mitihani ya darasa la nne.

Kutoambatanishwa vielelezo katika hati ya malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka
Muongozo unaonesha posho na gawio la faida upo.

Uchunguzi wa Kamati
Kamati imegundua kwamba muongozo upo tokea mwaka 2016 ila imeshindwa kufahamu kwanini hoja hiyo imebakia katika kitabu kwani Mamlaka ilieleza kwamba walimuonesha Mkaguzi muongozo huo.

Mapendekezo ya Kamati
Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ianzishe utaratibu wa kuwepo madaftari mawili (la Mkaguzi na Mkaguliwa) litakaloonesha makabidhiano ya mahitaji yote ya ukaguzi.

3.22.15 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 29,196,971
Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 29,196,971 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Chuo cha Mafunzo ya Amali lakini vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanishwa vielelezo katika hati ya malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

1. Vocha namba 1/8, malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa Chuo mwezi wa Juni, 2019. Kukosekana muongozo unaohusu ulipaji wa nauli za wafanyakazi wa Chuo. Ni kweli kuwa kwasasa Mamlaka haina muongozo wake wenyewe unaotumika kulipia nauli za wafanyakazi, ila inatumia muongozo wa Wiraza ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kulipa nauli hizo.
2. Vocha namba 7/1 malipo ya fedha kwa ajili ya usambazaji wa vyakula mbali mbali kwa ajili ya kambi ya usahihishaji wa mitihani ambayo imekosa ulizo la bei na barua ya maombi ya Mkuu wa Chuo. Ni kweli vielelezo hivyo

vilikosekana wakati wa ukaguzi, kwa sasa vielelezo hivyo vipo kama ulivyo utaratibu.

3. Vocha namba 4/2 malipo ya fedha za nauli na posho la kujikimu kwa safari kikazi Unguja kwa mkuu wa kituo na wasaidizi wake. Fomu za safari zipo, wakati wa ukaguzi hazikuonekana kutokana na mapungufu ya kibinaadamu.
4. Vocha namba 9/3 uhaulishaji wa fedha zilizotumika kwa ununuzi wa chakula cha mradi wa vijana na ajira - Kengeja kutoka A/C 0404068000 Vitongoji Skills Development Centre kwenda 044447000 Vocational Training Authority, kilichokosekana ni risiti ya mapokezi ya fedha. Ni kweli kuwa wakati wa ukaguzi risiti hiyo haikuwepo, kwa sasa risiti ipo yenye namba 05018 ya tarehe 23/3/2020.
5. Vocha namba 7/4 malipo ya fedha za posho ya chakula cha wanafunzi 240 wa mradi wa vijana na ajira katika kazi za vitendo Wilaya ya Mkoani, Chake, Wete na Micheweni, ambapo kilichokosekana ni muongozo wa malipo.
6. Mradi wa vijana na ajira ulitekelezwa katika awamu mbili, awamu ya kwanza wanafunzi walikaa katika vituo walivyopangiwa vya Vitongoji na Kengeja wakipatiwa mafunzo na huduma stahiki ikiwemo chakula na malazi kwa mujibu wa makubaliano. Awamu ya pili ya mradi wanafunzi walilazimika kuenda 'field' na kwamba Mamlaka ilipaswa iwawezeshe wanafunzi hao kujikimu katika maeneo yao ya 'field' ili kuwawezesha kufanya mafunzo yao viwandani kwa ufanisi. Kwa mukhtadha huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali alielekeza kuwa vijana hao wapatiwe posho ambalo litawawezesha kujikimu wakati wote watakapokuwa katika maeneo yao ya 'field' na ofisi ilitekeleza hilo.

Uchunguzi wa Kamati

1. Kuhusu majibu ya vocha nambari 1/8, kwa vile Mamlaka ilikubali kwamba walikuwa hawana muongozo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

2. Kwa upande wa majibu ya vocha nambari 7/1, Kamati iligundua kwamba vielelezo hivyo viliwasilishwa nje ya muda wa ukaguzi na kusababisha hoja hii kubakia katika ripoti ya Mdhibiti.

3. Kuhusu majibu ya vocha namba 4/2, Kamati ya LAAC haikufurahishwa na ilisikitishwa na majibu kwani jumla ya shilingi 1,725,000 zilitumika pasi na kuwepo vielelezo vinavyoonesha uhalali na usahihi wa matumizi hayo hasa ukizingatia kwamba hizo zote ni fedha za umma.

4. Kwa upande wa majibu ya vocha nambari 9/3, Kamati iligundua kwamba ni kweli risiti halasi ilikuwepo ila muda ambao risiti hiyo inapatikana (tarehe 23/3/2020)

Mkaguzi alikuwa ameshaondoka na hoja tayari imeshaingizwa kwenye kitabu.

5. Kuhusu majibu ya vocha nambari 7/4, Kamati iliridhishwa na majibu ya Watendaji wa Mamlaka na kwamba haikuwa na hoja zaidi.

Mbali na ukaguzi wa vocha za malipo, Kamati ilifanya ukaguzi maalum kuhusu upungufu mkubwa walimu unaopunguza kwa kiasi kikubwa ufanisi wa Vyuo vyote vinavyosimaiwa na Mamlaka ya Amali. Kamati lijibiwa kwamba Mamlaka ilichukua juhudi ya kuajiri walimu tofauti na tayari walikuwa washafikia hatua ya kufanyiwa 'vetting' katika ofisi ya 'GSO'. Lakushangaza, ajira hizo zimekwama kutokana na agizo la Serikali la kusimamisha ajira kwa kipindi hicho na kuelezwa kwamba watafute walimu kutoka katika Wizara za SMZ na kubahatika kupata walimu 14 wakati waliomba walimu 45.

Lakushangaza na kusikitisha zaidi kuna mwalimu ambaye alikuwa anawasaidia sana lakini amehamishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inaweka vizuri vielelezo vya matumizi iliyoyafanya ili viweze kupatikana wakati wa ukaguzi kama inavyotaka sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.
2. Mamlaka iwasilishe kwa wakati vielelezo vinavyohitajika na Mkaguzi anapokwenda katika maeneo yao ya kazi.
3. Mamlaka kwa vile Taasisi inayojitegemea katika baadhi ya mambo yake ihakikishe inaandaa muongozo unaohusu ulipaji wa nauli za wafanyakazi wa Chuo.

ZIARA MAALUM YA UKAGUZI WA KAMATI KATIKA DAKHALIA YA CHUO CHA MAFUNZO YA AMALI MKOKOTONI

Katika kufuatilia hoja nambari 3.22.4 iliyoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo inaelezea kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika Dakhalia kulinganisha na uwezo wa Dakhalia (Hostel). Tarehe 24 Januari, 2022, Kamati ilifanya ukaguzi maalum (ziara ya kushitukiza) wa kutembelea dakhalia hiyo na kukutana na viongozi wake ili kujiridhisha na majibu yaliyotolewa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar kwamba ni kweli katika dakhalia hizo katika mwaka wa fedha 2019/2020, chumba kimoja kilikuwa kinakaliwa na wanafunzi zaidi ya wanne kama vilivyo vitanda vilivyomo ndani ya chumba kimoja.

Pamoja na kwamba muda ambao kamati ilifika eneo hilo kulikuwa hakuna wanafunzi kwa vile chuo kilikuwa kimefungwa kwa likizo yake ya kawaida, mambo yafuatayo yaligundulika:

1. Kamati imethibitisha kwamba ni kweli mazingira yalikuwa yakionesha kitanda kimoja kilikuwa kinalaza wanafunzi zaidi ya wanane kama ilivyoelezwa na Mdhibiti. Kwa vile chumba kilikuwa na vitanda viwili vyenye magodoro manne

ambavyo vinachukua wanafunzi wanane wakati godoro moja linakuwa chini na kukamilisha hesabu ya wanafunzi kumi kwa chumba kimoja.
2. Dakhalia ilikuwa katika mazingira yenye mwitu jambo ambalo halitoi taswira nzuri ya kuwepo kwa chuo kinachotoa taaluma bora kwa watoto wetu.
3. Kamati imegundua chuo kinalo eneo linaloweza kutumika kwa kilimo cha mboga ambayo ingesaidia kulisha wanafunzi wanaosoma chuoni hapo lakini hakijaweza kulitumia ipasavyo eneo hilo ili liweze kutoa tija kwao.

Mapendekezo ya Kamati

1. Uongozi wa chuo uhakikishe unaweka katika dakhalia wanafunzi kwa mujibu wa nafasi za vitanda vilivyopo.
2. Uongozi wa Chuo uhakikishe dakhalia na Chuo kwa ujumla kinakuwa katika mazingira safi wakati wote ili kuleta taswira halisi ya chuo.
3. Uongozi wa chuo ubuni mbinu mbadala za kulitumia vizuri eneo lake hususan kwa shughuli za kilimo cha mboga ili kiepukana na gharama zisizo za lazima za ununuzi wa viungo.

3.22: MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR (VTA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 407,430,000. Hadi kufikia 30, Juni 2020 Mamlaka ilikusanya jumla ya shilingi 1,253,763,608 sawa na asilimia 307.72 ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mamlaka ilikusanya Jumla shilingi. 1,253,763,608 kutokana na vyanzo vyake vya ndani makusanyo hayo yameongezeka limetokana na sababu zifuatazo:-

1. Kuongezeka kwa vyanzo vya mapato ambavyo awali vilikuwa havijaingizwa katika bajeti ya mwaka 2019/2020, Makadirio ya makusanyo ya vyanzo hivi vilikuwa havijaingizwa katika makadirio ya makusanyo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Mamlaka ambazo ni shilingi 679,471,500/- ambazo ni sawa na asilimia 54.2% ya makusanyo halisi katika mwaka 2019/2020.

2. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliodahiliwa kwa mwaka wa masomo 2019/2020 kwa kozi mbali mbali zinazotolewa na Vituo vilivyo chini ya Mamlaka ya Elimu ya Amali.

Uchunguzi wa Kamati

Kufuatia majibu hayo, Kamati ilihoji ibainishiwe vyanza ambavyo Mamlaka haikuviingiza

katika makadirio ya mapato na kuelezwa kwamba kulikuwa na zabuni kutoka Wizara inayoshughulikia vijana pamoja na kikosi cha Polisi Tanzania ambavyo Mamlaka ilishinda na kupatiwa kazi ya utoaji mafunzo ya ujasiriamali ya kwa vijana na kupelekea kuwaingizia jumla ya shilingi 400,780,000 kwa mwaka 2019/2020.

Aidha Kamati ilibaini kuwa pamoja na kuvuka lengo la makusanyo hadi kufikia asilimia 307.07. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba fedha hizo hazikukatwa kodi kwa mujibu wa sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ili kodi hiyo iweze kuisaidia Serikali kutelekeza majukumu yake ipasavyo.

Kadhalika, Kamati iligundua kuwa mbali na sababu zilizoelezwa na Mamlaka zilizosababisha mapato kuongezeka, pia kulikuwa na sababu ya upatikanaji wa zabuni ya useremala katika chuo cha Daya na Makunduchi ambapo jumla ya shilingi 278,691,500 zilipatikana. Ongezeko hili ni fedha za Mradi wa Vijana na Ajira na fedha zilizoingizwa na Baraza la Mitihani kwa ajili ya utoaji wa huduma ya chakula kwa walimu wanaosahihisha Mitihani ya Taifa ya Zanzibar na fedha za Mradi wa Vitanda vya Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inapendekeza kwamba vyanzo vyote vya mapato vya Mamlaka ambavyo ina uwezo wa kuvikusanya viingizwe katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ili yaweze kuondoa mwaya kwa baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu kujinufaisha.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,168,630,000. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 6,174,273,998 ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 1,994,356,002.00 ikiwa ni matumizi ya maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni, 2020 kiasi cha shilingi 5,945,945,275.000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 96.30 ya makadirio na shilingi 1,082,127,320 zilitumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 54.25 ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwamba matumizi ya Mamlaka yanaonekana ni makubwa kulingana na kilichopatikana kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ambapo Mamlaka ilianza matumizi yake ikiwa na bakaa ya shilingi 436,310,593.05. Hata hivyo, makadirio ya makusanyo yatokanayo na ruzuku ya matumizi mengineyo (Other Charge - O/C) yamepungua kwa asilimia 30.39 ya makadirio kwa mwaka kutoka Serikali Kuu ndio yaliyopelekea Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya matumizi yake yaliyopangwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 kutokana na kuibuka kwa ungonjwa wa UVIKO 19 ambao umeathiri shughuli za kiuchumi katika Taasisi mbali mbali.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya LAAC imebaini kuwa jumla ya shilingi 436,310,593.05 zimetumika kinyume na

taratibu na maelekezo matumizi ya fedha za umma zanavyotaka. Utaratibu unataka, Taasisi inapobakisha fedha katika mwisho wake wa mwaka zinatakiwa kuwasilishwa katika hesabu ya hazina na baada ya mwaka mpya wa fedha kuanza, Mamlaka ilitakiwa iziombe ziingizwe katika hesabu ya Mamlaka tofauti na walivyofanya Mamlaka.

Vile vile, Kamati pia imegundua kuna ukiukwaji wa matumizi ya holela ya fedha za umma kwani matumizi katika kifungu cha posho maalum kilichoonekana katika hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka (Financial Statements) matumizi yake yalizidi bajeti iliyopangwa kwani jumla ya shilingi milioni 30 zilipangwa na kutumika shilingi 124,510,445. Mbali na hilo, Kamati iligundua kwamba Mamlaka inafanya kazi zake katika jengo la kukodi kutoka kwa mtu binafsi kwa shilingi milioni 26.3 kwa mwaka na tayari wameshapatiwa eneo liliopo karibu na Wizara ya Elimu lakini bado ujenzi kamili haujaanza.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inapofungua 'deposit account' kwa ajili ya kuweka fedha zilizokuwa hazijatumika hadi zikafikiwa na mwaka mwengine wa fedha.
2. Mamlaka ifanye matumizi yake kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bodi ya Mamlaka.
3. Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu iharakishe ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ili ipunguze upotevu wa fedha nyingi zinazotumika kwa kulipia kodi.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.22.1 Tofauti iliyojitokeza baina ya makusanyo halisi na kilichoripotiwa katika taarifa ya fedha shilingi 283,171,319.44

Katika kupitia stakabadhi za makusanyo ya mapato, taarifa za kibenki na daftari la fedha. Ukaguzi umebaini kwamba kuna tofauti ya upungufu wa shilingi 283,171,319.44 zilizoainishwa katika taarifa ikilinganishwa na iliyoripotiwa katika taarifa za makusanyo halisi yaliyopatikana vituoni na Afisi Kuu ya Mamlaka. Kuwepo kwa tofauti baina ya makusanyo halisi kutoka vituoni na Afisi kuu kunapelekea taarifa zote za fedha kutotoa sura nzuri na sahihi kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

Bajeti	Taarifa za kifedha	Makusanyo halisi	tofauti
214,800,000	1,245,036,512.56	1,528,207,832	283,171,319.44

Majibu ya Mamlaka

Kwa kuwa Mamlaka inatumia Mfumo wa Uandaaji wa Taarifa zake kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IPSAS Cash Basis), Sheria na Kanuni za Fedha za Ndani (Public Finance Managent Act ya Zanzibar) pamoja na Miongozo mbali mbali ya uandaaji wa hesabu inayotolewa na Ofisi ya Fedha na Mipango Zanzibar juu ya utayarishaji wa Hesabu, ambayo imeitaka Mamlaka kuandaa taarifa za fedha za mwaka kwa kuangalia kiwango cha fedha halisi zilizokusanywa katika hesabu za kibenki pamoja na matumizi halisi yaliyofanyika katika mwaka wa fedha husika bila ya kuzingatia kiwango cha fedha zitokanazo na madeni kwa kipindi cha Julai hadi Juni ya kila mwaka.

Kwa maelezo haya taarifa zilizowasilishwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa wakaguzi zilikuwa ni sahihi kwa mujibu wa vielelezo vya ''Bank Statement''. Hii ni kutokana na michango yote ya wanafunzi na Fedha zinazotoka kwa Wahisani wa Maendeleo zinawasilishwa kupitia Benki. Hivyo ukusanywaji wa fedha unategemea miamala ya Benki ambayo ipo sahihi.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipofuatilia hoja hii na kufuatilia majadiliano na malumbano yaliyokuwa yakitolewa na watendaji wa Mamlaka kwa watendaji wa Mdhibiti (CAG) kwamba taarifa zote zilizowasilishwa mbele ya Kamati walipatiwa CAG ila wanashangaa taarifa iliyotolewa dhidi yao. Kamati iligundua kuwa kulikosekana mashirikiano ya karibu baina ya pande mbili hizo. Hali hiyo, hupelekea kutofikia ipasavyo lengo la ukaguzi husika.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kuwepo mashirikiano ya karibu baina ya wakaguzi na wakaguliwa ili kuweza kufanikisha lengo la ukaguzi la kupata taarifa na vielelezo sahihi.
2. Kuwepo na madaftari mawili (la CAG na la Taasisi) yatakayosaidia kuweka kumbukumbu za vielelezo na taarifa kamili za Mkaguzi na Taasisi inayokaguliwa.

3.22.2 Kukosekana kwa uhalisia wa makisio ya makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi.

Ukaguzi ulipitia taarifa ya makisio ya makusanyo yasyo ya kodi pamoja na uhalisia wa makusanyo katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwka 2020 za Mamlaka na kubaini uwepo wa tofauti ya shilingi 1,313,407,832 iliyotokana na makusanyo halisi kuwa makubwa zaidi ya makisio na kupelekea uwepo wa tofauti isiyo ya kawaida. Ufafanuzi wa makusanyo hayo ni kama yanavyoonekana katika Jadweli:

Bajeti ya Mapato ya kodi (Tzs.)	Makusanyo halisi ya Mapato (Tzs.)	Tofauti
214,800,000	1,313,407,832	1,313,407,832.00

Majibu ya Mamlaka

Katika mwaka wa 2019/2020 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ilikuwa na makusanyo

yasio na kodi ya aina mbili kuu ambayo ni ada ya wanafunzi na fedha kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo. Kwa ujumla wake zilikadiriwa kuwa shilingi 407,430,000 ambazo makusanyo halisi zilikuwa ni shilingi 1,245,036,512.56.

Ni kweli katika mwaka wa fedha 2019/2020 kulikosekana uhalisia wa makisio ya makusanyo pamoja na makusanyo halisi ambayo yalisababishwa na kutokuwepo kwa matarajio ya makusanyo mpaka bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Kusababishwa kutokuwepo katika mipango ya Mamlaka kwa kipindi hicho. Hata hivyo kwa kuwa fedha hizo ziliingizwa katikati ya mwaka wa fedha ziliweza kutumika kwa mahitaji ya shughuli zilizopangiwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Ongezeko hili ni fedha za Mradi wa Vijana na Ajira na fedha zilizoingizwa na Baraza la Mitihani kwa ajili ya utoaji wa huduma ya chakula kwa walimu wanaosahihisha Mitihani ya Taifa ya Zanzibar na fedha za Mradi wa Vitanda vya Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imegendua kwamba uchunguzi wa hoja hii unafanana na hoja ya mwanzo ya ongezeko la Mapato. Hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

3.22.3 Vifaa vilivyohifadhiwa muda mrefu bila matumizi vyenye thamani ya shilingi 118,901,079

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imenunua vifaa mbali mbali kutoka kwa Mzabuni Furniture Centre Ltd. kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mamlaka inayotarajiwa kujengwa. Vifaa hivyo vimenunuliwa tarehe 3/4/2014 kupitia Mradi wa ALDL ambao ndio Mradi uliojenga kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni. Lakini ukaguzi umebaini vifaa hivyo vimehifadhiwa katika vyumba viwili vya dahalia ya wanawake kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita bila ya matumizi.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba vifaa vimekosa ushahidi wa nyaraka za kupokelewa mali ghalani. Vifaa hivyo vilikuwa na jumla ya shilingi 118,901,078.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli mradi wa ALSD II ulinunua vifaa mbali mbali vya kiofisi kupitia Mzabuni wa Furniture Center kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mamlaka inayotarajiwa kujengwa kupitia mradi huo. Ujenzi haukufanyika kutokana na uhaba wa fedha kwa kipindi hicho cha Mradi. Hata hivyo, baadhi ya vifaa hivyo vinatumiwa na Ofisi kuu na Maktaba iliyopo Chuo cha Mafunzo ya Amali Mwankwerekwe na vichache vilivyobaki vinatarajiwa kutumika katika majengo mapya yaliyojengwa katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni. Aidha, Vifaa hivyo vilipokelewa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

Uchunguzi wa Kamati

Pamoja na Kamati kukiri kununuliwa na kupelekwa Mkokotoni kuhifadhiwa vifaa hivyo, Kamati imebaini kwamba Mradi huo ulitekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha Amali Makunduchi, Daya na ujenzi wa Afisi Kuu ya Mamlaka kwa awamu tofauti pasi na kuwepo ushirikishwaji wa karibu kutoka kwa watendaji wa Mamlaka. Hili limethibitika kwamba wakati Mkaguzi amefika Mamlaka kwa ajili ya ukaguzi hakuweza kupatiwa vielelezo hivyo ambavyo vyengine vilikuwepo Wizarani kwa vile ndio waliokuwa wasimamizi wakuu wa mradi huo. Hata hivyo, Kamati ilipatiwa vielelezo hivyo kwa ukaguzi.

Aidha, Kamati imebaini kwamba Wizara au Mamlaka haikuwa na mpango mzuri wa matumizi ya fedha hizo kwani waliamua kununua vifaa (viti) pasi na kumaliza majengo ya kuingiza viti hivyo. Hali hiyo inapelekea kuwepo matumizi mabaya wa mali za umma.

Mapendekezo ya Kamati

1. Wizara au Mamlaka inapokopa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi fulani iwe na mpango na mikakati mizuri ya kujikita katika utekelezaji wa mradi huo na sio vyenginevyo.
2. Utekelezaji wa Miradi ufanywe na Mamlaka husika na sio kuchukuliwa na kutekelezwa na Wizara husika.
3. Kuwepo utaratibu mzuri wa uwekaji kumbukumbu na ziwe zinapatikana wakati vinapohitajika.

3.22.4 Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika Dakhalia kulinganisha na uwezo wa Dakhalia (Hostel)

Ukaguzi umebaini kwamba kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni kina upungufu wa dakhalia usiokidhi mahitaji ya wanafunzi, hivyo husababisha mrundikano wa wanafunzi katika vyumba vya dakhalia hizo. Mapitio ya ukaguzi yamebaini kwamba chumba kimoja chenye uwezo wa kulaza wanafunzi wa 4 kinalaza wanafunzi 10 hali inayohatarisha afya na usalama wa wanafunzi. Aidha, dakhalia hizo haina viingiza hewa vya kutosha ikiwemo madirisha na mafeni.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa hivi sasa ina matatizo ya uhaba wa majengo ya dakhalia kulinganisha na mahitaji ya wanafunzi wanaotaka kuishi katika dakhalia hizo. Mamlaka imeliona tatizo hilo na imeshaanza juhudi ya kuandaa michoro ya dakhalia mpya. Hata hivyo, kuanza kutumika kwa vyuo vipya vya Daya na Makunduchi itasaidia kupunguza ukali wa tatizo hilo.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hiyo, Kamati iligundua uwepo wa utata kwa vile watendaji wa

Mamlaka walikiri kuwepo kwa upungufu wa dakhalia za wanafunzi isipokuwa walikanusha hoja ya Mkaguzi kwamba kulikuwa na mrundikano wa wanafunzi hadi kufikia chumba kimoja kutumiwa kulaza wanafunzi 10. Kutokana na mkanganyiko huo, Kamati ilipanga kufanya ziara ya kushitukiza katika chuo cha Mkokotoni na Dakhalia yake ili kuweza kupata tswira kamili juu ya ukweli wa jambo hilo.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kwa vile mpango wa uendelezaji wa vyuo vya Amali upo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali iwaingizie fedha za kutosha ili Mamlaka iweze kutekeleza miradi yake.

2. Mamlaka iruhusiwe kuitekeleza Miradi yake wenyewe.

3.22.5 Dosari iliyobainika katika malipo ya mikataba ya zabuni yenye jumla ya shilingi 332,376,974

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari inayotokana na malipo ya mikataba ya zabuni ya wanaotoa huduma, kwa mujibu wa makubaliano ya pande zote mbili, malipo ya mikataba yote yatafanywa kwa awamu mbili ambayo ni asilimia 90 na asilimia 10 baada ya kumalizika kwa kazi. Mamlaka imekiuka masharti hayo kwa kulipa asilimia 100 kwa kila mkataba wa zabuni uliofungwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 31(f) cha sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Miongoni mwa watoa huduma waliogundulika kuwa na dosari katika mikataba yao ni Diamond Motor Ltd, Greenland General Supply Company Ltd na Visiwani General Supplies.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakubaliana na ushauri ulitolewa na Mkaguzi, ni kweli kiutaratibu malipo yalitakiwa kufanyika kwa awamu mbili, Awamu ya kwanza wakati anaposaini Mkataba kwa asilimia tisini (90%) na asilimia kumi (10%) baada ya kukamilika kwa kazi kama terms za mkataba zilivyotaka. Kwa kuwa Mamlaka ilishindwa kutekeleza mkataba katika kipengele cha malipo kwa muda na ni kwasababu ya kukosekana kwa fedha ndio ilipopelekea kulipwa kwa asilimia Mia Moja baada ya kumalizika kwa Kazi.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa vile Mamlaka ilikiri kutokezea kwa kosa hilo, na Kamati imejiridhisha kupitia Mkataba husika na kugundua kweli kosa lilifanyika na hatimae Kamati ilitoa mapendekezo yake.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka itekeleze mikataba yake kama inavyojieleza.

MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI (MMA) - PEMBA

3.22.6 Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya kukusanya mapato ya shilingi 51,620,000

Jumla ya shilingi 51,620,000 zilikadiriwa kukusanywa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio hayo ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 42,699,398 zilikusanywa sawa na asilimia 82.7 ya makadirio ambapo hali hii inaonesha Mamlaka imeshindwa kufikia malengo ya makusanyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 32(1)(2) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Makusanyo ya Mamlaka/Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji yanategemea ada za wanafunzi, ruzuku kutoka Serikali kuu na miradi midogo midogo ya ndani ikiwemo kodi za ukumbi, mauzo ya fomu za kujiunga na Chuo kwa kila mwaka.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Taasisi imeshindwa kufikia malengo ya makusanyo ya Tsh 51,620,000 na kufanikiwa kukusanya Tsh 42,699,398 ambayo ni sawa na 82.7% ya makadirio. Hii imetokana na changamoto kubwa ya kuibuka kwa maradhi ya Uviko 19, ambayo yalipelekea Chuo kufungwa na kusitisha njia zote za mapato, jambo hili lilipelekea kuzorota kwa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na shughuli walizozianisha hapo juu na kupelekea kuto kufikia malengo. Pia chuo kilitumika kama ni kituo cha kuhifadhia wagonjwa wa Uviko 19 kwa Pemba, na kupelekea shughuli zote za Chuo kusimama kwa muda.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iliridhishwa na majibu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba isipokuwa ilitaka kujua Wizara ya Afya ilichangia chochote katika kipindi chote waipokuwa wakilitumia eneo hilo na kuelezwa kwamba hawakuchangia kwa kutoa fedha taslim ila walikarabati jeng hilo.

3.22.7 Kukosekana kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba haina Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kuweza kusimamia shughuli za ukaguzi wa ndani na utoaji wa taarifa juu ya makusanyo na matumizi ya fedha za Serikali.

Kutokuwepo kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani inaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha na mali za umma, aidha ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma Zanzibar namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ina mfumo wa ukaguzi wa ndani ambao unajitegemea,

ambapo kila ifikapo mwisho wa kota wakaguzi wa Mamlaka kutoka Makao Makuu Unguja hukagua na kufunga mahesabu ya Idara zote za Mamlaka Unguja na Pemba, na huwasilisha ripoti ya ukaguzi kwenye vikao vya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka.

Suala hili limeonekana kua ni changamoto katika utendaji na tayari Ofisi imeshafanya juhudi mbali mbali za kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani Pemba, ikiwemo kuandika barua za maombi ya kupatiwa mkaguzi wa ndani, kufanya mazungumzo ya ana kwa ana na Afisa Mdhamini Wiraza ya Fedha - Pemba ya kumshawishi kutupatia watendaji wa ukaguzi wa ndani, pia Ofisi imeshaliwasilisha suala hili kwa Mkurugenzi Mtendaji na Bodi ya wakurugenzi kupitia ripoti za utekelezaji za robo mwaka.

Uchunguzi wa Kamati

Katika uchunguzi wake, Kamati imebaini kuwa barua za kuomba Mkaguzi wa ndani kweli zilikuwepo ila hazikuwa zikijibia kwa maandishi na Ofisi ya Afisa Mdhamini wa Wizara ya Fedha na Mipango - Pemba ili kupata kujua kwa kiasi gani suala hilo linafanyiwa kazi.

Mapendekezo ya Kamati

1. Wizara ya Fedha na Mipango iharakishe kuipatia Muhasibu Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba ili kupunguza gharama za kiutendaji.

2. Ofisi ya Afisa Mdhamini ijibu barua za maombi ya watendaji zinazoelekezwa kwao.

3.22.8 Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa Mamlaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka - Pemba haina Mpango wa Manunuzi wa Mwaka ili kuweza kuthibitisha Mpango wa Manunuzi mzima wa Mamlaka na utekelezaji wake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 29(e) cha sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma namba 11 ya mwaka 2016 pamoja na kifungu cha 46(1)(2) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Zanzibar namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba ni sehemu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mamlaka Pemba hupata fedha za kuendeshea shughuli za kiutendaji kutoka Makao Makuu ya Mamlaka Unguja. Aidha, Utaratibu unaofuatwa ndani ya Mamlaka ni kutumia mpango mmoja wa manunuzi Unguja na Pemba.

Uchunguzi wa Kamati

Kwa vile Mamlaka imekiri kutokezea kwa kasoro hiyo na kuomba kujirekebisha kwani walikuwa hawana uelewa kwamba wanahitajika kuwa na mpango wao unaojitegemea kama zilivyo Mamlaka nyengine ziliopo Pemba. Kwa hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

3.22.9 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 13,296,979

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 13,296,979 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba lakini vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo.

Kutoambatanishwa vielelezo katika hati ya malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

1. Vocha nambari 1/7 ya malipo ya fedha za posho na chakula kwa usimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali. Barua ya maombi hayo ipo yenye tarehe 02/07/2019 na risiti namba 0786. Kuhusu kukosekana kwa barua ya maombi kutoka kwa Mkuu wa Chuo ni kuwa, Mkuu wa chuo siye anayeratibu mitihani ya Taifa ya Mamlaka na kwamba mitihani hiyo huratibiwa na Mratibu wa Mafunzo Ofisi kuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba ambae ndie aliyeandika barua ya Maombi.
2. Vocha namba 1/1,19/1, 4/2, 1/3, 4/3, na 22/3 malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa Mamlaka. Kukosekana kwa muongozo unaohusu ulipajiwa nauli za wafanyakazi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Ni kweli kuwa kwasasa Mamlaka haina muongozo wake wenyewe unaotumia kulipia nauli za wafanya kazi, ila inatumia muongozo wa Wiraza ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kulipa nauli hizo.
3. Vocha namba 2/2 kukosekana kwa risiti ya malipo ya fedha kwa ajili ya usanifu wa mchoro na utayarishaji wa makadirio ya ujenzi wa nyumba ya wageni. Ni kweli kuwa wakati wa ukaguzi risiti ya malipo hayo haikuwepo, hii ni kutokana na kuwa risiti aliyoleta supplier ilikuwa na makosa ya jina la Taasisi, ambapo Ofisi iliirejesha kwa muhusika ili aifanyie marekebisho na kwamba hadi ukaguzi unakamilika risiti haikuwa imepatikana. Ofisi ilifanya jitihada za kuifatilia risiti hiyo na kwa sasa risiti hiyo ipo.
4. Kwa upande wa ramani na BOQ ni kuwa wakati wa ukaguzi ramani na BOQ ya jengo zilikuwepo ila kutokana na mapungufu ya kibinadamu vitu hivi havikuweza kuwasilishwa, kwa sasa vitu hivyo vipo na vipo tayari kukaguliwa.
5. Vocha namba 22/2 malipo ya fedha za posho la usimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali. Barua ya maombi hayo ipo yenye tarehe 26/02/2020 na orodha wa Mahudhurio ya wasimamizi wa mitihani. Kuhusu kukosekana kwa barua ya maombi kutoka kwa mkuu wa Chuo ni kuwa, Mkuu wa chuo siye anae ratibu mitihani ya Taifa ya Mamlaka na kwamba mitihani hiyo huratibiwa na Mratibu wa Mafunzo Ofisi kuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba ambae ndie alie andika barua ya Maombi hayo. Kuhusu Orodha wa mahudhurio ni kuwa orodha hizo zilikuwepo na mkaguzi alizipitia na kuziweka alama ya vyema.
6. Vocha namba 23/2 marejesho ya fedha zilizotumika kwa chai na chakula kwa wasimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali. Barua ya maombi hayo ipo yenye tarehe 26/02/2020 na orodha wa Mahudhurio ya

wasimamizi wa mitihani. Kuhusu kukosekana kwa barua ya maombi kutoka kwa Mkuu wa Chuo ni kuwa, Mkuu wa chuo siye anae ratibu mitihani ya Taifa ya Mamlaka na kwamba mitihani hiyo huratibiwa na Mratibu wa Mafunzo Ofisi kuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba ambae ndie alie andika barua ya Maombi hayo. Kuhusu Orodha wa mahudhurio ni kuwa orodha zilikuwepo.

7. Vocha namba 3/3 malipo ya fedha za imprest kwa matumizi madogo madogo ya Chuo cha Mafunzo ya Amali. Marejesho yapo na mkaguzi alikuja kuyahakiki na kuweka alama ya vyema baada ya uhakiki huo
8. Vocha namba 5/2 kuhusu malipo ya fedha za kodi ya TRA iliyokatwa kwa wafanyabiashara kwa mwezi wa Januari, 2020. Risiti ipo yenye nambari ZN21453341, tayari imefanyiwa verification.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kamati iliridhika na majibu ya vocha nambari 1/7 yaliyotolewa na Watendaji wa Mamlaka pamoja na kielelezo cha barua kilichokaguliwa. Kwa hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.
2. Kwa upande wa majibu ya vocha nambari 1/1,19/1, 4/2, 1/3, 4/3, na 22/3, Kamati imegundua kwamba Mkaguzi alipopita kwa ukaguzi, Mamlaka haikuwa na muongozo wa Wafanyakazi kwa vile uliwasilishwa katika Bodi kupitia waraka nambari 16.16.1 ikiwa ni agenda ya 16 ya barua ya tarehe 27 Septemba, 2021. Kwa maana hiyo, Muongozo huo uliandaliwa na kuwasilishwa nje ya muda wa ukaguzi wa 2019/2020.
3. Kwa upande wa majibu ya Vocha nambari 2/2, Kamati iliridhika na jibu la kutokuwepo kwa risiti ya usarifu wa mchoro wa jengo la nyumba ya wageni wakati wa ukaguzi ila haikuridhishwa na jibu la kutokuwepo kwa BOQ kwa vile hiyo ni kielelezo ambacho kinatakiwa kiwepo katika eneo la kazi ambalo Mkaguzi alikwenda kwa ajili ya ukaguzi lakini hakuikuta.
4. Kuhusu majibu ya vocha nambari 22/2, Kamati iliridhishwa na majibu na haikuwa na hoja zaidi.
5. Kuhusu majibu ya vocha nambari 23/2, Kamati iliridhishwa na majibu ya watendaji isipokuwa ilishangazwa na maelezo kwamba risiti za vielelezo zilikuwepo wakati wa Ukaguzi lakini hoja imeingia kwenye kitabu.
6. Kuhusu majibu ya vocha nambari 3/3, Kamati ilishangazwa na kwamba Mkaguzi alihakiki marejesho ya 'imprest' na kuyawekea alama ya vyema ambazo Kamati imeziona lakini hoja imeingizwa kwenye kitabu.
7. Kwa upande wa majibu ya vocha nambari 5/2, kuhusu malipo ya fedha za kodi ya TRA, Kamati imeridhishwa na majibu kwa vile imeweza kuona vielelezo vya malipo hayo ila ilishangazwa na uwepo wa hoja hii wakati kuna maelezo kwamba Mkaguzi alioneshwa vielelezo hivyo.

Uchunguzi wa Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inakamilisha muongozo wa wafanyakazi wake ili iwe dira katika utekelezaji wa majukumu yake.
2. Mamlaka ihakikishe inafuata kikamilifu sheria ya Usimamizi wa Fedha ili wanapotekeleza miradi yao kuwepo na vielelezo vyote vinavyohitajika kwa

ukaguzi ikiwemo BOQ.

3. Kuondosha utata katika utekelezaji wa kazi za ukaguzi, Mkaguzi na Mkaguliwa kila mmoja aandae daftari la makabidhiano ya mahitaji yote ya ukaguzi ambapo daftari la Mkaguzi litajazwa na Mkaguliwa na la Mkaguliwa litajazwa na Mkaguzi.

3.22.10 Kukosekana kwa zabuni ya Mkandarasi wa Ujenzi wa Jengo la Maabara katika Chuo cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba.

Jumla ya shilingi 107,147,338.78 zimelipwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba kwa Mkandarasi wa ujenzi wa jengo la Maabara katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji. Ukaguzi umebaini kwamba malipo ya Mkandarasi huyo hayakuzingatia uwepo wa zabuni kulingana na kiwango cha fedha alicholipwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 68(1)(2)(3)(4) cha sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar namba 11 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Ujenzi wa jengo hili ulidhamiriwa kuwa sehemu ya kuwajengea uwezo walimu na pia kuwapatia wanafunzi fursa ya kufanyakazi za vitendo kupitia 'live projects', kwa sababu hiyo, Mkurugenzi Mtendaji kwa nia njema alitoa agizo la kuwa, kazi ya ujenzi wa Jengo la Maabara ifanywe na Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji kupitia Idara zake. Kwa utaratibu huo kila Idara ilishiriki katika ujenzi huo kulingana na kazi/fani zao. Kitendo cha kukipatia Chuo kazi kama hizi kinapelekea kukitangaza chuo, kuwajengea uzoefu walimu pamoja na wanafunzi kupata uzoefu mkubwa wa kazi, jambo ambalo litawawezesha wanafunzi wanapohitimu kujiajiri wenyewe.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iliridhika na majibu ya hoja hiyo yaliyotolowa na watendaji kwa vile kufanya hivyo kunanusuru fedha nyingi za Serikali ambazo zilitakiwa zitolewe ili Mamlaka iweze kununua vifaa vya kuwafundishia kivitendo wanafunzi wao lakini pia inawapatia uzoefu (mazoezi) wa kutosha walimu na wanafunzi wao. Sambamba na hayo, inaimarisha mazingira ya chuo kwa kuwapatia majengo ya kisasa kwani Kamati ilipata fursa ya kuyaona majengo hayo na kuridhika na ujenzi wake.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka iiandikie barua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kupata ufafanuzi na muongozo wa kufanyakazi za ujenzi kama ni sehemu ya mafunzo lakini kwa upande mwengine kunatokea ukiukwaji wa sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar namba 11 ya mwaka 2016.

3.22.11 Kukosekana kwa zabuni ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi shilingi 236,296,842.1

Jumla ya shilingi 236,296,842.1 zimelipwa na Mamlaka - Pemba kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya ujenzi wa jengo la Maabara katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji.

Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakuzingatia uwepo wa zabuni kulingana na kiwango cha fedha kilichotumika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 68(1)(2)(3)(4) cha sheria ya Ununuzi na Uondoji wa mali za Umma Zanzibar namba 11 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Utaratibu kujenga kwa kutumia nguvu kazi ya walimu na wanafunzi katika ujenzi ulipelekea mfumo wa manunuzi ya vifaa kufanyika kwa mujibu wa mahitaji ya mafundi kwa wakati husika, na kwamba kama kungefanyika manunuzi ya vifaa kwa wingi kungepelekea vifaa kuharibika, hasa ukizingatia kuwa Chuo kina changamoto kubwa ya ufinyu wa nafasi ya ghala. Hivyo manunuzi yalikuwa yakifanyika pale inapotokezea mahitaji tu kwa wakati husika.

Ofisi ya Mamlaka Pemba iliingiziwa fedha kutoka Makao Makuu ya Mamlaka Unguja na kutakiwa kufanyakazi ya ujenzi kwa mujibu wa taratibu za manunuzi za kawaida, ambapo Ofisi ya Mdhamini Pemba ilifanya hivyo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilipofuatilia hoja hii ilibaini kweli kuna ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa vile taratibu za zabuni hazikufuatwa ipasavyo. Hata hivyo iliridhishwa na vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa na ujenzi wake kwa vile kama kungetumika utaratibu wa zabuni ingeilaziu Mamlaka kutumia fedha zaidi.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka ihakikishe inaandaa muongozo wake utakaopelekwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa ajili ya kuthibitishwa ili uwe ndio dira ya utekelezaji wa kazi zake.

3.22.12 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 21,225,000

Jumla ya shilingi 21,225,000 zimehaulishwa kutoka hesabu ya Vitongoji Development kwenda hesabu nyengine tofauti na baadhi ya fedha hizokulipwa kwa watoa huduma mbali mbali kwa matumizi ya Chuo cha Mafunzo ya Amali - Pemba. Ukaguzi umebaini kwamba vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati ya malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanishwa vielelezo katika hati ya malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

1. Vocha namba 3/7 uhaulishwaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0404447000 ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba. Risiti ipo yenye namba 03337 ya tarehe 27/06/2019
2. Vocha namba 1/8 yenye thamani ya shilingi 3,600,000/- uhaulishwaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0511030000 ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Zanzibar. Risiti ipo yenye namba 13405 ya tarehe 30/08/2019.
3. Vocha namba 1/3 yenye thamani ya shilingi 6,155,000/- uhaulishwaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0404163000 ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali - Pemba. Risiti ipo yenye namba 13406 ya tarehe 2/04/2020.
4. Vocha namba 1/5 yenye thamani ya shilingi 140,000/- malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya kusafirisha matufali kutoka kiwandani Vitongoji kwenda katika sehemu ya ujenzi wa vyoo na mashimo ya corona. Malipo hayo yalifanyika kwa kutumia subvoucher ya tarehe 4/5/2020, wakati wa ukaguzi hati hiyo haikuonekana kutokana na mapungufu ya kibinadamu, wakati wa uhakiki hati hiyo ilionekana na kuwekewa alama ya vyema.
5. Vocha namba 1/6 malipo ya fedha kwa ajili ya ushonaji wa barakowa kwa ajili ya matumizi ya Kituo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji (200pcs). Malipo hayo yalifanyika kwa kutumia risiti namba 5503 ya tarehe 30/6/2020. Wakati wa ukaguzi risiti hiyo haikuonekana, wakati wa uhakiki risiti hiyo ilionekana na kuwekewa alama ya vyema.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia ukaguzi wa hoja hiyo pamoja na majibu yake, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Mkaguzi hakupatiwa vielelezo wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, vielelezo hivyo viliwasilishwa nje ya muda wa ukaguzi na ndio maana baadhi ya hoja hizo zikaingizwa kitabuni.

Sambamba na hilo, Kamati imegundua kwamba Mamlaka haikuwa makini katika

utekelezaji wa sheria ya Fedha za Umma na sheria nyengine kwani ilishindwa kuambatanisha vielelezo vya malipo mara tu baada ya malipo kukamilika pamoja na kuhifadhi vizuri vielelezo vya matumizi yake.

Mapendekezo ya Kamati

3. Mamlaka ihakikishe inafuata sheria na taratibu za malipo kwa kuambatanisha vielelezo vya malipo mara tu inapokamilisha malipo ili kumuwezesha Mkaguzi kufanya kazi yake kwa mujibu wa sheria ziliopo.
4. Mamlaka ihakikishe inaweka vizuri kumbukumbu za matumizi yake ili zinapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati.

3.22.13 Vifaa ambavyo taratibu za mapokezi hazikuthibitishwa shilingi 16,323,817.20

Jumla ya shilingi 16,323,817.20 zimelipwa kwa ajili ya usambazaji wa chakula na vifaa mbali mbali katika kambi ya usahihishaji wa mitihani ya STD IV katika skuli ya Fidel Castro. Malipo hayo yalifanywa kwa kutumia hati nambari 4/1 ya tarehe 23/1/2020 kwa kutumia hundi 000404 ambayo alilipwa Ndugu Farouk Salim Said kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba vifaa vilivyonunuliwa havikuingizwa katika daftari la kutunzia vifaa ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi na matumizi ya vifaa hivyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar Namba 11 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwamba wakati wa ukaguzi utaratibu wa uingizaji vifaa katika daftari la kurekodia vifaa ghalani vya kambi ya usainishaji mitihani ulikuwa haujakamilika, kwa sasa vifaa vyote tayari vimeshaingizwa katika daftari la kumbukumbu kama ulivyo utaratibu.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati iligundua kwamba kukosekana kwa uelewa wa kuwepo mtendaji anayefahamu taratibu za kuweka kumbukumbu za vifaa vinavyoingia ghalani ilikuwa pia ni sababua nyengine iliyosababisha kuwepo kwa hoja hii. Kamati imelijua hili baada ya kuambiwa kwamba watendaji waliokuwepo walikuwa hawana ujuzi wa kutekeleza kazi hizo.

Mapendekezo ya Kamati

Mamlaka ihakikishe kunakuwepo daftari maalum la uhifadhi wa kumbukumbu za vifaa vinavyoingizwa na kutolewa ghalani.

3.22.14 Kukosekana kwa muongozo wa ulipwaji wa posho na gawio la faida shilingi 23,962,398

Jumla ya shilingi 23,962,398 zimelipwa na Chuo cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali -

Pemba kwa ajili ya posho pamoja na gawio la faida kwa watendaji walioshiriki katika kazi ya kutoa huduma kwa wasahihishaji wa mitihani ya darasa la nne.

Kutoambatanishwa vielelezo katika hati ya malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

Muongozo unaonesha posho na gawio la faida upo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati imegundua kwamba muongozo upo tokea mwaka 2016 ila imeshindwa kufahamu kwanini hoja hiyo imebakia katika kitabu kwani Mamlaka ilieleza kwamba walimuonesha Mkaguzi muongozo huo.

Mapendekezo ya Kamati

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ianzishe utaratibu wa kuwepo madaftari mawili (la Mkaguzi na Mkaguliwa) litakaloonesha makabidhiano ya mahitaji yote ya ukaguzi.

3.22.15 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 29,196,971

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 29,196,971 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Chuo cha Mafunzo ya Amali lakini vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanishwa vielelezo katika hati ya malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mamlaka

1. Vocha namba 1/8, malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa Chuo mwezi wa Juni, 2019. Kukosekana muongozo unaohusu ulipaji wa nauli za wafanyakazi wa Chuo. Ni kweli kuwa kwasasa Mamlaka haina muongozo wake wenyewe unaotumika kulipia nauli za wafanyakazi, ila inatumia muongozo wa Wiraza ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kulipa nauli hizo.

2. Vocha namba 7/1 malipo ya fedha kwa ajili ya usambazaji wa vyakula mbali mbali kwa ajili ya kambi ya usahihishaji wa mitihani ambayo imekosa ulizo la bei na barua ya maombi ya Mkuu wa Chuo. Ni kweli vielelezo hivyo vilikosekana wakati wa ukaguzi, kwa sasa vielelezo hivyo vipo kama ulivyo utaratibu.

3. Vocha namba 4/2 malipo ya fedha za nauli na posho la kujikimu kwa safari kikazi Unguja kwa mkuu wa kituo na wasaidizi wake. Fomu za safari zipo, wakati wa ukaguzi hazikuonekana kutokana na mapungufu ya kibinaadamu.

4. Vocha namba 9/3 uhaulishaji wa fedha zilizotumika kwa ununuzi wa chakula cha mradi wa vijana na ajira - Kengeja kutoka A/C 0404068000 Vitongoji Skills Development Centre kwenda 044447000 Vocational Training Authority, kilichokosekana ni risiti ya mapokezi ya fedha. Ni kweli kuwa wakati wa ukaguzi risiti hiyo haikuwepo, kwa sasa risiti ipo yenye namba 05018 ya tarehe 23/3/2020.

5. Vocha namba 7/4 malipo ya fedha za posho ya chakula cha wanafunzi 240 wa mradi wa vijana na ajira katika kazi za vitendo Wilaya ya Mkoani, Chake, Wete na Micheweni, ambapo kilichokosekana ni muongozo wa malipo.

Mradi wa vijana na ajira ulitekelezwa katika awamu mbili, awamu ya kwanza wanafunzi walikaa katika vituo walivyopangiwa vya Vitongoji na Kengeja wakipatiwa mafunzo na huduma stahiki ikiwemo chakula na malazi kwa mujibu wa makubaliano. Awamu ya pili ya mradi wanafunzi walilazimika kuenda 'field' na kwamba Mamlaka ilipaswa iwawezeshe wanafunzi hao kujikimu katika maeneo yao ya 'field' ili kuwawezesha kufanya mafunzo yao viwandani kwa ufanisi. Kwa mukhtadha huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali alielekeza kuwa vijana hao wapatiwe posho ambalo litawawezesha kujikimu wakati wote watakapokuwa katika maeneo yao ya 'field' na ofisi ilitekeleza hilo.

Uchunguzi wa Kamati

1. Kuhusu majibu ya vocha nambari 1/8, kwa vile Mamlaka ilikubali kwamba walikuwa hawana muongozo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

2. Kwa upande wa majibu ya vocha nambari 7/1, Kamati iligundua kwamba vielelezo hivyo viliwasilishwa nje ya muda wa ukaguzi na kusababisha hoja hii kubakia katika ripoti ya Mdhibiti.

3. Kuhusu majibu ya vocha namba 4/2, Kamati ya LAAC haikufurahishwa na ilisikitishwa na majibu kwani jumla ya shilingi 1,725,000 zilitumika pasi na kuwepo vielelezo vinavyoonesha uhalali na usahihi wa matumizi hayo hasa ukizingatia kwamba hizo zote ni fedha za umma.

4. Kwa upande wa majibu ya vocha nambari 9/3, Kamati iligundua kwamba ni kweli

risiti halasi ilikuwepo ila muda ambao risiti hiyo inapatikana (tarehe 23/3/2020) Mkaguzi alikuwa ameshaondoka na hoja tayari imeshaingizwa kwenye kitabu.

5. Kuhusu majibu ya vocha nambari 7/4, Kamati iliridhishwa na majibu ya Watendaji wa Mamlaka na kwamba haikuwa na hoja zaidi.

Mbali na ukaguzi wa vocha za malipo, Kamati ilifanya ukaguzi maalum kuhusu upungufu mkubwa walimu unaopunguza kwa kiasi kikubwa ufanisi wa Vyuo vyote vinavyosimaiwa na Mamlaka ya Amali. Kamati lijibiwa kwamba Mamlaka ilichukua juhudi ya kuajiri walimu tofauti na tayari walikuwa washafikia hatua ya kufanyiwa 'vetting' katika ofisi ya 'GSO'. Lakushangaza, ajira hizo zimekwama kutokana na agizo la Serikali la kusimamisha ajira kwa kipindi hicho na kuelezwa kwamba watafute walimu kutoka katika Wizara za SMZ na kubahatika kupata walimu 14 wakati waliomba walimu 45.

Lakushangaza na kusikitisha zaidi kuna mwalimu ambaye alikuwa anawasaidia sana lakini amehamishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

Mapendekezo ya Kamati

1. Mamlaka ihakikishe inaweka vizuri vielelezo vya matumizi iliyoyafanya ili viweze kupatikana wakati wa ukaguzi kama inavyotaka sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.
2. Mamlaka iwasilishe kwa wakati vielelezo vinavyohitajika na Mkaguzi anapokwenda katika maeneo yao ya kazi.
3. Mamlaka kwa vile Taasisi inayojitegemea katika baadhi ya mambo yake ihakikishe inaandaa muongozo unaohusu ulipaji wa nauli za wafanyakazi wa Chuo.

ZIARA MAALUM YA UKAGUZI WA KAMATI KATIKA DAKHALIA YA CHUO CHA MAFUNZO YA AMALI MKOKOTONI

Katika kufuatilia hoja nambari 3.22.4 iliyoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo inaelezea kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika Dakhalia kulinganisha na uwezo wa Dakhalia (Hostel). Tarehe 24 Januari, 2022, Kamati ilifanya ukaguzi maalum (ziara ya kushitukiza) wa kutembelea dakhalia hiyo na kukutana na viongozi wake ili kujiridhisha na majibu yaliyotolewa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar kwamba ni kweli katika dakhalia hizo katika mwaka wa fedha 2019/2020, chumba kimoja kilikuwa kinakaliwa na wanafunzi zaidi ya wanne kama vilivyo vitanda vilivyomo ndani ya chumba kimoja.

Pamoja na kwamba muda ambao kamati ilifika eneo hilo kulikuwa hakuna wanafunzi kwa vile chuo kilikuwa kimefungwa kwa likizo yake ya kawaida, mambo yafuatayo yaligundulika:

1. Kamati imethibitisha kwamba ni kweli mazingira yalikuwa yakionesha kitanda kimoja kilikuwa kinalaza wanafunzi zaidi ya wanane kama ilivyoelezwa na

Mdhibiti. Kwa vile chumba kilikuwa na vitanda viwili vyenye magodoro manne ambavyo vinachukua wanafunzi wanane wakati godoro moja linakuwa chini na kukamilisha hesabu ya wanafunzi kumi kwa chumba kimoja.
2. Dakhalia ilikuwa katika mazingira yenye mwitu jambo ambalo halitoi taswira nzuri ya kuwepo kwa chuo kinachotoa taaluma bora kwa watoto wetu.
3. Kamati imegundua chuo kinalo eneo linaloweza kutumika kwa kilimo cha mboga ambayo ingesaidia kulisha wanafunzi wanaosoma chuoni hapo lakini hakijaweza kulitumia ipasavyo eneo hilo ili liweze kutoa tija kwao.

Mapendekezo ya Kamati

1. Uongozi wa chuo uhakikishe unaweka katika dakhalia wanafunzi kwa mujibu wa nafasi za vitanda vilivyopo.
2. Uongozi wa Chuo uhakikishe dakhalia na Chuo kwa ujumla kinakuwa katika mazingira safi wakati wote ili kuleta taswira halisi ya chuo.
3. Uongozi wa chuo ubuni mbinu mbadala za kulitumia vizuri eneo lake hususan kwa shughuli za kilimo cha mboga ili kiepukana na gharama zisizo za lazima za ununuzi wa viungo.

3.24: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 2,061,400,000 kati ya fedha hizo Tsh. 1,095,900,000 kwa ajili ya mshahara na Tsh. 965,500,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Mamlaka imepokea na kutumia jumla Tsh. 1,741,092,718 sawa na asilimia 84 ya makadirio, kati ya fedha hizo Tsh. 1,0979,611,696 kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 100 ya makadirio na Tsh. 643,481,022 kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 67 ya makadirio.

Majibu ya Mamlaka

Ni kweli kwamba Mamlaka hii katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa na kutumia kiasi hicho cha fedha na ilifanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

1. Kutoa elimu kwa Taasisi za Umma na za Binafsi pamoja na Jamii kwa ujumla kupitia vyombo vya habari vya Radio na Televisheni ambapo, jumla ya vipindi vinne ilirushwa hewani, kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC), Swahiba FM, Mtegani FM na Chuchu FM.
2. Mikutano 78 iliandaliwa na kufanyika katika Shehia za Unguja na Pemba
3. Yalifanyika maonyesho ya shughuli za ZAECA katika mbio za Mwenge, ambayo yalisaidia kuongeza uelewa kwa jamii juu ya madhara ya rushwa na

uhujumu uchumi.

4. Iliokoa na kurejesha kiasi cha Tsh. 275,717,302 kupitia makosa mbali mbali, kama vile, matumizi mabaya ya mali na mapato, matumizi mabaya ya ofisi na kusafirisha magendo.

Pamoja na shughuli hizo zilizotekelezwa, Mamlaka haikuweza kutekeleza shughuli zifuatazo kutokana na kutopatikana kwa fedha. Miongoni mwa shuguli hizo ni kama zifuatazo:

1. Kufanya utafiti, shughuli hii ni muhimu sana katika kutambua maeneo yenye viashiria vya rushwa hasa katika maeneo ya utowaji huduma kwa jamii. Lengo la kufanya utafiti ni kuiwezesha ZAECA kupata taarifa muhimu zitakazowezesha kufanya maamuzi ya nini kifanyike katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi.

2. Uchunguzi wa malalamiko mengi yaliyowasilishwa ZAECA hususan kwa makosa yanayohusisha utafutaji na ufatiliaji wa taarifa kwa maeneo ya nje ya ofisi.

3. Kufanya mapitio ya mifumo ya kifedha katika baadhi ya Taasisi za Serikali, kwani ZAECA inaamini kuwa mifumo iliyokuwepo inasababisha upotevu wa fedha za Serikali kutokana na mianya inayojitokeza katika mifumo hiyo.

4. Kufanya Mafunzo ya Awali ya Uchunguzi kwa watendaji wake. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watendaji katika kazi zao.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Mamlaka huokoa fedha kupitia makosa mbali mbali yanayofanywa, isipokuwa kwamba, fedha hizo huwa haziripotiwi kama ni mapato na wala hazioneshwi kwenye Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka ya Mamlaka, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

   Kutokana na kasoro hiyo kubwa iliyobainika na Kamati, Kamati ilimuomba Mtendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maelezo juu ya fedha hizo na hasa ikizingatiwa kuwa Taasisi yao imefanya ukaguzi katika Ofisi hiyo na haikuweza kubaini jambo hilo muhimu kwa maendeleo ya nchi hii.

Kutokana na matakwa hayo ya Kamati, Mtendaji wa Afisi ya Mdhibiti aliieleza Kamati kuwa, kasoro hiyo imejitokeza ama Mkaguzi husika hakuwa na uelewa juu ya fedha hizo na Watendaji wa Mamlaka hawakumueleza au kutokana na ufinyu wa muda hakuweza kupata muda mzuri wa kufanya majadiliano na Watendaji wa Mamlaka. Hata hivyo, aliieleza Kamati kuwa fedha hizo zinatakiwa kuoneshwa kwenye Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka ya Mamlaka.

2. Mhasibu wa Mamlaka alikiri mbele ya Kamati kuwa fedha hizo alikuwa haziingizi kwenye Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka ya Mamlaka kwa kuwa hakuwa na uelewa.
3. Katika mwaka huo wa fedha Mamlaka imeokoa jumla ya Tsh. 275,717,302 kupitia makosa mbali mbali. Fedha hizo huingizwa kwenye akaunti ya hesabu ya mapato ya Mamlaka na Mamlaka huwa haizitumii fedha inazoziokoa kwa kuwa haina mamlaka ya kufanya hivyo.
4. Akaunti ya hesabu ya mapato ya Mamlaka imefunguliwa tarehe 07 Juni, 2019 na hadi kufikia tarehe 15 Septemba, 2021 akaunti hiyo ina jumla ya Tsh. 146,268,739.71.
5. Mamlaka ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 800,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo, hata hivyo, hadi mwaka wa fedha 2019/2020 unamalizika fedha hizo hazikuingizwa. Kutokuingizwa kwa fedha hizo kumeifanya Mamlaka kutozitolea taarifa fedha hizo kwenye Taarifa yake ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro hizo zilizobainika Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Mapato yanayokusanywa na Mamlaka yaingizwe kwenye Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka na yajulikane kama ni mapato halisi ya Mamlaka na kwa kuwa Mamlaka haina uwezo wa kuyatumia basi mapato hayo yasomeke kuwa ni Taarifa ya Hesabu ya Amana “Deposit Account” na endapo fedha hizo zitawasilishwa Hazina basi fedha hizo zisomeke kuwa ni “Transfer”.
2. Mamlaka ihakikishe kuwa inaingiza kwenye Taarifa yake ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka taarifa zote za fedha ilizokadiriwa kutumiwa ili iweze kujulikana ni kiasi gani cha fedha ambacho hakikupatikana katika mwaka husika.
3. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ijipange vyema katika kutekeleza shughuli zake ili ipate muda wa kutosha wa kufanya majadiliano na Watendaji wa Taasisi kwa dhamira ya kupata taarifa mbali

mbali zinazohusiana na Taasisi husika.

4. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ihakikishe kuwa inawapatia mafunzo Wahasibu wake mara kwa mara ili aweze kujua mabadiliko mbali mbali yanayotokea katika fani hiyo.
5. Serikali iandae utaratibu mzuri utakaoielekeza Mamlaka hii kuhusiana na matumizi bora ya fedha wanazozikusanya kwa maslahi ya taifa.

Mengineyo

Katika kuweka taarifa yake sawa juu ya zoezi la uchukuaji wa gari kutoka katika Taasisi mbali mbali za Serikali lililofanywa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na kuziwasilisha gari hizo katika kiwanja cha Afisi ya Mamlaka hii mnamo mwezi wa Februari, 2021, Kamati ya LAAC ilitaka kujua idadi halisi ya gari zilizopelekwa kiwanjani hapo na hivi sasa zimebakia gari ngapi.

Kutokana na suala hilo, Mamlaka iliieleza Kamati kuwa haikuelezwa idadi halisi ya gari hizo na wala haikutaka kujua kwa kuwa ilikuwa haihusiki moja kwa moja na kadhia hiyo, isipokuwa kwamba, baada ya gari kuuzwa hupatiwa nakala ya barua inayomjulisha kuwa gari fulani ameuziwa hivyo fulani hivyo amruhusu aichukue barua ya tarehe 20 Disemba, 2021 yenye kumbukumbu Namba BA.26/454/01/23/36 inathibitisha hilo.

Sambamba na maelezo hayo, Mamlaka ilizidi kuieleza Kamati hii kuwa hadi Kamati hiyo inafanya ukaguzi wake Afisini hapo tarehe 04 Februari, 2022 jumla ya gari 8 zilikuwa bado hazijachukuliwa.

3.29 TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Taarifa ya Matumizi

Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 1,653,200,000 kwa kazi za kawaida na mtumizi ya kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo jumla ya Tsh. 973,200,000 zilikadiriwa kutumika kwa kazi za kawaida na Tsh. 680,000,000 ikiwa ni matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 jumla ya Tsh. 1,550,814,388 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 94 ya makadirio. Kati ya hizo jumla ya Tsh. 870,814,388 zilitumika kwa kazi za kawaida Tsh. 680,000,000 zilitumika kwa matumizi

ya maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirio.

Majibu ya Tume

Mchanganuo wa bajeti na fedha zilivyokadiriwa na zilivyopatikana kwa utekelezaji wa kipindi cha Julai, 2019 – Juni, 2020

Namba	Maelezo	Makadirio Julai 2019/2020	Fedha Zilizopatikana (Tsh.)	Asilimia (%)
1.	Udhibiti na Uchunguzi wa Dawa za Kulevya	105,692,000	46,029,840	44
	Kinga, Tiba na Marekebisho ya Tabia	280,060,000	136,455,632	49
	Mradi wa Maendeleo wa Kidimni	680,000,000	680,000,000	100
	Jumla	**1,065,752,000**	**862,485,472**	**81**
2.	Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya	297,932,000	286,941,666	96
	Mishahara	186,586,320	271,417,055	145
	Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Pemba	69,316,000	64,009,575	92
	Mishahara	33,613,680	65,960,620	196
	Jumla	**587,448,000**	**688,328,916**	**117**
	Jumla Kuu	**1,653,200,000**	**1,550,814,388**	**94**

Ufuatao ni ufafanuzi wa baadhi ya vifungu:

1. Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni, fedha zilipatikana kwa asilimia 100, isipokuwa kwamba, fedha zilizotumika kwa ujenzi ni Tsh. 656,153,102.00. Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya

uendelezaji wa ujenzi wa maumbo ya ghorofa ya kwanza, ya pili na kuwezeka na bakaa ya Tsh. 23,846,898 ilihifadhiwa Hazina katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya malipo ya "Retention" ya Mjenzi ambaye ni Al- Hilal General Trading Company Ltd.

2. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume, kumekuwa na ongezeko la asilimia 45 kwa Unguja na Pemba asilimia 96 kwa upande wa mishahara kutokana na kuteuliwa kwa Kurugenzi za ndani na kupata waajiriwa wapya ambao bajeti zao zilikuwa hazikupangwa.

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalibainika:

1. Maelezo "Note" 13 ya Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) imeeleza viwango tofauti vya matumizi ndani ya taarifa hiyo, jambo ambalo ni kinyume na taratibu za uandishi wa hesabu.
2. Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni ulikadiriwa kutumia takriban Tsh. 4 bilioni. Hata hivyo, imebainika kuwa makadirio hayo hayatokidhi haja kwa kuwa yalifanywa tangu mwaka 2012, hivyo, Mamlaka hii inatarajia kuyafanyia mapito makadirio hayo ili kupata gharama halisi.
3. Kamati ilifanya ziara ya kukagua Kituo hicho na iliridhika na gharama za ujenzi zilizotumika hadi Kamati hiyo inafanya ukaguzi wake tarehe 19 Januari, 2022.

Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilishauriwa kufuata taratibu zote zinazotakiwa za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ili kuwa na hesabu iliyokidhi matakwa ya ufungaji wa hesabu kitaifa na kimataifa.
2. Tume izifanyie mapitio gharama za ujenzi wa Kituo hicho haraka iwezekanavyo ili ijulikane gharama halisi ya ujenzi huo kwa lengo la kukamilisha ujenzi huo.

SEHEMU YA TATU

HITIMISHO

Kamati ya LAAC kama zilivyo Kamati nyengine zinazosimamia masuala ya kifedha, hufanya kazi zake za ukaguzi kwa kupitia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuchunguza hoja mbali mbali zilizojitokeza katika Ripoti hizo pamoja na kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika yanayojitegemea kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020.

Katika kutekeleza hayo, Kamati ya LAAC ilieleza mambo ambayo imeyabaini kupitia majibu ya Watendaji na kutoa Mapendekezo kwa Wahusika kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Taasisi za Umma. Kwa mnasaba huo, Kamati hii inaliomba Baraza la Wawakilishi, kuipitia, kuijadili na hatimaye kuiridhia Ripoti hii kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali.

Kwa kuwa taratibu za kihasibu hubadilika mara kwa mara na kwa kuwa asilimia kubwa ya Wajumbe wa Kamati zinazosimamia masuala ya kifedha hawana taaluma ya kutosha juu ya masuala hayo, hivyo basi, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuiongezea fedha za matumizi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwa lengo la kuzijengea uwezo Kamati ya LAAC na Kamati ya PAC kama zinavyofanya nchi nyengine duniani.

Pamoja na sababu tulizozieleza hapo awali, Kamati ya LAAC inashauri hili pia, kwa kuwa Ofisi hiyo ilikaribia kushindwa kuwapatia uchambuzi wa Ripoti zake za mwaka wa fedha 2019/2020 Wajumbe wa Kamati hizo kutokana na uhaba wa fedha unaoukabili Ofisi hiyo.

Sambamba na hayo, licha ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kuruhusiwa kukodi (hire) mtu yoyote katika kutekeleza shughuli zake, hata hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Ofisi hiyo kuajiri Watendaji wenye sifa, taaluma na fani tofauti ili Ofisi yake iweze kutekeleza shughuli zake bila ya usumbufu wowote.

Kamati ya LAAC imelazimika kulishauri hili kwa kuwa kwa kawaida unapomkodi mtu inakugharimu kiasi kikubwa cha fedha tofauti na unapomuajiri mtu huyo.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya LAAC inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Serikali za Mitaa na Taasisi Zinazojitegemea za SMZ kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa

mashirikiano yao kwa Kamati hii.

Vile vile, tunatoa shukurani za pekee kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kuipatia mafunzo Kamati hii ili iweze kutekeleza shughuli zake kwa wepesi na kwa weledi mkubwa.

Mwisho na sio mwisho kwa umuhimu, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza hilo kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika.

****&&&****